JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI, 2020



MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA


NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: 255 (026) 2321759, Nukushi: 255(026)2117527, Baruapepe: ocag@nao.go.tz, Anwani: www.nao.go.tz

Kwa majibu taja:

Kumb. Na. CGA.319/421/01-A/07 **28 Machi 2021**

Mh. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere, Chamwino,
40400 DODOMA

KUWASILISHA RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

Kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (Kama ilivyorekebishwa), na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008, ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

Charles E. Kichere
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI


NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

DIRA, DHIMA, NA MISINGI YA MAADILI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

(Imeundwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania)

Majukumu na wajibu wa kikatiba wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (Kama ilivyorekebishwa) na Kifungu Na. 20(1) cha Sheria ya Ukaguzi ya Mwaka 2008.

Dira

Kuwa Taasisi ya kiwango cha hali ya juu katika ukaguzi wa sekta ya umma.

Dhima

Kutoa huduma za ukaguzi wa sekta ya umma zenye ubora wa hali ya juu zinazoimarisha utendaji, uwajibikaji, na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Misingi ya Maadili

Katika kutoa huduma zenye ubora, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaongozwa na misingi ya maadili ifuatayo:

✓ Kutopendelea	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
✓ Huduma Bora	Ni taasisi ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na viwango vinivyokubalika.
✓ Uadilifu	Ofisi inazingatia na kudumisha nidhamu kwa kiwango cha juu, utawala wa sheria, na malengo.
✓ Ubunifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo kutoka ndani na nje ya taasisi.
✓ Zingatio kwa Wadau	Tunathamini, tunaheshimu na tunatambua matakwa ya wadau wetu.

✓ Matokeo Yaliyoelekezwa	Tunaangazia mafanikio kulingana na malengo ya taasisi.
✓ Moyo wa Kufanya Kazi kwa Pamoja	Tunafanya kazi kama timu, kushirikishana kitaaluma, na kubadilishana ujuzi, mawazo na uzoefu.

Tunafanya haya kwa:

- ✓ Kufanikisha usimamizi bora wa fedha za umma kwa kuhakikisha kuwa wakaguliwa wanawajibika ipasavyo katika kusimamia rasilimali walizokabidhiwa.
- ✓ Kusaidia kuimarisha ubora wa huduma za jamii kwa kuunga mkono juhudi za ubunifu kwenye matumizi ya rasilimali za umma.
- ✓ Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakaguliwa kuhusu mapungufu ya kiutendaji kwenye mifumo yao ya uendeshaji.
- ✓ Kushirikisha wakaguliwa katika mchakato wa ukaguzi na hatua zake; na
- ✓ Kuwapatia wakaguzi mafunzo sahihi, na vitendeakazi vya kutosha ambavyo vitachangia kufanya kazi kwa uhuru.

© Taarifa hii Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Serikali za Mitaa ni kwa matumizi ya Mamlaka za Serikali zinazohusika. Hata hivyo, itatolewa kwa umma mara baada ya kuwasilishwa Bungeni.

YALIYOMO

DIRA, DHIMA, NA MISINGI YA MAADILI....ii
ORODHA YA MAJEDWALI v
ORODHA YA VIAMBATISHO.... xi
ORODHA YA MICHORO....xiv
VIFUPISHO NA MANENO xv
UTANGULIZI xvi
SHUKRANI xvii
MUHTASARI xix
SURA YA 1 1
USULI NA TAARIFA KWA UJUMLA 1
SURA YA 2 5
AINA NA MWENENDO WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA 5
SURA YA 3 22
HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI YA MIAKA ILIYOPITA 22
SURA YA 4 30
MAANDALIZI YA BAJETI NA UTEKELEZAJI WAKE 30
SURA YA 5 39
UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA 39
SURA YA 6 44
TATHMINI YA MFUMO YA UDHIBITI WA NDANI, USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA MIFUMO YA UTAWALA BORA.... 44
SURA YA 7 56
USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA 56
SURA YA 8 70
UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO NA MIRADI MINGINE 70
SURA YA 9 87
USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA 87
SURA YA 10 147
USIMAMIZI WA MATUMIZI 147
SURA YA 11 161
USIMAMIZI WA MAPATO 161
SURA YA 12 189
USIMAMIZI WA MALI.... 189
SURA YA 13 202
MATOKEO YA UKAGUZI MAALUM.... 202
SURA YA 14 332
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 332
VIAMBATISHO.... 353

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1-1: Idadi ya Halmashauri Zilizokaguliwa Mwaka 2019/20 3
Jedwali Na. 2-1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Mwaka Huu Na Miaka Mitatu Mfululizo Iliyopita 16
Jedwali Na. 2-2: Orodha ya Halmashauri Zilizojiimarisha Kutoka Hati mbaya na Kupata Hati Yenye Shaka au Kutoka Hati Yenye Shaka na Kupata Hati Inayoridhisha Mwaka Huu 17
Jedwali Na. 2-3: Mchanganuo wa Halmashauri Zilizokuwa na Aya Yenye Masuala ya Msisitizo Kwenye Ripoti Yake ya Ukaguzi 19
Jedwali Na. 3-1: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwa Mwaka 2018/19 24
Jedwali Na. 3-2: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Utekelezaji wa Mapendekezo Unaoendelea kwa Kipindi cha Miaka Miwili Hadi Kumi..... 25
Jedwali Na. 3-3: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Mapendekezo Yasiyotekelezwa Hadi Miaka 10 27
Jedwali Na. 3-4: Hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa 28
Jedwali Na. 3-5: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Maagizo ya Muda Mrefu Ambayo Hayajatekelezwa 29
Jedwali Na. 4-1: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato Ikilinganishwa na Bajeti Iliyoidhinishwa 31
Jedwali Na. 4-2: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato ya Ndani Ikilinganishwa na Matumizi ya Kawaida 32
Jedwali Na. 4-3: Kiwango cha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kujitegemea kwa Matumizi ya Kawaida 32
Jedwali Na. 4-4: Asilimia ya Makusanyo Pungufu Kutoka Vyanzo vya Mapato ya Ndani 33
Jedwali Na. 4-5: Mwenendo wa Fedha za Maendeleo Ambazo Hazikupokelewa 36
Jedwali Na. 4-6: Mwenendo wa Fedha Pungufu za Matumizi ya Kawaida . 36
Jedwali Na. 5-1: Mwenendo wa Madai na Malipo ya Awali ya Muda Mrefu 41
Jedwali Na.5-2: Mwenendo wa Madeni Yasiyolipwa 42
Jedwali Na. 6.1: Miamala Yenye Viashiria vya Udanganyifu 49
Jedwali Na. 7-1: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye Malipo kwa Wasio Watumishi 57
Jedwali Na. 7-2: Makato ya Mishahara ya Thamani ya Sh. 5,079,945,442 Ambayo Hayakuwasilishwa kwa Taasisi Husika 59
Jedwali Na. 7-3: Mwenendo wa Idadi ya Watumishi Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 60
Jedwali Na. 7-4: Watumishi wa Halmashauri wanaopata mishahara chini ya theluthi moja 61
Jedwali Na. 7-5: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye Mikopo ya Mishahara 63

Jedwali Na. 7-6: Halmashauri Zenye Mishahara Isiyolipwa Ambayo Haikurejeshwa Hazina 64
Jedwali Na. 7-7: Mwenendo wa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaokaimu 65
Jedwali Na. 7-8: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Ucheleweshaji wa Nyongeza ya Mishahara na Kupandisha Madaraja 67
Jedwali Na. 7-9: Serikali za Mitaa Zenye Watumishi Ambao Taarifa Zao Hazijahuishwa Katika Mfumo wa LAWSON 68
Jedwali Na. 8-1: Mwenendo wa Matumizi ya Fedha za Maendeleo..... 71
Jedwali Na. 8-2: Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Vyanzo vya Ndani 72
Jedwali Na. 8-3: Orodha ya Halmashauri Ambazo Hazikupeleka Ruzuku ya Fidia ya Vyanzo Vilivyofutwa 76
Jedwali Na. 8-4: Mwenendo wa Kutochangia Asilimia 10 ya Mapato ya Halmashauri kwa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu 77
Jedwali Na. 8-5: Mwenendo Wa Kutorejeshwa kwa Mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa Miaka Minne Mfululizo. 78
Jedwali Na. 8-6: Orodha ya Halmashauri Ambazo Hazijahamishia Fedha Kwenye Akaunti Maalumu ya Mikopo 79
Jedwali Na. 8-7: Hali ya Miundombinu Katika Shule za Msingi..... 82
Jedwali Na. 8-8: Hali ya Miundombinu katika Shule za Sekondari 82
Jedwali Na. 8-9: Orodha ya Halmashauri Zilizo na Kasoro 84
Jedwali Na. 8-10: Orodha ya Halmashauri Zenye Vitabu vya Risiti Visivyorudi 84
Jedwali Na. 8-11: Orodha ya Halmashauri Zilizotekeleza Miradi Isiyoanzishwa na Jamii..... 85
Jedwali Na. 8-12: Orodha ya Halmashauri Zilizotumia Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Kugharamia Taasisi za Kisiasa na Kidini..... 86
Jedwali Na. 9-1: Fedha za Mmma Zilizookolewa kutoka Malipo Yasiyostahiki 88
Jedwali Na. 9-2: Mikataba Iliyovunjwa..... 91
Jedwali Na. 9-3: Hasara Kutokana na Udanganyifu wa Bei Zilizonukuliwa 95
Jedwali Na. 9-4: Mwenendo wa Manunuzi Usio wa Shindani 96
Jedwali Na. 9-5: Mwenendo wa Manunuzi Yaliyofanywa Bila Idhini ya Bodi za Zabuni 97
Jedwali Na. 9-6: Mwenendo wa Manunuzi Bila ya Mikataba ya Makubaliano Kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma 98
Jedwali Na. 9-7: Mwenendo wa Bidhaa au Huduma Zilizopokelewa Bila Kukaguliwa au Kupimwa..... 99
Jedwali Na. 9-8: Mwenendo wa Manunuzi Yaliofanywa Nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka 100
Jedwali Na. 9-9: Dosari Zilizojitokeza Zaidi Katika Manunuzi ya Mwaka Huu 101
Jedwali Na. 9-10: Halmashauri Zilizobainika Kuwa na Dosari Nyingi Wakati wa Manunuzi 102

Jedwali Na. 9-11: Orodha ya Halmashauri Zenye Malipo Kwa Bidhaa Ambazo Hazikupokelewa 104
Jedwali Na. 9-12: Orodha ya Halmashauri Zenye Manunuzi Yaliyofanywa Kupitia Fedha Taslimu 105
Jedwali Na. 9-13: Orodha ya Halmashauri Zenye Manunuzi ya Bidhaa na Huduma bila Kutumia LPO 106
Jedwali Na. 9-14: Manunuzi Nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka..... 107
Jedwali Na. 9-15: Matumizi Hafifu ya Mfumo wa Manunuzi wa Kielekitroniki 108
Jedwali Na. 9-16: Vifaa Vilivyonunuliwa Zaidi ya Mahitaji 109
Jedwali Na. 9-17: Matengenezo na Ukarabati wa Magari ya Serikali 110
Jedwali Na. 9-18: Halmashauri Ambazo Kumbukumbu za Manunuzi Zilizokosekana 112
Jedwali Na. 9-19: Orodha ya Halmashauri Zenye Miradi Iliyotekelezwa Bila Kuwa na Hati za Dhamana 113
Jedwali Na. 9-20: Orodha ya Halmashauri Zenye Mikataba Ambayo Haikuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali/Halmashauri 114
Jedwali Na. 9-21: Kuchelewa kwa Malipo ya Kazi Zilizothibitishwa 115
Jedwali Na. 9-22: Orodha ya Halmashauri zenye Malipo Yaliyofanywa bila Vipimo wala Kuthibitishwa na Wasimamizi wa Miradi..... 115
Jedwali Na. 9-23: Miradi Iliyotekelezwa Bila Kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira 116
Jedwali Na. 9-24: Halmashauri Zilizokaguliwa 117
Jedwali Na. 9-25: Mawanda ya Ukaguzi wa Kina Katika Usimamizi wa Mikataba 118
Jedwali Na. 9-26: Miradi Iliyoanzishwa Bila Umiliki wa Ardhi na Upembuzi Yakinifu 120
Jedwali Na. 9-27: Mikataba Iliyotekelezwa Bila Kufanyiwa Tathmini ya Athari za Mazingira..... 121
Jedwali Na. 9-28: Miradi Iliyotekelezwa Ambayo Haikuwepo Katika Mipango Ya Manunuzi..... 123
Jedwali Na. 9-29: Miradi Iliyotekelezwa Bila Kutengewa Fedha..... 124
Jedwali Na. 9-30: Miradi Inayotekelezwa Bila Washauri..... 126
Jedwali Na. 9-31: Miradi Yenye Usanifu wenye Mapungufu 128
Jedwali Na. 9-32: Miradi Ambayo Nyaraka za Manunuzi Zilikosekana 129
Jedwali Na. 9-33: Mikataba Ambayo Zabuni Zake Zilitangazwa Bila Kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni..... 131
Jedwali Na. 9-34: Mikataba Ambayo Taarifa za Zabuni na Tuzo Hazikuchapishwa 132
Jedwali Na. 9-35: Mikataba iliyo na Marekebisho ya Kimahesabu Yasiyo Sahihi..... 136
Jedwali Na. 9-36: Mikataba Iliyotekelezwa Pasipo Upembuzi Baada ya Tathmini 138
Jedwali Na. 9-37: Mikataba Ambayo Wazabuni Wake Hawakupewa Siku Saba za Kuwasilisha Malalamiko 139

Jedwali Na. 9-38: Mikataba Ambayo Nakala za Barua za Tuzo Hazikuwasilishwa kwa Mamlaka Husika 141
Jedwali Na. 9-39: Mapungufu Yaliyobainika Katika Upekuzi wa Mikataba 142
Jedwali Na. 9-40: Mikataba Iliyochelewa Kukabidhiwa na Kuanza Kutekelezwa..... 146
Jedwali Na. 10-1: Kukosekana Kwa Hati Za Malipo..... 148
Jedwali Na. 10-2: Mwenendo wa Matumizi Yasiyo na Viambatisho 150
Jedwali Na. 10-3: Malipo Yasiyo Ambatishwa Risiti za Kielekitroniki 151
Jedwali Na. 10-4: Muhtasari wa Mapungufu ya Usimamizi wa Masurufu . 152
Jedwali Na. 10-5: Muhtasari wa Mapungufu ya Uandaaji na Uidhinishaji wa Hati za Malipo..... 153
Jedwali Na. 10-6: Halmashauri zenye Mapungufu Kuhusu Kodi ya Zuio .. 155
Jedwali Na. 10-7: Mapungufu Kwenye Uendeshaji wa Akaunti za Amana 155
Jedwali Na. 10-8: Uhamisho Wa Ndani Kwenye Akaunti (Mikopo) Isiyorejeshwa..... 156
Jedwali Na. 10-9: Mapungufu Kwenye Matumizi ya Mafuta 157
Jedwali Na. 10-10: Matumizi yasiyokuwepo kwenye bajeti na fedha zilizobadilishwa matumizi..... 158
Jedwali Na. 10-11: Orodha ya halmashauri ambazo hazikuripoti Madeni 158
Jedwali Na. 10-12: Fedha za Zuio Zisizo Pelekwa Kwenye Mamlaka Husika 160
Jedwali Na. 10-13: Fedha za Zuio Zisizo Pelekwa RUWASA 160
Jedwali Na. 10-14: Fedha za Zuio Zisizo Pelekwa TARURA..... 160
Jedwali Na. 11-1: Orodha ya Vituo vya Afya na Zahanati Ambazo Hazijasimikwa Mfumo Wa Mapato..... 162
Jedwali Na. 11-2: Mamlaka Ambazo Hazijahuisha Sheria Ndogondogo ... 163
Jedwali Na. 11-3: Udhaifu Katika Usimamizi wa Mashine za Kukusanyia Mapato 165
Jedwali Na. 11-4: Orodha ya Halmashauri Zenye Changamoto za Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato 166
Jedwali Na. 11-5: Kutokusanywa kwa Ushuru wa Huduma Kwenye Taasisi za Kibiashara 169
Jedwali Na. 11-6: Ushuru wa Hoteli Kutokusanywa Kutoka kwa Walipaji 170
Jedwali Na. 11-7: Kodi ya Huduma Iliyokusanywa Bila Ushahidi Wa Mauzo 171
Jedwali Na. 11-8: Mapato Yaliyopelekwa Benki kwa Kuchelewa 173
Jedwali Na. 11-9: Mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo 174
Jedwali Na. 11-10: Wadaiwa Mbalimbali Ambao Miamala yao Haikusuluhishwa Kwenye Mfumo 175
Jedwali Na. 11-11: Miamala Iliyofutwa Kwenye Mfumo wa Mapato Bila Kuwa na Viambatisho 179
Jedwali Na. 11-12: Bajeti Kutoingizwa Kwenye Mfumo wa Mapato 180
Jedwali Na. 11-13: Mapato Yaliyokusanywa Pungufu Kutokana na Kutoza Kiwango Kisicho Sahihi..... 181

Jedwali Na. 11-14: Wakusanyaji wa Mapato na Wapangaji Wasio na Mikataba na Halmashauri 182
Jedwali Na. 11-15: Mapato Yaliyokusanywa Yenye Taarifa Zinazokinzana 183
Jedwali Na. 11-16: Mapato ya Ndani Yaliyohamishiwa Kwenye Akaunti ya Amana 185
Jedwali Na. 11-17: Fedha za Mapato ya Ndani Zilizotumika Kabla ya Kupelekwa Benki 186
Jedwali Na. 11-18: Mapato Yaliyokusanywa na Mawakala Ambayo Hayakuwasilishwa 187
Jedwali Na. 11-19: Vitabu vya Kukusanyia Mapato Visivyotumika..... 188
Jedwali Na. 12-1: Mwenendo wa Umiliki wa Ardhi Bila Hati kwa Miaka Mitatu 190
Jedwali Na. 12-2: Mali Zinazomilikiwa na Halmashauri Bila Kuwepo kwa Hati Miliki 190
Jedwali Na. 12-3: Magari na Pikipiki Ambazo Hazina Kadi za Usajili 191
Jedwali Na. 12-4: Mali Ambazo Zimetelekezwa na Hazijafanyiwa Matengenezo Kwa Muda Mrefu 193
Jedwali Na. 12-5: Mwenendo wa Magari na Pikipiki Zinazoendeshwa Bila Kukatiwa Bima 193
Jedwali Na. 12-6: Mwenendo wa Dawa Zilizokwisha Muda Wake Lakini Hazikuteketezwa kwa Miaka Mitatu 194
Jedwali Na. 12-7: Dawa Zilizokwisha Muda Wake Bila Kuteketezwa..... 195
Jedwali Na. 12-8: Mapungufu Kwenye Utunzaji wa Rejesta ya Magari, Mitambo na Vifaa 196
Jedwali Na. 12-9: Mali za Kudumu Zilizonunuliwa na Kutowekewa Namba za Utambulisho 198
Jedwali Na. 12-10: Mali Za Kudumu Zilizonunuliwa Bila Kuwekewa Namba za Utambulisho 198
Jedwali Na. 12-11: Kutokuandaliwa kwa Rejesta ya Matengenezo..... 199
Jedwali Na. 12-12: Mali Ambazo Hazitumiki..... 201
Jedwali Na. 13-1: Kaguzi Maalumu Zilizofanyika Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa Maombi ya TAKUKURU 203
Jedwali Na. 13-2: Kaguzi Maalumu Zilizofanyika Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa Maombi ya LAAC..... 203
Jedwali Na. 13-3: Kaguzi maalumu zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa maelekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 204
Jedwali Na. 13-4: Matumizi Fedha za Miradi ya Maji Kinyume na Malengo Yaliyokusudiwa 215
Jedwali Na. 13-5: Mikataba iliyolipiwa gharama za dhamana na Bima ... 220
Jedwali Na. 13-6: Mikataba iliyosainiwa na kutekelezwa na kampuni za ubia zisizosajiliwa 222
Jedwali Na. 13-7: Mikataba Ambayo Haikutozwa Fidia ya Ucheleweshaji Mradi 225

Jedwali Na. 13-8: Mikataba ya Mabadiliko Yasiyoidhinishwa..... 227
Jedwali Na. 13-9: Fedha Zilizotumwa Kutoka Wizara ya Maji Na Kutumika Bila Kibali cha Wizara Husika 229
Jedwali Na. 13-10: Kukosekana kwa Nyaraka Timilifu za Miradi ya Maji Kwa Ajili ya Ukaguzi 231
Jedwali Na. 13-11: Malipo ya awali ambayo hayakurejeshwa na wakandarasi 233
Jedwali Na. 13-12: Kazi Zilizolipwa Bila Kufanyiwa Vipimo 235
Jedwali Na. 13-13: Kodi ya Zuio Ambayo Haikukatwa 236
Jedwali Na. 13-14: Mapato Yaliyokusanywa na Mawakala Kupitia Mfumo wa LGRCIS Ambayo Hayakuwasilishwa Benki 237
Jedwali Na. 13-15: Halmashauri Zenye Miamala Iliyorekebishwa Kwenye Mfumo wa Mapato Bila Idhini ya Afisa Masuuli na Vielelezo Stahiki..... 239
Jedwali Na. 13-16: Mapato ambayo Hayakukusanywa Kutoka Vyanzo Mbalimbali vya Mapato ya Ndani 241
Jedwali Na. 13-17. Mapato ya ushuru wa Huduma ambayo hayajakusanywa na Halmashauri 242
Jedwali Na. 13-18: Halmashauri Zilifanya Malipo Bila Kudai Stakabadhi za Mashine ya Kielektroniki (EFD receipts)..... 244
Jedwali Na. 13–19: Hati za Malipo Ambazo Hazikuwasilishwa kwa Ajili ya Ukaguzi 245

ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. 2-1: Orodha ya Halmashauri Zilizopata Hati Inayoridhisha 353
Kiambatisho Na. 2-2: Orodha ya Halmashauri Zilizopata Hati yenye Shaka na Sababu Zake 356
Kiambatisho Na. 2-3: Orodha na Halmashauri Zilizopata Hati Mbaya na Sababu Zake 415
Kiambatisho Na. 2-4: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Miaka Minne .. 434
Kiambatisho Na. 2-5: Orodha ya Halmashauri Zilizokuwa na Aya ya Masuala ya Mkazo 447
Kiambatisho Na. 3-1: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa kwa Serikali kwa Mwaka 2018/19 450
Kiambatisho Na. 3-2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa Mwaka 2018/19 460
Kiambatisho Na. 3-3: Mapendekezo ambayo Utekelezaji Umekuwa Ukiendela kwa Muda Mrefu 467
Kiambatisho Na. 3-4: Mapendekezo Yasiyotekelezwa kwa Muda Mrefu .. 473
Kiambatisho Na. 3-5: Hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya LAAC 479
Kiambatisho Na. 4-1: Mtiririko wa Mapato ya Ndani Ukilinganisha na Bajeti 485
Kiambatisho Na. 4-2: Mapato ya Ndani Yaliyokusanywa Ikilinganishwa na Matumizi ya Kawaida 492
Kiambatisho Na. 4-3: Orodha ya Halmashauri Zenye Makusanyo Pungufu 499
Kiambatisho Na. 4-4: Orodha ya Halmashauri Zenye Mapato Zaidi ya Bajeti 504
Kiambatisho Na. 4-5: Kiwango cha Ruzuku ya Maendeleo Kilichotolewa Zaidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa 506
Kiambatisho Na. 4-6: Ruzuku za Matumizi ya Kawaida Zilizopokelewa Zaidi ya Bajeti 507
Kiambatisho Na. 4-7: Kiwango cha Ruzuku ya Maendeleo Kilichotolewa Pungufu ya Bajeti Iliyoidhinishwa 509
Kiambatisho Na. 4-8: Ruzuku za Matumizi ya Kawaida Zilizopokelewa Pungufu ya Bajeti 514
Kiambatisho Na. 4-9: Mapato ya Ndani Ambayo Hayakupeleka Kwenye Miradi ya Maendeleo 520
Kiambatisho Na. 5-1: Miamala Iliyotakiwa Kurekebishwa na Thamani ya Jumla ya Makossa Yaliyobainika 526
Kiambatisho Na. 5-2: Madai ya Mda Mrefu na Malipo Yaliyofanywa na Halmashauri Kabla ya Kupokea Huduma 530
Kiambatisho Na. 5-3: Madeni Yasiyolipwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mda Mrefu 534
Kiambatisho Na. 5-4: Kesi ya Madai Zilizoko Mahakamani 539
Kiambatisho Na. 6-1: Mapungufu Kwenye Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani 543
Kiambatisho Na. 6-2: Mapungufu Kwenye Udhibiti wa Jumla wa TEHAMA 546

Kiambatisho Na. 6-3: Mapungufu Kwenye Tathmini ya Vihatarishi vya Udanganyifu 548
Kiambatisho Na. 6-4: Mapungufu Kwenye Utendaji wa Kamati ya Ukaguzi kwenye Halmashauri 551
Kiambatisho Na. 7-1: Makato ya Mishahara Ambayo Hayajawasilishwa Kwenye Taasisi Husika 553
Kiambatisho Na. 7-2: Upungufu wa watumishi 119,753 katika Halmashauri 123..... 555
Kiambatisho Na. 7-3: Wakuu wa Idara na Vitengo Wanaokaimu kwa Kipindi cha Zaidi ya Miezi Sita 558
Kiambatisho Na. 7-4: Watumishi Wanaopata Mishahara Chini ya Moja ya Tatu 560
Kiambatisho Na. 8-1: Mapato na Matumizi ya Miradi Mikubwa ya Maendeleo 561
Kiambatisho Na. 8-2: Orodha ya Halmashauri Zenye Fedha za Utekelezaji wa Miradi Zisizotumika 567
Kiambatisho Na. 8-3: Miradi Ambayo Haikukamilika 572
Kiambatisho Na. 8-4: Miradi Ambayo Haikutekelezwa 589
Kiambatisho Na. 8-5: Kasoro Zilizobainishwa Katika Utekelezaji wa Miradi 593
Kiambatisho Na. 8-6: Miradi Iliyokamilika lakini Haitumiki 624
Kiambatisho Na. 8-7: Orodha ya Halmashauri Zisizochangia Asilimia 10 ya Chanzo kwa WYDF 629
Kiambatisho Na. 8-8: Mikopo Iliyotolewa kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu Isiyorejeshwa..... 631
Kiambatisho Na. 8-9: Orodha ya Halmashauri Zenye Kiasi Kilichokataliwa na Kisichorejeshwa kutoka NHIF 636
Kiambatisho Na. 8-10: Fedha za Ruzuku ya Uendeshaji, Fidia ya Ada na Chakula ambazo Hazijatolewa kwa shule za msingi na sekondari..... 638
Kiambatisho Na. 8-11: Uhaba wa Miundombinu Katika Shule za Msingi .. 641
Kiambatisho Na. 8-12: Uhaba wa Miundombinu Katika Shule za Sekondari 647
Kiambatisho Na. 9-1: Orodha ya Halmashauri Zilizofanya Manunuzi Bila Ushindanishi 653
Kiambatisho Na. 9-2: Orodha ya Halmashauri Ambazo Zilipokea Bidhaa Bila Kukaguliwa 655
Kiambatisho Na. 9-3: Orodha ya Halmashauri Ambazo Zilinunua Bidhaa na Huduma Kutoka kwa Wasambazaji Wasioidhinishwa na Wakala ya Ununuzi Serikalini..... 657
Kiambatisho Na. 9-4: Ununuzi na Utoaji Tuzo za Zabuni Bila Idhini ya Bodi ya Zabuni 659
Kiambatisho Na. 10-1: Matumizi Yasiyo na Manufaa 660
Kiambatisho Na. 10-2: Matumizi Yasiyo na Viambatanisho..... 662
Kiambatisho Na. 10-3: Mapungufu Katika Usimamizi wa Masurufu..... 663

Kiambatisho Na. 10-4: Mapungufu Katika Kuandaa na Uidhinishaji wa Hati za Malipo 665
Kiambatisho Na. 10-5: Malipo Yasiyostahili 667
Kiambatisho Na. 10-6: Kodi ya Zuio Isiyokatwa na Kuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania 669
Kiambatisho Na. 10-7: Ukiukwaji uliobainika kwenye uendeshaji wa Akaunti ya Amana 670
Kiambatisho Na. 10-8: Mapungufu Yaliyobainika Kwenye Matumizi ya Mafuta 672
Kiambatisho Na. 10-9: Matumizi Yasiyokuwepo Kwenye Bajeti na Fedha Zilizobadilishwa Matumizi 673
Kiambatisho Na. 11-1: Mapato Yaliyokusanywa Lakini Hayakupelekwa Benki 675
Kiambatisho Na. 11-2: Mapato Ambayo Hayakukusanywa Kutoka Kwenye Vyanzo Mbalimbali 678
Kiambatisho Na. 12-1: Mali Ambazo Hazijafanyiwa Matengenezo au Kuondoshwa 681
Kiambatisho Na. 12-2: Magari na Pikipiki ambayo Hayajakatiwa Bima ... 685
Kiambatisho Na. 13-1: Miradi ya Maji Isiyotoa Huduma kwa Jamii 687
Kiambatisho Na. 13-2: Mikataba Yenye Ucheleweshwaji Katika Utekelezaji na Ukamilishaji 690
Kiambatisho Na. 13-3: Wakandarasi Kutolipwa Madai Yao kwa Muda Mrefu na Kupelekea Kuondoka Eneo la Mradi na Kuchelewesha Utekelezaji wa Miradi 694
Kiambatisho Na. 13-4: Mikataba Iliyojumuishwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) 696
Kiambatisho Na. 13-5: kodi ya ongezeko la thamani (VAT) iliolipwa kwa Mikataba yenye Misamaha ya Kodi 698
Kiambatisho Na. 13-6: Malipo kwa Wakandarasi kwa Kazi Ambazo Hazikufanyika 699
Kiambatisho Na. 13-7: Mikataba Iliyotolewa kwa Wakandarasi Wasiostahili 701
Kiambatisho Na. 13-8: Mikataba Iliyotekelezwa Bila Kuwa na Hati za Dhamana ya Utendaji 705
Kiambatisho Na. 13-9: Hasara iliyotokana na kuwaondoa wazabuni wenye bei za chini 709
Kiambatisho Na. 13-10: Mapungufu Yaliyobainika Wakati wa Kutembelea Miradi ya Maji 711

ORODHA YA MICHORO

Mchoro Na. 2-1: Mazingira Yanayopelekea Utoaji wa Hati za Ukaguzi 12
Mchoro Na. 2-2: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka 2019/20 15
Mchoro Na. 3-1: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Serikali 23
Mchoro Na. 7-1: Mwenendo wa Malipo ya Wasio Watumishi kwa Miaka Mitatu 58
Mchoro Na. 9-1: Mwenendo wa Ununuzi Usio Shindanishi 96
Mchoro Na. 9-2: Mwenendo wa Ununuzi Bila Idhini ya Bodi ya Zabuni 97
Mchoro Na. 9-3: Mwenendo wa Ununuzi bila Mkataba Kutoka GPSA 98
Mchoro Na. 9-4: Mwenendo wa Bidhaa Zilizopokelewa bila Kukaguliwa au Kupimwa 99
Mchoro Na. 9-5: Mwenendo wa Ununuzi Uliofanywa nje ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka 100
Mchoro Na. 10-1: Mwenendo wa Hati za Malipo Zilizokosekana 148
Mchoro Na. 11-1: Mapato Yaliyokusanywa Lakini Hayakupelekwa Benki . 173
Mchoro Na. 11-2: Mwenendo Wa Mapato Ambayo Hayakukusanywa 178

VIFUPISHO NA MANENO

AFROSAI	Muungano wa Asasi Kuu za Ukaguzi katika Nchi za Afrika
AFROSAI-E	Muungano wa Asasi Kuu za Ukaguzi katika Nchi za Afrika Zinazozungumza Lugha ya Kiingereza
BoQ	Mchanganuo wa Idadi ya Bidhaa
EMA	Sheria ya Usimamizi wa Mazingira
EPICOR	Mfumo Funganifu wa Usimamizi a Fedha
FFARS	Mfumo wa Taarifa za Kifedha Unaotumiwa katika Ngazi za Chini za Serikali
FYDP-II	Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano – II
GCC	Masharti ya Jumla ya Mkataba
GoTHoMIS	Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Hospitali Tanzania
H/JIJI	Halmashauri ya Jiji
H/M	Halmashauri ya Manispaa
H/MJI	Halmashauri ya Mji
H/W	Halmashauri ya Wilaya
HCMIS	Mfumo wa Utumishi
INTOSAI	Taasisi ya Kimataifa ya Taasisi Kuu za Ukaguzi
ISSAIS	Viwango vya Kimataifa kwa Taasisi Kuu za Ukaguzi
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
LAWSON	Mfumo wa Kielekitroniki wa Kumbukumbu za Watumishi
LGFM	Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009
MoU	Mkataba wa Makubaliano
Na.	Namba
OR-TAMISEMI	Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PLANREP	Mfumo wa Kielekitroniki wa Bajeti
PO-PSM	Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma
PO-RALG	Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PPA	Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011
PPR	Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013
PPRA	Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma
SCC	Masharti Maalumu ya Mkataba
Sh.	Shilingi
STD	Hati ya Kawaida ya Utoaji Zabuni
TBA	Wakala wa Majengo Tanzania
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TEMESA	Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania
WSDP	Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani

UTANGULIZI



Kwa heshima kubwa ninawasilisha Taarifa ya Ukaguzi ya Mwaka wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (Kama ilivyorekebishwa) na Kifungu namba 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008

Taarifa hii inaainisha kwa kifupi mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi pamoja na mapendekezo yaliyotolewa kwa ukaguzi wa taarifa za fedha na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, na Miongozo mbalimbali uliofanyika kwenye Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Matumizi ya Teknolojia yamechangia kuongezeka uwezo kwa Serikali za Mitaa katika usimamizi wa masuala ya kifedha, ikiwemo kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato ya ndani. Hata hivyo Serikali bado inachangia kwa kiwango kikubwa kwenye mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, na kuzipangia vipaumbele vyake. Kutokana na hilo, ukaguzi wangu umepitia kwa kina changamoto zinazozikumba Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kukusanya mapato pamoja na matatizo ya mifumo. Taarifa hii pia imeelezea kukosekana kwa ufanisi katika kusimamia matumizi, rasilimali watu, mali, udhibiti wa ndani pamoja na manunuzi.

Katika mwaka wa fedha wa 2019/20, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Ofisi yangu, tuliagiza kufanyika kwa kaguzi maalumu 72 zikiwa na Hadidu za Rejea, ambapo matokeo ya kaguzi hizo yameelezwa katika taarifa hii.

Ni matumaini yangu kuwa taarifa hii itawezesha kuongezeka kwa ufanisi katika matumizi ya rasilimali za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jukumu la Ofisi yangu litabaki kuwa ni kuhakikisha kuna uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama misingi ya kulinda ustawi wa jamii.

Charles E. Kichere,
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
28 Machi, 2021

SHUKRANI

Ni heshima kubwa kwangu kuweza kufanikisha jukumu langu la kikatiba la kuwasilisha ripoti kuu ya mwaka ya ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa wakati.

Nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na ninaahidi kutoa ushirikiano kamili kwa Serikali yake katika kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi kwa ajili ya kuboresha nchi yetu na maisha ya watanzania.

Aidha, ningependa pia kutambua msaada wa Marehemu, Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli Rais wa awamu ya Tano alioutoa kwa Ofisi yangu. Dkt Magufuli alikuwa mzalendo na kiongozi mkuu wa wakati wake. Ni kupitia msaada wake, Ofisi yangu iliweza kutimiza jukumu lake la kikatiba na kufanikisha dhamira yake ya kutoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu ambazo zinaboresha utendaji wa sekta ya umma, uwajibikaji, na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Roho yake ipumzike kwa amani.

Ningependa pia kulishukuru Bunge, hususan wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa(LAAC) kwa kuzifanyia kazi taarifa ninazozitoa na kuhakikisha kuwa mapendekezo yangu yanatekelezwa kwa nia ya kuboresha usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeendelea kuchukua jukumu muhimu katika kuboresha udhibiti wa ndani kwa kutoa miongozo ya mara kwa mara na kuongoza michakato ya kiutendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ikiwa ni matokeo ya mapendekezo yangu ya ukaguzi. Jitihada hizi zinathaminiwa sana.

Pia ninatoa shukrani kwa Maafisa Masuuli wote, menejimenti za taasisi zilizokaguliwa pamoja na wafanyakazi kwa ushirikiano uliotolewa wakati wote wa ukaguzi.

Kwa kuzingatia changamoto zilizokuwepo katika mwaka wa fedha 2019/20, kufanikiwa kwa ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kumetokana na juhudi za wafanyakazi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Ningependa kushukuru menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na wafanyakazi wote

waliofanya kazi kwa bidii, kwa kujitolea na kwa utulivu mkubwa katika kipindi chote cha mwaka kilichokuwa na changamoto kubwa.

Napenda pia kushukuru mashirika yasiyo ya kiserikali, Washirika wa Maendeleo, taasisi za kusimamia sheria ikiwa ni pamoja na TAKUKURU, na mashirika ya kitaalam na sekta pana ya umma, ambao walihusika katika kazi yetu, kwa msaada wao na ushirikiano katika kukamilisha ukaguzi wa mwaka huu, pamoja na wataalam anuwai ambao kwa namna mbalimbali walishirikiana nasi.

Ninatarajia ushirikiano endelevu kati ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na wadau wetu wote katika kaguzi zijazo.

MUHTASARI

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa kina wa matokeo, mapendekezo na hitimisho lililotokana na ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020. Maeneo yafuatayo yamejadiliwa kwa kina katika taarifa hii:

(i) Aina na Hali za Hati za Ukaguzi

Katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2020, nimekagua na kutoa hati kwa Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa. Kati ya Mamlaka hizo 185; halmashauri 124 sawa na asilimia 67 zilipata hati inayoridhisha, halmashauri 53 sawa na asilimia 29 zilipata hati zenye mashaka na halmashauri 8 sawa na asilimia 4 zilipata hati mbaya. Ingawa Mamlaka nyingi zimepata hati zinazoridhisha, bado kuna mapungufu mengi yaliyobainika yanayotokana na Mamlaka hizo kushindwa kufuata maagizo ya Bunge, Sheria, Kanuni, Sera za Serikali, na Miongozo mbalimbali. Hata hivyo, mapungufu haya hayakuwa na athari za moja kwa moja kwenye hesabu za mwisho zilizoletwa.

(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka ya Nyuma

Nikiwa natambua juhudi za Serikali, Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maafisa Masuuli katika utekelezaji wa mapendekezo yangu, bado hali ya utekelezaji wa mapendekezo inaonyesha kati ya mapendekezo ya jumla 15 niliyoyatoa katika taarifa yangu ya mwaka wa fedha 2018/19, mapendekezo 6 (40%) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, 5 (33%) hayajatekelezwa na 4 (27%) yamejirudia.

Aidha, kwa mapendekezo yaliyotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, jumla ya mapendekezo 6,607 yalitolewa katika mwaka wa fedha 2018/19. Hata hivyo, utekelezaji wake hauridhishi kwani mapendezo 2,875 (44%) kati ya mapendekezo yaliyotolewa hayakuwa yametekelezwa kikamilifu.

(iii) Maandalizi na Utekelezaji wa Bajeti

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapata fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato vikiwemo vyanzo vya ndani, Serikali, pamoja na misaada mbalimbali ya fedha za kujiendesha na fedha za maendeleo. Ukaguzi wangu wa utekelezaji wa Bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umebaini kuwa katika kipindi cha miaka mitano mfululizo, mapato ya ndani yamekuwa hayakusanywi kikamilifu huku fedha zinazotoka Serikali Kuu kwa

ajili ya matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo zikiwa kidogo. Katika mwaka wa fedha 2019/20, kiasi cha Sh. 50,333,856,397 (7%) kati ya bajeti ya mapato ya ndani ya Sh. 759,907,423,938 hakikukusanywa kutokana na mapungufu katika ukusanywaji wa mapato.

Ukaguzi pia ulibaini kuwa kiasi cha Sh. 410,417,526,825 kati ya bajeti ya Sh. 890,315,258,723 sawa na asilimia 46% ya fedha za maendeleo hakikupokelewa katika Halmashauri 152, huku kiasi cha Sh. 774,457,317,170 (18%) cha fedha za maendeleo kilitolewa kati ya Sh. 4,190,275,598,449 za bajeti katika Halmshauri 150. Kutokupokelewa kwa fedha hizi kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

(iv) Ukaguzi wa Hesabu za Halmashauri

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatengeneza taarifa zake za fedha ambazo zinajumuisha shughuli zote zilizofanyika katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2020 kwa mujibu wa Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Umma (IPSAS). Licha ya taarifa hizo kuwasilishwa kwangu kwa wakati, taarifa nyingi zilikuwa na makosa mengi ya kihasibu hali iliyopelekea kuwa na hati za ukaguzi zenye walakini.

(v) Tathmini ya Udhibiti wa Mifumo ya Ndani, Utawala Bora na Usimamizi wa Vihatarishi

Ukaguzi wangu wa tathmini ya vihatarishi vya udanganyifu uliofanywa kwenye Halmashauri 185 ulibaini kuwa Halmashauri 33 hazikufanya tathmini rasmi ya vihatarishi au kuhuisha tathmini iliyopo ya vihatarishi vya udanganyifu kutokana na kutowasilisha taarifa ya tathmini hiyo ilipoombwa kwa ajili ya ukaguzi; Halmashauri 22 hazikuandaa au kuhuisha kwa wakati rejesta ya vihatarishi.

Halmashauri 16 hazikuandaa na kupitisha sera ya usimamizi wa vihatarishi au mfumo; Halmashauri za wilaya 7 hazikutoa elimu juu ya sera yao ya vihatarishi kwa watumishi wote; Halmashauri 13 hazina utaratibu wa kimaandishi wa kutambua na kukabiliana na vihatarishi vya udanganyifu na vihatarishi vinginevyo.

Pia nilibaini mapungufu mbalimbali kama vile mifumo ya uhasibu inayotumiwa na Halmashauri kama EPICOR, FFARS, LGRCIS, GoT-HoMIS kutokuunganishwa ili kuweza kuwasiliana moja kwa moja; mfumo wa ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS) hauruhusu kupanga kwa

muda maalumu orodha ya wadaiwa wa fedha zilizokusanywa kupitia kifaa cha makusanyo (POS) na hivyo kuwa vigumu kuchambua wadaiwa kwa kuangalia muda wa deni lake. Mfumo wa uhasibu unaotumika yaani EPICOR unafanya kazi kama chombo cha kudhibiti mapato na malipo ya fedha taslimu tu na kushindwa kuripoti mapato na matumizi ambayo sio taslimu (accrual); Matumizi hafifu ya FFARS na GOT-HOMIS kwani sio moduli zote za mfumo zinatumika, hakuna mafunzo rasmi yaliyotolewa kwa watumiaji, ukosefu wa vifaa vya TEHAMA kwenye vituo vya afya, kukosekana kwa huduma ya mtandao ya uhakika na uhaba wa wataalamu wa TEHAMA katika Halmashauri.

(vi) Usimamizi wa Rasilimali-Watu na Mishahara

Rasilimali Watu ni kiungo muhimu katika kuongeza ufanisi na tija kwenye utoaji huduma wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Licha ya umuhimu wake, inakabiliwa na changamoto nyingi kama vile malimbikizo ya stahiki za watumishi kiasi cha Sh. 27,840,078,824; kutorejeshwa kwa Mishahara isiyolipwa kwa sababu mbalimbali kiasi cha Sh. 82,580,992. Pia nilibaini kuwa Watumishi 3,038 kutoka katika Halmashauri 35 walikuwa wakipokea mishahara chini ya theluthi moja, huku watumishi 7,992 kutoka katika Halmashauri 14 wakichelewa kupandishwa vyeo ingawa walikuwa na vigezo.

Nimeendelea kubaini upungufu wa watumishi kwani katika Halmshauri 123 nilibaini upungufu wa Watumishi 119,753; watumishi 510 katika Halmshauri 117 walikuwa kwenye nafasi za kukaimu kama Wakuu wa Idara na Vitengo kwa zaidi ya miezi 6, huku pia nikibaini kutokuhuishwa kwa taarifa za watumishi 612 kutoka kwenye Halmashauri 26 kwenye mfumo wa LAWSON. Nilibaini pia kuwa fedha zilizokatwa kutoka kwa watumishi kiasi cha Sh. 5,079,945,442 hazikuwasilishwa kwa taasisi husika. Nilibaini Halmshauri 10 kulipa kiasi cha Sh. 138,203,000 kwa watumishi ambao hawapo tena kwenye utumishi.

Vilevile, niliendelea kubaini udhaifu wa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo yanayohusiana na usimamizi wa rasilimali-watu na mishahara

(vii) Tathmini ya Miradi ya Maendeleo na Miradi Mingineyo

Nilibaini mapungufu mbalimbali katika miradi ya maendeleo na miradi mingineyo kama vile kutotumika kwa fedha zilizapangwa kutumika katika miradi husika kiasi cha Sh. 202,874,554,913 sawa na 20% ya fedha

zilizopaswa kutumika; miradi isiyokamilika yenye thamani Sh. 184,006,287,121 katika halmashauri 101; miradi ambayo haijatekelezwa yenye thamani Sh. 14,903,593,785; na miradi iliyokamilika lakini haitumiki yenye thamani ya Sh. 18,329,377,858.

Katika kupitia Mfuko wa Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu, nilibaini kuwa Mamlaka 82 za Serikali za Mitaa hazikuchangia kiasi cha Sh. 5,720,140,159 kwenye Mfuko kama inavyotakiwa kisheria; na kiasi cha Sh. 27,790,189,049 hakikukusanywa kutoka kwa wafaidika wa mikopo hiyo. Nilibaini pia kutotolewa kwa fedha zinazohusiana na fidia ya ada, vifaa na miundombinu pamoja na chakula kiasi cha Sh. 4,359,778,542, jambo linaloweza kuathiri utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo.

(viii) Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba

Mwenendo wa mapungufu katika manunuzi na kiasi cha fedha kilichohusika kwa kipindi cha miaka minne unaonesha maendeleo mazuri kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kufuata Sheria na taratibu mbalimbali, ukiacha mapungufu kwenye mikataba ya makubaliano kutoka GPSA ambayo imeonekana kuongezeka.

Nimeendelea kubaini matatizo yanayojirudia katika usimamizi wa mikataba, kama vile kasoro zilizobainika kwenye matumizi ya *force account*, kasoro ambazo zimeshindwa kutafutiwa ufumbuzi ingawa nimekuwa nikitoa mapendekezo mara kwa mara. Kwa mfano, nilibaini mikataba kwenye Halmashauri 8 yenye thamani ya Sh. 12,494,616,080 isiyokuwa na dhamana iliyotekelezwa kwa kutumia *force account*; na malipo ya Sh. 5,793,618,406 ambayo hayakuwa yamehakikiwa na mameneja wa miradi husika.

Pia kwa kupitia nyaraka mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2019/20, nilibaini kuwa kiasi cha Sh. 9,143,192,259 kililipwa na Halmshauri 57 katika manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali bila kuzingatia taratibu za ushindani.

(ix) Usimamizi wa Matumizi

Nilibaini kuwa Halmashauri 29 zilitumia kiasi cha Sh. 2,192,675,594 bila kuwa na tija; malipo ya Sh. 3,971,965,956 yaliyofanywa na Halmshauri 80 hayakuwa na viambatanisho vya kutosha kuhakiki usahihi wake; na Sh. 5,541,159,468 zililipwa kwa Halmashauri 58 kwa wauzaji wa bidhaa na watoa huduma mbalimbali, hata hivyo hapakuwa na risiti za kielektroniki (*EFD*).

Nilibaini pia kuwa, hadi tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya Halmashauri 11 hazikuwa zimehamisha kwenda RUWASA kiasi cha Sh. 1,115,088,297 kama fedha za *retention* iliyokatwa kutoka kwenye malipo yanayohusiana na miradi ya WSDP; huku Halmshauri 3 zikiwa hazijahamisha kwenda TARURA kiasi cha Sh. 242,253,572 cha fedha za *retention* zilizokatwa katika malipo ya mfuko wa barabara.

(x) Usimamizi wa Mapato

Tathmini yangu juu ya sera, mikakati na mifumo ya udhibiti wa ndani katika ukusanyaji wa mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ilibaini mapungufu kadhaa kama vile usimamizi hafifu wa mashine za kukusanyia mapato, kutokukusanywa kikamilifu kwa mapato kutoka vyanzo mbalimbali, ukosefu au kutohuishwa kwa sheria ndogondogo, kutosimikwa kwa mfumo wa kukusanyia mapato (GoT-HoMIS) katika vituo vya afya, mapato yaliyokusanywa lakini hayakuwasilishwa benki, kuwepo kwa miamala ambayo haijasuluhishwa, mapato kukusanywa nje ya mfumo, kutofautiana kwa mapato yaliyokusanywa baina ya taarifa na kuwepo kwa vitabu vya kukusanyia mapato ambavyo kwa sasa havistahili kutumika.

Nilipitia taarifa mbalimbali zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka 22 za Serikali za Mitaa na kubaini kuwa mapato kiasi cha Sh. 1,337,063,592 yatokanayo na leseni za biashara na vyanzo vinginevyo yalikusanywa nje ya mfumo wa mapato (LGRCIS). Pia, Mamlaka 135 za Serikali za Mitaa zilikusanya kiasi cha Sh. 18,769,299,624 kwa kutumia mashine za kukusanyia (POS) kutoka vyanzo mbalimbali, hata hivyo, fedha hizo hazikupelekwa Benki katika Akaunti za Halmshauri husika.

Pia nilipitia mikataba 18 iliyoingiwa baina ya Halmashauri na mawakala wa kukusanya mapato pamoja na taarifa kutoka kwenye mfumo wa mapato (LGRICS) na kubaini kuwa kiasi cha Sh. Sh. 2,345,843,498 kilikuwa kimekusanywa na Mawakala hao, hata hivyo, hakikuingizwa katika Akaunti za Benki za Halmshauri husika. Wakati nikipitia mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye mapato, nilibaini katika mfumo wa mapato wa Halmashauri 35 yenye jumla ya Sh. 4,792,502,078 iliyorekebishwa bila kuwa na viambatanisho wala idhini ya kufanya hivyo.

(xi) Usimamizi wa Mali za Kudumu

Nilipitia rejista ya dawa zilizoharibika na kubaini uwepo dawa zilizoharibika katika Halmshauri 31 zenye thamani ya Sh. 1,537,713,125 ambazo hazikuwa

zimeharibiwa, jambo ambalo linazidisha kiasi cha mali zilizoripotiwa kwenye hesabu. Pia, nilipopitia rejista ya mali na nilipokwenda kuzitembelea mali hizo zinazomilikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, nilibaini kuwa katika Mamlaka 113 za Serikali za Mitaa, jumla ya magari 727, pikipiki 138 na vifaa vingine kama kompyuta na samani zilikuwa ama hazitumiki, zimetelekezwa au hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu na Manejimenti husika hazikuwa na mpango wa kuzikarabati au kuziuza.

(xii) Matokeo ya Kaguzi Maalumu

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilifanya kaguzi maalumu 72 katika Mamlaka 67 za Serikali za Mitaa. Kati ya kaguzi hizo 72, 5 ziliombwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), 3 ziliombwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na 64 zilianzishwa na Ofisi yangu.

Kaguzi 64 zilizoanzishwa na Ofisi yangu zililenga kufichua ubadhirifu katika ukusanyaji wa mapato, kati ya hizo kaguzi 59 zilizingatia kipindi cha miaka mitatu ya fedha yaani 2017/18, 2018/19 na 2019/20. Kaguzi hizo pia ziliangalia utekelezaji wa miradi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kipindi hicho. Matokeo ya Kaguzi hizo kwa kila Halmshauri yamejadiliwa kwa kina katika Sura ya 13 ya taarifa hii.

SURA YA 1

USULI NA TAARIFA KWA UJUMLA

1.1 Utangulizi

Ripoti hii inawasilisha uchambuzi wa kina wa matokeo, mapendekezo, na hitimisho lililotokana na ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020. Ingawa idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa haijabadilika katika kipindi cha mwaka wa fedha uliokaguliwa, jina la Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero lilibadilishwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba kupitia Tangazo la Serikali Na. 75A lililochapishwa tarehe 31/01/2020.

Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 143(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 pamoja na Kifungu cha 45 cha Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya Mwaka 1982 (Iliyorekebishwa mwaka 2019).

Matokeo ya kina na mapendekezo yanayotokana na ukaguzi yameandikiwa taarifa rasmi na kupelekwa kwa kila halmashauri kwa ajili ya utekelezaji. Ripoti hii imejumuisha masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi na kuandikwa katika taarifa za halmashauri husika.

Halikadhalika, taarifa hii inajumuisha matokeo ya kaguzi maalumu zilizofanyika katika halmashauri 64 ambazo kati ya hizo kaguzi katika halmashauri 59 mawanda yake yalijumuisha kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 na ripoti ya matokeo ya kaguzi maalumu 8 zilizoombwa na Bunge pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

1.2 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kutoa maoni huru ya kikaguzi juu ya taarifa za fedha zinazoandaliwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa kujiridhisha iwapo taarifa hizo ziliandaliwa kulingana na Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Umma (IPSAS).

Halikadhalika, ukaguzi ulilenga kujiridhisha iwapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizingatia sheria na kanuni mbalimbali ikiweko Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 9 ya Mwaka 2011 na Kanuni zake wakati wa kutekeleza majukumu yao hususani michakato mbalimbali ya manunuzi. Lengo hili linaendana na Kiwango Na. 4000 cha Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi kinachonitaka kuwapa watumiaji wa taarifa maoni yangu juu ya taasisi nilizozikagua iwapo zinazingatia maamuzi ya Bunge, sera, sheria, na kanuni mbalimbali zilizopo kwa mujibu wa sheria.

1.3 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs), na taratibu zingine za ukaguzi kama ilivyoonekana inafaa kulingana na mazingira yaliyokuwepo. Hii ilijumisha tathmini ya mifumo ya uhasibu pamoja na mifumo ya udhibiti wa ndani katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ukaguzi ulifanyika kwa misingi ya sampuli; kwa hiyo matokeo ya ukaguzi yanategemea aina na kiasi cha nyaraka zilizoombwa na kuletwa kwangu kwa ajili ya ukaguzi. Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yaliyotolewa kutokana na uchunguzi wa taarifa za uhasibu, tathmini ya shughuli zilizofanyika, pamoja na tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani ambayo yanahitaji umakini na hatua za kuchukua yametolewa katika barua za mapungufu ambazo zimeandaliwa kwa kila halmashauri.

Ukaguzi wangu ulipangwa kwa namna ambayo ingeniwezesha kubaini dosari zenye madhara katika uandaaji wa taarifa za fedha zinazotokana na udanganyifu au makosa. Hata hivyo, ni jukumu la menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kutengeneza mifumo bora ya udhibiti wa ndani itakayowezesha kuzuia au kubaini dosari zote katika uandaaji wa hesabu zitokanazo na udanganyifu au makosa.

Mchanganuo wa Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni kama ilivyoorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 1-1**.

Jedwali Na. 1-1: Idadi ya Halmashauri Zilizokaguliwa Mwaka 2019/20

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Halmashauri
1.	Halmashauri za Jiji	6
2.	Halmashauri za Manispaa	20
3.	Halmashauri za Miji	22
4.	Halmashauri za Wilaya	137
Jumla		**185**

1.4 Mbinu za Ukaguzi

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni mwanachama wa taasisi za kitaaluma (INTOSAI, AFROSAI na AFROSAI-E) na inatumia viwango na miongozo mbalimbali inayotolewa na taasisi hizo. INTOSAI hutoa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) katika sekta ya umma. Viwango hivi vya ukaguzi vinataka wakaguzi kuzingatia maadili, kupanga, na kufanya ukaguzi ili kupata uthibitisho kuwa taarifa za fedha hazina dosari zinazosababishwa na udanganyifu au makosa.

Ukaguzi wangu ulijikita katika taratibu za kikaguzi ili kupata uthibitisho wa kutosha na sahihi juu ya taarifa za fedha zilizowasilishwa. Taratibu zilizozingatiwa ni pamoja na kukagua sera za uhasibu zilizotumika, kutathmini makadirio ya kiuhasibu yaliyofanywa na menejimenti, na kutathmini kwa ujumla uwasilishaji wa taarifa za fedha.

Pia, nilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa matokeo ya kaguzi za miaka ya nyuma na mapendekezo niliyoyatoa, pamoja na maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ili kujiridhisha kuwa hatua stahiki zilichukuliwa na menejimenti kwa kuzingatia mambo yote yaliyoibuliwa.

1.5 Mchakato wa Kuandaa Taarifa

Mchakato wa ukaguzi hufuata mbinu shirikishi, ambapo taasisi zinazokaguliwa zinashirikishwa kikamilifu wakati wa mchakato wa ukaguzi. Ukaguzi shirikishi unahusisha maofisa masuuli, maofisa waandamizi, kamati za ukaguzi, na vitengo vya ukaguzi wa ndani. Ninaamini kuwa wadau hawa wana nafasi nzuri zaidi ya kutoa majibu thabiti kuhusu usahihi wa taarifa za fedha na nyaraka zingine muhimu kwa ajili ya ukaguzi, ikijumuisha uzingatiaji wa sheria na kanuni.

Vilevile, matokeo ya ukaguzi yanazingatia zaidi vigezo vilivyowekwa au taratibu zilizozoeleka na kupendekeza hatua za kuchukua ili kuboresha

uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa; hili hufanyika kupitia barua za mapungufu zinazotolewa kwa kila Mamlaka ya serikali za mitaa.

Halikadhalika, ninatoa maoni ya ukaguzi yanayoonesha masuala muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha, uzingatiaji wa sheria na kanuni pamoja na mapungufu yaliyobainika kwenye mifumo ya udhibiti wa ndani.

1.6 Maandalizi na Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha

Kifungu cha 43 cha Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa Na.9 ya Mwaka 1982 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2019) kinazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutunza vitabu vya hesabu na kumbukumbu zinazohusu mapato na matumizi, miamala mingine, pamoja na mali na madeni ya Mamlaka hizo.

Halikadhalika, Agizo la 31(1) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linamtaka ofisa masuuli kuandaa taarifa za fedha za mwisho na kuzipeleka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi kabla au tarehe 30 Septemba ya kila mwaka. Agizo hilohilo linazitaka menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa taarifa za fedha kwa mujibu wa sheria, kanuni, na maagizo yaliyotolewa na waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa, Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.

SURA YA 2

AINA NA MWENENDO WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

2.1 Utangulizi na Maana ya Hati za Ukaguzi

Madhumuni ya ukaguzi wa taarifa za fedha ni kuwahakikishia watumiaji[1] wa taarifa hizo iwapo kwa ujumla wake taarifa hizo hazina mapungufu makubwa yaliyosababishwa na udanganyifu au yaliyotokea bila kukusudia. Hakikisho hilo hutolewa kwa kutoa hati za ukaguzi zinazokuwa kwenye ripoti ya ukaguzi.[2]

Hivyo, hati ya ukaguzi ni taarifa fupi inayoeleza wazi maoni juu ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha. Hati hiyo hutolewa baada ya mkaguzi kupata uhakika wa kutosha[3] kuwa taarifa za fedha kwa ujumla wake hazina mapungufu makubwa yaliyosababishwa na udanganyifu au bahati mbaya. Mkaguzi hujiridhisha na usahihi wa taarifa hizo pale ambapo amepata ushahidi wa kutosha kuhusiana na ukaguzi uliofanyika ili kujiridhisha kuwa hati zinazotolewa ni sahihi na zinaakisi hali halisi ya ukaguzi uliofanyika.

Kwa mujibu wa matakwa ya Aya za 11 na 12 za Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi[4] (ISSAI 2700), ili kutoa hati sahihi za ukaguzi, mkaguzi anatakiwa kujielekeza kwenye kujiridhisha iwapo uandaaji wa taarifa za fedha ulizingatia mahitaji ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma pamoja na sera za uhasibu zilizokubalika na taasisi husika, sera za uhasibu zilizotumika ni sahihi na zinaendana na matakwa ya viwango vya uhasibu vilivyokubalika na kama sheria na miongozo mbalimbali

---

[1] *Bunge, vyombo vya usimamizi vyenye dhamana ya kusimamia na umma kwa ujumla.*

[2] *Ripoti ya ukaguzi ni zao la mwisho la mchakato mzima wa ukaguzi, ambayo inaandaliwa kwa kuzingatia ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi.*

3 Uhakika wa kutosha ni kiwango cha juu cha uhakika lakini haimaanishi kwamba ukaguzi uliofanywa kwa mujibu wa ISSAIs utagundua mapungufu yaliyopo.

4 Kutoa hati za ukaguzi na kutoa ripoti kuhusu taarifa za fedha

imezingatiwa. Pia, kujiridhisha na uhalisia wa makadirio ya kihasibu, ukamilifu wa taarifa zilizowasilishwa pamoja na vielelezo vyake, ukubwa wa mapungufu yaliyobainika na madhara yake, na kama taarifa zilizopo kwenye taarifa za fedha ni sahihi, zinalinganishika na zinaeleweka. Vilevile, ukaguzi ulijikita katika kuangalia ubora wa taarifa zilizoandaliwa na kama kulikuwa na viashiria vyovyote vya mapungufu kwenye maamuzi ya menejimenti ya taasisi zilizokaguliwa.

Hati nilizozitoa zilifikiwa kutokana na maamuzi ya kitaalamu baada ya tathmini ya madhara ya mapungufu yaliyobainika ambayo hayakurekebishwa ikilinganishwa na ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi.

Mapungufu yanaweza kutokea kutokana na udanganyifu au bila kukusudia; na mapungufu hayo huchukuliwa kuwa makubwa ikiwa, pungufu moja moja au mapungufu mbalimbali yakijumuishwa pamoja, yanaweza kuathiri maamuzi ya watumiaji wa taarifa za fedha.

Agizo la Utendaji Na. 3 la Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi linatambua kuwa, malengo ya ukaguzi wa taarifa za fedha katika taasisi za umma ni mapana zaidi ya kutoa hati za ukaguzi juu ya usahihi wa taarifa hizo. Pia, Kifungu cha 26 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 kinataka katika ukaguzi wangu wa taarifa za fedha kukagua pia ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani; taratibu za manunuzi ya umma; uzingatiaji wa sheria, kanuni, na miongozo mbalimbali; na kuangalia jambo jingine lolote nitakaloona linafaa kukaguliwa. Vilevile, Kifungu cha 48(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 kinanitaka kutoa taarifa kwenye ripoti yangu ya ukaguzi iwapo manunuzi ya bidhaa, huduma, na kazi za ujenzi yalifanyika kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa kwenye Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2013 (zilizorekebishwa mwaka 2016).

Kwa mantiki hiyo, malengo ya ukaguzi wangu ni kuwaaminisha watumiaji wa taarifa za fedha juu ya usahihi wa taarifa hizo na uzingatiaji wa sheria na kanuni mbalimbali ambazo zinaathiri moja kwa moja uandaaji wa taarifa za fedha na zile ambazo haziathiri kwa mujibu wa Kifungu cha 26 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2011 pamoja na zile ambazo ni sehemu ya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria unaofanywa na Ofisi yangu. Mapungufu yanayobainika kutokana na kutozingatia sheria yanaelezwa kwenye ripoti yangu chini ya kichwa cha habari, “Ripoti ya Masuala Mengine ya Kisheria na Masharti ya Udhibitl”. Kupitia ripoti zangu zenye taarifa kuhusiana na

maeneo tajwa hapo juu, Ofisi yangu inachochea uwajibikaji na utawala bora kwa wale waliopewa dhamana ya kusimamia rasilimali za umma.

2.2 Aina za Hati za Ukaguzi Zilizotolewa[5]

Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 700 na 705), aina nne za hati za ukaguzi zinaweza kutolewa ni hati inayoridhisha, hati yenye shaka, hati mbaya na kushindwa kutoa maoni. Pia, kwa mujibu wa Aya za 16 na 17 za Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 700) na Aya ya 5B ya Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 705), aina hizi nne za Hati za ukaguzi zimewekwa kwenye makundi mawili makubwa. Kundi la kwanza lina aina moja ya hati inayoridhisha na kundi la pili linajumuisha hati yenye shaka, hati mbaya na kushindwa kutoa hati. Aina hizi za hati hutolewa kulingana na hali halisi ya ukaguzi, yaani kulingana na tathmini ya ukubwa wa mapungufu yaliyobainika ambapo menejimenti ya halmashauri husika imeshindwa kuyarekebisha madhara ya mapungufu hayo wakati wa ukaguzi. Maelezo ya kina kuhusiana na aina za ukaguzi na sababu zinazopelekea hati hizo kutolewa ni kama yalivyoahinishwa hapo chini.

2.2.1 Hati Inayoridhisha

Aina hii ya hati hutolewa baada ya kujiridhisha kuwa, kutokana na ushahidi uliokusanywa wakati wa ukaguzi, halmashauri zilizokaguliwa zimeandaa taarifa zao za fedha kwa usahihi kwa kuzingatia vigezo vyote vinavyotumika vya uandaaji wa taarifa za fedha, yaani Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma pamoja na miongozo mingine

[5] *Mwaka huu majina ya hati za Ukaguzi yamebadilika. Kwa miaka iliyopita, "Adverse Opinion" illiitwa "Hati Isiyoridhisha" na "Disclaimer of Opinion" iliitwa "Hati Mbaya". Kwa mwaka huu, "Adverse Opinion" imeitwa "Hati Mbaya" na "Disclaimer of Opinion" imeitwa "Kushindwa kutoa Maoni". Mabadiliko haya yametokea kwa kuzingatia kuwa majina mapya yanaakisi zaidi maana halisi ya hati zilizotolewa.*

ikiwemo waraka wa uandaaji wa taarifa za fedha uliotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali. Hii inamaanisha kuwa taarifa za fedha zilizoandaliwa zinajitosheleza, zinaelezea sera zote za uhasibu zilizokubaliwa, na sera hizo zimeandaliwa kuendana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma, makisio ya kihasibu yaliyofanywa na menejimenti yana mantiki, taarifa zimeandaliwa kwa usahihi na zinalinganishika na zinaeleweka. Kwa maana nyingine, taarifa za fedha zilizoandaliwa na kukaguliwa hazina mapungufu makubwa, na taarifa na vielelezo vyote muhimu viliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Hati hii inajulikana zaidi kwa jina la hati safi, na inatazamiwa kuwa halmashauri zote zinajitahidi na kuwa na kiu ya kupata hati hii kwani inaonesha usimamizi imara wa masuala ya kifedha unaotokana na ufanisi mkubwa wa mfumo wa udhibiti wa ndani.

Kwa mwaka ulioshia tarehe 30 Juni 2020, kati ya halmashauri 185 zilizokagualiwa, halmashauri 124 (67%) zimepata hati inayoridhisha. Idadi hii inaonesha kupungua kwa taasisi zilizopata hati inayoridhisha kwa asilimia 30 ikilinganishwa na hati zinazoridhisha zilizotolewa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019. Kupungua huku kulisababishwa na menejimenti za halmashauri kutozingatia kikamilifu na kuhakikisha uwepo wa mfumo imara wa usimamizi wa fedha za umma. Halmashauri hazikuwa na utaratibu madhubuti wa kuhakikisha uhifadhi wa nyaraka zote za kifedha, kuweka kumbukumbu za miamala katika akauti sahihi, kutofanya usuluhisho wa akaunti na taarifa mbalimbali kila mara, na kutokuwepo kwa usimamizi mzuri (utaratibu wa uhakiki ubora) wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha.

Utoaji wa hati zinazoridhisha ulitokana na jitihada kubwa za Ofisi yangu, kwani taarifa nyingi za fedha zilizopokelewa kufikia tarehe ya mwisho ya kuwasilisha taarifa hizo yaani tarehe 30 Septemba 2020, pamoja na marekebisho yake yaliyofuata, zilikuwa na makosa mengi ambapo ililazimu kutumia muda mwingi (taarifa kurudishwa mara kwa mara kwa wakaguliwa kwa kuwa marekebisho ya makosa yalikuwa yanazalisha makosa mapya) wa ukaguzi katika kujaribu kuhakikisha makosa hayo yanarekebishwa na menejimenti ya halmashauri husika. Kumekuwa na mazoea ya wakaguliwa wetu kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi ili kuwahi tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa taarifa za fedha pasipo kuzingatia ubora wa taarifa hizo na hivyo kutegemea ofisi yangu ibaini mapungufu ili wao wayarekebishe na hatimaye wapate hati zinazoridhisha kupitia jitihada za Ofisi yangu. Mazoea haya hayakubaliki, na taasisi husika zinapaswa kuachana nao mara moja, na badala yake, zijiridhishe kuwa hesabu

zinazoandaliwa zinakidhi viwango vilivyowekwa kabla ya kuziwasilisha kwangu kwa ajili ya ukaguzi.

Baadhi ya mapungufu yaliyobainika na baada ya jitihada kubwa za Ofisi yangu, halmashauri husika zilifanikiwa kuyarekebisha ni kama ifuatavyo:

- ✓ Viwango vya uchakavu wa mali, mitambo na vifaa vilivyokuwa vimetumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha za awali vilitofautiana na viwango vilivyotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kupitia Waraka Na. EG.3/102/106 wa tarehe 13 Septemba 2017. Pia, baada ya kuhoji viwango vilivyotumika, halmashauri zilifanya marekebisho kwenye sera zake za uhasibu zilizokuwa sehemu ya taarifa za fedha zilizowasilishwa bila ya kuvitumia katika kufanya marekebisho ya thamani ya mali, mitambo, na vifaa kwenye taarifa za fedha zilizowasilishwa, jambo ambalo lililazimu taarifa hizo kurudishwa tena kwa ajili ya marekebisho;

- ✓ Makosa katika bakaa za kuanzia hasa kwenye mali, mitambo na vifaa. Vilevile, kiasi cha fedha katika maeneo kadhaa kilichoripotiwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2019 kilitofautiana na kiasi kilichooneshwa mwaka huu ulioshia tarehe 30 Juni 2020 na hakukuwa na maelezo yaliyotolewa kwenye taarifa za fedha kuhusiana na uhalali wa tofauti hizo;

- ✓ Kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha hakikuwa na maelezo kuhusu undani wa gharama hizo. Kulikuwa na changamoto kubwa katika kutafuta kiasi cha malipo na makusanyo kwa ajili ya uandaaji wa taarifa ya mtiriko wa fedha kutokea kwenye matumizi na mapato yaliyoripotiwa kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha;

- ✓ Taarifa nyingi za fedha zilizowasilishwa hazikuwa na taarifa ya usuluhisho kati ya faida au hasara halisi na mtiririko halisi wa fedha kutoka kwenye shughuli za kawaida kulingana na matakwa ya Waraka Na.EG.3/102/05/03/009 wa tarehe 8 Mei 2020 kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali;

- ✓ Halmashauri nyingi ziliandaa na kutekeleza sera za uhasibu zinazopingana na matakwa ya Kiwango Na.23 cha Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma, kwenye utambuzi wa ruzuku ya Serikali. Sera iliyokuwa inatumika ilikuwa kwa mujibu wa Kiwango na 20 cha Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu, badala ya

Kiwango Na. 23 cha Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma,

- ✓ Taarifa nyingi za fedha zilizowasilishwa hazikuonesha ujira wa menejimenti na madiwani kwa mujibu wa matakwa ya Kiwango Na. 20 cha Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma,

- ✓ Kulikuwa na ukinzani wa kiasi cha fedha kilichooneshwa kwenye jalada la taarifa za fedha na kiasi kilichooneshwa kwenye maelezo;

- ✓ Baadhi ya vipengele vilivyoripotiwa kwenye taarifa za fedha, kwa mfano, madai, madeni, na mikopo havikuwa na majedwali na vielelezo ili kujiridhisha na usahihi wa vipengele hivyo;

- ✓ Taarifa nyingi za fedha zilizowasilishwa zilikuwa na makosa mengi ya uhariri, uandishi wa vichwa vya habari, kuchanganya miaka ya taarifa za fedha, kutumia nukuu za sheria zisizo sahihi, na kutumia sheria na kanuni zilizopitwa na wakati (hazitumiki tena).

Vilevile, pamoja na kuwa halmashauri hizo zimepata hati inayoridhisha, nilibaini mapungufu mengine yanayotokana na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani hasa kwenye kushindwa kufuata matakwa ya sheria na miongozo mbalimbali ambapo mapungufu hayo hayakuwa na madhara ya moja kwa moja kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa. Mapungufu hayo yameripotiwa kwenye barua za mapungufu zilizowasilishwa kwa halmashauri husika pamoja na ripoti ya ukaguzi. Orodha ya halmashauri zilizopata hati inayoridhisha ni kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 2.1**

2.2.2 Hati Zenye Shaka


Kuna mazingira mbalimbali yanayopelekea utoaji wa hati zenye kasoro. Kuna pale ambapo mkaguzi anatakiwa kuongeza aya ya masuala ya mkazo au aya ya masuala mengine kwenye ripoti ya ukaguzi kwa mujibu wa matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Ugaguzi (ISA 706) *(masuala yenye mkazo na masuala mengine yamefafanuliwa zaidi kwenye aya ya 2.5.1 & 2.5.2 hapo chini)*. Kwa upande mwingine, kuna mazingira ambayo yanapelekea tathmini yenye madhara kwenye taarifa za fedha kwa mujibu wa matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 705) ambapo mkaguzi huhitimisha kuwa taarifa za fedha kwa ujumla wake zina makosa makubwa yaliyosababishwa ama na menejimenti ya halmashauri husika

kushindwa kufikia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa hizo[6] au kushindwa kupata ushahidi wa kutosha. Hivyo, kulingana na ukubwa na madhara ya makosa ambayo hayakurekebishwa, aina tatu za hati zinazoweza kutolewa ni hati yenye shaka, hati mbaya, na kushindwa kutoa maoni (hati mbaya).

Kama ilivyoelezwa hapo juu, ili kuhakikisha hati zinazotolewa ni sahihi, inahitaji maamuzi juu ya aina ya makosa yaliyobainika ambayo hayakurekebishwa na madhara yaliyojitokeza au yanayoweza kujitokeza kutokana na makosa hayo. **Mchoro Na. 2-1** unaelezea kwa ufupi mazingira na ukubwa wa madhara ya mapungufu yanayopelekea maamuzi ya utoaji wa hati za ukaguzi tajwa hapo juu.

6 Kutokana na kutotumia kwa usahihi Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma na sera za uhasibu wakati wa kuandaa taarifa za fedha au kutoa taarifa juu ya kiasi cha miamala kisicho sahihi kwenye taarifa za fedha.

Mchoro Na. 2-1: Mazingira Yanayopelekea Utoaji wa Hati za Ukaguzi



2.2.2.1 Hati Yenye Shaka

Hati hii hutolewa pale ambapo nimejiridhisha kuwa, kulingana na ushahidi uliopatikana, taarifa za fedha zilizokaguliwa zina makosa makubwa, ama kwa kutozingatia ipasavyo viwango vya kimataifa vya uhasibu pamoja na sera za uhasibu au kulikuwa na kushindwa kukidhi mawanda ya ukaguzi kutokana na kutopatikana kwa nyaraka zote zilizohitajika ili kufanikisha malengo ya ukaguzi lakini makosa hayo hayakuwa na madhara makubwa kiasi cha taarifa hizo kwa ujumla wake kushindwa kutumika katika kufanya maamuzi. Hii inamaanisha kuwa makosa hayo au madhara ya kushindwa kupata ushahidi wa kutosha yamejikita kwenye baadhi ya maeneo ya taarifa za fedha lakini sehemu kubwa ya taarifa hizo zimeandaliwa kwa usahihina zinaonesha hali halisi ya utendaji wa halmashauri husika, ndiyo maana hati hii pia hujulikana kama 'kizuizi cha maoni ya ukaguzi".

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, nimetoa jumla ya hati zenye shaka kwenye taarifa za fedha za halmashauri 53 (29%). Hii ilichangiwa kwa kiasi kukubwa na mambo yafuatayo:

- ✓ Kutofuatwa kwa usahihi matakwa ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha pamoja na sera za uhasibu; na makosa ya kimahesabu ambayo halmashauri husika zilishindwa kuyarekebisha pamoja na jitihada kubwa za Ofisi yangu kuhakikisha makosa hayo yanarekebishwa wakati wa ukaguzi;

- ✓ Baadhi ya masuala yaliyooneshwa kwenye taarifa za fedha hazikuwa zimeambatishwa na vielelezo muhimu kama vile hati za malipo, hati za madai, hati za kupokea/kuwasilisha vifaa, dhamana za manunuzi, hati za kutolea vifaa, na leja za vifaa, jambo ambalo lilisababisha kushindwa kukidhi mawanda ya ukaguzi wangu;

- ✓ Baadhi ya halmashauri kushindwa kutekeleza matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma hasa kwenye eneo la kufanya majaribio ya kuangalia iwapo mali (madai) zimepoteza thamani kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma, 29;

- ✓ Baadhi ya halmashauri kushindwa kufanya mapitio ya muda wa matumizi wa mali za kudumu kila mwisho wa mwaka kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma, 17 na

Waraka Na. No.EG.3/102/02/03 wa tarehe 28 Mei 2019 kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali. Matokeo yake, halmashauri hizo zimekuwa na mali zilizoisha muda wake wa matumizi lakini bado zilikuwa zinatumika;

- ✓ Kutofautiana kwa kiasi kilichoripotiwa kwenye jalada la taarifa za fedha na kiasi kilichopo kwenye maelezo;

Orodha ya halmashauri zilizopata hati yenye shaka na sababu za kupata hati hiyo zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2-2.**

2.2.2.2 Hati Mbaya

Hati hii hutolewa pale ambapo nimejiridhisha kuwa, kulingana na ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi, taarifa za fedha zilizokaguliwa zina makosa makubwa na yaliyoathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha, hivyo kupelekea taarifa hizo kutokuwa sahihi. Hii inamaanisha kuwa tofauti na hati yenye shaka, taarifa za fedha zilizoandaliwa zina makosa makubwa yatokanayo na kutokukubaliana au kushindwa kukidhi mawanda na makosa hayo hayajajikita sehemu moja bali yameathiri maeneo mengi katika taarifa za fedha na hivyo kuathiri kueleweka kwa taarifa hizo kwa watumiaji wake kwa ajili ya kufanyia maamuzi.

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, nimetoa hati mbaya kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 8. Orodha na halmashauri zilizopata hati mbaya na sababu zilizopelekea hati hizo zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 2-3.**

2.2.2.3 Kushindwa Kutoa Maoni


Mazingira ya ukaguzi yanaweza kupelekea kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi. Hii inatokea pale ambapo nimeshindwa kupata ushahidi wa kutosha au taarifa muhimu ili kufikia malengo ya ukaguzi, na endapo madhara ya kushindwa kupata ushahidi au nyaraka hizo ni makubwa sana. Hivyo, ninaonesha kwenye ripoti yangu ya ukaguzi kuwa kutokana na ukubwa wa madhara yaliyopo au yanayoweza kutokea kutokana na kukosa ushahidi wa kutosha, nimeshindwa kutoa maoni ya ukaguzi.

Kama ilivyo kwa hati mbaya, ninaposhindwa kutoa maoni, maana yake ni kuwa sehemu kubwa ya kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha

hakiaminiki hivyo taarifa za fedha zilizokaguliwa hazifai kwa ajili ya kufanyia maamuzi mbalimbali.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020, hakukuwa na halmashauri yeyote niliyoshidwa kutoa maoni ya ukaguzi. **Mchoro Na. 1-2** unaonesha kwa ufupi aina na kiasi cha hati ambazo nimezitoa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020.

Mchoro Na. 2-2: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka 2019/20



2.3 Msingi wa Hati za Ukaguzi

Ili kufikia kwenye hati nilizozitoa, nilizingatia hali halisi ya matokeo ya ukaguzi kwa kila mkaguliwa. Ukaguzi wangu ulifanyika kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguizi (ISSAIs). Viwango hivyo vinanitaka kuandaa mpango wa ukaguzi, kufanya ukaguzi, na kutoa ripoti ya matokeo ya ukaguzi huo. Pia, vinanitaka kufuata maadili ya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa ukaguzi uliofanyika una ubora unaokubalika kwa hali ya juu. Ukaguzi ulijumuisha uchunguzi wa nyaraka mbalimbali zinazohusiana na kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha. Pia, ulijumuisha tathmini ya makadirio na maamuzi yaliyofanywa na menejimenti ya halmashauri husika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha, utoshelezi wa mambo yaliporipotiwa kwenye taarifa za fedha, iwapo sera za uhasibu zinazotumika zinaendana na mazingira halisi ya utekelezaji wa majukumu ya mkaguliwa na kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya

Uhasibu katika Sekta ya Umma, na kama sera hizo zinajitosheleza na zimekuwa zikitumika mwaka hadi mwaka.

Kaguzi zilizofanyika zilipangwa na kutekelezwa kwa namna ambayo iliwezesha ukusanyaji wa taarifa zote muhimu na maelezo ya menejimenti yaliyokuwa yanahitajika ili kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa nyaraka kwa ajili ya kutoa uhakika wa kutosha iwapo taarifa za fedha zilizokaguliwa hazina mapungufu makubwa yaliyosababishwa na ubadhirifu au kwa bahati mbaya.

Nilifanya ukaguzi wangu kwa uhuru na sikuwa na mgongano wa maslahi na taasisi yoyote niliyoikaguwa kwa mujibu wa kanuni za maadili zilizotolewa na Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Maadili kwa Wahasibu pamoja na Kanuni za Maadili zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania na nilitekeleza wajibu wangu wa kimaadili kwa mujibu wa matakwa hayo.

Ni imani yangu kuwa ushahidi nilioupata ulikuwa sahihi na ulijitosheleza katika kutoa hati za ukaguzi na pale ambapo nilishindwa kupata ushahidi wa kutosha sikutoa hati za ukaguzi.

2.4 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Miaka Minne

Kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2-1** hapa chini, kwa ujumla, utendaji wa halmashauri kwenye ubora wa taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020 si mzuri ikilinganishwa na taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa miaka mitatu mfululizo ya nyuma. Idadi ya halmashauri zilizopata hati inayoridhisha imeshuka kwa halmashauri 52 kwa mwaka wa fedha 2018/19. Kutokana na kushuka huko, kumepelekea ongezeko la idadi ya halmashauri zilizopata hati yenye shaka na hati mbaya.

Jedwali Na. 2-1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Mwaka Huu Na Miaka Mitatu Mfululizo Iliyopita

Mwaka wa Fedha	Hati Inayoridhisha	Hati Yenye Shaka	Hati Mbaya	Kushindwa Kutoa Maoni	Jumla ya Hati
2019/20	124	53	8	0	185
2018/19	176	9	0	0	185
2017/18	176	7	1	1	185
2016/17	166	16	3	0	185

Licha ya utendaji huo usioridhisha, halmashauri 102 (55%) zimeendelea kupata hati inayoridhisha kwa miaka minne mfululizo; ninazipongeza sana na ninazitia moyo kuendelea na jitihada hizo ili kujihakikishia usimamizi madhubuti wa masuala ya kifedha. Orodha ya halmashauri hizo imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 2-4.**

Vilevile, halamashauri tano (5) zilijitahidi kujiimarisha kutoka kwenye hati mbaya zilizopata kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019 na kupata hati yenye shaka au kutoka hati yenye shaka na kupata hati inayoridhisha kwa mwaka huu kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 2-2** hapa chini.

Jedwali Na. 2-2: Orodha ya Halmashauri Zilizojiimarisha Kutoka Hati mbaya na Kupata Hati Yenye Shaka au Kutoka Hati Yenye Shaka na Kupata Hati Inayoridhisha Mwaka Huu

Na.	Jina la Halmashauri	Aina ya Hati Iliyotolewa Mwaka Jana	Hati Iliyotolewa Mwaka Huu
1	Halmashauri ya Wilaya ya Karatu	Yenye Shaka	Inayoridhisha
2	Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama	Yenye Shaka	Inayoridhisha
3	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	Yenye Shaka	Inayoridhisha
4	Halmashauri ya Manispaa ya Songea	Yenye Shaka	Inayoridhisha
5	Halmashauri ya Wilaya ya Handeni	Yenye Shaka	Inayoridhisha

Hata hivyo, baadhi ya halmashauri zimeendelea kuwa na mwelekeo wa hati za ukaguzi usioridhisha, ambapo halmashauri 3 zimeendelea kupata hati yenye shaka ikilinganishwa na mwaka jana, wakati halmashauri 50 zimeporomoka kutoka kupata hati inayoridhisha mwaka jana na kupata hati yenye shaka mwaka huu. Halmashauri 7 zimeporomoka kutoka hati inayoridhisha mwaka jana na kupata hati mbaya mwaka huu na halmashauri 1 imeporomoka kutoka hati yenye shaka mwaka jana na kupata hati mbaya mwaka huu ulioishia tarehe 30 Juni 2020.

Mchanganuo kamili wa hati za ukaguzi kwa miaka minne mfululizo umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 2-4**.

2.5 Matakwa Mengine ya Kutoa Ripoti

Aidha, mbali na utoaji wa hati za ukaguzi kwa mujibu wa matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 700 an ISA 705), 'Maagizo ya Utendaji' kwenye viwango hivyo imetoa matakwa ya ziada wakati wa kuandaa ripoti ya ukaguzi kwa lengo la kutoa angalizo kwa watumiaji wa taarifa za fedha na namna ukaguzi ulivyofanyika ili kuongeza uelewa wa

taarifa za fedha zilizokaguliwa. Matakwa hayo ni pamoja na kutoa taarifa juu ya mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi kwa mujibu wa Kiwango cha 701 cha Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi, kuwa na aya ya masuala ya mkazo na masuala mengine kwenye taarifa ya ukaguzi kwa mujibu wa Kiwango cha 706 cha Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi, na wajibu wa mkaguzi kuhusiana na taarifa zingine kwa mujibu wa Kiwango cha 720 cha Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi.

Vilevile, Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vinatambua majukumu ya ziada ya kuripoti wakati wa ukaguzi kulingana na matakwa ya sheria na kanuni za nchi mbalimbali. Kwa maana hiyo, Kifungu cha 48(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011, kinanitaka kueleza kwenye ripoti yangu ya ukaguzi kila mwaka iwapo manunuzi ya bidhaa, huduma na kazi za ujenzi yalifanyika kwa kufuata taratibu zilizopo kwenye Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016).

Ili kuendana na matakwa hayo, matakwa yote muhimu[7] yamezingatiwa kwenye ripoti yangu ya ukaguzi, wakati matakwa mengine yaliyobaki (masuala ya mkazo na masuala mengine) yamewekwa pale ambapo ilikuwa ni muhimu kufanya hivyo. Maelezo ya kina kuhusiana na matakwa hayo ni kama ifuatavyo.

2.5.1 Masuala ya Mkazo

Aya yenye masuala ya mkazo inawekwa kwenye kila ripoti ya ukaguzi wa halmashauri husika ili kutoa angalizo kwa watumiaji wa taarifa za fedha juu ya masuala ambayo ingawa yameoneshwa kwa usahihi kabisa kwenye taarifa za fedha, masuala hayo yalichukuliwa kuwa muhimu sana kwa watumiaji wa taarifa hizo kuyafahamu ili waweze kuzielewa vizuri zaidi[8] taarifa za fedha zilizokaguliwa. Masuala ambayo yana vigezo vya kuripotiwa kwenye aya hii ni pamoja na shaka kubwa kuhusiana na uwezo wa taasisi kuendelea kutoa huduma kwa miezi 12 ijayo kuanzia mwisho wa mwaka wa fedha husika; kubadilisha mara kwa mara kwa viwango vya uhasibu vya uandaaji wa taarifa za fedha; shaka kuhusiana na matokeo ya siku zijazo ya mashauri ya madai yaliyopo mahakamani; na kuanza kutumia viwango vipya vya uhasibu

7 Aya husika zinatakiwa kuwekwa hata kama mkaguzi hana chochote cha kuripoti.
8 Aya ya 8 ya Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 706.8)

mapema kabla ya muda rasmi wa kuanza kutumika. Masuala mengine ni taarifa zinazohusiana na wakaguzi wengine; kuonesha kutofautiana kwa kiasi kikubwa na taarifa zingine zilizopo kwenye ripoti ya kifedha ya mwaka ambapo halmashauri husika inatakiwa kufanya marekebisho lakini haikufanya hivyo; na kuonesha mabadiliko kwenye taarifa za fedha zilizotolewa kwa miaka ya nyuma na matukio baada ya kipindi cha taarifa za fedha.

Kuwepo kwa aya ya masuala ya msisitizo kwenye ripoti ya ukaguzi hakuathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa. Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020, nimejumuisha aya yenye masuala ya msisitizo kwenye ripoti 93 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 2-3.**

Jedwali Na. 2-3: Mchanganuo wa Halmashauri Zilizokuwa na Aya Yenye Masuala ya Msisitizo Kwenye Ripoti Yake ya Ukaguzi

Aina ya Hati ya Ukaguzi	Idadi ya Halmashauri/Ripoti Zenye Aya ya Masuala ya Mkazo
Hati Inayoridhisha	75
Hati Yenye Shaka	16
Hati Mbaya	2
Kushindwa Kutoa Maoni	0
Jumla	**93**

Orodha ya halmashauri zilizokuwa na aya ya masuala ya mkazo kwenye ripoti zake za ukaguzi ni kama zilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 2-5.**

2.5.2 Masuala mengine

Aya yenye masuala mengine inajumuishwa kwenye ripoti ya ukaguzi ili kutoa taarifa juu ya masuala ambayo hayapo kwenye taarifa za fedha lakini ni muhimu kuyaweka kwenye ripoti ya ukaguzi ili watumiaji waweze kuelewa ukaguzi, wajibu wa mkaguguzi au ripoti ya mkaguzi[9]. Masuala hayo ni pamoja na masharti au zuio kwenye ugawaji wa ripoti ya ukaguzi (yaani, taarifa za fedha ambazo ripoti yake ya ukaguzi imeandaliwa kwa ajili ya matumizi au madhumuni maalumu); pale ambapo sheria na viwango vya uhasibu vilivyotumika vinamtaka mkaguzi kutekeleza majukumu mengine; pale ambapo mkaguzi anashindwa kujitoa kwenye zoezi la ukaguzi hata

[9] *Aya ya 10 ya Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 706.10)*

kama madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na kushindwa kupata nyaraka toshelezi zinazotakiwa ni makubwa sana (kuelezea sababu za kushindwa kujitoa kwenye zoezi la ukaguzi); mapungufu kwenye mfumo wa udhibiti wa ndani; na mambo ya kiutawala na masuala yanayohusu ukiukaji wa sheria ambayo hayana madhara ya moja kwa moja kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa.

Kuwepo kwa aya ya masuala mengine kwenye ripoti ya ukaguzi hakuathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa. Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020, sikuwa na aya yenye masuala mengine kwenye ripoti zangu za ukaguzi.

2.5.3 Masuala Muhimu ya Ukaguzi

Masuala muhimu ya ukaguzi ni yale ambayo, kulingana na maamuzi yangu ya kiweledi, yalikuwa ya muhimu sana wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha kwa kipindi husika. Masuala hayo yalifanyiwa kazi (yalisuluhishwa) katika mazingira niliyokuwa ninafanyia ukaguzi wangu wa taarifa za fedha kwa ujumla wake na kutoa hati za ukaguzi kwa taarifa hizo, ila sikutoa hati inayojitegemea kuhusiana na masuala hayo. Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, sikuwa masuala muhimu ya kuripoti.

2.5.4 Taarifa Nyingine

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 720) pamoja na ‘maagizo ya utendaji’ yanataka aya inayotokana na upitiaji wa taarifa zingine ijumuishwe kwenye ripoti ya ukaguzi. Taarifa zingine zinajumuisha ripoti za madiwani, maelezo ya ziada yaliyojumuishwa kwenye taarifa za fedha, na tamko la mkuu wa idara ya fedha lililopo kwenye taarifa za fedha. Menejimenti ya halmashauri iliyokaguliwa inawajibika na taarifa zingine zilizopo kwenye taarifa za fedha.

Kama mkaguzi, ninatakiwa kusoma taarifa zingine zilizopo kwenye taarifa za fedha. Kwa kufanya hivyo, ninajiridhisha iwapo taarifa hizo zinakinzana kwa kiasi kikubwa na taarifa za fedha au taarifa hizo ni tofauti na uelewa wangu nilioupata wakati wa ukaguzi; au vinginevyo, zinaonekana kuwa na mapungufu makubwa na ninatakiwa kuripoti kikamilifu. Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, sikuwa na chochote cha kuripoti kuhusiana na taarifa zingine.

2.5.5 Uchambuzi wa Utekelezaji na Usimamizi wa Sheria

Aya ya 43 ya Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 700) inatoa mwongozo kwa wakaguzi juu ya majukumu yao ya kutoa taarifa kulingana na matakwa ya sheria na miongozo ya nchi husika. Pia, Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 kinanitaka kueleza kwenye ripoti yangu ya kila mwaka ya ukaguzi iwapo taasisi nilizozikagua zilitekeleza matakwa ya sheria na kanuni za manunuzi ya umma. Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 200, nilikagua mchakato wa manunuzi wa kila halmashauri kwa lengo la kujiridhisha juu ya utekelezaji wa Sheria ya Manunuizi ya Umma ya Mwaka 2011 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016). Halmashauri zote 185 nilizozikagua ukiachilia mapungufu niliyobainisha katika Sura ya 9 ya Ripoti hii, kwa ujumla wake, zilitekeleza matakwa ya sheria na kanuni za manunuzi ya umma.

SURA YA 3

HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI YA MIAKA ILIYOPITA

3.0 Utangulizi

Nimekamilisha ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya miaka iliyopita ili kubaini iwapo Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na maofisa masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wamechukua hatua za kutekeleza mapendekezo niliyoyatoa kwa mwaka 2018/19.

Ili kuhakikisha uwepo wa mfumo wa udhibiti wa ndani ulio thabiti, menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kutathmini na kuchukua hatua zinazofaa kushughulikia matokeo ya ukaguzi na mapendekezo kwa wakati muafaka.

Aidha, kama sehemu ya majukumu yake ya usimamizi, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa inafanya vikao na kufuatilia mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na maofisa masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanachukua hatua stahiki za kutekeleza mapendekezo yangu ya ukaguzi na maagizo ya Kamati yanayotolewa mara kwa mara.

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka ya nyuma na maagizo ya Kamati yanachambuliwa katika aya zinazofuata.

3.1 Mlipaji Mkuu wa Serikali Kuchelewa Kutekeleza Mapendekezo Yaliyotolewa


Kifungu cha 40(2)(b) na (4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008 kinanitaka kujumuisha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita katika ripoti yangu ya ukaguzi inayofuata baada ya kuwasilishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Ninampongeza Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ufuatiliaji na utekelezaji wa maagizo yangu, kwani majibu ya Serikali ya ripoti kuu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2018/19 yalipokelewa kupitia barua yenye Kumb. Na.CHA.116/474/01/57 ya tarehe 2 Julai 2020.

Tathmini yangu juu ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo yangu inaonesha kwamba, katika mapendekezo 15 ambayo yalitolewa katika mwaka wa fedha 2018/19, mapendekezo 6 sawa na asilimia 40 yametekelezwa; mapendekezo 5 sawa na asilimia 33 hayakutekelezwa, na mapendekezo 4 sawa na asilimia 27 yalirudiwa katika ripoti ya ukaguzi ya mwaka huu.

Hali na mwenendo wa utekelezaji wa mapendekezo kwa miaka mitatu mfululizo ni kama inavyooneshwa katika **Mchoro Na. 3-1** hapa chini; na hali ya utekelezaji kwa mwaka 2018/19 imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3-1** cha ripoti hii.

Mchoro Na. 3-1: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Serikali



Pamoja na juhudi zinazofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ninayoyatoa, bado kuna haja ya kuzingatia kuwa, muda unaotumika katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotajwa ufupishwe ili kuhakikisha kuwa kasoro zilizobainika zinashughulikiwa mara moja. Kushindwa kuchukua hatua kwa wakati dhidi ya mapendekezo yangu kunaweza kusababisha kujirudia kwa udhaifu kama huo katika miaka inayofuata.

Kama ilivyooneshwa kwenye **Mchoro Na. 3-1**, mapendekezo manne ambayo yalitolewa katika mwaka wa fedha wa 2018/19 yamerudiwa katika ripoti yangu ya sasa. Aidha, utekelezaji usio timilifu wa mapendekezo yangu umeongezeka ikilinganishwa na hali ya utekelezaji wa mwaka uliopita.

Ninapendekeza kuwa, Mlipaji Mkuu wa Serikali atekeleze kwa wakati mapendekezo ya ukaguzi yanayotolewa na kuhakikisha kuwa mapungufu yote yaliyotajwa katika ripoti zilizotangulia yanarekebishwa.

3.2 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2018/19

Kwa mujibu wa Kanuni ya 93 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009, kila ofisa masuuli wa taasisi iliyokaguliwa anatakiwa kuandaa majibu ya ripoti yake ya ukaguzi na kuiwasilisha ndani ya kipindi cha siku 21 tangu tarehe ambayo ripoti kuu imewasilishwa mbele ya Bunge.

Tathmini yangu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa mwaka 2018/19 imeonesha kuwa, jumla ya mapendekezo 6,607 yalitolewa. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo hayo hairidhishi kwani mapendekezo 2,875 sawa na asilimia 44, utekelezaji wake haukuwa timilifu na haukufanyika kwa wakati; na mapendekezo 1,257 sawa na asilimi 20 yamerudiwa tena katika mwaka huu. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa mwaka 2018/19 ni kama inavyoainishwa katika **Jedwali Na. 3-1** na kuoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3-2** cha ripoti hii.

Jedwali Na. 3-1: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwa Mwaka 2018/19

Hali ya mapendekezo	2018/19
Yametekelezwa	2,275
Utekelezaji unaendelea	1,782
Hayajatekelezwa	1,093
Yamejirudia katika mwaka 2019/20	1,257
Yamepitwa na wakati	200
Jumla ya mapendekezo	**6,607**

Ninatoa wito kwa maofisa masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa, mapendekezo yote yaliyosalia yanafanyiwa kazi kwa wakati bila kuchelewa.

3.3 Mapendekezo Ambayo Utekelezaji Wake Umekuwa Ukiendelea kwa Muda Mrefu

Uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo yangu kwa miaka iliyopita umebaini kuwa, Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa hazitekelezi mapendekezo yanayotolewa kama inavyopaswa.

Nilibaini kuwa kuna mapendekezo ambayo utekelezaji wake umekuwa ukiendelea kwa kipindi cha hadi miaka kumi toka tarehe ya kutoa mapendekezo hayo. Maofisa masuuli wamekuwa wakiwasilisha majibu ambayo hayaondoi udhaifu uliotajwa na hivyo kusababisha utekelezaji wa mapendekezo usiokamilika.

Katika mapendekezo yaliyotolewa tangu mwaka 2006/07 hadi 2017/18, mapendekezo 1,594 kutoka Mamlaka 170 za Serikali za Mitaa yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji, na mengi ya mapendekezo ambayo utekelezaji wake umekuwa wa muda mrefu ni yale yanayohusu marejesho ya mishahara iliyolipwa kwa watu wasio katika utumishi yaani watumishi hewa.

Mifano michache ni kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 3-2** na orodha ya kina ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na idadi ya mapendekezo yameoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3-3** cha ripoti hii.

Jedwali Na. 3-2: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Utekelezaji wa Mapendekezo Unaoendelea kwa Kipindi cha Miaka Miwili Hadi Kumi

Jina	Muhtasari wa Hoja	Mwaka wa Kutoa Pendekezo
H/Jiji Dodoma	**2.2.6.3 Mishahara yenye thamani ya Sh. 6,205,215 iliyolipwa kwa watumishi waliostaafu** Kiasi hicho cha fedha kinatakiwa kirejeshwe Hazina	2008/09
	2.2.11.1 Malipo ya mishahara yenye thamani ya Sh. 4,989,681 kwa wasio watumishi Menejimenti ya halmashauri inatakiwa kusimamia orodha ya walipwa mishahara ili kuhakiki usahihi wa mishahara inayotakiwa kulipwa. Pia, halmashauri inapaswa kurejesha kiasi hicho chote kilicholipwa kama mshahara pamoja na makato yake ya kisheria yaliyokatwa isivyostahili.	2009/10
	2.2.11.3 Sh. 50,830,735 ambazo ni mishahara iliyozuiwa ambayo haikurejeshwa Hazina	2009/10

Jina	Muhtasari wa Hoja	Mwaka wa Kutoa Pendekezo
	Fedha hizo zirejeshwe Hazina kwa kupitia Hazina ndogo Dodoma	
	2.2.12.1 Kukosekana kwa hati miliki Halmashauri inashauriwa kutafuta hatimiliki za majengo yote kama yanavyoonekana katika hesabu zao za mwisho ili kuhalalisha umiliki wao.	2009/10
H/M Ilala	**2.2.14.1 Malipo ya awali ya Sh. 364,534,000 kwenda MEATCO ambayo utendaji wake haujaanza, kiasi hicho hakikurejeshwa** Halmashauri ifuatilie kwa karibu utaratibu wote wa mambo ya kuzingatia kuhusu ukiukwaji wa mkataba na kiasi husika kiweze kulipwa kwa Halmashauri.	2009/10

Ninapendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia sekretarieti za mikoa na OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa, mapendekezo yote ambayo utekelezaji wake umekuwa endelevu kwa muda mrefu, yajibiwe na kutekelezwa kwa ukamilifu.

3.4 Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Mapendekezo Yaliyokaa Bila Kutekelezwa kwa Muda Mrefu

Nilibaini mapendekezo 1,231 yaliyotolewa kati ya mwaka wa fedha 2006/07 na 2017/18 katika Mamlaka 137 za Serikali za Mitaa hayajatekelezwa kwa kipindi cha hadi miaka 10. Pia, nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika hazikuwa na mipango-mkakati ya utekelezaji wa mapendekezo hayo ya ukaguzi kwa kipindi hicho.

Licha ya wito wa mara kwa mara kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutakiwa kutekeleza mapendekezo hayo, bado hali ya utekelzaji si ya kuridhisha. Muhtasari wa masuala muhimu kwa kipindi cha hadi miaka 10 ambayo yanahitaji utekelezaji wa haraka yameoneshwa kwenye **Jedwali Na. 3-3.** Pia, orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na idadi ya mapendekezo yasiyotekelezwa hadi miaka 10 imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3-4**.

Jedwali Na. 3-3: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Mapendekezo Yasiyotekelezwa Hadi Miaka 10

Jina	Muhtasari wa Hoja	Mwaka wa Kutoa Pendekezo
H/W Bukoba	3.2.2 Mapato ya ndani ya kiasi cha Sh. 2,400,000 ambayo hayakuwasilishwa na mawakala wa kukusanya mapato Halmashauri ikusanye fedha hizo kutoka kwa mawakala wa mapato	2006/07
	2.2.7.1 Fedha Sh. 9,045,000 zilizokusanywa na wakala wa mapato lakini hazikuwasilishwa Halmashauri ihakikishe kuwa wakusanya mapato wanarejesha fedha na kuingizwa katika akaunti za Halmashauri mara moja	2009/10
H/W Sikonge	Kiasi cha Sh. 58,345,000 cha fedha za makusanyo ya ndani ambacho hakijawasilishwa na mawakala Halmashauri ifuatilie mawakala wote waliokusanya mapato hayo na kuhakikisha yanaingizwa katika akaunti za halmashauri. Pia, adhabu za kimkataba zichukuliwe dhidi ya mawakala kwa kuvunja makubaliano ya mkataba.	2009/10
H/W Karatu	2.2.9.4 Fedha Sh. 61,891,594.80 za ujenzi usioridhisha wa bwalo la chakula na ukumbi wa mikutano katika Kituo cha Walimu Ayalabe Halmashauri isimamie usawazishaji wa eneo la mradi, kurekebisha ujenzi wa msingi, na marekebisho ya kuta na sakafu. Aidha, ujenzi wake ukamilishwe haraka iwezekanavyo.	2009/10
	Fedha Sh. 66,123,990 za ujenzi wa hosteli na nyumba ya mganga katika Kituo cha Walimu Ayalabe Uongozi wa Halmashauri uhakikishe kuwa hosteli na nyumba ya mganga vinaanza kutumika.	2009/10

Kushindwa kutekeleza kwa wakati mapendekezo ya ukaguzi yaliyoibuliwa kunaashiria kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapata hasara ya mapato ambayo hayakuwasilishwa, kuwa na miradi isiyokamilika kwa muda mrefu, pamoja na kushindwa kwa udhibiti wa ndani hasa katika eneo la usimamizi wa amana.

Ninapendekeza Sekretarieti za Mikoa na OR-TAMISEMI kuchukua hatua stahiki kwa Mamlaka 137 za Serikali za Mitaa zenye mapendekezo ya

ukaguzi ya muda mrefu na kuhakikisha kuwa hatua za uboreshaji zinachukuliwa.

3.5 Hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Kifungu cha 40(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa na Marekebisho Namba 1 ya Mwaka 2013) kinamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali na maofisa masuuli kuzingatia hoja na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Tathmini ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa hadi mwaka wa fedha 2018/19 ilibainisha kuwa, kati ya maagizo 811 yaliyotolewa na Kamati katika Mamlaka 151 za Serikali za Mitaa, maagizo 350 sawa na asilimi 43 yalitekelezwa; maagizo 278 sawa na asilimia 34 utekelezaji ulikuwa unaendelea; maagizo 161 sawa na asilimia 20 yalikuwa hayajatekelezwa; na maagizo 22 sawa na asilimia 3 yalipitwa na wakati kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 3-4** hapa chini na kuorodheshwa katika **Kiambatisho Na. 3-5** cha ripoti hii.

Jedwali Na. 3-4: Hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Halmashauri	Idadi ya Maagizo	Yaliyotekelezwa	Utekelezaji Unaende	Hayajatekelezwa	Yamepitwa na Wakati
2018/19	151	811	350	278	161	22
2017/18	158	958	388	274	281	16
2016/17	138	882	391	322	169	0
2015/16	115	748	233	256	259	0

Mwelekeo wa miaka minne mfululizo unaonesha kuwa, maagizo yaliyotekelezwa ni chini ya asilimia 45 ya maagizo yaliyotolewa. Hii inamaanisha kuwa, zaidi ya asilimia 55 ya maagizo yaliyotolewa hayakutekelezwa kwa wakati.

Vilevile, nilibaini Mamlaka 4 za Serikali za Mitaa zenye maagizo ya muda mrefu ambayo bado hayajatekelezwa. Maagizo hayo yametolewa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2011/12 hadi 2013/14 na hadi mwaka huu 2019/20 maagizo hayo hayajatekelezwa kabisa na mengine yapo katika hatua ya utekelezaji. **Jedwali Na. 3-5** hapa chini linaonesha baadhi ya maagizo hayo.

Jedwali Na. 3-5: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Maagizo ya Muda Mrefu Ambayo Hayajatekelezwa

Jina	Maagizo	Hali ya Utekelezaji	Mwaka
H/W Mkuranga	Kamati iliiagiza menejimenti ya Halmashauri kufanya ufuatiliaji wa magari 2 yaliyoibwa na kuchukua hatua stahiki kwa watumishi waliohusika.	Halijatekelezwa.	2011/12
H/W Bahi	Halmashauri iliagizwa kuhamisha Sh. 131,264,757 kwenda vijijini ikiwa ni asilimia 20 ya fedha za ruzuku ya fidia kwa vyanzo vya mapato vilivyofutwa.	Utekelezaji unaendelea.	2011/12
	Halmashauri iliagizwa kulipa madeni yake yote kiasi cha Sh. 407, 011,317 iliyokuwa inadaiwa	Utekelezaji unaendelea.	2011/12
	Halmashauri iliagizwa kujibu hoja zote za ukaguzi.	Utekelezaji unaendelea	2011/12
H/W Biharamulo	Halmashauri iliagizwa kuhakikisha kuwa inaongeza ukusanyaji wa mapato yake ya ndani na kufikia asilimia 25 ya uwezo wake wa kujiendesha bila kutegemea ruzuku toka Serikali kuu au ufadhili wowote.	Utekelezaji unaendelea	2011/12
	Halmashauri iliagizwa ndani ya miaka 2 ya fedha iwe imehamisha kiasi cha Sh. 97,529,920 ikiwa ni asilimia 20 ya fedha za ruzuku ya fidia kwa vyanzo vya mapato vilivyofutwa.	Utekelezaji unaendelea	2011/12
H/W Korogwe	Halmashauri iliagizwa kuhamisha fedha kiasi cha Sh. 87,194,100 ikiwa ni asilimia 20 ya ya fedha za ruzuku ya fidia kwa vyanzo vya mapato vilivyofutwa katika vipindi vya mwaka 2006/2007 na 2008/09, kabla ya tarehe 31 Desemba 2009.	Utekelezaji unaendelea	2013/14
	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliagizwa kufanya ukaguzi maalumu wa ujenzi wa Soko la Kimataifa la Makuyuni. Pia, Halmashauri iliagizwa kuandaa mpango wa biashara wa soko hilo.	Halijatekelezwa	2013/14

Ninatoa wito kwa maofisa masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye maagizo ambayo hayajatekelezwa kuchukua hatua za haraka na za makusudi kuhakikisha kuwa maagizo yote yanatekelezwa bila kuchelewa na taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

SURA YA 4

MAANDALIZI YA BAJETI NA UTEKELEZAJI WAKE

4.0 Utangulizi

Sura hii inalenga kueleza matokeo ya ukaguzi kuhusu utekelezaji wa mipango na bajeti za Mamlaka ya serikali za mitaa; na ukusanyaji na matumizi yenye ufanisi ya fedha zilizopatikana kutokana na mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani, ruzuku kutoka serikali kuu, pamoja na misaada kutoka kwa wahisani na wadau wa maendeleo.

4.1 Mtazamo wa Jumla wa Bajeti

Bajeti iliyoidhinishwa maana yake ni Mamlaka ya matumizi inayotokana na sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya serikali, na maamuzi mengine yanayohusiana na mapato yaliyotarajiwa au yatakayopokelewa katika kipindi cha bajeti. Nchini Tanzania, Serikali huandaa bajeti kwa msingi wa uwepo wa fedha taslimu wakati taarifa za kifedha huandaliwa kwa msingi wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma.

Kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2019) kinazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa muda usiopungua miezi miwili kabla ya kila mwanzo wa mwaka wa fedha, katika kikao maalumu, kupitisha bajeti ya makadirio ikionesha kiasi cha mapato kinachotarajiwa kupokelewa; kiasi kinachotarajiwa kutolewa na Mamlaka katika mwaka wa fedha husika; na kukiwa na ulazima Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kupitisha bajeti za ziada katika mwaka wa fedha husika.

Mfumo wa Upangaji wa Matumizi ya Fedha kwa Muda kwa kawaida huandaliwa kila mwaka kwa kulinganisha miaka miwili inayofuatana ili kuona iwapo inaendana na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano II, sera, pamoja na mikakati ya kitaifa. Ukaguzi wa bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/20 umeonesha mapungufu mbalimbali kama yanavyoelezwa hapa chini.

4.1.1 Mwenendo wa Mapato ya Ndani Ikilinganishwa na Bajeti Iliyoidhinishwa kwa Miaka Mitano Mfululizo

Mapato ya ndani yanajumuisha kodi za ndani, ada, tozo, ushuru, vibali vya ujenzi, na mapato mengineyo. Fedha hizi ni sehemu ya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ukiachia ruzuku inayotolewa na Serikali Kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, nilitathmini Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa ambazo kulingana na taarifa za fedha zilizowasilishwa, zilifanikiwa kukusanya jumla ya Sh. 709,573,567,541 kutoka vyanzo vyake vya ndani ikilinganishwa na bajeti ya Sh. 759,907,423,938 ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha Sh. 50,333,856,397 sawa na asilimia 7 ya bajeti iliyopitishwa. **Kiambatisho Na. 4-1** na **Jedwali Na. 4-1** hapa chini linaonesha mwenendo wa makusanyo ya mapato ikilinganishwa na bajeti kwa muda wa miaka mitano mfululizo.

Jedwali Na. 4-1: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato Ikilinganishwa na Bajeti Iliyoidhinishwa

Mwaka wa Fedha	Bajeti Iliyoidhinishwa (Sh.)	Makusanyo Halisi (Sh.)	Tofauti (Sh.)	%
2019/20	759,907,423,938	709,573,567,541	(50,333,856,397)	7
2018/19	725,633,451,671	639,401,151,405	(86,232,300,266)	11
2017/18	677,965,549,714	566,729,291,189	(111,236,258,525)	16
2016/17	628,045,048,644	523,564,835,716	(104,480,212,928)	17
2015/16	536,203,527,158	482,898,501,332	(53,305,025,824)	10

Jedwali Na. 4-1 linaonesha kuwa, kwa miaka mitano mfululizo, kumekuwa na upungufu wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa.

4.1.2 Mwenendo wa Mapato Yatokanayo na Vyanzo vya Ndani Ikilinganishwa na Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida

Ruzuku ya matumizi ya kawaida inahusisha fedha za uendeshaji wa shughuli za kila siku ikijumuisha malipo ya mishahara ya watumishi, na manunuzi ya vifaa na huduma mtambuka ambapo chanzo cha fedha ni ruzuku ya matumizi ya kawaida kutoka Serikali kuu na makusanyo ya ndani.

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2019/20, Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa zilikusanya jumla ya Sh. 709,573,567,541 kutokana na vyanzo vya ndani na kuwa na matumizi ya kawaida ya jumla ya Sh. 4,773,489,160,809. Maelezo zaidi yametolewa katika **Kiambatisho Na. 4-2**.

Jedwali Na. 4-2 linaonesha kwa ufupi mwenendo wa makusanyo ya mapato ya ndani ikilinganishwa na matumizi ya kawaida kwa miaka mitano.

Jedwali Na. 4-2: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato ya Ndani Ikilinganishwa na Matumizi ya Kawaida

Mwaka wa Fedha	Makusanyo Halisi (Sh.)	Matumizi ya Kawaida (Sh.)	Asilimia ya Kujitegemea
2019/20	709,573,567,541	4,773,489,160,809	15
2018/19	639,401,151,405	4,139,568,491,180	15
2017/18	566,729,291,189	4,373,555,868,608	13
2016/17	523,564,835,716	4,656,643,395,963	11
2015/16	482,898,501,334	4,453,470,809,033	11

Jedwali Na. 4-2 linaonesha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kujitegemea kwa wastani wa asilimia 15 tu kwa matumizi ya kawaida, ikiashiria kuwa asilimia 85 ya matumizi ya kawaida hutegemea ruzuku toka Serikali kuu. Kwa hali hii, Mamlaka za Serikali za Mitaa haziwezi kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi na huenda zikashindwa kutimiza majukumu ya msingi ya kutoa huduma kwa jamii endapo ruzuku ya Serikali kuu itasitishwa.

Aidha, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilifanikiwa kupata makusanyo ya ndani zaidi ya ruzuku ya kawaida toka Serikali Kuu kwa kiasi cha Sh. 13,106,263,432 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.4-3** hapa chini.

Jedwali Na. 4-3: Kiwango cha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kujitegemea kwa Matumizi ya Kawaida

Jina la Halmashauri	Kiasi Kilichokusanywa (Sh.)	Matumizi ya Kawaida (Sh.)	Tofauti (Sh.)	% ya kujitegemea
H/jiji Dar es Salaam	16,520,316,583	3,414,053,151	13,106,263,432	484

Ninashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza makusanyo ya ndani kwa kutanua wigo wa vyanzo vya makusanyo ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali kuu.

4.2 Makusanyo ya Vyanzo vya Mapato ya Ndani

Katika mwaka wa fedha 2019/20, ukaguzi wa Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa katika vyanzo vyake vya mapato ya ndani ulibaini mambo yafuatayo.

4.2.1 Makusanyo Pungufu Yatokanayo na Vyanzo vya Ndani Sh. 98,613,186,963

Katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya Mamlaka 123 za Serikali za Mitaa zilikadiria kukusanya Sh. 442,034,532,275 kutoka kwenye vyanzo vya mapato ya ndani lakini ziliweza kukusanya Sh. 343,421,345,312 hivyo kuwa na upungufu wa Sh. 98,613,186,963 sawa na asilimia 22 ya makisio ya mapato ya ndani kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 4-3**.

Jedwali Na. 4-4 hapa chini linaonesha kiwango cha upungufu kwa asilimia cha makusanyo ya mapato ya vyanzo vya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Jedwali Na. 4-4: Asilimia ya Makusanyo Pungufu Kutoka Vyanzo vya Mapato ya Ndani

Kiwango cha Asilimia	Idadi ya Halmashauri		
	2019/20	2018/19	2017/18
81-90	-	2	-
61-80	1-	5	5
41-60	15	23	22
21-40	40	39	44
01-20	67	57	80

Nina shaka na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo makusanyo yake yapo kwa kiwango cha chini kulingana na kiasi cha makisio kwa kiwango cha asilimia kati ya 21-40 na zaidi.

Hali hii inaashiria kuwa, kuna uwezekano mapato haya kutokusanywa kutoka kwenye vyanzo vyote vya ndani, hivyo kusababisha kutokutekelezwa kwa wakati shughuli zilizopangwa kwa kutumia mapato ya ndani.

Ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kutimiza malengo yenye tija, ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchambua na kubainisha vyanzo vipya vya mapato ikiwa pamoja na: a) kuweka kanzidata za taarifa za biashara; b) kuanzisha biashara za ubia na sekta binafsi; na

c) kutathmini vyanzo vya kodi/ushuru kwa nia ya kuhamasisha utekelezaji wa sheria kwa hiari.

4.2.2 Makusanyo ya Sh. 48,279,330,566 ya Mapato ya Ndani Zaidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Mamlaka 62 za Serikali za Mitaa zilifanikiwa kukusanya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani kiasi cha Sh. 363,859,170,229 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. 315,579,839,663 hivyo kuwa na ziada ya Sh. 48,279,330,566 sawa na asilimia 15 ya bajeti iliyopitishwa kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 4-4**.

Wakati ninasisitiza jitihada zifanyike, ninashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha mchakato wa kutengeneza bajeti zinazozingatia uhalisia na kuhuisha mara kwa mara taarifa za vyanzo vya mapato ya ndani ili ziendane na uhalisia.

4.3 Kiwango cha Ruzuku Kilichotolewa Zaidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Ukaguzi wangu katika mwaka wa fedha 2019/20, masuala mawili yalibainika kuhusiana na kiwango cha ruzuku kinachotolewa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa ambayo ni ruzuku za miradi ya maendeleo zilizopokelewa zaidi ya bajeti; na ruzuku ya matumizi ya kawaida zilizopokelewa zaidi ya bajeti kama inavyoelezwa hapa chini.

4.3.1 Ruzuku za Miradi ya Maendeleo za Thamani ya Sh. 20,047,551,253

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Mamlaka 29 za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa bajeti ya miradi ya maendeleo ya jumla ya Sh. 67,272,409,002. Hata hivyo, kiasi cha Sh. 87,319,960,255 kilipokelewa na kufanya ziada ya kiasi cha Sh. 20,047,551,253 sawa na asilimia 30 ya bajeti iliyoidhinishwa kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 4-5**.

4.3.2 Ruzuku za Matumizi ya Kawaida za Sh. 62,411,302,499 Zilizopokelewa Zaidi ya Bajeti

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Mamlaka 35 za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa bajeti ya matumizi ya kawaida ya jumla ya Sh. 868,358,072,467. Hata hivyo, kiasi cha Sh. 930,769,374,966 kilipokelewa na kufanya ziada ya jumla ya Sh. 62,411,302,499 sawa na asilimia 15 ya jumla ya makisio kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 4-6**.

Kutolewa kwa fedha zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kunaweza kusababisha kiasi kilichozidi kutumika kutekeleza shughuli ambazo hazikuwa kwenye mpango wala bajeti.

Ninaishauri Serikali kupitia Hazina kupeleka fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa. Endapo kutakuwa na fedha zaidi zimepelekwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, zipate idhini kutoka kwenye mamlaka husika kabla ya kufanyika matumizi ya fedha hizo. Kwa kuzingatia kuwa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipokea fedha pungufu kulingana na bajeti zao, ninasisitiza Serikali kuchunguza sababu za kupeleka fedha zaidi ili kuthibitisha kwamba hakuna miamala yenye ubadhirifu.

4.4 Kiasi cha Fedha Kilichotolewa Pungufu ya Bajeti

Ukaguzi wangu katika mwaka wa fedha 2019/20, masuala mawili yalibainika kuhusiana na kiasi cha fedha kilichotolewa pungufu ya bajeti, ambayo ni fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa; na ruzuku za matumizi ya kawaida zilizopokelewa pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa kama inavyofafanuliwa Zaidi hapa chini.

4.4.1 Fedha za Miradi ya Maendeleo Ambazo Hazikupokelewa Sh. 410,417,526,825

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Mamlaka 152 za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa jumla ya Sh. 890,315,258,723 za ruzuku ya matumizi ya maendeleo. Katika ukaguzi nilioufanya, nilibaini kuwa kiasi kilichopokelewa ni Sh. 479,897,731,898 kukiwa na upungufu wa Sh. 410,417,526,825 sawa na asilimia 46 ya bajeti iliyoidhinishwa. **Jedwali Na. 4-5** hapa chini linaonesha mwenendo wa fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazikupokelewa kwa miaka mitano mfululizo.

Jedwali Na. 4-5: Mwenendo wa Fedha za Maendeleo Ambazo Hazikupokelewa

Mwaka wa Fedha	Bajeti ya Maendeleo (Sh.)	Kiasi Kilichopokelewa (Sh.)	Pungufu (Sh.)	%	Idadi ya Halmashauri
2019/20	890,315,258,723	479,897,731,898	410,417,526,825	46	152
2018/19	1,185,489,718,682	628,636,740,919	556,852,977,763	47	157
2017/18	977,228,000,000	497,282,000,000	480,007,000,000	49	156
2016/17	1,034,123,000,000	501,908,000,000	532,214,000,000	51	167
2015/16	1,010,650,000,000	390,525,000,000	620,124,000,000	61	151

Kwa mujibu wa **Jedwali Na. 4-5** hapo juu, upungufu wa fedha za miradi ya maendeleo ni asilimia 46. Mamlaka 73 za Serikali za Mitaa ziliathirika zaidi kwani zilipokea chini ya asilimia 46 ya bajeti ya ruzuku za maendeleo kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 4-7** cha ripoti hii.

4.4.2 Ruzuku za Matumizi ya Kawaida Zilizopokelewa Pungufu ya Bajeti Iliyoidhinishwa Sh. 774,457,317,170

Katika mwaka wa fedha 2019/20, bajeti iliyoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida katika Mamlaka 150 za Serikali za Mitaa ilikuwa Sh. 4,190,275,598,449. Hata hivyo, kiasi kilichopokelewa ni Sh. 3,415,818,281,279 kukiwa na upungufu wa kiasi cha Sh. 774,457,317,170 sawa na asilimia 18 ya bajeti ya matumizi yote ya kawaida iliyopitishwa. Hii inaashiria kuwa asilimia 18 ya shughuli zilizopangwa hazikuweza kutekelezwa. **Jedwali Na. 4-6** linaonesha mtiririko wa upungufu wa fedha za matumizi ya kawaida kwa miaka mitano mfululizo.

Jedwali Na.4-6: Mwenendo wa Fedha Pungufu za Matumizi ya Kawaida

Mwaka wa Fedha	Makisio ya Mapokezi ya Ruzuku ya Kawaida (Sh.)	Kiasi Halisi Kilichopokelewa (Sh.)	Kiasi ambacho Hakikutolewa (Sh.)	% ya upungufu	Idadi ya Halmashauri
2019/20	4,190,275,598,449	3,415,818,281,279	774,457,317,170	18	150
2018/19	4,935,980,658,547	3,947,829,713,378	988,150,945,169	20	167
2017/18	4,850,300,634,913	3,862,510,618,291	987,889,016,622	20	165
2016/17	3,989,650,046,115	3,408,122,819,649	581,527,226,466	15	146
2015/16	1,010,650,744,099	390,525,992,297	620,124,751,801	61	151

Kwa mujibu wa **Jedwali Na. 4-6** hapo juu, kuna upungufu wa asilimia 18 ya ruzuku ya matumizi ya kawaida. Maelezo ya hamashauri na kiasi cha fedha kilichopokelewa pungufu kinaonesha katika **Kiambatisho Na. 4-8** cha ripoti hii.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kupokea fedha pungufu za matumizi ya kawaida pamoja na za maendeleo ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Sababu kubwa ni mipango-mkakati na vipaumbele vya kitaifa juu ya kuendeleza ukuaji na maendeleo ya miundombinu kwa uchumi endelevu.

Kwa kuzingatia hayo, mwenendo wa kupokea fedha pungufu kwa shughuli za kawaida na miradi ya maendeleo hufifisha uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhudumia wanawake.

4.5 Fedha za Mapato ya Vyanzo vya Ndani Sh. 33,959,724,965 Hazikupelekwa kwenye Miradi ya Maendeleo

Agizo Maalumu 5.0 (xiii) la Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti la Mwaka 2019/20 linazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa asilimia 40 na 60 (kulingana na Mamlaka ilivyopangiwa) ya mapato yake ya ndani inatengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo. Msukumo mkubwa ni kuwekeza katika vyanzo vikuu vya mapato (kilimo, uvuvi, biashara na mifugo) ili kuviboresha na viwe vya kudumu.

Kwa mantiki hiyo, OR-TAMISEMI ilitoa barua yenye Kumb. Na. CBD.421/422/01/43 ya tarehe 3/1/2018 ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilitengwa katika makundi “A” na “B” na kuzitaka kutenga asilimia 60 na 40 mtawalia ya vyanzo vyao vya ndani kwa kila kundi.

Tathmini ya ulinganisho wa bajeti na kiasi halisi cha matumizi ya maendeleo imebainika kuwa, Mamlaka 95 za Serikali za Mitaa zilikusanya mapato ya ndani kiasi cha Sh. 200,993,464,338 na hivyo jumla ya Sh. 93,220,353,209 zilipaswa kupelekwa kwa ajili ya fedha za miradi ya maendeleo ikiwa ni asilimia 40 na 60. Hata hivyo, kiasi cha Sh. 59,260,628,245 ndicho kilichohamishiwa kwenye akaunti za maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na kuacha kiasi cha Sh. 33,959,724,965 pasipo kupelekwa kama **Kiambatisho Na. 4-9** kinavyoonesha.

Mamlaka 3 za Serikali za Mitaa hazikuweza kabisa kupeleka fedha za mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo kwa asilimia 100 na zingine 41 kati

ya 95 zilipeleka chini ya asilimia 50 kama **Kiambatisho Na. 4-9** kinavyoonesha.

Kwa kuzingatia hali niliyoibaini, ninazishauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa: a) kuzingatia maelekezo ya Serikali na kufuata mwongozo wa bajeti kwa kuhakikisha kuwa kiasi kilichotengwa kutoka mapato ya ndani kinatolewa ili kutekeleza miradi ya maendeleo, b) kuhakikisha kuwa fedha zote zilizoainishwa kwenye miradi ya maendeleo zinatumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika na si kwa matumizi ya kawaida.

SURA YA 5

UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA

5.0 Utangulizi

Katika sura hii, nimegusia masuala muhimu yaliyojitokeza yakiambatana na mapendekezo ya kuboresha, katika ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Lengo kuu la ukaguzi wa taarifa za fedha ni kuniwezesha kutoa maoni iwapo taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na miongozo yote, kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.

Ili kuboresha ufanisi wa utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, nimebainisha maeneo ambayo menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuyazingatia ili kuongeza thamani katika taarifa za fedha zinazoandaliwa na hivyo kuwezesha upatikanaji wa thamani ya fedha katika huduma zitolewazo na halmashauri kwa jamii lengwa.

5.1 Miamala Iliyorekebishwa Baada ya Ukaguzi wa Toleo la Kwanza la Taarifa za Fedha

Agizo la 31 la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Kifungu cha 45(4) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka, 1982 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2019) inamtaka ofisa masuuli kutayarisha taarifa za fedha na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi ifikapo au kabla ya tarehe 30 Septemba ya kila mwaka.

Taarifa za fedha za Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020 ziliwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali katika tarehe ya ukomo. Hata hivyo, baada ya ukaguzi wa toleo la kwanza la taarifa hizo za fedha, baadhi ya miamala ilibainika kuwa na makosa mengi na makubwa ya kiuhasibu, hali ilyosababisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kurudia mara kadhaa kuwasilisha vitabu vya fedha vilivyofanyiwa marekebisho.

Kiambatisho Na. 5-1 kinaonesha kwa muhtasari idadi ya miamala iliyotakiwa kurekebishwa na thamani ya jumla ya makosa yaliyobainika kwa kila halmashauri, baada ya ukaguzi wa toleo la kwanza la taarifa ya fedha zilizowasilishwa na Mamlaka 116 za Serikali za Mitaa, kwa kulinganisha na toleo la taarifa za fedha lililorekebishwa.

Uwasilishaji wa taarifa za fedha zisizo sahihi kutokana na makosa ya kiuhasibu ni kiashiria kuwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa haziupi kipaumbele udhibiti wa mchakato wa maandalizi ya taarifa za fedha na hivyo kusababisha uwepo wa makosa mengi na makubwa ya kiuhasibu katika taarifa za fedha zinazowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuimarisha taratibu za udhibiti ubora ili kuhakikisha taarifa za fedha zinazoandaliwa na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi zinaonesha uhalisia wa shughuli za halmashauri kwa kutokuwa na udanganyifu na makosa ya kiuhasibu na pia kuwajengea uwezo watumishi waliopo katika idara ya fedha na kitengo cha ukaguzi wa ndani.

5.2 Madai ya Muda Mrefu na Malipo Yaliyofanywa Kabla ya Kupokea Bidhaa au Huduma ya Sh. 103,304,511,810

Madai na malipo yaliyofanywa kabla ya kupokea bidhaa au huduma yanahusisha miamala iliyofanywa na halmashauri kwa wateja wake waliopata huduma kwa mkopo, mapato ambayo hayajawasilishwa, masurufu ambayo hayajarejeshwa na watumishi, pamoja na mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, na malipo ya awali yaliyofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya huduma au bidhaa ambazo hazijapokelewa.

Uzoefu unaonesha uwezekano wa halmashauri kutopokea mapato ambayo hayajawasilishwa au huduma ambazo hazijatolewa unakuwa mkubwa kadri mdaiwa anapochelewa kulipa deni au kutoa huduma tarajiwa.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020, taarifa za fedha pamoja na viambatisho vyake vilibainisha kuwa madai yenye thamani ya Sh. 103,304,511,810 katika Mamlaka 158 za Serikali za Mitaa yalikuwa hayajalipwa na wadaiwa kwa kipindi cha zaidi ya miezi 12, kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 5-2** cha taarifa hii.

Madai ya muda mrefu kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo yanaonesha a kupungua kwa kiasi cha Sh. 20,437,989,375 kutoka Sh. 131,854,275,521 katika Mamlaka 170 za Serikali za Mitaa zilizobainika kuwa na madai katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi Sh. 103,304,511,810 katika Mamlaka 158 za Serikali za Mitaa ambazo madai yeke yalikaguliwa katika mwaka wa fedha 2019/20. Mwenendo wa madai ya muda mrefu na malipo yaliyofanywa kabla ya kupokea bidhaa au huduma kwa miaka ya fedha minne inayofuatana ni kama ilivyo kwenye **Jedwali Na. 5-1.**

Jedwali Na. 5-1: Mwenendo wa Madai na Malipo ya Awali ya Muda Mrefu

Mwaka wa Fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Halmashauri
2019/20	103,304,511,810	158
2018/19	131,854,275,521	170
2017/18	143,045,745,088	166
2016/17	138,907,446,027	161

Upatikanaji wa kiasi hiki cha madai kutoka kwa wadaiwa unatia shaka kwa kuwa madai haya yamedumu kwa muda mrefu bila kukusanywa na hatimaye yanaweza kuwa madeni yasiyolipika. Hivyo, menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kufanya ufuatiliaji wa uhakika ili ziweze kujiridhisha iwapo madai haya yanaweza kurejeshwa na wadaiwa, vinginevyo yaorodheshwe kama madai yenye shaka.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuweka mikakati thabiti itakayoboresha mchakato wa urejeshwaji wa madai haya kutoka kwa wadaiwa kadiri iwezekanavyo.

5.3 Madeni ya Muda Mrefu Kiasi cha Sh. 190,951,431,050

Madeni ni madai halali kwa ajili ya kulipia bidhaa au huduma zilizotolewa kwa mkopo na watoahuduma kwa halmashauri na madai ya stahiki za watumishi. Madai kwa halmashauri huwasilishwa na watoahuduma na bidhaa kwa njia ya hati za madai. Hujumuisha pia huduma za kimkataba zinazotolewa na watumishi na wadau wengine kwa halmashauri bila kuambatana na malipo stahiki.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020, halmashauri 172 zilikuwa na malimbikizo ya madeni ya muda mrefu yenye jumla ya Sh. 190,951,431,050 kama ilivyo kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa, ambazo muhtasari wake uko katika **Kiambatisho Na. 5-3.**

Madeni haya yamepungua kwa kiasi cha Sh. 16,284,286,083 ikilinganishwa na madeni ya mwaka wa fedha 2018/19 ya kiasi cha Sh. 207,235,717,133 katika halmashauri 169, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 5-2**.

Jedwali Na.5-2: Mwenendo wa Madeni Yasiyolipwa

Mwaka wa fedha	Kiasi (Sh.)	Idadi ya Hamashauri
2019/20	190,951,431,050	172
2018/19	207,235,717,133	169
2017/18	185,645,016,191	172
2016/17	165,562,212,375	158

Kutokulipa madeni kwa wakati kunawakatisha tamaa watoahuduma na bidhaa na kunaweza kusababisha washindwe kuzihudumia Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mkopo; aidha wadau wengine wenye madai hukosa imani ya kufanya kazi na halmashauri. Hii ni sababu kubwa ya uwepo wa mashauri ya madai mahakamani dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambazo zinapelekea halmashauri nyingi kulipa viwango vikubwa vya tozo na faini zinazotokana na hukumu za mahakama.

Kwa upande wa watumishi, madai yao ya muda mrefu yanapunguza morali na moyo wa kujitoa katika utoaji wa huduma kwa jamii. Ni muhimu kudumisha mahusiano mema ya kiutendaji kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wake, wakiwemo watumishi na watoa huduma na bidhaa, kwa kuhakikisha zinatimiza wajibu wake kwa kulipa madeni kwa wakati na hivyo kujenga imani kwa jamii inayohudumiwa na taasisi hizo.

Ninashauri Serikali kupitia OR-TAMISEMI kuwa na mkakati imara na endelevu wa kuhakikisha madeni ya muda mrefu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yanalipwa kwa wakati. Pia, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuandaa mchanganuo wa umri wa madeni katika kusaidia kutambua madeni sugu. Kipaumbele cha ulipaji kiwekwe kwenye madeni yaliyodumu muda mrefu ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa usahihi wa madeni kabla ya kuyalipa.

5.4 Mashauri dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Yenye Jumla ya Sh. 123,970,292,298 na Madai ya Halmashauri Dhidi Watoa Huduma Yaliyoko Mahakamani Kiasi cha Sh. 13,400,471,759

Kifungu cha 5 cha Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mamlaka za miji na wilaya) ya Mwaka 1983 kinaeleza malengo ya uanzishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa ni pamoja na kuanzisha, kuhamasisha, kuendeleza,

na kudumisha mfumo bora na fanisi wa serikali za mitaa ili kutoa huduma endelevu zinazokidhi mahitaji ya watu, na kwa kiasi kikubwa, kuboresha huduma za jamii katika mamlaka husika.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2010/20, nilibaini uwepo wa mashauri katika mahakama mbalimbali yanayozigusa halmashauri katika nyanza zifuatazo:

- ✓ Madai dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye madeni tarajiwa yanayotokana na mashauri 117 yaliyo mahakamani yanayohusu watoahuduma, watumishi, taasisi mbalimbali za fedha,mikopo, na jamii inayohudumiwa na mamlaka hizo.

- ✓ Mashauri 60 yaliyopelekwa mahakamani na Mamlaka za Serikali za Mitaa dhidi ya wadau wake, ikijumuisha watoahuduma na bidhaa; na jamii inayohudumiwa na mamlaka hizo.

Mamlaka za Serikali za Mitaa a 117 kati ya 185 zilizokaguliwa zilikuwa zinadaiwa kutokana na mashauri yaliyo mahakamani yenye thamani Sh. 123,970,292,298; na Mamlaka za Serikali za Mitaa 60 zilikuwa na mashauri ya madai mahakamani ya jumla ya Sh. 13,400,471,759 dhidi ya wadau wake. Mchanganuo wa mashauri yote ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 5-4.**

Madeni tarajiwa yanaweza kuleta athari kubwa kwenye rasilimali fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama vile gharama za uendeshaji wa mashauri na hatari ya kulipa kiwango kikubwa cha pesa baadaye kutokana na halmashauri kushindwa kesi. Hali hiyo ikitokea inaweza kuathiri utoaji endelevu wa huduma za jamii.

Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuzingatia matakwa ya sheria, taratibu, na kanuni mbalimbali za kiutendaji wakati wa kufanya maamuzi ili kupunguza athari zitokanazo na kushitakiwa na kulazimika kulipa fedha nyingi kama tozo na faini zinazotokana na hukumu za mahakama pale halmashauri zinaposhindwa kesi. Vilevile, menejimenti za halmashauri zenye mashauri mahakamani zifanye ufautiliaji muafaka kutatua migogoro inayoendelea na kuhakikisha mashauri hayo yanahitimishwa mapema na kwa faida ya halmashauri husika.

SURA YA 6

TATHMINI YA MFUMO YA UDHIBITI WA NDANI, USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA MIFUMO YA UTAWALA BORA

6.1 Utangulizi

Udhibiti wa ndani ni kipengele muhimu katika mfumo wa utawala bora wa taasisi na huwezesha kugundua na kudhibiti vihatarishi; na ni muhimu katika kusaidia kufanikisha malengo ya taasisi kwa kuunda, kuimarisha, na kulinda maslahi ya wadau wake mbalimbali. Kushindwa kwa taasisi nyingi kubwa husababisha kuwekwa kwa sheria na matakwa ya ziada, pamoja na kuongeza juhudi zaidi za kutii sheria ambazo zinapoteza muda na huongeza gharama. Hata hivyo, hii haiondoi ukweli kuwa uwepo wa mfumo sahihi wa udhibiti wa ndani (kuiwezesha taasisi kutumia vyema fursa na kuondoa changamoto) kunawezesha kuokoa muda na fedha na huchochoea uvumbuzi na ulindaji wa thamani ya taasisi. Mfumo wa udhibiti wa ndani wenye ufanisi pia huipa taasisi faida ya ushindani, na huifanya kuwa taasisi yenye mfumo wa udhibiti wa ndani wenye ufanisi na huiwezesha kutekeleza, bila wasiwasi, miradi mbalimbali ya ziada yenye vihatarishi.

Ndani ya mfumo wa utawala bora, udhibiti wa ndani unatakiwa kueleweka, kutekelezwa na kufuatiliwa kikamilifu na watawala, menejimenti ya taasisi, na watu wengine katika kutumia vyema fursa na kupambana na changamoto zinazojitokeza ili kufanikisha malengo ya taasisi.

Kwa mujibu wa Agizo la 11 la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuwa na taratibu za kimaandishi kwa ajili ya udhibiti ndani makini na wa mara kwa mara ili kutathmini ufanisi wake na ili kufahamu iwapo bado unaendana na sheria zilizopo.

Sura hii imejikita kwenye mapungufu niliyoyabaini wakati wa tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, ikijumuisha mifumo ya uhasibu, ufanisi wa vitengo vya ukaguzi wa ndani, utendaji wa kamati za ukaguzi, usimamizi wa vihatarishi, udhibiti wa jumla wa mazingira ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA); na usimamizi na udhibiti wa udanganyifu.

Kwa mwaka wa fedha 2019/20, nimefanya tathmini ya utendaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi, na mfumo wa utawala bora na kubaini mapungufu mbalimbali kama inavyooneshwa kwenye aya ya 6.1 hadi ya 6.6 kama ifuatavyo.

6.1 Mapungufu Yaliyobainika Kwenye Utendaji wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani Kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa

Majukumu ya ukaguzi wa ndani ni kutoa ushauri na maoni huru kwa menejimenti iwapo usimamizi wa vihatarishi, utawala bora, na mifumo ya udhibiti wa ndani inafanya kazi kwa ufanisi.

Kitengo cha ukaguzi wa ndani kinafanya shughuli zinazohusisha kupanga, kuratibu na kufanya ukaguzi, kuchambua, na kutathmini shughuli zote zinazofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na sheria, kanuni na miongozo ya kitaaluma iliyopo.

Agizo la 13(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Kifungu cha 48 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2019) inaitaka Mamlaka ya serikali za mitaa kuajiri mkaguzi wa ndani ambaye atafanya kazi kwa karibu na wakuu wa idara na kuripoti moja kwa moja kwa ofisa masuuli.

Tathmini niliyofanya juu ya utendaji wa vitengo vya ukaguzi wa ndani kwenye halmashauri za wilaya 185, nimebaini mapungufu mbalimbali ambayo yamechangia utendaji usioridhisha kama inavyoelezwa kwenye **Kiambatisho Na. 6-1** ikiwa pamoja na haya yafyatayo:

Kwenye halmashauri za wilaya 79 nimebaini kuwa vitengo vya ukaguzi wa ndani vina upungufu mkubwa wa watumishi na kupelekea kushindwa kukamilisha shughuli za kitengo zilizopangwa kwa mwaka husika. Baadhi ya halmashauri zina mkaguzi mmoja kinyume na mahitaji ya wakaguzi wasiopungua watano.

Tathmini iliyofanyika kwenye halmashauri za wilaya 40 imebaini vitengo vya ukaguzi wa ndani havikuwa na vitendeakazi muhimu kama vile kompyuta, kamera, printa na gari la kitengo kwa ajili ya kutembelea miradi ya maendeleo. Katika baadhi ya halmashauri, vitengo vya ukaguzi wa ndani havikuwa na ofisi.

- ✓ Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani (IIA) imetafsiri ukaguzi wa maeneo yenye vihatarishi kama njia inayounganisha kati ya ukaguzi na mfumo wa usimamizi wa vihatarishi. Ukaguzi wa maeneo yenye vihatarishi

unalenga hatua iliyochukuliwa na taasisi katika kushughulikia vihatarishi ili kufanikisha malengo ya taasisi. Ukaguzi umebaini kuwa halmashuri za wilaya 8 zimeshindwa kufanya ukaguzi wa maeneo yenye vihatarishi kwa mujibu wa matakwa ya Agizo la 14(2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

- ✓ Kwenye halmashauri za wilaya 73 kulikuwa na mgawanyo usiotosheleza wa bajeti kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani na kupelekea kushindwa kukamilisha baadhi ya shughuli zilizopangwa.

- ✓ Nimebaini kuwa katika halmashauri za wilaya 40, baadhi ya shughuli zilizopangwa kama vile ukaguzi wa fedha za elimu bila malipo zilizopokelewa mashuleni, miradi inayotekelezwa kwa kutumia wataalamu wa ndani (force account), na fedha zilizopokelewa na kutumika kwenye vituo vya afya hazikukaguliwa kutokana na upungufu wa watumishi na bajeti isiyotosheleza.

- ✓ Serikali inatumia mifumo mbalimbali ya uhasibu kama vile FFARS, Epicor, LGRCIS, GOT-HOMIS n.k na mifumo mingine ya teknolojia ya habari na mawasiliano kama vile PLAN-REP, LAWSON, GSPP, n.k. Hata hivyo nimebaini kwenye halmashauri za wilaya 31, wakaguzi wa ndani walikosa uelewa wa mifumo hiyo na hawajapata mafunzo ya jinsi mifumo hiyo inavyofanya kazi na maboresho yaliyofanyika hivyo kuwawia ngumu kukagua vizuri mifumo hiyo.

Mambo mengi yaliyobainika yamekuwa yakiripotiwa kwenye taarifa zangu za miaka ya nyuma. Ninasisitiza kwa menejimenti za halmashauri kuhakikisha kuwa vitengo vya ukaguzi wa ndani vinapatiwa watumishi wa kutosha na vitendeakazi vya kutosha kama vile kompyuta, printa na magari kwa ajili ya kutembelea miradi. Pia, ziongeze bajeti kwa kutenga fedha kutokana na bajeti iliyopitishwa na kutoa mafunzo ya mara kwa mara ya utendaji wa mifumo ya TEHAMA ya uhasibu na maboresho yake yanayofanyika.

6.2 Mapungufu Yaliyobainika kwenye Mazingira ya Jumla ya TEHAMA Kwenye Halmashauri

Udhibiti wa jumla wa mifumo ya TEHAMA ni shughuli muhimu kwenye utendaji wa Serikali na udhibiti wa taarifa za kifedha. Unatoa msingi wa kuaminika kwa data, taarifa, udhibiti wa kimfumo unaojiendesha wenyewe,

na kazi zingine za mfumo zinazoongoza utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi. Usalama, ukamilifu, na usahihi wa taarifa za fedha unategemea udhibiti wa kimfumo wa taarifa, usimamizi wa mabadiliko ya mifumo ya TEHAMA, na udhibiti wa utendaji wa jumla wa mfumo.

Umuhimu na manufaa ya udhibiti wa jumla wa TEHAMA kwa Serikali, wawekezaji, wadhibiti ubora, kamati za ukaguzi, menejimenti, na wakaguzi unaendelea kuongezeka.

Tathmini niliyofanya kwenye udhibiti wa jumla wa mifumo ya TEHAMA kwa halmashauri za wilaya 185 nimebaini mapungufu mbalimbali kama inavyoelezwa kwenye **Kiambatisho Na. 6-2** ikiwa pamoja na haya yafyatayo:

- ✓ Tathmini iliyofanyika kwenye halmashauri za wilaya 18 nimebaini kuwa Sera ya TEHAMA na Mpango-mkakati wa TEHAMA haukuandaliwa na hivyo malengo na mikakati katika TEHAMA hayaendani na malengo na mikakati ya jumla ya halmashauri.

- ✓ Kutokuwepo kwa programu za mafunzo kwa watumishi kwenye halmashauri za wilaya 24 ili kuongeza uelewa wao na kujifunza mabadiliko mapya ya kiteknolojia.

- ✓ Nimebaini kutokuwepo kwa programu ya kuzuia virusi kwenye kompyuta (antivirus) kwenye halmashauri za wilaya 36. Hakuna utaratibu uliowekwa wa kudhibiti na kusimamia uwekaji wa programu za kuzia virusi kwenye kompyuta ili kuhakikisha kuwa programu hizo zimethibitishwa na mara kwa mara zinauhishwa, pamoja na kuzuia uwekaji wa programu za kompyuta ambazo hazijathibitishwa. Hivyo, kompyuta za halmashauri zinaweza kushambuliwa na virusi vya kumpyuta na programu zenye lengo ovu (malware) na kupelekea kuvuja au kuharibika kwa taarifa na data za Serikali.

- ✓ Tathmini niliyofanya kwenye udhibiti wa jumla wa TEHAMA nimebaini kwamba halmashauri za wilaya 13 ama hazikuanzisha kamati za uendeshaji wa TEHAMA au zilikuwa na kamati za uendeshaji wa TEHAMA zisizofanya kazi kutokana na kutofanyika kwa vikao toka kuanzishwa kwake. Hii inaweza kusababisha shughuli za TEHAMA kutosimamiwa vyema ikiwa moja ya sehemu ya utawala ya halmashauri.

- ✓ Katika halmashauri za wilaya 18, ilibainika kuwa vitengo vya TEHAMA vilikuwa na upungufu mkubwa wa watumishi. Baadhi ya halmashauri zilikuwa na mtumishi mmoja badala ya kiwango cha chini cha watumishi watatu. Pia, halmashauri nyingi hazikuwa na maofisa TEHAMA.

- ✓ Licha ya juhudi za Serikali katika kuhamia kwenye mifumo ya kielekitroniki ya kutoa huduma, nimebaini katika halmashauri za wilaya 18 kulikuwa na mgawanyo wa bajeti usiotosheleza kwa kitengo cha TEHAMA ambapo imepelekea kushindwa kutimiza majukumu yake vizuri na kusababisha juhudi hizo za Serikali kutofanikiwa vyema.

- ✓ Nilibaini katika halmashauri za wilaya 12 kulikuwa na uhaba wa vifaa vya TEHAMA na kusababisha halmashauri hizo kushindwa kutoa huduma bora kwa wananchi.

- ✓ Mpango wa kurejesha huduma yanapotokea majanga unaelezea njia ya kurejesha huduma kwa haraka na kupunguza usumbufu baada ya kutokea majanga. Ni sehemu muhimu ya mpango wa mwendelezo wa utoaji huduma na unasaidia kurejesha huduma za TEHAMA kwa haraka na kuzuia upotevu wa taarifa muhimu. Katika tathmini yangu nimebaini kuwa halmashauri za wilaya 18 hazikuwa na mpango ulioandaliwa wa kurejesha huduma inapotokea majanga na hatua za dharura zilizojaribiwa yanapotokea janga.

- ✓ Mapungufu yaliyobainika kwenye udhibiti wa jumla wa mazingira ya TEHAMA yanaweza kusababisha menejimenti ya halmashauri kushindwa kuandaa taarifa sahihi za kifedha na kuziweka taarifa muhimu za Serikali kwenye hatari za kupotea na/au mifumo ya TEHAMA kushindwa kufanya kazi.

Nininapendekeza kwa menejimenti za halmashauri husika, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, kushughulikia mapungufu yaliyotajwa hapo juu ili kujihakikishia usalama, ukamilifu, kupatikana kwa taarifa za fedha za halmashauri, na matumizi sahihi ya rasilimali za umma

6.3 Miamala yenye Viashiria vya Udanganyifu ya Thamani ya Sh. 614,505,563

Miamala ya kidanganyifu ni ile inayosababisha upotevu wa fedha za umma ama kwa malipo hewa, miamala isiyo ya kweli, au kwa ufujaji wa mapato yaliyokusanywa. Ukaguzi uliofanyika kwenye malipo kwa wadai mbalimbali

na makusanyo ya mapato kwa mwaka huu wa ukaguzi ulibaini malipo na makusanyo yenye viashiria vya udanganyifu yenye thamani ya Sh. 614,505,563 kwenye halmasahuri za wilaya tisa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 6-1**. Maelezo Zaidi ya Miamala yenye viashiria vya udanganyifu yameoneshwa katika **Kiambatisho Na. 6-3**.

Jedwali Na. 6.1: Miamala Yenye Viashiria vya Udanganyifu

Na	Halmashauri	Maelezo ya Muamala	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Nkasi	Manunuzi yenye udanganyifu ya vifaa vya ujenzi vya hospitali ya wilaya	21,557,000
		Marekebisho ya gharama kwenye nukuu ya bei na hati ya madai yenye udanganyifu	2,220,000
2.	H/W Buhigwe	Manunuzi yaliyoambatishwa stakabadhi za kielekitroniki zenye kutia shaka	34,720,000
3.	H/W Kakonko	Ufujaji wa mapato yaliyokusanywa	31,493,000
		Malipo ya mishahara yenye shaka kwa wakusanya mapato	56,126,092
4.	H/M Tabora	Miamala yenye shaka inayohusisha kughushi kumbukumbu za kihasibu	40,014,591
		Fedha zilizorejeshwa kutoka kwenye malipo ya madiwani ambazo hazijawekwa benki	6,790,000
5.	H/W Korogwe	Wizi wa vifaa vya ujenzi wa hospitali ya wilaya	12,757,910
6.	H/W Mbinga	Wizi wa mapato yaliyokusanywa	270,046,700
7.	H/W Muheza	Stakabadhi za kielekitroniki zenye udanganyifu zilizotolewa na wazabuni	123,817,600
8.	H/W Longido	Upotevu wa mapato yatokanayo na leseni za biashara	2,970,000
9.	H/W Mvomero	Wizi wa dawa, vifaatiba na vifaa vya ofisi	11,992,670
Jumla			**614,505,563**

Miamala hii imefanyika kutokana na udhaifu katika udhibiti wa ndani wa halmashauri na halmashauri husika kushindwa kufanya tathmini ya vihatarishi vya udanganyifu ili kubaini na kuzuia kutokea kwake.

TAKUKURU ifanye uchunguzi wa kina katika halmashauri husika ili kubainisha kiasi halisi cha upotevu wa fedha za umma na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika. Ninashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha udhibiti wa ndani na mara kwa mara kufanya tathmini ya vihatarishi vya udanganyifu ili kubaini na kuzuia udanganyifu kabla haujatokea.

6.4 Mapungufu Yaliyobainika Kwenye Tathmini ya Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi vya Udanganyifu

ISA 240 inatafsiri udanganyifu kama "kitendo cha makusudi kinachoweza kufanywa na mtu mmoja au zaidi miongoni mwa menejimenti, watawala, wafanyakazi, au wahusika wengine, ikihusisha udanganyifu ili kupata faida haramu au isiyo ya haki".

Jukumu la msingi la kuzuia na kubaini udanganyifu unaoweza kutokea lipo chini ya menejimenti, uongozi wa halmashauri, na wafanyakazi wa halmashauri husika. Ukaguzi wa tathmini ya vihatarishi vya udanganyifu iliofanywa kwenye halmashauri 185 kwa mwaka huu wa ukaguzi umebaini mapungufu yafuatayo:

- ✓ Halmashauri za wilaya 33 kwa mwaka wa fedha 2019/20 hazikufanya tathmini rasmi ya vihatarishi au kuhuisha tathmini iliyopo ya vihatarishi vya udanganyifu kutokana na kutowasilisha taarifa ya tathmini hiyo ilipoombwa kwa ajili ya ukaguzi.

- ✓ Baada ya kufanyika kwa tathmini ya vihatarishi vinavyoikabili halmashauri, vihatarishi vilivyotambuliwa vinapaswa kurekodiwa kwenye rejesta ya vihatarishi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kwenye halmashauri za wilaya 22, rejesta ya vihatarishi hazikuandaliwa au kuhuishwa kwa wakati.

- ✓ Mapitio niliyoyafanya kwenye halmashauri za wilaya 16 yalibaini kuwa menejimenti ya halmashauri hazikuandaa na kupitisha sera au mfumo wa usimamizi wa vihatarishi vya udanganyifu. Vilevile, halmashauri za wilaya 7 hazikutoa elimu juu ya sera yao ya vihatarishi kwa watumishi wote.

- ✓ Ripoti ya utekelezaji wa vihatarishi kwa mwaka wa fedha 2019/20 haijaandaliwa na halmashauri za wilaya nne.

- ✓ Halmashauri za wilaya 13 hazikuwa na utaratibu wa kimaandishi wa kutambua na kukabiliana na vihatarishi vya udanganyifu na vihatarishi vinginevyo.

Nininapendekeza kwa menejimenti ya halmashauri husika kuweka taratibu nzuri za utambuzi, tathmini, uainishaji, uchambuzi wa athari, pamoja na udhibiti wa vihatarishi kwa ajili ya urahisi kwenye ufuatiliaji na kupunguza vihatarishi.

6.5 Mapungufu yaliyobainika kwenye utendaji wa kamati za ukaguzi kwenye halmashauri

Madhumuni ya msingi ya kuwepo kwa kamati ya ukaguzi kwa taasisi ni kutoa mwongozo wa mchakato wa kuandaa taarifa za fedha, mchakato wa ukaguzi, mfumo wa udhibiti wa ndani wa taasisi, na utii wa sheria na kanuni.

Agizo la 12(1) (2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaitaka kila halmashauri iwe na kamati ya ukaguzi ambayo inajumuisha si zaidi ya wajumbe watano na si chini ya wajumbe watatu. Kati ya wajumbe hao, angalau wajumbe wawili wateuliwe kutoka miongoni mwa wakuu wa idara za halmashauri na wawili kutoka taasisi zilizo nje ya halmashauri.

Tathmini yangu ya utendaji wa kamati za ukaguzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa imebaini mapungufu mbalimbali kama inavyoelezwa kwenye **Kiambatisho Na. 6-4** ikiwa pamoja na haya yafyatayo:

- ✓ Kamati za ukaguzi katika halmashauri za wilaya 29 hazikuandaa taarifa za kamati za ukaguzi za kila mwaka na kwa kila robo mwaka na kuipeleka TAMISEMI, kwa mkuu wa mkoa, na kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Agizo la 12(5)(g) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

- ✓ Agizo la 12(5) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaitaka kamati ya ukaguzi kutoa ushauri kwa ofisa masuuli juu ya maandalizi na uhakiki wa taarifa ya fedha za halmashauri. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kwenye halmashauri za wilaya 20, kamati za ukaguzi hazikupitia taarifa za fedha za halmashauri zilizowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea taarifa hizo kukutwa na makosa mengi wakati wa ukaguzi.

- ✓ Tathmini niliyofanya kwenye utendaji wa kamati za ukaguzi nimebaini kuwa kwenye halmashauri za wilaya 19, kamati hazikufanya tathmini ya vihatarishi kwenye shughuli za uendeshaji wa kila siku wa halmashauri.

- ✓ Agizo la 12(5)(a) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linazitaka kamati za ukaguzi kukutana angalau mara moja kila robo mwaka. Hata hivyo, nilibaini kwenye halmashauri za wilaya 22 kamati hazikufanya vikao vya kila robo mwaka kama inavyotakiwa. Kamati za ukaguzi kwenye baadhi ya halmashauri hizo hazikufanya kabisa vikao kwa mwaka mzima na halmashauri zingine kamati zilikutana chini ya mara nne kama Agizo linavyotaka.

- ✓ Nilibaini kuwa kamati za ukaguzi kwenye halmashauri za wilaya 14 hazijapitia na kupitisha programu za ukaguzi na mipango-kazi ya mwaka wa ukaguzi.

- ✓ Baada ya uteuzi, wajumbe wa kamati za ukaguzi wanapaswa kupewa mafunzo ya msingi kuhusu uendeshaji wa halmashauri ili waweze kutoa mapendekezo yenye mashiko kwa uongozi. Hata hivyo, nilibaini kwenye halmashauri za wilaya 19 hakukufanyika mafunzo yoyote kwa wajumbe wapya wa kamati za ukaguzi kuhusu uendeshaji wa halmashauri, ikiwa pamoja na mafunzo kuhusu uendeshaji wa mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na halmashauri husika.

Ninazitaka menejimenti za halmashauri husika kuhakikisha kuwa kamati za ukaguzi zinafanya kazi kwa ubora kwa kuwapatia mafunzo stahiki wajumbe wa kamati hizo na kutenga bajeti ya kutosha ya kufanya vikao vya kila robo mwaka kama matakwa ya sheria na kanuni ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

6.6 Udhaifu kwenye uendeshaji wa mifumo ya kielekitroniki ya uhasibu kwenye halmashauri

Mfumo wa upashaji habari za kihasibu ni muundo ambao taasisi hutumia kukusanya, kuhifadhi, kusimamia, kuchakata, na kutoa taarifa za kifedha za taasisi ambazo zinaweza kutumiwa na wahasibu, washauri, wachambuzi wa masuala ya kifedha, mameneja, maofisa wakuu wa fedha, wakaguzi, wasimamizi, na mawakala wa kodi.

Mfumo wa upashaji habari za kihasibu kwa ujumla una vipengele vya msingi sita ambavyo ni watu, taratibu na maelekezo, data, programu, miundombinu ya TEHAMA, na udhibiti wa ndani. Kwa mujibu wa Kifungu cha 2 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019, kwa matumizi sasa ya Mifumo Shirikishi ya Taarifa za Usimamizi wa Fedha (IFMIS), OR-TAMISEMI na sekretarieti za mikoa zitakuwa na majukumu maalumu ya kusimamia na kuelekeza matumizi sahihi ya mifumo hiyo. Itakuwa ni jukumu la halmashauri kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusanywa, kupokelewa au kutumika zinarekodiwa ipasavyo na kuhifadhiwa kwenye mfumo ya uhasibu.

Mapitio yangu juu ya mifumo mbalimbali ya uhasibu inayotumiwa na halmashauri kwa mwaka wa fedha 2019/20 yamebaini mapungufu yafuatayo:

- ✓ Mapungufu kwenye utambuzi na utoaji wa taarifa za wadaiwa kwenye Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS). Mfumo hauruhusu kupanga kwa muda maalumu orodha ya wadaiwa wa fedha zilizokusanywa kupitia kifaa cha makusanyo (POS) na hivyo kuwa ngumu kuchambua wadaiwa kwa kuangalia muda wa deni lake. Hii inamaanisha kuwa orodha ya wadaiwa wa makusanyo ya mapato iliyoripotiwa na halmashauri kwenye hesabu za mwisho kwa mwaka 2019/20 haikuwa na uhalisia kwani inaweza kujumuisha wadaiwa wa miaka ya nyuma au mwaka wa mbele.

- ✓ Kuwepo kwa mifumo zaidi ya mmoja ya uhasibu katika halmashauri kunaleta changamoto juu ya usahihi wa data zinazotakiwa kuripotiwa kwenye hesabu za mwisho za pamoja. Halmashauri zinatumia mfumo wa EPICOR kwa malipo; Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS) kukusanya maduhuli; Mfumo wa FFARS kwa mapato na malipo katika utendaji wa ngazi za chini za Serikali; na GOT-HOMIS kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato katika vituo vya afya, zahanati, na hospitali za Serikali. Hata hivyo, mifumo yote hiyo haiwasiliani moja kwa moja yenyewe kwa yenyewe na hivyo halmashauri haziwezi kuandaa hesabu za mwisho za ujumla zinazojumuisha taarifa na data kutoka mifumo hiyo yote. Hali hii inasababisha ukamilifu na usahihi wa taarifa na data hizo kutothibitishwa pasi na shaka. Ukaguzi zaidi ulionesha kuwa serikali za kata na vijiji hazikuwa zinachakata malipo yao kupitia mfumo wa

uhasibu jambo ambalo linafanya iwe vigumu zaidi kuingiza malipo yake kwenye hesabu za mwisho za ujumla za halmashauri husika.

- ✓ Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSAS Accrual) kwa ajili ya uandaaji na utoaji wa taarifa za fedha. Hata hivyo, mfumo wa uhasibu unaotumika yaani EPICOR unafanya kazi kama chombo cha kudhibiti mapato na malipo ya fedha taslimu tu na kushindwa kuripoti mapato na matumizi ambayo si taslimu (accrual); Hivyo, miamala ambayo si ya fedha taslimu iliyofanyika kwa mwaka wa fedha husika inaingizwa na kuripotiwa kwenye hesabu za mwisho za jumla za halmashauri kama marekebisho ya nje ya mfumo hivyo ukamilifu na usahihi wa taarifa za fedha zilizoripotiwa kuwa na shaka.

- ✓ Nimebaini matumizi na utendaji usioridhisha wa Mfumo wa Kukusanya Mapato kwenye Vituo vya Afya (GOT-HOMIS) kwani si moduli zote za mfumo zinatumika, hakuna mafunzo rasmi yaliyotolewa kwa watumiaji, kukosekana kwa vifaa vya TEHAMA kwenye vituo vya afya, kukosekana kwa huduma ya uhakika ya mtandao, na mfumo kufanya kazi kwenye kituo kimoja bila kuwa na mawasiliano ya moja kwa moja ya kimfumo baina ya vituo vya afya.

- ✓ Matumizi ya FFARS yasiyo na ufanisi kwenye vituo vya afya na shule yanayosababishwa na uhaba wa vifaa vya TEHAMA, watumiaji kukosa mafunzo na ujuzi, halmashauri kutotoa ushirikiano wa kutosha kwa watumiaji wa mfumo, kutokuwepo kwa huduma ya uhakika ya mtandao, na uhaba wa wahasibu na wataalamu wa TEHAMA katika halmashauri.

- ✓ Mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani (LGRCIS) kushindwa kufanya kazi vizuri hivyo kusabisha kuwa na wadaiwa kwenye mfumo kwa halmashauri nyingine na hivyo kuongeza wadaiwa wasio sahihi na bila sababu. Hii pia inaweza kupelekea kuwepo wa miamala yenye udanganyifu.

- ✓ Kukosekana kwa utaratibu wa kuwaondoa kwenye mfumo wadaiwa hasa wa leseni za biashara. Mfumo hauzingatii utaratibu wa utoaji wa leseni za biashara ambao hautegemei mwaka wa fedha wa

Serikali. Hii ni kwa sababu baadhi ya leseni huisha muda wake baada ya miezi 12 tangu kutolewa kwake. Hata hivyo, mfumo unatengeneza wadaiwa wa leseni zote hai kila mwanzoni mwa mwaka wa fedha bila kujali kuwa baadhi ya leseni muda wake haujaisha.

Nininapendekeza OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, kuunganisha mifumo yote ya uhasibu inayotumika katika halmashauri kwa kuhakikisha kuwa mifumo yote imeunganishwa na kuwasiliana moja kwa moja na mfumo mkuu yaani EPICOR ili kuwezesha uwepo wa ukamilifua, usiri na upatikanaji wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye mfumo mmoja mkuu wa uhasibu.

SURA YA 7

USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

7.0 Utangulizi

Utendaji mzuri wa taasisi yoyote unategemea rasilimali-watu ikiwa moja ya rasilimali muhimu. Malipo ya mishahara na usimamizi wa rasilimali-watu ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa shughuli za Serikali na kwa hivyo lazima yaangaliwe na kutekelezwa kwa ufanisi. Aidha, mishahara na usimamizi wa rasilimali-watu hutumia sehemu kubwa ya matumizi ya serikali ambayo yanahitaji umakini wakati wa utekelezaji wake.

Vilevile, mifumo ya ulipaji wa mishahara na mifumo ya usimamizi wa rasilimali-watu ina jukumu kubwa katika kuongeza utendaji wa wafanyakazi hivyo kuongeza tija na utoaji wa huduma kwa wananchi wa kawaida.

Pamoja na umuhimu wake, mfumo wa usimamizi wa rasilimali-watu umeonekana kuwa na changamoto zinazotokana na usimamizi wa mishahara pamoja na ustawi, na usalama wa watumishi kwa kuzingatia sheria za kazi na sera zilizopo. Katika kipindi cha ukaguzi, nilichunguza masuala mbalimbali katika mfumo mzima wa mishahara na usimamizi wa rasilimali-watu na kubaini udhaifu mbalimbali.

7.1 Malipo ya Sh. 138,203,000 ya Mishahara kwa Wasio Watumishi wa Umma

Aya ya 7.4.8(a) ya Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 inaelezea kuwa 'Mamlaka za Serikali za Mitaa zitawaondoa wafanyakazi wake kutoka kwenye orodha ya walipwaji kwa sababu ya kifo, kustaafu, kufukuzwa kazi au kuhamishwa. Pia, Agizo la 20(3) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linasema kuwa madiwani na maofisa wa serikali za mitaa watawajibika kwa kufanya malipo yasiyo halali na kuisababishia Serikali hasara.

Wakati wa ukaguzi wa mifumo kwa mwaka uliomalizika tarehe 30 Juni 2018, nilibaini uwepo wa barua za ajira za kughushi kutoka Sekretarieti ya Ajira ya Watumishi wa Umma ndani ya Mfumo wa Lawson kutokana na kutokuwepo kwa muunganiko wa taarifa kati ya mfumo wa dirisha la ajira na Mfumo wa Lawson. Kwa kuwa Mfumo wa Lawson haujaunganishwa na Mfumo wa Epicor, udhibiti wa malipo ya mishahara unafanyika kwa kuingiza

data kwa mkono, utaratibu ambao ninaamini ni wa gharama kubwa, unachukua muda mwingi, na unakabiliwa na makosa ya kibinadamu.


Katika kipindi cha ukaguzi wangu, nimeendelea kuona mapungufu ya kutozingatia sheria, miongozo, na maagizo katika kusimamia mishahara na rasilimali-watu. Kwa mfano, katika Mamlaka 10 za Serikali za Mitaa, waliokuwa watumishi 46 ambao utumishi wao ulikoma wamelipwa jumla ya Sh. 138,203,000, katika kiasi hicho, Sh. 55,353,956 ni makato ya mishahara hiyo. **Jedwali Na. 7-1** hapa chini linaonesha Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizofanya malipo hayo.

Jedwali Na. 7-1: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye Malipo kwa Wasio Watumishi

Na.	Jina	Idadi ya Watumishi	Kiasi cha Mshahara (Sh.)	Makato (Sh.)	Jumla ya Kiasi (Sh.)
1.	H/W Kilindi	17	6,563,006	14,144,994	20,708,000
2.	H/Jiji Mbeya	8	12,142,066	18,277,934	30,420,000
3.	H/Jiji Arusha	6	8,802,184	6,716,816	15,519,000
4.	H/W Kigoma	4	6,640,159	5,148,841	11,789,000
5.	H/W Mufindi	3	38,595,000	0	38,595,000
6.	H/W Korogwe	2	995,874	1,919,126	2,915,000
7.	H/W Kwimba	2	4,345,239	4,497,761	8,843,000
8.	H/W Sengerema	2	1,756,076	1,497,924	3,254,000
9.	H/W Muheza	1	1,232,360	2,457,640	3,690,000
10.	H/W Rombo	1	1,777,080	692,920	2,470,000
	Jumla	**46**	**82,849,044**	**55,353,956**	**138,203,000**

Mwenendo wa miaka mitatu unaonesha kuwa, kuna kupungua kwa idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye malipo ya mishahara hewa pamoja na kiasi husika kama inavyooneshwa kwenye **Mchoro Na. 7-1**.

Mchoro Na. 7-1: Mwenendo wa Malipo ya Wasio Watumishi kwa Miaka Mitatu



Pamoja na mwelekeo mzuri hapo juu, bado ninasisitiza kuhusu hatari ya upotevu wa fedha za umma kila mwaka licha ya hatua zote zinazochukuliwa na Serikali. Kuna uwezekano kuwa malipo haya ni ulaghai au uzembe uliofanywa na maofisa wa halmashauri ambao kwa maoni yangu unapaswa kuchukuliwa kama makosa ya jinai.

Ninapendekeza hatua kali zichukuliwe dhidi ya maofisa wa halmashauri waliopewa dhamana ya usimamizi wa rasilimali za umma kwa mujibu wa Agizo la 20(3) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009. Aidha, ninatoa wito kwa TAKUKURU ipitie kasoro zote zilizobainika na kuchukua hatua za kisheria zinazotakiwa.

7.2 Makato ya Mishahara ya Sh. 5,079,945,442 ambayo Hayajawasilishwa kwenye Taasisi Husika

Dhamira kuu ya usimamizi wa mishahara ni kuhakikisha kuwa wafanyakazi wote wanalipwa kwa usahihi na kwa wakati, na makato yote yanafanyika kwa usahihi ikiwa pamoja na michango yao ya hifadhi ya jamii.

Nchini Tanzania, mishahara ya wafanyakazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa inatozwa makato ya kisheria na yasiyo ya kisheria ikiwa pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii, kodi ya mapato, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, na ulipaji wa mikopo kwa taasisi za kifedha, vyama vya akiba na mikopo, pamoja na michango kwenye vyama vya wafanyakazi. Makato haya yote

hukatwa na Hazina wakati wa ulipaji wa mishahara isipokuwa kwa watumishi ambao mishahara yao inatokana na fedha za mapato ya ndani, ambao makato yao hufanywa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

Kwa mujibu wa Aya ya 7.4.6(d) ya Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Mitaa wa Mwaka 2019, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuandaa na kulipa kwa wakati makato ya mishahara kwa taasisi husika. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi kwa mwaka uliomalizika tarehe 30 Juni 2020, nilibaini kuwa Mamlaka 46 za Serikali za Mitaa zilishindwa kuwasilisha jumla ya Sh. 5,079,945,442 katika taasisi husika. Miongoni mwa fedha ambazo hazikuhamishwa ni Sh. 3,919,411,819 za mifuko ya hifadhi ya jamii.

Hali hii ya kutowasilisha makato haya ya mishahara kwa wakati imepelekea Serikali kupata hasara ya kulipa riba inayofikia kiasi cha Sh. 2,764,185,509 katika Mamlaka 7 za Serikali za Mitaa. Kwa maoni yangu, fedha hizi zingeweza kutekeleza miradi au huduma zingine kwa manufaa ya umma.

Mwenendo huu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kuwasilisha makato haya hasa ya mifuko ya hifadhi ya jamii umekuwa ikiathiri wastaafu kukamilisha malipo ya mafao yao wakati wa kustaafu. **Jedwali Na. 7-2** linaonesha muhtasari wa kiasi ambacho hakijawasilishwa hadi kufikia Juni 2020, na orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 7-1** cha ripoti hii.

Jedwali Na. 7-2: Makato ya Mishahara ya Thamani ya Sh. 5,079,945,442 Ambayo Hayakuwasilishwa kwa Taasisi Husika

Jina la Taasisi	Kiasi (Sh.)
Mamlaka ya Mapato Tanzania	149,872,690
Mifuko ya Hifadhi ya Jamii	3,919,411,819
Makato mengine	1,010,660,933
Jumla	**5,079,945,442**

Sambamba na hilo, Halmashauri ya Jiji la Dodoma haikuwakata wachezaji 40 wa timu yake ya mpira kiasi cha Sh. 13,617,700 ikiwa ni kodi ya mapato kutoka katika mishahara yao. Hali hii imesababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

Ninapendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa husika ziwasilishe makato hayo kwa wakati bila kuchelewa zaidi ili kuepusha matumizi yasiyokuwa na faida kwa njia ya adhabu.

7.3 Upungufu wa Watumishi 119,753 katika Mamlaka 123 za Serikali za Mitaa

Mapitio ya ikama za Mamlaka 123 za Serikali za Mitaa yalibaini idadi halisi ya watumishi waliopo ni 233,281 ikilinganishwa na mahitaji ya watumishi 353,034 na kusababisha upungufu wa watumishi 119,753 sawa na asilimia 34 ya idadi inayohitajika. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza morali ya kazi kwa watumishi waliopo.

Pia, nilibaini kuwa, malengo ya Serikali ya kutekeleza miradi mingi kwa kutumia utaratibu wa nguvukazi ambayo inahitaji wataalamu wa kutosha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yanaweza yasifikiwe kwa mafanikio kutokana na upungufu huu wa watumishi. Vivyo hivyo, uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari pamoja na huduma bora za afya katika ngazi za vijiji na kata umekuwa ukiongezeka kila mwaka, ambao pia unahitaji walimu na wahudumu zaidi wa afya.

Mwenendo wa miaka minne wa idadi ya watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 7-3 na umeelezewa kwa kina katika Kiambatisho Na. 7-2.

Jedwali Na. 7-3: Mwenendo wa Idadi ya Watumishi Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mwaka	Halmashauri Husika	Mahitaji "A"	Upungufu "B"	Asilimia (%) $\frac{B}{A} \times 100$
2019/20	123	353,034	119,753	34
2018/19	166	473,060	167,078	35
2017/18	158	460,438	149,943	33
2016/17	161	477,829	155,013	32

Upungufu wa watumishi ulisababishwa na menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Idara ya Utumishi, pamoja na OR-TAMISEMI kwa kutochukua hatua zinazofaa kuziba nafasi zilizo wazi.

Ufanisi na utoaji huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umeathiriwa sana hasa katika idara ya ujenzi na sekta za afya na elimu. Watumishi wachache waliopo wanalazimika kufanya kazi zaidi ya saa za kazi ili kufikia matarajio ya utendaji. Hali hii inaweza kusababisha shida za kiafya na kiakili kwa wafanyakazi na vilevile kupunguza ari ya kazi.

Ninatoa wito kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Idara ya Utumishi na OR-TAMISEMI kuwa na utaratibu ambao utahakikisha upatikanaji wa fedha za kuajiri watumishi ili kujaza nafasi zilizo wazi; pia kuwe na utaratibu wa kudumisha kazini watumishi wenye ujuzi wa kutosha na utoaji motisha kwa watumishi waliopo katika maeneo ya pembezoni ili wasiondoke.

7.4 Mikopo Iliyopindukia kwa Watumishi bila Kudhibitiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Maofisa Waliobainishwa (Urejeshwaji wa Madeni) Sheria Na. 7 ya Mwaka 1970 kama ilivyosisitizwa na Mwongozo wenye Kumb. Na. 26/46/01/1/66 wa tarehe 28 Novemba 2012, watumishi wanatakiwa kulipwa si chini ya theluthi moja ya mishahara yao ya kila mwezi.

Kama ilivyooneshwa katika ripoti zangu za miaka iliyopita, bado kuna watumishi wa umma ambao mishahara yao ya kila mwezi inapunguzwa zaidi ya 2/3. Uchambuzi uliofanywa katika Mamlaka 35 za Serikali za Mitaa ulibaini watumishi 3,038 waliokuwa wakipokea chini ya 1/3 ya mishahara yao. Utaratibu huu wa kukopa usiodhibitiwa unaweza kuathiri utendaji wa watumishi na kuathiri utendaji wa jumla wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, nilibaini kuwa hali hii ilichangiwa na ulipaji wa deni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambalo hutoza asilimia 18 ya mshahara wa mtumishi ambaye ni mnufaika wa mkopo. **Jedwali Na. 7-4** kinaonesha orodha ya halmashauri ambazo zina wafanyakazi wanaopokea chini ya 1/3 ya mishahara yao ya mwezi.

Jedwali Na. 7-4: Watumishi wa Halmashauri wanaopata mishahara chini ya theluthi moja

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya watumishi	Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya watumishi
1.	H/Jiji Arusha	105	**19.**	H/Mji Mbulu	26
2.	H/W Arusha	69	**20.**	H/W Meru	97
3.	H/W Bagamoyo	84	**21.**	H/W Mkinga	41
4.	H/W Buhigwe	41	**22.**	H/W Mkuranga	156
5.	H/W Bumbuli	13	**23.**	H/W Moshi	145
6.	H/W Chalinze	49	**24.**	H/M Moshi	212
7.	H/Jiji Dar es Salaam	06	**25.**	H/W Msalala	216
8.	H/W Hai	89	**26.**	H/W Muheza	58
9.	H/Mji Handeni	21	**27.**	H/W Mwanga	90
10.	H/M Ilala	25	**28.**	H/Mji Njombe	106

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya watumishi	Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya watumishi
11.	H/Mji Kasulu	36	**29.**	H/W Pangani	17
12.	H/W Kibiti	82	**30.**	H/W Rombo	80
13.	H/M Kigamboni	121	**31.**	H/W Same	86
14.	H/W Kigoma	27	**32.**	H/W Siha	31
15.	H/W Kiteto	31	**33.**	H/Jiji Tanga	107
16.	H/Mji Korogwe	33	**34.**	H/M Temeke	143
17.	H/W Lushoto	428	**35.**	H/M Ubungo	138
18.	H/W Mafia	29	**Jumla**		**3,038**

Katika hali isiyo ya kawaida, pia nilibaini watumishi 8 katika Mamlaka 6 za Serikali za Mitaa ambao kila mwisho wa mwezi hawapati kiasi chochote cha mshahara. Mamlaka hizo na idadi ya watumishi ni H/Jiji Arusha (1), H/W Kiteto (1), H/W Njombe (1), H/M Temeke (1), H/W Rombo (3) na H/W Same (1).

Ninapata wasiwasi na ustawi wa watumishi hawa katika kupata mahitaji yao muhimu kama vile chakula, mavazi na malazi. Hali hii inasababisha watumishi kutumia muda wa kazi kwa shughuli zao binafsi ili kujipatia kipato cha ziada, hali inayoweza kudumaza utoaji wa huduma kwa jamii.

Maofisa masuuli wanapaswa kutoidhinisha mikopo ya watumishi inayozidi kiasi kilichoidhinishwa. Aidha, ninaishauri Serikali kuangalia tena kiasi cha makato ya mkopo wa elimu ya juu ili kupunguza makali kwa watumishi.

7.5 Mikopo ya Mshahara ya Thamani ya Sh. 95,573,060 kwa Watumishi ambayo Haikurejeshwa

Kuna haki mbalimbali ambazo watumishi wa umma wanazipata kutoka kwa mwajiri wao. Kama ilivyo kwa watumishi wengine wa Serikali, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, watumishi hupata mikopo ya mshahara ili kujikimu kwa matukio ya dharura kama malipo ya ada ya shule kwa ajili ya mtumishi au watoto wa mtumishi, na malipo ya gharama za matibabu ya haraka.

Agizo Na. 41(1) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaeleza kuwa, mkopo wa mshahara uliotolewa kwa mtumishi unatakiwa kurudishwa si zaidi ya kipindi cha miezi 12. Aidha, Kanuni Na. N.7(1) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 inaeleza kuwa, kiasi hicho kinapaswa kulipwa ndani ya mwaka mmoja wa fedha.

Kinyume na Agizo hilo pamoja na Kanuni, nilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020, Mamlaka 4 za Serikali za Mitaa zilikuwa hazijakusanya marejesho ya mikopo ya mishahara yenye jumla ya Sh. 95,573,060 kama inavyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 7-5** hapa chini.

Jedwali Na. 7-5: Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye Mikopo ya Mishahara

Na.	Jina	Idadi ya Watumishi	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Igunga	127	53,910,000
2.	H/W Kakonko	18	26,872,600
3.	H/W Kaliua	68	13,614,260
4.	H/W Korogwe	7	1,176,200
	Jumla	**220**	**95,573,060**

Hii inaashiria kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina mifumo madhubuti ya kutoa na kurejesha mikopo ya mishahara inayotolewa kwa watumishi. Madeni haya yakikaa kwa muda mrefu yatazuia shughuli zingine kufanyika kutokana na upungufu wa fedha na yanaweza yasilipike kabisa.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia Agizo Na. 41(1) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Kanuni Na. N.7 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 na kuhakikisha kuwa madeni ya mshahara yanakusanywa kwa wakati. Vilevile, kiasi kilichohojiwa kinapaswa kurejeshwa kutoka kwa watumishi husika.

7.6 Kutorejeshwa Hazina kwa Mishahara Isiyolipwa Sh. 82,580,992

Mishahara ya kila mwezi ya watumishi inalipwa moja kwa moja na Hazina katika akaunti za benki za watumishi. Lakini zipo sababu kama vile za kinidhamu, kustaafu, kufariki, kufukuzwa au utoro wa muda mrefu ambazo zinaweza kusababisha mtumishi asilipwe mshahara wake wa mwezi.

Kiasi hiki kisicholipwa hutunzwa katika akaunti za amana kwa ajili ya kuwalipa watumishi watakaodai au hurudishwa Hazina. Agizo Na. 79(6) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaelekeza kuwa, mishahara ambayo haikulipwa kwa ajili ya waliofariki, waliofukuzwa au watoro irudishwe Hazina ndani ya wiki mbili baada ya tarehe ya kulipa mishahara.

Kinyume na Agizo hilo, Mamlaka 4 za Serikali za Mitaa zimebaki na mishahara isiyolipwa kiasi cha Sh. 82,580,992 kwa ajili ya waliofariki,

waliofukuzwa au watoro bila kurudishwa Hazina kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7-6** hapa chini.

Jedwali Na. 7-6: Halmashauri Zenye Mishahara Isiyolipwa Ambayo Haikurejeshwa Hazina

Na.	Jina	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Iringa	60,165,378
2.	H/W Korogwe	14,016,359
3.	H/W Namtumbo	6,099,255
4.	H/W Itilima	2,300,000
	Jumla	**82,580,992**

Kwa mwenendo huu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, nina wasiwasi zinaweza kutumia fedha hizi kwa matumizi mengine kwa kuwa zinaweza kushindwa kuzirejesha na hivyo kuongeza madeni.

Ofisa masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatakiwa kuhakikisha kuwa kiasi chote cha mishahara ambacho hakijalipwa kinalipwa katika akaunti ya Hazina. Pia, mfumo wa udhibiti wa ndani uzingatiwe kwa kufuata Agizo Na. 79(6) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

7.7 Uwepo wa Watumishi Wanaokaimu Vyeo kwa Muda Mrefu

Kanuni ya D.24(3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 inasema kuwa, kadiri inavyowezekana, mtumishi wa umma hatakiwi kukaimu nafasi kwa kipindi kinachozidi miezi sita. Mamlaka ya uteuzi ihakikishe kuwa mchakato wa kumteua mtumishi atakayefaa katika nafasi hiyo unakamilika ndani ya muda wa miezi sita.

Kwa kuzingatia kanuni hii, maofisa masuuli kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI wahakikishe kwamba, watumishi wanaokaimu wanapaswa kuthibitishwa si zaidi ya miezi sita ya kipindi cha kukaimu ikiwa wanastahili au kujaza nafasi hiyo na ofisa anayestahili.

Mapitio yaliyofanywa kwenye taarifa mbalimbali za watumishi, hasa wakuu wa idara na vitengo katika Mamlaka 117 za Serikali za Mitaa, nilibaini uwepo wa watumishi 510 waliokuwa wakikaimu nafasi za wakuu wa idara na vitengo kwa zaidi ya miezi sita. Pia, nilibaini uwepo wa watumishi waliokaimu nafasi hizo kipindi kirefu cha hadi miaka kumi na hakukuwa na utaratibu wowote wa kuondoa tatizo hilo.

Mapungufu haya yamebainika katika H/W Kigoma (mhandisi wa ujenzi, miezi 123), H/W Kongwa (mkaguzi mkuu wa ndani, miezi 120), H/W Bunda (mkuu wa kitengo cha TEHAMA, miezi 109), H/W Serengeti (mkaguzi mkuu wa ndani, miezi 108) na H/W Bukombe (mazingira na majitaka, miezi 107). Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye watumishi wanaokaimu kwa kipindi cha zaidi ya miezi 6 imo katika **Kiambatisho Na. 7-3**.

OR-TAMISEMI na Idara ya Utumishi haijalichukulia suala hili kwa uzito unaotakiwa, kwa sababu wengi kati ya watumishi wanaokaimu nafasi hizi hawana sifa zinazotakiwa; wengine wanasubiria utaratibu wa kuthibitishwa; na wengine ni kwa sababu tu mamlaka husika hazijateua watu wenye sifa.

Mwenendo wa miaka minne mfululizo unaonesha kupungua kwa idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye watumishi wanaokaimu kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 7-7** hapa chini.

Jedwali Na. 7-7: Mwenendo wa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaokaimu

Mwaka	Idadi ya Halmashauri	Watumishi wanaokaimu
2019/20	117	510
2018/19	137	554
2017/18	129	491
2016/17	113	586

Kwa mtazamo wangu, watumishi kukaimu nafasi kwa muda mrefu kunawapunguzia morali ya kuhudumia jamii. Hali hii inaweza kuwazuia kufanya maamuzi sahihi katika idara na vitengo vyao; pia inaweza kupelekea kushuka kwa ari ya kufanya kazi.

Ninazihimiza menejimenti husika kwa kushirikiana na Idara ya Utumishi pamoja na OR-TAMISEMI kuharakisha michakato yote inayoendelea ili kukamilisha uteuzi wa maofisa wenye sifa kujaza nafasi zilizo wazi. Pia, ninaihimiza OR-TAMISEMI kuhakikisha kwamba kila wakuu wa idara na vitengo wanapohamishwa, nafasi zao zijazwe mara moja.

7.8 Madai Mbalimbali ya Sh. 27,840,078,424 ya Watumishi Ambayo Hayajalipwa

Kanuni za Kudumu za Watumishi wa Umma za Mwaka 2009 zinaelezea haki mbalimbali ambazo mtumishi wa umma anatakiwa kulipwa. Haki hizi zinajumuisha posho mbalimbali zilizopo kwa mujibu wa sheria na zingine

ambazo si kwa mujibu wa sheria lakini zinalipwa kwa mujibu wa miongozo na sheria zingine mbalimbali. Malipo haya ya posho yanafanywa kutoka katika makusanyo ya mapato ya ndani na zingine zinalipwa kutoka Serikali kuu.

Ukaguzi wangu kuhusu haki hizi za watumishi ulibaini kuwa, hadi kufikia 30 Juni 2020, Mamlaka 36 za Serikali za Mitaa zilikuwa na jumla ya Sh. 27,840,078,424 ikiwa ni madai ya stahiki za watumishi. Madeni haya yalijumuisha posho za madiwani, ongezeko la mishahara, malipo ya vibarua, posho za likizo (hasa za walimu na watumishi wa afya), na posho za madaraka kwa wakuu wa idara na vitengo. **Kiambatisho Na. 7-4** kinaonesha kiasi kinachodaiwa katika kila Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Madai haya yamekuwa yakiongezeka kutokana na ukweli kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashindwa kukusanya mapato yake ya ndani kwa mujibu wa bajeti yake. Pia, Serikali kuu imekuwa ikitoa fedha za matumizi ya kawaida chini ya bajeti.

Ninatoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali kupitia OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa zinajumuisha katika bajeti zao malipo ya madai haya ili kuepusha kuendelea kukua.

7.9 Ucheleweshaji wa Nyongeza ya Mishahara na Kupandisha Madaraja

Kanuni ya D. 51 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 inataka tarehe ya kupandishwa daraja ya mtumishi wa umma iamuliwe na mamlaka sahihi ya uteuzi ambayo haitakuwa kabla ya tarehe ya nafasi ilipokuwa wazi. Ofisa anakuwa na sifa stahili za kupandishwa daraja na kutekeleza majukumu katika nafasi yake mpya.

Kinyume na kanuni hiyo, nilipitia mafaili ya watumishi pamoja na Mfumo wa LAWSON wenye taarifa mbalimbali za watumishi na kubaini kuwa, watumishi 7,992 katika Mamlaka 14 za Serikali za Mitaa hawakupandishwa madaraja ingawa walikuwa na sifa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 7-8** hapa chini.

Jedwali Na. 7-8: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Ucheleweshaji wa Nyongeza ya Mishahara na Kupandisha Madaraja

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Watumishi
1.	H/W Bagamoyo	891
2.	H/W Hai	1,176
3.	H/W Kakonko	18
4.	H/Mji Kasulu	155
5.	H/W Manyoni	10
6.	H/W Mbozi	826
7.	H/W Mbulu	730
8.	H/W Moshi	1,848
9.	H/M Moshi	1,523
10.	H/W Mtwara	34
11.	H/W Newala	164
12.	H/W Siha	590
13.	H/W Singida	22
14.	H/W Ukerewe	5
	Jumla	**7,992**

Katika ripoti yangu ya mwaka uliopita niliripoti jambo hili na nikaishauri Idara ya Utumishi wa Umma kuharakisha upandishaji wa madaraja na mishahara. Kwa bahati mbaya, suala hili bado halijapewa kipaumbele.

Kushindwa kupandisha madaraja na kutoa nyongeza ya mishahara kwa wakati kwa watumishi wa umma husababisha utendaji duni katika utoaji wa huduma na hii huhatarisha nia njema ya Serikali ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

Ninazisihi menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa na OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuharakisha mchakato wa idhini ya kupandishwa vyeo na kuhakikisha kuwa marekebisho yanayotakiwa kwa mishahara ya watumishi yanafanywa mara tu baada ya kupandishwa vyeo ili kuepusha madeni kwa Serikali.

7.10 Taarifa za Watumishi Kutohuishwa Katika Mfumo wa LAWSON

Agizo Na. 79(1) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linahitaji ofisa rasilimali-watu au mkuu wa idara husika kuweka rejesta iliyohuishwa ya watumishi wote na maelezo yao na kumtaarifu mweka hazina mara moja mambo yanayoathiri malipo ya mishahara, ikiwemo uteuzi, kujiuzulu, kufukuzwa kazi, kusimamishwa kazi, kubadilishiwa majukumu, pamoja na uhamisho. Pia, linataka mabadiliko

katika malipo, nje ya nyongeza ya kawaida ya mshahara na makubaliano ya malipo na namna ya kukokotoa; na taarifa muhimu kuhifadhiwa katika kumbukumbu za utumishi kwa ajili ya kodi ya mapato, na kuchangia mifuko ya hifadhi.

Taarifa za ajira za watumishi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama watumishi wengine wa umma huhifadhiwa na idara ya utumishi wa umma kwa kutumia Mfumo wa LAWSON. Taarifa mbalimbali za watumishi hujazwa katika mfumo huu mara kwa mara kulingana na hali ya mtumishi. Hii ni pamoja na uhamisho au kituo cha sasa cha kazi cha mtumishi, kustaafu, na kubadilishiwa majukumu ya ajira na utoro.

Nilikagua taarifa za mishahara, majalada binafsi ya watumishi, rejesta za kuhama au kuhamia na nilibaini watumishi 612 katika Mamlaka 26 za Serikali za Mitaa ambao taarifa zao hazikuwa zimehuishwa kwenye Mfumo wa LAWSON. Baadhi ya watumishi waliokuwa wamehamishwa kutoka kituo kimoja cha kazi, taarifa za mshahara wake hazikuhamishiwa katika kituo kipya. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye kasoro zilizobainika na idadi ya watumishi inaoneshwa katika **Jedwali Na. 7-9** hapa chini.

Jedwali Na. 7-9: Serikali za Mitaa Zenye Watumishi Ambao Taarifa Zao Hazijahuishwa Katika Mfumo wa LAWSON

Na.	Jina la Halmashauri	idadi ya Watumishi	Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Waajiriwa
1.	H/Jiji Arusha	21	2.	H/W Makete	18
3.	H/W Bagamoyo	2	4.	H/Jiji Mbeya	32
5.	H/W Chamwino	18	6.	H/W Mbulu	2
7.	H/W Hai	3	8.	H/W Mkinga	4
9.	H/M Ilemela	1	10.	H/W Moshi	22
11.	H/W Karatu	164	12.	H/M Moshi	27
13.	H/Mji Kasulu	32	14.	H/W Mpanda	7
15.	H/M Kigamboni	162	16.	H/W Mpwapwa	2
17.	H/W Kigoma	12	18.	H/Jij Mwanza	6
19.	H/M Kinondoni	13	20.	H/W Rombo	21
21.	H/W Kongwa	1	22.	H/W Siha	9
23.	H/W Kyerwa	6	24.	H/M Temeke	15
25.	H/W Mafia	7	26.	H/Mji Tunduma	5
				Jumla	**612**

Udhibiti duni wa Mfumo wa LAWSON pamoja na kushindwa kuhuisha taarifa za watumishi kwa kuweka taarifa zao halisi imeonekana kuwa sababu kuu ya udhaifu huu. Hali hii inasababisha taarifa za watumishi kutokuwa sahihi

wakati wowote zikihitajika kwa matumizi mbalimbali hasa wakati wa kustaafu.

Ninatoa wito kwa maofisa masuuli wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, OR-TAMISEMI, pamoja na Idara ya Utumishi kuhuisha kwa wakati taarifa za watumishi ndani ya Mfumo wa LAWSON ili kuwa na taarifa sahihi muda wote.

SURA YA 8

UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO NA MIRADI MINGINE

8.0 Utangulizi

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilitekeleza shughuli za miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia fedha za makusanyo ya mapato ya ndani, fedha kutoka serikali kuu, wahisani, na michango ya wananchi. Baadhi ya vyanzo vya fedha hizo ni ruzuku ya maendeleo ya serikali za mitaa (LGDG), ruzuku ya maendeleo ya sekta ya afya (HSCDG), mfuko wa kuchochea maendeleo ya jimbo (CDCF), malipo ya matokeo (EP4R), na mpango wa kuboresha ubora wa elimu (EQUIP-T).

Miradi mingine ya maendeleo iliyotekelezwa mwaka huu ilifadhiliwa kupitia Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Mfuko wa Afya ya Jamii, Mradi wa Uimarishaji wa Serikali za Mitaa, Mradi wa Ariel Glaser wa Kutokomeza UKIMWI kwa Watoto na Familia (AGPAHI), Mfuko wa Elizabeth Glaser wa Kusaidia Afya ya Mtoto (EGPAF), Menejimenti na Maendeleo ya Afya (MDH), Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Mradi wa Ushirika wa Kilimwengu kwa ajili ya Elimu - II (GPE II), Mradi wa Ufadhili kwa Matokeo (RBF), Mradi wa Maji, Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (SWASH), Uwajibikaji wa Taasisi kwa Jamii, na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Taarifa za fedha na utendaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mfuko wa Pamoja wa Afya (HBF) zimetolewa katika ripoti ya miradi ya maendeleo hivyo haijajumuishwa katika ripoti hii.

8.1 Mapungufu Yaliyoonekana Wakati wa Kupitia Ripoti ya Mapato na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

Wakati wa kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo, nilibaini masuala mbalimbali kuhusiana na matokeo ya utekekelezaji wa miradi na taarifa za fedha kama inavyoainishwa hapa chini.

8.1.1 Kasi Ndogo ya Matumizi ya Fedha kwa Ajili ya Kutekeleza Miradi ya Maendeleo Kiasi cha Sh. 202,874,554,913

Miradi mikubwa ya maendeleo inahusisha uwekezaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye miradi ya kudumu ikijumuisha uanzishaji wa miradi mipya, kudumisha, na kuongeza thamani ya miradi iliyopo na ambayo inakaa kwa muda mrefu. Miradi hii ya kudumu ni pamoja na majengo, mitambo, na miundombinu ya ofisi.

Tathmini ya mapato na matumizi ya miradi mikubwa ya maendeleo katika Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa ilibainika kuwa, jumla ya Sh. 1,031,295,956,766 zilipatikana ili kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020, kiasi cha Sh. 828,218,103,088 kilikuwa kimetumika na kuacha bakaa ya Sh. 202,874,554,913 sawa na asilimia 20 ya jumla ya fedha zilizokuwepo. Mwenendo wa mapato na matumizi umeoneshwa katika **Jedwali Na. 8-1**. Mchanganuo wa bakaa wa kila halmashauri umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-1**.

Jedwali Na. 8-1: Mwenendo wa Matumizi ya Fedha za Maendeleo

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Halmashuri	Fedha Zilizokuwepo (Sh.)	Fedha Zilizotumika (Sh.)	Bakaa ya Fedha (Sh.)	% ya Bakaa (Sh.)
2019/20	185	1,031,295,956,766	828,218,103,088	202,874,554,913	20
2018/19	185	923,650,715,481	664,353,118,381	259,297,597,100	28
2017/18	185	793,817,895,707	532,367,976,921	261,449,918,916	33
2016/17	185	796,708,520,009	531,652,643,504	265,055,876,504	33

Kupitia tathmini zaidi ya matumizi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopangwa kulingana na vyanzo mbalimbali vya fedha nilibaini kuwa kiasi cha fedha zisizotumika zilikuwa kati ya asilimia 53 na 76, sawa na wastani asilimia 41 ya fedha zilizokuwepo kutokana na vyanzo vya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ufafanuzi unaoneshwa katika **Jedwali Na. 8-2.**

Jedwali Na. 8-2: Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Vyanzo vya Ndani

Chanzo cha Fedha	Idadi ya H/Shauri	Fedha Zilizopo (A) (Sh.)	Matumizi Halisi (B)(Sh.)	Bakaa (Sh.)	% ya Bakaa (A-B)/A
TEA	3	389,665,761	169,731,028	219,934,733	56
EP4R	35	23,646,413,201	5,763,155,184	17,883,258,016	76
EGPAF	5	331,603,555	296,146,462	35,457,093	11
Equip-T	2	488,537,656	443,338,512	45,199,144	9
Global Fund	9	952,963,439	444,220,254	508,743,184	53
HSDG	3	2,808,001,367	2,142,172,499	665,828,868	24
LGCDG	4	2,765,293,785	2,374,831,293	390,462,492	14
Hazina	6	3,050,822,862	2,000,111,116	1,050,711,746	34
Mapato ya Ndani	4	14,490,363,258	13,466,525,971	1,023,837,287	7
ULGSP	2	5,412,520,708	5,059,434,935	353,085,773	7
Mfuko wa Jimbo	7	371,460,518	140,153,986	231,306,532	62
Vyazo vingine	15	2,892,557,998	1,797,673,917	1,094,884,081	38
Jumla	**95**	**57,600,204,108**	**34,097,495,157**	**23,502,708,950**	**41**

Kwa ujumla, kuwa na fedha ambayo haijatumika hadi mwisho wa mwaka inaonesha kwamba baadhi ya shughuli zilizopangwa zilikuwa zimetekelezwa kiasi au hazijatekelezwa kabisa kutokana na usimamizi na ufuatiliaji dhaifu pamoja na kuchelewa kutolewa kwa fedha.

Kutotumia fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa kunaziweka fedha hizo katika hatari ya kubadilishiwa matumizi na kutekeleza shughuli zingine ambazo awali hazikupangwa. Pia, huweza kuzuia wanufaika kupata manufaa yaliyotarajiwa ikiwa pamoja na ukuaji wa uchumi wa nchi. Vilevile, kunaweza kupelekea ongezeko la gharama za utekelezaji zinazotokana na ongezeko la bei ya vifaa na huduma. Mchanganuo wa hali ya matumizi ya fedha za miradi umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-2**.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka utaratibu madhubuti utakaohakikisha kuwa miradi yote ya maendeleo iliyotengewa fedha inatekelezwa na kukamilika kwa kuzingatia muda na gharama ili kuongeza manufaa yanayoweza kupatikana kwa jamii na nchi. Nininapendekeza zaidi kwa Hazina kuhakikisha fedha za maendeleo

zinatolewa kwa haraka kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa ili kuwezesha utekelezaji wa miradi kwa wakati na kukamilika kwa miradi iliyopangwa.

8.2 Masuala Yaliyobanika Wakati Wa Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Katika kipindi cha ukaguzi, halmashauri zilitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Tathmini yangu ya hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri 185 imebaini kuwa kulikuwa na miradi ambayo haikutekelezwa; miradi iliyokamilika lakini haijaanza kutumika; miradi iliyoko katika hatua mbalimbali za utekelezaji; na miradi ambayo fedha zake zilielekezwa katika shughuli zisizokusudiwa.

8.2.1 Miradi Ambayo Haikukamilika ya Thamani ya Sh. 184,006,287,121

Wakati wa tathmini ya hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, nilibaini miradi mbalimbali isiyokamilika yenye thamani ya Sh. 184,006,287,121 katika halmashauri 101. Hii ilisababishwa na kutolewa kwa fedha pungufu za miradi, usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa menejimenti za halmashauri, kutelekezwa kwa miradi kwa muda mrefu, pamoja na ushiriki usiotosheleza wa jamii katika utekelezaji wa shughuli za miradi. Gharama zilizotumika katika ujenzi wa miradi hii iliyotelekezwa kwa muda mrefu haziwezi kurudishwa ikiwa miradi itabaki bila kukamilika. Hali hii inaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma na hivyo jamii kutopata manufaa yaliyokusudiwa. Maelezo ya halmashauri zenye miradi ambayo haijakamilika yanaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-3**.

Kutokamilika kwa miradi kunaweza kupelekea kupitiwa upya kwa makadirio ya gharama za miradi (BOQ) kutokana na kuongezeka kwa gharama za miradi zinazoweza kusababishwa na ongezeko la bei za vifaa na huduma kutokana na athari hasi za mfumuko wa bei; na jamii zinazolengwa kuchelewa kunufaika kama ilivyokusudiwa.

Ninazishauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mikakati ya ukamilishaji wa miradi yote ambayo bado haijakamilika ili kuondoa uwezekano wa kuongezeka kwa gharama za utekelezaji. Pia, iimarishe usimamizi na ufuatiliaji wa miradi yote inayotekelezwa ngazi ya chini ili iweze kukamilika kwa wakati.

8.2.2 Miradi ya Thamani ya Sh. 14,903,593,785 Ambayo Haikutekelezwa

Nilikagua utekelezaji wa miradi katika Mamlaka 26 za Serikali za Mitaa na kubaini kuwa miradi iliyopangwa yenye thamani ya Sh. 10,550,487,205 haikuanza kutekelezwa licha ya fedha za utekelezaji wa miradi husika kuwepo. Kutotekelezwa kwa miradi kulisababishwa na kuchelewa kutolewa kwa fedha ambazo zilitolewa kati ya tarehe 26 na 30 Juni 2020 ambapo ulikuwa ni mwisho wa mwaka wa fedha.

Aidha, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwenye halmashauri 6 zenye thamani ya Sh. 4,353,106,580 hazikutekelezwa kutokana kutotolewa kwa fedha na Hazina. Halmashauri ambazo hazikutekeleza miradi zinaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-4**.

Kutotekelezwa kwa wakati miradi iliyopangwa kunaweza kupelekea kuwepo kwa mrundikano wa miradi inayotekelezwa na hivyo kuwa na uwezekano wa halmashauri kushindwa kutekeleza kwa ufanisi miradi hiyo. Hali hii pia inaashiria kutofikiwa kwa malengo hali inayoweza kupelekea halmashauri kushindwa kutimiza majukumu yake ya kutoa huduma kwa wananchi.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuweka utaratibu madhubuti ili kuhakikisha kuwa miradi yote iliyopangwa kutekelezwa na kutengewa fedha inatekelezwa na kukamilika kwa wakati. Pia, ziimarishe usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa ili kupata matokeo chanya.

8.2.3 Kasoro Zilizobainishwa Katika Utekelezaji wa Miradi Yenye Thamani ya Sh.1,184,868,370

Wakati wa uhakiki wa utekelezaji wa miradi, nilibaini mapungufu mbalimbali katika halmashauri 22 katika miradi ya maendeleo iliyotekelezwa yenye thamani ya Sh. 1,184,868,370. Kasoro hizi zilitokana na kukosekana kwa usimamizi wa karibu na uhaba wa msaada wa kitaalamu unaotolewa na idara za ujenzi za halmashauri pamoja na usanifu usioridhisha wa miradi hiyo, kwa kuwa usanifu wa miradi ulikuwa unakosa vipimo, michoro na miundo. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitapata hasara kwa kurekebisha kasoro zilizopo na kuongezeka kwa gharama za ziada kwenye miradi. Maelezo ya kasoro mbalimbali yameoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-5**.

Nininapendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye miradi yenye kasoro kuifanyia marekebisho; na zihakikishe kuna usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wakati wa utekelezaji wa miradi ili kufikia thamani ya fedha na kuitumia miradi hiyo.

8.2.4 Miradi Iliyokamilika Lakini Haitumiki Yenye Jumla ya Sh. 18,329,377,858

Wakati wa ukaguzi nilibaini miradi iliyokamilika yenye thamani ya Sh. 18,329,377,858 katika halmashauri 40 lakini haikuwa ikitumika kama ilivyopangwa. Hii inaonesha kuwa thamani ya fedha za miradi husika haipatikani na kuna hatari ya kuharibika kwa miradi hiyo. Ufafanuzi zaidi unatolewa katika **Kiambatisho Na. 8-6**.

Ninapendekeza kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuchukua hatua mwafaka ili kuhakikisha miradi yote iliyokamilika inatumika kikamilifu ili kufikia lengo lililokusudiwa na thamani ya fedha ya miradi.

8.3 Mapungufu Mengine Yanayotokana na Programu za Maendeleo

8.3.1 Asilimia 20 ya Ruzuku ya Fidia ya Thamani ya Sh.1,545,173,184 Kutopelekwa Ngazi za Vijiji

Mamlaka ya serikali za mitaa zilielekezwa kupeleka katika kata na vijiji asilimia 20 ya fedha za fidia iliyopokelewa kutokana na vyanzo vya mapato vilivyofutwa.

Katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi, nilibaini halmashauri 39 zilizopokea ruzuku ya fidia za vyanzo vya mapato vilivyofutwa (GPG) ambapo kiasi cha Sh. 1,545,173,184 ambacho ni asilimia 20 ya fedha hizo hakikupelekwa vijijini.

Kwa kutopeleka fedha, vijiji husika vimeshindwa kukamilisha shughuli zilizojipangia ikiwa pamoja na kulipia gharama za ofisi za vijiji. Vilevile, fedha ambazo hazijahamishwa huenda zikatumika kwa shughuli zingine za halmashauri. Orodha ya halmashauri ambazo hazikupeleka ruzuku ya fidia ya vyanzo kwenye kata na vijiji imeonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 8-3**.

Jedwali Na. 8-3: Orodha ya Halmashauri Ambazo Hazikupeleka Ruzuku ya Fidia ya Vyanzo Vilivyofutwa

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Bariadi	295,839,703	21	H/W Newala	14,118,000
2	H/W Maswa	122,144,800	22	H/W Biharamulo	10,375,000
3	H/W Chemba	2,611,800	23	H/W Kyerwa	4,014,600
4	H/W Kondoa	6,532,517	24	H/W Rorya	11,460,489.47
5	H/W Kongwa	54,571,800	25	H/W Busega	101,571,400
6	H/W Mpwapwa	57,971,575	26	H/W Meatu	81,855,733
7	H/W Buhigwe	178,004,179	27	H/W Lushoto	51,690,752
8	H/W Kasulu	14,491,400	28	H/W Bumbuli	49,710,600
9	H/W Kigoma	27,803,200	29	H/W Karagwe	39,512,800.00
10	H/W Iramba	11,294,800	30	H/Mji Babati	6,065,400
11	H/W Igunga	6,959,906	31	H/Mji Handeni	19,021,200
12	H/W Uyui	18,922,200	32	H/W Muheza	19,969,530
13	H/W Ngorongoro	93,013,742	33	H/W Longido	70,135,750
14	H/W Misenyi	22,584,236	34	H/W Handeni	64,287,064
15	H/W Itilima	56,536,567	35	H/W Bukoba	5,467,200
16	H/W Nanyamba	5,138,050	36	H/W Chalinze	3,371,830
17	H/W Ruangwa	6,080,800	37	H/W Masasi	2,642,180
18	H/W Ushetu	1,752,132	38	H/W Kibiti	14, 639,748
19	H/W Lindi	8, 687,000	39	H/W Kisarawe	2,512,199
		Jumla			**1,545,173,184**

Ninazishauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha udhibiti wa bajeti na utekelezaji wake na kuhakikisha kuwa asilimia 20 ya fedha za ruzuku ya fidia iliyopokelewa kutoka Serikali kuu inalipelekwa kwa wakati vijijini ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za maendeleo zilizopangwa.

8.3.2 Halmashauri Kutochangia Sh. 5,720,140,159 za Asilimia 10 ya Vyanzo vya Ndani Kwenda Mfuko Wa Wanawake, Vijana Na Watu Wenye Ulemavu

Kifungu cha 37(A) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwak 2019) kinazitaka halmashauri kuchangia asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Matakwa ya kisheria ya kuchangia mfuko huo yalianza mwaka wa fedha 2018/19 kwa Sheria ya Fedha Na. 4 ya Mwaka 2018 Kifungu cha 35. Tarehe 17 Desemba 2019 OR-TAMISEMI ilitoa barua yenye kumbukumbu

Na.CE.151/498/01/88 ambayo ilielekeza kufuta malimbikizo ya michango kwa miaka ya nyuma ambayo haikuchangwa katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.
Nilifanya ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa matakwa haya na kubaini kuwa halmashauri 82 hazikuchangia Mfuko jumla ya Sh. 5,720,140,159 kutoka kwenye mapato yake ya ndani. Orodha ya halmashauri ambazo hazikuchangia mfuko wa wanawake zimeonyeshwa katika **Kiambatisho Na. 7.**

Jedwali Na. 8-4 linaonesha mwenendo wa fedha ambazo hazikuchangwa kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Jedwali Na. 8-4: Mwenendo wa Kutochangia Asilimia 10 ya Mapato ya Halmashauri kwa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

Mwaka	Mamlaka za Serikali za Mitaa	Kiasi ambacho Hakijachangwa (Sh.)
2019/20	82	5,720,140,159
2018/19	115	9,930,902,514

Kutochangia katika Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kunakwamisha malengo ya Serikali ya kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kiuchumi na kupunguza umaskini.

Ninazishauri mamlaka husika za usimamizi zilizoainishwa katika Kanuni kuimarisha usimamizi na kuzifuatilia kwa karibu halmashauri ili kuhakikisha michango inalipwa kwa ukamilifu katika Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu na vikundi husika vinapewa mkopo ipasavyo.

8.3.3 Mikopo Isiyorejeshwa Yenye Thamani ya Sh. 27,790,189,049 Iliyotolewa kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

Mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ilikuwa na lengo la kukuza uchumi miongoni mwao kwa kuviwezesha kujihusisha na shughuli za maendeleo zinazolenga kuboresha kiwango cha maisha ya wananchi. Ili kuhakikisha fedha zinazochangiwa katika akaunti ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu zinazunguka, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuhakikisha udhibiti na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zinafuatwa ili

kuwezesha kiasi cha mikopo kilichotolewa kinarejeshwa kulingana na makubaliano yaliyofikiwa kati ya halmashauri na vikundi vya wanufaika.

Nilikagua mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020 katika halmashauri 130 na nilibaini kuwa mikopo ya kiasi cha Sh. 27,790,189,049 ilikuwa haijarejeshwa. Hii inaonesha kwamba halmashauri husika hazikufuatilia kwa ukaribu marejesho ya mikopo kutoka kwa vikundi kulingana na makubaliano. **Kiambatasho Na. 8-8** kinaonesha orodha ya halmashauri zenye mikopo ambayo haikurejeshwa.

Jedwali Na. 8-5 linaonesha kiwango cha mikopo isiyorejeshwa ya vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu kwa miaka minne mfululizo. Katika mwaka wa fedha 2019/20 inaonesha kuna ongezeko la mikopo ambayo haijarejeshwa kwa asilimia 6 ikilinganishwa na mwaka 2018/19. Hii inamaanisha kuwa halmashauri hazikufanya jitihada katika ukusanyaji wa mikopo.

Jedwali Na. 8-5: Mwenendo Wa Kutorejeshwa kwa Mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa Miaka Minne Mfululizo

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Halmashauri	Kiasi ambacho Hakijarejeshwa (Sh.)	Asilimia
2019/20	130	27,790,189,049	65
2018/19	111	13,794,359,981	59
2017/18	90	10,044,453,656	59
2016/17	84	5,809,326,477	63

Nininapendekeza kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya ufuatiliaji wa karibu ili mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inarejeshwa kwa mujibu wa makubaliano. Pia, kufanyike uhamasishaji na kujenga uelewa wa ulazima na umuhimu wa kurudisha mikopo ili vikundi hivyo viweze kurudisha mikopo bila shinikizo kwa lengo la kufikia malengo yaliyokusudiwa ya Mfuko ya kutoa mikopo kwenye vikundi mbalimbali.

8.3.4 Fedha Kutopelekwa Katika Akaunti Maalumu ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu Kiasi cha Sh. 3,072,080,867

Kanuni ya 22(1) na (2) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za Mwaka 2019 inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kufungua na kuendesha akaunti

maalumu ya mikopo na kuhakikisha kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mikopo na fedha za marejesho ya mikopo hiyo zinaingizwa katika akaunti maalumu ya mikopo.

Ukaguzi nilioufanya katika Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu na akaunti za benki zilizofunguliwa umebaini kuwa Mamlaka 28 za Serikali za Mitaa hazikuwa zimehamisha kiasi cha sh. 3,072,080,867 kutoka katika akaunti ya amana kwenda akaunti maalumu za mikopo ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ambazo zimefunguliwa ili kurahisisha shughuli za mikopo. Nina shaka kuwa fedha hizo zinaweza kutumika kutekeleza shughuli zisizokusudiwa na kuchelewa kutoa mikopo kwa vikundi vya wanufaika. Orodha ya halmashauri ambazo hazijahamisha fedha kwenda akaunti maalumu ya mikopo zinaonekana katika **Jedwali Na.8-6**.

Jedwali Na. 8-6: Orodha ya Halmashauri Ambazo Hazijahamishia Fedha Kwenye Akaunti Maalumu ya Mikopo

Na	Jina la Halmashauri	Kiasi kisichohamishwa (Sh.)	Na	Jina la Halmashauri	Kiasi Kisichohamishwa (Sh.)
1	H/W Magu	4,351,500	15	H/W Songea	14,066,500
2	H/W Misenyi	86,248,192	16	H/M Iringa	149,871,074
3	H/M Temeke	663,754,253	17	H/W Mpimbwe	59,781,500
4	H/M Ubungo	538,234,553	18	H/W Tarime	94,870,490
5	H/W Kaliua	56,282,458	19	H/W Mbinga	70,078,500
6	H/W Newala	74,618,600	20	H/W Mbalali	52,140,000
7	H/W Biharamulo	27,936,357	21	H/W Arusha	422,357,655
8	H/W Bumbuli	6,442,317	22	H/Mji Babati	2,310,840
9	H/W Mlele	9,891,806	23	H/W Kiteto	10,746,838
10	H/Mji Makambako	92,264,500	24	H/W Bagamoyo	176,000,000
11	H/Mji Njombe	95,216,152	25	H/W Kibaha	100,375,296
12	H/W Wanging'ombe	123,555,400	26	H/M Lindi	18,427,200
13	H/W Madaba	33,746,500	27	H/W Mafia	22,665,467
14	H/W Nyasa	20,399,100	28	H/W Kibiti	45,447,820
	Jumla				**3,072,080,867**

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye fedha za Mfuko Wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu katika akaunti ya amana zihamishe fedha hizo na kuziweka katika akaunti maalumu ya mikopo na kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa shughuli zilizokusudiwa.

8.3.5 Hasara Itokatokanayo na Kukataliwa kwa Madai ya Fedha za Bima ya Afya Kiasi cha Sh. 2,280,350,860

Tathmini niliyofanya katika zahanati, vituo vya afya, na hospitali katika Mamlaka 60 za Serikali za Mitaa kuhusiana na madai yaliyowasilishwa katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ikiwa ni gharama za matibabu kwa wagonjwa wanaotumia huduma za bima ya afya ilibaini kuwa madai ya kiasi cha Sh. 2,280,350,860 yalikataliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutokana na kutozingatia taratibu kama vile idhini batili, alama zisizofaa za magonjwa, kutozingatia miongozo ya matibabu, kutoonesha vipimo vya utambuzi, na kuingizwa kwa huduma ambazo hazikuwa katika Mfuko. Madai yaliyokataliwa yanaathiri uwezo wa zahanati, vituo vya afya na hospitali katika kutoa huduma za afya kwa jamii kwani hii ni sawa na kutoa huduma za matibabu bure.

Uhakiki zaidi wa madai yaliyowasilishwa katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulibaini kuwa madai yenye thamani ya Sh. 463,443,229 hayakurejeshwa kwa halmashauri 17 hadi tarehe 30 Juni 2020. Orodha ya halmashauri zenye madai yaliyokataliwa na madai yasiyorejeshwa kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yanaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-9**.

Nininapendekeza kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuata taratibu zinazotakiwa wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa wanaotumia huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuhakikisha madai yanajazwa ipasavyo kabla ya kuwasilishwa kwenye Mfuko. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwasiliane na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili ziweze kutoa mafunzo na semina kwa watumishi wa halmashauri kuhusu taratibu zinazohusiana na huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

8.3.6 Fedha za Ruzuku ya Uendeshaji, Fidia ya Ada na Chakula Ambazo Hazijapelekwa Shule za Msingi na Sekondari Kiasi cha Sh. 4,359,778,542

Wakati wa ukaguzi niliofanya kuhusu utekelezaji wa mpango wa elimu bila malipo nilibaini halmashauri 23 zilipata fedha pungufu za ruzuku ya uendeshaji wa shule na fidia ya ada kiasi cha Sh. 3,527,069,651 kwa shule za msingi na sekondari. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali ilitoa jumla ya Sh. 11,690,861,834 sawa na asilimia 77 ya kiasi cha Sh. 15,217,931,485 ya bajeti kwenye shule zilizokaguliwa.

Hata hivyo, fedha pungufu ziliyotolewa ni kinyume na mwongozo uliotolewa ambao unaitaka Serikali kuzifidia shule kiwango cha Sh. 10,000 kwa mwaka

kwa kila mwanafunzi katika shule za msingi; ambapo Sh. 6,000 zitapelekwa moja kwa moja shuleni Sh. 4,000 zitumike kununua vitabu katika ngazi ya Wizara na kuvipeleka shuleni. Wakati huohuo, fidia ya ada pamoja na ruzuku ya uendeshaji wa shule kiasi cha Sh. 25,000 hutolewa kwa kila mwanafunzi kwa shule za sekondari.

Hivyo, kutolewa kwa fedha chini ya kiwango kumehusishwa na taarifa zisizo toshelevu juu ya idadi halisi ya wanafunzi shuleni ambao walipata ruzuku ya uendeshaji pamoja na utekelezaji wa bajeti katika ngazi ya wizara. Kutolewa kwa fedha pungufu za ruzuku kuna athari mbaya juu ya utekelezaji wa sera na utendaji wa wanafunzi. Ufafanuzi unaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-10 (A)**.

Katika kufanya tathmini zaidi kuhusu ruzuku ya chakula shuleni, nilibaini kutolewa kwa fedha pungufu kiasi cha Sh. 832,708,891 katika halmashauri 9. Katika utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo, Serikali ilipanga kutoa Sh. 1,500 kwa siku kwa kila mwanafunzi katika shule za bweni. Athari ya kutolewa fedha pungufu ni pamoja na kusababisha mrundikano wa madeni ya wazabuni shuleni kama invyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-10 (B)**.

Vilevile, nilibaini kasoro katika baadhi ya shule kuhusu matumizi ya ruzuku ya sera ya elimu bila malipo. Uhakiki nilioufanya wa matumizi yaliyofanywa katika shule kwa halmashauri nne ulibaini kuwa jumla ya Sh. 71,808,967 zilitumika kinyume na mwongozo uliotolewa na Serikali. Orodha ya halmashauri zenye kasoro zinaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-10 (C)**.

Ninaishauri Serikali kuzingatia masharti ya bajeti kwa kutoa fedha kwa mujibu wa bajeti na kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa sera hii sambamba na idadi iliyopo ya wanafunzi. Aidha, menejimenti za shule zizingatie taratibu zilizoainishwa katika mwongozo wa matumizi ya fedha.

8.3.7 Uhaba wa Miundombinu Katika Shule za Msingi na Sekondari

Sera ya elimu ya msingi bila malipo iliyoanzishwa mwaka wa fedha 2015/16 imepelekea ongezeko la haraka la idadi ya watoto wanaoandikishwa darasa la kwanza. Uandikishaji wa darasa la kwanza umeongezeka kwa kiasi kikubwa na kusababisha msongamano katika madarasa, hivyo kuleta uhitaji mkubwa kwenye miundombinu mingine ya shule. Pia, kuna ongezeko kubwa la idadi ya watoto wanaostahili kudahiliwa kutoka shule za msingi kwenda sekondari kila mwaka. Nyongeza hii ya uandikishaji mashuleni inatakiwa kwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya shule.

Nilifanya tathmini ya utoshelevu wa miundombinu ya elimu katika halmashauri 51 hususani katika shule za msingi na sekondari na kubaini kuwa, kulikuwa na upungufu mkubwa wa miundombinu ya shule kama vile madarasa, ofisi, mabweni, maabara, vyoo, kumbi za chakula, madawati, meza, viti na nyumba za watumishi. Upungufu wa miundombinu huleta athari katika ubora wa elimu. Upungufu wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari unaoneshwa katika Jedwali Na. 8-7 na 8-8.

Jedwali Na. 8-7: Hali ya Miundombinu Katika Shule za Msingi

	Jengo la Utawala	Meza za walimu	Viti vya walimu	Nyumb za walimu	Madarasa	Matundu ya vyoo	Madawati
Mahitaji	9,313	54,791	62,646	66,435	77,437	142,750	1,074,795
Kilichokuwepo	4,705	27,802	33,361	11,785	39,284	59,106	608,789
Upungufu	4,608	26,989	29,285	54,650	38,153	83,644	466,006

Jedwali Na. 8-8: Hali ya Miundombinu katika Shule za Sekondari

	Jengo la Utawala	Meza za walimu	Viti vya walimu	Nyumb za walimu	Madarasa	Maabara	Matundu ya vyoo	Meza za wanafunzi	Viti vya wananfunzi	Mabweni
Mahitaji	1,073	70,603	68,979	25,965	16,415	3,303	30,346	393,910	387,558	823
Kilichokuwepo	463	53,508	52,149	4,008	13,632	1,257	18,573	328,699	328,615	287
Upungufu	610	17,095	16,830	21,957	2,783	2,046	11,773	65,211	58,943	536

Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zilikaguliwa zenye upungufu wa miundombinu kwa shule za msingi na sekondari zinaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-11** na **Kiambatisho Na. 8-12**.

Ninapendekeza kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI kuchukua hatua zinazoweza kurekebisha au kutokomeza tatizo la upungufu wa miundombinu ya shule ili kuimarisha ubora wa elimu nchini.

8.3.8 Mapungufu Katika Uendeshaji wa Mfuko Ulioboreshwa wa Afya ya Jamii

Serikali ilianzisha Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) chini ya Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii ya Mwaka 2001. Hivi sasa Serikali imeanzisha Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF) ili kurahisisha utoaji wa huduma bora, zenye usawa, na kwa bei nafuu. Mfuko huu umekusudiwa kutoa huduma nyeti na zenye kujali matabaka ya kijinsia kwa jamii za wanyonge ili kufikia malengo ya kitaifa. Mfuko huu unaendeshwa kwa jamii kuchangia fedha kila mwaka kisha Serikali inachangia kiasi saw ana kilichochangwa na mtu binafsi au familia. Mfuko huu ulioboreshwa una utaratibu wa kulipa kwa kudai fedha za iCHF kwa huduma zinazotolewa sawa na Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF).

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilifanya tathmini juu ya ufanisi wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF) katika kutekeleza malengo yaliyokusudiwa katika halmashauri 8 kama zilizoorodheshwa katika **Jedwali Na. 8-9** na kubaini changamoto zifuatazo:

- ✓ Mtandao usio thabiti katika maeneo ya kata na vijiji wakati wa usajili hivyo kucheleweshaji usajili wa kaya kwa wakati na upakiaji wa haraka wa taarifa.

- ✓ Uhaba wa simu na vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya usajili kama vile vitabu vya kusajili, fomu za madai (vitabu), kadi za usajili na fomu za kubadilishana katika vijiji ndani ya kata kwa ajili ya uandikishaji wa kaya.

- ✓ Mawasiliano duni kati ya halmashauri na katibu tawala wa mkoa juu ya usimamizi wa fedha zilizotolewa dhidi ya kiasi kilichorejeshwa hivyo hakuna usuluhishi unaofanywa katika madai.

- ✓ Hali ya madai yaliyowasilishwa na madai ya iCHF yaliyotayarishwa hayaoneshwi katika mfumo wa iCHF. Vilevile, takwimu za kaya zilizochangia zinatofautiana kutoka moduli moja hadi nyingine.

- ✓ Kuchelewa kurejeshwa kwa madai katika vituo vya afya kwa madai yaliyoibuliwa kwa kuzingatia huduma zinazotolewa; pia kuna fomula isiyobainishwa wakati wa kukokoa kiasi cha malipo kwa vituo vya afya.

- ✓ Mafunzo ya kutosha hayakutolewa kwa maofisa wa kusajili; hivyo hawakutumia vizuri Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Bima (IMIS) katika usajili wa kaya.

- ✓ Uhaba wa fedha katika kuwezesha usafiri wakati wa usajili na usimamizi katika kata.

Jedwali Na. 8-9: Orodha ya Halmashauri Zilizo na Kasoro

Na.	Jina la Halmashauri
1.	H/W Mbeya
2.	H/W Kyela
3.	H/W Rungwe
4.	H/W Njombe
5.	H/Mji Njombe
6.	H/Mji Mbinga
7.	H/W Tunduru
8.	H/M Songea

Aidha, nilipitia vitabu vya kukusanya mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa viwili. Hata hivyo, sikuweza kuthibitisha mapato yaliyokusanywa katika vitabu thelathini na nane (38) vya kukusanya mapato ambavyo stakabadhi zake zimefungwa kwa kiasi maalumu vyenye thamani ya Sh. 21,750,000 kwa sababu sikupewa vitabu hivyo vya risiti. Hivyo, mapato yanayotokana na vitabu hivi vya risiti hayakuweza kuthibitishwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 8-10**.

Jedwali Na. 8-10: Orodha ya Halmashauri Zenye Vitabu vya Risiti Visivyorudi

Na.	Jina la Halmashauri	Vitabu vya Risiti	Kiasi (Sh.)
1	H/W Uyui	31	11,250,000
2	H/W Bumbuli	7	10,500,000
	Jumla	**38**	**21,750,000**

Ninazishauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kuchukua hatua stahiki za kerekebisha mapungufu yaliobainishwa hapo juu ili kuhakikisha mfumo unatumika kwa ufanisi, na mapungufu ambayo nimeangazia hapo juu yanatatuliwa.

8.3.9 Utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo isiyoanzishwa na jamii

Kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya Mwaka 2009 kinaeleza kuwa, orodha ya miradi ambayo fedha kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zinaweza kutolewa itaibuliwa na jamii ya wakazi kutoka katika eneo la Jimbo. Pia, Kifungu cha 10(4) kinataka kila kata kuleta orodha ya miradi ya kipaumbele itakayowasilishwa katika Kamati ya Maendeleo ya Jimbo.

Nilikagua utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo katika Mamlaka 9 za Serikali za Mitaa na kubaini kuwa, miradi wenye thamani ya Sh. 219,755,150 ilitekelezwa kinyume na matakwa ya sheria na hakukuwa na ushahidi kwamba miradi iliyotekelezwa ilianzishwa na jamii za jimbo husika. Orodha ya halmashauri inaoneshwa katika **Jedwali Na. 8-11**.

Jedwali Na. 8-11: Orodha ya Halmashauri Zilizotekeleza Miradi Isiyoanzishwa na Jamii

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/Mji Korogwe	6,000,000
2	H/W Kyela	-
3	H/M Singida	26,575,000
4	H/W Biharamulo	32,570,000
5	H/W Butiama	50,499,000
6	H/W Bumbuli	10,420,900
7	H/W Karatu	45,629,000
8	H/W Pangani	17,635,250
9	H/W Longido	30,426,000
	Jumla	**219,755,150**

Aidha, Kifungu cha 19(1) kinataka miradi yote iliyo chini ya Sheria hii kuwa ya kijamii ili kuhakikisha kuwa faida zinazotarajiwa zinapatikana kwa maslahi mapana ya wakazi wa eneo husika. Pia, Kifungu cha 19(3) kinataka fedha zinazotolewa chini ya Sheria hii zisitumike kwa lengo la kusaidia taasisi au shughuli za kisiasa na kidini.

Hata hivyo, tathmini niliyofanya katika matumizi yaliyofanywa kupitia Mfuko wa Jimbo katika Mamlaka 6 za Serikali za Mitaa, nilibaini jumla ya Sh. 81,591,650 zilitumika kufadhili miradi ya taasisi za kisiasa na kidini, ambayo haikuwa na manufaa mapana ya jamii kinyume na matakwa ya

sheria. Orodha za Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotekeleza miradi kinyume na Sheria zipo katika **Jedwali Na. 8-12**.

Jedwali Na. 8-12: Orodha ya Halmashauri Zilizotumia Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Kugharamia Taasisi za Kisiasa na Kidini

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Ludewa	2,335,000
2.	H/W Tunduru	9,209,000
3.	H/W Songwe	4,710,000
4.	H/Msp Songea	38,000,000
5.	H/W Karagwe	6,902,400
6.	H/W Pangani	20,435,250
	Jumla	**81,591,650**

Ninazishauri Kamati za Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo kuzingatia masharti ya Sheria ya Mfuko na kuidhinisha na kuhamishia fedha kwenye miradi inayoanzishwa na wanajamii.

SURA YA 9

USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

9.0 Utangulizi

Mamlaka za Serikali za Mitaa hutumia rasilimali-fedha kutoka serikali kuu na kutoka katika makusanyo ya vyanzo vya ndani kununua bidhaa na huduma mbalimbali. Ununuzi wa kandarasi, bidhaa na huduma katika sekta ya umma ikijumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa huchukua kiwango kikubwa cha matumizi ya serikali hivyo inahitaji umakini katika kuangazia jinsi matumizi haya yanavyofanyika na kusimamiwa.

Sheria ya Manunuzi ya Umma inamtaka ofisa masuuli, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, kuhakikisha manunuzi ya bidhaa na huduma unafuata taratibu zilizowekwa katika sheria au kanuni zake.

Hivyo, Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 kinanihitaji nieleze katika ripoti yangu ya kila mwaka endapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikidhi vigezo na masharti ya sheria na kanuni zake wakati wa kufanya manunuzi.

9.1 Malipo Yasiyostahiki ya Sh. 563,638,450 Wakati wa Mchakato wa Manunuzi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008, nina jukumu la kuhakikisha kuwa matumizi yote ya fedha za umma yameidhinishwa ipasavyo na kutumika kwa madhumuni ambayo yamelengwa na kwa kuzingatia sheria, maelekezo, na miongozo mbalimbali.

Wakati wa utekelezaji wa jukumu hilo la kikatiba, niliweza kuokoa pesa za umma jumla ya Sh. 563,638,450 zisipotee au kutumika vibaya na wazabuni na maofisa wa serikali wasio waaminifu. Muhtasari wa malipo yenye makosa na kiasi kilichookolewa umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 9-1**.

Jedwali Na. 9-1: Fedha za Mmma Zilizookolewa kutoka Malipo Yasiyostahiki

Na	Jina la Halmashauri	Muhtasari wa Malipo Yasiyostahiki	Kiasi Kilichookolewa
1.	H/W Chunya	Makosa yaliyopelekekea kuongeza kiasi cha malipo katika hati za ukaguzi wa kazi za ujenzi tofauti na malipo halisi yaliyopasika kulipwa	326,843,491
2.	H/M Morogoro	Malipo ya awali (advance payments) ambayo hayakurejeshwa baada ya kuvunjwa kwa mkataba	44,114,375
3.	H/M Sumbawanga	Malipo kwa mkandarasi yanayozidi viwango vilivyotajwa katika mkataba	36,697,000
4.	H/M Sumbawanga	Malipo yasiyostahiki kwa ajili ya gharama ya bima ya mradi	36,242,873
5.	H/M Shinyanga	Kutorejeshwa kwa mwajiri gharama ya ziada zilizotokana na kuvunjika kwa mkataba	33,940,774
6.	H/M Sumbawanga	Malipo kwa mkandarasi mshauri bila ya kuwepo kwa dhamana ya benki kama mkataba unavyosema	32,080,000
7.	H/M Kinondoni	Malipo ya awali (advance payment) zaidi ya kiasi kilichotajwa na mkataba	31,620,171
8.	H/M Tabora	Makosa yaliyopelekekea kuongeza kiasi cha malipo katika hati za ukaguzi wa kazi za ujenzi tofauti na malipo halisi yaliyopasika kulipwa	12,594,977
9.	H/W Kakonko	Makosa yaliyopelekekea kuongeza kiasi cha malipo katika hati za ukaguzi wa kazi za ujenzi tofauti na malipo halisi yaliyopasika kulipwa	9,504,789
		Jumla	**563,638,450**

Maelezo ya mapendekezo ya ukaguzi na hatua zilizochukuliwa na menejimenti husika kurekebisha dosari zilizobainika ili kurejesha malipo yasiyostahiki zimefafanuliwa hapa chini.

- ✓ **Makosa yenye Thamani ya Sh. 326,843,4910 Katika Vyeti vya Malipo vya Muda Vilivyoidhinishwa**

  Katika mapitio ya mkataba Na. LGA/075/W/BLD/2016-2017/01 ulioingiwa mwaka wa fedha 2016/17 kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya na JV Sapa Construction Co. Ltd. ikishirikiana na Inter Frempa Co. Ltd. kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za halmashauri awamu ya kwanza wenye thamani ya Sh. 2,191,731,764, nilibaini makosa katika malipo yaliyoidhinishwa katika hati namba 3 hadi 5 za ukaguzi wa kazi zilizofanyika na kuidhinishwa kulipwa ambapo kuna na ziada ya Sh. 326,843,491 ambazo hazikusitahiki kulipwa.

  Nilishauri menejimenti ya halmashauri kurekebisha dosari katika hati za ukaguzi wa kazi zilizofanyika ili kuondoa malipo yasiyostahiki kwa Mkandarasi. Menejimenti ilikiri mapungufu haya na kuahidi kuyarekebisha na kunihakikishia kuwa makosa yaliyobainika yatarekebishwa kuepuka malipo zaidi ya kiwango kinachotakiwa kulipwa.

- ✓ **Fedha Sh. 44,114,375 za Malipo ya Awali Kutorejeshwa Baada ya Mkataba Kuvunjika**

  Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro iliingia mkataba Na. LGA/079/2018-2019/HQ/W/08 na Mkandarasi M/S Fast Construction Co Ltd. kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya mabasi ya Kaloleni uliosainiwa tarehe 18/10/2019 na kazi za ujenzi zilitarajiwa kukamilika ndani ya miezi minne.

  Hata hivyo, mkandarasi alishindwa kutekeleza kazi za ujenzi kulingana na makubaliano na hivyo kupelekea kuvunjika kwa mkataba tarehe 19 Februari 2020 mkandarasi akiwa tayari ameshalipwa malipo ya awali ya jumla ya Sh. 108,714,375. Hadi ukaguzi unafanyika, kiasi cha Sh. 44,114,375 kilikuwa bado hakijarejeshwa.

  Kufuatia pendekezo langu juu ya suala hili, menejimenti iliandika barua yenye kumbukumbu. Na. T20/MMC-145/Vol./191 ya tarehe 14/06/2020 na barua yenye kumbukumbu. Na.T20/MMC-145/Vol./190 ya tarehe 14/06/2020 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa M/S Fast Construction Co Ltd. na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara ya China kurejesha kiasi cha Sh. 44,114,375.

- ✓ **Malipo ya Sh. 36,697,000 Kwa Bei ya Wakandarasi Zaidi ya Viwango Vilivyowekwa Katika Mkataba**

  Mapitio ya cheti cha malipo namba saba yalibainisha kuwa, menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga iliidhinisha malipo ya Sh. 872,404,145 kwa mkandarasi. Hata hivyo, vifaa vya uwekaji wa madirisha ya chuma na ujenzi wa tenki la kutibu maji viliidhinishwa kwa bei kubwa kuliko iliyotajwa katika mkataba na kupelekea ziada ya malipo kiasi cha Sh. 12,135,000 kinyume na Kifungu cha 39.2 cha masharti ya jumla ya Mkataba Na. LGA/098/HQ/2018/19/W/10.

  Pia, kupitia uhakiki wa cheti cha malipo na.1 cha mkataba huo ilibainika kuwa, menejimenti iliidhinisha ununuzi wa vifaa vya mawasiliano kwa thamani ya Sh. 24,562,000, ingawa vifaa vilivyotajwa havikuthibitishwa kununuliwa na mkandarasi.

  Menejimenti imeanza kuchukua hatua za kurekebisha dosari hiyo na tayari imemwagiza M/S Cons Africa Limited kwa barua yenye kumbukumbu Na. SMC / C. 100/220/01/87 ya tarehe 03/12/2020 kukatwa kiasi cha Sh. 24,562,000 kutoka cheti cha malipo yatakayofuata kulingana na kifungu cha 45.6 cha masharti ya jumla ya mkataba.

- ✓ **Malipo ya Sh. 36,242,873 ya Gharama ya Bima Isiyostahiki**

  Mapitio ya jalada la mkataba Na. LGA/098/HQ/2018/19/W/10 ya ujenzi wa kituo cha mabasi cha kisasa cha Katumba Azimio katika Manispaa ya Sumbawanga ilibainisha kuwa, halmashauri ilijumuisha gharama ya bima ya Sh. 36,242,873 kwenye nukuu za gharama za mkataba (BOQ). Gharama hizo za bima zililipwa katika cheti namba moja kiasi cha Sh. 3,077,627; Cheti namba nne cha malipo kiasi cha Sh. 29,719,156; na cheti namba tano cha malipo kiasi cha Sh. 3,446,091 kinyume na masharti ya mkataba.

  Menejimenti ilinihakikishia kuwa itarekebisha dosari za malipo yasiyostahiki. Pia, kama sehemu ya hatua za kurekebisha, mkandarasi mshauri M/S Cons Africa Limited ameagizwa kupitia barua yenye kumbukumbu Na. SMC/C. 100/220/01/88 ya tarehe 04/12/2020 kutojumuisha kiasi kilicholipwa zaidi katika cheti cha

malipo kitakachofuata kulingana na kifungu cha 45.6 cha masharti ya jumla ya mkataba.

- ✓ **Kutorejeshwa kwa Sh. 33,940,774 Ambazo ni Gharama za Mwajiri Zitokanazo na Mkataba Kuvunjika**

Kifungu cha 68 cha masharti ya jumla ya mkataba kinaeleza kuwa, ikiwa mkataba utasitishwa kwa sababu ya mkandarasi kukiuka kwa kiwango kukubwa vipengele vya mkataba, meneja wa mradi atoe cheti cha thamani ya kazi iliyofanywa na vifaa vilivyonunuliwa baada ya kupunguza malipo ya awali yaliyokwisharejeshwa kufikia siku ya utoaji wa cheti hicho na asilimia itakayotumika kukokotoa thamani ya kazi ambazo hazijakamilika. Pia, Kifungu cha 27 cha Masharti Maalumu ya Mkataba kinataka asilimia itakayotumika kukokotoa kazi ambayo haijakamilika inayowakilisha gharama ya mwajiri ya kukamilisha kazi iwe asilimia 20.

Ukaguzi wa usimamizi wa mikataba ulibaini kuwa, halmashauri ilivunja mikataba hiyo miwili kwa sababu ya ukiukaji mkubwa wa vipengele vya mikataba uliofanywa na wakandarasi lakini makato ya gharama ya ziada ya mwajiri kumaliza kazi ambazo hazikutekelezwa wakati mkataba unavunjwa kiasi cha Sh. 33,940,774 hayakufanyika kutoka malipo ya mkandarasi kinyume na mahitaji ya mkataba kama ilivyoainishwa hapo awali. Maelezo ya mikataba iliyovunjwa yameoneshwa katika **Jedwali Na. 9-2**.

Jedwali Na. 9-2: Mikataba Iliyovunjwa

Namba ya Mkataba	Kiasi cha Mkataba (Sh.)	Thamani ya Kazi iliyofanyika (Sh.)	Gharama za ziada Mwajiri ambazo hazikukatwa (Sh.)
LGA/112/2019-2020/ULGSP/W/05	166,583,000	121,433,000	24,286,600
LGA/112/2019-2020/ULGSP/W/04 Lot 2	142,800,000	48,270,870	9,654,174
Jumla	**309,383,000**	**169,703,870**	**33,940,774**

Nilijulishwa na menejimenti kuwa, makato ya gharama za ziada za mwajiri kwa ajili ya kukamilisha kazi ambayo haikutekelezwa kiasi

cha Sh. 33,940,774 yatakatwa wakati wa kutoa cheti cha uvunjaji wa mkataba.

- ✓ **Malipo ya Sh. 32,080,000 ya Mkandarasi Mshauri Pasipo Dhamana Halali ya Benki**

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Mkandarasi Mshauri Cons Africa Ltd. alilipwa kiasi cha Sh. 105,900,000 kama jumla ya thamani ya mkataba ikijumuisha kiasi cha Sh. 21,180,000 (sawa na asilimia 20 ya mkataba) ambayo kwa mujibu wa masharti maalumu ya Mkataba Na. LGA/098/HQ/2019/2020/C/01, fedha hizo zingelipwa endapo angewasilisha dhamana halali ya benki ambayo hata hivyo haikuwasilishwa.

Pia, nilibaini kutofuatwa kwa masharti maalumu ya Mkataba Na. LGA/098/HQ/2019/2020/C/01 hivyo kusababisha madai na malipo yasiyostahiki ya kiasi cha Sh. 10,590,000 (sawa na asilimia 10 ya mkataba) kinyume na masharti ya mkataba.

Menejimenti iliahidi kuhakikisha inazingatia kanuni, sheria na masharti ya mikataba kama ilivyopendekezwa. Pia, mkandarasi mshauri atapewa hati ya kumtaka kurejesha malipo hayo yasiyostahiki kwa kuyakata katika vyeti vya malipo vitakavyofuata.

- ✓ **Malipo ya Awali Sh. 31,620,171 Yaliyolipwa Zaidi ya Kiwango**

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ilitoa malipo ya awali kwa mkandarasi JWTZ Kikosi cha 361 kwa kiwango cha asilimia 22 ya jumla ya mkataba wa Sh. 421,171,590 badala ya kiwango cha asilimia 15 kilichoainishwa katika Kifungu Na. 23.1 cha masharti ya jumla ya mkataba Namba LGA/017/2019-20/HQ/W/58 na kusababisha malipo ya ziada kiasi cha Sh. 31,620,171.

Menejimenti ilikubaliana na pendekezo langu la kurudisha malipo yaliyolipwa zaidi katika malipo ya cheti cha madai ya ujenzi yatakayofuata na kuimarisha udhibiti ili kuzuia kujirudia kwa dosari hiyo.

- ✓ **Kiasi Sh. 12,594,977 Kilichookolewa Kutokana na Makosa Yaliyogunduliwa Katika Vyeti vya Malipo Vilivyoidhinishwa**

Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilisaini mkataba Na. LGA/124/2018/2019/W/01 na M/s Chongqing International Construction Corporation (CICO) wenye jumla ya Sh. 6,668,527,455 wa kuboresha barabara za urefu wa kilometa 6.02 kwa kiwango cha lami ikiwa pamoja na Barabara za Kuya, Majengo, Nyerere, Transfoma na Heri. Mapitio ya malipo yaliyoidhinishwa katika cheti namba 1 cha malipo ilibainika kuwa malipo ya Sh. 9,600,000 yakifuatiwa na malipo ya Sh. 2,994,977 yalilipwa kimakosa kwa mkandarasi M/S Advanced Engineering.

Menejimenti ilinihakikishia kuwa Mkandarasi Mshauri M/S Advanced Engineering hajawasilisha cheti cha kuhitimisha kazi. Hivyo, Sh. 2,994,977 zitakatwa atakapowasilisha cheti cha madai yake ya mwisho. Pia, Mkandarasi M/s Chongqing International Construction Corporation (CICO) hajalipwa fedha za zuio; hivyo, kiasi cha Sh. 9,600,000 kitatolewa pindi atakapoomba kurejeshewa fedha zake za zuio.

- ✓ **Makosa Katika Cheti cha Malipo ya Ujenzi Kupelekea Ongezeko la Sh. 9,504,789**

Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko ilisaini mkataba na Kampuni ya M/S Sugwa Contractors Enterprises iliyokuwa ikishirikiana na JV M/S Chiganda Constructions wenye namba. LGA/139/HQ/2018/2019/W/01 kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi kwa gharama ya Sh. 2,146,996,676. Baada ya kupitia upya cheti namba 1 cha malipo ya ujenzi, nilibaini ziada ya Sh. 9,504,789 ambazo hazikutakiwa kulipwa.

Menejimenti ilikiri dosari hiyo na kuahidi kukata malipo hayo ya ziada katika hati za madai za mkandarasi huyo zitakazofuata.

9.2 Hasara Zilizobainika Wakati wa Manunuzi Na Usimamizi wa Mikataba

9.2.1 Hasara ya Sh. 186,316,650 Kutokana na Udanganyifu wa Nukuu za Gharama Katika Nyongeza ya Mkataba

Kifungu cha 42.2 cha masharti ya jumla ya mkataba kinasema kwamba "Ikiwa maelezo ya kazi ya nyongeza ya mkataba yatafanana na maelezo ya kazi katika mkataba mama, na ikiwa, kwa maoni ya meneja wa mradi, idadi ya kazi haiko juu ya kikomo kilichotajwa au wakati wa utekelezaji wake hausababishi gharama kubadilika, kiwango cha gharama katika mkataba

mama kitatumika kukokotoa bei ya kazi za nyongeza. Endapo kutakuwa na mabadiliko ya gharama, au ikiwa wakati wa utekelezaji wake utasababisha gharama kubadilika, nukuu ya mkandarasi itakuwa katika mfumo wa viwango vipya vya bei za kazi za nyongeza".

Nilitilia shaka ongezeko la gharama lisilo la kawaida katika kazi ya nyongeza ya mkataba Na. LGA/098/HQ/2018/19/W/10 ya ujenzi wa Stendi ya Kisasa ya Mabasi ya Katumba Azimio kiasi cha Sh. 186,316,650 ambalo liliidhinishwa na bodi ya zabuni mnamo tarehe 27 Novemba 2019.

Mkataba ulianza tarehe 24 Aprili 2019 na ilikuwa imepita miezi saba hadi tarehe ya kuidhinishwa nyongeza hiyo, ambapo kwa muda huo kupita ni jambo ambalo lingeweza kuathiri gharama za nyongeza ya kazi. Hata hivyo, ulinganifu wa bei katika mkataba wa awali na zile zilizo kwenye kazi ya nyongeza zilionesha ongezeko kubwa la bei hadi kufikia asilimia 2,567.

Uchambuzi kulingana na kiwango cha wastani cha mfumuko wa bei uliotolewa na Benki Kuu ya Tanzania katika kipindi hicho ulionesha kwamba bei haiwezi kupanda maradufu katika kazi za nyongeza ikilinganishwa na bei halisi ya mkataba ndani ya kipindi cha miezi 7 na hivyo kuonesha udanganyifu wa wazi uliolenga kusababisha hasara. Pia, menejimenti haikutunza kumbukumbu zozote zilizotumika kujiridhisha na bei hizo kubwa kupindukia kabla ya kuweka saini kati yake na mkandarasi.

Nininapendekeza hatua zichukuliwe dhidi ya mwenendo wa wajumbe wa bodi ya zabuni na maofisa wa serikali ambao walihusika katika ulaghai uliolenga kusababisha hasara ya fedha za umma kulingana na Kifungu cha 104(1e) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011.

9.2.2 Hasara ya Sh. 7,533,700 Kutokana na Udanganyifu wa Bei Zilizonukuliwa

Mnamo tarehe 18/03/2020, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ilinunua vifaa vya ujenzi kwa miradi inayoendelea kama ilivyoorodheshwa katika **Jedwali Na. 9-3** kwa gharama ya Sh. 18,481,300 kutoka Kamaka Co. Ltd. Hata hivyo, kwa wastani wa wiki moja baada ya ununuzi wa vifaa hivyo, menejimenti ilinunua vifaa kama hivyo kutoka Kansai Plascon (T) Ltd. kwa gharama ya Sh. 26,015,000 bila hata kufanya nukuu za ushindani wa bei. Matokeo yake, halmashauri ilipata hasara ya Sh. 7,533,700.

Jedwali Na. 9-3: Hasara Kutokana na Udanganyifu wa Bei Zilizonukuliwa

Bidhaa	Kiasi	Kansai Plascon (T) Ltd. (Sh.)	Kamaka Co. Ltd. (Sh.)	Hasara(Sh.)
1. Vinyl Silk Cream	56	9,240,000	6,787,200	2,452,800
2. Vinyl Silk Cream	18	2,970,000	2,181,600	788,400
3. Weather Guard Cream	48	6,960,000	4,800,000	2,160,000
4. Weather Guard Summer Blue	21	3,045,000	2,100,000	945,000
5. Hi Cover White	95	3,800,000	2,612,500	1,187,500
Jumla		**26,015,000**	**18,481,300**	**7,533,700**

Menejimenti ilikubali udhaifu uliobainika wakati wa ukaguzi na kuahidi kuimarisha udhibiti wa ndani juu ya manunuzi ya vifaa vya ujenzi na vitu vingine ili kuepusha upotevu zaidi wa pesa za umma ama kwa uzembe au udanganyifu.

Ninarudia wito wangu kwamba hatua kali zichukuliwe dhidi ya mwenendo mbaya wa wajumbe wa bodi ya zabuni na watumishi wa umma ambao walihusika kwa njia moja au nyingine katika hasara hii kwa kuzingatia Sehemu ya 104(1e) ya Sheri ya Manunuzi ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011.

9.3 Muhtasari wa Mwenendo wa Dosari za Manunuzi Zilizobainika

Mwenendo wa dosari zilizobainika katika manunuzi unakusudia kutoa ufahamu wa dosari hizo ikilinganishwa na miaka iliyopita kwa kutumia takwimu za kila kasoro ya manunuzi iliyooneshwa katika ripoti zangu ili kubaini iwapo mwenendo katika kujirudia kwa kasoro hizo umeongezeka, umepungua, au kubaki palepale. Uchambuzi huo umejikita katika halmashauri zote 185 pamoja na kiwango cha fedha kinachohusika katika kipindi cha miaka minne mfululizo.

Ilibainika kuwa uchambuzi wa mwenendo wa kasoro za manunuzi uliowasilishwa katika sura hii unaonesha matokeo chanya katika kupungua kwa kasoro kwa mwaka huu wa fedha ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia kuwa matokeo ya tathmini hii huenda pia yakaathiriwa na kupungua kwa fedha za manunuzi kutokana na kupungua kwa ufadhili wa miradi kutoka serikali kuu wakati wa mwaka wa fedha 2019/20 ikilinganishwa mwaka wa fedha 2018/19.

Hivyo, hatua madhubuti za kushughulikia dosari zilizobainika ziendelee kuimarishwa bila kujali mwenendo mzuri ulioonekana katika kipindi cha ukaguzi.

9.3.1 Mwenendo wa Manunuzi Usio wa Ushindani


Katika **Jedwali Na. 9-4** inaweza kubainishwa kwa ujumla kuwa kuna uboreshaji wa kufuata manunuzi ya ushindani kwani idadi ya halmashauri zilizohusika na manunuzi bila ushindani zilipungua kwa asilimia 26 kutoka halmashauri 74 mwaka 2018/19 hadi halmashauri 57 mwaka 2019/20 na kiwango cha fedha pia kimepungua kwa Sh. 23,317,813,694 sawa na asilimia 72.

Jedwali Na. 9-4: Mwenendo wa Manunuzi Usio wa Shindani

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
2019/20	57	9,143,192,259
2018/19	74	32,461,005,953
2017/18	48	3,936,238,236
2016/17	32	1,413,388,622

Mchoro Na.9-1 hapa chini kinaonesha mwenendo kwa kipindi cha miaka minne kwa halmashauri zilizobainika kuwa na manunuzi bila zabuni ya ushindani.

Mchoro Na. 9-1: Mwenendo wa Ununuzi Usio Shindanishi



9.3.2 Mwenendo wa Manunuzi Yaliyofanywa Bila Idhini ya Bodi za Zabuni


Taarifa iliyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-5** inaonesha kuwa kuna maboresho kwa kuwa manunuzi ambayo hayakuidhinishwa na bodi za zabuni za halmashauri husika yalipungua kwa Sh. 2,271,218,690 kutoka Sh. 9,234,451,830 zilizobainika katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi Sh. 6,963,233,140 katika mwaka wa fedha 2019/20 sawa na asilimia 25. Pia, kuna upungufu mkubwa katika idadi ya halmashauri zinazohusika na manunuzi bila kupata idhini ya bodi ya zabuni.

Jedwali Na. 9-5: Mwenendo wa Manunuzi Yaliyofanywa Bila Idhini ya Bodi za Zabuni

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
2019/20	39	6,963,233,140
2018/19	47	9,234,451,830
2017/18	32	9,047,221,353
2016/17	25	2,703,509,121

Mchoro Na. 9-2 hapa chini inaonesha mwenendo kwa kipindi cha miaka minne kwa halmashauri zilizobainika kuwa na manunuzi bila idhini ya bodi za zabuni.

Mchoro Na. 9-2: Mwenendo wa Ununuzi Bila Idhini ya Bodi ya Zabuni



9.3.3 Mwenendo wa Manunuzi Bila Mikataba ya Makubaliano Kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma

Jedwali Na. 9-6 linaonesha kuwa mwenendo wa bidhaa na huduma zilizonunuliwa na halmashauri kutoka kwa wasambazaji bila mikataba ya


makubaliano kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma imeongezeka kutoka Sh. 4,353,203,757 hadi Sh. 5,130,195,752 na halmashauri zilizohusika ziliongezeka kutoka halmashauri 34 zilizoripotiwa mwaka 2018/19 hadi kufikia halmashauri 39 zilizoripotiwa mwaka 2019/20.

Jedwali Na. 9-6: Mwenendo wa Manunuzi Bila ya Mikataba ya Makubaliano Kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
2019/20	39	5,130,195,752
2018/19	34	4,353,203,757
2017/18	18	923,836,408
2016/17	27	936,775,623

Mchoro Na. 9-3 hapa chini kinaonesha mwenendo kwa kipindi cha miaka minne kwa halmashauri zilizobainika kuwa na manunuzi bila ya mikataba ya makubaliano kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma.

Mchoro Na. 9-3: Mwenendo wa Ununuzi bila Mkataba Kutoka GPSA



9.3.4 Mwenendo wa Bidhaa Zilizopokelewa Bila Kukaguliwa au Kupimwa

Taarifa iliyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 9-7** inaonesha kuwa kuna uboreshaji kwani manunuzi au bidhaa ambazo zilikubaliwa bila kukaguliwa au kupimwa yalipungua kwa Sh. 1,904,409,219 kutoka Sh. 5,007,530,026 zilizoonekana katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi Sh. 3,103,120,807 zilizoainishwa katika mwaka wa fedha 2019/20 sawa na asilimia 38. Hata


hivyo, kuna ongezeko la halmashauri 1 katika manunuzi bila kukaguliwa au kupimwa kutoka halmashauri 43 hadi 44 kwa mwaka huu.

Jedwali Na. 9-7: Mwenendo wa Bidhaa au Huduma Zilizopokelewa Bila Kukaguliwa au Kupimwa

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
2019/20	44	3,103,120,807
2018/19	43	5,007,530,026
2017/18	31	1,412,005,295
2016/17	25	644,312,449

Mchoro Na. 9-4 hapa chini kinaonesha mwenendo kwa kipindi cha miaka minne kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizobainika kuwa na manunuzi ambayo yalikubaliwa bila kukaguliwa au kupimwa.

Mchoro Na. 9-4: Mwenendo wa Bidhaa Zilizopokelewa bila Kukaguliwa au Kupimwa



9.3.5 Mwenendo wa Manunuzi Yaliofanywa Nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka


Jedwali Na. 9-8 linaonesha kuwa manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka yalipungua kutoka Sh. 25,928,485,461 hadi Sh. 5,012,044,504 na halmashauri zilizohusika zilipungua kutoka 38 zilizoripotiwa mwaka 2018/19 hadi 17 za zilizoripotiwa mwaka 2019/20.

Jedwali Na. 9-8: Mwenendo wa Manunuzi Yaliofanywa Nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
2019/20	17	5,012,044,504
2018/19	38	25,928,485,461
2017/18	14	28,540,519,010
2016/17	21	2,384,412,108

Mchoro Na. 9-5 hapa chini unaelezea mwenendo kwa kipindi cha miaka minne kwa halmashauri zilizobainika kuwa na manunuzi nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka.

Mchoro Na. 9-5: Mwenendo wa Ununuzi Uliofanywa nje ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka



9.4 Dosari Zilizojitokeza Zaidi Katika Usimamizi wa Manunuzi Katika Mwaka Huu

Sehemu hii inaangazia tathmini na mambo ya kuzingatia kuhusu ukiukaji katika usimamizi wa manunuzi ya umma ambao ulijitokeza katika halmashauri nyingi. Lengo la tathmini hii ni kutoa mwelekeo kwa wadau wote na vyombo vingine vya udhibiti kuelekeza juhudi zao pamoja na rasilimali zingine katika kutatua dosari hizi ambazo kwa maoni yangu zinatia shaka.

9.4.1 Dosari Zilizojitokeza Zaidi Katika Manunuzi ya Mwaka Huu

Inadhihirika katika muhtasari wa dosari za manunuzi zilizoorodheshwa katika **Jedwali Na. 9-9** kwamba, manunuzi yasiyo na ushindani ndio kasoro inayoongoza ambapo manunuzi yenye thamani ya Sh. 9,143,192,259 katika halmashauri 57 yalifanyika bila ya ushindani wa bei.

Dosari zote zilizoorodheshwa zimejadiliwa katika aya zinazofuata pamoja hatua za marekebisho zilizochukuliwa na Serikali.

Jedwali Na. 9-9: Dosari Zilizojitokeza Zaidi Katika Manunuzi ya Mwaka Huu

Na.	Dosari Zilizobainika	Idadi ya H/Shauri	Kiasi (Sh.)
1.	Manunuzi yasiyo na ushindani	57	9,143,192,259
2.	Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kukaguliwa au kupimwa	44	3,103,120,807
3.	Manunuzi na tuzo za zabuni bila idhini ya bodi za zabuni	39	6,948,439,587
4.	Manunuzi kutoka kwa wasambazaji bila mikataba ya makubaliano kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma	39	5,130,195,752
5.	Manunuzi yaliyofanywa kupitia pesa taslimu	24	752,071,479
6.	Malipo ya bidhaa, kazi au huduma ambazo hazikupokelewa	24	1,561,310,401
7.	Manunuzi ya bidhaa na huduma bila mkataba mdogo	17	676,005,295
8.	Manunuzi yaliyofanyika nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka ulioidhinishwa na halmashauri	17	5,012,044,504
9.	Kutowasilisha ripoti za kila mwaka za utekelezaji wa ununuzi kwa PPRA	17	1,828,187,880
10.	Kutotumika kwa Mfumo wa Kitaifa wa Manunuzi ya Kimtandao (TANePS)	15	N/A
11.	Kununuliwa kwa vifaa zaidi ya mahitaji ya halmashauri	11	586,458,238
12.	Matengenezo ya magari ambayo hayajapitishwa TEMESA	10	153,057,506
13.	Nyaraka za manunuzi zinazokosekana kwa ajili ya ukaguzi	9	3,662,901,212

9.5 Halmashauri Zilizobainika Kuwa na Dosari Nyingi Wakati wa Manunuzi

Kati ya dosari za manunuzi 429 zilizobainika katika halmashauri zote 185, kasoro 153 sawa na asilimia 36 zilibainika katika halmashauri 24. Makosa mengi yaliyoonekana yalikuwa yanajirudiarudia katika halmashauri nyingi. Hata hivyo, halmashauri ambazo zilionesha dosari nyingi zaidi katika manunuzi zingefuatiliwa kwa karibu kwani zinaweza kuwa mwanya wa upotevu wa pesa za umma kupitia manunuzi. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zilionekana kuwa na dosari nyingi wakati wa manunuzi zinaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-10**.

Jedwali Na. 9-10: Halmashauri Zilizobainika Kuwa na Dosari Nyingi Wakati wa Manunuzi

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Dosari za Manunuzi
1.	H/M Kinondoni	9
2.	H/W Nkasi	9
3.	H/M Sumbawanga	9
4.	H/M Songea	9
5.	H/W Ushetu	9
6.	H/W Iringa	8
7.	H/W Itigi	8
8.	H/W Uyui	7
9.	H/W Kakonko	6
10.	H/W Tarime	6
11.	H/W Buchosa	6
12.	H/W Mbinga	6
13.	H/W Lushoto	6
14.	H/Jiji Arusha	5
15.	H/W Karatu	5
16.	H/W Mafia	5
17.	H/W Mkuranga	5
18.	H/W Moshi	5
19.	H/W Mbeya	5
20.	H/W Sengerema	5
21.	H/W Namtumbo	5
22.	H/W Tunduru	5
23.	H/W Momba	5
24.	H/W Kaliua	5

9.5.1 Manunuzi ya Thamani ya Sh. 9,143,192,259 Bila Ushindani

Mapitio ya kumbukumbu za manunuzi kwa mwaka 2019/20 yalibaini kuwa jumla ya Sh. 9,143,192,259 zililipwa na halmashauri 57 kwa ajili ya manunuzi ya kazi za ujenzi, bidhaa, na huduma bila kuzingatia mchakato wa zabuni na ushindani.

Ninasisitiza uzingatiaji wa Kanuni za 163 & 164 za Manunuzi wa Umma za Mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 ili kuhakikisha kuwa manunuzi yanafanyika kwa ushindani ili bei zinalizolipwa zioneshe thamani ya fedha zilizotengwa.

Orodha ya halmashauri ambazo zilinunua bidhaa na huduma bila ushindani na kiwango cha fedha kilichohusika zinaoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 9-1**.

Ninasisitiza halmashauri zihakikishe kuwa manunuzi ya siku zijazo yafanyike kwa kuzingatia ushindani wa zabuni ili kuwepo uwazi na haki katika matumizi ya fedha za umma.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini manunuzi ya bidhaa mbalimbali katika halmashauri 44 zenye thamani ya Sh. 3,103,120,808 zilizopokelewa bila kukaguliwa au kupimwa na kamati za ukaguzi kinyume na Kanuni za 244 na 245 za Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013. Orodha ya halmashauri ambazo zilipokea bidhaa bila kukaguliwa zinaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 9-2**.

Ninatoa wito kwa maofisa masuuli wa halmashauri husika kuteua kamati za ukaguzi wa bidhaa kabla hazijapokelewa kutoka kwa wauzaji ili kujiridhisha endapo bidhaa hizo zipo katika vipimo sahihi, ubora unaotakiwa na bei inayotakiwa.

9.5.2 Manunuzi Kutoka kwa Wazabuni Bila Kuwa na Mikataba ya Makubaliano Kutoka kwa Wakala wa Ununuzi Serikalini Sh. 5,130,195,752

Wakati wa ukaguzi, nilibaini Halmashauri 39 ambazo zimenunua bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni ambao hawakuwa na mkataba wa makubaliano kutoka Wakala wa Manunuzi Serikalini zenye thamani ya Sh. 5,130,195,752 kinyume na Kanuni ya 131(4)(b) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016. Orodha ya halmashauri ambazo zilinunua bidhaa na huduma kutoka kwa wasambazaji

wasioidhinishwa na Wakala wa Manunuzi Serikalini inaoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 9-3**.

Ninazisihi menejimenti za halmashauri husika kuhakikisha kuwa bidhaa na huduma zinazonunuliwa zifanyike kutoka kwa wazabuni ambao wamekidhi vigezo vilivyoainishwa katika sheria na kanuni za manunuzi.

9.5.3 Manunuzi na Utoaji Tuzo za Zabuni Zenye Thamani ya Sh. 6,948,439,588 Bila Idhini ya Bodi za Zabuni

Kinyume na Kanuni ya 55(2), 163(4) na 1985(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013, niliona katika kipindi hiki cha ukaguzi kwamba halmashauri 39 zilinunua bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. 6,948,439,588 bila idhini ya bodi ya zabuni. Orodha ya halmashauri na kiasi kinachohusika kinaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 9-4**.

Ninapendekeza kwa halmashauri husika kuhakikisha kuwa kabla ya manunuzi na utoaji wa zabuni zihakikishe zinapata idhini ya bodi za zabuni kama inavyotakiwa na sheria ya manunuzi wa umma na kanuni zake.

9.5.4 Malipo ya Bidhaa, Kazi au Huduma Zenye Thamani ya Sh. 1,561,310,401 Ambazo Hazikupokelewa

Kanuni ya 242(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 na Agizo la 70 la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 inaitaka taasisi inayonunua kupata ripoti juu ya upokeaji wa bidhaa kadri ya matakwa ya mikataba kisha kuidhinisha malipo kwa mzabuni mara moja.

Kinyume na Kanuni iliyotajwa hapo juu, nilibaini kuwa halmashauri 24 zililipa Sh. 1,561,310,401 kwa manunuzi ya bidhaa, lakini bidhaa hizo hazikuwa zimepokelewa na halmashauri husika. Orodha ya halmashauri na thamani ya bidhaa ambazo hazikupokelewa zinaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 9-11.**

Jedwali Na. 9-11: Orodha ya Halmashauri Zenye Malipo Kwa Bidhaa Ambazo Hazikupokelewa

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Tarime	366,512,812			
2.	H/M Kinondoni	48,620,725	14.	H/W Nyasa	42,335,036
3.	H/M Sumbawanga	24,562,000	15.	H/W Sengerema	106,219,293

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
4.	H/W Chamwino	36,397,500	16.	H/W Karatu	40,313,638
5.	H/Mji Kibaha	387,757,726	17.	H/Jiji Dodoma	9,875,000
6.	H/W Itigi	10,776,760	18.	H/W Mkalama	46,256,000
7.	H/W Nkasi	2,090,000	19.	H/W Iringa	12,738,214
8.	H/W Mpwapwa	9,948,799	20.	H/Mji Nanyamba	109,462,960
9.	H/M Bukoba	20,000,000	21.	H/W Kasulu	20,499,000
10.	H/W Igunga	12,251,500	22.	H/W Hanang'	68,777,094
11.	H/W Uyui	14,851,766	23.	H/Mji Makambako	74,182,872
12.	H/W Kakonko	42,421,456	24.	H/M Morogoro	46,055,250
13.	H/W Mbogwe	8,405,000		**Jumla**	**1,561,310,401**

Ninashauri halmashauri zinazohusika kuhakikisha kwamba bidhaa na huduma zinapokelewa na malipo yafanyike baada ya kuthibitisha usahihi wa viwango vya bidhaa kama ilivyoainishwa katika mkataba wa manunuzi ili kupunguza hatari ya upotevu wa fedha za umma kwa manunuzi hewa au yasiyoendana na mahitaji yaliyoainishwa.

9.5.5 Manunuzi Yenye Thamani ya Sh. 752,071,479 Yaliyofanywa kwa Fedha Taslimu

Kanuni ya 166 na Jedwali la Saba la Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 na marekebisho yake linaruhusu taasisi inayonunua kutumia pesa taslimu kufanya manunuzi madogomadogo ambapo ukomo ni hadi Sh. 5,000,000.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilibaini halmashauri 24 zilizokuwa zimetoa masurufu yenye jumla ya Sh. 752,071,479 kwa wafanyikazi mbalimbali kufanya manunuzi kwa fedha taslimu bila kuzingatia masharti yaliyowekwa na sheria husika. Orodha ya halmashauri na manunuzi yaliyofanywa kupitia fedha taslimu inaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-12.**

Jedwali Na. 9-12: Orodha ya Halmashauri Zenye Manunuzi Yaliyofanywa Kupitia Fedha Taslimu

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Momba	106,722,742			
2.	H/M Songea	66,070,060	14.	H/W Ludewa	22,265,000
3.	H/W Mbeya	65,562,520	15.	H/W Monduli	18,338,500
4.	H/M Kinondoni	56,000,000	16.	H/M Sumbawanga	17,940,000
5.	H/W Tunduru	50,913,500	17.	H/W Tarime	17,200,000

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
6.	H/W Iringa	49,749,000	18.	H/W Chunya	16,416,000
7.	H/W Ushetu	49,352,068	19.	H/W Kyela	12,263,000
8.	H/Jiji Dodoma	32,097,135	20.	H/W Hai	12,262,350
9.	H/Mji Handeni	29,821,649	21.	H/W Missenyi	10,750,000
10.	H/Mji Mbulu	26,855,700	22.	H/W Moshi	9,600,000
11.	H/Mji Tunduma	25,059,975	23.	H/W Rombo	5,478,500
12.	H/M Mpanda	23,365,200	24.	H/W Longido	5,103,780
13.	H/W Kilolo	22,884,800		**Jumla**	**752,071,479**

Sishauri matumizi ya masurufu katika mchakato wa manunuzi kwa sababu kuna athari nyingi zinazohusika na manunuzi kwa pesa taslimu, mojawapo ikiwa ugumu katika kudhibiti matumizi ya fedha hizo.

Ninatoa wito kwa halmashauri husika kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 166 na Jedwali la Saba la Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 wakati wa kuamua kufanya manunuzi kupitia masurufu.

9.5.6 Manunuzi Yenye Thamani ya Sh. 676,005,295 ya Bidhaa na Huduma bila Kutumia Hati ya Kuagiza Vifaa (LPO)

Agizo la 69 la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka bidhaa, huduma, na kazi zote zilizofanyika katika halmashauri kuthibitishwa kwa hati ya kuagiza vifaa (LPO), isipokuwa manunuzi madogo kwa pesa taslimu au huduma na malipo yanayojirudia.

Kinyume na Agizo lililotajwa hapo juu, nilibaini kuwa halmashauri 17 zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. 676,005,295 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila kutumia LPO. Orodha ya halmashauri zenye manunuzi ya bidhaa na huduma bila kutumia LPO inaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 9-13.**

Jedwali Na. 9-13: Orodha ya Halmashauri Zenye Manunuzi ya Bidhaa na Huduma bila Kutumia LPO

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Namtumbo	149,789,392	10.	H/W Meru	22,350,000
2.	H/W Momba	145,339,316	11.	H/Mji Handeni	21,845,719
3.	H/W Mkalama	61,058,969	12.	H/W Mbeya	21,672,911
4.	H/W Itigi	43,372,563	13.	H/W Kiteto	19,270,962
5.	H/W Mbarali	36,874,265	14.	H/Mji Mbulu	12,941,750

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
6.	H/W Bagamoyo	33,920,892	15.	H/W Shinyanga	11,049,320
7.	H/W Moshi	29,144,560	16.	H/W Iramba	9,571,784
8.	H/W Uyui	27,514,000	17.	H/Mji Babati	5,027,392
9.	H/W Kaliua	25,261,500		**Jumla**	**676,005,295**

Ninapendekeza halmashauri zihakikishe kwamba bidhaa na huduma na kazi zilizopokelewa halmashauri zinaagizwa kwa kutumia LPO.

9.5.7 Manunuzi Yenye Thamani ya Sh. 5,012,044,504 Nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka wa Halmashauri

Katika ukaguzi wangu, nilibaini Mamlaka 17 zilinunua bidhaa, kazi, na huduma za kiasi cha Sh. 5,012,044,504 ambazo hazikuwepo katika mpango wa manunuzi wa mwaka.

Kitendo hiki kinakiuka Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 ambapo inataka taasisi inayonunua kufanya makisio ya mahitaji yake ya bidhaa, huduma, na ujenzi kwa usahihi kadiri iwezekanavyo kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo zipo katika mpango-kazi na kujumuishwa katika makadirio ya kila mwaka.

Orodha ya halmashauri ambazo zilinunua bidhaa, huduma, na kazi za ujenzi nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka ulioidhinishwa inaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 9-14**.

Jedwali Na. 9-14: Manunuzi Nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/M Temeke	2,355,636,382	10.	H/W Mbinga	63,697,270
2.	H/W Mlimba	849,330,173	11.	H/M Mpanda	63,530,575
3.	H/Mji Kibaha	518,566,000	12.	H/Mji Mafinga	49,337,657
4.	H/W Nsimbo	288,400,000	13.	H/W Mufindi	36,108,426
5.	H/W Namtumbo	251,407,103	14.	H/Mji Nzega	26,232,202
6.	H/W Tunduru	201,366,276	15.	H/W Hanang’	18,800,000
7.	H/Mji Bunda	103,313,770	16.	H/W Kiteto	15,606,056
8.	H/W Serengeti	93,295,614	17.	H/W Mkuranga	3,417,000
9.	H/W Iringa	74,000,000		**Jumla**	**5,012,044,504**

Kupanga manunuzi ipasavyo kuna umuhimu si tu kwamba hufanya shughuli ziende vizuri bali pia huokoa fedha, wakati, na rasilimali. Pia, husaidia upatikanaji wa huduma na bidhaa kama inavyotakiwa ili kuwezesha kutekeleza kwa mafanikio, miradi na shughuli zingine.

Ninatoa wito kwa menejimenti za halmashauri husika kuhakikisha kuwa manunuzi yanafanywa kulingana na mpango wa manunuzi na kwa mujibu wa Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa mwaka 2016 ili kuepuka matumizi yasiyo katika mpango.

9.5.8 Matumizi Hafifu ya Mfumo wa Manunuzi wa Kielekitroniki (TANePS)

Sehemu ya 9(1)(j) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na marekebisho ya mwaka 2016, inataka Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma kubuni, kukuza, kuanzisha, kusimamia na kuhuisha mfumo ili kuwezesha manunuzi kwa njia ya kielekitroniki.

Pia, Kanuni ya 342 ya Kanuni za Manunuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi za umma kufanya manunuzi kwa kutumia mfumo wa kielekitroniki katika mchakato wote wa manunuzi ya umma.

Katika kipindi cha ukaguzi, nilibaini kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ilianzisha Mfumo wa Manunuzi wa Kielekitroniki (TANePS) ambapo mipango ya manunuzi, mialiko ya zabuni na utoaji wa kandarasi huwasilishwa kwa njia ya mtandao. Hata hivyo, kupitia tathmini katika sampuli ya halmashauri 15 nilibaini kuwa zilikuwa hazitumii kabisa au kulikuwa na matumizi hafifu ya mfumo huo.

Jedwali Na. 9-15: Matumizi Hafifu ya Mfumo wa Manunuzi wa Kielekitroniki

Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri
1.	H/W Meru	9.	H/W Bumbuli
2.	H/W Hai	10.	H/W Mbulu
3.	H/Jiji Korogwe	11.	H/W Kyela
4.	H/W Korogwe	12.	H/W Chalinze
5.	H/Jiji Arusha	13.	H/W Busokelo
6.	H/W Siha	14.	H/W Rungwe
7.	H/W Kibaha	15.	H/W Ukerewe
8.	H/W Buchosa		

Nilibaini pia kuwa uelewa mdogo wa mfumo na upungufu wa vitendeakazi kama kompyuta na mtandao wa uhakika wa intaneti umekwamisha ufanisi wa halmashauri katika matumizi ya TANePS.

Ninatoa wito kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma kushirikiana na OR-TAMISEMI ili kuwajengea uwezo wafanyikazi juu ya matumizi ya TANePS na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vyote muhimu vyitakavyowezesha matumizi ya mfumo huo katika halmashauri.

9.5.9 Vifaa Vyenye Thamani ya Sh. 586,458,238 Vilivyonunuliwa Zaidi ya Mahitaji

Aya ya 4(1) ya mwongozo wa *"force account"* wenye kumbukumbu Na.CAB.39/156/01/111 uliotolewa tarehe 10/05/2019 na OR-TAMISEMI unazitaka taasisi zinazofanya manunuzi kuandaa takwimu za vifaa vitakavyotumika katika utekelezaji wa miradi.

Hata hivyo, ama kwa sababu ya makadirio yasiyo sahihi au kuzidisha kwa makusudi vifaa vinavyohitajika, nilibaini wakati wa ukaguzi idadi kubwa ya vifaa vya ujenzi vyenye thamani inayofikia Sh. 586,458,238 katika halmashauri 11 vikiwa zimekaa bila kazi kwa muda mrefu. Orodha ya halmashauri ambazo zilinunua vifaa zaidi ya mahitaji inaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-16.**

Jedwali Na. 9-16: Vifaa Vilivyonunuliwa Zaidi ya Mahitaji

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Buhigwe	143,490,849
2.	H/M Songea	89,366,901
3.	H/M Kinondoni	87,978,723
4.	H/W Kaliua	64,364,337
5.	H/W Muleba	57,395,568
6.	H/M Tabora	43,890,780
7.	H/W Chamwino	39,300,000
8.	H/W Uyui	34,248,500
9.	H/W Kilolo	13,331,200
10.	H/W Sengerema	8,091,380
11.	H/W Bukoba	5,000,000
	Jumla	**586,458,238**

Nina wasiwasi kwamba, kutokana na ukosefu wa vifaa vya kuhifadhia kama ilivyoonekana katika halmashauri husika, kuna uwezekano wa kupoteza vitu vilivyonunuliwa kupitia wizi au kuharibika.

Ninatoa wito kwa halmashauri husika kuhakikisha kwamba, katika siku zijazo, takwimu za mahitaji ya vifaa kwa kazi za ujenzi zinapaswa kuandaliwa vizuri ili kuepuka manunuzi ya vifaa vingi kuliko mahitaji. Vilevile, zihakikishe kuwa vifaa ambavyo havikutumika vinahesabiwa na kutunzwa ipasavyo ili vitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

9.5.10 Malipo ya Matengenezo na Ukarabati wa Magari ya Serikali

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini baadhi ya matengenezo ya magari ambayo hayakupitishwa kwa Wakala wa Huduma za Mitambo na Umeme Tanzania (TEMESA) kinyume na Kanuni ya 137(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa katika Kanuni ya 47 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa mwaka 2016. Hata hivyo, nilibaini halmashauri 10 zilitumia Sh. 153,057,506 kwa ajili ya matengenezo ya magari yanayomilikiwa na serikali katika karakana binafsi bila kuhusisha TEMESA. Maelezo ya magari yaliyotengenezwa katika karakana binafsi yameoneshwa katika **Jedwali 9-17**.

Jedwali Na. 9-17: Matengenezo na Ukarabati wa Magari ya Serikali

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Sengerema	33,545,406
2.	H/W Nkasi	27,781,193
3.	H/W Mbinga	19,225,500
4.	H/W Tandahimba	17,978,366
5.	H/W Buchosa	16,021,822
6.	H/W Mkalama	13,965,599
7.	H/W Lushoto	9,157,740
8.	H/W Muheza	6,433,500
9.	H/W Kwimba	6,380,400
10.	H/W Lindi	2,567,980
	Jumla	**153,057,506**

Ingawa ipo haja ya halmashauri kufanya matengenezo ya magari kupitia TEMESA, nina wasiwasi juu ya uwezo wake hasa kifedha na kiteknolojia pamoja na nguvukazi ya ama kusimamia au kutoa huduma zinazotarajiwa kwa wateja wake.

Katika mapitio ya muundo wa taasisi pamoja na ufanisi wa TEMESA, nimebaini mapungufu kadhaa ambayo yanahitaji kushughulikiwa. Kaguzi zangu zilizopita juu ya usimamizi wa matengenezo ya magari ya serikali zilibainisha kuwa, matengenezo hayakusimamiwa kwa ufanisi kwani si magari yote yanayomilikiwa na serikali yalikaguliwa kabla ya matengenezo. Aidha, kulikuwa na ukosefu wa mrejesho uliotolewa kwa TEMESA juu ya ubora wa kazi zinazofanywa na karakana binafsi kwa sababu ukaguzi wa baada ya matengenezo haukufanyika.

Aidha, TEMESA haikuwa na utaratibu wa kufuatilia utendaji wa karakana binafsi na kulikuwa na ucheleweshaji wa uteuzi wa karakana binafsi kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa magari ya serikali.

Pia, katika kipindi cha miaka ya fedha 2017/18 na 2018/19, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ilitoa ripoti ya tathmini ya utendaji ambayo pamoja na mambo mengine, iliangazia udhaifu juu ya matengenezo na ukarabati wa magari uliofanywa na TEMESA. Ripoti hizo zilibainisha kuwa, huduma zilizokuwa zikitolewa na TEMESA si za kuaminika kutokana na ukweli kwamba vifaa vilivyotumika vilikuwa vya ubora wa chini hivyo kupelekea magari husika kuharibika mara tu baada ya kufanyiwa matengenezo au ukarabati. Zaidi ya hayo, ripoti hizo zilibainisha pengo la kiteknolojia hasa juu ya utambuzi wa matatizo ya magari ya kisasa na upungufu wa mafundi wanaohitajika katika kutoa huduma.

Ninatoa wito kwa Serikali kuhakikisha kuwa TEMESA inachukua hatua madhubuti za kurekebisha dosari zinazoikabili ikiwa pamoja na kuweka mkakati wa namna ya kupata rasilimali mbalimbali za kujiendesha kwa kuzingatia nguvu kazi, fedha, ubora, muda, gharama na masuala ya kiteknolojia; na kufanya mapitio ya kimuundo ili kuimarisha ufanisi katika utendaji wake na usimamizi mzuri wa matengenezo na ukarabati wa magari ya Serikali.

9.5.11 Kushindwa Kukidhi Mawanda ya Ukaguzi Kutokana na Kukosekana kwa Kumbukumbu za Manunuzi

Kanuni ya 15(6) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inataka nyaraka za kumbukumbu za manunuzi zihifadhiwe kwa kipindi kisichopungua miaka mitano kuanzia tarehe ya kukamilika kwa mkataba na ziweze kupatikana kwa wakati zitakapohitajika kwa waziri na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali, mamlaka au ofisa mwingine yeyote

aliyeidhinishwa na ofisa masuuli na kwa matakwa maalumu. Kumbukumbu hizo zinaweza kuhifadhiwa hadi miaka saba.

Kifungu cha 15(2) cha Sheria Na. 11 ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 pia kinamtaka ofisa masuuli wa taasisi iliyokaguliwa kuhakikisha kuwa mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali anapata wakati wote nyaraka zote za taasisi husika zinazomwezesha kutekeleza majukumu yake.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini baadhi ya mazingira ambayo yanaonesha udhaifu katika usimamizi wa kumbukumbu za manunuzi ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Udhaifu mkubwa ulionekana hasa katika utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi na usimamizi wa mikataba ambapo majalada ya manunuzi na mikataba ilikosa baadhi ya nyaraka muhimu.

Kwa mfano, nilibaini katika halmashauri sita manunuzi yenye thamani ya Sh. 3,020,708,828 yakiwa hayana nyaraka mbalimbali za kuyathibitisha. Kwa maana hiyo, wigo wangu wa ukaguzi ulikuwa mdogo, na sikuweza kuthibitisha uhalali wa manunuzi haya. Orodha ya halmashauri ambazo kumbukumbu za manunuzi zilikosekana inaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-18**.

Jedwali Na. 9-18: Halmashauri Ambazo Kumbukumbu za Manunuzi Zilizokosekana

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Mlele	2,195,082,530
2.	H/W Madaba	442,078,923
3.	H/W Tarime	234,144,400
4.	H/M Songea	80,891,880
5.	H/Mji Tunduma	61,311,095
6.	H/W Ushetu	7,200,000
	Jumla	**3,020,708,828**

Ninawakumbusha maofisa masuuli wa halmashauri husika kutunza ipasavyo kumbukumbu za manunuzi na nyaraka zingine zote zinazohusiana na manunuzi na kuziwasilisha pale zinapohitajika.

9.6 Upungufu katika Mikataba na Usimamizi wa Kazi kwa Njia ya "Force Account"

9.6.1 Mikataba Yenye Thamani ya Sh. 6,955,382,637 Iliyotekelezwa Bila Kuwa na Hati za Dhamana

Kanuni ya 29 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 inazitaka taasisi zote zinazofanya manunuzi kupewa dhamana ya utekelezaji wa kazi au mkataba kutoka kwa wazabuni walioshinda zabuni ili kuhakikisha utekelezaji wa mikataba unafanyika kwa uaminifu.

Hata hivyo, nilibaini miradi kadhaa iliyotekelezwa katika halmashauri nane yenye thamani ya Sh. 12,494,616,080 ambayo ama dhamana zake zilikuwa zimekwisha muda wake au kutokuwepo kwa dhamana kabisa.

Jedwali Na. 9-19: Orodha ya Halmashauri Zenye Miradi Iliyotekelezwa Bila Kuwa na Hati za Dhamana

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Mafia	5,539,233,443
2.	H/W Wang'ing'ombe	2,748,230,000
3.	H/W Madaba	2,291,322,509
4.	H/W Simanjiro	585,587,836
5.	H/W Ushetu	452,495,984
6.	H/W Mlele	439,016,506
7.	H/M Kinondoni	345,061,402
8.	H/W Ruangwa	93,668,400
	Jumla	**12,494,616,080**

Kutokuwapo kwa hati ya dhamana kunaziweka halmashauri kwenye hatari ya kupoteza rasilimali zake kwenye miradi inayotekelezwa pindi mkandarasi anapokiuka masharti na kushindwa kutekeleza mkataba.

Ninarudia pendekezo langu la mwaka uliopita kwamba menejimenti za halmashauri husika zihakikishe kuwa mikataba yote inayotekelezwa imewekewa dhamana kwa mujibu wa sheria na kanuni za manunuzi ili kulinda maslahi ya halmashauri na kuleta mafanikio katika utekelezaji wa miradi husika.

9.6.2 Mikataba Yenye Thamani ya Sh. 6,431,507,185 Ambayo Haikuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu Wa Serikali/Halmashauri

Kanuni ya 59 na ya 60 za Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) zinamtaka mwanasheria mkuu wa Serikali au mwanasheria wa taasisi inayofanya manunuzi kuhakiki mkataba uliotokana na makubaliano husika kabla ya mkataba kusainiwa na pande mbili husika. Mara tu baada ya kupokea ushauri wa kisheria, ofisa masuuli anatakiwa kuingiza marekebisho hayo katika rasimu ya mkataba.

Hata hivyo, katika halmashauri tisa nilizozikagua, nilibaini mikataba yenye thamani ya Sh. 7,880,846,290 ambayo haikuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au halmashauri.

Jedwali Na. 9-20: Orodha ya Halmashauri Zenye Mikataba Ambayo Haikuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali/Halmashauri

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Ushetu	4,562,307,443
2.	H/Jiji Arusha	1,395,904,605
3.	H/W Moshi	725,759,760
4.	H/Mji Kahama	603,675,407
5.	H/W Mbulu	351,604,600
6.	H/W Mpwapwa	99,648,805
7.	H/M Moshi	55,548,170
8.	H/W Mbinga	53,434,500
9.	H/W Singida	32,963,000
	Jumla	**7,880,846,290**

Kwa maoni yangu, kusaini mkataba kabla ya kuhakikiwa na kujumuisha maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali/halmashauri kunaziweka halmashauri husika katika hatari zinazoweza kusababishwa na kukiuka kisheria.

Ninapendekeza kwamba katika siku zijazo, halmashauri zihakikishe mikataba inahakikiwa na kujumuisha ushauri wa kisheria unaotolewa ili kuepuka migogoro ya kisheria inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mikataba hiyo.

9.6.3 Kuchelewa kwa Malipo ya Thamani ya Sh. 2,725,823,110 ya Kazi Zilizothibitishwa

Mapitio ya vifungu vya mikataba mbalimbali yalibainisha kuwa kila mwezi wakandarasi wanatakiwa kuwasilisha makisio ya thamani ya kazi zilizotekelezwa, ambazo zitakaguliwa na kuthibitishwa na meneja wa mradi ndani ya siku 28. Kushindwa kufanya hivyo, mkandarasi anaweza kutoza riba kwa kiasi kisicholipwa kwa kutumia kiwango cha riba katika soko.

Kinyume chake, nilibaini kuchelewa kwa malipo ya kazi zilizothibitishwa zenye thamani ya Sh. 3,161,373,378 katika halmashauri saba kama zinavyoorodheshwa hapa chini:

Jedwali Na. 9-21: Kuchelewa kwa Malipo ya Kazi Zilizothibitishwa

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/M Kigamboni	1,706,753,726
2.	H/W Ruangwa	646,171,354
3.	H/M Sumbawanga	325,097,746
4.	H/W Mafia	252,768,445
5.	H/M Iringa	117,827,815
6.	H/W Mbinga	64,954,008
7.	H/W Kilolo	47,800,284
	Jumla	**3,161,373,378**

9.6.4 Malipo ya Sh. 3,449,099,591 Yaliyofanywa Bila ya Vipimo Wala Kuthibitishwa na Wasimamizi wa Miradi

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi kuidhinisha malipo kwa kuzingatia vipimo na kwa vipindi au hatua zilizoelezwa katika mkataba. Hata hivyo, nilibaini katika halmashauri 24 malipo ya kazi za ujenzi zenye thamani ya Sh. 5,793,618,406 yalifanywa bila vipimo wala uthibisho wa mhandisi.

Jedwali Na. 9-22: Orodha ya Halmashauri zenye Malipo Yaliyofanywa bila Vipimo wala Kuthibitishwa na Wasimamizi wa Miradi

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/M Temeke	2,355,636,382			
2.	H/W Itigi	529,171,878	14.	H/W Kalambo	64,896,280
3.	H/W Buchosa	392,897,238	15.	H/W Masasi	61,036,760
4.	H/W Uvinza	353,443,477	16.	H/W Korogwe	39,640,720

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
5.	H/M Songea	343,980,659	17.	H/Mji Nanyamba	35,295,000
6.	H/W Mlimba	337,500,000	18.	H/M Kinondoni	31,620,171
7.	H/W Chunya	326,843,491	19.	H/W Mpimbwe	30,013,375
8.	H/W Nkasi	175,778,504	20.	H/W Newala	27,914,000
9.	H/W Momba	167,306,900	21.	H/W Bagamoyo	22,426,000
10.	H/Jiji Mbeya	162,000,000	22.	H/M Tabora	12,594,977
11.	H/W Nachingwea	146,340,805	23.	H/W Kakonko	9,504,789
12.	H/M Lindi	94,000,000	24.	H/W Uyui	5,000,000
13.	H/M Sumbawanga	68,777,000		**Jumla**	**5,793,618,406**

Halmashauri kushindwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 na udhibiti usioridhisha katika usimamizi wa mikataba ndio sababu za malipo ya kazi kufanyika bila vipimo. Hali hii inaweza kusababisha malipo kwa kazi ambazo hazikufanyika.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri husika kuimarisha mifumo yao ya udhibiti na usimamizi wa mikataba ili malipo yote ya kazi yafanyike kulingana na vipimo na kwa kazi zilizotekelezwa tu.

9.6.5 Miradi Iliyotekelezwa Bila Kufanya Tathmini ya Athari Kwa Mazingira

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inataka taasisi zinazofanya manunuzi kufanya tathmini ya athari kwa mazingira katika hatua ya awali ya mradi kabla ya mchakato wa manunuzi kuanza.

Kinyume chake, nilibaini miradi yenye thamani ya Sh. 2,541,183,834 katika halmashauri tatu ambazo zilitekelezwa bila kufanya tathmini ya athari kwa mazingira.

Jedwali Na. 9-23: Miradi Iliyotekelezwa Bila Kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/Mji Geita	1,798,647,724
2.	H/Mji Masasi	675,536,110
3.	H/Mji Tunduma	67,000,000
	Jumla	**2,541,183,834**

Utekelezaji wa miradi bila kufanya tathmini ya athari za mazingira unaziweka halmashauri katika hatari za kupata athari za mazingira ambazo zinaweza kuathiri ustawi wa jamii katika maeneo husika.

Ninapendekeza halmashauri zihakikishe kuwa katika siku zijazo tathmini ya athari kwa mazingira inafanyika kabla ya kuanza miradi ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza kuhusiana na mazingira.

9.7 Ukaguzi wa Kina Katika Usimamizi wa Mikataba

Ukaguzi wa kina wa usimamizi wa mikataba ulifanyika katika halmashauri 25 zilizopo katika mikoa 15 Tanzania Bara. Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo kuna mifumo madhubuti katika kusimamia mikataba ya ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwa na matumizi bora ya rasilimali na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

A. Maeneo yaliyokaguliwa

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilikagua masuala yanayohusiana na ufanisi katika usimamizi wa mikataba katika halmashauri 25 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-24**.

Jedwali Na. 9-24: Halmashauri Zilizokaguliwa

Na.	Mkoa	Halmashauri Zilizokaguliwa	Miradi/Mikataba Iliyokaguliwa
1.	Dodoma	H/W Bahi	1
2.	Geita	H/W Bukombe & Geita	2
3.	Katavi	H/W Mpanda & Nsimbo	2
4.	Kigoma	H/W Kigoma & H/M Kigoma-Ujiji	2
5.	Kilimanjaro	H/W Moshi & Rombo	4
6.	Lindi	H/W Lindi	1
7.	Mbeya	H/W Chunya & Mbarali	3
8.	Mtwara	H/W Masasi	2
9.	Mwanza	H/W Magu & Sengerema	2
10.	Njombe	H/Mji Makambako & H/W Wanging'ombe	2
11.	Pwani	H/W Mkuranga	2
12.	Rukwa	H/W Kalambo & Sumbawanga	2
13.	Ruvuma	H/W Namtumbo	1
14.	Singida	H/W Ikungi & H/M Singida	2
15.	Tanga	H/W Lushoto & Mkinga	2
Jumla			**30**

Ukaguzi huu umefanyika kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2005); na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008, Kifungu

cha 10 pamoja na Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Kikaguzi (ISSAI). Sheria hizi zinanipa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa ufanisi (thamani ya fedha) kwa lengo la kuthibitisha uwekevu, tija, na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma zinazoelekezwa kwenye wizara, idara na wakala wa serikali, serikali za mitaa, mashirika ya umma, na taasisi nyinginezo.

Kwa kuzingatia hatua kuu nne katika usimamizi wa mikataba/miradi ambazo ni sababu ya uhitaji wa mradi; taratibu za zabuni zilizotumika; ufanyaji wa tathmini na utoaji tuzo wa mkataba; na usimamizi wa utekelezaji wa mradi na ufikiaji wa malengo, nimeonesha ukiukwaji wa taratibu zilizowekwa kisheria na kuhitimisha kwa kutoa mapendekezo.

Mawanda ya ukaguzi yalihusisha miradi 30 ya maji yenye thamani ya Sh. 62,016,521,705. Kati ya mikataba iliyokaguliwa, mikataba 27 (87%) ilinunuliwa kupitia zabuni za ushindani wa kitaifa wakati miradi 4 (13%) ilitumia njia ya 'force account'. Sampuli hiyo ilijumuisha miradi iliyotekelezwa kuanzia miaka ya fedha 2013/14 na 2018/19 pamoja na miradi mingine inayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2019/20. **Jedwali Na. 9-25** linaonesha miradi iliyokaguliwa kwa kila mwaka.

Jedwali Na. 9-25: Mawanda ya Ukaguzi wa Kina Katika Usimamizi wa Mikataba

Mwaka	Idadi Ya Miradi	Asilimia (%)	Kipindi wa Utekelezaji (Miaka)
2013/14	5	17	7
2014/15	2	7	6
2015/16	1	3	5
2016/17	5	17	4
2017/18	11	36	3
2018/19	3	10	2
2019/20	3	10	1
Jumla	**30**	**100**	

Jedwali Na. 9-25. linaonesha asilimia 80 ya miradi iliyokaguliwa imetekelezwa kwa zaidi ya miaka 3 hadi 7 bila kutimiza malengo yaliyokusudiwa ya kusambaza maji kwa jamii. Utekelezaji wa miradi kwa muda mrefu umesababishwa na ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi, mchakato wa tathmini usiofaa ambao umesababisha kutolewa zabuni kwa wakandarasi wenye uwezo mdogo wa kifedha na kitaalamu, pamoja na uzoefu mdogo wa wakandarasi ikilinganishwa na ugumu na aina ya miradi wanayopewa.

Katika halmashauri 25 zilizokaguliwa, nimebaini mapungufu 25 ambayo yanahitaji kushughulikiwa na Serikali.

B. Masuala Muhimu Yaliyojiri Wakati wa Ukaguzi wa Kina wa Mikataba

Mapungufu yaliyojitokeza katika sehemu hii yanahusiana na halmashauri 25 kama inavyoelezwa hapa chini:

9.7.1 Kutoshirikisha Jamii Katika Uchaguaji wa Miradi

Kanuni ya 168 (1)(a) ya Kanuni za Manunuzi wa Umma za Mwaka 2013 inataka ushiriki wa jamii katika kubuni miradi kwa nia ya uendelevu au kufikia malengo husika ya kijamii ya miradi.

Katika mapitio ya majalada ya mikataba Na. LGA/161/2017-2018/BHL/W/05/LOT wenye thamani ya Sh. 600,702,298 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji kwa Vijiji vya Mtakuja na Songambele katika ya Halmashauri ya Wilaya Nsimbo nilibaini kuwa tarehe 31 Oktoba 2018, menejimenti ya halmashauri iliwasilisha muundo wa mradi Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ajili ya kuidhinishwa na Wizara ilipitisha muundo huo tarehe 8 Januari 2019. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi wowote unaoonesha ushiriki wa jamii husika katika uchaguaji wa mradi huo.

Kwa maoni yangu, kutoshirikishwa kwa jamii wakati wa uanzishaji wa miradi kunazuia hali ya umiliki na uendelevu wa miradi hiyo.

Ninapendekeza katika siku zijazo, menejimenti za halmashauri zihusishe na kushirikisha jamii katika uchaguaji wa miradi na utambuzi wa mahitaji ili kuongeza umiliki na uendelevu wa miradi husika.

9.7.2 Kuanzishwa kwa Miradi Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 3.8 Bila Umiliki wa Ardhi na Upembuzi Yakinifu

Sehemu ya 29 (1)(b) ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 Sura ya 334 inasema "Endapo kamishna anaamua kutoa haki ya umiliki kwa mtu ambaye anamiliki ardhi au yupo katika ofa ya kumilikishwa, atatoa cheti kinachojulikana kama cheti cha umiliki wa ardhi".

Katika Halmashauri ya Wilaya Masasi, matanki 11 ya usambazaji wa maji yenye thamani ya Sh. 432,212,850 yalijengwa kwenye ardhi ambayo haikuwa na milki ya kisheria ikimaanisha kuwa upembuzi yakinifu wa kisheria haukufanyika kabla ya mradi kuanza. Aidha, katika Halmashauri ya

Wilaya ya Sumbawanga nilibaini kuwepo kwa mizozo kutokana na mabadiliko ya eneo la shughuli za kibinadamu kuzunguka eneo la bwawa kutoka mita 60 hadi 500 wakati wa utekelezaji wa mradi. Hii ilisababishwa na menejimenti ya halmashauri kutofanya upembuzi yakinifu wa kisheria na wa kitaalamu ili kutenganisha eneo la mradi kwa lengo la kuepusha athari za kilimo kwenye bwawa. Maelezo ya mikataba yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 9-26**.

Jedwali Na. 9-26: Miradi Iliyoanzishwa Bila Umiliki wa Ardhi na Upembuzi Yakinifu

Mkoa	Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)
Rukwa	H/W Sumbawanga	Ujenzi wa bwawa la maji Kijiji cha Ikozi awamu ya II	LGA/097/2017/2018/WS/W/05	2,943,086,780
Mtwara	H/W Masasi	Ukarabati wa miundombinu ya maji kuanzia Mwena hadi Vijiji vya Liloya	LGA/083/2016 LOT 01/W/37	857,962,800
Jumla				**3,801,049,580**

Kwa maoni yangu, kuanzisha miradi bila upembuzi yakinifu na kukosekana kwa hatimiliki ya eneo la mradi kumesababisha mzozo wa ardhi na kunaweza kusababisha gharama za miradi kuongezeka na hivyo kupoteza fedha za serikali.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri kuhakikisha mazungumzo yanafanyika kwa faida ya pande zote ikiwa pamoja na kupata sehemu zingine za ardhi kwa ajili shughuli za kilimo za kijiji ili kuepuka hasara zinazohusiana na migogoro. Katika siku zijazo, halmashauri zihakikishe zinapata hati za umiliki wa ardhi na kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa miradi ili kuepusha migogoro na upotevu wa fedha.

9.7.3 Kushindwa Kutathmini Athari za Mazingira kwa Miradi Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 23.6

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inasema "taasisi inayofanya manunuzi ya kazi yoyote, inapaswa kufanya tathmini ya athari za mazingira katika hatua za maandalizi ya mradi na kabla ya manunuzi kuanza". Aidha, Kifungu cha 81(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kinaelekeza kufanyika kwa tathmini ya athari za mazingira kabla ya kutenga fedha au kuanza kwa mradi.

Nilibaini mikataba 15 (asilimi 37 ya mikataba iliyokaguliwa) yenye thamani ya Sh. 23,671,175,752 ilitekelezwa bila kufanya tathmini ya athari za mazingira. Vilevile, nilibaini kutofanyika kwa tathmini ya athari ya mazingira kulisababisha uharibifu wa miundombinu ya mradi wa usambazaji maji wa Mgumile katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma-Ujiji na kusababisha upotevu wa Sh. 48,873,250. Orodha ya mikataba iliyotekelezwa bila kufanyiwa tathmini ya athari za mazingira inaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-27**.

Jedwali Na. 9-27: Mikataba Iliyotekelezwa Bila Kufanyiwa Tathmini ya Athari za Mazingira

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)
H/W Nsimbo	Ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji cha Mtakuja na Songambele	LGA/161/2017-2018/BHL/W/05 /LOT 2	600,702,298
H/W Sumbawanga	Ujenzi wa bwawa la maji Kijiji cha Ikozi awamu ya II	LGA/097/2017/ 2018/WS/W/05	2,943,086,780
H/W Kalambo	Ujenzi wa mradi wa maji Mambwekenya	LGA/144/2016-2017/KDC/W/02	651,008,400
H/M Kigoma-Ujiji	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Mgumile	LGA/042/2013-2014/12	721,438,645
H/W Bahi	Ujenzi wa miundombinu ya maji katika Kijiji cha Mkakatika	LGA/024/2017/ 2018/W/02-LOT II	637,897,271
H/W Magu	Manunuzi ya vifaa na ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Nsola-Bubiza	LGA/90/W/2013 /2014/42 LOT 03	1,001,742,500
H/W Sengerema	Ujenzi wa kisima cha maji Kijiji cha Kasisa	"FORCE ACCOUNT"	321,536,644
H/W Bukombe	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Nampalahala	LGA113/2017/2 018/RWSSP/03 LOT II	514,915,618
H/W Ikungi	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Mtunduru	LGA/146/2018/ 2019/W/02	405,007,269
H/M Singida	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Mungumaji	LGA/115/SMC/2 018/2019/W/NO . 1	339,375,031
H/W Mbarali	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Luduga na Mawindi awamu ya I	LGA/076/W/201 4-2015/27 Lot1	1,007,832,375

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)
	Ujenzi wa mradi wa maji Vijiji vya Luduga na Mawindi awamu ya II	LGA/076/W/2014-2015/27 Lot2	3,683,571,612
H/W Chunya	Ujenzi wa mradi wa maji Mji wa Makongolosi	LGA /075/W/2017/2018/29	2,809,674,260
H/W Lushoto	Ujenzi wa mradi wa maji Vijiji vya Shume, Manolo na Madala	LDC/LGA/004/RWSSP/PHASE I& II/2013-2014/W/11	2,961,216,624
H/W Mkinga	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Mwakijembe	LGA/133/2015-2016/HQ/W/20	1,742,436,894
H/W Mkuranga	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Mwanambaya	LGA/012/WS/2017/2018/W/01-02	2,347,737,221
	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Mkerezange	LGA/012/WS/2017/2018/W/01-03	981,996,310
	Jumla		**23,671,175,752**

Kwa maoni yangu, kutekeleza miradi bila tathmini ya athari za mazingira kumeziweka halmashauri kwenye hatari za mazingira ambazo zinaweza kuwa mbaya kwa ustawi wa jamii zinazohusika. Vilevile, kulisababisha upotevu wa Sh. 48,873,250 kutokana na kuharibika kwa mradi uliokuwa umejengwa na inaweza kusababisha upotevu zaidi wa rasilimali za umma.

Ninapendekeza kwa menejimenti za halmashauri husika kuhakikisha katika siku zijazo tathmini ya athari ya mazingira inafanyika kama inavyotakiwa kisheria kabla ya kuanza kwa miradi ili kuepusha athari kwa mazingira na upotevu wa rasilimali za umma.

9.7.4 Kuanzisha Miradi Bila Kibali cha Ujenzi na Mipango ya Maeneo ya Miradi

Kwa mujibu wa Kanuni za Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji, Udhibiti na Uendelezaji), Sura 124(1)(c) ya Mwaka 2008 na Tangazo la Serikali Na. 242 la Tarehe 24/10/2004) "Hakuna mtu anaruhusiwa kujenga au kuanza kujenga jengo lolote hadi awe amepata kibali cha ujenzi kutoka mamlaka husika. Aidha, Kanuni ya 22(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016) inaelekeza uainishaji

wowote wa mipango, michoro, miundo na ujenzi uandaliwe kutokana na malengo, sifa za kitaalamu, na ubora wa ujenzi.

Mapitio ya mikataba iliyochaguliwa yalibaini ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika Kijiji cha Nyakagwe Geita ambapo miradi yenye thamani ya Sh. 428,367,976 ilianzishwa bila kibali cha ujenzi na mpango wa eneo la mradi.

Kwa maoni yangu, kutopata vibali vya ujenzi na kutokuwa na mipango ya maeneo ya miradi kunaweza kusababisha faini na uharibifu wa miradi na hivyo kupoteza fedha za umma.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri husika kupata vibali vya ujenzi na kuwa na mipango ya maeneo ya miradi inayoendelea na siku zijazo.

9.7.5 Miradi ya Ujenzi Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 3.4 Haikujumuisha Mipango ya Manunuzi ya Mwaka Iliyoidhinishwa

Kanuni ya 69(7) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inasema, “taasisi inayofanya manunuzi inapaswa kuandaa mpango wa manunuzi kwa mahitaji ambayo yamepitishwa katika bajeti ya mwaka husika wa fedha au kama malipo yatalipwa kwa mwaka wa fedha unaofuata, malipo ya fedha hizo yawe yalitengewa bajeti”.

Nilikagua mipango ya mwaka ya manunuzi na kubaini kuwa mikataba miwili yenye thamani ya Sh. 3,458,002,398 haikujumuishwa kwenye mipango ya manunuzi ya mwaka ikimaanisha miradi ilitekelezwa bila mipango. **Jedwali Na. 9-28** linaonesha orodha ya miradi iliyotekelezwa ambayo haikuwepo katika mipango ya manunuzi.

Jedwali Na. 9-28: Miradi Iliyotekelezwa Ambayo Haikuwepo Katika Mipango Ya Manunuzi

Mkoa	Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)
Rukwa	H/W Sumbawanga	Ujenzi wa bwawa la maji Kijiji cha Ikozi awamu ya II	LGA/097/2017/2018/WS/W/05	2,943,086,780
Geita	H/W Bukombe	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha	LGA113/2017/2018/RWSSP/03 LOT II	514,915,618

Mkoa	Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)
		Nampalahala awamu ya II		
Jumla				**3,458,002,398**

Kwa maoni yangu, utekelezaji wa miradi isiyopangwa yenye thamani ya Shilingi Bilioni 3.4 unaweza kusababisha mchakato mbovu wa manunuzi na matumizi yasiyopangwa. Mbali na hilo, inaweza kusababisha kushindwa kutekeleza miradi iliyopangwa na kutengewa bajeti.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri zihakikishe katika siku zijazo manunuzi yote yanazingatia mipango ya manunuzi na bajeti ili kuepusha matumizi yasiyopangwa.

9.7.6 Kushindwa Kutenga Fedha Kabla ya Miradi Kuanza na Kusababisha Ucheleweshaji wa Malipo kwa Wakandarasi na Huduma ya Maji kwa Jamii

Kanuni ya 75(1) na (3) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inaitaka taasisi inayofanya manunuzi kutenga fedha kabla ya kuanza kwa shughuli za manunuzi na ambapo mkataba unaendelea kwa miaka kadhaa, mgawanyo wa fedha unaweza kutolewa kila mwaka.

Nimebaini halmashauri 7 zilianza kutekeleza mikataba 7 (ikiwa na miezi 6 hadi mwaka mmoja wa utekelezaji) yenye thamani ya Sh. 13,678,605,730 bila kutengewa fedha. **Jedwali Na. 9-29** lina orodha ya halmashauri na miradi ambayo ilitekelezwa bila kutengewa fedha.

Jedwali Na. 9-29: Miradi Iliyotekelezwa Bila Kutengewa Fedha

Mkoa	Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)
Kilimanjaro	H/W Moshi	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Tella Mande	LGA/046/2017/2018/W/01	905,475,000
Katavi	H/W Nsimbo	Ujenzi wa mradi wa maji Vijiji vya Mtakuja na Songambele	LGA/161/2017-2018/BHL/W/05/LOT 2	600,702,298
Kigoma	H/W Kigoma	Ujenzi wa mradi wa maji Vijiji vya Kaseke, Kimbwela, na Nyamoli	LGA/043/2016/2017/W/15	1,163,496,000

Mkoa	Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)
Singida	H/W Ikungi	Ujenzi wa mradi wa maji kwa Kijiji cha Mtunduru	LGA/146/2018/2019/W/02	405,007,269
Ruvuma	H/W Namtumbo	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Likuyusekamaganga	LGA/105/CTR/2016/2017/W/RWSSP/01	4,915,864,910
Lindi	H/W Lindi	Ujenzi wa mradi wa maji Vijiji vya Cheleweni, Narunyu, Tandangongoro na Muungano	LGA/053/2017/2018/HQ/W/35/LOT 2	2,726,843,629
Tanga	H/W Lushoto	Ujenzi wa mradi wa maji Vijiji vya Shume, Manolo na Madala	LDC/LGA/004/RWSSP/PHASE I& II/2013-2014/W/11	2,961,216,624
Jumla				**13,678,605,730**

Kwa maoni yangu, kutekeleza miradi bila kutenga fedha kumesababisha kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi na kukamilika kwa miradi mapema. Aidha, hali hii inaweza kusababisha gharama za miradi kuongezeka na hatari ya riba inayoweza kudaiwa na wakandarasi kwa sababu ya kuchelewa kulipwa.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri kutenga na kutoa fedha kabla ya kuanza kwa shughuli za manunuzi na kuzingatia utekelezaji wa miradi kwa awamu kama hakutakuwa na fedha za kutosha.

9.7.7 Miradi Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 23.3 Ilitekelezwa Bila Washauri na Kusababisha Ucheleweshaji wa Huduma ya Maji kwa Jamii

Kanuni ya 127 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inataka taasisi kuteua mshauri wa ujenzi ili kuwa na ufanisi wa kazi na kuingia mkataba na mshauri aliyechaguliwa kwa kutoa muda wa kutosha kwa mshauri huyo kukagua nyaraka za zabuni kabla ya kutoa zabuni hiyo. Vilevile, Kifungu cha 4.2.3 cha Mwongozo wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji wa Mwaka 2016 kinaitaka miradi yote inayozidi gharama ya Shilingi Bilioni moja (1) kubuniwa na kusimamiwa na washauri.

Katika ukaguzi wa majalada ya mikataba ya miradi iliyochaguliwa, nimebaini halmashauri mbili zilitekeleza mikataba mitatu yenye thamani ya Sh. 23,376,725,445. Katika miradi hii, washauri hawakuhusika kuhakiki miundo ya miradi na kusimamia utekelezaji wake. Hali hii ilisababisha kuongezeka kwa muda (miradi ilichukua miezi 19 hadi 30 kutoka miezi 6 hadi 12 iliyopangwa) wa miradi kwa sababu ya kusimamishwa kwa kazi na kushindwa kukabili mabadiliko ya mawanda, wakati, na matokeo kinyume na maagizo. Orodha ya miradi iliyotekelezwa bila washauri inaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-30**.

Jedwali Na. 9-30: Miradi Inayotekelezwa Bila Washauri

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Tarehe ya Kuanza Na Kumaliza Ujenzi	% Ya Utekelezaji
H/W Sumbawanga	Ujenzi wa bwawa la maji Kijiji cha Ikozi awamu ya II	LGA/097/2017/2018/WS/W/05	2,943,086,780	02.10.2018 - 01.04.2019	50
H/W Wanging'ombe	Ujenzi wa mradi wa maji Igando - Kijombe	LGA/153/2017/2018/W/01	12,437,407,360	09.07.2018 - 08.07.2019	20
H/M Makambako	Ujenzi wa mradi wa maji Vijiji vya Usetule na Mahongole	LGA/166/2018/2019/W/01	7,996,231,305	23.05 2019 - 22.11.2019	17
	Jumla		**23,376,725,445**		

Kwa maoni yangu, kutekeleza miradi bila washauri kumesababisha kusimama kwa kazi ili kusubiri wataalamu kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa sababu ya kutokuwepo kwa wataalamu wakati wa utekelezaji wa mradi. Vilevile, imechangia kucheleweshaa kukamilika kwa miradi kwa zaidi ya miezi 13 na hivyo kucheleweshaa huduma ya maji kwa walengwa.

Ninapendekeza kwa menejimenti za halmashauri husika kushirikisha washauri katika utoaji wa ushauri wa kitaalamu na usimamizi mzuri katika utekelezaji wa miradi. Aidha, menejimenti zihakikishe zinashirikisha wataalamu wa mabwawa ili kuzuia kuchelewesha zaidi ukamilishaji wa miradi na hatari ya kutekeleza miradi bila mwongozo wa kitaalamu.

9.7.8 Mikataba Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 3.5 Imetekelezwa Bila Uanishaji wa Sifa

Kanuni ya 239 (8) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inataka taasisi zinazofanya manunuzi zitangaze zabuni za kazi ikiwa tu imeandaa michoro, maelezo kamili, na makadirio thabiti ya gharama. Kifungu cha 7, Sehemu ya II (Maagizo kwa Wanunuzi Zabuni) na Kifungu cha 2.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba yaliyopo katika Mwongozo wa Nyaraka za Zabuni wa mwaka 2018 (uliorekebishwa mwaka 2019) kinaagiza uainishaji wa sifa za mradi kuwa sehemu ya nyaraka za mwongozo wa utoaji zabuni na mkataba.

Nimebaini kuwa Halmashauri ya Sumbawanga ilitekeleza mkataba Na. LGA/097/2017/2018/WS/W/05 wenye thamani ya Sh. 2,943,086,780 wa ujenzi wa bwawa la maji katika Kijiji cha Ikozi awamu ya II na Halmashauri ya Kalambo ilitekeleza mkataba Na. LGA/097/2016-2017/KDC/W/02 wenye thamani ya Sh. 651,008,400 wa ujenzi wa mradi wa usambazaji maji wa Kijiji cha Mambwekenya. Mkataba huu ulitekelezwa bila uainishaji wa sifa za zege, chuma kwa uimarishaji, aina na daraja la bomba, kujaza mifereji ya bomba, vifaa vya mbao na vitambaa, rangi, ukandamizaji, na vifaa vya mashimo.

Vilevile, nilibaini mkandarasi alifanya majaribio ya uimara wa mgandamizo zegemiraba na majaribio ya chujio la maji na chujio kavu. Hata hivyo, nilishindwa kubaini iwapo vipimo vilifanikiwa au la kwa sababu ya kutokuwepo kwa uainishaji wa sifa.

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa uainishaji wa sifa kunaweza kusababisha kazi ya kiwango cha chini kwa sababu ya utumiaji wa vifaa duni na hivyo kupoteza rasilimali za umma.

Ninapendekeza kwa menejimenti za halmashauri kuainisha vipimo vinavyohitajika kwa kazi zinazoendelea. Vilevile, kuhakikisha katika siku zijazo, uainishaji unaopendekeza sifa za kitaalamu au ubora wa kazi na

mahitaji ya njia za majaribio ziwekwe kwenye nyaraka za zabuni na kuingizwa kwenye mkataba uliosainiwa.

9.7.9 Usanifu wa Miradi Wenye Mapungufu Iliyosababisha Gharama za Ziada za Sh. 171,610,300 na Kuchelewesha Kukamilika kwa Miradi

Kanuni ya 69(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inasema "Mipango ya manunuzi itaanza katika hatua ya usanifu wakati wa utambuzi na hatua za maandalizi ya mradi".

Nimebaini kisa kimoja katika Halmashauri ya Kigoma-Ujiji ambapo gharama za mradi zilibadilika kutoka Sh. 549,828,345 hadi Sh. 721,438,645 (ongezeko la Sh. 171,610,300) kwa sababu ya makosa katika usanifu ambao ulisababisha mabadiliko ya eneo la chanzo cha maji. Aidha, nilibaini kulikuwa na mabadiliko ya eneo lililopangwa kutoka 1222m hadi 1230m (tofauti ya 8m) katika ujenzi wa tanki la maji lenye mita za ujazo 135 na urefu wa mita 6 na kusababisha migogoro ya ardhi kati ya halmashauri na wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Halmashauri ya Wilaya Geita. Mabadiliko ya usanifu wa tanki kutoka tanki la juu lililoinuliwa kwa mita 6 hadi tanki la ardhini yalichelewesha kukamilika kwa mradi huo kwa mwezi mmoja. Miradi yenye usanifu yenye mapungufu imeorodheshwa katika **Jedwali Na. 9-31**.

Jedwali Na. 9-31: Miradi Yenye Usanifu wenye Mapungufu

Mkoa	Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama za Mkataba (Sh.)
Kigoma	H/M Kigoma-Ujiji	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mgumile	LGA/042/2013-2014/12	721,438,645
Geita	H/W Geita	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Nyakagwe	2019/20	428,367,976
Jumla				**1,149,806,621**

Kwa maoni yangu, kutekeleza miradi bila usanifu sahihi kumesababisha mabadiliko ya eneo la chanzo cha maji na hivyo kuongezeka kwa gharama kwa Sh. 171,610,300. Kwa kuongezea, kasoro hii imezua migogoro ambayo inaweza kusababisha gharama za mradi kuongezeka na kuchelewesha utekelezaji wake.

Ninapendekeza kwa menejimenti za halmashauri kuhakikisha katika siku zijazo, miradi inasanifiwa kwa usahihi wakati wa hatua ya kupanga ili kuzuia ucheleweshaji na gharama kuongezeka.

9.7.10 Kukosekana kwa Nyaraka za Mchakato wa Manunuzi kwa Miradi Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 2.5

Kanuni ya 15(1) (b-d) na (6) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inataka taasisi za manunuzi kutunza kumbukumbu za manunuzi ikiwa pamoja na matangazo ya zabuni, uteuzi wa wazabuni, na utoaji wa zabuni kwa muda usiopungua miaka mitano tangu tarehe ya kukamilika kwa mkataba.

Ukaguzi wangu wa majalada ya zabuni za mikataba iliyochaguliwa umebaini kutokuwepo kwa nyaraka muhimu za shughuli za manunuzi. Nyaraka zilizokosekana zilizuia ukaguzi wa miradi iliyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 9-32**.

Jedwali Na. 9-32: Miradi Ambayo Nyaraka za Manunuzi Zilikosekana

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama za Mkataba (Sh.)	Nyaraka Zilizokosekana
H/W Mpanda	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Kabungu	LGA.099/2017/2018/W/WATER/02/Lot 1	634,810,489	Mpango wa manunuzi, mihtasri ya kikao cha bodi ya zabuni kupitisha tangazo la zabuni na mihtasari ya kikao cha bodi ya zabuni na kamati ya fedha na mipango kupitisha mzabuni aliyeshinda na nakala ya barua zilizotumwa kwa wazabuni walioshindwa.
H/M Kigoma - Ujiji	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mgumile	LGA/042/2013-2014/12	721,438,645	Mkataba, nyaraka za zabuni, taarifa ya tathmini ya zabuni, mihtasari ya kitengo cha usimamizi wa manunuzi na bodi ya zabuni, vyeti vya malipo, dhamana ya mkataba, hati za malipo, taarifa za

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama za Mkataba (Sh.)	Nyaraka Zilizokosekana
				utelekezaji wa mradi, taarifa ya tathmini ya athari za mazingira, barua ya kukubaliwa zabuni, na barua za kuongeza muda wa utekelezaji wa mradi.
H/W Kigoma	Ujenzi wa mradi wa maji wa Vijiji vya Kaseke, Kimbwela, na Nyamoli	LGA/043/2016/2017/W/15	1,163,496,000	Barua za uteuzi wa wajumbe wa kufanya tathmini ya zabuni, na barua za kuonesha nia ya kutoa zabuni kwa mkandarasi aliyeshinda.
	Jumla		**2,519,745,134**	

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa nyaraka za zabuni kunazuia wigo wa ukaguzi wangu. Vilevile, huashiria ukiukaji wa kanuni za manunuzi ya umma yaani uaminifu, uadilifu, uwazi, na uwajibikaji.

Ninapendekeza kwa menejimenti za halmashauri kuwasilisha nyaraka zilizokosekana ofisini kwangu kwa ajili ya ukaguzi; na katika siku zijazo ziweke vizuri nyaraka zote za manunuzi kwa ajili ya marejeleo na madhumuni mengine ya ukaguzi.

9.7.11 Bodi za Zabuni Hazikupitisha Nyaraka za Zabuni kwa Mikataba Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 7.9

Kanuni ya 185(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inasema "Nyaraka za zabuni zinapaswa kuidhinishwa na bodi ya zabuni kabla ya kutangazwa".

Mapitio ya mihtasari ya bodi ya zabuni yamebaini kuwa zabuni za mikataba 6 yenye thamani ya Sh. 7,861,881,442 katika halmashauri 5 zilitangazwa bila nyaraka za zabuni kuidhinishwa na bodi za zabuni. Aidha, nilibaini katika Halmashauri ya Bukombe, bodi ya zabuni haikuidhinisha uamuzi wa tuzo ya mkataba. Mikataba ambayo zabuni zake zilitangazwa bila kuidhinishwa na bodi ya zabuni ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-33**.

Jedwali Na. 9-33: Mikataba Ambayo Zabuni Zake Zilitangazwa Bila Kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Haikuidhinishwa
H/W Kalambo	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mambwekenya	LGA/144/2016 - 2017/KDC/W/02	651,008,400	Nyaraka ya zabuni
H/W Bukombe	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Nampalahala	LGA113/2017/2018/RWSSP/03 LOT II	514,915,618	Tuzo ya mkataba
H/W Ikungi	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mtunduru	LGA/146/2018/2019/W/02	405,007,269	Nyaraka ya zabuni
H/W Lushoto	Ujenzi wa mradi wa maji wa Vijiji vya Shume, Manolo na Madala	LDC/LGA/004/RWSSP/PHASE I&II/2013-2014/W/11	2,961,216,624	Nyaraka ya zabuni
H/W Mkuranga	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mwanambaya	LGA/012/WS/2017/2018/W/01-02	2,347,737,221	Nyaraka ya zabuni
	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mkerezange	LGA/012/WS/2017/2018/W/01-03	981,996,310	Nyaraka ya zabuni
	Jumla		**7,861,881,442**	

Kwa maoni yangu, kutoidhinishwa kwa nyaraka za zabuni na tuzo ya mikataba kulizinyima bodi za zabuni fursa ya kuchunguza nyaraka jambo linaloweza kuruhusu kutokuwepo kwa vitu muhimu kwenye nyaraka za zabuni na kusababisha ushindani usiofaa na ukosefu wa uwazi katika mchakato wa manunuzi.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri vihakikishe katika siku zijazo bodi za zabuni zinakagua na kupitisha nyaraka za zabuni kabla ya tangazo ili kuepusha makosa kama vile kuachwa kwa vipengele muhimu na kuingizwa vipengele visivyo vya lazima kwenye nyaraka za zabuni.

9.7.12 Matangazo ya zabuni na tuzo za mikataba zenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.6 hazikuchapishwa katika jarida na tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma

Kanuni ya 19(1) na 20(1) za Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 zinazitaka taasisi zinazofanya manunuzi kuandaa tangazo na taarifa ya tuzo

ya mkataba kuhusiana na manunuzi yoyote na kuwasilisha kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma kwa ajili ya uchapishaji katika jarida na tovuti la zabuni ya Mamlaka. Aidha, Kanuni ya 8 (a) inaelekeza kuhakikisha ushiriki mpana wa wazabuni kwa masharti sawa. Hivyo, katika kutangaza zabuni za kazi, taasisi zinazofanya manunuzi zinapaswa kuchapisha zabuni katika jarida na tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na magazeti ya kawaida yanayosomwa mara kwa mara.

Nimebaini halmashauri 5 zilitekeleza mikataba 6 yenye thamani ya Sh. 13,105,212,085 bila kuchapisha tangazo la zabuni na tuzo katika jarida na tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma. Vilevile, nimebaini katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe zabuni ya kandarasi yenye thamani ya Sh. 514,915,618 haikutangazwa katika magazeti. Mikataba ambayo taarifa za zabuni na tuzo hazikuchapishwa katika tofuti na jadida la Mamlaka inaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-34**.

Jedwali Na. 9-34: Mikataba Ambayo Taarifa za Zabuni na Tuzo Hazikuchapishwa

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Makataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)
H/W Moshi	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Tella Mande	LGA/046/2017/2018/W/01	905,475,000
H/W Mpanda	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Kabungu	LGA.099/2017/2018/W/WATER/02/Lot 1	634,810,489
H/W Nsimbo	Ujenzi wa mradi wa maji wa Vijiji vya Mtakuja na Songambele	LGA/161/2017-2018/BHL/W/05/LOT 2	600,702,298
H/W Sumbawanga	Ujenzi wa bwawa la maji wa Kijiji cha Ikozi awamu ya II	LGA/097/2017/2018/WS/W/05	2,943,086,780
H/W Bukombe	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Nampalahala	LGA113/2017/2018/RWSSP/03 LOT II	514,915,618
H/W Mbarali	Ujenzi wa mradi wa maji wa Vijiji vya Luduga na Mawindi awamu ya I	LGA/076/W/2014-2015/27 Lot1	1,007,832,375
	Ujenzi wa mradi wa maji Kijiji cha Luduga na Mawindi awamu ya II	LGA/076/W/2014-2015/27 Lot2	3,683,571,612
H/W Mkuranga	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mwanambaya	LGA/012/WS/2017/2018/W/01-02	2,347,737,221
	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mkerezange	LGA/012/WS/2017/2018/W/01-03	981,996,310
	Jumla		**13,620,127,703**

Vilevile, nimebaini tangazo la zabuni ya mkataba Na. LGA/053/2017/2018/HQ/W/35/LOT 2 yenye thamani ya Sh. 2,726,843,629 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa Vijiji vya Cheleweni, Narunyu, Tandangongoro na Muungano katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi (Mtama) lilichapishwa bila kutaja muda unaohitajika kukamilisha kazi kinyume na Kanuni ya 182(c) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013.

Kwa maoni yangu, kutangaza zabuni kwa wazabuni wachache kulisababisha halmashauri kupunguza wigo wa ushindani na hivyo kutopata bei nafuu. Aidha, hali hii ilizuia uwazi na haki ya ushindani kwa wazabuni.

Ninapendekeza katika siku zijazo menejimenti za halmashauri ziongeze wigo wa ushiriki wa wazabuni kwa kuchapisha zabuni zote kwenye jarida na tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma na magazeti yanayosomwa zaidi. Hii itaongeza uwazi, usawa na ushindani na kufikia thamani ya fedha.

9.7.13 Kamati za Tathmini Hazikujaza Matamko ya Mgongano wa Kimaslahi

Sehemu ya 40(6) ya Sheria ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 inawataka wajumbe wa kamati za tathmini ya zabuni kusaini fomu za maadili ili kuweka wazi kuwa hawana mgongano wa kimaslahi katika mahitaji ya manunuzi.

Mapitio ya taarifa za tathmini ya zabuni ya mkataba Na. LGA/161/2017-2018/BHL/W/05/LOT 2 wenye thamani ya Sh. 600,702,298 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji kwa Vijiji vya Mtakuja na Songambele katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo yalibaini timu ya tathmini hazikukiri kutokuwepo kwa mgongano wa kimaslahi kwa kusaini fomu za tamko kabla ya kuanza kwa tathmini.

Kwa maoni yangu, kamati za tathmini kutokiri mgongano wa kimaslahi kunaiweka halmashauri katika hatari ya upendeleo na uwezekano wa njama ambazo zinaweza kusababisha tathmini isiyo ya haki na utoaji wa mikataba kwa wazabuni wasio na sifa.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri kuhakikisha katika siku zijazo wajumbe wa kamati za tathmini wanatangaza maslahi yao kabla ya kutathmini ya zabuni ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi wa shughuli za manunuzi.

9.7.14 Ufunguzi wa zabuni wenye mapungufu

Kanuni ya 56(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inaelekeza ufunguzi wa zabuni za umma kutohusisha mjumbe wa bodi ya zabuni. Aidha, Kanuni ya 196(2) inataka muda wa ufunguzi wa zabuni kuwa tarehe ya mwisho ya kupokea zabuni na itatangazwa pamoja na mahali pa ufunguzi wa zabuni katika mwaliko wa zabuni.

Mapitio ya mihtasari ya ufunguzi wa zabuni ya mkataba Na. LGA/144/2016-2017/KDC/W/02 wenye thamani ya Sh. 651,008,400 kwa ajili ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mambwekenya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo yalibaini kuwa mjumbe wa bodi ya zabuni alishiriki ufunguzi wa zabuni. Kwa upande mwingine, nilikagua tangazo na mihtasari ya ufunguzi wa zabuni Na. LDC/LGA/004/RWSSP/AWAMU YA I & II/2013-2014/W/11 katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto na kubaini siku ya mwisho ya kuwasilisha zabuni ilikuwa tarehe 16 Novemba 2013 lakini zabuni zilifunguliwa tarehe 18 Novemba 2013.

Kwa maoni yangu, uwepo wa wajumbe wa bodi ya zabuni katika ufunguzi wa zabuni kunaweza kuzuia uadilifu, uhuru na ufanisi wa mchakato wa manunuzi. Aidha, kucheleweshwa kwa hafla ya ufunguzi wa zabuni kunasababisha upokeaji wa zabuni zilizochelewa na kupelekea tuzo ya zabuni isiyo na usawa.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri zihakikishe wajumbe wa bodi za zabuni hawashiriki katika hafla ya ufunguzi wa zabuni. Vilevile, zihakikishe muda wa kufungua zabuni ni sawa na tarehe ya mwisho ya kupokea zabuni.

9.7.15 Mkataba wenye thamani ya Sh. milion 405 amepewa mzabuni asiyekidhi vigezo kwa kiasi kikubwa

Kanuni ya 202 (4)(a) na (5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inaitaka kamati ya tathmini kufanya uchunguzi wa awali wa zabuni kabla ya tathmini ya kina ili kubaini kama kila zabuni inakidhi vigezo kwa kiasi kikubwa (kukidhi vigezo vyote, masharti na uainishaji wa sifa katika nyaraka ya zabuni bila kupungukiwa au kutokuwa na baadhi ya matakwa) kama vilivyoainishwa katika nyaraka za zabuni. Kwa kuongezea, Kanuni ya 203 (1) inasema kuwa “Tathmini ya zabuni inapaswa kuwa sambamba na vigezo na masharti yaliyowekwa katika nyaraka za zabuni na tathmini hiyo itafanyika kwa kutumia vigezo vilivyoainishwa wazi kwenye nyaraka za zabuni”.

Mapitio ya taarifa ya tathmini ya zabuni Na. LGA/146/2018/2019/W/02 ya ujenzi wa mradi wa kusambaza maji wa Kijiji cha Mtunduru katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi yalibaini kuwa mkandarasi M/s TAISH Construction Ltd. alipewa zabuni kwa kuwa amekidhi vigezo kuwazidi wazabuni wengine na si kwa kukidhi vigezo vya zabuni kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, mzabuni hakukidhi vigezo vilivyowekwa katika Kifungu cha 12.5 cha nyaraka ya zabuni kwa sababu mzabuni:

- ✓ Hakuwasilisha ushahidi wa kufanya kazi kama mkandarasi mkuu katika miradi mitatu iliyokamilika katika miaka mitatu iliyopita;

- ✓ Aliwasilisha ushahidi wa kuwa na boza moja la maji badala ya mawili kama ilivyohitajika;

- ✓ Aliwasilisha fundi mwenye cheti cha ufundi katika uhandisi kama wakala wa saiti na si msimamizi wa mradi aliye na shahada ya uhandisi kama inavyotakiwa;

- ✓ Hakuwahi kufanya kazi za mradi wenye wastani wa gharama ya Sh. milioni 250 kwa miaka mitatu. Taarifa za kazi alizowasilisha zilikuwa za kazi alizokuwa akifanya kama mkandarasi mdogo na si mkandarasi mkuu;

- ✓ Hakuwasilisha ushahidi wa uwezo wa kifedha kulingana na kipengele 1.8 cha nyaraka ya zabuni yaani akiba ya fedha au vifaa vingine vya mikopo vinavyokadiriwa kuwa vya Sh. milioni 100; na

- ✓ Aliwasilisha taarifa za kifedha kwa mwaka mmoja tu ulioishia tarehe 31 Desemba 2018 badala ya miaka mitatu kama inavyotakiwa na Kifungu 1.7.

Kwa maoni yangu, kutoa kandarasi kwa mzabuni ambaye hana vigezo vya uwezo wa kifedha, kitaalamu na uzoefu wa kazi kama hiyo kulisababisha kutokamilika kwa mradi huo na hivyo kupelekea kuchelewesha huduma ya maji kwa jamii.

Ninapendekeza katika siku zijazo menejimenti za halmashauri kupitia kamati za tathmini na vitengo vya manunuzi zitekeleze majukumu yake ipasavyo na kutoa kandarasi kwa wazabuni wenye vigezo ili kupata thamani ya fedha.

9.7.16 Marekebisho ya Makosa ya Kihesabu Yasiyo Sahihi na Kukosa Ushahidi Yaliyosabisha Ongezeko la Gharama ya Miradi kwa Shilingi Milioni 57.9

Kanuni ya 207 (2)(a) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inasema "Bila kukinzana na kanuni ya 202(5), taasisi inayofanya manunuzi itasahihisha makosa ya kimahesabu ambayo yatagundulika wakati wa uchunguzi wa zabuni na kutoa taarifa haraka ya marekebisho yoyote kwa mzabuni aliyewasilisha zabuni". Vilevile, sehemu ya 38(l) ya Sheria ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 inazitaka vitengo vya manunuzi kutunza kumbukumbu za mchakato wa manunuzi.

Nimepitia taarifa za tathmini ya mikataba mitatu yenye thamani ya Sh. 4,045,187,047 na kubaini marekebisho ya kihesabu kwenye makadirio ya vifaa na gharama za ujenzi yalifanyika kimakosa na mengine yalikosa ushahidi. **Jedwali Na. 9-35** linaonesha orodha ya mikataba iliyo na marekebisho ya kimahesabu yasiyo sahihi.

Jedwali Na. 9-35: Mikataba iliyo na Marekebisho ya Kimahesabu Yasiyo Sahihi

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama za Mkataba (Sh.)	Mapungufu
H/W Mpanda	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Kabungu	LGA.099/2017/2018/W/WATER/02/Lot 1	634,810,489	Kamati ya tathmini ilifanya makosa katika marekebisho ya kihesabu ya zabuni ya Morden Agrico Ltd. na kusababisha utoaji wa kandarasi kwa gharama ya Sh. 634,810,489 badala ya Sh. 632,810,489 iliyopelekea ongezeko la Sh. milioni 2.
H/W Nsimbo	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mtakuja na Songambele	LGA/161/2017-2018/BHL/W/05/LOT 2	600,702,298	Zabuni za M/S Seba Construction and Drilling na M/s Modern Agrico Ltd. zilikuwa na makosa ya kihesabu ya Sh. 297,000 na Sh. 193,624,640 kwa mfuatano huo lakini hakukuwa na nyaraka yoyote iliyothibitisha uwepo

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama za Mkataba (Sh.)	Mapungufu
				na usahihisho wa makosa hayo.
H/W Chunya	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Makongolosi	LGA /075/W/ 2017/2018/29	2,809,674,260	Timu ya tathmini ilisahihisha gharama za zabuni ya M/S Make Engineering na Cosmos Engineering Co Ltd. JV kutoka Sh. 2,660,667,319 hadi Sh. 2,809,674,259 (ongezeko la Sh. 149,006,940). Hata hivyo, hesabu niliyofanya nimebaini gharama sahihi ya zabuni ilitakiwa kuwa Sh. 2,753,770,644.52 badala ya Sh. 2,809,674,259.52 na kwa hivyo kandarasi iliyosainiwa ilizidi kwa Sh. 55,903,614.48.
	Jumla		**4,045,187,047**	

Kwa maoni yangu, masahihisho ya makosa ya kihesabu yasiyo sahihi na yasiyo na ushahidi yameongeza gharama za mradi kwa Sh. 57,903,614 na inaweza kuzuia ushindani wa haki na usawa. Mbali na hilo, kunaweza kuondoa uwazi katika mchakato wa tathmini.

Ninapendekeza menejimenti ya halmashauri husika katika siku zijazo itunze kumbukumbu za marekebisho ya kihesabu na kufanya marekebisho kwa usahihi ili kuepuka kuongezeka kwa gharama za mikataba. Hii itaongeza haki, uaminifu, uwajibikaji na uwazi katika mchakato wa tathmini za zabuni.

9.7.17 Uhakiki Wa Taarifa Zilizotolewa na Wazabuni Haukufanyika Ipasavyo kwa Mikataba Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 22

Kanuni ya 124 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (zilizorekebishwa mwaka 2016) inataka uhakiki wa taarifa zilizotolewa katika hatua za awali za upembuzi kuthibitishwa kupitia upembuzi utakaofanyika baada ya tathmini kabla ya kukabidhi zabuni na kumkataa

mzabuni asiyekuwa na uwezo au rasilimali za kutekeleza mkataba ipasavyo. Aidha, Kanuni ya 224 (2) inataka vigezo vitakavyotumika kuhakiki taarifa za mzabuni viainishwe katika nyaraka za zabuni ikiwemo uzoefu, utendaji kwenye mikataba inayofanana na kazi anayoomba, na uwezo wa kutekeleza mkataba.

Ukaguzi wangu wa taarifa za tathmini kwa zabuni zilizochaguliwa ulibaini kuwa timu za tathmini katika halmashauri 4 hazikufanya uhakiki wa uwezo wa wakandarasi walioshinda zabuni za mikataba yenye thamani ya Sh. 22,002,141,934 ili kuthibitisha uwepo wa vifaa na zana za kazi kwa wakandarasi. Mikataba iliyotekelezwa pasipo upembuzi baada ya tathmini inaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-36**.

Jedwali Na. 9-36: Mikataba Iliyotekelezwa Pasipo Upembuzi Baada ya Tathmini

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)
H/W Kigoma	Ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika Vijiji vya Kaseke, Kimbwela na Nyamoli	LGA/043/2016/2017/W/15	1,163,496,000
H/W Ikungi	Ujenzi wa mradi maji kwa ajili ya Kijiji cha Mtunduru	LGA/146/2018/2019/W/02	405,007,269
H/W Wanging'ombe	Ujenzi wa mradi wa maji wa Igando- Kijombe	LGA/153/2017/2018/W/01	12,437,407,360
H/Mji Makambako	Ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika Kijiji cha Usetule-Mahongole	LGA/166/2018/2019/W/01	7,996,231,305
	Jumla		**22,002,141,934**

Kwa maoni yangu, kutohakiki taarifa za wazabuni baada ya tathmini kumesababisha kuchelewa miradi na utoaji huduma ya maji kwa jamii kwa kuwa wakandarasi walikosa vigezo stahiki.

Ninapendekeza halmashauri husika zihakikishe kwa siku zijazo uhakiki wa taarifa za mzabuni aliyeshinda unafanyika kwa ufanisi na tija ili kuepuka ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi.

9.7.18 Wazabuni Walioshindwa Hawakupewa Siku Saba Kuwasilisha Malalamiko

Sehemu ya 60(3) ya Sheria ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) inaelekeza kuwa “baada ya kupokea taarifa ya uamuzi wa tuzo kutoka bodi ya zabuni na kujiridhisha, ofisa masuuli atoe taarifa ya nia ya kutangaza tuzo ya mkataba na kuwapa wazabuni siku saba za kuwasilisha malalamiko, kama yapo".

Nimebaini mikataba miwili yenye thamani ya Sh. 3,329,733,531 katika Mkoa wa Pwani wazabuni walioshindwa hawakupewa siku saba za kazi kuwasilisha malalamiko yao. Mikataba ambayo wazabuni wake hawakupewa siku saba za kuwasilisha malalamiko inaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-37**.

Jedwali Na. 9-37: Mikataba Ambayo Wazabuni Wake Hawakupewa Siku Saba za Kuwasilisha Malalamiko

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Mapungufu
H/W Mkuranga	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mwanambaya.	LGA/012/WS/2017/2018/w/01-02	2,347,737,221	Hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha kuwa ofisa masuuli aliwaarifu wazabuni walioshindwa na kuwapa siku saba za kuwasilisha malalamiko yao (kama yapo).
	Ujenzi wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mkerezange.	LGA/012/WS/2017/2018/w/01-03	981,996,310	
	Jumla		**3,329,733,531**	

Kwa mtazamo wangu, kwa kutowapa wazabuni walioshindwa haki ya kukata rufaa halmashauri haikufuata Kanuni za Manunuzi ya Umma yaani uaminifu, haki, uadilifu, na uwazi katika kufanya tathmini na kutoa tuzo za mikataba.

Ninapendekeza katika siku zijazo, halmashauri zitoe siku saba za kuwasilisha malalamiko kwa wazabuni walioshindwa. Hii itaongeza uwazi na haki katika mchakato wa manunuzi.

9.7.19 Kukosekana kwa Taarifa Muhimu Katika Barua za Kusudio la Kutangaza Tuzo za Mkataba

Kanuni ya 231(4) (a & b) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inataka taarifa ya nia ya kutangaza tuzo za zabuni kuwa na jina la mzabuni aliyeshinda, gharama ya mkataba, na kipindi cha utekelezaji na ukamilishaji wa kazi.

Mapitio ya majalada ya mkataba Na. LGA/115/SMC/2018/2019/W/No. 1/lot 2 wenye thamani ya Sh. 339,375,031 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika Kijiji cha Mungumaji katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida yalibaini taarifa ya nia ya kutangaza tuzo ya mkataba ambayo ilitolewa kwa wazabuni walioshindwa haikubainisha jina la mzabuni aliyeshinda, gharama ya mkataba, na kipindi cha utekelezaji na ukamilishaji wa kazi.

Kwa maoni yangu, kushindwa kutaja jina la mzabuni aliyeshinda, gharama ya mkataba na muda wa kutekeleza mkataba katika barua za kusudio la kutangaza tuzo za zabuni kunapunguza uaminifu, haki, uadilifu na uwazi katika mchakato wa manunuzi.

Ninapendekeza menejimenti ya manispaa ihakikishe kwamba, katika siku zijazo, barua za kusudio la kutangaza tuzo za mkataba zijumuishe majina ya wazabuni waliofanikiwa, gharama za mikataba na muda wa utekelezaji.

9.7.20 Kutowasilisha Nakala za Barua za Tuzo kwa Mamlaka Husika

Kanuni ya 232(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) inamtaka ofisa masuuli kupeleka nakala ya barua ya tuzo kwa Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kitengo cha Usimamizi wa Mali za Serikali, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Nimekagua majalada ya mikataba na kubaini nakala za barua za tuzo kwa mikataba mitano yenye thamani ya Sh. 5,564,948,507 hazikuwasilishwa kwa mamlaka husika kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-38**.

Jedwali Na. 9-38: Mikataba Ambayo Nakala za Barua za Tuzo Hazikuwasilishwa kwa Mamlaka Husika

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama Mkataba (Sh.)
H/W Moshi	Ujenzi wa Mradi wa Maji wa Tella Mande	LGA/046/2017/2018/W/01	905,475,000
H/W Rombo	Ukamilishaji wa mradi wa usambazaji wa maji wa Leto	LGA/HQ/044/2013/2014/CW/RWSSP/05	605,500,538
	Ukamilishaji wa Mradi wa usambazaji wa maji wa Shimbi	LGA/HQ/044/2013/2014/CW/RWSS/03	724,239,438
H/W Mkuranga	Ujenzi wa visima vya maji katika Kijiji cha Mwanambaya	LGA/012/WS/2017/2018/w/01-02	2,347,737,221
	Ujenzi wa visima vya maji katika Kijiji cha Mkerezange	LGA/012/WS/2017/2018/w/01-03	981,996,310
	Jumla		**5,564,948,507**

Kwa maoni yangu, kutowasilisha nakala za barua za tuzo kwa mamlaka husika kunakwamisha mamlaka hizo kufanya maandalizi ya ukaguzi wa mikataba na masuala yanayohusu kodi. Hii inaweza pia kusababisha kupungua kwa mawanda ya kazi na upotevu wa mapato kwa serikali.

Ninapendekeza katika siku zijazo menejimenti za halmashauri zihakikishe nakala za barua za tuzo zinatumwa kwa mamlaka husika ili kuondokana na athari zinazoweza kujitokeza.

9.7.21 Kushindwa Kukataa Zabuni ya Shilingi Milioni 468 Iliyo na Mabadiliko ya Matakwa ya Kitaalamu

Kanuni ya 4(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 zinahitaji maofisa masuuli na bodi za zabuni wakati wa kufanya au kupitisha manunuzi kuongozwa na kanuni za manunuzi zikiwemo uadilifu, uwajibikaji, haki na uwazi.

Mapitio ya majalada kwa mkataba Na. LGA/144/2016-2017/KDC/W/02 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kusambaza maji wa Mambwekenya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo yalibaini kuwa, awali zabuni hiyo ilitolewa kwa Mhandisi Mselem kwa Sh. 467,896,906. Baada ya mabadiliko ya matakwa ya kitaalamu ya mradi (kuongezeka muda wa uhai wa mradi kutoka miaka 10 hadi 20, halmashauri ilimtaka mzabuni Mselem kuwasilisha

nukuu ya gharama za mradi iliyosababisha ongezeko la gharama za mradi hadi Sh. 651,008,400 (ongezeko la Sh. 183,111,494).

Kwa maoni yangu, kushindwa kukataa zabuni na kutoa nukuu kwa mzabuni mmoja kulizuia halmashauri kupata bei za chini zaidi na za ushindani.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri ihakikishe katika siku zijazo zabuni zote zenye mabadiliko ya kitaalamu au yenye kuathiri gharama na matakwa ya miradi kwa sababu zozote zikataliwe na kutangazwa upya na si kutoa zabuni kwa mkandarasi mmoja. Hii itaimarisha kanuni za manunuzi ikiwemo uaminifu, haki, uadilifu, uwazi na uwajibikaji na kupata thamani ya fedha kwa miradi.

9.7.22 Mikataba Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 25.6 Haikufanyiwa Upekuzi wa Kisheria

Kanuni ya 59(1&5) na 60 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) zinaelekeza Mwanasheria Mkuu au mwanasheria wa taasisi inayofanya manunuzi kufanya upekuzi wa mikataba iliyotokana na kukubali ofa za zabuni kabla mkataba haujasainiwa na pande zote.

Nimebaini mikataba minne katika halmashauri tatu ambayo haikufanyiwa upekuzi na mikataba miwili katika Halmashauri ya Mji Makambako na Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe ambayo ilipekuliwa kabla ya mwajiri kukubali ofa ya wakandarasi. Mapungufu yaliyobainika katika upekuzi wa mikataba yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-39**.

Jedwali Na. 9-39: Mapungufu Yaliyobainika Katika Upekuzi wa Mikataba

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Mapungufu
H/W Mpanda	Ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika Kijiji cha Kabungu	LGA.099/2017/2018/W/WATER/02/Lot 1	634,810,489	Haukupekuliwa na Mwanasheria wa Halmashauri
H/W Kigoma	Ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika Vijiji vya Kaseke, Kimbwela na Nyamoli	LGA/043/2016/2017/W/15	1,163,496,000	Haukupekuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Mapungufu
H/W Wanging'ombe	Ujenzi wa mradi wa maji wa Igando-Kijombe	LGA/153/2017/2018/W/01	12,437,407,360	Mikataba ilipekuliwa kabla ya halmashauri mkandarasi kukubaliwa ofa
H/W Makambako	Ujenzi wa mradi wa kusambaza maji wa Usetule-Mahongole	LGA/166/2018/2019/W/01	7,996,231,305	
H/W Mkuranga	Ujenzi wa mradi wa maji Mwanambaya	LGA/012/WS/2017/2018/w/01-02	2,347,737,221	Haukupekuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
	Ujenzi wa mradi wa visima vya maji katika Kijiji cha Mkerezange	LGA/012/WS/2017/2018/w/01-03	981,996,310	Haukupekuliwa na mwanasheria wa halmashauri.
	Jumla		**25,561,678,685**	

Kwa maoni yangu, kutofanya upekuzi wa mikataba kunaziweka halmashauri katika hatari za kisheria na kunaweza kuhatarisha thamani ya fedha kwa miradi hiyo. Aidha, barua za kukubali ofa ni sehemu ya mikataba hivyo lazima ifanyiwe upekuzi kwa kuwa inahusisha bei ya mkataba baada ya kusahihishwa na masharti mengine kwa mzabuni aliyeshinda kuyatekeleza. Hivyo, inaweza kusababisha wazabuni waliofanikiwa kushindwa kuwajibikaji ipasavyo.

Ninapendekeza katika siku zijazo menejimenti za halmashauri zihakikishe mikataba inafanyiwa upekuzi na barua za kukubali ofa ziwe sehemu ya rasimu ya mikataba ili kuangaliwa kama vigezo na masharti vipo kisheria na kuepuka migogoro ya kisheria inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji.

9.7.23 Ofisa Masuuli na Bodi ya Zabuni Hazikuidhinisha Timu za Maridhiano, Mihtasari na Mpango wa Maridhiano

Kanuni ya 226(6) na 227 (1-2) za Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 zinaelekeza, pamoja na mambo mengine, bodi za zabuni kukagua na kuidhinisha makubaliano ya maridhiano kabla ya kuyaingiza katika mikataba pamoja na kuandaa na kuidhinisha mpango wa maridhiano kabla ya kuanza mazungumzo.

Halmashauri za Wilaya za Kalambo na Sumbawanga zilipendekeza na kuteua timu za maridhiano kwa zabuni Na. LGA/144/2016-2017/KDC/W/02 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kusambaza maji wa Mambwekenya na zabuni Na. LGA/097/2017/2018/WS/W/05 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la maji katika Kijiji cha Ikozi awamu ya II. Hata hivyo, nilibaini kuwa mwenyekiti wa timu ya maridhiano aliteuliwa na kaimu mkuu wa kitengo cha usimamizi wa manunuzi badala ya ofisa masuuli. Aidha, nilibaini kuwa timu ya maridhiano haikuandaa mpango wa mazungumzo; mihtasari ya mazungumzo haikuidhinishwa na bodi ya zabuni; na haikusainiwa na mtu mwenye nguvu ya kisheria ya kusaini nyaraka.

Kwa maoni yangu, ufanyaji wa maridhiano bila kufuata utaratibu hauna manufaa kwa halmashauri kigharama na katika kufikia thamani ya fedha ya mradi husika. Aidha, kutoidhinishwa kwa mihtasari ya maridhiano kumeinyima bodi za zabuni haki ya kuchunguza kwa undani na kuidhinisha makubaliano hayo.

Ninapendekeza menejimenti ya halmashauri kwa siku zijazo zihakikishe bodi za zabuni zinapitia makubaliano ya maridhiano kabla ya kujumuishwa kwenye mikataba. Mbali na hilo, ihakikishe mipango ya mazungumzo imeandaliwa na kuidhinishwa na bodi za zabuni kabla ya kuanza maridhiano.

9.7.24 Mikataba Yenye Thamani ya Sh. 154,416,118 Ilisainiwa na Kutekelezwa Bila ya Kupata Msamaha wa Kodi

Vifungu vya 4.3, 4.5 na 4.6.5 vya Mwongozo wa Hazina Na.6 wenye Kumb: Na. CLA.321/369/02 uliotolewa tarehe 22 Januari 2018 kuhusu taratibu za msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa miradi inayotekelezwa na Serikali na washirika wa maendeleo vinaelekeza mkataba unaostahili msamaha wa kodi kusainiwa baada ya kuidhinishwa na waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha. Msamaha wa kodi ni lazima uwasilishwe

ndani ya siku 30 kabla ya kuanza kwa mradi ili kutoa fursa kwa wizara kuchambua maombi husika.

Mapitio ya mkataba Na. LGA113/2017/2018/RWSSP/LOT II wenye thamani ya Sh. 514,640,825.15 (pamoja na kodi) kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa Nampalahala katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe yalibaini kuwa mkataba ulisainiwa na kuanza kutekelezwa kabla ya kupata msamaha wa kodi wa Sh. 92,635,348.53 kama ilivyoainishwa katika makadirio ya vifaa na gharama ya ujenzi. Vilevile, nilibaini mkataba Na. LGA/146/2018/2019/W/02 wa Sh. 405,007,269 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji cha Mtunduru wilayani Ikungi ambapo kodi ya Sh. 61,780,770 ilijumuishwa na kati yake Sh. 10,479,779 ililipwa kupitia cheti Na. 1 cha malipo cha muda mfupi.

Kwa maoni yangu, kushindwa kuomba msamaha wa kodi kumesababisha kulipa kodi ya Sh. 154,416,118 ambayo ingeweza kutumika kugharamia shughuli zingine za mradi.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri kwa siku zijazo ziishauri Wizara ya Fedha na Mipango kutoa msamaha wa kodi kwa wakati kabla ya kusaini mikataba.

9.7.25 Ucheleweshaji Katika Kuanza Kutekeleza Miradi

Kifungu cha 1 cha SCC kwa mkataba No. LGA/024/2017/2018/W/02-LOT II uliosainiwa tarehe 23 Agosti 2018 na mkataba Na. LDC/LGA/004/RWSSP/Loti ya I & II/2013-2014/W/11 uliosainiwa tarehe 23 Februari 2014 kinawataka wakandarasi kuanza kazi hizo ndani ya siku saba na siku 14 kwa mfuatano huo kutoka tarehe ya kusaini mkataba.

Nimebaini mikataba mitatu yenye thamani ya Sh. 6,325,957,524 ambapo kulikuwa na ucheleweshaji wa kukabidhi miradi kwa wakandarasi na kuanza kazi bila sababu za msingi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-40**.

Jedwali Na. 9-40: Mikataba Iliyochelewa Kukabidhiwa na Kuanza Kutekelezwa

Halmashauri	Jina la Mradi	Namba ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Tarehe ya Kuanza Mkataba	Tarehe Halisi ya Kuanza Utekelezaji
H/W Bahi	Ujenzi wa mradi wa maji kwa Kijiji cha Kimara	LGA/024/2017/2018/W/02-LOT II	637,897,271	30.08.2018	18.09.2018
H/W Lushoto	Ujenzi wa mradi wa maji katika Vijiji vya Shume, Manolo, Madala	LDC/LGA/004/RWSSP/AWAMU ya I&II/2013-2014/W/11	2,961,216,624	09.03.2014	12.07.2016
H/W Lindi	Ujenzi wa mradi wa maji wa Vijiji vya Cheleweni, Narunyu, Tandangongoro na Muungano	LGA/053/2017/2018/HQ/W/35/LOT 2	2,726,843,629	28.08.2018	14.06.2019
Jumla			**6,325,957,524**		

Kwa maoni yangu, kuchelewa kukabidhi na kuanza kwa miradi kumechelewesha utekelezaji na ukamilikaji wa miradi hiyo kwa wakati na hivyo kuchelewesha utoaji wa huduma ya maji kwa jamii na kunaweza kuongeza gharama za miradi.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri zihakikishe katika siku zijazo makabidhiano na kuanza kwa utekelezaji wa miradi kunafanyika kwa mujibu wa muda uliokubalika ili wanufaika waweze kufaidika na matokeo kwa wakati uliokusudiwa.

SURA YA 10

USIMAMIZI WA MATUMIZI

10.0 Utangulizi

Usimamizi wa matumizi ya umma hutafsiriwa kama njia ambayo Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapewa mamlaka ya usimamizi wa rasilimali za umma kwa kuzingatia nidhamu kwenye matumizi ya fedha, kuweka kipaumbele kimkakati na kupata thamani ya fedha. Hujumuisha taratibu zote zinazohitajika na kuhakikisha malipo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanafanywa kwa usahihi, ufanisi na kwa wakati muafaka. Pia, usimamizi wa matumizi ya umma huhakikisha halmashauri zinapopokea rasilimali za umma zinazitumia kwa kufuata kanuni, sheria, miongozo na maagizo kwa madhumuni yaliyokusudiwa *(Rejea Utangulizi uliotolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, LAAM, 2019)*.

Matokeo ya ukaguzi yanaonesha utofauti mkubwa wa kutozingatia sheria na maagizo ya usimamizi wa fedha yanayosababishwa na matumizi mabaya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Masuala ya kutofuata sheria yaliyoibuliwa kwenye eneo hili la ukaguzi wangu yameainishwa kwenye barua ya kuonesha udhaifu katika kila halmashauri.

Sura hii kwa muhtasari inaelezea masuala muhimu ambayo yasiporekebishwa yanaweza kuleta athari kubwa kwa usimamizi wa fedha zilizokabidhiwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

10.1 Kukosekana kwa Hati za Malipo Sh. 374,879,224

Agizo la 34(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linatoa jukumu kwa mwekahazina wa halmashauri kuwa mtunzaji wa nyaraka zote muhimu ikiwamo hati za malipo.


Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa halmashauri 15 zilishindwa kuwasilisha hati za malipo kwa ajili ya ukaguzi zenye jumla ya Sh. 374,879,224 kama ilivyoelezewa kwenye **Jedwali Na. 10-1**, hivyo kuzuia mawanda ya ukaguzi kwa kuwa sikuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi yaliyotokea kwenye halmashauri hizo.

Jedwali Na. 10-1: Kukosekana Kwa Hati Za Malipo

Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Bahi	31,772,200	9.	H/W Misenyi	10,000,000
2.	H/W Chemba	7,845,485	10.	H/W Mkinga	16,859,150
3.	H/Mji Handeni	10,660,000	11.	H/W Sengerema	22,789,600
4.	H/W Kakonko	62,104,000	12.	H/W Shinyanga	5,400,000
5.	H/W Karagwe	4,209,020	13.	H/W Siha	59,273,255
6.	H/W Kasulu	19,289,124	14.	H/W Tarime	53,433,701
7.	H/W Kishapu	27,223,421	15.	H/W Urambo	5,413,168
8.	H/W Mbogwe	38,607,100		**Jumla**	**374,879,224**

Kielelezo kifuatacho kinachanganua mwenendo wa kutowasilisha hati za malipo kwa miaka mitatu ambapo inaonesha mabadiliko chanya katika kurekebisha tatizo hili.

Mchoro Na. 10-1: Mwenendo wa Hati za Malipo Zilizokosekana



Rejea ushauri wangu wa mwaka uliopita kwamba, wawekahazina wanapaswa kutunza nyaraka zote muhimu ikiwamo hati za malipo kama inavyoagizwa na Agizo la 34(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

10.2 Matumizi yenye Thamani ya Sh. 2,192,675,594 Yasiyo na Manufaa

Kanuni ya 21(2) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 kama zilivyorekebishwa mwaka 2004 inasema "Kwa madhumuni ya Kanuni hii, malipo yasiyokuwa na manufaa humaanisha malipo yasiyoepukika na hakuna manufaa yatakayopatikana". Kinyume na Kanuni hii, menejimenti za halmashauri 29 zilitumia kiasi cha Sh. 2,192,675,594 kwa matumizi yasiyo na manufaa kwa umma kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 10-1**.

Mfano wa matumizi hayo ni malipo baada ya kushindwa kesi mahakamani; faini ya kucheleweshaa malipo ya makato ya wafanyakazi; malipo kwa kazi isiyofanyika; na faini inayotozwa kwa kucheleweshaa malipo ya mkopo. Matumizi yasiyokuwa na tija yaliyofanywa na halmashauri yanaathiri utekelezaji wa shughuli zilizo ndani ya bajeti kwa kuwa fedha hizo zimetumika isivyokusudiwa.

Ninashauri menejimenti za halmashauri ziimarishe udhibiti wa ndani na zizingatie kanuni na sheria kabla ya kufanya maamuzi. Pia, ziwajengee uwezo wanasheria wa halmashauri.

10.3 Matumizi yenye Thamani ya Sh. 3,971,965,956 Yasiyo na Viambatisho

Agizo la 8(2)(c) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 inasema "Mwekahazina ana jukumu la kuweka vema mfumo wa kiuhasibu na utunzaji wa nyaraka zote muhimu". Pia, Kifungu cha 6.6.2 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 unasema "Ni lazima ikumbukwe kwamba maofisa wanaoidhinisha malipo lazima wapitie nyaraka zote na kuhakikisha mchakato wa malipo umefuatwa ipasavyo kabla ya kuchukua hatua".

Kinyume chake, kwa mwaka wa fedha 2019/20, nilibaini kwamba matumizi ya jumla ya Sh. 3,971,965,956 katika halmashauri 87 hayakuwa na viambatisho ipasavyo na kusababisha kutothibitishwa kwa usahihi wa malipo yaliyofanyika kama ilivyofafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 10-2**.

Suala hili limekuwa likijirudia kwenye ukaguzi wa siku za nyuma. Halmashauri hazijaonesha utayari wa kurekebisha mapungufu haya. Kwa mfano, kwa miaka mitatu 2017/18, 2018/19 na 2019/20, halmashauri 26 zimekua zikifanya malipo yasiyo na viambatisho yenye thamani ya Sh. 3,474,079,485 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 10-2**.

Jedwali Na. 10-2: Mwenendo wa Matumizi Yasiyo na Viambatisho

Na.	Halmashauri	2017/18	2018/19	2019/20	Jumla Kuu
1	H/Jiji Arusha	5,880,000	23,990,860	32,524,972	62,395,832
2	H/W Bahi	1,893,551	2,877,000	22,709,606	27,480,157
3	H/W Buchosa	9,368,000	32,395,000	83,833,127	125,596,127
4	H/W Busokelo	21,650,000	10,000,000	10,750,000	42,400,000
5	H/W Chamwino	101,590,959	11,835,000	8,885,649	122,311,608
6	H/W Chunya	16,615,200	96,632,380	7,230,000	120,477,580
7	H/W Igunga	10,768,500	7,829,780	3,593,698	22,191,978
8	H/W Kilindi	7,180,000	7,425,000	9,991,616	24,596,616
9	H/W Kilosa	200,597,406	57,424,366	52,288,646	310,310,418
10	H/W Kishapu	43,251,589	68,694,833	157,385,946	269,332,368
11	H/W Kiteto	1,117,500	4,190,504	14,450,980	19,758,984
12	H/W Kongwa	50,131,840	9,211,800	12,905,339	72,248,979
13	H/W Mkalama	7,630,000	15,991,230	7,300,080	30,921,310
14	H/W Mkinga	18,502,372	20,477,750	32,846,325	71,826,447
15	H/W Momba	5,745,000	56,872,476	46,078,406	108,695,882
16	H/W Moshi	54,656,110	12,071,123	8,333,092	75,060,325
17	H/M Mpanda	9,832,644	34,205,400	5,956,000	49,994,044
18	H/W Mpwapwa	108,220,573	34,195,137	20,039,826	162,455,536
19	H/W Nanyumbu	13,251,800	9,951,100	8,313,000	31,515,900
20	H/W Pangani	3,603,585	22,838,342	29,725,072	56,166,999
21	H/W Rungwe	73,129,400	38,046,794	38,342,000	149,518,194
22	H/W Siha	362,098,590	34,167,199	112,683,100	508,948,889
23	H/W Sikonge	85,509,950	18,551,737	36,306,229	140,367,916
24	H/W Songea	25,512,060	273,330,325	19,436,000	318,278,385
25	H/M Songea	35,057,710	18,971,239	48,096,000	102,124,949
26	H/M Temeke	201,040,758	80,690,470	167,372,834	449,104,062
	Jumla	**1,473,835,097**	**1,002,866,845**	**997,377,543**	**3,474,079,485**

Watunzahazina wameshindwa kuweka udhibiti na kutunza nyaraka muhumu hasa hati za malipo pamoja na viambatisho vyake. Hii inaashiria ubadhirifu wa fedha za umma kwenye shughuli mbalimbali. Hivyo, ukaguzi haukuweza kubaini uhalali wa malipo hayo.

Ninazishauri menejimenti za halmashauri ziimarishe utunzaji wa hati za malipo pamoja na viambatisho vyake.

10.4 Malipo Yenye Thamani ya Sh. 5,541,159,468 Yasiyoambatishwa Risiti za Kielekitroniki

Kanuni ya 55(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi (za jumla) za Mwaka 2016 zinamtaka kila mtu kudai na kuhifadhi risiti ya kielekitroniki.

Kinyume chake, nimebaini kuwa halmashauri 58 zimeshindwa kuwasilisha risiti za kielekitroniki baada ya kuzitaka kuonesha risiti za manunuzi yenye jumla ya Sh. 5,541,159,468 kama inavyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 10-3**.

Jedwali Na. 10-3: Malipo Yasiyo Ambatishwa Risiti za Kielekitroniki

Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Babati	35,557,530	30	H/W Mkalama	198,762,039
2	H/W Buhigwe	37,375,000	31	H/W Moshi	14,381,980
3	H/W Bumbuli	158,747,346	32	H/M Moshi	16,956,132
4	H/W Busokelo	36,584,255	33	H/M Mtwara-Mikindani	2,704,525
5	H/W Chamwino	36,274,700	34	H/W Mwanga	9,444,170
6	H/W Chunya	28,707,656	35	H/Jiji Mwanza	252,310,826
7	H/Mji Ifakara	18,642,714	36	H/W Namtumbo	175,396,368
8	H/W Igunga	5,856,500	37	H/Mji Nanyamba	3,472,400
9	H/W Ileje	19,935,938	38	H/W Ngorongoro	4,619,000
10	H/W Iramba	18,650,288	39	H/W Nkasi	122,694,353
11	H/W Itigi	10,713,906	40	H/W Nzega	13,838,600
12	H/W Kalambo	112,031,331	41	H/Mji Nzega	5,629,700
13	H/W Kaliua	93,372,900	42	H/W Pangani	25,613,938
14	H/W Karagwe	127,967,000	43	H/W Rombo	97,318,156
15	H/W Kibaha	50,617,999	44	H/W Rufiji	5,055,300
16	H/Mji Kibaha	22,384,823	45	H/W Sengerema	20,406,035
17	H/W Kigoma	4,929,753	46	H/W Serengeti	22,755,204
18	Kigoma-Ujiji	38,712,984	47	H/W Shinyanga	5,304,000
19	H/W Kilindi	95,018,508	48	H/W Siha	134,829,471
20	H/M Kinondoni	193,647,400	49	H/W Sikonge	138,850,356
21	H/W Kisarawe	71,095,816	50	H/W Songwe	133,358,224
22	H/W Kiteto	28,171,302	51	H/M Tabora	64,669,135
23	H/W Kondoa	26,750,489	52	H/Jiji Tanga	40,158,654
24	H/W Korogwe	159,160,760	53	H/W Tarime	59,677,648
25	H/Mji Korogwe	28,870,178	54	H/W Tunduru	31,984,103
26	H/W Lushoto	33,070,000	55	H/W Ukerewe	89,634,542
27	H/W Mbozi	20,350,683	56	H/W Ushetu	1,409,688,866
28	H/W Mbulu	10,330,000	57	H/W Uyui	33,262,338

Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
29	H/Mji Mbulu	64,661,496	58	H/W Wanging'ombe	820,194,149
	Jumla				**5,541,159,468**

Tabia hii inachochea wafanyabiashara kukwepa kodi na kupelekea ukusanyaji mdogo wa mapato ya Serikali.

Ninashauri menejiment za halmashauri zidai na kutunza risiti za kielekitroniki ili kuchochea ukusanyaji wa kodi.

10.5 Mapungufu Katika Usimamizi wa Masurufu Yenye Jumla ya Sh. 2,513,637,730

Agizo Na. 40 la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Kifungu Na. 6.8 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 unatoa maelekezo ya jinsi ya uombaji wa masurufu, utoaji na urejeshaji wake, zuio la utoaji wa masurufu zaidi ya mara moja kwa ofisa wa serikal; uandaaji wa rejesta ya masurufu; na adhabu kwa kuchelewa kurejesha masurufu.

Ukaguzi wangu ulibanini halmashauri 105 zililipa masurufu ya jumla ya Sh. 2,513,637,730 kinyume na kifungu na kanuni vinavyoelekeza. **Jedwali Na. 10-4** na **Kiambatisho Na. 10-3** kinaonesha muhtasari wa mapungufu ya usimamizi wa masurufu, idadi na kiasi kwa halmashauri husika.

Jedwali Na. 10-4: Muhtasari wa Mapungufu ya Usimamizi wa Masurufu

Maelezo	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
Masurufu yasiyorekodiwa kwenye rejesta	11	162,262,252
Masurufu yaliyolipwa kama matumizi ya kawaida	25	1,007,120,807
Masurufu yaliyotumika kuwalipa wazabuni	13	325,499,039
Utoaji wa masurufu kabla ya kurejesha masurufu ya awali	2	143,171,924
Kuchelewa kurejesha masurufu	13	234,683,634
Masurufu yasiyorejeshwa	41	640,900,074
Jumla	**105**	**2,513,637,730**

Mapungufu kwenye usimamizi wa masurufu unaonesha udhaifu kwenye halmashauri unaowapa fursa watumishi wasio waaminifu kutumia vibaya fedha za umma.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri zifuatilie kwa umakini kuanzia utoaji, urejeshaji wa masurufu na viambatisho vya masurufu hayo kama inavyotakiwa sheria na kanuni husika.

10.6 Mapungufu Katika Kuandaa na Kuidhinisha Hati za Malipo Zenye Jumla ya Sh. 6,043,952,108

Kifungu 6.6.2(d) cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2019 kinatoa maelekezo ya kuandaa hati za malipo hadi kuidhinishwa kwake kama vile uandaaji unaostahili na kupanga namba za hati kwa mfuatano; ukaguzi wa awali ili kuangalia usahihi wa maelezo ya hati pamoja na viambatisho vyake; na mwidhinishaji sahihi wa hati za malipo. Pia, Kifungu 6.7.3 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 unasema kwamba "Halmashauri itafanya malipo yote kielekitroniki na kwenye akaunti ya mlipwaji. Halmashauri haipaswi kulipa kwa hundi wala taslimu".

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa halmashauri 64 zilionesha mapungufu katika uandaaji hadi uidhinishaji wa hati za malipo na kufanya makosa mbalimbali yenye thamani ya Sh. 6,043,952,108 kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 10-5**. Mfano wa makosa hayo ni malipo yaliyofanywa bila kuandika hati ya malipo kwenye mfumo wa Epicor; malipo yaliyoanzishwa na kuidhinishwa na ofisa mmoja; malipo yaliyoidhinishwa kimakosa; kutofanyika kwa ukaguzi wa awali; na hati za malipo zisizotiwa muhuri wa kulipwa. **Kiambatisho Na. 10-4** kinatoa orodha ya makosa kwa kila halmashauri husika.

Jedwali Na. 10-5: Muhtasari wa Mapungufu ya Uandaaji na Uidhinishaji wa Hati za Malipo

Maelezo	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
Malipo yaliyofanyika bila kuandika hati ya malipo kwenye mfumo wa epicor	4	412,129,826
Malipo yaliyoanzishwa na kuidhinishwa na ofisa mmoja	2	106,106,410
Hati za malipo pamoja na viambatisho visivyotiwa muhuri wa kulipwa	8	801,344,154
Malipo yaliyo idhinishwa kimakosa	12	1,525,258,344
Malipo yaliyofanyika bila ukaguzi wa awali	22	2,470,787,618
Malipo ya taslimu kwa mlipwaji	16	728,325,756
Jumla	**64**	**6,043,952,108**

Ninapata wasiwasi kwamba uandaaji na uidhinishaji usiofaa wa hati za malipo unaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma.

Ninazishauri menejimenti za halmashauri zihakikishe kuwa hati za malipo zinaandaliwa na kuidhinishwa ipasavyo kabla ya malipo.

10.7 Malipo Yasiyostahili ya Thamani ya Sh. 2,089,295,143

Ukaguzi wa matumizi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 ulibaini kuwa halmashauri 45 zilitumia jumla ya Sh. 2,089,295,143 kulipa shughuli mbalimbali bila kuzingatia sheria na kanuni kama ilivyo kwenye **Kiambatisho Na. 10.5**. Matumizi yasiyostahiki ni pamoja na posho yaliyozidi kiwango, malipo ya vibarua bila mikataba, na malipo mengineyo yasiyozingatia viwango maalumu vya posho na malipo yenye viambatisho yenye shaka. Matumizi haya yanaathari utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Sababu ya matumizi yasiyostahili ni idara ya fedha kushindwa kudhibiti matumizi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, kushindwa kutenga fedha kwenye vifungu stahiki vya malipo.

Ninazishauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa ziimarishe udhibiti wa ndani kwenye malipo na kuwa na vitengo vya ukaguzi wa awali vitakavyoangalia usahihi wa hati za malipo kabla ya kuidhinishwa.

10.8 Kodi ya Zuio ya Thamani ya Sh. 761,752,024 Isiyokatwa na Kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania

Vifungu Na. 23 na 24 vya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2013 na Kifungu Na. 83 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 vinaagiza taasisi za Serikali kukata kodi ya zuio kwa asilimia mbili kutoka kwa malipo ghafi wakati wanapofanya biashara na watoahuduma na wauzaji wa bidhaa.

Kinyume chake, nilibaini kuwa malipo kwa wauzaji wa bidhaa kwa halmashauri 25 hayakukatwa kodi ya zuio ya jumla ya Sh. 223,603,084. Pia, kiasi cha Sh. 538,148,940 cha kodi ya zuio iliyokusanywa na halmashauri 17 hakikuwasilishwa katika Mamlaka ya Mapato Tanzania. **Jedwali Na. 10-6** linatoa muhtasari wa mapungufu yaliyobainika; na **Kiambatisho Na. 10-6** kinatoa muhtasari wa kodi ya zuio isiyokatwa kutoka kwa watoahuduma na kodi ya zuio isiyopelekwa katika Mamlaka ya Mapato Tanzania. Tabia hii inatishia malengo ya Serikali ya kuongeza makusanyo ya kodi ya mapato.

Jedwali Na. 10-6: Halmashauri zenye Mapungufu Kuhusu Kodi ya Zuio

Na.	Maelezo	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Kodi ya zuio isiyokatwa kutoka kwa watoa huduma	25	223,603,084
2	Kodi ya zuio isiyopelekwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania	17	538,148,940
Jumla		42	761,752,024

Menejimenti za halmashauri zinashauriwa kuongeza udhibiti wa ndani kwenye malipo yanayofanyika ngazi za kata na mitaa na malipo madogomadogo; ziimarishe vitengo vya ukaguzi wa awali; na zidai kodi ya zuio kwa watoahuduma wote ambao hawakukatwa kodi hiyo.

10.9 Deni la Sh. 9,830,045,745 Kutokana na Ukiukaji Kwenye Uendeshaji wa Akaunti za Amana

Aya ya 5.19 ya Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 inaelekeza kuwa "Halmashauri hupokea amana mbalimbali. Kwa kuzingatia madhumuni tofauti ya amana hizo, rejesta za amana zinapaswa kutunzwa kwa kila amana peke yake".

Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2020, nimekagua matumizi yaliyofanyika kwenye akaunti za amana na kubaini mapungufu mbalimbali yenye thamani ya Sh. 9,830,045,745 katika halmashauri 86 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 10-7**. Mapungufu haya ni pamoja na malipo yaliyofanyika bila idhini, malipo yaliyozidi kutoka kwenye akaunti ya amana; na kutorejesha mkopo kutoka akaunti ya amana kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 10-7**.

Fedha zisizorejeshwa kwenye akaunti za amana zinaacha deni kubwa kwa menejimenti za halmashauri na inaweza kusababisha kutoaminiwa na wafadhili na wadau wengine wa maendeleo.

Jedwali Na. 10-7: Mapungufu Kwenye Uendeshaji wa Akaunti za Amana

Na.	Maelezo	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Malipo yaliyofanyika bila idhini	30	2,450,944,924
2	Malipo yaliyozidi kutoka kwenye akaunti ya amana	28	4,602,015,935
3	Mikopo isiyorejeshwa kwenye akaunti ya amana	28	2,777,084,886
Jumla		**86**	**9,830,045,745**

Usimamizi dhaifu wa fedha zinazolipwa hasa utunzaji duni wa rejesta ya akaunti ya amana na upangaji mbaya wa bajeti husababisha ukopaji wa fedha kutoka kwenye akaunti za amana unaofanywa na halmashauri.

Ninashauri menejimenti za halmashauri ziimarishe udhibiti wa akaunti za amana. Pia, halmashauri zilizokopa fedha kwenye akaunti za amana zirejeshe fedha hizo mara moja.

10.10 Uhamisho Katika Akaunti za Ndani Kiasi cha Sh. 222,704,137 Ambazo Hazikurejeshwa

Agizo Na. 23(1-2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kudhibiti matumizi yake kwa kutumia vifungu vya bajeti. Pia, inawapa kazi wawekahazina wa halmashauri kuwa waangalizi wa vifungu vya bajeti kwa kila idara ndani ya halmashauri.

Ukaguzi wa uhamishaji wa fedha kwenye akaunti mbalimbali ulibaini kuwa halmashauri 30 zinadaiwa mikopo ya ndani ya jumla ya Sh. 222,704,137 hadi tarehe 30 Juni 2020 kama **Jedwali Na. 10-8** linavyoonesha. Hii inaashiria kwamba shughuli zenye jumla ya Sh. 222,704,137 hazikutekelezwa licha ya kuwa kwenye bajeti.

Jedwali Na. 10-8: Uhamisho Wa Ndani Kwenye Akaunti (Mikopo) Isiyorejeshwa

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/M Morogoro	23,318,060
2	H/W Nyang'hwale	43,447,000
3	H/M Tabora	155,939,077
Jumla		**222,704,137**

Ninaziagiza menejimenti za halmashauri husika kurejesha fedha zilizokopa; na ziimarishe udhibiti wa ndani kwa kutumia vifungu vya bajeti kwa kila idara.

10.11 Mapungufu Kwenye Matumizi ya Mafuta Yenye Jumla ya Sh. 1,561,318,703

Agizo Na. 89(3) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 limetoa maelekezo kwa madereva wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu ujazaji wa kitabu cha kumbukumbu za magari; pia Agizo Na. 89(7) la

Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 limemwagiza ofisa usafirishaji kukagua mara kwa mara kama kitabu cha kumbukumbu za magari kinajazwa ipasavyo.

Ukaguzi nilioufanya kuhusu usimamizi wa mafuta kwenye halmashauri 68 nilibaini kuwa madereva wa serikali za mitaa hawajazi ipasavyo vitabu cha kumbukumbu za magari kwa kutojaza kumbukumbu za mafuta kwenye vitabu vyao kiasi cha Sh. 1,545,314,548. Pia, sikuweza kuthibitisha matumizi ya mafuta ya thamani ya Sh. 16,004,155 kwa sababu ya kutoa mafuta hayo kwenye magari binafsi kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 10-8**.

Vilevile, nilibaini kuwa maofisa usafirishaji hawakagui vitabu vya kumbukumbu ili kuthibitisha kiasi cha mafuta waliyopewa madereva wa serikali za mitaa na hivyo kupelekea madereva kutotimiza wajibu wao.

Jedwali Na. 10-9: Mapungufu Kwenye Matumizi ya Mafuta

Na.	Maelezo	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Mafuta yasiyojazwa kwenye Vitabu vya kumbukumbu	68	1,545,314,548
2	Mafuta yaliyotolewa kwenye magari binafsi bila kibali	2	16,004,155
	Jumla	**70**	**1,561,318,703**

Manunuzi ya mafuta yanagharimu fedha nyingi kwenye matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Usimamizi mbovu wa leja na vitabu vya kumbukumbu unapelekea matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Ninashauri menejimenti za halmashauri ziimarishe udhibiti wa matumizi ya mafuta. Pia, maofisa usafirishaji wakague vitabu vya kumbukumbu mara kwa mara kama inyotakiwa kwenye maagizo yaliyoainishwa hapo juu.

10.12 Matumizi ya Sh. 7,806,190,916 Yasiyo Katika Bajeti na Fedha Zilizobadilishwa Matumizi

Agizo Na. 18(5) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa la Mwaka 2009 linakataza matumizi kabla ya kupata idhini kutoka baraza la madiwani isipokuwa malipo ya watumishi na fedha zinazofadhiliwa na serikali kuu. Pia, Agizo Na. 23(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa la Mwaka 2009 linaelekeza kutumia fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na kwa malengo yaliyokusudiwa.

Katika ukaguzi wangu ilibainika kuwa halmashauri 45 zilifanya matumizi ya Sh. 3,513,433,014 bila kuidhinishwa; na halmashauri 51 zilitumia jumla ya Sh. 4,292,757,902 kwa vifungu tofauti kinyume na magizo tajwa hapo juu kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 10-9**

Jedwali Na. 10-10: Matumizi yasiyokuwepo kwenye bajeti na fedha zilizobadilishwa matumizi

Na.	Maelezo	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Matumizi yaliyolipwa kwa vifungu tofauti	51	4,292,747,902
2	Matumizi yasiyokuwepo kwenye bajeti	45	3,513,433,014
	Jumla	**96**	**7,806,180,916**

Udhibiti mdogo wa bajeti ni chanzo cha kuwa na matumizi nje ya bajeti. Matumizi hayo yanasababisha kutofanyika kwa shughuli zilizo ndani ya bajeti.

Ninashauri menejimenti za halmashauri zitekeleze shughuli zilizopangwa ili kufikia malengo ya bajeti. Pia, menejimenti za halmashauri husika ziombe kibali cha kuhalalisha matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti zao.

10.13 Madeni ya Sh. 825,320,001 Kulipwa pasipo kuoneshwa Kwenye Hesabu za Mwaka Uliopita

Agizo Na. 22(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 inasema “Matumizi yanayostahili kulipwa yalipwe mwaka husika; malipo yasiyolipwa yatakuwa deni ili kuepuka matumizi zaidi kwa mwaka unaofuata”.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa halmashauri 27 hazikuweka madeni yao yenye thamani ya Sh. 825,320,001 kwenye taarifa za fedha za mwaka uliopita, hivyo kusababisha kuongezeka kwa malipo nje ya bajeti. Menejimeni za halmashauri husika hazikuweza kuthibitisha iwapo malipo ya madeni hayo yalitengewa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2020 kama inavyoelezwa kwenye **Jedwali Na. 10-11**.

Jedwali Na. 10-11: Orodha ya halmashauri ambazo hazikuripoti Madeni

Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Arusha	7,487,500	15	H/W Momba	18,150,000
2	H/W Bumbuli	144,111,455	16	H/W Monduli	42,057,200

Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
3	H/W Chamwino	13,000,000	17	H/W Moshi	15,572,145
4	H/Jiji Dodoma	34,310,000	18	H/W Pangani	10,408,874
5	H/W Hai	27,297,000	19	H/W Rombo	23,500,000
6	H/W Handeni	20,595,000	20	H/W Shinyanga	8,014,841
7	H/Mji Handeni	2,484,120	21	H/W Siha	18,405,800
8	H/W Karatu	14,704,000	22	H/M Sumbawanga	9,822,800
9	H/W Kibondo	28,320,500	23	H/M Tabora	65,527,580
10	H/W Kilolo	54,016,464	24	H/Jiji Tanga	114,959,880
11	H/W Longido	6,291,177	25	H/Mji Tunduma	20,380,000
12	H/Mji Mbulu	15,821,479	26	H/W Ukerewe	21,456,123
13	H/W Meru	27,268,343	27	H/W Urambo	12,112,000
14	H/W Missenyi	49,245,720			

Ulipaji wa madeni yasiyotambuliwa awali unasababisha kuzidishwa kwa matumizi kwa mwaka husika.

Menejimenti za halmashauri zinatakiwa kuweka madeni yote kwenye taarifa za fedha wakati wa kuandaa bajeti ijayo.

10.14 Fedha za Zuio Kiasi cha Sh. 1,357,341,869 Kutopelekwa Kwenye Mamlaka Husika

Agizo kutoka Wizara ya Maji (Kumb. CAB 544/693/01/24) la tarehe 27 Juni 2019 linazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhamisha mali na madeni ikiwemo fedha za zuio za miradi ya maji kwenda Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa mkoa husika kabla ya tarehe 30 Septemba 2019. Pia, agizo kutoka OR – TAMISEMI kwa barua ya tarehe 03 Disemba 2016 yenye Kumb. Na. EA.194/283/01/D/93 linazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhamisha mali na madeni ikiwemo fedha za zuio za miradi ya barabara kwenda kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

Kiyume na maagizo tajwa hapo juu, ukaguzi wangu ulibaini kuwa hadi tarehe 30 Juni 2020, halmashauri 11 hazikuhamisha kiasi cha Sh. 1,115,088,297.02 cha fedha za zuio ya miradi ya maji kwenda RUWASA; na Sh. 242,253,572 kwa halmashauri 3 kwenda TARURA kama inavyooneshwa kwenye **Majedwali Na. 10-12**, **10-13** na **10-14.**

Halmashauri hizi zimeshindwa kuhamisha fedha hizo kwa sababu zilizikopa kutoka kwenye akaunti za amana. Kutohamisha fedha za zuio kwenda TARURA na RUWASA kwa mkoa husika kunasababisha wakandarasi kutolipwa fedha zao punde miradi itanapokamilika.

Jedwali Na. 10-12: Fedha za Zuio Zisizo Pelekwa Kwenye Mamlaka Husika

Na.	Maelezo	Idadi ya Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Fedha za zuio zisizopelekwa RUWASA	11	1,115,088,297
2	Fedha za zuio zisizopelekwa TARURA	3	242,253,572
	Jumla	**14**	**1,357,341,869**

Jedwali Na. 10-13: Fedha za Zuio Zisizo Pelekwa RUWASA

Fedha za zuio zisizopelekwa RUWASA Sh. 1,115,088,297					
Na.	**Halmashauri**	**Kiasi (Sh.)**	**Na.**	**Halmashauri**	**Kiasi (Sh.)**
1	H/W Bumbuli	323,576,891	7	H/W Lushoto	162,690,983
2	H/W Karatu	36,782,981	8	H/W Monduli	12,732,046
3	H/W Kibondo	117,190,899	9	H/W Njombe	68,858,405
4	H/W Kilindi	94,011,730	10	H/W Nsimbo	54,098,057
5	H/Mji Korogwe	21,422,163	11	H/W Nyasa	146,463,722
6	H/W Longido DC	77,260,420		**Jumla**	**1,115,088,297**

Jedwali Na. 10-14: Fedha za Zuio Zisizo Pelekwa TARURA

Fedha za zuio zisizopelekwa TARURA Sh.. 242,253,572					
Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Lushoto DC	93,913,817	3	Nyasa DC	83,181,836
2	Momba DC	65,157,919		**Jumla**	**242,253,572**

Ninazishauri menejimenti za halmashauri husika kutii maagizo yaliyotolewa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na OR-TAMISEMI kwa kuhamisha fedha zote za zuio kwenda TARURA na RUWASA kadiri ya madai husika.

SURA YA 11

USIMAMIZI WA MAPATO

11.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea mambo yaliyotokana na ukaguzi wangu juu ya ufanisi wa usimamizi wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ukaguzi wangu ulijikita katika kujiridhisha namna Mamlaka za Serikali za Mitaa zinavyotathmini, kukusanya na kuhakikisha kuwa mapato yanapelekwa benki kwa wakati; na kuchambua utoshelevu wa mifumo ya udhibiti wa ndani katika jitihada za kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Tathmini yangu juu ya sera, mikakati na mifumo ya udhibiti wa ndani wa ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ilibaini mapungufu kadhaa kama vile usimamizi hafifu wa mashine za kukusanyia mapato; ukosefu au kutohuishwa kwa sheria ndogondogo; na kutowekwa kwa mifumo ya usimamizi na uendeshaji wa huduma za afya katika hospital, vituo vya afya, na zahanati. Maeneo mengine yaliyobainika kuwa na mapungufu ni mapato yaliyokusanywa lakini hayakuwasilishwa benki; kuwepo kwa miamala ambayo haijasuluhishwa; mapato kukusanywa nje ya mfumo; kutofautiana kwa taarifa mbalimbali za mapato yaliyokusanywa; na kuwepo kwa vitabu vya kukusanyia mapato ambavyo kwa sasa havistahili kutumika.

11.1 Kutokuwekwa kwa Mfumo wa Kielekitroniki wa Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Afya Kwenye Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati

Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliagizwa na Katibu Mkuu wa OR-TAMISEMI kufunga mifumo ya kielekitroniki ya usimamizi na uendeshaji wa huduma za afya kwenye hospitali, vituo vya afya, na zahanati kwa lengo la kufuatilia taarifa za wagonjwa, ankara za malipo, na kudhibiti mapato yanayokusanywa. Maagizo hayo yalitolewa kupitia barua yenye Kumb. Na. CEB.151/297/02/“N”/61 ya tarehe 17 Oktoba 2016. Nilipitia utekelezaji wa maelekezo hayo na kubaini kwamba vituo vya afya na zahanati 1,439 katika halmashauri 58 zilikuwa hazijawekewa mfumo huo kinyume na maelekezo ya hapo juu. Badala yake, mapato yaliendelea kukusanywa kwa kutumia stakabadhi kutoka kwenye vitabu vya kukusanyia mapato vya kawaida.

Jedwali Na. 11-1 linaonesha orodha ya vituo vya afya na zahanati ambazo hazijasimikwa mfumo wa mapato.

Jedwali Na. 11-1: Orodha ya Vituo vya Afya na Zahanati Ambazo Hazijasimikwa Mfumo Wa Mapato

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya vituo	Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya vituo
1.	H/W Kalambo	59	30.	H/W Simanjiro	34
2.	H/W Sumbawanga	59	31.	H/W Mwanga	12
3.	H/M Sumbawanga	20	32.	H/W Same	44
4.	H/W BAHI	39	33.	H/Mji Geita	11
5.	H/W Mpwapwa	4	34.	H/W Missenyi	25
6.	H/W Kasulu	3	35.	H/Mji Bunda	12
7.	H/W Ikungi	36	36.	H/W Serengeti	46
8.	H/W Igunga	51	37.	H/Jiji Mwanza	8
9.	H/W Kaliua	38	38.	H/W Ruangwa	38
10.	H/W Uyui	24	39.	H/M Temeke	14
11.	H/Jiji Dodoma	35	40.	H/W Lindi	26
12.	H/W Kigoma	33	41.	H/W Kilosa	41
13.	H/W Mpanda	12	42.	H/W Nsimbo	16
14.	H/W Mbogwe	7	43.	H/W Namtumbo	1
15.	H/W Kwimba	47	44.	H/W Momba	37
16.	H/W Monduli	35	45.	H/W Karagwe	37
17.	H/W Ngorongoro	27	46.	H/W Mbarali	51
18.	H/W Hai	4	47.	H/W Kiteto	12
19.	H/W Moshi	46	48.	H/W Muheza	32
20.	H/Mji Mbulu	8	49.	H/W Rombo	26
21.	H/Mji Masasi	1	50.	H/M Shinyanga	6
22.	H/W Bukombe	8	51.	H/W Longido	23
23.	H/W Geita	5	52.	H/M Lindi	13
24.	H/W Kyerwa	24	53.	H/W Kisarawe	33
25.	H/M Musoma	2	54.	H/W Kibaha	20
26.	H/W Babati	43	55.	H/Mji Kibaha	12
27.	H/M Moshi	12	56.	H/W Kilwa	54
28.	H/W Mlele	1	57.	H/W Siha	11
29.	H/W Mkinga	12	58.	H/W Ngara	49
	Jumla				**1,439**

Kutowekwa kwa mfumo wa mapato kunatokana na uhaba wa fedha za kununulia vifaa vinavyotumika kwenye mfumo huo ulioidhinishwa na serikali. Mapato yanayokusanywa katika vituo vya afya na zahanati ambazo

hazijawekewa mfumo wa kukusanyia mapato yanaweza kutumika vibaya bila kugundulika na uongozi wa vituo husika.

Ninaishauri halmashauri kutenga fedha za kutosha zitakazowezesha kununua vifaa muhimu kwa ajili ya kuweka mfumo huo katika vituo vyote vya afya na zahanati na hospitali sambamba na maelekezo tajwa hapo juu.

11.2 Kutohuishwa au Kutotungwa kwa Sheria Ndogondogo kwa Ajili ya Kukusanya Mapato

Sheria ndogondogo huwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato ya ndani kutoka vyanzo mbalimbali katika maeneo yao ya utawala. Utungaji wa sheria ndogondogo unaenda sambamba na matakwa ya Kifungu cha 89(1-3) cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ya Mwaka 1982 (iliyorekebishwa mwaka 2006) na Kifungu cha 153(1)(2) cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya Mwaka 1982 (iliyorekebishwa mwaka 2006). Hata hivyo, baada ya kupitia nyaraka mbalimbali nilibaini halmashauri 8 hazikuhuisha au zilikosa kabisa sheria ndogondogo kinyume na vifungu tajwa hapo juu. Kutohuishwa au kutungwa kwa sheria ndogondogo kunatokana na mchakato wa kuidhinisha sheria hizo OR-TAMISEMI kuchukua muda mrefu. Mamlaka ambazo hazikuhuisha sheria ndogondogo zinaoneshwa katika **Jedwali Na. 11-2**.

Jedwali Na. 11-2: Mamlaka Ambazo Hazijahuisha Sheria Ndogondogo

Na.	Jina la Halmashauri	Hali ya Sheria Ndogondogo
1.	H/W Meatu	**Sheria ndongondogo za minara ya simu hazijaanzishwa**
2.	H/W Shinyanga	Sheria ndogondogo zilizopo hazijahuishwa
3.	H/W Kibondo	Sheria ndogondogo zilizopo za mwaka 2017 hazijahuishwa
4.	H/W Iramba	Sheria ndogondogo zilizopo hazijahuishwa
5.	H/W Itigi	Sheria ndogondogo hazijaanzishwa
6.	H/Jiji Mwanza	Sheria ndogondogo zilizopo za mwaka 2008 hazijahuishwa
7.	H/W Itilima	Sheria ndogondogo hazijaanzishwa
8.	H/W Handen	Sheria ndogondogo hazijaanzishwa

Kutohuisha au kutotunga sheria ndogondogo kunapunguza wigo wa vyanzo vya ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na

hatimaye hivyo kushindwa kutoa huduma tarajiwa kwenye jamii kutokana na uhaba wa fedha.

Ninashauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa sheria ndogondogo zinatungwa au zinahuishwa ili kuimarisha hali ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, na hivyo kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali kuu.

11.3 Udhaifu Uliobainika Katika Usimamizi wa Mashine za Kukusanyia Mapato (POS)

Agizo la 45(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka mali zote ambazo hazihitajiki, hazitumiki au zimepitwa na wakati kutambuliwa na kuondolewa kwa kuuzwa au kuteketezwa baada ya kupata idhini kutoka kamati ya fedha na hatimaye baraza la madiwani.

Katika kupitia usimamizi wa mashine za kukusanyia mapato, nilibaini kwamba mashine 613 katika halmashauri 19 zilikuwa zimeharibika na hazitumiki, na hakuna hatua zilizochukuliwa na mamlaka husika ama kuzitengeneza au kuziondoa kinyume na Agizo tajwa hapo juu. Pia, halmashauri hizo hazikufanya uhakiki wa mapato yaliyokusanywa na mashine zilizoharibika ili kujiridhisha iwapo fedha zote zilizokusanywa na kwa kutumia mashine hizo zilipelekwa benki. Halikadhalika, nilipitia "dashboard' kwenye mfumo wa kukusanyia mapato katika halmashauri 54 na kubaini kuwa mashine 1,469 zilikuwa nje ya mtandao kwa siku zinazoanzia 2 hadi siku 1,570.

Mapungufu yaliyobainika katika usimamizi wa mashine za mapato yalitokana na kukosekana kwa miongozo mahususi kutoka mamlaka husika juu ya nini kifanyike baada ya mashine za kukusanyia mapato kuharibika, kutokuwepo kwa mtandao katika baadhi ya maeneo, na baadhi ya watumiaji wa mfumo kutoelewa uzuri wa mfumo huo. Mashine zilizoharibika na zilizokuwa nje ya mtandao ni kama zinavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 11-3**.

Jedwali Na. 11-3: Udhaifu Katika Usimamizi wa Mashine za Kukusanyia Mapato

Na	Jina la Halmashauri	Mashine Zilizoharibika	Mashine zilizokuwa nje ya Mtandao	Na	Jina la Halmashauri	Mashine Zilizoharibika	Mashine zilizokuwa nje ya Mtandao
1.	H/W Kwimba	41	22	32.	H/Mji Nanyamba	10	16
2.	H/W Sengerema		23	33.	H/W Ruangwa		29
3.	H/Mji Mafinga		14	34.	H/M Ubungo		134
4.	H/W Kyela	48		35.	H/M Ilala	39	20
5.	H/W Kalambo		9	36.	H/W Kilosa		53
6.	H/W Nkasi		26	37.	H/W Ulanga		14
7.	H/W Sumbawanga		15	38.	H/Mji Masasi	15	
8.	H/W Chamwino		56	39.	H/W Newala	12	72
9.	H/W Chemba		45	40.	H/Mji Newala		35
10.	H/Jiji Dodoma		46	41.	H/W Mkuranga		24
11.	H/Mji Kondoa		12	42.	H/W Chato		10
12.	H/W Kongwa		12	43.	H/W Rorya		8
13.	H/W Mpwapwa		18	44.	H/W Mbulu		7
14.	H/W Uvinza		38	45.	H/W Nyasa	12	12
15.	H/W Sikonge		7	46.	H/W Tunduru		54
16.	H/W Ngorongoro		51	47.	H/W Ileje	13	36
17.	H/W Hai	59	46	48.	H/W Mbozi	53	
18.	H/W Moshi		45	49.	H/W Iringa		19
19.	H/W Same	56		50.	H/M Iringa		21
20.	H/W Ukerewe	32		51.	H/W Chunya		13
21.	H/W Rungwe		24	52.	H/M Songea		8
22.	H/Mji Makambako	74	12	53.	H/W Mbinga		45
23.	H/W Makete		18	54.	H/W Tandahimba	12	58
24.	H/W Wanging'ombe	16	10	55.	H/W Siha		26
25.	H/W Madaba		13	56.	H/W Chalinze		6
26.	H/Mji Kahama	4		57.	H/Mji Chalinze		8
27.	H/Jiji Mbeya	88	72	58.	H/W Mafia		10
28.	H/W Bagamoyo		7	59.	H/M Mtwara	21	
29.	H/W Rombo		16	60.	H/Mji Ifakara		14
30.	H/M Shinyanga	8		61.	H/W Kibiti		13
31.	H/W Longido		12	62.	H/W Kisarawe		35
					Jumla	**613**	**1,469**

Mashine za kukusanyia mapato ambazo zimeharibika zinaongeza hatari ya kupoteza mapato kutokana na kutochunguzwa na menejimenti ya halmashauri husika mara baada ya kuharibika. Pia, usimamizi usioridhisha wa mashine za kukusanyia mapato ulisababisha menejimenti za halmashauri husika kushindwa kugundua mashine ambazo zinakuwa nje ya mtandao kwa muda mrefu, hivyo kusababisha mapato yaliyokusanywa na mashine hizo kuchelewa kupelekwa benki au kutopelekwa kabisa.

Ninashauri menejimenti za halmashauri husika zichunguze mashine zote zilizoharibika ili kubaini kama kuna mapato yaliyokusanywa na mashine hizo na hayakupelekwa benki, na kuchukua hatua stahiki. Pia, ninashauri menejimenti za halmashauri husika zihakikishe mashine zote za kukusanyia mapato zinaunganishwa na mtandao wakati wote wa kukusanya mapato na fedha zote zilizokusanywa na mashine zilizokuwa nje ya mtandao zipelekwe benki mapema iwezekanavyo.

11.4 Changamoto Zilizobainika Kwenye Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato (LGRCIS)

Lengo la kuanzishwa kwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa lilikuwa kuondoa udhaifu uliokuwa umekithiri katika taratibu za ukusanyaji wa mapato, ikiwa pamoja na kuzuia uvujaji wa mapato yaliyokusanywa, kuwepo kwa uwazi, na kuwezesha taarifa muhimu za ukusanyaji wa mapato kupatikana kwa wakati.

Nilifanya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa kukusanyia mapato katika halmashauri zote 185 na changamoto mbalimbali zilibainika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 53 zilizoainishwa kwenye **Jedwali Na. 11-4**.

Jedwali Na. 11-4: Orodha ya Halmashauri Zenye Changamoto za Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato

Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri
1.	H/W Kwimba	19.	H/W Hai	37.	H/W Wanging'ombe
2.	H/W Misungwi	20.	H/W Moshi	38.	H/W Madaba
3.	H/W Sengerema	21.	H/W Simanjiro	39.	H/W Tunduru
4.	H/W Msalala	22.	H/W Meru	40.	H/W Chunya
5.	H/W Shinyanga	23.	H/W Mwanga	41.	H/W Mbinga
6.	H/M Sumbawanga	24.	H/W Serengeti	42.	H/M Ilemela
7.	H/W Chemba	25.	H/W Ukerewe	43.	H/W Mbarali
8.	H/W Kondoa	26.	H/M Temeke	44.	H/W Karatu

Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri
9.	H/Mji Kondoa	27.	H/M Ilala	45.	H/W Malinyi
10.	H/W Mpwapwa	28.	H/W Kilosa	46.	H/W Tandahimba
11.	H/W Buhigwe	29.	H/W Mlimba	47.	H/W Siha
12.	H/W Iramba	30.	H/W Newala	48.	H/W Masasi
13.	H/M Ubungo	31.	H/W Mkuranga	49.	H/W Mvomero
14.	H/W Itigi	32.	H/Mji Bariadi	50.	H/W Makete
15.	H/W Mkalama	33.	H/W Meatu	51.	H/Mji Njombe
16.	H/W Igunga	34.	H/W Mbulu	52.	H/W Monduli
17.	H/W Kaliua	35.	H/M Moshi	53.	H/W Ngorongoro
18.	H/W Uyui	36.	H/W Rungwe		

Changamoto zilizobainika kuhusiana na uendeshaji wa mfumo wa mapato zimeelezewa kama ifuatavyo:

- ✓ Mfumo unaruhusu mlipaji mmoja kuwa na namba ya utambulisho zaidi ya moja (payer IDs) na hivyo kusababisha changamoto kwenye ufuatiliaji wa historia ya malipo ya walipaji. Mfumo unatakiwa kuzuia mlipaji mmoja kuwa na namba ya utambulisho zaidi ya moja kwa kuhakikisha kila akaunti ya mlipaji inahusishwa na utambulisho binafsi wa mlipaji kama vile namba ya mlipakodi (TIN).

- ✓ Mfumo wa mapato kuwa na mwingiliano baina ya halmashauri. Kwa nyakati tofauti watumiaji wa mfumo hujikuta wameingia kwenye halmashauri zisizo zao wakati wamesajiliwa kuingia kwenye halmashauri zao tu. Changamoto hii inapelekea kukosekana kwa usiri na uadilifu wa taarifa za mfumo kuwa shakani na hivyo kutoa mwanya wa kufanya udanganyifu.

- ✓ Mfumo wa mapato haujawekwa vyanzo vyote vya mapato kwenye baadhi ya halmashauri kama ada ya matangazo na ushuru wa huduma na kupelekea vyanzo hivi kukusanywa kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato (miscellaneous sources) kwenye mfumo.

- ✓ Mfumo wa mapato hauwezi kuwasiliana moja kwa moja na mfumo wa usimamizi wa fedha (Epicor) bila kuhusisha mtumiaji.

- ✓ Mfumo wa mapato hauna utaratibu rasmi wa kufanya usuluhishi kati ya miamala ya kwenye mashine za kukusanyia mapato (POS) na mapato yaliyopo kwenye mfumo (LGRCIS).

- ✓ Kukosekana kwa huduma ya kuaminika ya mtandao na kusababisha shughuli za ukusanyaji wa mapato kusimama kwa muda kwenye baadhi ya maeneo. Hii hupelekea taarifa za ukusanyaji wa mapato kutokufika kwa wakati kwenye mfumo wa mapato.

- ✓ Kutokana na kuwepo changamoto za mtandao mashine za kukusanyia mapato zinaweza kuwa kwenye mtandao lakini hushindwa kupeleka taarifa za kila siku kwenye seva kuu na hivyo kuonekana kuwa zipo nje ya mtandao.

- ✓ Mfumo wa mapato hautambui miamala ambayo si ya pesa taslimu, hivyo fedha ambazo hazikukusanywa miaka ya nyuma hata kama zilitambuliwa kwenye hesabu za mwisho hutambulika kama mapato ya mwaka ambao pesa hizo hupokelewa. Mfumo wa mapato unatakiwa kuwezeshwa kutambua mapato yanayotambuliwa kwenye hesabu hata kama mapato hayo yanakuwa hayajawasilishwa kwa pesa taslimu ili kuendana na matakwa ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu za mwisho.

- ✓ Kwenye baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa watumiaji wa mfumo waliendelea kuwa hai hata kama watumiaji hao walikoma kuwa watumishi kwenye mamlaka hizo kwa sababu mbalimbali.

- ✓ Mapato yanayokusanywa kutokana na mauzo ya viwanja yanapokelewa nje ya mfumo wa mapato na hivyo kuongeza hatari ya kutumika vibaya bila kugundulika kirahisi na menejimenti ya halmashauri.

- ✓ Mfumo wa mapato hauwezi kukokotoa tozo au adhabu ambayo mlipaji atatakiwa kulipa kutokana na kutokufuata taratibu na sheria za ukusanyaji wa mapato au uendeshaji wa halmashauri.

Kukosekana kwa ufanisi wa mfumo wa kukusanyia mapato kunaongeza shaka juu ya kuaminika kwa taarifa zinazotokana na mfumo huo na kupelekea kuandaliwa taarifa za fedha zenye dosari. Halikadhalika, changamoto za kimfumo zinaongeza uwezekano wa watumishi wasio waaminifu kufanya

vitendo vya ulaghai na hivyo kutumia vibaya mapato yanayokusanywa. Mfano halisi ni ulaghai uliotekea katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambapo mtaalamu wa TEHAMA na mhasibu msaidizi walituhumiwa kuiba kiasi cha Sh 270,046,700, ambapo mtaalamu wa TEHAMA alianzisha mashine yake ya kukusanyia mapato ambayo ilikuwa haionekani kwenye mtandao na taarifa zake zilikuwa haziendi kwenye mfumo wa mapato.

Ninaishauri OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa changamoto za kimfumo nilizoainisha zinatafutiwa ufumbuzi wa kudumu ili kupunguza uwezekano wa mapato ya halmashauri husika kufujwa.

11.5 Kutokusanywa kwa Ushuru wa Huduma na Hoteli Kwenye Taasisi za Kibiashara 36,284

Kifungu Na. 6(1)(u) na Kifungu 7(1) vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019) vinataka Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya fedha zote zinazotokana na ushuru wa huduma inayolipwa na makampuni kwa kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya mauzo ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa. Hivyo, kodi ya huduma inapaswa kulipwa na taasisi zote za kibiashara zinazofanya kazi ndani ya endeo la halmashauri.

(i) Kutokusanywa kwa Ushuru wa Huduma Kutoka Katika Taasisi za Kibiashara

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilitathmini ufanisi wa ukusanyaji wa ushuru wa huduma na kubaini kwamba halmashauri 44 hazikukusanya ushuru wa huduma kwenye makampuni 35,284 yaliyokuwa yanafanya kazi ndani ya maeneo ya halmashauri hizo, hivyo kupelekea kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji. Orodha ya halmashauri ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma na idadi ya taasisi imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 11-5**.

Jedwali Na. 11-5: Kutokusanywa kwa Ushuru wa Huduma Kwenye Taasisi za Kibiashara

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Taasisi / Makampuni	Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Taasisi / Makampuni
1.	H/W Magu	21	23.	H/W Mufindi	662
2.	H/W Msalala	39	24.	H/W Mlele	7
3.	H/W Kalambo	324	25.	H/Jiji Mbeya	24,479
4.	H/W Nkasi	201	26.	H/W Madaba	4
5.	H/W Sumbawanga	2,175	27.	H/Mji Mbinga	24

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Taasisi / Makampuni	Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Taasisi / Makampuni
6.	H/Mji Nzega	3	28.	H/W Nyasa	25
7.	H/W Monduli	33	29.	H/W Mpimbwe	795
8.	H/W Ngorongoro	151	30.	H/W Mbinga	10
9.	H/W Moshi	232	31.	H/Jiji Arusha	713
10.	H/W Korogwe	16	32.	H/W Arusha	9
11.	H/W Meru	56	33.	H/W Karatu	41
12.	H/W Mwanga	31	34.	H/W Chalinze	41
13.	H/Jiji Mwanza	135	35.	H/W Kibaha	21
14.	H/M Temeke	7	36.	H/W Mafia	48
15.	H/M Ilala	2,387	37.	H/W Kisarawe	13
16.	H/M Kinondoni	1,642	38.	H/M Morogoro	5
17.	H/W Mkuranga	14	39.	H/W Bagamoyo	11
18.	H/W Rorya	5	40.	H/M Shinyanga	259
19.	H/Mji Kahama	13	41.	H/W Longido	139
20.	H/W Kilolo	342	42.	H/W Siha	37
21.	H/M Handen	54	43.	H/W Hanang	36
22.	H/W Muheza	18	44.	H/W Mkinga	6
	Jumla				**35,284**

(ii) Kutokusanywa Ushuru wa Hoteli Kutoka kwa Walipaji Mbalimbali

Nilibaini kuwa halmashauri 16 zilishindwa kukusanya ushuru wa hoteli kutoka kwa walipaji 1,014 wa ushuru huo kinyume na Kifungu 7(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019). Hali hii ilisababishwa na halmashauri kutoweka juhudi za kutosha katika ukusanyaji wa ushuru wa kutoka taasisi husika. Halmashauri ambazo hazikukusanya ushuru wa hoteli kutoka kwa walipaji ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 11-6.**

Jedwali Na. 11-6: Ushuru wa Hoteli Kutokusanywa Kutoka kwa Walipaji

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Walipaji	Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Walipaji
1.	H/W Monduli	16	9.	H/W Pangani	11
2.	H/W Moshi	37	10.	H/W Bagamoyo	6
3.	H/W Mwanga	17	11.	H/W Siha	33
4.	H/W Bukombe	113	12.	H/Jiji Arusha	550
5.	H/W Bumbuli	14	13.	H/W Arusha	111
6.	H/M Mpanda	7	14.	H/W Karatu	55

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Walipaji	Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Walipaji
7.	H/W Kibaha	11	15.	H/W Kisarawe	3
8.	H/Mji Kibaha	8	16.	H/W Mafia	22
	Jumla				**1,014**

Ushuru wa huduma na hoteli ambao haukukusanywa kutoka kwa taasisi mbalimbali za kibiashara ulizinyima uwezo halmashauri husika kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri kuongeza juhudi zitakazowezesha kukusanya ushuru wa huduma na hoteli kutoka kwa taasisi zote za kibiashara zinazotakiwa kulipa ushuru huo.

(iii) Kodi Ya Huduma Iliyokusanywa Bila Ushahidi Wa Mauzo

Halmashauri 28 zilikusanya kiasi cha Sh. 7,924,291,456 kutoka kwenye makampuni mbalimbali kama ushuru wa huduma bila kupata ushahidi wa mauzo kutoka kwenye mamlaka inayohusika au kutoka kwenye makampuni hayo ili kujiridhisha iwapo kiasi kilichokusanywa ni sahihi, kinyume na vifungu tajwa hapo juu. **Jedwali Na. 11-7** linaonesha orodha ya halmashauri zilizokusanya ushuru wa huduma bila kupata ushahidi wa mauzo.

Jedwali Na. 11-7: Kodi ya Huduma Iliyokusanywa Bila Ushahidi Wa Mauzo

Na	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh)	Na	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Bagamoyo	6,874,676	15	H/W Chato	88,512,200
2	H/W Buhigwe	7,264,071	16	H/W Bunda	105,899,232
3	H/W Manyoni	17,111,861	17	H/W Musoma	115,318,559
4	H/W Itilima	19,010,711	18	H/W Butiama	148,553,311
5	H/W Tunduru	23,893,487	19	H/Jiji Mwanza	150,643,317
6	H/Mji Mbulu	32,709,105	20	H/W Rorya	164,012,707
7	H/W Kilindi	36,617,426	21	H/W Magu	221,741,566
8	H/W Meatu	58,044,121	22	H/M Songea	263,688,289
9	H/W Kyela	59,202,878	23	H/W Chalinze	280,152,578
10	H/Mji Bariadi	69,230,870	24	H/W Msalala	294,570,183
11	H/M Temeke	70,209,808	25	H/W Ngorongoro	300,336,015
12	H/W Shinyanga	71,471,102	26	H/W Mbinga	320,748,355
13	H/W Mkuranga	76,854,618	27	H/W Kishapu	741,671,618
14	H/M Kinondoni	3,549,908,900	28	H/W Morogoro	630,039,891
	Jumla				**7,924,291,456**

Kiasi cha ushuru wa huduma kilichokusanywa kinaweza kuwa kidogo kuliko kiasi kilichotakiwa kukusanywa kutokana na kukosekama kwa ushahidi wa mauzo ambayo yangetumika kukokotoa kiasi kilichotakiwa kulipwa na makampuni hayo.

Ninazishauri halmashauri husika kuhakikisha zinapata ushahidi wa mauzo ya makampuni husika kutoka kwenye vyanzo vya kuaminika ili kusaidia kukokotoa kiasi sahihi cha ushuru wa huduma kinachotakiwa kulipwa na makampuni yanayofanya kazi kwenye maeneo yao.

11.6 Mapato ya Sh. 18,769,299,624 Yaliyokusanywa Pasipo Kupelekwa Benki


Agizo la 50(5) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka fedha zote zilizopokelewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kupelekwa benki kila siku au siku ya kazi inayofuata baada ya kukusanywa. Kuzingatia agizo hili kunapunguza vishawishi vya kutumia fedha hizo kwa shughuli ambazo hazikukusudiwa.

Nilipitia taarifa za makusanyo za halmashauri 135 na kubaini kwamba kiasi cha Sh 18,769,299,624 kilikusanywa kutoka vyanzo mbalimbali. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi dhahiri kuwa kiasi hicho kiliwasilishwa benki, kinyume na agizo tajwa hapo juu. Kiambatisho Na. 11-1 kinaonesha orodha ya halmashauri ambazo hazikupeleka benki mapato yaliyokusanywa.

Pia, nilipitia taarifa za makusanyo ya kodi za maegesho ya bajaji katika Manispaa ya Kigoma-Ujiji na kubaini kwamba halmashauri ilitoa stika kwa wamiliki wa bajaji zenye thamani ya Sh. 172,848,000 kama kodi ya maegesho. Hata hivyo, kiasi cha Sh 67,067,100 tu ndicho kilithibitishwa kupelekwa benki, na kiasi cha Sh. 105,780,900 hakikupelekwa benki kinyume na agizo tajwa hapo juu.

Mchoro Na.11-1 unaonesha kuwa mapato ambayo hayapelekwi benki yamekuwa yakiongezeka kila mwaka ikilinganishwa na miaka iliyopita. Hii inaonesha kuwa bado kuna usimamizi hafifu wa mapato. Vilevile, inaashiria kuwa mapendekezo niliyoyatoa miaka ya nyuma hayakutekelezwa ipaswavyo ili kuondoa hali hiyo.

Mchoro Na. 11-1: Mapato Yaliyokusanywa Lakini Hayakupelekwa Benki



Kutopatikana kwa nyaraka zinazoonesha mapato yaliyokusanywa yalipelekwa benki kulinizuia kujiridhisha kuhusu uhalali, usahihi na ukamilifu wa kiasi cha mapato kilichokusanywa na kuwekwa kwenye taarifa za fedha za halmashauri husika.

Ninazishauri halmashauri ziimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani iliyopo ya ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha kuwa mapato yaliyokusanywa yanapelekwa benki kwa wakati sambamba na kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyopo. Halikadhalika, halmashauri husika zinatakiwa kufanya ufuatiliaji wa mapato hayo na kuhakikisha yanapelekwa benki haraka iwezekanavyo.

Pia, nilibaini kwamba halmashauri 5 zilikusanya kiasi cha Sh 2,036,203,930 ambazo hazikupelekwa benki kwa wakati kinyume na agizo tajwa hapo juu. **Jedwali Na. 11-8** linaonesha orodha ya halmashauri ambazo fedha hazikupelekwa benki kwa wakati.

Jedwali Na. 11-8: Mapato Yaliyopelekwa Benki kwa Kuchelewa

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Siku za Kuchelewesha	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Babati	Siku 7 hadi 307	250,009,180
2.	H/W Bumbuli	Siku 4 hadi 12	9,782,000

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Siku za Kuchelewesha	Kiasi (Sh.)
3.	H/W Arusha	Siku 4 hadi 311	49,838,400
4.	H/W Karatu	Siku 3 hadi 59	125,191,500
5.	H/Jiji Dar es Salaam	Siku 3 hadi 85	1,601,382,850
	Jumla		**2,036,203,930**

Mapato kutopelekwa benki kwa wakati kunadhihirisha kuwa fedha zilizokusanywa zilikuwa zinatumika kabla ya kupelekwa benki; na vitendo hivi vinaongeza hatari ya fedha zilizokusanywa kutumika vibaya na maofisa wanahosika na makusanyo.

Ninazishauri halmashauri kuchukua hatua stahiki dhidi ya wakusanyaji wanaochelewa kupeleka fedha benki ikiwa pamoja na kutoza faini; hii itasaidia kuhakikisha mapato yanayokusanywa yanapelekwa benki kwa wakati.

11.7 Mapato ya Sh. 1,337,063,592 Yaliyokusanywa Nje ya Mfumo

Kifungu cha 17A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019) inazitaka halmashauri kukusanya mapato kwa kutumia mfumo wa ukusanyaji wa mapato. Halikadhalika, aya ya 5.2.1 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 unazitaka halmashauri kukusanya mapato kwa kutumia Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS).

Nilipitia taarifa mbalimbali za ukusanyaji wa mapato katika halmashauri 22 na kubaini kwamba kiasi cha Sh. 1,337,063,592 kilikusanywa kutoka kwenye leseni za biashara na vyanzo vinginevyo. Hata hivyo, kiasi hicho kilikusanywa nje ya mfumo wa mapato kinyume na kifungu tajwa hapo juu. **Jedwali Na. 11-9** linaonesha orodha ya halmashauri zilizokusanya mapato nje ya mfumo.

Jedwali Na. 11-9: Mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo

Na	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh)	Na	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Wang'ing'ombe	3,981,700	12	H/Mji Korogwe	18,534,660
2	H/W Monduli	5,479,000	13	H/W Kishapu	20,668,838
3	H/W Longido	5,812,500	14	H/W Tandahimba	34,578,750
4	H/W Nanyumbu	7,517,000	15	H/W Moshi	34,941,800

Na	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh)	Na	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
5	H/Mji Kahama	9,054,600	16	H/W Rombo	51,115,059
6	H/W Njombe	10,729,000	17	H/W Bunda	55,655,510
7	H/W Karatu	11,482,413	18	H/W Babati	67,344,531
8	H/W Mbulu	14,154,850	19	H/W Kilwa	67,868,700
9	H/W Musoma	15,056,000	20	H/W Msalala	86,594,000
10	H/M Tabora	16,801,062	21	H/M Shinyanga	159,950,750
11	H/W Mkinga	18,408,000	22	H/Jiji Arusha	621,334,869
	Jumla				**1,337,063,592**

Mapato yanayokusanywa nje ya mfumo yanaweza kutumiwa vibaya na wakusanyaji bila kugundulika kwa kuwa hayaonekani kwenye mfumo. Pia, makusanyo yanayofanyika nje ya mfumo yanaongeza hatari ya watumishi au wakusanyaji kujihusisha na vitendo vya rushwa na ubadhirifu.

Ninazishauri halmashauri kuacha kabisa kukusanya mapato nje ya mfumo sambamba kwa mujibu wa kifungu cha sheria tajwa hapo juu. Pia, hatua stahiki zichukuliwe na OR-TAMISEMI kwa halmashauri zote zilizokusanya mapato nje ya mfumo kinyume na kufungu tajwa hapo juu.

11.8 Miamala ya Sh. 35,997,956,890 ya Wadaiwa Mbalimbali Ambayo Haijasuluhishwa Kwenye Mfumo

Nilipitia taarifa mbalimbali zinazotokana na mfumo wa ukusanyaji mapato katika halmashauri 67 na kubaini kwamba kiasi cha Sh. 35,997,956,890 kilikuwa hakijawasilishwa na wadaiwa wanaokusanya mapato kwenye vyanzo mbalimbali. Kuwepo kwa wadaiwa ambao hawajawasilisha mapato kutokana na kutofanya usuluhishi ni kinyume na agizo la 29(2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linalomtaka mwekahazina kufanya usuluhishi kwa wakati. **Jedwali Na. 11-10** linaonesha wadaiwa ambao miamala yao haikusuluhishwa.

Jedwali Na. 11-10: Wadaiwa Mbalimbali Ambao Miamala yao Haikusuluhishwa Kwenye Mfumo

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/MJI Babati	4,252,890	35	H/W Makete	96,746,893
2	H/W Karagwe	6,973,707	36	H/W Hai	105,197,047
3	H/MJI Nzega	12,788,114	37	H/W Moshi	110,712,582
4	H/W Nsimbo	16,163,297	38	H/Mji Masasi	115,155,297

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
5	H/W Rungwe	18,141,278	39	H/M Ilala	117,456,100
6	H/W Korogwe	19,166,330	40	H/W Nzega	124,102,635
7	H/W Handeni	19,350,544	41	H/W Nyasa	129,039,498
8	H/W Kibiti	21,265,050	42	H/Mji Geita	130,600,847
9	H/W Masasi	23,280,251	43	H/W Mpanda	133,001,769
10	H/W Longido	24,343,955	44	H/W Nachingwea	141,841,282
11	H/W Pangani	24,827,904	45	H/W Same	150,463,186
12	H/W Tandahimba	24,850,534	46	H/W Songea	174,624,200
13	H/W Kiteto	26,338,864	47	H/M Morogoro	189,137,940
14	H/M Songea	26,615,666	48	H/W Chemba	194,989,020
15	H/W Bukombe	28,076,104	49	H/W Simanjiro	197,995,300
16	H/Jiji Mbeya	28,137,367	50	H/W Mbozi	214,832,707
17	H/W Kasulu	28,193,795	51	H/W Siha	242,747,150
18	H/Mji Bariadi	41,014,664	52	H/W Nanyumbu	250,176,085
19	H/W Bumbuli	42,786,225	53	H/W Mbogwe	268,490,389
20	H/Mji Mafinga	46,060,208	54	H/W Busokelo	289,263,996
21	H/W Kilindi	46,591,500	55	H/W Namtumbo	335,285,397
22	H/W Mwanga	49,429,000	56	H/W Morogoro	346,256,817
23	H/W Mkinga	57,108,723	57	H/W Mlele	379,381,653
24	H/W Newala	60,626,199	58	H/Jiji Arusha	516,009,298
25	H/W Iringa	64,316,266	59	H/Mji Ifakara	522,221,823
26	H/W Muheza	64,892,351	60	H/W Meru	552,430,585
27	H/Mji Handeni	67,068,042	61	H/M Iringa	577,618,675
28	H/W Busega	70,822,000	62	H/W Momba	583,092,186
29	H/W Mvomero	75,362,396	63	H/M Mpanda	620,189,563
30	H/Mji Tunduma	82,774,602	64	H/Mji Korogwe	647,221,005
31	H/W Mbinga	84,419,482	65	H/W Mlimba	788,658,256
32	H/W Gairo	89,610,516	66	H/W Hanang’	1,045,646,733
33	H/W Maswa	91,198,412	67	H/Jiji Dar es Salaam	24,225,812,741
34	H/M Moshi	94,712,000		**Jumla**	**35,997,956,890**

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilishindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kutokana na kushindwa kukusanya kiasi ambacho kilichokuwa kwa wadaiwa ambao miamala yao ilikuwa haijasuluhishwa, hivyo kushindwa kutekeleza shughuli mbalimbali zilizokuwa zimepangwa. Pia, uwepo wa mapato yasiyowasilishwa kutokana na kutofanya usuluhishi kunaongeza hatari ya wakusanya mapato wasio waaminifu kutumia vibaya kiasi kilichokusanywa.

Ninashauri menejimenti za halmashauri kufanya usuluhishi wa kiasi ambacho hakijaletwa na wakusanyaji wa mapato; na kuhakikisha kuwa kiasi chochote kinachotakiwa kuwasilishwa na wakusanyaji kinawasilishwa kwenye mamlaka husika mapema iwezekanavyo. Halikadhalika, halmashauri zihakikishe kuwa usuluhishi wa miamala unafanyika kwa wakati kwa mujibu wa Agizo la 29(2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 ili kupunguza uwezekano wa mapato kutumika vibaya.


11.9 Mapato ya Sh. 30,856,567,370 Ambayo Hayakukusanywa Kutoka Kwenye Vyanzo Mbalimbali

Agizo la 38(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linasema kuwa "litakuwa jukumu la mwekahazina kuweka taratibu za kifedha na kihasibu zitakazowezesha kuhakikisha fedha zote za halmashauri zinakusanywa, kutunzwa na kupelekwa benki kwa wakati".

Nilipitia taarifa mbalimbali za mapato zinazotokana na mfumo wa mapato wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS) na kubaini kuwa kiasi cha Sh. 30,856,567,370 hakikukusanywa katika halmashauri 124 kutokana na mauzo ya viwanja, ukodishaji wa vibanda, leseni za biashara, leseni za vileo, na vyanzo vingine kinyume na agizo tajwa hapo juu. Kiambatisho Na. 11-2 kinaonesha mapato ambayo hayakukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali.

Mwenendo wa mapato ambayo hayakusanywi kutoka vyanzo mbalimbali yanaelekea kuwa sawa na mwaka uliopita kama inavyoonekana kwenye **Mchoro Na. 11-2**. Mapato mengi kutokusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kunaashiria kuwa halmashauri hazikuwa na ufanisi wa ukusanyaji mapato; na kwamba mapendekezo yangu niliyoyatoa miaka ya nyuma yamekuwa hayatekelezwi ipasavyo.

Mchoro Na. 11-2: Mwenendo Wa Mapato Ambayo Hayakukusanywa



Kukosekana kwa dhamira ya dhati ya usimamizi wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususani kutokusanya kiasi kilichotajwa hapo juu kunaweza pelekea mapato hayo kutopatikana kabisa na hivyo kusababisha hasara kwa mamlaka husika.

Ninazishauri halmashauri husika zibuni mikakati thabiti itakayosaidia kukusanya mapato hayo kutoka kwa wadaiwa. Vielelezo vyote vya kukusanya kiasi tajwa hapo juu viletwe kwangu kwa ajili ya uhakiki.

11.10 Miamala ya Sh. 4,792,502,078 Iliyofutwa Kwenye Mfumo Wa Mapato Bila Kuwa na Viambatisho Muhimu

Agizo la 37(6) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaagiza kuwa ikiwa makosa yatajitokeza wakati wa kuandika risiti ya mapato, risiti hiyo itatakiwa kufutwa na kuandikwa nyingine mara moja. Risiti iliyofutwa inatakiwa kutunzwa vyema kwa ajili ya kuhakikiwa wakati wa ukaguzi. Kwa maana hiyo, miamala inayofutwa kwenye mfumo ni lazima iambatishwe na nyaraka muhimu ili kujiridhisha kama marekebisho hayo ni halali.

Nilipitia marekebisho ya miamala kwenye mfumo wa mapato katika halmashauri 35 na kubaini kuwa kiasi cha Sh. 4,792,502,078 kilifutwa kwenye mfumo bila kuambatishwa nyaraka muhimu za marekebisho hayo; na wakati mwingine marekebisho hayo hayakuidhinishwa na mwekahazina au ofisa masuuli, kinyume na agizo tajwa hapo juu. Miamala iliyofutwa kwenye mfumo wa mapato bila kuwa na viambatisho inaoneshwa katika **Jedwali Na. 11-11**.

Jedwali Na. 11-11: Miamala Iliyofutwa Kwenye Mfumo wa Mapato Bila Kuwa na Viambatisho

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Tunduru	1,210,981,227	19	H/M Sumbawanga	45,478,900
2	H/W Siha	624,153,964	20	H/W Urambo	36,613,598
3	H/W Nanyumbu	497,991,938	21	H/W Kilolo	34,754,281
4	H/W Kilindi	320,033,902	22	H/W Ruangwa	32,379,700
5	H/W Kasulu	297,066,660	23	H/M Kigoma-Ujiji	31,301,318
6	H/W Liwale	258,737,465	24	H/MJI Kasulu	28,696,931
7	H/W Nyasa	242,833,600	25	H/W Handeni	15,562,504
8	H/W Namtumbo	191,935,660	26	H/W Busokelo	14,063,170
9	H/M Songea	184,370,128	27	H/W Buhigwe	13,681,473
10	H/M Tabora	149,385,887	28	H/W Shinyanga	12,239,000
11	H/W Bahi	74,906,064	29	H/W Mpwapwa	10,722,000
12	H/W Songea	72,464,000	30	H/W Kyela	10,605,558
13	H/W Mbinga	66,095,877	31	H/JIJI Tanga	10,602,250
14	H/W Kakonko	64,651,714	32	H/W Mufindi	7,401,250
15	H/W Bariadi	63,040,546	33	H/W Mbeya	7,067,154
16	H/W Ulanga	57,933,852	34	H/W Mlimba	4,374,104
17	H/W Nsimbo	51,352,326	35	H/W Kongwa	3,184,184
18	H/W Morogoro	45,839,893		**Jumla**	**4,792,502,078**

Miamala inayofutwa bila kuwepo kwa viambatisho muhimu inaongeza hatari ya kutumika vibaya kwa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa kuwa miamala ya fedha zilizokusanywa kihalali inawezafutwa kwenye mfumo na hatimaye fedha hizo kutumika kwa matumizi yasiyo kusudiwa.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa mifumo ya udhibiti wa ndani inayohusika na ufutaji wa miamala inaimarishwa ili kuhakikisha kuwa marekebisho yote ya miamala yanakuwa na viambatisho muhimu na hatimaye kuzuia matumizi mabaya ya fedha zinazokusanywa.

11.11 Kutoingizwa kwa Bajeti ya Mapato Kwenye Mfumo wa Kukusanyia Mapato

Aya 5.2 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Ukusanyaji Mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 unataka halmashauri kuweka malengo ya ukusanyaji wa mapato yanayofikika baada ya kuzingatia mambo kama vile mfumuko wa bei, ongezeko la idadi ya watu, na mabadiliko ya sheria na kanuni kwa mwaka wa bajeti husika. Halikadhalika, Aya ya 3.2.9.2 ya

Mwongozo wa Mtumiaji wa Mfumo wa Kukusanyia Mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa unataka bajeti ya vyanzo vyote vya mapato kuingizwa kwenye mfumo wa mapato.

Nilipitia mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa halmashauri 11 na kubaini kwamba kiasi cha Sh. 16,338,391,958 kilikusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali bila kuingizwa kwenye mfumo wa mapato, kinyume na sheria na kanuni. Kiasi cha bajeti hakikuingizwa kwenye mfumo kutokana na jitihada ndogo za mamlaka husika kuhakikisha udhibiti wa bajeti unaimarishwa katika ukusanyaji wa mapato. Maelezo zaidi ya vyanzo ambavyo **havikuwekewa bajeti kwenye mfuko ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali Na. 11-12.**

Jedwali Na. 11-12: Bajeti Kutoingizwa Kwenye Mfumo wa Mapato

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Magu	9,829,185	7	H/MJI Babati	1,370,365,318
2	H/W Wang'ing'ombe	16,303,616	8	H/W Mpimbwe	1,490,838,097
3	H/W Meatu	40,322,400	9	H/W Tunduru	2,443,426,799
4	H/W Ulanga	279,655,503	10	H/W Geita	4,290,193,444
5	H/W Gairo	524,768,865	11	H/MJI Njombe	4,903,425,064
6	H/W Nyang'hwale	969,263,667		**Jumla**	**16,338,391,958**

Kutokuingizwa kwa bajeti kwenye mfumo wa mapato kunaongeza hatari ya kufanyika makosa ya kibinadamu na kupelekea kuandaliwa taarifa za fedha zisizo sahihi hususani wakati wa kupima ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kwa kila chanzo.

Ninazishauri halmashauri kuzingatia matakwa ya Aya ya 3.2.9.2 ya Mwongozo wa Mtumiaji wa Mfumo wa Kukusanyia Mapato (toleo la 0.1), kwa kuhakikisha bajeti ya vyanzo vyote vya mapato inaingizwa kwenye mfumo wa mapato ili kuongeza udhibiti wa kibajeti katika ukusanyaji wa mapato.

11.12 Mapato ya Sh. 140,131,679 Yaliyokusanywa Pungufu Kutokana na Kutoza Kiwango Kisicho Sahihi

Nilipitia taarifa mbalimbali za makusanyo ya mapato kwa kila chanzo ili kujiridhisha kama viwango vilivyokuwa vinatumika wakati wa kukusanya mapato vinaendana na viwango vilivyoidhinishwa kwenye sheria ndogondogo

za mamlaka husika. Baada ya kupitia taarifa hizo nilibaini kwamba halmashauri 7 zilikusanya mapato pungufu kwa kiasi cha Sh. 140,131,679 kutokana na kutumia viwango vidogo kuliko vilivyoidhinishwa kwenye sheria ndogondogo za mamlaka hizo kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 11-13**.

Jedwali Na. 11-13: Mapato Yaliyokusanywa Pungufu Kutokana na Kutoza Kiwango Kisicho Sahihi

Na.	Jina la Halmashauri	Upungufu wa Makusanyo (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Upungufu wa Makusanyo (Sh.)
1.	H/W Kishapu	41,643,000	5.	H/W Bumbuli	47,800,000
2.	H/W Nkasi	2,070,000	6.	H/W Arusha	10,568,679
3.	H/W Ngorongoro	3,070,000	7.	H/W Karatu	7,080,000
4.	H/W Mwanga	27,900,000		**Jumla**	**140,131,679**

Kutumika kwa viwango ambavyo si sahihi kumepelekea hasara ya kiasi cha Sh. 140,131,679 katika halmashauri 7. Hii imepelekea mamlaka husika kushindwa kutekeleza baadhi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa kutumia vyanzo vya ndani.

Halmashauri zinashauriwa kuhakikisha kuwa viwango vilivyoidhishwa kwenye sheria ndogondogo vinatumika wakati wote wa kukusanya mapato. Aidha, halmashauri zinashauriwa pia kufuata taratibu za kubadilisha sheria ndogondogo kwa kushirikisha wadau wote ikiwa viwango vya awali vilivyoidhishwa kwenye sheria za sasa vinadhaniwa kuwa vikubwa kuliko uhalisia.

11.13 Mawakala wa Ukusanyaji wa Mapato na Wapangaji Wanaofanya Kazi Bila Mikataba

Kifungu cha 28(1) (a) na (b) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorejewa mwaka 2019) kinazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kumteua mtu au watu kama mawakala watakaojihusisha na shughuli za ukusanyaji mapato na kuingia nao mikataba kwa namna itakavyokuwa inafaa. Hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuingia makubaliano ya kimkataba na mawakala wanaokusanya mapato ya ndani.

Kinyume na kifungu tajwa hapo juu, nilibaini halmashauri 9 zilikuwa na mawakala wa kukusanya mapato wapatao 532 ambao halmashauri hazikuwa na mikataba ya kisheria na mawakala hao. Halikadhalika, nilibaini halmashauri 13 zilikuwa na wapangaji mbalimbali 2,989 wa majengo lakini

halmashauri husika hazikuwa na mikataba iliyosainiwa na wapangaji hao. Uwepo wa wapangaji na mawakala wasio na mikataba unatokana na vitengo vya sheria vya halmashauri kutokutimiza wajibu wao katika kutoa ushauri mwafaka. **Jedwali Na. 11-14** linaonesha wakusanyaji wa mapato na wapangaji wasio na mikataba na halmashauri.

Jedwali Na. 11-14: Wakusanyaji wa Mapato na Wapangaji Wasio na Mikataba na Halmashauri

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya Mawakala	Idadi ya Wapangaji
1.	H/W Kishapu		29
2.	H/W Kyela	169	
3.	H/W Mkalama	21	
4.	H/W Hai	25	
5.	H/W Moshi		447
6.	H/W Kilindi		64
7.	H/W Meru		504
8.	H/W Mwanga		198
9.	H/M Ubungo	29	
10.	H/M Ilala		Idadi ya wapangaji haikupatikana
11.	H/M Musoma		704
12.	H/M Mpanda	33	604
13.	H/Mji Njombe		42
14.	H/W Chunya	31	
15.	H/M Songea		19
16.	H/W Siha		172
17.	H/W Hanang		135
18.	H/W Handen	153	
19.	H/W Gairo	7	
20.	H/Mji Kibaha		71
21.	H/W Kibiti	64	
	Jumla	**532**	**2,989**

Kukosekana kwa makubaliano ya kisheria kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na wapangaji au wakusanyaji wa mapato kunaweza kupelekea mamlaka husika kupoteza mapato kutokana na kushindwa kuwashitaki wahusika mahakamani kama hawataleta fedha walizokusanya au kodi ya pango inayotakiwa kulipwa na wapangaji.

Ninazishauri halmashauri husika kuhakikisha kuwa zinakuwa na mikataba halali na wakusanyaji wa mapato au wapangaji itakayosimamia ukusanyaji na uwasilishaji wa mapato ya mamlaka hizo.

11.14 Utofauti wa Mapato Yaliyokusanywa Baina ya Taarifa za Mapato

Agizo la 29(2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linamtaka mwekahazina wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya usuluhishi kati ya daftari la fedha na taarifa za benki angalau mara moja kwa mwezi na kuhakikisha kuwa tofauti zozote zinazobainika zinafanyiwa marekebisho ipasavyo.

Nilipitia taarifa mbalimbali za mapato na kubaini kwamba halmashauri 19 zilikuwa zimeonesha mapato ambayo taarifa zake zilikuwa zinakinzana kwa kiasi cha Sh. 6,057,141,857. Taarifa za mapato zilizopitiwa ni pamoja na taarifa za mfumo wa mapato, taarifa za mfumo wa uhasibu (epicor) na taarifa za leseni za biashara. Utofauti uliobainika ulitokana na kutokufanya kwa usuluhishi baina ya taarifa kama ilivyoelekezwa kwenye Agizo tajwa hapo juu. **Jedwali Na. 11-15** linaonesha orodha ya halmashauri zilizokuwa na taarifa za mapato zinazokinzana.

Jedwali Na. 11-15: Mapato Yaliyokusanywa Yenye Taarifa Zinazokinzana

Na.	Jina la Halmashauri	Taarifa zenye ukinzano	Utofauti (Sh.)
1.	H/W Shinyanga	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	24,909,563.54
2.	H/W Manyoni	Taarifa ya mfumo wa mapato na taarifa za kamati ya fedha	120,355,398
3.	H/Mji Bunda	Taarifa za makusanyo ya fedha za leseni za biashara na taarifa za idadi ya leseni zilizotolewa.	100,345,400
4.	H/Mji Nzega	Taarifa ya ujumla ya makusanyo na taarifa ya daftari la fedha taslimu	77,648,741
5.	H/W Korogwe	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	87,888,537
6.	H/W Ushetu	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	36,621,580
7.	H/M Ubungo	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	112,556,183
8.	H/M Ilala	Taarifa ya vitabu vya leseni za biashara na taarifa ya mfumo wa mapato	10,142,000
9.	H/M Ilala	Taarifa ya vitabu vya leseni za biashara na taarifa ya mfumo wa mapato	1,802,931,551

Na.	Jina la Halmashauri	Taarifa zenye ukinzano	Utofauti (Sh.)
10.	H/W Nachingwea	Taarifa ya vitabu vya leseni za biashara na taarifa ya mfumo wa mapato	8,155,000
11.	H/W Butiama	Taarifa za makusanyo ya fedha za leseni za biashara na taarifa za idadi ya leseni zilizotolewa	21,517,000
12.	H/Mji Njombe	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	346,111,544
13.	H/W Wanging'ombe	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	692,486,520
14.	H/W Momba	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	477,693,266
15.	H/Mji Tunduma	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	971,905,052
16.	H/W Chunya	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	515,671,877
17.	H/W Tarime	Taarifa za makusanyo ya fedha za leseni za biashara na taarifa za idadi ya leseni zilizotolewa.	37,739,993
18.	H/Jiji Tanga	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	38,934,161
19.	H/W Chalinze	Taarifa za mfumo wa mapato na taarifa ya mfumo wa uhasibu (epicor)	573,528,490
	Jumla		**6,057,141,857**

Utofauti wa mapato yaliyokusanywa baina ya taarifa unadhihirisha kwamba mapato kwenye baadhi ya vyanzo yanaweza kuwa yanakusanywa nje ya mfumo na hivyo kushindwa kuonekana kwenye taarifa zinazotoka kwenye mfumo. Tofauti hizi pia zinapelekea taarifa za mapato zinazoandaliwa kutoaminika na hesabu za mwisho za mamlaka husika zinazondaliwa kwa kutumia taarifa hizo huweza siziwe na usahihi.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuhakikisha kuwa Agizo la 29 (2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linazingatiwa ili kuhakikisha kuwa taarifa za mapato zinazoandaliwa hazikinzani ili wadau au watumiaji wa taarifa hizo waziamini.

11.15 Uhamisho wa Fedha Sh 196,428,864 Kutoka Kwenye Akaunti ya Mapato ya Ndani Kwenda Akaunti ya Amana Bila Kuzingatia Taratibu

Maelekezo yalitolewa na OR-TAMISEMI mnamo mwezi Septemba 2017 kuhusu Mfumo wa Malipo ya Kielekitroniki (TISS) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yalitaka fedha zilizopo kwenye akaunti ya mapato ya ndani kuhamishiwa kwenye akaunti ya Mfuko Mkuu au akaunti ya maendeleo angalau mara moja kwa wiki, na matumizi yalitakiwa kufanyika kwenye akaunti hizo.

Kinyume na maelekezo tajwa haya, nilipopitia mapato yaliyokusanywa katika halmashauri 5 nilibaini kwamba kiasi cha Sh. 196,428,864 kilihamishwa kutoka akaunti ya mapato ya ndani kwenda akaunti ya amana kama **Jedwali Na. 11-16** linavyoonesha.

Jedwali Na. 11-16: Mapato ya Ndani Yaliyohamishiwa Kwenye Akaunti ya Amana

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Kalambo	32,360,000	4.	H/W Longido	67,762,364
2.	H/W Lindi	10,000,000	5.	H/W Handen	19,593,000
3.	H/M Shinyanga	66,713,500		**Jumla**	**196,428,864**

Mapato ya ndani yaliyohamishiwa na kutumika kwenye akaunti ya amana hayakuwa na vifungu vya kufanyia malipo kwa fedha zinazotokana na mapato ya ndani. Hali hii inaweza pelekea kuonesha matumizi madogo kuliko uhalisia kwenye hesabu za mwisho za halmashauri husika. Pia, fedha zilizohamishwa bila kufuata taratibu zinaweza kutumika kwenye shughuli ambazo hazikukusudiwa.

Ninashauri menejimenti za halmashauri husika kuimarisha udhibiti wa ndani katika usimamizi wa fedha inayokusanywa, kwa kuhamisha fedha hizo kwenda kwenye akaunti ambazo zinakubalika kulingana na maagizo tajwa hapo juu.

11.16 Mapato ya Sh. 179,539,936 Yaliyokusanywa na Kutumika Kabla ya Kupelekwa Benki

Agizo la 50(5) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka fedha zote zilizopokelewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kupelekwa benki kila siku au siku ya kazi inayofuata baada ya kukusanywa.

Pia, Agizo la 37(3) na (9) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linazuia kutumia fedha zilizokusanywa kabla ya kupelekwa benki.

Nilipitia taarifa mbalimbali za makusanyo na kubaini kwamba halmashauri 4 zilitumia kiasi cha Sh. 179,539,936 kama marejesho ya fedha zilizotumika kwa shughuli mbalimbali kabla hazijapelekwa benki. Fedha hizo zilikuwa zinalipwa ili kufuta madeni yaliyopo kwenye mfumo kwa kuwa fedha zilizokusanywa zilitumika kabla ya kwenda benki. Orodha ya halmashauri zilizotumia fedha kabla ya kupelekwa benki ni kama zinavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 11-17**.

Jedwali Na. 11-17: Fedha za Mapato ya Ndani Zilizotumika Kabla ya Kupelekwa Benki

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Sumbawanga	154,164,250	**3.**	H/W Masasi	7,174,000
2.	H/W Kaliua	14,048,800	**4.**	H/W Ngara	4,152,886
	Jumla				**179,539,936**

Kutumia fedha za mapato ya ndani kabla ya kupeleka benki kunaongeza uwezekano wa fedha hizo kutumika kwa shughuli zisizokusudiwa na hivyo kuongeza hatari ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia Maagizo ya 37(3)(9) na 50(5) ya Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 kwa kuimarisha udhibiti wa ndani juu ya mapato yanayokusanywa ili kuzuia kabisa fedha zinazokusanywa kutumika kabla ya kupelekwa benki.

11.17 Mapato ya Sh. 2,345,843,498 Yaliyokusanywa na Mawakala Ambayo Hayakuwasilishwa

Nilipitia mikataba iliyoingiwa kati ya halmashauri 18 na mawakala wa kukusanya mapato pamoja na taarifa za mapato za mfumo nikabaini kwamba kiasi cha Sh. 2,345,843,498 kilikusanywa na mawakala mbalimbali. Hata hivyo, kiasi hicho hakikuwasilishwa kwenye mamlaka hizo kwa ajili ya kupelekwa benki. Hii ni kinyume na Agizo la 37(2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linalotaka fedha zinazokusanywa kupelekwa kwa mtunzafedha kwa ajili ya kutunzwa kila siku au siku ya kazi inayofuata baada ya kukusanya. **Jedwali Na. 11-18** lina orodha ya halmashauri ambazo mawakala hawakuwasilisha fedha.

Jedwali Na. 11-18: Mapato Yaliyokusanywa na Mawakala Ambayo Hayakuwasilishwa

Na	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/W Ushetu	1,440,889,650	10	H/M Iringa	23,860,100
2	H/Mji Makambako	434,675,164	11	H/M Ilala	22,946,760
3	H/W Ulanga	100,450,739	12	H/W Tunduru	20,036,054
4	H/W Igunga	82,339,496	13	H/JIJI Tanga	19,825,264
5	H/W Muheza	38,467,000	14	H/W Wang'ing'ombe	15,090,445
6	H/W Hanang'	36,821,538	15	H/M Lindi	12,900,000
7	H/W Kisarawe	31,090,466	16	H/W Kibiti	7,062,231
8	H/W Kwimba	28,819,950	17	H/MJI Babati	5,540,000
9	H/M Shinyanga	23,932,141	18	H/W Babati	1,096,500
	Jumla				**2,345,843,498**

Mawakala kutowasilisha mapato kwa wakati kunasababishwa na menejimenti za halmashauri kutokuwa makini katika kuwasimamia mawakala; hali hii inaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma.

Ninazishauri menejimenti za halmashauri zihakikishe kuwa mawakala wote wanazingatia masharti ya mikataba waliyosaini. Halikadhalika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya mawakala wote walioshindwa kutimiza masharti ya mkataba ili kuhakikisha fedha zilizokusanywa zinawasilishwa na kupelekwa benki.

11.18 Vitabu 30,446 vya Mapato Havikutumika Katika Halmashauri Mbili

Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliagizwa kuachana na utaratibu wa kukusanya mapato kwa kutumia vitabu vya mapato na kuanza kukusanya mapato kwa kutumia Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS). Mfumo huu ulianza kutumika rasmi kuanzia mwaka 2016. Kutokana na kuanzishwa kwa mfumo huo, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliachana na utaratibu wa awali na kuanza kutumia mashine za kukusanyia mapato kwa mujibu wa matakwa ya Kifungu cha 17A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, Sura ya 290 (kama iliyorekebishwa mwaka 2019).

Nilitembelea stoo maalumu za kutunzia nyaraka muhimu kwenye halmashauri 2 na kubaini kwamba mamlaka hizo zilikuwa zimefungia

vitabu 30,446 vya kukusanyia mapato ambavyo kwa sasa havitumiki. Vitabu hivyo vimehifadhiwa kwenye stoo hizo tangu mfumo mpya wa mapato ulipoanza kutumika. Jedwali Na. 11-19 linaonesha halmashauri na idadi vitabu vya kukusanyia mapato visivyotumika.

Jedwali Na. 11-19: Vitabu vya Kukusanyia Mapato Visivyotumika

Na.	Jina la Halmashauri	Idadi ya vitabu visivyotumika
1.	H/W Moshi	21,880
2.	H/W Mwanga	8,566
	Jumla	**30,446**

Uwepo wa vitabu vya mapato ambavyo havitumiki kunaweza sababisha vitabu hivyo kutumika kwa malengo yasiyotarajiwa na watumishi ambao si waaminifu na hatimaye kupoteza mapato ya halmashauri.

Ninashauri menejimenti za halmashauri husika kuainisha vitabu vyote ambavyo havitumiki kutokana na kuanzishwa kwa mfumo mpya wa mapato na kuomba mwongozo kutoka mamlaka inayohusika ili kupata maelekezo ya hatua za kuchukua ikiwa pamoja na kuvirejeha kwenye mamlaka husika au kuviteketeza.

SURA YA 12

USIMAMIZI WA MALI

12.1 Utangulizi

Usimamizi wa mali ni mchakato unaohusisha kujenga au kununua, kuendesha, kukarabati na kuondosha mali pasipo kutumia gharama kubwa. Serikali ina mali nyingi zilizonunuliwa au kujengwa kwa ajili ya matumizi ya umma. Ni muhimu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia vizuri mali zake kwa matumizi bora ili ziweze kunufaika nazo kwa muda mrefu.

Mali zinazomilikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zipo katika makundi makuu mawili, ambayo ni mali za kudumu na mali za muda mfupi. Mali za kudumu ni zile zinazoweza kutumika kwa muda mrefu, wakati mali za muda mfupi ni zile ambazo zinaweza kugeuzwa kuwa fedha au mfanano wa fedha ndani ya muda mfupi.

Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMD), kupitia Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa Mwaka 2019 imetoa utaratibu wa manunuzi, mgawanyo, matengenezo, uthaminishaji, uhasibu, uondoshaji, na shughuli zingine zinazohusisha usimamizi wa mali za umma. Kupitia Mwongozo huo Serikali itaweza kuzifuatilia na kuzitathmini mali zote inazozimiliki na kufanya uamuzi kadri inavyofaa.

Tathmini niliyoifanya kwenye usimamizi wa mali kwenye halmashauri 185 kwa mwaka wa fedha unaoishia mwezi Juni 2020 nimebaini mapungufu yafuatayo:

12.1 Kutokuwepo kwa Hati za Umiliki wa Ardhi Zenye Thamani ya Sh. 1,136,131,586,291 Kwenye Halmashauri

Kifungu cha 29(1) (b) cha Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, Na. 4, Sura ya 334 inasema "Pale kamishna wa ardhi anapoamua kutoa haki ya umiliki wa ardhi kwa mtu ambaye yuko katika miliki ya ardhi au ana ofa ya umiliki wa ardhi, atatoa cheti kinachojulikana kama hati ya umiliki wa ardhi kwa mtu huyo".

Nilipitia rejesta ya mali za kudumu za hesabu za mwisho zilizowasilishwa na halmashauri na kufanya mahojiano na menejimenti juu ya umiliki wa ardhi

na kubaini kuwa halmashauri 27 zilikuwa na ardhi yenye thamani ya jumla ya Shs 1,136,131,586,291 zilizoripotiwa kwenye hesabu zao za mwisho wa mwaka bila kuwa na hati ya umiliki kama inavyotakiwa na kifungu tajwa hapo juu.

Hii imesababishwa na uzembe wa menejimenti za halmashauri husika katika kupima ardhi wanayoimiliki ambayo ina majengo ya umma kama vile shule, vituo vya afya, na miradi mingine bila kuwa na hati ya umiliki. Hii inaweza kusababisha kupoteza mali hizo inapotokea mashauri au migogoro ya ardhi mahakamani dhidi ya umiliki wa ardhi ya halmashauri.

Vilevile, katika thamani ya mali za kudumu iliyoripotiwa kwenye hesabu za mwisho wa mwaka, halmashauri zimeshindwa kuthibitishwa usahihi wake kutokana na kukosekana kwa hati za umiliki wa ardhi na kushindwa kufanya uthaminishaji wa ardhi.

Mapungufu haya pia yemeripotiwa kwenye taarifa zangu za miaka ya nyuma pasipo Serikali kuchukua hatua stahiki kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 12-1**.

Jedwali Na. 12-1: Mwenendo wa Umiliki wa Ardhi Bila Hati kwa Miaka Mitatu

Maelezo	2017/18	2018/19	2019/20
Thamani ya ardhi (Shs)	25,709,450,864	85,688,595,997	1,136,131,586,291
Idadi ya Halmashauri	9	31	27

Mwenendo wa halmashauri kuwa na ardhi bila kuwa na hati ya umiliki umekuwa ukiongezeka kila mwaka, hivyo Serikali inatakiwa kufanya maamuzi ya kupima ardhi yote yenye majengo ya umma.

Jedwali Na. 12-2: Mali Zinazomilikiwa na Halmashauri Bila Kuwepo kwa Hati Miliki

Na.	Jina la Halmashauri	Thamani (Sh.)
1.	H/W Biharamulo	Hakuna maelezo.
2.	H/W Bukombe	8,934,586,000
3.	H/W Bumbuli	Hakuna maelezo.
4.	H/Mji Bunda	43,205,000
5.	H/W Chamwino	8,963,043,363
6.	H/W Chato	4,399,597,150
7.	H/W Gairo	7,914,429,327
8.	H/M Ilala	925,280,229,267

Na.	Jina la Halmashauri	Thamani (Sh.)
9.	H/W Karagwe	Hakuna maelezo.
10.	H/W Kibiti	5,080,650,000
11.	H/M Kigamboni	50,100,506,000
12.	H/W Kisarawe	1,909,435,000
13.	H/W Mafia	751,965,000
14.	H/W Makete	1,733,485,000
15.	H/W Mbogwe	4,416,164,000
16.	H/W Mkinga	269,593,350
17.	H/W Mlele	Hakuna maelezo.
18.	H/W Mlimba	4,294,589,900
19.	H/M Musoma	22,897,876,049
20.	H/W Nachingwea	13,381,083,000
21.	H/W Ngara	Hakuna maelezo.
22.	H/W Nyanghwale	3,774,909,000
23.	H/W Rorya	4,912,933,385
24.	H/W Simanjiro	Hakuna maelezo.
25.	H/W Singida	67,022,578,000
26.	H/W Songwe	Hakuna maelezo.
27.	H/Mji Tunduma	50,728,500
		1,136,131,586,291

Vilevile, nilibaini katika halmashauri 8 magari 77 na pikipiki 81 hazikuwa na kadi za usajili na kufanya nishindwe kuthibitisha uhalali wa umiliki. Hivyo, thamani ya mali iliyoripotiwa na halmashauri husika kwenye hesabu za mwisho inaweza kuwa imetolewa zaidi ya uhalisia.

Jedwali Na. 12-3: Magari na Pikipiki Ambazo Hazina Kadi za Usajili

Na.	Halmashauri	Magari	Pikipiki	Jumla
1	H/W Bagamoyo	13	-	13
2	H/W Bunda	4	4	8
3	H/W Chalinze	9	-	9
4	H/W Itigi	1	-	1
5	H/W Kibaha	1	4	5
6	H/M Kigamboni	34	-	34
7	H/W Kisarawe	12	59	71
8	H/W Serengeti	3	14	17
Jumla		**77**	**81**	**158**

Ninazishauri halmashauri husika kuandaa mpango wa kupima ardhi yao ili kuhakikisha kuwa ardhi yote yenye mali na miundombinu ya umma inamilikiwa kisheria na halmashauri. Pia, halmashauri husika zinapaswa kutafuta kadi za usajili wa magari na pikipiki inazozimiliki.

12.2 Magari na Mali Zingine Kutofanyiwa Matengenezo au Kuondoshwa kwa Muda Mrefu

Agizo la 45(1) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka mali zote ambazo hazihitajiki, zilizoshindikana matengenezo, zilizoharibika au vifaa chakavu kutambuliwa na kuondolewa baada ya kupata ruhusa ya kamati ya fedha na baadaye ruhusa ya baraza la madiwani.

Aya ya 27 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma, Sura ya 21 inataka wakati wa kutathmini iwapo kuna dalili ya mali ya kudumu kutofanya kazi au kutoa huduma ipasavyo, taasisi inapaswa kwa uchache kuangalia mambo yafuatayo kutoka vyanzo vya ndani (i) ushahidi uliopo wa kuharibika kwa mali hiyo, na (ii) ushahidi kutoka kwa wataalamu unaoonesha kuwa mali husika imeshindwa au itashindwa kufanya kazi au kutoa huduma kama inavyotegemewa.

Ukaguzi wa rejesta ya mali za kudumu na uthibitisho wa kushuhudia mali zinazomilikiwa na halmashauri ulibaini kwenye halmashauri jumla ya magari 727, pikipiki 138, na mali zingine 31 kama vile kompyuta na samani zilikuwa hazitumiki, zimetelekezwa, au kutofanyiwa matengenezo kwa muda mrefu bila menejimenti kuonesha juhudi za kuzifanyia matengenezo ili kuzitumia au kuziondoa kama inavyotakiwa na agizo tajwa hapo juu, kama **Kiambatisho Na. 12-1** kinavyoonesha**.**

Thamani ya mali za kudumu husika zinaweza kushuka zaidi na hivyo Serikali kushindwa kunufaika nazo wakati ingeweza kunufaika iwapo halmashauri zingeamua kuzifanyia matengenezo au kuziondoa mapema inavyowezekana.

Hoja hii imekuwa ikijirudia kwenye ripoti zangu zilizopita jambo linaloashiria kuwa kuna juhudi ndogo za halmashauri kutekeleza mapendekezo yangu kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 12-4**

Jedwali Na. 12-4: Mali Ambazo Zimetelekezwa na Hazijafanyiwa Matengenezo Kwa Muda Mrefu

	2017/18	2018/19	2019/20
Magari/pikipiki na mali zingine	504	912	896
Idadi ya Halmashuri	97	121	113

Mwenendo unaonesha kuwa mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma hayajafanyiwa kazi kikamilifu na halmashauri kwa kuwa inaonesha hakuna maboresho kwenye kufanya matengenezo au kuondoa mali chakavu na ambazo hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu.

Ninasisitiza mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma kwa menejimenti za halmashauri husika kujumuisha kwenye bajeti zao fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo na marekebisho ya mali za kudumu. Pia, kuongeza kasi kwenye mchakato wa kuondoa mali ambazo hazitengenezeki. Tathmini ya kuona kama mali imeshindwa kufanya kazi au kutoa huduma kama inavyotakiwa inapaswa kufanyika kila mwaka kama inavyotakiwa na Aya za 52 na 57 za Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma Sura ya 21.

12.3 Magari na Pikipiki za Mamlaka za Serikali za Mitaa Kutokukatiwa Bima

Agizo la 95(1) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linamtaka ofisa usafirishaji wa wilaya kuhakikisha kuwa magari yote yanakatiwa bima kulingana na matakwa ya sheria.

Ukaguzi nilioufanya wa mafaili ya magari na pikipiki kwenye halamshauri 185 umebaini kuwa kwenye halmashauri 61, jumla ya magari 441 na pikipiki 228 zimetumika bila kuwa na bima kinyume na agizo tajwa hapo juu kama K**iambatisho 12-2** kinavyoonesha**.**

Kutokukatia bima magari na pikipiki, halmashauri husika zinakuwa kwenye hatari ya kupata hasara kubwa pale magari au pikipiki zitakapopata ajali kama ilivyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 12-5.**

Jedwali Na. 12-5: Mwenendo wa Magari na Pikipiki Zinazoendeshwa Bila Kukatiwa Bima

	2017/18	2018/19	2019/20
Magari/pikipiki	266	617	669
Idadi ya Halmashauri	34	51	61

Uchambuzi wa mwenendo wa magari na pikipiki ambazo hazina bima unaonesha kuendelea kuongezeka licha ya mapendekezo yangu kwenye ripoti za miaka ya nyuma.

Ninazitaka menejimenti za halmashauri husika kukatia bima magari na pikipiki zote zinazomiliki kama inavyotakiwa na Agizo la 95(1) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009. Pia, zinapaswa kuingiza gharama za bima ya magari na pikipiki kwenye bajeti za mwaka.

12.4 Dawa zenye Thamani ya Sh. 1,537,713,125 Zilizokwisha Muda Wake lakini Hazikuteketezwa kwa Muda Mrefu

Kwa mujibu wa Agizo la 45(1) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka ya Mwaka 2009, mali zote ambazo hazihitajiki, zilizoshindikana matengenezo, zilizoharibika, au vifaa chakavu vinatakiwa kutambuliwa na kuondolewa kwa ruhusa ya kamati ya fedha na baadaye ruhusa ya baraza la madiwani.

Ukaguzi wa rejesta ya dawa ulibaini kuwepo kwa dawa zilizokwisha muda wake katika halmashauri 31 zenye thamani ya Sh. 1,537,713,125 ambazo hazikuteketezwa hadi wakati wa ukaguzi huu. Dawa hizi zilizokwisha muda wake zipo kwenye stoo za dawa za halmashauri kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 20.

Halmashauri kuendelea kuhifadhi dawa zilizokwisha muda wake kunaweza kusababisha athari za kiafya kwa watunza stoo. Vilevile, dawa zilizoripotiwa kwenye hesabu za mwisho zinaweza kuwa zimeripotiwa zaidi ya thamani yake kutokana na kutoondolewa kwa dawa zilizokwisha muda wake.

Jedwali Na. 12-6: Mwenendo wa Dawa Zilizokwisha Muda Wake Lakini Hazikuteketezwa kwa Miaka Mitatu

Miaka	Idadi ya Halmashauri zilizohojiwa	Mfuatano wa muda (miaka)	Kiasi kilichohojiwa
2017/18	6	0-30	276,887,999
2018/19	14	0-19	7,334,114,927
2019/20	31	0-20	1,537,713,125

Mwenendo unaonesha kuwa idadi ya halmashauri zenye dawa zilizokwisha muda wake imekuwa ikiongezeka hali inayoashiria kuwa mapendekezo

yangu niliyoyatoa kwenye ripoti za miaka ya nyuma bado hayajafanyiwa kazi na halmashauri.

Jedwali Na. 12-7: Dawa Zilizokwisha Muda Wake Bila Kuteketezwa

Na.	Halmashauri	Muda zilizokaa stoo toka kuisha kwa muda wake (Miaka)	Thamani (Sh.)
1.	H/W Arusha	0-2	2,539,458
2.	H/W Hai	2-6	43,807,181
3.	H/Mji Kibaha	0-6	10,874,164
4.	H/M Kigamboni	0-5	187,263,376
5.	H/W Kigoma	Zaidi ya miaka 5	127,886,008
6.	H/W Kilosa	0-10	52,916,637
7.	H/W Kilwa	0-10	37,308,732
8.	H/W Kongwa	0-5	154,474
9.	H/W Korogwe	0-10	64,404,725
10.	H/W Kwimba	0-20	46,396,510
11.	H/W Magu	0-5	5,869,309
12.	H/W Malinyi	0-2	215,945,011
13.	H/W Manyoni	0-1	8,378,150
14.	H/Mji Masasi	0-10	68,228,868
15.	H/W Mbulu	0-5	4,958,915
16.	H/Mji Mbulu	0-3	10,181,646
17.	H/W Mkuranga	Hakuna maelezo	9,853,137
18.	H/W Morogoro	0-14	14,577,105
19.	H/M Morogoro	1-5	13,583,704
20.	H/W Moshi	0-3	16,129,391
21.	H/W Nachingwea	0-10	116,971,261
22.	H/W Newala	0-3	75,606,085
23.	H/Mji Newala	0-5	237,888,738
24.	H/W Ngara	0-5	86,330,050
25.	H/W Panganl	0-10	3,163,310
26.	H/W Rombo	0-2	1,039,575
27.	H/W Rufiji	Hakuna maelezo	15,023,110
28.	H/W Same	0-6	16,651,161
29.	H/Jiji Tanga	0-4	4,751,500
30.	H/W Ukerewe	Hakuna maelezo	16,420,000
31.	H/W Ulanga	2-8	22,611,834
Jumla			**1,537,713,125**

Ninazitaka menejimenti za halmashauri zilizotajwa hapo juu kuhakikisha kuwa dawa zote zilizokwisha muda wake zinateketezwa kwa mujibu wa matakwa ya sheria. Pia, kabla ya kuagiza dawa, halmashauri zinapaswa kufanya hesabu ya dawa zilizopo na zinazotakiwa ili kupata kiasi cha kuagiza ili kuepuka kuagiza zaidi ya mahitaji.

12.5 Mapungufu Kwenye Utunzaji wa Rejesta ya Magari, Mitambo Na Vifaa

Agizo la 103(1) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linazitaka halmashauri kutunza rejesta ya usajili wa mali zake au za kukodisha.

Aidha, Kifungu cha 5.3.13 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 kinaelezea rejesta ya mali zisizohamishika kama rekodi ya mali zote za kudumu ambazo halmashauri inamiliki kwa kipindi cha kutoa taarifa hiyo.

Vilevile, Kifungu cha 6.2(ii) cha Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa Mwaka 2019 kinaagiza kuwa Ofisa Masuuli katika fungu husika awe mtunzamali zote za umma kwa niaba ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, na atatoa nakala ngumu na laini ya rejesta ya mali ili kurahisisha uhakiki wa mali na taarifa zake.

Mapitio ya rejesta ya mali za kudumu kwa mwaka wa fedha 2019/20 yamebaini halmashauri 16 zimeshindwa kutunza na mara kwa mara kuhuisha taarifa za mali za kudumu zilizoripotiwa kwenye rejesta kama inavyotakiwa na kifungu tajwa hapo juu.

Kushindwa kutunza au kuhuisha mara kwa mara rejesta ya mali kunaweza kusababisha upotevu wa mali za umma na /au kuripoti pungufu mali kwenye hesabu za mwisho za halmashauri.

Jedwali Na. 12-8: Mapungufu Kwenye Utunzaji wa Rejesta ya Magari, Mitambo na Vifaa

Na.	Halmashauri	Kutohifadhi rejesta ya Mali	Kutohuisha mara kwa mara rejesta ya mali	Rejesta ya mali kutotolewa kwenye mfumo au nakala laini
1.	H/W Chamwino		x	

Na.	Halmashauri	Kutohifadhi rejesta ya Mali	Kutohuisha mara kwa mara rejesta ya mali	Rejesta ya mali kutotolewa kwenye mfumo au nakala laini
2.	H/W Ikungi	x		
3.	H/Mji Kahama	x		
4.	H/W Kaliua			x
5.	H/W Kishapu	x		
6.	H/W Kiteto		x	
7.	H/W Korogwe		x	
8.	H/W Mbalali	x		
9.	H/W Newala	x		
10.	H/W Nzega			x
11.	H/Mji Nzega			x
12.	H/W Pangani	x		
13.	H/W Sikonge			x
14.	H/W Urambo			x
15.	H/W Ushetu	x		
16.	H/W Uyui			x

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatakiwa kuanzisha utaratibu wa kutunza rejesta ya mali kwenye mfumo na kutunza kumbukumbu kwa usahihi na umakini taarifa ya mali zote za kudumu za halmashauri ili kusaidia urahisi wa ufuatiliaji na kuweza kuzuia upotevu wa mali unaoweza kutokea.

12.6 Kutowekwa Namba za Utambulisho Wala Kuhifadhiwa Vyema kwa Mali za Kudumu Zilizonunuliwa za Thamani ya Sh. 2,805,639,190

Kwa mujibu wa Agizo la 63(5) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, mali zote za kudumu zitawekwa namba za utambulisho wa mali na kuhifadhiwa kwenye rejesta ya mali za kudumu.

Sehemu ya 9.3(e) ya Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2019 inataka mali zote za kudumu ziwe na namba inayozitambulisha, zikionesha pamoja na taarifa zingine, umiliki wake, mahali zilipo, na miaka ya kutumika.

Ukaguzi niliofanya ulibaini kuwa kati ya halmashauri 185 zilizokaguliwa, halmashauri 18 zilinunua mali mbalimbali za kudumu zenye thamani ya Sh.

2,805,639,190 lakini hazikuwekewa namba za utambulisho na hivyo kutorekodiwa kwenye rejesta ya mali za kudumu.

Udhaifu wa udhibiti wa ndani kwenye usimamizi na udhibiti wa mali za umma unaweza kusababisha upotevu wa mali za umma bila kutambua upotevu huo.

Jedwali Na. 12-9: Mali za Kudumu Zilizonunuliwa na Kutowekewa Namba za Utambulisho

	2017/18	2018/19	2019/20
Thamani ya mali za kudumu ambazo hazina namba ya utambulisho (Sh.)	151,444,230	604,066,669	2,805,639,190
Idadi ya Halmashauri	7	12	18

Uchambuzi wa mwenendo unaonesha ongezeko la idadi ya halmashauri ambazo hazijaweka namba za utambulisho kwenye mali za kudumu pamoja na ongezeko la thamani ya mali husika. Hii inamaanisha kuwa kuna udhaifu kwenye menejimenti ya halmashauri juu ya udhibiti wa mali zilizonunuliwa na utunzaji wa rejesta ya mali za kudumu.

Ninapendekeza menejimenti za halmashauri kuanzisha mfumo wa udhibiti kwenye uwekaji wa namba za utambulisho kwenye mali za kudumu zilizonunuliwa/kujengwa ili kuepuka uwezekano wa upotevu wa mali bila kutambua.

Jedwali Na. 12-10: Mali Za Kudumu Zilizonunuliwa Bila Kuwekewa Namba za Utambulisho

Na	Halmashauri	Mali iliyonunuliwa	Kiasi (Sh.)
1	H/W Babati	Samani, kompyuta na televisheni	8,258,568.81
2	H/W Bumbuli	Kompyuta mpakato, mashine ya fotokopi, printa, na jenereta	198,979,218
3	H/W Busega	Mashine ya fotokopi	14,688,694
4	H/Jiji Dodoma	Samani na mashine ya fotokopi	15544000
5	H/W Itigi	Samani	19,580,400
6	H/Mji Kahama	Samani na mashine ya kufulia	9,142,753
7	H/W Kibondo	Samani, kompyuta, na vifaa vya TEHAMA	91,720,000
8	H/M Kigamboni	Samani, kompyuta, na vifaa vya hospitali	2,259,869,488
9	H/M Kigoma Ujiji	Kompyuta mpakato, meza, viti, na kabati	34,322,140.00

Na	Halmashauri	Mali iliyonunuliwa	Kiasi (Sh.)
10	H/W Mafia	Kompyuta mpakato, samani, na vifaa vya maji	31,798,700.00
11	H/W Maswa	Kompyuta na mashine ya fotokopi	24,000,000
12	H/W Meru	Kompyuta mpakato na samani	1,343,228
13	H/W Mkuranga	Samani, kompyuta na vifaa vya hospitali	18,290,000
14	H/W Monduli	Meza, viti, makabati, na mabenchi	4,000,000
15	H/W Rombo	Kompyuta mpakato	12,126,000
16	H/W Simanjiro	Madawati	34,000,000
17	H/M Singida	Mashine ya fotokopi	13,176,000
18	H/W Ushetu	Kompyuta	14,800,000
Jumla			**2,805,639,190**

12.7 Kutokuwepo kwa Kumbukumbu za Matengenezo, Ukarabati na Marekebisho ya Magari, Mitambo na Vifaa vya Halmashauri Vyenye Thamani ya Sh. 280,872,608

Kanuni ya 137(4a) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inamtaka ofisa usafirishaji au ofisa mwingine yeyote aliyeteuliwa kutunza taarifa ya matengenezo, ukarabati, na marekebisho kwa kila gari, mitambo na vifaa na taarifa hiyo ipelekwe kwa wizara inayohusika na masuala ya umeme, mitambo na uhandisi wa mitambo na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

Kinyume na kanuni tajwa hapo juu, kumbukumbu za matengenezo na ukarabati wa magari, pikipiki, mitambo na vifaa vingine haikutunzwa na halmashauri 17. Gharama za matengenezo na ukarabati wa mali hizo inafikia kiasi cha Sh. 280,872,608. Tathmini na ufuatiliaji wa matengenezo na ukarabati wa magari na mitambo inaweza isifanyike kwa urahisi na hivyo halmashauri zinaweza kuwa zimetumia gharama kubwa za matengenezo ambayo hayaendani na ufanisi wa magari, pikipiki, na mitambo hiyo.

Jedwali Na. 12-11: Kutokuandaliwa kwa Rejesta ya Matengenezo

Na	Halmashauri	Maelezo	Kiasi (Sh.)
1	H/Jiji Arusha	Ukarabati na matengenezo ya magari ambayo hayajaingizwa kwenye rejesta ya matengenezo	74,691,600
2	H/W Chalinze	Rejesta ya matengenezo ya magari, mitambo na vifaa haijandaliwa na kutunzwa na halmashauri	-

Na	Halmashauri	Maelezo	Kiasi (Sh.)
3	H/Jiji Dodoma	Rejesta ya matengenezo ya magari, mitambo na vifaa kutohuishwa kwa wakati	-
4	H/W Hanang'	Vipuri vya magari kutoingizwa kwenye rejesta ya matengenezo	5,522,858
5	H/W Handeni	Udhibiti mbovu wa vipuri vya magari, mitambo na vifaa vingine vilivyobadilishwa	10,459,000
6	H/W Iramba	Vipuri vya magari kutoingizwa kwenye rejesta ya matengenezo	2,945,405
7	H/W Itigi	Ukarabati na matengenezo ya magari ambayo hayajaingizwa kwenye rejesta ya matengenezo	6,031,293
8	H/W Karatu	Vipuri vya magari kutoingizwa kwenye rejesta ya matengenezo	26,000,431
9	H/W Kibondo	Ukarabati na matengenezo ya magari ambayo hayaingizwa kwenye rejesta ya matengenezo	29,623,000
10	H/W Longido	Ukarabati na matengenezo ya magari ambayo hayajaingizwa kwenye rejesta ya matengenezo	14,834,047
11	H/W Ludewa	Rejesta ya matengenezo ya magari, mitambo na vifaa haijandaliwa na kutunzwa na halmashauri	-
12	H/W Mafia	Ukarabati na matengenezo ya magari ambayo hayajaingizwa kwenye rejesta ya matengenezo	8,663,000
13	H/W Monduli	Rejesta ya matengenezo ya magari, mitambo na vifaa haijandaliwa na kutunzwa na halmashauri	-
14	H/W Mwanga	Rejesta ya matengenezo ya magari, mitambo na vifaa haijandaliwa na kutunzwa na halmashauri	-
15	H/W Nzega	Ukarabati na matengenezo ya magari ambayo hayajaingizwa kwenye rejesta ya matengenezo	12,712,165
16	H/W Singida	Utunzaji usio sahihi wa mafaili ya magari	-
17	H/W Sumbawanga	Rejesta ya matengenezo ya magari, mitambo na vifaa haijandaliwa na kutunzwa na halmashauri	89,389,809
Jumla			**280,872,608**

Ninazitaka menejimenti ya halmashauri husika kuandaa na kutunza kumbukumbu za matengenezo, ukarabati na marekebisho ya magari,

pikipiki, mitambo na vifaa vingine vya halmashauri ili kurahisisha ufuatiliaji wa mali zilizoharibika.

12.8 Mali za Kudumu Zenye Thamani ya Sh. 1,923,440,279 Zilizonunuliwa Lakini Hazitumiki

Wakati wa ukaguzi, nimebaini halmashauri 10 zilifanya manunuzi ya mali za kudumu zenye thamani ya Sh. 1,923,440,279 lakini hazikuwa zinatumika kutokana na sababu mbalimbali kama vile kutokuwepo kwa vyumba vya kutosha vya kuhifadhia baadhi ya mali, kukosekana kwa umeme, na kutokuwepo kwa mafundi wa kuendesha mali hizo na hivyo thamani ya fedha kutopatikana.

Jedwali Na. 12-12: Mali Ambazo Hazitumiki

Na	Halmashauri	Mali iliyonunuliwa	Kiasi (Sh.)
1	H/Jiji Arusha	Mashine ye fotokopi na mashine ya kukata plastiki	128,884,839
2	H/W Bariadi	Jengo	1,232,000,000
3	H/M Ilemela	Mashine ya kufulia na nondo	46,796,170
4	H/Mji Kahama	Vifaa vya hospitali	240,705,170
5	H/W Kishapu	Mashine ya kufulia	17,890,000
6	H/Mji Mafinga	Vifaa vya hospitali	47,617,500
7	H/W Mbogwe	Vifaa vya hospitali	23,844,200
8	H/Jiji Mwanza	Mashine ya kufulia	17,890,000
9	H/Jiji Tanga	Mashine ya Matofali	130,000,000
10	H/W Ukerewe	Kompyuta	37,812,400
Jumla			**1,923,440,279**

Menejimenti za halmashauri husika zinahimizwa kuhakikisha kuwa manunuzi yote yanatokana na mpango wa manunuzi wa mwaka. Pia, mpango wa manunuzi uandaliwe kuendana na mahitaji ya halmashauri kwa wakati husika. Vilevile, mali za kudumu zilizonunuliwa lakini hazitumiki zinapaswa kuanza kutumika haraka ili kulinda thamani na ubora wake.

SURA YA 13

MATOKEO YA UKAGUZI MAALUM

13.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa hoja muhimu zilizoko kwenye ripoti za kaguzi maalum kuanzia mwaka wa fedha 2011/12 hadi kufikia 2019/20. Ukaguzi huu ulifanyika katika kipindi cha mwaka fedha unaoishia 2019/20.

Ukaguzi maalumu ni ukaguzi wa kina unaofanyika eneo maalumu la shughuli za taasisi inayokaguliwa ili kukidhi matakwa ya hadidu za rejea katika kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

Kifungu Na. 29 cha Sheria ya ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na kanuni ya 79 (1) ya Sheria ya ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inampa mamlaka CAG kufanya ukaguzi maalum juu ya ombi lililolotwa kwa maandishi kutoka kwa Afisa Masuuuli, au mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara inayojitegemea, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na chombo kingine chochote. Mawanda ya ukaguzi maalum hufanyika kwa mujibu wa kanuni ya 79 ya Kanuni ya Ukaguzi wa Umma na huamuliwa na mtu au taasisi inayoomba ukaguzi huo. Hata hivyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kurekebisha mawanda akiona ni lazima na sahihi kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 80 (2) ya Kanuni ya ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009.

Kwa kuongezea, kwa mujibu wa kanuni ya 78 ya kanuni za ukaguzi wa umma, CAG anaweza kuanzisha uhitaji wa ukaguzi maalum wa akaunti ya mamlaka yoyote ya umma au taasisi yoyote, Wizara, Idara inayojitegemea, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na chombo chochote kingine.

Kwa Muktadha huo, Sura hii imejumuisha matokeo ya kaguzi maalum sabini na mbili (72) zilizofanyika katika Mamlaka sitini na nane (68) za Serikali za mitaa zilizoombwa na wadau mbalimbali pamoja na zilizofanyika na kutokana na kuanzishwa na utashi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Matokeo ya kina ya kaguzi hizi yanapatikana katika taarifa mahususi za kila kaguzi. Kaguzi hizi maalumu zimeanishwa kama ifuatavyo:

(i) Kaguzi maalumu zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa maombi ya TAKUKURU

Kaguzi hizi maalumu zilifanyika katika Mamlaka 5 za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia matakwa la Kifungu cha 29(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 na Kanuni ya 79(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009. Ombi la kufanya kaguzi hizo liliwasilishwa kwangu na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa muhtasari ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 13-1** hapa chini:

Jedwali Na. 13-1: Kaguzi Maalumu Zilizofanyika Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa Maombi ya TAKUKURU

Na.	Jina la Halmashauri	Mwaka wa Fedha uliokaguliwa
1	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	2011/12 hadi 2018/19
2	Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda	2009/10 hadi 2018/19
3	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe	2017/18 hadi 2018/19
4	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	2017/18 hadi 2018/19
5	Halmashauri ya Mji Kibaha	2017/18 hadi 2018/19

(ii) Kaguzi maalumu zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa maombi ya LAAC

Kaguzi hizi maalumu zilifanyika katika Mamlaka 3 za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 29(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 na Kanuni ya 79(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009. Ombi la kufanya kaguzi hizo liliwasilishwa kwangu na Kamati ya Bunge ya Hesabu kwa Serikali za Mitaa (LAAC). Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa muhtasari ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 13-2** hapa chini:

Jedwali Na. 13-2: Kaguzi Maalumu Zilizofanyika Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa Maombi ya LAAC

Jina la Halmashauri	Mwaka wa Fedha uliokaguliwa
Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba	2015/2016 hadi 2018/2019
Halmashauri ya wilaya ya Nkasi	2016/2017 hadi 2018/2019
Halmashauri ya Manispaa ya Songea	2018/2019

(iii) Kaguzi maalumu zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa maelekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kaguzi hizi maalumu zilifanyika katika Mamlaka 64 za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Namba 11 ya mwaka 2008 na Kanuni ya 78 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 ambazo zinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wowote kadri atakavyoona inafaa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa muhtasari ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.13-3** hapa chini:

Jedwali Na. 13-3: Kaguzi maalumu zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa maelekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Na.	Jina la Halmashauri	Mwaka wa Fedha uliokaguliwa
1	H/Jiji Arusha	2017/18 hadi 2019/20
2	H/W Karatu	2017/18 hadi 2019/20
3	H/W Meru	2017/18 hadi 2019/20
4	H/W Bagamoyo	2017/18 hadi 2019/20
5	H/Mji Kibaha	2017/18 hadi 2019/20
6	H/Jiji Dar es Salaam	2017/18 hadi 2019/20
7	H/M Ilala	2017/18 hadi 2019/20
8	H/M Kinondoni	2017/18 hadi 2019/20
9	H/M Temeke	2017/18 hadi 2019/20
10	H/W Chamwino	2017/18 hadi 2019/20
11	H/W Chemba	2017/18 hadi 2019/20
12	H/Jiji Dodoma	2017/18 hadi 2018/19
13	H/W Kongwa	2017/18 hadi 2019/20
14	H/Mji Geita	2017/18 hadi 2019/20
15	H/W Nyang'wale	2017/18
16	H/M Iringa	2017/18 hadi 2019/20
17	H/W Kilolo	2017/18 hadi 2019/20
18	H/W Bukoba	2017/18 hadi 2019/20
19	H/W Karagwe	2017/18 hadi 2019/20
20	H/M Mpanda	2017/18 hadi 2019/20
21	H/W Buhigwe	2017/18 hadi 2019/20
22	H/W Kasulu	2017/18 hadi 2019/20
23	H/W Kibondo	2017/18 hadi 2019/20
24	H/W Uvinza	2016/17 hadi 30/04/ 2020
25	H/M Moshi	2017/18 hadi 2019/20
26	H/W Same	2017/18 hadi 2019/20

Na.	Jina la Halmashauri	Mwaka wa Fedha uliokaguliwa
27	H/W Siha	2017/18 hadi 2019/20
28	H/W Kilwa	2017/18 hadi 2019/20
29	H/M Lindi	2017/18 hadi 2019/20
30	H/W Babati	2017/18 hadi 2019/20
31	H/W Kiteto	2017/18 hadi 2019/20
32	H/W Mbulu	2017/18 hadi 2019/20
33	H/M Musoma	2017/18 hadi 2019/20
34	H/W Rorya	2017/18 hadi 2019/20
35	H/W Busokelo	2017/18 hadi 2019/20
36	H/W Rungwe	2017/18 hadi 2019/20
37	H/W Kilosa	2017/18 hadi 2019/20
38	H/W Morogoro	2017/18 hadi 2019/20
39	H/M Morogoro	2017/18 hadi 2019/20
40	H/W Masasi	2017/18 hadi 2019/20
41	H/W Magu	2017/18 hadi 2019/20
42	H/Jiji Mwanza	2017/18 hadi 2019/20
43	H/Mji Makambako	2017/18 hadi 2018/19
44	H/W Makete	2017/18 hadi 2019/20
45	H/W Njombe	2017/18 hadi 2019/20
46	H/W Sumbawanga	2017/18 hadi 2019/20
47	H/M Sumbawanga	2017/18 hadi 2019/20
48	H/W Nyasa	2017/18 hadi 2019/20
49	H/M Songea	2017/18 hadi 2019/20
50	H/Mji Kahama	2017/18 hadi 2019/20
51	H/M Shinyanga	2017/18 hadi 2019/20
52	H/W Bariadi	2017/18 hadi 2019/20
53	H/W Itilima	2017/18 hadi 2019/20
54	H/W Itigi	2017/18 hadi 2019/20
55	H/W Mkalama	2017/18 hadi 2019/20
56	H/M Singida	2017/18 hadi 2019/20
57	H/W Mbozi	2017/18 hadi 2019/20
58	H/W Momba	2017/18 hadi 2018/19
59	H/Mji Nzega	2017/18 hadi 2019/20
60	H/W Sikonge	2017/18 hadi 2019/20
61	H/MTabora	2017/18 hadi 2019/20
62	H/Mji Korogwe	2017/18 hadi 2019/20
63	H/W Mkinga	2017/18 hadi 2019/20
64	H/Jiji Tanga	2017/18 hadi 2019/20

13.1 Muhutasari wa Matokeo ya Kaguzi Maalumu

Masuala ya msingi yaliyojitokeza na kupewa umuhimu mkubwa katika taarifa za kaguzi maalumu nilizofanya kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, yameelezewa kwa muhutasari kama ifuatavyo:

13.2 Kaguzi Maalumu Zilizofanyika Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa Maombi ya LAAC

Nilifanya kaguzi maalumu 3 kama ilivyokuwa imeombwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na kubaini mambo muhimu yafuatayo:

HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA

13.2.1 Halmashauri Kupewa Stakabadhi za Kugushi kwa Malipo ya Sh. 87,090,035

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ililipa Sh. 87,090,035 kwa mkandarasi, ikiwa ni gharama ya ujenzi wa miundombinu katika shule za sekondari za Rwazi na Rutunga kwa ufadhili wa SEDP. Nilifanya jitihada za kuwasiliana na ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Ili kuhikiki uhalali wa risiti alizotoa mkandarasi. Ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ilinipa taarifa kuwa sio kwamba tu risiti alizozileta mkandarasi ni za kughushi kwa kuwa hazipo kwenye mifumo yao bali pia mkandarasi huyo aliomba na kupatiwa mashine yenye namba ya utambulisho 03TZ842038279 tarehe 4/1/2019 Kutokana na uthibitisho huo, stakabadhi zilizowasilishwa zilighushiwa na hivyo zimesababisha hasara ya Sh. 13,284,951 inayohusiana na Kodi ya Ongezeko la Thamani.

13.2.2 Hasara ya Sh. 1,406,017,209 Kutokana na Dhamana ya Malipo ya Awali Iliyoghushiwa

Mnamo tarehe 29 Mei, 2018, Halmashauri iliingia mkataba Na. LGA/034/2017-18/W/05 na mkandarasi, kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami. Manamo tarehe 1/6/2018, Mkandarasi aliwasilisha dhamana ya malipo ya awali (Advance Payment guarantee) namba 186522GG4677TZ. Mara baada ya kuipokea, uongozi wa Halmashauri ulitaka kuhakikisha uhalali wa dhamana iliyowasilishwa na mkandarasi kutoka benki na hivyo kupelekea

kuandikwa kwa barua yenye kumbukumbu namba BMC/C/T/14/1/VOL.V.10 ya tarehe 1/06/2018 kwenda kwa uongozi wa Benki, ambapo Ukaguzi wangu ulibaini kuwa benki iliridhia na kuthibitisha uhalali wa dhamana hiyo mnamo tarehe 4/06/2018.

Baada ya mchakato wa juu, Nilibaini kuwa mkandarasi aliomba kulipwa fedha za malipo ya awali kwa kupitia barua yake yenye kumbukumbu namba NLC/HQ/APR/2018/06 ya tarehe 1/06/2018. Baada ya maombi hayo Halmashauri ilimlipa mkandarasi huyo kiasi cha Sh. 1,406,017,209 kupitia hati ya malipo Na. 872002V1800990 ya tarehe 6/6/2018. Hata hivyo, kufuatia mwenendo usioridhisha wa mkandarasi ikiwa ni pamoja na mkandarasi kutokufuata matakwa ya mkataba, Mkurugenzi Mtendaji alivunja rasmi mkataba na mkandarasi kupitia barua BMC/C/T/14/1/VOL./V/13 ya tarehe 2/11/2018. Baada ya mkataba kuvunjwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa aliiandikia barua benki ili kutaka kufidiwa malipo ya awali aliyokuwa amelipwa mkandarasi kwa kuzingatia dhamana iliyowasilishwa. Hata hivyo, nilibaini kuwa, benki ilikana kutoa dhamana hiyo kupitia barua ya tarehe 31/12/2018. Nina wasiwasi juu ya taarifa kutoka taasisi hiyo ya kifedha kukinzana kwa kuwa mwanzoni Ilikubali kutoa dhamana hiyo.

13.2.3 Hasara ya Sh. 855,600,561 Kutokana na Mkataba Kuvunjwa

Ukaguzi wa mkataba kati ya Halmashauri na Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 5 za barabara za lami katika manispaa ya Bukoba ulibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ilipata hasara ya jumla ya kiasi cha Sh. 600,561,855 katika utekelezaji wa mradi huu katika maeneo mawili kama ilivyoelezwa hapa chini;

Mnamo tarehe 29/05/2018 Manispaa ya Bukoba ilitia saini na kuingia mkataba wenye kumbukumbu nambari LGA /034 /2017-18/W/05 na mkandarasi mmoja kwa ajili ya mkataba na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 5 za barabara za lami ya keki (asphalt concrete) wenye thamani ya Sh. 7,030,086,046 (Bila Kodi). Mkataba huu ulivunjwa kwa kupitia barua yenye kumbukumbu namba BMC/C/T/14/1/VOL./V/13 ya tarehe 2/11/2018. Kufuatiwa kuvunjwa kwa mkataba huo, Halmashauri ilifanya makubaliano kupitia mkataba mwingine wenye thamani ya Sh. 7,332,150,000 (Bila Kodi) na kumbukumbu namba

LGA/034/2018-19/W/01 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo lakini kwa kiwango cha matabaka matatu ya lami. Kwa sababu hiyo Halmashauri ilikuwa imepata hasara ya Sh. 302,063,953 ikiwa ni tofauti ya bei kati ya mkataba wa kwanza na wa pili hasa ikizingatiwa kuwa kiwango cha ubora wa lami kilipungua.

Vilevile, ukaguzi wangu ulibaini kuwa, wakati mkataba wa kwanza unavunjwa, Manispaa ya Bukoba ilikuwa tayari imekwisha lipa Sh. 298,497,901 kama malipo ya cheti cha kwanza cha malipo. Malipo haya yaliidhinishwa na Mkandarasi mshauri. Kwakuzingatia kuwa mkandarasi wa pili ana mkataba unaojumuisha kufanya kazi ambazo mkandarasi wa kwanza alikwisha lipwa kuzifanya, ni maoni yangu kuwa malipo ya cheti cha kwanza hayakuwa na tija yoyote kwa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba.

Kwa msingi wa udhaifu uliioonekana, napendekeza OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na mamlaka zingine kama vile ERB na CRB wachukue hatua stahiki dhidi ya mkandarasi kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na masharti ya mkataba. Vilevile, hatua zinazofaa zinapaswa pia kuchukuliwa dhidi ya washiriki wa timu ya tathmini (Due diligence) kutokana na kutofanya kazi yao ipasavyo na hivyo kupelekea Halmashauri kuingia mkataba na mkandarasi asiye na sifa. Kwa kuongezea, OR-TAMISEMI na Bodi ya Wakandarasi kwa kushirikiana na TAKUKURU wanapaswa kuchukua hatua stahiki dhidi ya mkandarasi kwa kuwasilisha taarifa za kughushi zilizosaidia kushinda zabuni ya ujenzi wa barabara wenye thamani ya Sh. 7,030,086,046 katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba

HALMASHAURI YA WILAYA NKASI

13.2.4 Wakandarasi Kutekeleza Miradi ya Sh. 8,019,312,496 bila Kuwa na Usajili wa Kisheria

Uongozi wa Halmashauri uliingia mikataba yenye jumla ya thamani ya Sh. 8,019,312,496 na kampuni ambayo hayana usajili wa kisheria. Miongoni mwa kampuni hizo ni M/s Fally Enterprises Ltd aliyesaini mkataba wa Sh. 7,492,675,575 kwa ajili ya mradi wa maji wa Isale, bila kuwa na usajili wa bodi ya

wakandarasi(CRB), katika mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2018/2019 kwa vipindi tofauti halmashauri ililipa jumla ya Sh. 376,006,229 kwa M/s Ngejito Group Ltd, M/s Isunta Carpenters Group na Rehema Selemani Mwenda, kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Namanyere, ununuzi wa samani za vituo vya afya na ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa hospitali ya Wilaya, bila kuwa na usajili wa BRELA na mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018, Halmashauri katika vipindi tofauti ilifanya malipo ya jumla ya Sh. 150,630,692 kwa wazabuni kwa ajili ya manunuzi ya vifaa mbalimbali, bila ya kuwa na usajili wa mlipa kodi toka TRA (TIN No.)

13.2.5 Kutorejeshwa kwa Fedha ya Malipo ya Awali Kiasi cha Sh. 1,082,080,576 Baada ya Mkandarasi Kufutiwa Usajili

Tarehe 29/06/2017, Halmashauri iliingia mkataba na mkandarasi M/s Fally Enterprises Ltd kwa ajili ya mradi wa maji wa Mpasa na Isale. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Halmashauri ilimlipa mkandarasi huyo jumla ya Sh. 1,498,535,115, ikiwa ni gharama ya malipo ya awali. Ilibainika kuwa mkandarasi alifutiwa usajili wa kandarasi kwa barua yenye kumb. Na. C6/1224/8/2002/17 ya tarehe 19/10/2019. Kati ya kiasi alichopewa kama malipo ya awali Halmashauri ilifanikiwa kurejesha toka kwa mkandarasi Sh. 416,454,539 tu hivyo Halmashauri haikufanikiwa kurejesha kiasi cha Sh. 1,082,080,576.

13.2.6 Mabadiliko ya Nyongeza ya Gharama ya Mikataba Bila Idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali Sh. 10,581,410,942

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2018/19, nilibaini nyongeza yenye jumla ya Sh. 10,581,410,942, kwa wakandarasi waliotekeleza miradi ya maji. Mradi wa maji wa Isale Sh. 2,466,750,721, mradi wa maji wa Mpasa Sh. 1,248,120,164 na mradi wa maji wa Kamwanda Sh. 6,866,540,057. Nyongeza hiyo ilipitishwa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 10/06/2017, na si Katibu Mkuu Wizara ya Fedha (Mlipaji Mkuu wa Serikali), kinyume na matakwa ya kanuni ya 110(4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 (zilizorekebishwa 2016), inayotaka taasisi kupata kibali cha

Mlipaji Mkuu wa Selikali kabla ya kufanya nyongeza ya gharama ya mkataba.

13.2.7 Manunuzi Kutoka Kwenye Biashara za Watumishi wa Halmashauri Sh.182,004,440

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Halmashauri ilifanya manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na vituo vya afya yenye thamani ya Sh. 182,004,440 , kutoka katika biashara mbali mbali zinazomilikiwa na watumishi wa Halmashauri, kinyume na matakwa ya sheria. Miongoni mwao ni Mhasibu Msaidizi na Mtunza Fedha Mkuu (Main Cashier), na mwingine ni Mwenza wa Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Halmashauri, hali hii inaweza kuleta mgongano wa kimaslahi na kupelekea kuwepo na upendeleo katika mchakato wa manunuzi.

13.2.8 Hasara Iliyotokana na Malipo kwa Kazi Ambazo Hazikutekelezwa Sh. 2,360,700,958

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2017/18 nilibaini kiasi cha Sh. 2,360,700,958 kililipwa kwa makandarasi kwa kazi ambazo hazikutekelezwa, kati ya fedha hizo Sh 1,234,155,123, zililipwa kwenye miradi kumi na saba (17) ya Maji, mradi wa Umwagiliaji, mradi wa Bwawa na mradi wa Chumba cha Ubaridi (Cold room) na Sh. 1,126,545,835 zililipwa zaidi ya kiwango cha mkataba katika miradi kumi na saba (17) ya maji na miradi miwili (2) ya barabara, hivyo kusababisha hasara kwa Halmashauri.

13.2.9 Malipo ya Usanifu na Usimamizi wa Miradi ya Maji Kulipwa kwa Kampuni ya Mtumishi wa Wizara ya Maji Sh. 255,825,327

Kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2018/2019, Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 255,825,327 kwenda kwa mkandarasi M/s O&A Co. Ltd, kwa ajili ya usanifu na usimamizi wa Mradi wa maji wa Kabwe, King'ombe, Tambaruka na Kisula, mradi wa maji wa Itete, Mtakuja, Katongolo, Msilihofu, Ntuchi, Kitosi, Nkata, Chala A na C, Mpasa na Mlambo na mradi wa maji wa Mkinga na Matala. Nilibaini mmoja wa wamiliki wa kampuni hiyo ni mtumishi wa Wizara ya maji katika Kitengo cha Opareshen na Matengenezo. Hii inaonesha mgongano wa maslahi na kuminya usawa katika

mchakato wa manunuzi. Hata hivyo mpaka kufikia April, 2020 miradi ya kijiji cha Matala na Kamwanda haikutoa matokeo chanya, kutokana na mapungufu katika usanifu uliofanywa na kampuni hiyo.

Ninapendekeza OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa, kuhakikisha kuwa Halmashauri ya wilaya ya Nkasi inaandaa nyaraka za zabuni ambazo zinakidhi mahitaji yote ya kisheria na kukataa zabuni kutoka kwa wakandarasi na wafanyabiashara ambao hawana vigezo vilivyowekwa. Kwa kuongezea, hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya Maafisa wa Halmashauri waliotajwa katika ripoti maalum za ukaguzi kwa kushindwa kuweka mfumo madhubuti wa ndani ambao ungeweza kuwabaini na kutowashirikisha wafanyabiahsara na wakandarasi ambao hawajatimiza vigezo vyote vya usajili wa kisheria.

OR-TAMISEMI, Wizara ya Maji, pamoja na Taasisi zingine za Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Sekretarieti ya Mkoa zinashauriwa kuanza kuchukua hatua stahiki kadri inavyoonekana inafaa ili kuhakikisha kuwa Halmashauri inarudishiwa fedha ilizozilipa kama malipo ya awali kwa mkandarasi. Kwa kuongezea, hatua zinazofaa zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya Maafisa wa Halmashauri waliotajwa katika ripoti maalum za ukaguzi kwa kukosa kutekeleza majukumu yao yanayotarajiwa katika kudai fidia/ marejesho ya fedha za Malipo ya awali yaliyotolewa kulingana na vifungu vya mkataba.

Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wanyakazi wa Halmashauri na Maafisa wa Wizara waliotajwa katika ripoti maalumu ya ukaguzi kwa kuruhusu na kuidhinisha malipo bila kupata idhini kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Ofisi ya Sekretarieti ya Mkoa zinashauriwa kufanya usimamizi wa karibu wa mikataba na shughuli zingine za ununuzi ili kuhakikisha kwamba Halmashauri linazingatia Sheria na Kanuni za Ununuzi. Kwa kuongezea, hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya Maafisa wa Halmashauri ambao wametajwa katika ripoti

maalum za Ukaguzi kwa kufanya biashara na Halmashauri na kuhatarisha ushindani wa bei na kusababisha mgongano wa kimasilahi.

OR-TAMISEMI, Wizara ya Maji na Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Rukwa wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kuwa wakandarasi husika wa miradi yote iliyoainishwa wanarejesha fedha zote walizolipwa isivyo halali kwa shughuli ambazo hazikutekelezwa. Vilevile, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya Maafisa wa Halmashauri ambao wametajwa katika ripoti maalum za Ukaguzi wa kuidhinisha na kulipa Wakandarasi kwa kazi ambayo haikutekelezwa.

OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Maji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya mfanyakazi wa Wizara ya Maji ambaye alifanya kazi kama Mshauri wa mradi wakati pia alikuwa akitekeleza jukumu la usimamizi chini ya Kitengo cha Uendeshaji (Operations) na Matengenezo katika Wizara kwani hii inaleta na mgongano wa kimaslahi

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

13.2.10 Mapato toka Vyanzo Mbalimbali vya Ndani Yasiyowasilishwa Benki Sh. 229,251,495

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/2020, makusanyo ya jumla ya Sh 229,251,495 toka vyanzo mbalimbali vya ndani, yalibainika kutowasilishwa benki kutokana na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani. Makusanyo haya ya mapato yanajumuisha mapato yaliyokusanywa na kukatiwa stakabadhi halali kwa njia ya mashine za POS Sh. 164,170,084; mapato yaliyokusanywa na kukatiwa stakabadhi za kughushi kwa njia ya POS Sh. 27,952,057 na mapato yaliyokusanywa na kukatiwa stakabadhi zenye namba zinazofanana zilizotolewa kwa njia ya POS Sh. 37,129,354

13.2.11 Kuondolewa kwa Wazabuni Wenye Bei za Chini Bila Sababu za Msingi na Kusababisha Hasara ya Sh. 2,143,715,995.

Ukaguzi ulibaini Kamati za tathmini kwa mikataba Na. LGA/103/2017/2018W/43 - Ujenzi wa Stendi Mpya ya Mabasi Kata

ya Tanga na Na. LGA/103/2017/2018W/54 wa Ujenzi wa Barabara za Manispaa ya Songea, uliwaondoa wazabuni wenye bei za chini katika hatua za awali (Preliminary Stages) kwa kigezo cha kutowasilisha nyaraka za uthibitisho wa mlipa kodi (Tax clearance) kwa Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa ajili ya uhakiki wa nyaraka hizo. Menejimenti ya Halmashauri ilishindwa kuwasilisha nyaraka za zabuni zilizowasilishwa na wazabuni hao walioondolewa kwenye mchakato na hivyo haikuthibitisha uhalali wa wakandarasi hao kuwaondoa.

Aidha, mapitio ya taarifa ya ufunguzi wa zabuni ya Mkataba Na. LGA/103/2014/2015/W/02 yalibaini kuwa, Mzabuni M/s Lukolo Company Ltd, alipewa kandarasi ya ujenzi wa barabara za lami kwa Sh.14,320,586,464 bila ya kuwasilisha nakala ya hati ya uthibitisho wa mlipa kodi iliyoidhinishwa na Mamlaka ya Mapato (TRA), ambayo ilikuwa ni Kigezo Stahiki (Eligibility Criteria) cha kumuwezesha mzabuni kushiriki kwenye mchakato wa manunuzi kama ilivyotumika katika kuwaondoa kandarasi wengine katika Kandarasi za ujenzi wa kituo cha mabasi na ujenzi wa barabara. Kuondolewa kwa wazabuni hao waliokuwa na bei za chini ya Sh.15,007,703,160 katika hatua za awali , ukilinganisha na bei kwenye mkataba ya Sh.17,149,419,155, kumesababisha Serikali kupoteza Sh. 2,143,715,995.

13.2.12 Kutowasilishwa kwa Nyaraka za Zabuni na Taarifa za Tathmini ya Miradi yenye Thamani ya Sh. 39,501,461,526

Menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea, ilishindwa kuwasilisha ripoti za tathmini na zabuni zilizowasilishwa na wazabuni mbalimbali, kwa miradi 12 ya ujenzi na usimamizi yenye thamani ya Sh. 39,501,461,526, kwa ajili ya ukaguzi. Hivyo kumnyima Madhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kushindwa kutimiza majukumu yake.

Ninapendekeza OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma kuchukua hatua madhubuti kushughulikia mifumo ya udhibiti wa ndani juu ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuziba mianya yote inayoweza kupelekea kupotea kwa mapato ya ndani.

Ninapendekeza kuwa Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa Ruvuma aisimamie Halmashauri ya Manispaa ya Songea katika

michakato ya ununuzi ili tathmini za zabuni zifanyike kulingana na vigezo vilivyowekwa katika kabrasha za zabuni ambazo zinakidhi mahitaji ya kisheria ili kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma na pia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mradi.

Pia, hatua stahiki zichukuliwe na Ofisi ya Katibu Tawala mkoa wa Ruvuma pamoja na OR-TAMISEMI dhidi ya wahusika wote ambao wameshindwa kuhifadhi na kuwasilisha taarifa mbalimbali kwa ajili ya Ukaguzi kama ilivyoelezwa hapo juu.

13.3 Kaguzi Maalumu zilizofanywa kwa Maelekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nilifanya kaguzi maalumu 64 katika mamlaka za serikali za mitaa, kwa mujibu wa mamlaka niliyopewa katika Kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na Kanuni ya 78 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009. Masuala ya msingi yaliyojitokeza na kupewa umuhimu mkubwa katika taarifa za kaguzi hizi yamegawanywa katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo:

(i) Matokeo ya kaguzi za miradi ya maji
(ii) Hoja zenye mwelekeo unaofanana katika Halmashauri nyingi zilizokaguliwa
(iii) Hoja zenye mahudhui tofauti kwa kila Halmashauri zilizokaguliwa

13.3.1 MIRADI YA MAJI

13.3.1.1 Fedha za Miradi ya Maji kiasi cha Sh. 2,216,645,340 Zilizotumika kwa Matumizi Mengine

Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (Kama zilivyorekebishwa mwaka 2004), inamtaka Afisa anayeidhinisha fedha kutoka katika akaunti ya amana kujiridhisha pasipo shaka kuwa anayeomba fedha hizo ni yule aliyezihifadhi katika akaunti hiyo na si vinginevyo.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa Halmashauri 14 zilikata kiasi cha Sh. 2,216,645,340 kutoka katika malipo ya wakandarasi kama

fedha za matizamio na kuzitunza katika akaunti ya amana. Hata hivyo, baadaye fedha hizo zilitumika kwa matumizi mengineyo yasiyohusiana na ujenzi wa miradi ya maji. Hii inamaanisha kuwa fedha za matazamio zilitumika kwa matumizi mengine katika Halmashuri kama zinavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 13-4** hapa chini, na hazikuwa zimerejeshwa mpaka wakati ukaguzi huu unakamilika

Jedwali Na. 13-4: Matumizi Fedha za Miradi ya Maji Kinyume na Malengo Yaliyokusudiwa

Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Maelezo
H/W Rorya	146,932,728	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Meru	126,520,954	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Siha	40,998,021	Fedha za Usimamizi wa miradi hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Kilosa	193,051,360	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Morogoro	325,329,093	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/M Singida	265,766,172	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Kibondo	22,000,000	Fedha za mradi wa maji Mgoboka zimetumika kulipa gharama za umeme zilizotakiwa kulipwa na Mamlaka ya Maji Kibondo Mjini
H/W Kasulu	195,382,273	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Kongwa	220,151,459	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Mbulu	170,028,525	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Kiteto	76,282,058	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Itilima	201,252,801	Matumizi ya fedha za matazamio katika Akaunti ya Amana
H/W Sumbawanga	164,091,492	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
H/W Njombe	68,858,405	Fedha za matazamio hazikuhamishwa kwenda RUWASA
Jumla	**2,216,645,340**	

Ninapendekeza hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya Watendaji wa Halmashauri kama walivyotajwa kwenye ripoti za ukaguzi maalumu kwa kushindwa kusimamia fedha za Serikali na kupelekea matumizi mabaya ya fedha. Aidha, Halmashauri husika wahakikishe kiasi hicho kinarejeshwa nakupelekwa RUWASA.

13.3.1.2 Ujenzi wa Miradi ya Maji Yenye Thamani ya Sh. 4,701,208,798 Isiyofanya Kazi wala Kutoa Huduma kwa Jamii

Kanuni ya 239(8) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 inazitaka taasisi zinazofanya manunuzi kutotangaza zabuni kwa ajili ya kazi mpaka michoro na uainisho wa mradi ukamilike na makadirio thabiti ya gharama yaandaliwe. Kifungu cha 4.2.2 (i) cha Mwongozo wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Awamu ya Pili (Water Sector Development Programme, Phase II) wa Disemba, 2016, kinahitaji uhakiki wa ubunifu na idhini ya Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa Maji na Wizara ya Maji ipatikane kabla ya utekelezaji wa mradi.

Nimebaini miradi yenye thamani ya Sh. 4,709,208,798 katika Halmashauri 11 isiyofanya kazi kutokana na miradi hiyo kutotoa huduma ya maji, miundombinu ya mabomba kutelekezwa, kutoendelezwa kwa miradi baada ya mikataba kuvunjwa na uharibifu utokanao na majanga ya asili, kama ilivyoelezewa katika **Kiambatisho Na. 13-1**.

Kwa maoni yangu, kutofanya upembuzi yakinifu na usanifu duni wa miradi ya maji kulipelekea kutobaini mapema vyanzo vya maji vilivyolengwa kutokuwa na maji ya kutosha, hivyo kupelekea miundombinu ya maji isiyofanya kazi, na kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kwa jamii na hivyo upotevu wa fedha za Umma.

Ninapendekeza hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watendaji,wakandarasi na washauri waelekezi waliohusika. Aidha Wizara ya Maji, na menejimenti ya RUWASA husika waandae mpango mkakati wa kuhakikisha jamii iliyolengwa kwenye miradi hii inapata huduma ya maji kama ilivyokusudiwa.

13.3.1.3 Kuchelewa Kutekeleza na Kukamilisha Miradi ya Maji yenye Thamani ya Sh. 32,486,341,363

Kifungu cha 20.1 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba (GCC) ya Hati ya kawaida ya utoaji zabuni (STD, 2018) kinataka Wakandarasi kuanza utekelezaji wa kazi kwa wakati na kufanya majukumu hayo kulingana na programu zilizowasilishwa, kuhuishwa na

kupitishwa na msimamizi wa mradi na kukamilisha kazi hizo kwa tarehe iliyokusudiwa.

Nimebaini matukio 42 ambapo ukamilishwaji wa miradi yenye thamani ya Sh 32,486,341,363 umecheleweshwa, kinyume na vifungu vya mikataba ambavyo vinahitaji miradi kuanza na kukamilika kwa wakati uliowekwa katika mikataba husika. Maelezo zaidi yanaonekana katika **Kiambatisho Na. 13-2**.

Kwa maoni yangu, ucheleweshaji wa malipo, utekelezaji wa miradi kwa kasi ndogo, usanifu duni wa miradi na kutunuku zabuni kwa wakandarasi wasio na vigezo stahiki imezuia jamii husika kunufaika na miradi hiyo. Hii pia imeziweka Halmashauri kwenye hatari ya kuongezeka kwa gharama za miradi kunakoweza kusababishwa na mabadiliko ya bei.

Ninapendekeza hatua stahiki kuchukuliwa kwa watendaji, wakandarasi na washauri waelekezi waliotajwa kusababisha ucheleweshaji katika taarifa maalumu. Aidha, wasimamizi wa Halmashauri husika wanapaswa kutoza fidia ya uchelewashaji wa miradi hiyo kutoka kwa Wakandarasi.

13.3.1.4 Wakandarasi Kutolipwa Madai Yao kwa Muda Mrefu Kiasi cha Sh. 4,055,776,641 Yaliyopelekea Kuondoka Eneo la Mradi na Kuchelewesha Utekelezaji wa Miradi

Kanuni ya 44(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 inaeleza kuwa, kwa madhumuni ya kusaidia na kukuza Makampuni ya ndani na kuyawezesha kutimiza majukumu yao ya kandarasi, taasisi zinazofanya manunuzi zihakikishe malipo kwa Wazabuni yanafanyika kwa wakati.

Aidha, Kifungu cha 51.1 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba (GCC) ya Hati ya kawaida ya utoaji zabuni (STD, 2018), kinamtaka mwajiri awalipe Wakandarasi kiasi kilichothibitishwa na wasimamizi wa miradi hiyo, ndani ya siku 28 tokea tarehe ya kila cheti. Malipo yatakayochelewa yatasababisha riba katika malipo yanayofuata, kwa kiwango cha riba cha mikopo ya kibiashara kilichopo kwa wakati huo.

Nimebaini Halmashauri 11 zimeshindwa kutekeleza majukumu yao ya kuwalipa wakandarasi kwa muda unaotakiwa, kutokana na kuchelewa kuletewa fedha kutoka Wizara ya Maji na hivyo

kusababisha kuvunjika kwa mikataba, ikiwa ni pamoja na kucheleweshwa kukamilika miradi hiyo, kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 13-3**

Kucheleweshwa kwa malipo kumesabisha kuchelewa kukamilika kwa miradi, hivyo kuwanyima walengwa kupata huduma tarajiwa kwa muda muafaka na kusababisha ongezeko la gharama. Pia kumepelekea kusimama kwa Wakandarasi kutekeleza Miradi na hata wengine kuamua kuondoka katika eneo la mradi, bila taarifa ya maandishi kwa Mameneja wa Miradi.

Ninapendekeza kwa Mamlaka za serikali husika, Wizara ya Maji na RUWASA kuchukuwa hatua za haraka za kulipa madeni yote ya wakandarasi kwa muda muafaka ili kuinusuru miradi yote ya maji

13.3.1.5 Kujumuishwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) Kwenye Miradi Yenye Msamaha wa Kodi Sh. 3,026,021,318

Waraka Na. 6 wenye kumb. Na. CLA 321/369/02 wa tarehe 22 Januari, 2018 uliotolewa na Hazina, unahitaji miradi yote ya wafadhili na inayofadhiliwa na Serikali kusamehewa kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilitoa maagizo kwa njia ya barua yenye Kumb.Na.CCE.383/509/01 ya tarehe 15 Februari 2018, kuwataka watekelezaji wa miradi kuomba msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kabla ya utekelezaji wa miradi ya Serikali.

Nimebaini matukio 22 katika Halmashauri sita, ambapo kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya Sh. 3,026,021,318 ilijumuishwa kwenye mikataba na kiasi kilicholipwa kufikia Agosti 2020 kilikuwa ni Sh. 1,756,099,464.04 katika miradi iliyosamehewa kodi, kama ilivyoorodheshwa kwenye **Kiambatisho Na. 13-4 na 13-5**

Kwa maoni yangu, kujumuisha VAT katika miradi iliyosamehewa kodi kumeongeza gharama za miradi kwa Sh. 3,026,021,318, ambayo ingeweza kugharamia miradi mingine. Aidha, kutofuata miongozo kunawakatisha tamaa Wafadhili kuendelea kutoa ruzuku katika miradi mingine.

Ninapendekeza Afisa Masuuli wachukuliwe hatua stahiki kwa kushindwa kutekeleza mwongozo wa kuomba msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika miradi ya maji. Aidha,

katika siku zijazo, Halmashauri zifuate miongozo kwa kuomba msamaha wa kodi kwa mamlaka husika.

13.3.1.6 Hasara ya Sh. 1,047,439,828 Iliyotokana na Malipo kwa Wakandarasi kwa Kazi Ambazo Hazikufanyika

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inahitaji taasisi zinazofanya manunuzi kuidhinisha malipo kulingana na vipimo na cheti cha malipo, katika vipindi au hatua zilizooneshwa katika mikataba.

Aidha, Kifungu cha 45.2 cha masharti ya jumla ya mkataba (GCC) ya Hati ya kawaida ya utoaji zabuni (STD, 2018), kinataka wakandarasi kulipwa kwa kiasi cha kazi zilizofanywa na kuthibitishwa kwa vipimo kwa kulinganishwa na kazi zilizoko kwenye makadirio ya ujenzi. Kifungu cha 50.4 pia kinahitaji kiasi cha kazi zilizotekelezwa kuwa ni kiasi kilichopo katika makadirio ya ujenzi.

Nilikagua mikataba 12 yenye thamani ya Sh 11,324,164,235 katika Halmashauri sita na kubaini malipo ya Sh 1,047,439,828 kwa wakandarasi kwa kazi ambazo hazikufanyika kama ilivyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 13- 6**

Kwa maoni yangu, Halmashauri hazikuwa makini kupima kazi zilizofanyika kabla ya kufanya malipo na kupelekea ubadhirifu wa fedha za umma.

Ninapendekeza mamlaka husika zichukuwe hatua stahiki kwa watendaji wote wa Halmashauri ambao hawakutekeleza majukumu yao ipasavyo na kusababisha malipo kufanyika. Aidha, Halmashauri husika zirejeshe Sh. 1,047,439,828 kutoka kwa wakandarasi waliolipwa fedha hizi kwa kuwakata kwenye vyeti vya malipo vitakavyolipwa baadae (kwa wale ambao mikataba yao inaendelea) na ambao mikataba yao imekwisha, watafutwe na kiasi hicho kirejeshwe. Pia katika siku zijazo, Halmashauri zihakikishe vipimo vinafanywa na wakandarasi na wahandisi washauri kwa pamoja ili kuepuka upotevu wa fedha za umma kwa kulipa kazi ambazo hazikutekelezwa.

13.3.1.7 Hasara ya Sh. 403,600,000 Kutokana na Gharama Zilizolipwa kwa Ajili ya Dhamana na Bima kwa Wakandarasi Isivyotakiwa

Kanuni ya 185 (2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 inataka kabla ya kuwasilisha nyaraka ya zabuni kwa Bodi kwa ajili ya kupitishwa, kitengo cha manunuzi, kihakikishe kuna orodha yenye mahitaji yote muhimu kwa wazabuni watarajiwa. Kifungu cha 16 cha masharti ya jumla ya hati ya kawaida ya utoaji zabuni (STD, 2018) vinataka bima na dhamana vitolewe na mkandarasi kwa mwajiri.

Nilipitia mikataba 11 katika Halmashauri tano na kubaini nukuu za bei za mikataba (BoQs) zilijumuisha gharama za dhamana za kazi na bima za mitambo zenye thamani ya Sh. 403,900,000, ambazo zilikuwa zimelipwa kwa wakandarasi. Hii ni kinyume na utaratibu, kwani gharama hizo zilipaswa kulipwa na mkandarasi na sio kulipwa na Halmashauri. Mikataba hiyo ni kama ilivyoorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 13-5** hapa chini.

Jedwali Na. 13-5: Mikataba iliyolipiwa gharama za dhamana na Bima

Halmashauri	Mkataba	Kiasi Cha dhamana (Sh.)	Kiasi cha Bima (Sh.)
H/W Same	LGA/049/W/2018/2019/01 LOT II	10,000,000	-
	LGA/049/W/WSDP/2013/2014/11 LOT VII	8,000,000	5,000,000
	LGA/049/W/WSDP/2013/2014/11 LOT IV	1,000,000	2,000,000
	LGA/049/W/2013/2014/02 LOT III	3,000,000	-
	LGA/049/WSDP/2013/2014/11 LOT VI	10,000,000	5,000,000
	LGA/049/W/2017/2018/21	3,000,000	-
	LGA/049/W/WSDP/2013/2014/11 LOT V	4,000,000	-
H/W Rungwe	LGA/071/RDC/2009/10/36	188,800,000	141,600,000
H/W Morogoro	LGA/080/2014/2015/W/WSDP/02/40	5,500,000	5,000,000
H/W Karagwe	LGA/033/2013/14/W/002-LOT 4	4,000,000	3,000,000
H/W Sikonge	LGA/121/2015-2016/W/8	-	5,000,000
	Jumla	**237,300,000**	**166,600,000**

Ninapendekeza Mamlaka husika iwachukulie hatua stahiki watendaji wote walioshiriki kuandaa, kupitisha na kusaini

mikataba hii. Aidha wakandarasi waliolipwa kiasi hicho cha fedha watafutwe na kurejesha fedha hizo. Vilevile katika siku zijazo Halmashauri zihakikishe kwamba, nukuu za bei zinapitiwa ili kuepuka kujumuishwa kwa gharama zisizostahiki kwa Serikali.

13.3.1.8 Mikataba Iliyotunukiwa kwa Wakandarasi Wasio na Vigezo/Sifa Stahiki Yenye Thamani ya Sh. 6,909,932,608

Kanuni ya 202(4)(a) na (5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013, inaitaka kamati ya nyaraka za zabuni bila kupungukiwa au kutokuwa na baadhi ya matakwa) kama vilivyoainishwa na tathmini kufanya uchunguzi wa awali wa zabuni kabla ya tathmini ya kina, ili kubaini iwapo kila zabuni inakidhi vigezo kwa kiasi kikubwa.

Jedwali Na. 1 (Ukomo wa madaraja kwa aina mbalimbali za wakandarasi) la; Sheria ya Usajili wa Wakandarasi ya Mwaka 1997 inaweka sharti la kazi za umma za thamani kuanzia milioni 300 hadi 750 ziainishwe kama daraja la VI wakati kazi za thamani ya Sh. bilioni 1.5 hadi bilioni 3 kuwekwa katika daraja la IV na zaidi na bilioni 5 hadi ukomo ziainishwe kama daraja la kwanza. Sehemu za 21(3) na 6(5) za Sheria hiyo zinataka kila mkandarasi kutoa huduma katika aina ya usajili wake kwa kuzingatia ukomo wa daraja lililowekwa. Mkandarasi yeyote anayefanya kazi zilizo juu ya kikomo cha daraja bila kupata ruhusa toka kwa Bodi, atakuwa anafanya kosa la kuadhibiwa faini ya Sh. milioni moja. Aidha, Kanuni ya 9(10)(b) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013, inataka pande zote za ubia kuwa na sifa ya kushiriki katika manunuzi na pale mkandarasi mmoja atakapokuwa hastahili, ubia wote utatangazwa kuwa haustahili.

Nilikagua zabuni zilizowasilishwa na ripoti za tathmini za zabuni 14 katika Halmashauri tisa na kubaini mikataba ya thamani ya Sh. 6,909,932,608 ilipewa wakandarasi wasiostahili, kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 13-7.**

Kwa maoni yangu, tuzo za mikataba kwa wakandarasi wasiostahili, kumechelewesha kukamilika kwa miradi. Kutowajibika ipasavyo kwa kamati za tathmini, kunaweza kusababisha kutofikiwa kwa thamani ya fedha kwa miradi inayotekelezwa.

Ninapendekeza Mamlaka husika iwachukulie hatua stahiki wajumbe wa timu iliyofanya tathmini ya zabuni na kuwapendekeza wakandarasi wasiokidhi vigezo. Aidha, siku zijazo, Halmashauri ihakikishe mikataba wanapewa wakandarasi waliokidhi vigezo ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa miradi na kupatikana kwa thamani ya fedha ya miradi.

13.3.1.9 Mikataba yenye Thamani ya Sh. 3,236,968,179 Iliyosainiwa na Kutekelezwa na Kampuni za Ubia Zisizosajiliwa

Sehemu ya 22 (4) ya Sheria ya Usajili wa Makandarasi, CAP 235 (marekebisho ya 2015) inasema kuwa, mwajiri anayefanya kazi na kampuni zisizosajiliwa anatenda kosa na ikithibitika atalipa faini isiyozidi 10% ya jumla ya mkataba lakini isiwe chini ya asilimia moja ya jumla ya mkataba au Sh. 5,000,000, kutegemea kiasi chochote kilicho kikubwa au kifungo kwa muda usiopungua miaka mitatu au vyote viwili.

Mapitio ya majalada ya mikataba na nyaraka za zabuni yalibaini kuwa, Halmashauri tatu ziliingia mikataba yenye thamani ya Sh 3,236,968,179 na kampuni zenye ubia ambao haujasajiliwa kama Sheria ya Usajili wa Makandarasi inavyotaka, kama invyoonekana kwenye **Jedwali Na.13-6** hapa chini.

Jedwali Na. 13-6: Mikataba iliyosainiwa na kutekelezwa na kampuni za ubia zisizosajiliwa

Halmashauri	Namba ya Mkataba	Maelezo ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Maelezo
H/W Mkinga	LGA/133/2013-2014/WS/W/05	Ujenzi wa miundombinu ya maji katika kijiji cha Parungu Kasera	955,818,325	Kampuni iliyopewa kandarasi ya M/s Eker Co. Ltd Joint Venture M/s Daman Construction Co. Ltd haijasajiliwa
H/W Kibondo	LGA/041/HQ/WSDP/MKAB/2017-18/03	Ujenzi wa mradi wa maji kijiji cha Mukabuye	1,021,088,581	Hati ya usajili wa ubia ilioyotolewa na CRB iliisha muda wake tarehe 30 Disemba, 2018 hivyo ilihitaji kuhuishwa. Hata hivyo, ubia haukuhuisha usajili huo.

Halmas hauri	Namba ya Mkataba	Maelezo ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Maelezo
H/W Rungwe	LGA/071 /2016/20 17/RDC/ W/10 LOT 03	Mradi wa Maji Masoko (skimu ya Lufumbi na Masoko)	1,260,061,273	Kampuni liyopewa kandarasi SUKWA GENERAL ENTERPRISES CO. LTD JV KIBAHA BUILDING AND CIVIL CONTRACTORS Ltd-hawakuwa na cheti cha usajili wa ubia wao toka Bodi ya wakandarasi na walipewa kazi zilizozidi uwezo wao
	Jumla		**3,236,968,179**	

Kwa maoni yangu, kutoa zabuni kwa Wakandarasi wasiosajiliwa kunaziweka Halmashauri katika hatari ya kupoteza fedha kutokana na uwezekano wa fidia ya Sh. 323,696,818 (Asilimia 10 ya gharama ya mkataba). Aidha, mwenendo huu unaweza kusababisha hasara zaidi, endapo itatokea migogoro ya kisheria itokanayo na Mkandarasi kushindwa kutekeleza mkataba

Ninapendekeza Mamlaka husika kuwachukulia hatua stahiki wajumbe wa bodi za zabuni za Halmashauri husika pamoja na watendaji wote waliohusika kutunuku zabuni kwa kampuni zisizo na ubia uliosajiliwa. Pia Halmashauri katika siku zijazo ziingie mikataba na kampuni za ubia zilizosajiliwa ili kuepuka uwezekano wa kupoteza fedha za Umma na ucheleweshwaji wa huduma tarajiwa kwa jamii.

13.3.1.10 Mikataba Iliyotekelezwa Bila kuwa na Hati za Dhamana ya Utendaji Yenye Thamani ya Sh. Bilioni 29,274,980,546

Kanuni ya 29 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013, inahitaji taasisi zinazofanya manunuzi kutaka dhamana ya utendaji kazi kutoka kwa Wazabuni walioshinda zabuni, ili kuhakikisha mikataba inatekelezwa kwa uaminifu na malipo ya wafanyakazi wote, wasambazaji, mafundi, na Wakandarasi Wasaidizi wa mradi (kama wapo) yanafanyika kwa uaminifu.

Nimepitia majalada ya mikataba na kubaini mikataba yenye thamani ya Sh. 29,274,980,546, ilitekelezwa bila hati za dhamana za utendaji kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.13-8**.

Kwa maoni yangu, kutokuwepo kwa hati za dhamana za utendaji kunaziweka Halmashauri katika hatari ya kupoteza rasilimali zake kwa miradi inayoendelea kama ikitokea Wakandarasi wakashindwa kutekeleza mkataba au kukiuka matakwa ya mkataba.

Ninapendekeza Mamlaka husika kuwachukulia hatua stahiki watendaji wote waliohusika katika usimamizi wa mikataba isiyo na dhamana ya utendaji. Aidha, Halmashauri zihakikishe, Wakandarasi wanaleta na kuhuisha dhamana za utendaji kwa mikataba yote ambayo bado inaendelea. Vilevile, katika siku zijazo Halmashauri zihakikishe mikataba yote inalindwa kwa hati za dhamana kwa kipindi chote cha mkataba ili kuzuia kupoteza rasilimali za Umma.

13.3.1.11 Kutotoza Tozo ya Ucheleweshaji wa Kazi Kiasi cha Sh. 280,664,326

Kanuni ya 112(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013, inahitaji taasisi inayofanya manunuzi kutoza fidia kwa Mzabuni kwa kuacha kupeleka vifaa, kutoa bidhaa au huduma au kuchelewa kufanyakazi. Aidha, Kifungu cha 57.1 cha masharti ya jumla (GCC) cha Hati ya kawaida ya utoaji zabuni (STD, 2018) kinataka tozo ya ucheleweshaji wa kazi iwe kati ya 0.1% na 0.15% ya jumla ya mkataba, ambayo itatozwa kwa siku kwa kazi iliyocholeweshwa.

Uhakiki wa majalada ya mikataba ya maji ulibaini kuwa Halmashauri saba zilishindwa kuwatoza tozo ya fidia kiasi cha Sh. 280,664,326 wakandarasi ambao hawakumaliza kazi kwa wakati, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 13-7** hapa chini:

Jedwali Na. 13-7: Mikataba Ambayo Haikutozwa Fidia ya Ucheleweshaji Mradi

Halmashauri	Namba ya Mkataba	Maelezo ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Kiasi cha Tozo (Sh.)	Muda uliochelewa eweshwa (Siku)
H/Mji Nzega	LGA/170/2017-18/02	Mradi wa Maji katika vijiji vya Nhobola, Kitengwe, Idudumo, Mwanzoli, Iyuki na Igalali	398,530,840	39,853,084	102
H/W Itigi	LGA/117/IDC/2017/2018/HQ/W/01-LOT 1	Mradi wa maji wa Vijiji sita (6) vya Songambele, Mlowa, Majengo, Tambukareli, Zinginali na Itigi mjini	1,640,149,965	82,007,498	50
H/W Buhigwe	LGA/138/HQ/W/2017-2018/01	Shughuli ya ukarabati na ujenzi wa Mfumo wa usambazaji mabomba ya maji katika Kijiji cha Kasumo	306,271,351	30,627,135	67
H/W Kongwa	LGA/022/2017/2018/HQ/W/01/1	Ujenzi wa miundombinu ya maji katika kijiji cha Vihingo	646,680,042	64,668,000	100
H/W Babati	LGA/057/2016-2017/W/02	Ujenzi wa mradi wa maji Ufana-Diffir na Walahu	370,967,780	25,596,776	46
H/Mji Geita	LGA/160/W/RWSSP/2017/2018/W/LOT I	Utafiti wa maji ardhini na uchimbaji wa visima 28 na uwekaji wa pampu za mkono	89,047,500	2,671,425	30
	LGA/160/	Utafiti wa maji ardhini na	199,840,000	5,995,200	30

Halmashauri	Namba ya Mkataba	Maelezo ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Kiasi cha Tozo (Sh.)	Muda uliochelewa eweshwa (Siku)
	W/R WSSP /2017 /2018 /W/L OT II	uchimbaji wa visima 28 na uwekaji wa pampu za mkono			
	LGA/ 160/ W/R WSSP /2017 /2018 /W/L OT III	Utafiti wa maji ardhini na uchimbaji wa visima 28 na uwekaji wa pampu za mkono	197,003,450	5,910,104	30
	LGA/ 160/ W/R WSSP /2017 /2018 /W/L OT IV	Utafiti wa maji ardhini na uchimbaji wa visima 28 na uwekaji wa pampu za mkono	119,132,450	3,570,104	30
H/W Chemba	LGA/ 136/2 016- 2017/ W/22 /6	Kufanya utafiti wa Maji chini ya Ardhi na uchimbaji wa Visima virefu 2 katika Makao Makuu ya Wilaya na Visima virefu 3 katika Vijiji vya Mrijo juu, Itolwa na Igunga	197,650,000	19,765,000	283
	Jumla		4,165,273,336	280,664,326	

Ninapendekeza kwa mamlaka husika kuchukua hatua stahiki kwa watendaji wote walioshiriki kuzisababishia hasara Halmashauri hizo. Aidha, kwa mikataba inayoendelea Halmashauri ihakikishe inatoza kiasi hicho kutoka kwa wakandarasi wa miradi iliyocheleweshwa na kuendelea kuhakikisha kuwa mikataba inatekelezwa kwa mujibu wa masharti ya mikataba.

13.3.1.12 Mabadiliko ya Mikataba Yaliyotekelezwa Bila Kuidhinishwa Yenye Thamani ya Sh. 293,918,655

Kanuni ya 110(5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inahitaji mapendekezo ya marekebisho kama kuongeza au kupunguza kazi ambayo si ya lazima au yanayotoka nje ya mkataba na ambayo hubadilisha mawanda, kiwango au lengo la mkataba husika, yapelekwe kwa bodi ya zabuni kabla maelekezo hayajatolewa kwa mkandarasi. Pia kanuni ya 61(1) za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013, inahitaji marekebisho yoyote ya mkataba ambayo yanaweza kubadilisha vigezo na masharti ya mkataba kutayarishwa na kitengo cha manunuzi kwa kushauriana na idara ya watumiaji, kabla ya kuwasilishwa kwenye bodi ya zabuni kwa ajili ya kuidhinishwa.

Nilipitia majalada ya mikataba katika Halmashauri nne na kubaini mabadiliko ya kiasi cha Sh. 293,918,655, yalifanyika katika mikataba minne ya ujenzi wa miundombinu ya maji, bila kupitishwa na bodi za zabuni, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 13-8** hapa chini.

Jedwali Na. 13-8: Mikataba ya Mabadiliko Yasiyoidhinishwa

Halmashauri	Namba ya Mkataba	Maelezo ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Tofauti (Sh.)	Mapungufu
H/W Siha	LGA/050/2017/2018/W/01 (LOT II)	ujenzi wa mradi wa maji wa LOSAA-KIA (Tenki la Munge)	752,888,512	88,675,500	Mabadiliko ya kazi kwa ujenzi wa mradi wa maji wenye kiasi cha Sh. 88,675,500 hayakuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.
H/W Nyasa	LGA/145/2013-2014/W/22-LOT 7	ujenzi wa mradi wa maji katika vijiji vya Mbamba bay – Ndesule	199,922,575	83,722,500	Kuongeza vituo vitatu vya kuchotea maji yalisababisha ongezeko la kazi zenye thamani ya Sh. 17,605,000 na mabadiliko

Halmashauri	Namba ya Mkataba	Maelezo ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Tofauti (Sh.)	Mapungufu
					ya ongezeko la kazi yenye jumla ya Sh. 66,117,500, lililoandikwa na Mhandisi wa maji bila kupata idhini ya bodi ya zabuni
H/W Mbozi	LGA/073/2016/2017/W/12	ujenzi wa mradi wa maji Itaka	1,674,145,006	88,909,955	Ongezeko la kazi zenye thamani ya Sh. 88,909,955 kwa ajili ya ukarabati wa Tenki la zamani la Itewe, kuweka transfoma na kujenga Tenki la chini la kukusanyia maji (sump-well) bila kuidhinishwa na bodi ya zabuni
H/W Kibondo	LGA/041/HQ/WSDP/IOM/2017-2018/W/04	Ujenzi miundo mbinu ya maji kwa kutumia kisima cha IOM	359,568,272	32,610,700	Mhandisi alitoa maelekezo ya nyongeza za kujenga miundo mbinu ya maji katika mradi wa kutumia Kisima cha IOM Kibondo ya kiasi tajwa ambayo hayakupata idhini ya bodi ya zabuni
	Jumla		2,986,524,365	293,918,655	

Ninapendekeza hatua stahiki zichukuliwe kwa watendaji wote waliofanya mabadiliko yasiyo na ushahidi baada ya kusaini mkataba. Aidha Halmashauri zihakikishe idhini ya baada ya mabadiliko inaombwa kwenye bodi ya zabuni, vilevile kwa siku zijazo Halmashauri zihakikishe mabadiliko ya mikataba yanaidhinishwa na bodi za zabuni.

13.3.1.13 Fedha Zilizotumwa Kutoka Wizara ya Maji na Kutumika Bila Kibali cha Wizara Husika Sh. 236,289,302

Wizara ya Maji iliweka utaratibu wa kutuma fedha za wakandarasi kwenye akaunti za maji za Wilaya, baada ya Halmashauri kujiridhisha na kuthibitisha kazi za mkandarasi na kwa kupitia Ofisi za Mkoa, kuomba fedha hizo Wizarani.

Nilipitia hati za madai za wakandarasi (certificates), hati za malipo pamoja taarifa za benki na kubaini kwamba fedha zilizotumwa kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi kwa kazi zilizofanyika, zilitumwa zaidi kutoka Wizara ya Maji kwa kiasi cha Sh. 236,289,302. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 13-9** hapa chini.

Jedwali Na. 13-9: Fedha Zilizotumwa Kutoka Wizara ya Maji Na Kutumika Bila Kibali cha Wizara Husika

Halmashauri	Tarehe	Jina la Mkandarasi	Kiasi kilichoombwa A (Sh.)	Kiasi Kilichokuja B (Sh.)	Kiasi Kilichozidi (A-B) (Sh.)
H/W Kiteto	20/02/2018	Medes Co. Ltd IPC No 1	134,626,345	158,859,087	24,232,742
		Olsh Co. Ltd IPC No 1	67,314,220	79,430,780	12,116,560
H/W Magu	22/02/2018				199,940,000
				Jumla	236,289,302

Halmashauri ya Wilaya ya Magu ilifanya jitihada ya kuwasiliana na Wizara ya Maji kuomba kibali cha kutumia fedha katika kutekeleza mradi wa maji wa Kabila – Ndagalo, mpaka wakati wa ukaguzi huu maalumu, Halmashauri ilikuwa haijapata majibu kutoka wizara husika, hata hivyo Halmashauri iliamua kuendelea na utekelezaji wa mradi kwa kutumia fedha hizo bila kibali cha Wizara. Pia Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto ilitumia fedha zilizozidi kiasi cha Sh. 36,349,302 katika matumizi mengine, bila kupata kibali kutoka

Wizara ya Maji.

Matumizi ya fedha za miradi zilizozidi bila kupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji, kutaipelekea Halmashauri kutengeneza madeni yasiyo ya lazima pindi ambapo fedha hizo zitaamuliwa kurudishwa wizarani, kwa ajili ya kupangiwa matumizi mingine.

Ninapendekeza hatua stahiki zichukuliwe kwa Watendaji wa Halmashauri waliohusika katika matumizi ya fedha zilizozidi bila kibali kutoka Wizara ya Maji, Aidha Halmashauri husika zifuatilie vibali vya kutumia fedha hizo kutoka Wizarani.

13.3.1.14 Hasara Kutokana na Kuondolewa kwa Wazabuni Wenye Bei za Chini Bila Sababu za Msingi ya Sh. 144,438,434

Kanuni ya 203(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 inataka tathmini za zabuni ziwe sawa na masharti yaliyo katika nyaraka za zabuni na kwa kutumia vigezo vilivyoainishwa bayana katika nyaraka za zabuni.

Mapitio ya ripoti za tathmini kwa zabuni tatu katika Halmashauri mbili yalibaini mikataba kupewa wazabuni wenye bei za juu na kuwatoa wazabuni wenye bei za chini bila kuwepo sababu za msingi, kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 13-9**.

Kwa maoni yangu, kutumia vigezo vya tathmini ambavyo havikujumuishwa katika nyaraka za zabuni, kumesababisha kuondolewa kwa wazabuni waliokuwa na bei za chini na kusababisha hasara ya Sh. 144,438,434

Ninapendekeza mamlaka husika kuchukua hatua stahiki kwa Afisa Masuuli pamoja na wajumbe wa bodi ya zabuni kwa kusababisha hasara hiyo. Aidha, Halmashauri zihakikishe, siku zijazo, tathmini ya zabuni zinafanywa kwa kutumia vigezo vilivyowekwa.

13.3.1.15 Kukosekana kwa Nyaraka Timilifu za Miradi ya Maji Zenye Thamani ya Sh. 9,152,032,514

Kanuni ya (6) na 15 (1) (b-d) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 (kama ilivyoboreshwa mwaka 2016) inahitaji taasisi zinazofanya manunuzi kutunza taarifa za michakato ya manunuzi, ikiwa ni pamoja na mialiko, uteuzi wa zabuni na taratibu za utoaji tuzo, kwa muda usio chini ya miaka mitano tangu tarehe ya kukamilika kwa mkataba.

Aidha, Kifungu cha 8 (2)(c) cha Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa 2009, kinataja kuwa miongoni mwa majukumu ya Mweka Hazina wa Halmashauri ni pamoja na kuhakikisha udhibiti mzuri wa mfumo wa kihasibu na utunzaji wa nyaraka mbalimbali.

Tofauti na matakwa ya sheria zilizotajwa hapo juu, wakati wa ukaguzi nilibaini matumizi ya Sh. 9,152,032,514 kwa ajili ya miradi ya maji 21, ambayo hayakuweza kuthibitika, kwa sababu Halmashauri zilishindwa kuwasilisha nyaraka za matumizi husika.

Mahojiano yaliyofanyika kati ya timu ya ukaguzi na uongozi wa Halmashauri husika yalibaini kuwa, nyaraka hizo hazikuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kwa sababu baadhi ya nyaraka hizo zilikuwa TAKUKURU na nyingine hazikuweza kupatikana kwa ajili ya utunzwaji dhaifu, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 13-10** hapa chini:

Jedwali Na. 13-10: Kukosekana kwa Nyaraka Timilifu za Miradi ya Maji Kwa Ajili ya Ukaguzi

Halmashauri	Jina la Mkandarasi na Namba ya Mkataba	Nyaraka zilizokosekana	Kiasi (Sh.)
H/W Bukoba	LGA 035/W/RWSSP/FY2013/2014 /01(4) Yell Limited	Nyaraka mbalimbali za mchakato wa kumpata mkandarasi zilikuwa TAKUKURU	596,804,000
H/W Rorya	Maginga Business Holding Co. Ltd na National Services Construction Department	Hati za malipo	976,942,815
H/W Mbulu	M/s Jemason Investment Co. Ltd- LGA/061/WKS/2013/2014/WSDP/NC/12,	Nyaraka mbalimbali za mchakato	4,986,894,343

Halmashauri	Jina la Mkandarasi na Namba ya Mkataba	Nyaraka zilizokoseka na	Kiasi (Sh.)
	M/s PNR Services Ltd-LGA/061/2011/2012/WSDP/NC/LOT 1, M/s Dabenco Enterprices Ltd-LGA/061/2011/2012/WSDP/NC/LOT 3, M/s Nyangera Construction-LGA/061/WSDP/NC/01 na M/s UNEE (T) Investment Company Ltd JV Yumbaka Eng. and General Works-LGA/061/WKS/2013/2014/WSDP/14	wa kumpata mkandarasi	
H/W Kasulu	M/s Earth Plan Contractor Company Ltd	Hati za malipo	31,487,338
H/W Sikonge	Ujenzi wa mradi wa chujio la maji katika bwawa la Igumila lililopo kijiji cha Kapumpa Kata ya Kitunda Ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika kijiji cha Usunga Ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika Kijiji cha Msuva Ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika Kijiji cha Utimle. Ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika Kijiji cha Nyahua. Upanuzi wa mradi wa maji wa kijiji cha Ipole kwenda Kijiji cha Kabanga.	Nyaraka zote zinazohusiana na miradi 6 iliyotajwa ya mwaka 2019/20	1,097,724,217
H/W Bagamoyo	M/S Sife General Enterprises Ltd-BDC/2013/2014/WT/03, Coast Belt Construction Co. LTD-BDC/2012/2013/03, Jonenac Construction Co. LTD-BDC/2013/2014/WT/04, M/S Chakwale Company Ltd-LGA/014/2015/2016/QT/W/17 na M/S Sea Shoe Civil Works-LGA/014/2016/2017/QT/W/R/02 M/S Sea Shoe Civil Works-LGA/014/2017/2018/QT/W/R/01	Nyaraka zote za utaratibu wa manunuzi	1,462,179,801
	Jumla		9,152,032,514

Ninapendekeza kwa Mamlaka husika kuchukuwa hatua stahiki kwa watendaji wote waliohusika na kukosekana kwa nyaraka hizo. Aidha, katika siku zijazo, Halmashauri ziwe na mfumo madhubuti wa utunzaji wa nyaraka zote za manunuzi na zile za matumizi ya fedha.

13.3.1.16 Malipo ya awali kwa wakandarasi ambayo hayajarejeshwa Sh. milioni 298,492,924

Kifungu cha 59.1 cha masharti ya jumla ya mkataba (GCC) na 24 ya Masharti maalum ya mkataba(SCC) ya Hati ya Zabuni ya Kawaida, 2018 (Iliyorekebishwa Juni 2019), inahitaji kiasi cha malipo ya awali kupunguzwa hatua kwa hatua kutoka kwenye kiasi kinacholipwa na Mkandarasi katika Cheti cha Malipo ya Muda.

Nilipitia mikataba minne katika Halmashauri nne yenye thamani ya Sh. 3,531,835,932, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji na kubaini kuwa, kiasi cha Sh 298,492,924, ikiwa ni malipo ya awali kwa wakandarasi, hayakurejeshwa baada ya mikataba yao kuvunjika kwa sababu mbalimbali. Orodha ya mikataba na kiasi husika ni kama ilivyoambatishwa kwenye **Jedwali Na. 13-11** hapa chini:

Jedwali Na. 13-11: Malipo ya awali ambayo hayakurejeshwa na wakandarasi

Halmashauri	Mkataba	Kiasi cha Mkataba (Sh)	Kiasi ambacho hakijarejeshwa (Sh)	Maelezo
H/W Rorya	LGA/068/16/W/2012/2013/3	572,387,651	114,134,097	Malipo ya awali ambayo hayakurejeshwa
H/W Magu	LGA/090/W/2012/2013/42 Lot Na. 03	1,379,485,195	45,786,569	Kiasi ambacho Halmashauri imeshindwa kumdai mdhamini wa mkandarasi (Insurer) ikiwa ni kiasi cha malipo ya awali.
H/W Mbulu	LGA/061/2011/12/WSDP/NC/LOT3	1,129,721,448	126,072,257	Malipo ya awali ya mkataba ambayo hayakurejeshwa na Mkandarasi

Halmashauri	Mkataba	Kiasi cha Mkataba (Sh)	Kiasi ambacho hakijarejeshwa (Sh)	Maelezo
				baada ya mkataba kuvunjika.
H/W Kongwa	HWK/KOG/RWSSP/C1/2004 LOT NO. KOGG2	450,241,638	12,500,000	Malipo ya awali ambayo hayakurejeshwa na mkandarasi kupitia cheti cha malipo.
	Jumla	3,531,835,932	298,492,923	

Ninapendekeza kwa Mamlaka husika kuwachukulia hatua stahiki watendaji wote walioisababishia Serikali hasara kwa kushindwa kuwafuatilia wakandarasi hao ili kurejesha fedha za umma. Aidha, mamlaka husika zihakikishe wakandarasi hao wanapatikana na kurejesha kiasi tajwa.

13.3.1.17 Mapungufu Yaliyobainika Wakati wa Kutembelea Miradi ya Maji Yenye Thamani ya Sh. 10,765,918,464

Nilitembelea miradi ya maji iliyotekelezwa na Halmashauri kumi kwa miaka ya fedha kuanzia 2017/18 hadi 2019/20 kwa ajili ya kuona iwapo imetekelezwa na kufanya kazi kulingana na matakwa ya mkataba. Mapungufu yaliyobainika kwa ufupi ni kama yanavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 13-10**

Kwa maoni yangu, kutofanyika kwa usanifu na upembuzi yakinifu, kutofanyika vipimo na majaribio ya vifaa vya ujenzi na kutochukua tahadhari ya maafa asilia, kunaziweka Halmashauri kwenye hatari ya kutumia vifaa visivyo na ubora stahili na kuwa na miradi inayotoa huduma kwa muda mfupi (isiyo endelevu), vyote hivi vinaweza kuathiri utendaji wa miradi na kusababisha upotevu wa fedha za Serikali.

Ninapendekeza hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watendaji wa Halmashauri hizo waliosababisha mapungufu hayo. Vileviele Halmashauri kwa kushirikiana na meneja wa RUWASA kuyafanyia kazi mapungufu yote yaliyobainishwa ili kufanya miradi ya maji idumu kwa muda mrefu. Pia ukaguzi wa mara kwa mara ufanyike ili kuweza kubaini mapungufu mapema kabla hayajaleta madhara makubwa na kusababisha gharama

kubwa za matengenezo.

13.3.1.18 Kazi Zilizolipwa Bila Kufanyiwa Vipimo Zenye Thamani ya Sh. 1,352,102,200

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013, inahitaji taasisi zinazofanya manunuzi kuidhinisha malipo kulingana na vipimo na uthibitisho, katika vipindi au hatua zilizooneshwa katika mikataba.

Mapitio ya hati za malipo na majalada ya mikataba yalibaini Halmashauri mbili kulipa kiasi cha Sh. 1,352,102,200 kwa wakandarasi kwa kazi zilizotekelezwa. Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka za vipimo vya kuhalalisha kiasi cha kazi kilichofanyika, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 13-12** hapo chini.

Jedwali Na. 13-12: Kazi Zilizolipwa Bila Kufanyiwa Vipimo

Halmashauri	Namba ya Mkataba	Maelezo ya Mkataba	Gharama ya Mkataba (Sh.)	Kiasi kilicholipwa (Sh.)
H/W Makete	LGA/028/2016/2017/W/08	Mradi wa Maji wa Magoma - Burongwa	498,821,400	490,265,092
H/W Njombe	LGA/031/2017/2018/HQ/W/01 LOT No. 1	Ujenzi wa mradi wa maji Kidegembye	1,354,308,804	861,837,108
		Jumla	1,853,130,204	1,352,102,200

Ninapendekeza hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watendaji wa Halmashauri hizo waliohusika kuidhinisha na kulipa malipo hayo. Aidha, katika siku zijazo Halmashauri zinapaswa kukagua na kupima kiasi cha kazi zilizotekelezwa kabla ya kuthibitisha malipo ili kuzuia malipo kwa kazi zisizotekelezwa

13.3.1.19 Kodi ya Zuio Ambayo Haikukatwa ya Kiasi cha Sh. 50,222,337

Sehemu ya 83A ya Sheria ya Kodi ya Mapato (ITA), 2004 (na marekebisho ya 2008) na Sehemu ya 24 ya Sheria ya Fedha ya Umma (iliyorekebishwa mwaka 2016) inahitaji kila taasisi kutoza 2% kwa bidhaa na 5% kwa huduma iliyotolewa kwa Serikali, kama

kodi ya zuio kwa huduma iliyotolewa kwa taasisi ya Umma na makato hayo yatumwe kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato na ikiwa malipo yanajumuisha kazi za ujenzi, malipo yatatozwa kwa kufuata uwiano wa 3:2 kwa vifaa na huduma kwa mtiririko huo.

Mapitio ya hati za malipo na mikataba ya miradi ya maji yalibaini kuwa, Halmashuari ya Wilaya ya Mbulu na Sikonge hazikukata kodi ya zuio kiasi cha Sh. 50,222,337 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 13-13** hapa chini.

Jedwali Na. 13-13: Kodi ya Zuio Ambayo Haikukatwa

Halmas hauri	Maelezo ya Mikataba	Kiasi kilichotumika kama msingi wa kodi (Tax-Base) Sh.	Kiasi kilichotakiwa kukatwa (Sh.) (A)	Kiasi kilichokatwa (Sh.) (B)	Kiasi kisichokatwa (Sh.) (A-B)
H/W Mbulu	Malipo ya wazabuni na wakandarasi mbalimbali wa miradi ya maji	80,875,029	4,043,751	-	4,043,751
H/W Sikonge	Mradi wa maji Igumila awamu ya pili	1,397,800,165	69,890,002	23,711,422	46,178,586
	Jumla				**50,222,337**

Ninapendekeza hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watendaji wa Halmashauri hizo zilizohusika na upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, Halmashauri zihakikishe katika siku zijazo, kodi ya zuio inakatwa kulingana na matakwa ya sheria.

13.3.2 Hoja zenye Mwelekeo Unaofanana Katika Halmashauri Nyingi Zilizokaguliwa

13.3.2.1 Mapato Yaliyokusanywa na Mawakala Kupitia Mfumo wa LGRCIS Ambayo Hayakuwasilishwa Benki Sh. 23,879,894,957

Matokeo ya ukaguzi uliofanyika katika Mamlaka 59 za serikali za mitaa yanaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka ya fedha 2017/18

hadi 2019/20, makusanyo ya jumla ya Sh. 23,879,894,957 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani yalibainika kutowasilishwa benki kutokana na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani. Hii ni kinyume na Agizo la 50 (5) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Muhutasari wa mapato yaliyobainika kutowasilishwa benki kwa kila halmashauri ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 13-14** hapa chini:

Jedwali Na. 13-14: Mapato Yaliyokusanywa na Mawakala Kupitia Mfumo wa LGRCIS Ambayo Hayakuwasilishwa Benki

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/M ya Kinondoni	5,983,799,498
2	H/Jiji Dar es Salaam	1,677,018,980
3	H/J la Arusha	1,256,788,700
4	H/W ya Songea	1,011,379,373
5	H/W ya Chemba	769,172,024
6	H/W ya Itilima	714,457,233
7	H/W ya Kilosa	713,695,590
8	H/W ya Kasulu	612,853,913
9	H/W ya Mbozi	603,530,832
10	H/W ya Meru	557,829,134
11	H/M ya Ilala	552,456,653
12	H/W ya Kilwa	512,210,970
13	H/J la Mwanza	496,153,502
14	H/W ya Kongwa	490,603,427
15	H/M ya Temeke	478,520,015
16	H/W ya Makete	476,584,694
17	H/Jiji la Tanga	444,269,885
18	H/W ya Kibondo	430,336,652
19	H/W Morogoro	420,872,288
20	H/W ya Sumbawanga	418,116,333
21	H/M ya Iringa	409,051,598
22	H/Ma ya Shinyanga	406,591,529
23	H/W ya Rungwe	370,279,219
24	H/J la Dodoma	347,781,513
25	H/W ya Momba	338,643,215
26	H/W ya Uvinza	318,728,573
27	H/W ya Siha	288,691,349
28	H/W ya Itigi	283,782,266
29	H/M ya Lindi	271,893,261
30	H/M ya Songea	229,251,495
31	H/W ya Masasi	167,984,487
32	H/M ya Mpanda	155,173,450
33	H/W ya Kilolo	146,542,908
34	H/W ya Chamwino	139,550,670
35	H/M ya Moshi	134,044,850

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
36	H/W ya Kiteto	118,918,000
37	H/W ya Sikonge	115,255,248
38	H/W ya Nyasa	115,028,471
39	H/W ya Bariadi	111,085,799
40	H/W ya Karagwe	109,472,791
41	H/W ya Karatu	80,214,500
42	H/M ya Kahama	78,764,853
43	H/W ya Mbulu	74,726,150
44	H/W ya Buhigwe	74,223,744
45	H/M ya Singida	47,658,041
46	H/M ya Musoma	46,732,360
47	H/M ya Tabora	34,789,687
48	H/W ya Nyang'wale	33,299,341
49	H/W ya Njombe	32,858,050
50	H/W ya Magu	29,552,820
51	H/W ya Korogwe	27,375,492
52	H/M ya Morogoro	24,528,420
53	H/W ya Mkinga	21,462,486
54	H/Mji wa Nzega	19,108,030
55	H/W ya Bukoba	15,182,040
56	H/W ya Same	13,393,755
57	H/W ya Mkalama	11,605,250
58	H/M ya Sumbawanga	9,974,650
59	H/W ya Babati	6,044,900
Jumla		**23,879,894,957**

Kwa maoni yangu, haya ni mapato halisi ya Serikali yaliyochepushwa na kutumiwa kwa matumizi binafsi kwa njia ya ubadhilifu. Nashauri mamlaka husika washirikiane na TAKUKURU kuhakikisha wahusika wanawajibika kurejesha fedha walizochukua au wanafikishwa kwenye vyombo vya sheria kujibu mashitaka. Vilevele Katibu Mkuu OR TAMISEMI kwa kushirikiana na makatibu Tawala wa Mikoa wanashauriwa kuhakikisha Mamlaka husika zinachukua hatua stahiki za kuborersha mfumo wa mapato (LGRCIS), kwa kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya ndani.

Ninapendekeza kuwa mamlaka zinazohusika kwa kushirikiana na TAKUKURU zihakikishe kuwa watu wote waliohusika katika kukkusanya miamala hii na kutokuipeleka benki wanawajibika ili kurudisha fedha hazikuwasilishwa. Pia, Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Makatibu Tawala wa Mikoa wanashauriwa kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa katika kuboresha Mfumo wa Habari wa Ukusanyaji Mapato ya Serikali

za Mitaa kwa kuondoa mianya inayowezesha matumizi mabaya ya mapato ya serikali.

13.3.2.2 Miamala iliyorekebishwa kwenye mfumo wa mapato (LGRCIS) bila ya kuwa na idhini ya Afisa Masuuli na vielelezo vya uthibitisho Sh. 37,842,260,778

Katika kipindi cha miaka ya fedha 2017/18 hadi 2019/20, ukaguzi maalumu ulibaini kwamba mamlaka 29 za serikali za mitaa zilifanya marekebisho ya miamala kwenye mfumo wa mapato ya ndani (LGRCIS) yenye thamani ya Sh. 327,815,714,881,270 bila kufuata taratibu za mfumo wa udhibiti na uhakiki wa mapato ya ndani kama vile; uwepo wa barua za maombi ya kurekebishiwa miamala iliyokosewa, uwepo wa stakabadhi za mapato kuonyesha kukosewa kwa miamala iliyohitaji marekebisho na idhini ya Afisa Masuuli kufanya marekebisho yaliyoombwa. Hii ni kutokana na mfumo dhaifu wa udhibiti wa mapato ya ndani. Muhutasari wa halmashauri zilizobainika kufanya marekebisho yasiyoidhinishwa ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 13-15** hapa chini

Jedwali Na. 13-15: Halmashauri Zenye Miamala Iliyorekebishwa Kwenye Mfumo wa Mapato Bila Idhini ya Afisa Masuuli na Vielelezo Stahiki

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W ya Chamwino	18,377,751,920
2.	H/W ya Nyasa	7,302,645,573
3.	H/W ya Bariadi	3,092,854,825
4.	H/M ya Temeke	2,003,392,627
5.	H/M ya Sumbawanga	922,938,181
6.	H/J Mwanza	917,594,396
7.	H/Mji wa Geita	792,594,615
8.	H/W ya Kibondo	632,512,448
9.	H/Mji wa Kahama	578,909,103
10.	H/W ya Rungwe	367,645,563
11.	H/W ya Sikonge	355,625,976
12.	H/W ya Morogoro	340,356,347
13.	H/W ya Kilosa	310,568,090
14.	H/W ya Itigi	271,521,006
15.	H/W ya Mbozi	249,407,555
16.	H/Mji wa Korogwe	241,215,220
17.	H/Mji wa Nzega	195,343,548
18.	H/M ya Kinondoni	170,763,912
19.	H/W ya Sumbawanga	140,587,500
20.	H/W Karagwe	127,888,199

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
21.	H/W ya Chemba	118,736,749
22.	H/W ya Kasulu	100,527,559
23.	H/W ya Masasi	93,970,194
24.	H/W ya Njombe	50,656,612
25.	H/M ya Mpanda	47,893,841
26.	H/M ya Musoma	25,475,799
27.	H/M ya Songea	9,692,400
28.	H/W ya Meru	3,191,020
Jumla		**37,842,260,778**

Kwa maoni yangu, marekebisho yasiyo na idhini, yalifanyika ili kuficha ubadhilifu wa mapato au matumizi mabaya ya fedha za mapato ya ndani yaliyofanyika. Mfumo huu wa usuluhishi kwa njia ya kufuta au kurekebisha taarifa za mapato bila idhini, unachangia kwa kiasi kikubwa katika upotevu wa fedha za Serikali.

Nashauri Mamlaka husika zichukue hatua stahiki dhidi ya wote waliokiuka utaratibu wa marekebisho ya miamala ya mapato iliyokosewa, kwa kuzingatia matakwa ya mfumo wa udhibiti wa mapato ya ndani, pia OR TAMISEMI ihakikishe mfumo wa mapato ya ndani (LGRCIS) unatoa nafasi kwa mwidhinishaji kutoa kibali cha marekebisho na zuio la kufanya marekebisho bila idhini.

13.3.2.3 Mapato ambayo hayakukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani Sh. 60,805,505,343

Katika ukaguzi maamlu kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/2018 hadi 2019/2020 ukaguzi nilibaini kuwa jumla ya Halmashauri 42 hazikuweza kukusanya mapato kiasi cha Sh. 60,805,505,343 kutoka vyanzo mbalimbali, vikijumuisha kodi za vibanda vya Halmashauri, madeni kutoka kwa mawakala wa ukusanyaji mapato ya ndani, Leseni za biashara zisizolipiwa na malipo yanayotokana na ukusanyaji wa Taka ngumu; kama ilivyoanishwa katika **Jedwali Na. 13-16**

Kwa maoni yangu, upotevu huu wa mapato unatokana na udhaifu wa mamlaka husika kushindwa kufuatilia na kuhakikisha wadaiwa wote wanalipa madeni yao kwa wakati na kuchukua hatua stahiki kwa wanaoshindwa kutimiza wajibu wao wa kulipa.

Jedwali Na. 13-16: Mapato ambayo Hayakukusanywa Kutoka Vyanzo Mbalimbali vya Mapato ya Ndani

Na.	Mkoa	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Dar es Salaam	H/Manispaa Kinondoni	28,996,482,240
2	Mwanza	H/Jiji Mwanza	6,674,588,103
3	Arusha	H/Jiji Arusha	5,096,082,536
4	Tanga	H/Jiji Tanga	3,571,460,410
5	Rukwa	H/W Sumbawanga	3,464,662,856
6	Dar es Salaam	H/Jiji Dar es Salaam	2,529,445,783
7	Tanga	H/Mji Korogwe	1,855,512,000
8	Iringa	H/W Kilolo	1,250,418,957
9	Dodoma	H/W Kongwa	861,484,756
10	Manyara	H/W Kiteto	625,779,028
11	Kilimanjaro	H/Manispaa Moshi	609,742,907
12	Kilimanjaro	H/W Same	570,828,500
13	Songwe	H/W Mbozi	466,336,477
14	Mwanza	H/W Magu	450,839,043
15	Dodoma	H/W Chamwino	370,121,628
16	Kagera	H/W Karagwe	342,154,922
17	Njombe	H/W Makete	295,118,952
18	Dodoma	H/Jiji Dodoma	268,991,230
19	Dar es Salaam	H/Manispaa Ilala	241,235,806
20	Ruvuma	H/Manispaa Songea	210,319,829
21	Kigoma	H/W Uvinza	206,031,703
22	Tabora	H/ManispaaTabora	199,556,934
23	Arusha	H/Wilaya Karatu	194,512,788
24	Simiyu	H/W Bariadi	164,089,366
25	Pwani	H/W Bagamoyo	135,430,352
26	Katavi	H/Manispaa Mpanda	134,515,000
27	Tanga	H/W Mkinga	126,632,060
28	Shinyanga	H/Mji Kahama	104,678,353
29	Mara	H/W Rorya	99,511,249
30	Tabora	H/Mji Nzega	96,727,295
31	Mara	H/Manispaa Musoma	88,690,000
32	Manyara	H/W Mbulu	74,726,150
33	Dodoma	H/W Chemba	73,121,393
34	Kigoma	H/W Kasulu	59,314,231
35	Njombe	H/W Njombe	58,948,704
36	Lindi	H/W Kilwa	51,175,024
37	Arusha	H/W Meru	40,988,000
38	Mbeya	H/W Busokelo	39,344,000
39	Kigoma	H/W Buhigwe	31,549,418
40	Singida	H/W Itigi	29,572,710
41	Singida	H/W Mkalama	19,828,000
42	Ruvuma	H/W Nyasa	16,203,900
43	Geita Mji	H/Mji Geita	8,752,750
Jumla			**60,805,505,343**

Nashauri mamlaka husika ziongeze nguvu katika kufuatilia madeni haya kwa kushirikiana Serikali ya Mikoa au Wilaya husika.

13.3.2.4 Mapato ya ushuru wa Huduma ambayo hayajakusanywa na Halmashauri Sh. 8,457,954,064

Katika ukaguzi maalumu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 ukaguzi maalumu ulibaini kuwa Halmashauri 21 zilishindwa kukusanya mapato ya ushuru wa huduma kiasi cha Sh. 8,457,954,064, kutokana na shughuli mabalimbali za kiuchumi zilizofanyika ndani ya halmashauri husika, kama ilivyoanishwa kwenye J**edwali namba.13-17**

Kwa maoni yangu, upotevu huu wa mapato unatokana na udhaifu wa mamlaka husika kushindwa kufuatilia vyanzo vya mapato ikiwemo ushuru wa huduma ili kujua kampuni na wadau wote wanaoendesha shughuli za kiuchumi ndani ya maeneo yao ya kiutawala na kuhakikisha kuwa yanalipa ushuru kadri ya matakwa ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Na. 9 ya 1982, (Ilivyorekebishwa 2000) inayosema kwamba mapato na rasilimali za Halmshauri ya Wilaya yatajumuisha mapato yote yaliyotokana na huduma zitolewazo na kupokelewa na taasisi, kwa kiwango kisichozidi 0.3 asilimia ya mapato hayo, baada ya kutoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa.

Nashauri mamlaka husika ziongeze nguvu katika kufuatilia na kujua mapato halisi ya Taasisi zinazofanya kazi au kutoa huduma ndani ya maeneo yao ya kiutawala ya halmashauri husika kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ili waweze kukusanya mapato stahiki toka katika taasisi hizo.

Jedwali Na. 13-17. Mapato ya ushuru wa Huduma ambayo hayajakusanywa na Halmashauri

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi
1	H/Manispaa Ilala	3,075,963,095
2	H/Mji Kahama	1,211,482,633
3	H/W Kilosa	962,165,908
4	H/Mji Geita	654,935,880
5	H/W Kilolo	618,071,741
6	H/Manispaa Songea	501,276,586

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi
7	H/W Rungwe	459,091,770
8	H/W Bagamoyo	191,997,408
9	H/W Rorya	163,468,114
10	H/Manispaa Mpanda	140,022,735
11	H/W Kibondo	111,026,052
12	H/W Magu	72,215,601
13	H/W Makete	67,421,870
14	H/W Kilwa	51,175,024
15	H/W Kiteto	49,363,229
16	H/W Nyasa	44,924,745
17	H/W Kongwa	39,051,604
18	H/ManispaaTabora	23,077,333
19	H/W Same	10,910,631
20	H/W Njombe	5,172,040
21	H/W Mkinga	5,140,065
Jumla		**8,457,954,064**

Ninapendekeza mamlaka zinazohusika kuongeza juhudi katika kufuatilia na kutambua mapato sahihi ya kampuni zinazotoa huduma katika eneo la utawala wa Halmashauri husika kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuwezesha ukusanyaji wa ushuru wa huduma kutoka kwa kampuni hizo.

13.3.2.5 Manunuzi ya vifaa na huduma yaliyofanyika bila kudai stakabadhi za mashine ya Kielektroniki (EFD receipts) kutoka kwa wazabuni Sh. 46,500,102,763

Katika ukaguzi maalumu kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/2018 hadi 2019/2020 nilibaini kuwa Halmashauri 25 zilifanya manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali zenye jumla ya Sh. 46,500,102,763 kutoka kwa wazabuni mbalimbali, bila kudai stakabadhi za mashine ya Kielektroniki (EFR receipts), kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 13-18.** Manunuzi ya aina hii yanasaidia wazabuni kutolipa kodi stahiki kutokana na mapato ya shughuli wanazozifanya. Ni jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha ukwepaji wa Kodi kwa njia ya kutotoa stakabadhi za kielektroniki kwa malipo yaliyofanyika, unasitishwa,

Jedwali Na. 13-18: Halmashauri Zilifanya Malipo Bila Kudai Stakabadhi za Mashine ya Kielektroniki (EFD receipts)

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	H/Manispaa Musoma	11,694,518,761
2	H/Manispaa Songea	11,374,480,196
3	H/Manispaa Morogoro	9,135,494,022
4	H/W Songea	8,044,462,363
5	H/Manispaa Shinyanga	1,313,770,897
6	H/Manispaa Iringa	1,266,441,061
7	H/W Bagamoyo	681,187,539
8	H/W Kilolo	644,690,624
9	H/Jiji Arusha	463,065,088
10	H/W Makete	274,740,846
11	H/W Mbozi	272,489,500
12	H/Manispaa Ilala	259,336,750
13	H/W Siha	194,832,334
14	H/W Bukoba	126,115,377
15	H/W Magu	108,903,893
16	H/Manispaa Temeke	102,805,550
17	H/W Mkalama	91,474,066
18	H/W Kasulu	74,844,500
19	H/Manispaa Mpanda	72,566,500
20	H/W Karatu	72,176,877
21	H/Manispaa Sumbawanga	70,543,777
22	H/W Kilosa	66,676,642
24	H/W Meru	61,777,600
25	H/Mji Kahama	20,008,000
26	H/W Morogoro	12,700,000
		46,500,102,763

Ninapendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kudai risiti za EFD kutoka kwa wauzaji au watoa huduma kila manunuzi yanapofanywa ili kutii Kanuni ya 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Uma 2016. TRA ifanye uchunguzi wa malipo yote ambayo yalifanyika bila ya wazabuni kutoa risiti za EFD.

13.3.2.6 Hati za Malipo ya Sh. 5,796,326,524 Ambazo Hazikuwasilishwa Kwa Ajili ya Ukaguzi

Ukaguzi maalumu uliofayika kati ya miaka ya fedha 2017/18 hadi 2019/20, ulibaini uwepo wa hati za malipo zenye thamani ya jumla ya Sh. 5,796,326,524 ambazo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo uhalali wa malipo yaliyofanyika haukuweza kuthibitishwa. Hii ni kinyume na Kifungu Na.15(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, kinachomtaka Afisa Masuuli wa taasisi inayokaguliwa, kuhakikisha kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapata nyaraka zote za mkaguliwa zinazomuwezesha kutimiza kazi na majukumu yake, pia ni kunyime na kifungu cha 8 (2) (c) cha Memoranda ya Serikali za Mitaa, 2009 kinachotaja kuwa miongoni mwa majukumu ya Mweka Hazina wa Halmashauri ni kuhakikisha kunakuwa na mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani na utunzaji wa nyaraka za mapato na matumizi ya ofisi. Kutowasilishwa kwa nyaraka kunazuia ofisi yangu kukidhi mawanda ya ukaguzi. Haikuwezekana kujiridhisha kama malipo yaliyofanyika yalihusu shughuli lengwa za mamlaka husika. Mchanganuo wa nyaraka za malipo ambazo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi uo katika **Jedwali Na. 13-19**

Jedwali Na. 13-19: Hati za Malipo Ambazo Hazikuwasilishwa kwa Ajili ya Ukaguzi

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi
1	H/W Rorya	976,942,815
2	H/W Kilosa	815,376,829
3	H/Manispaa Kinondoni	540,605,920
4	H/W Itigi	482,116,753
5	H/W Morogoro	387,671,740
6	H/W Njombe	286,049,700
7	H/W Bariadi	267,859,305
8	H/Manispaa Ilala	241,235,806
9	H/Manispaa Singida	239,071,596
10	H/W Mbozi	222,822,766
11	H/W Kasulu	214,683,142
12	H/W Siha	194,832,334
13	H/W Kibondo	162,556,940
14	H/Manispaa Iringa	162,438,044
15	H/Manispaa Sumbawanga	153,401,656
16	H/Jiji Arusha	135,774,270
17	H/W Rungwe	119,774,590

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi
18	H/W Kilwa	103,287,218
19	H/W Uvinza	70,186,700
20	H/W Kongwa	19,638,400
Jumla		**5,796,326,524**

Ninapendekeza kwamba mamlaka husika zichukue hatua stahiki dhidi ya wafanyikazi wa Halmashauri waliotajwa katika ripoti maalum za ukaguzi kwa kutokuwa makini katika utunzaji wa hati za malipo. Vilevile, uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuimarisha taratibu za kushughulikia na kuhifadhi nyaraka mbalimbali zikiwa ni pamoja na Hati za malipo. Pia Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuhakikisha kuwa zina zingatia sheria pamoja na miongozo mbali mbali kama ilivyotajwa hapo juu.

13.3.3 Hoja zenye Maudhui Tofauti kwa kila Halmashauri Zilizokaguliwa

HALMASHAURI YA WILAYA YA KARATU

13.3.3.1 Ubadhirifu Uliotokana na Malipo hewa ya Vifaa vya Ujenzi Sh. 63,745,000

Katika Mwaka wa fedha 2017/18 H/W Karatu kupitia hati ya malipo Na.703084V1803074 na hundi Na.50000784 ya tarehe 23/05/2018 ilimlipa Mkandarasi Anatoly Construction kiasi cha Sh.132,690,200 kwa ajili ya kuleta vifaa vya ujenzi wa soko kuu la Halmashauri.

Hata hivyo ukaguzi wangu ulibaini kuwa jumla ya vifaa vyenye thamani ya Sh.63,745,000 vilivyodaiwa kuletwa na mzabuni kwa Halmashauri havikuwa vimewasilishwa na mzabuni huyo na hivyo kufanya malipo hayo kuwa malipo hewa.

Vilevile katika hali isyo ya kawaida nilibaini kuwa jumla ya Sh. 59,145,000 zililipwa kwa mzabuni tofauti na aliyeleta vifaa vya ujenzi.

Ninapendekeza uongozi wa Halmashauri kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ili kupunguza hatari za udanganyifu huu na ubadhirifu wa fedha za umma. Pamoja na hayo, napendekeza

hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa wote waliotajwa katika ripoti maalum ambao walihusika katika mapungufu hayo.

HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA

13.3.3.2 Ada za Leseni zilizokusanywa nje ya mfumo wa mapato Sh. 689,214,391

Katika kipindi cha miaka ya fedha 2017/18 na 2018/2019 Halmashauri ya Jiji la Arusha ilikusanya ada za leseni kiasi cha Sh.689,214,391 nje ya Mfumo wa Serikali za Mitaa wa Kukusanyia Mapato (LGRCIS) kinyume na maelekezo ya serikali yanayosisitiza kukusanya mapato kwa njia ya mfumo. Hali hii inaashiria udhaifu katika mfumo wa uthibiti wa ndani wa makusanyo ya mapato

13.3.3.3 Malipo ya fidia yasiyo na tija kwa Halmashauri ya Jiji la Arusha na bila kuzingatia sheria na mwongozo wa uthaminishaji wa ardhi Sh.1,575,000,000

Katika kipindi cha mwaka 2017/18 na 2018/19 Halmashauri ya Jiji la Arusha ilifanya makubaliano na mwananchi mmoja ya kumlipa fidia ya eneo la ekari 50 kwa gharama ya Sh 2,125,000,000. Makubaliano yalikuwa ni kupima viwanja na kuviuza kwa wananchi na kuwa muuzaji angelipwa ndani ya mwaka mmoja kutegemeana na mauzo ya viwanja hivyo.

Ukaguzi ulibaini kuwa kufikia tarehe 31 Julai, 2020, Halmashauri ilikuwa imeuza viwanja vinane tu (8) kwa jumla ya Sh. 78,615,400 kati ya viwanja 291 vilivyopimwa. Fedha kiasi cha Sh.1,575,000,000 zililipwa kama fidia, kinyume na matakwa ya mkataba yaliyoitaka Halmashauri ya Jiji la Arusha kulipa kulingana na mauzo ya viwanja. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa malipo hayo yalifanyika bila kuwepo kwa taarifa ya uthaminishaji wa eneo, iliyoidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali.

13.3.3.4 Malipo ya fidia ya ardhi kufanyika kabla ya taarifa ya uthamini kuandaliwa na kupitishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali Sh. 243,000,000

Timu ya ukaguzi maalum ilibaini kuwa Halmashauri ya Jiji la Arusha ilifanya malipo ya Sh.243,000,000 kwa fidia ya eneo la kituo cha afya Muriet kabla ya taarifa ya uthaminishaji wa eneo hilo kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Ukaguzi ulibaini kuwa taarifa hiyo iliandaliwa mwezi Juni, 2018 na iliidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali tarehe 20 Agosti, 2018 wakati malipo yalifanyika kati ya mwezi Februari na Mwezi Aprili, 2018

13.3.3.5 Malipo ya ziada kwa manunuzi ya ardhi bila mkataba na bila kupitishwa na vikao vya kudumu vya Halmashauri Sh. 30,940,000

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri ya Jiji la Arusha ilifanya makubaliano ya kununua eneo la ekari moja (1) kutoka kwa mwananchi kwa bei ya Sh.50,000,000. Hata, hivyo baada ya kufanya malipo ya fedha kwa mujibu wa makubaliano, muuzaji aliwasilisha barua ya malalamiko tarehe 27 Desemba, 2017 akidai kupunjwa kiasi cha Sh.30,940,000 kutokana na ardhi aliyoiuzia Halmashauri. Kiasi hiki cha fedha za nyongeza kililipwa kupitia hati ya malipo namba 702001V1801800 ya tarehe 9 Januari, 2018 bila ya uwepo wa mkataba wa nyongeza (addendum) na bila taarifa ya uthamini wa ardhi ili kujua thamani halisi ya eneo husika. Kwa madai hayo mapya Halmashauri ya Jiji la Arusha ilinunua ekari moja kwa Sh. 80,940,000

13.3.3.6 Malipo ya Sh. 154,668,483.87 yaliyolipwa bila kuidhinishwa na Afisa Masuuli

Katika kipindi cha mwaka 2017/2018 hadi 2019/2020, ukaguzi maalumu ulibaini kuwa Halmashauri ya Jiji la Arusha iliwalipa wazabuni wawili jumla ya Sh. 154,668,483.87 kutoka akaunti ya maendeleo bila kuidhinishwa na Afisa Masuuli kinyume na Agizo la 10(2)(a) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 na Kanuni ya 89(4) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001

13.3.3.7 Manunuzi yaliyoidhinishwa na wajumbe wawili kati ya watano wa Bodi ya Zabuni Sh.289,043,152

Mapitio ya nyaraka za manunuzi yaliyofanywa na Halmashauri ya Jiji la Arusha yalibaini manunuzi ya jumla ya Sh.289, 043,152.16 yaliyofanywa kupitia 'circular resolution' ambazo ziliidhinishwa na wajumbe wawili (2) badala ya watano (5) kinyume na matakwa ya Kanuni ya 58(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013. Kanuni ya 58(4) ya Kanuni hizo inaelekeza maamuzi yafanywe baada ya kupitishwa na zaidi ya nusu (wajumbe 3) ya wajumbe wa bodi ya zabuni

13.3.3.8 Uwekezaji usio na tija kati ya Halmashauri ya Jiji la Arusha na kampuni ya Happy Sausage katika kampuni ya Arusha Meat Company Limited (AMCL).

Ukaguzi maalum ulibaini kuwa tarehe 29 Novemba 1986 Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Arusha ilipima viwanja eneo la Sakina Arusha na kugawa kiwanja Na 1 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Arusha (Kwa sasa Jiji) . Tarehe 6 Desemba 1986 Halmashauri ilipewa haki ya kumiliki (Offer of Right of Occupancy) kiwanja Na. 1 Kitalu "FF" chenye ukubwa wa hecta 10.879 na tarehe 19 Oktoba, 1994 ilipewa Hati miliki ya kiwanja hicho kwa muda wa miaka 99.

Ukaguzi maalumu ulibaini kuwa tarehe 9 Januari, 1993 Halmashauri ya Manispaa ya Arusha (Jiji) iliingia makubaliano na Kampuni ya Happy Sausage Limited (HSL) ya kuendesha kwa ubia kiwanda cha nyama, Arusha Meat Company Limited (AMCL). Sehemu ya tatu (3) ya makubaliano hayo ilieleza kuwa Manispaa ya Arusha itamiliki asilimia 49 ya hisa sawa na Sh.14,700,000 na Happy Sausage itamiliki asilimia 51 sawa na Sh.15,300,000. Sehemu ya nne (4) ya makubaliano hayo ilikubalika kuwa wakurugenzi wa bodi watakuwa sita (6); watatu (3) kutoka Halmashauri ya Manispaa na watatu (3) kutoka Happy Sausage Ltd. Pia sehemu ya tano ilikubalika kuwa masuala yote yanayoihusu kampuni yatajadiliwa kwa pamoja na kufanyiwa maamuzi ya pamoja kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Arusha na Kampuni ya Happy Sausage Ltd.

Hata hivyo mapitio ya utekelezaji wa makubaliano hayo yalibaini mapungufu yafuatayo:

- ✓ Kiwanja cha Halmashauri ya Jiji la Arusha kumegwa na kutengenezwa Kiwanja Na.2 Kitalu "FF" na kumilikiwa na Kampuni ya Happy Sausages Ltd isivyo halali
- ✓ Maamuzi ya kuuzwa na kuwekwa rehani kwa mali (ardhi) ya kampuni ya Arusha Meat Company Limited (AMCL) ambayo hayakuridhiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Arusha licha ya kuwa ni mwanahisa wa kampuni hiyo.
- ✓ Halmashauri kushindwa kurasimisha umiliki wa Hisa 3420 kutoka Hanns Seidel Foundation zilizohamishiwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Arusha.
- ✓ Halmashauri kutoshirikishwa kwenye maamuzi mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa Kampuni ya Arusha Meat Company Limited (AMCL).

Katika mazingira hayo napendekeza;

- ✓ **Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha aongeze usimamizi katika kuhakikisha kwamba leseni zote za biashara zinazotolewa na Halmashauri ya Jiji la Arusha ni halali na zimetolewa kutoka kwenye mfumo wa mapato – LGRCIS**
- ✓ **Katibu Mkuu OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, wahakikishe kuwa Halmashauri ya Jiji inatekeleza taratibu za kulipa fidia na kuhakikisha pia kuwa inafuata miongozo na sheria kabla ya kuingia makubaliano ya kununua au kufidia ardhi. Uchunguzi ufanyike ili kubaini ubadhirifu uliofanywa na kampuni ya Happy Sausages Ltd.**
- ✓ **Mamlaka husika kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wa Halmashauri waliotajwa katika taarifa husika kwa kutosimamia na kutotekeleza ipasavyo maeneo yao ya kazi na hivyo kupelekea mapungufu mbali mbali yaliyobainika.**

13.3.3.9 Hasara iliyotokana na kutokujumishwa kwa baadhi ya kazi katika mkataba, kinyume na ilivyokuwa imeainishwa katika kabrasha la zabuni (RFP) la kumpata Mshauri Mwelekezi Sh 207,403,925

Timu ya ukaguzi maalumu ilipitia kabrasha la zabuni lililotolewa na halmashauri na kulilinganisha na mkataba uliosainiwa tarehe 6/5/2014 baina ya M/s Tanzania Investment Bank (TIB) na Mshauri Mwelekezi wa mradi kwa kazi ya kusanifu jengo la Soko la Kisasa Kisutu kwa niaba ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Ilibainika kuwa mkataba haukujumuisha kazi zote kama ilivyokuwa imeainishwa kwenye kabrasha la zabuni na hivyo kusababisha halmashauri kuingia mkataba mwingine wenye namba LGA/015/ /2017/2018/HQ/CS/07 LOT 3 wa kutoa huduma ya mshauri mwelekezi katika ujenzi wa Soko Jipya la Kisasa Kisutu kwa gharama ya Sh 200,139,800 ambazo zingeweza kuepukika endapo mkataba wa kwanza ungekuwa umejumuisha kazi zote.

13.3.3.10 Hasara iliyosababishwa na kutokujumuishwa kwa baadhi ya kazi katika mkataba, kinyume na zilivyokuwa zimeainishwa katika kabrasha la zabuni Sh. 653,990,198

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ilipata hasara ya jumla ya Sh. 653,990,198 zinazohusiana na ujenzi wa Hospitali ya Kivule kama inavyoonekana hapa chini;

Halmashauri ya Manispaa ya Ilala iliingia mkataba na Mkandarasi wa ujenzi wa Hospitali ya Kivule kwa mkataba wenye Kumb. Na. LGA/015/IMC/2014/2015/W/06 uliosainiwa tarehe 19/06/2015 kwa bei ya mkataba Sh.1,019,298,868 ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani. Halmashauri ilimsimamisha Mkandarasi kuendelea na kazi kwa muda wa miezi miwili (2) kupitia barua yenye Kumb. Na. IMC/HC.110/1/ ya tarehe 13/09/2016 ili Halmashauri ifanyie kazi mapungufu yaliyokuwa kwenye mchoro ikiwemo kukosekana kwa maelezo ya ulazaji wa nondo (bar bending schedule) na michoro ya huduma ya majisafi na majitaka, na miundombinu ya tehama pia kutofanyika kwa usanifu (design) na mchanganuo unaoonesha namna ya kujenga barabara. Kwa

kuvunjwa mkataba huo kulipelekea Halmashauri kutozwa fidia ya Sh. 56,147,819 kwa mujibu wa kipengele 63.1 cha masharti ya jumla ya mkataba (GCC).

Vilevile, Halmashauri iliingia mkataba mwingine na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) wenye Kumb. Na. LGA/015/2017/2018/HQ/C/01 kwa gharama ya Sh.134,881,579 kwa ajili ya kufanya mapitio ya kazi alizofanya Mkandarasi aliyesimamishwa, kufanya usanifu na kuandaa michoro na michanganuo pamoja na usimamizi wa mradi.

Zaidi ya hayo, kufuatia kuvunjwa kwa mkataba wa kwanza, Halmashauri iliingia mkataba na SUMA JKT ambaye alilipwa kiasi cha ziada cha Sh. 462,960,800 kwa shughuli zingine mbali mbali ikiwa ni pamoja na kazi ambazo nilibaini mkandarasi wa awali alikuwa amekwisha lipwa.

13.3.3.11 Kutokamilika ujenzi wa Zahanati katika Kata ya Kipunguni kutokana na upotevu wa fedha Sh. 74,093,000

Mapitio ya jalada IMC/JW.12/1 la maendeleo ya Kata ya Kipunguni na Daftari la makosa ya kinidhamu yalibaini kuwa Afisa Mtendaji wa Kata ya Kipunguni na mtia saini wa akaunti ya maendeleo ya Kata ya Kipunguni walikutwa na kosa la upotevu wa fedha Sh.74,093,000 zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati ya Kata ya Kipunguni. Upotevu huo ulisababisha mradi wa ujenzi kutokukamilika.

Ninapendekeza kwamba uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala idai marejesho ya Sh. 207,403,925 kutoka TIB ambayo ni hasara kwa kuingia mkataba mwingine kama matokeo ya kuondoa baadhi ya vipengele ambavyo vilikuwa kwenye kabrasha la zabuni la awali (RFP). Kwa kuongezea, ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI ichunguze uzembe na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wale wote waliohusika na upotevu na matumizi mabaya ya fedha kama ilivyoelezwa katika ripoti maalum ya ukaguzi.

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR-ES-SALAAM

13.3.3.12 Ununuzi wa "excavator" wenye shaka Sh.359,862,240

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliingia makubaliano na mzabuni kupitia mkataba Na.LGA/018/2019/2020/G/22, wenye thamani ya Sh. 359,862,240 kununua **excavator" kwa ajili ya** dampo la Pugu Kinyamwezi. Manunuzi haya yanatia shaka kutokana na mzabuni huyo kutokuwa na leseni ya uuzaji wa Mitambo. Mzabuni huyo alikuwa na leseni ya ukodishaji wa mitambo kama inavyothibitishwa na nakala ya leseni yake ya biashara Na. B 3190519 ya tarehe 26 Juni, 2019.

13.3.3.13 Malipo hewa ya fedha za barabara Sh. 311,329,650

Mnamo tarehe 22/02/2020, halmashauri iliingia makubaliano ya kujenga mita 300 za barabara ya zege na uwekaji wa miundombinu ya umeme katika dampo la Pugu kinyamwezi na mkandarasi M/s Summertech kupitia mkataba Na. LGA/018/2019/2020/W/01 na 02 wenye thamani ya Sh. 525,749,000 uliotakiwa kuanza tarehe 21/01/2020 hadi tarehe 25/3/2020. Kazi hizo hazikuthibitika kufanyika hadi kufikia Agosti, 2020, kinyume na matakwa ya mkataba.

Kwa mujibu wa madhaifu yaliyotajwa hapo juu, ninapendekeza hatua stahiki zichukuliwe ili kuhakikisha kuwa mkandarasi anarejesha kiasi cha Sh. 311,329,650 zilizolipwa kwa kazi ambazo hazijatekelezwa. Aidha, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa waliotajwa katika ripoti husika kwa kushindwa kusimamia misingi ya fedha kama ipasavyo na hivyo kupelekea matumizi holela ya fedha za serikali.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

13.3.3.14 Upotevu wa mapato ya Halmashauri yaliyopokelewa kwa kutumia hundi zilizokataliwa na benki Sh. 172,150,636

Katika kipindi cha fedha mwaka 2017/18 hadi 2019/20 Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilipokea hundi zenye thamani ya Sh. 172,150,636, kwa ajili ya malipo ya kodi mbalimbali za

wafanyabiashara, baada ya hundi hizi kupelekwa benki na kukataliwa. Hakuna ufuatiliaji wowote ulifanyika hivyo, mapato haya hayakupokelewa na Halmashauri ya Temeke.

13.3.3.15 Malipo ya Sh. 44,413,281 yalilipwa zaidi ya kazi zilizofanyika Katika mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari Mbagala

Ukaguzi umebaini Mkandarasi alilipwa kiasi cha Sh. 44, 413,281.25 kwa kazi ambazo hazikufanyika katika utekelezaaji wa Mkataba Na.LGA /016/2019-2020/HQ/W/14

Ninapendekeza Serikali itekeleze mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti yangu maalum ya ukaguzi ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua zinazofaa dhidi ya maafisa waliohusika katika matukio hayo

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

13.3.3.16 Manunuzi yaliyofanyika bila ushindani wala idhini ya bodi ya zabuni Sh. 288,169,350.48

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Manispaa ilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. 288,169,350.48, wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa kituo cha mabasi Mwenge, bila kutafuta nukuu za bei wala idhini ya Bodi ya Zabuni, kinyume na Kanuni 163 na 164 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2013, inayoelekeza kuwa taasisi nunuzi kabla ya kufanya manunuzi ipate angalau nukuu tatu za bei, kutoka kwa watoa huduma/wauza vifaa

13.3.3.17 Kutorejeshwa kwa fedha zilizolipwa kama mkopo wa mshahara (salary advance) kwa mwalimu wa timu ya mpira wa miguu inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni Sh. 33,000,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri ilimpatia mkopo wa mshahara (salary advance) wa Sh. 33,000,000 mwalimu wa timu ya mpira wa miguu (Kocha) inayomilikiwa na Manispaa, ya Kinondoni (KMC FC) kupitia hundi Na. 000368 ya tarehe 21 Juni, 2019. Mpaka ukaguzi huu unakamilika Mwezi Agosti, 2020, mkopo huo ulikuwa bado kurejeshwa

13.3.3.18 Malipo ya uzoaji taka yaliyolipwa zaidi ya gharama ya makubaliano kimkataba Sh. 162,500,000

Halmashauri ya Manispaa iliingia Mkataba Na. LGA/017/2018-2019/HQ/NC/01 na timu ya mpira wa miguu (KMC-FC), kwa kazi ya uzoaji wa taka, kwa gharama ya Sh. 216,000,000 kwa muda wa miezi kumi na mbili (12), kuanzia Januari 2019 hadi Januari 2020.

Hata hivyo, ukaguzi maalumu ulibaini kuwa, Halmashauri ya Manispaa iliilipa timu ya mpira wa miguu ya Kinondoni (KMC-FC) Sh.378,500,000 na kusababisha malipo ya zaidi juu ya makubaliano ya mkataba kwa Sh. 162,500,000

13.3.3.19 Malipo ya ununuzi wa magari ya kuzolea taka usiozingatia taratibu za manunuzi Sh. 352,928,349

Ukaguzi maalumu ulibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ilifanya ununuzi wa magari mawili (2) ya uzoaji taka kutoka kwa kampuni ya GF Truck & Equipment Ltd, kwa gharama ya Sh. 352,928,349. Hata hivyo, ilibainika kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za manununuzi ya magari hayo ikiwemo;

(a) (Kufanya manunuzi ya magari bila kuomba kibali cha ununuzi wa magari kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, kinyume na waraka wa Hazina Na. 3 wa 11 Novemba, 2014 wenye Kumb. Na. CJA.233/362/01

(b) Kufanya manunuzi ya magari bila kupitishwa na Bodi ya Zabuni na bila kuomba na kupewa vipimo (specification) vya magari kutoka Wizara ya Miundombinu na kisha kuwasilisha vipimo hivyo pamoja na kibali toka Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa Mtendaji Mkuu Wakala wa Manunuzi Serikalini (GPSA), kwa ajili ya ununuzi wa magari husika.

(c) Kutumia fedha za mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kununua magari hayo, kiasi cha Sh. 102,000,000 ambazo hazikurejeshwa hadi ukaguzi unakamilika mwezi Agosti, 2020.

13.3.3.20 Malipo ya Vibarua yasiyostahili Sh. 284,850,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Manispaa ilifanya malipo ya Sh. 284,850,000 kwa ajili ya kuwalipa

vibarua wa usafi wa barabara na kuzoa taka. Hata hivyo kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za malipo kutokana na nyaraka zilizoambatanishwa kuwa na kasoro mbali mbali ikiwamo; hati za malipo kutoambatana na daftari la kuonyesha siku walizofanya kazi vibarua; sahihi za vibarua kutofautiana ikilinganishwa kati ya nyaraka za malipo ya vibarua (payroll) moja na nyingine ingawa majina ni yale yale; barabara walizofanyia usafi kutotajwa; kukosekana uthibitisho wa wenyeviti wa Serikali za Mitaa na wasimamizi wa vibarua husika, unaothibitisha kufanyika kwa zoezi la usafi/kuzoa taka na kukosekana kwa dokezo lililotoka idara tumizi kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji kuomba malipo.

13.3.3.21 Mapungufu ya kimkataba kati ya Manispaa na Oysterbay villa yaliyosababisha hasara ya Sh. 218,091,820

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa tarehe 13 Disemba, 2007 Manispaa iliingia mkataba na mwekezaji Oysterbay Villa, kwa ajili ya kujenga majengo manne yenye jumla ya vyumba 40, kwa ajili ya upangishaji kwa makubaliano kuwa mwekezaji atamiliki 75% sawa vyumba 30 ya mradi huo na Manispaa itamiliki asilimia 25% sawa na vyumba 10. Ujenzi ulikamilika tarehe 06 Agosti 2010 na vyumba kukabidhiwa Halmashauri ya Manispaa tarehe 16 Machi, 2019.

Aidha, kuanzia Septemba, 2010 mpaka ukaguzi huu unafanyika Agosti, 2020, Halmashauri ya Manispaa ilitarajiwa kuwa imekusanya Sh 246,930,120 kutokana na upangishaji vyumba 10 kwa bei ya Sh. 2,057,751 kwa miezi 120, tangu ujenzi ulipokamilika. Hata hivyo ni Sh.28,838,300 tu zilizolipwa na wapangaji waliongia mikataba na Manispaa, kuanzia 18 Machi, 2019 na hivyo kusababisha hasara ya Sh 218,091,820 kutokana na kitendo cha mwekezaji kutokukabidhi sehemu inayomilikiwa na Manispaa kimkataba kwa wakati (tangu 6 Agosti 2010).

Ninapendekeza kwa mamlaka husika kuhakikisha kuwa, udhaifu wote ulioainishwa wakati wa ukaguzi unashughulikiwa. Pia, uchunguzi unapaswa kufanywa ili kurekebisha makosa yaliyojulikana ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wale waliohusika. Kwa kuongezea, Ninatoa wito kwa uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kuzingatia njia za ushindani za ununuzi na hivyo kuzipa kipaumbele kabla

ya kutoa kazi za zabuni za kandarasi siku zijazo ili kupata thamani ya fedha katika ununuzi na ili kutii Sheria na kanuni za Manunuzi ya Umma. Kwa kuongezea, Menejimenti inapaswa kufanya juhudi zaidi kuhakikisha malipo yaliyotolewa kwa Kocha yanarudishwa na kocha huyo tena kwa wakati.

JIJI LA DODOMA

13.3.3.22 Kampuni ya Green Waste Pro ilikusanya kiasi cha Sh.186,370,700 bila kuwa na mkataba na kushindwa kuziwasilisha fedha hizo Halmashauri ya Jiji la Dodoma

Kampuni ya M/s Green Waste Pro Ltd ilikusanya mapato ya kiasi cha Sh. 186,370,700 kama tozo ya uzoaji wa taka ngumu katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa miezi 5 kuanzia tarehe 01/08/2018 hadi tarehe 03/01/2019 bila kuwa na Mkataba na Halmashauri na pia kampuni hiyo haikuwasilisha fedha hizo Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Ninapendekeza kuwa uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma ukishirikiana na Mamlaka husika zihakikishe kuwa kwa menejimenti ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuchukua hatua stahiki ambazo zitahakikisha kwamba Wakala anarejesha jumla ya Sh. 186,370,700 zilizokusanywa kabla ya kutiwa saini kwa mkataba

HALMASHAURI YA WILAYA KONGWA

13.3.3.23 Kukosekana thamani ya fedha katika miradi iliyokamilika lakini haitumiki Sh. 571,682,550

Wakati wa kutembelea miradi ya maendeleo tarehe 25/07/2020, ukaguzi maalumu ulibaini uwepo wa miradi ya Halmashauri yenye jumla ya Sh. 571,682,550 iliyokamilika lakini haitumiki. Miradi husika ni mradi wa ujenzi wa kituo cha Kongano la biashara ya kuku kijiji cha Mbande uliogharimu jumla ya Sh. 506,133,700 uliokamilika mnamo mwezi Julai 2019 na ujenzi wa Kiwanda cha kusindika maziwa katika kijiji cha Mbande uliogharimu Sh. 65,548,850 uliokamilika mnamo mwezi Juni 2020 . Hadi kufikia tarehe 19/08/2020, miradi hiyo ilikuwa haijaanza kutumika kama ilivyopangwa.

13.3.3.24 Malipo kwa wakandarasi kwa kazi ambazo hazijafanyika Sh. 32,883,000

Katika miaka ya fedha 2018/19 na 2019/20 Halmashauri iliwalipa wakandarasi Sh. 32,883,000 kwa kazi ambazo hazikufanyika. Kati ya malipo hayo Sh. 29,330,000 zililipwa kwa M/s Iwawa Civil and Building Works Co. Ltd kwa jili ya ujenzi wa sehemu ya kuhifadhia mazao katika kijiji cha Mkoka, na Sh. 3,553,000 zililipwa kwa Mkandarasi M/s Mia Brothers Tanzania Ltd kwa ajili ya ujenzi wa soko pamoja na eneo la kuanika mahindi katika kijiji cha Mkoka. Ukaguzi uliofanyika katika eneo la mradi mnamo tarehe 26/07/2020 na tarehe 27/07/2020 ulibaini kuwa malipo hayo yalilipwa kwa shughuli ambazo hazikufanyika na kusababisha hasara kwa Halmashauri.

13.3.3.25 Hasara ya Sh.55,500,000 kutokana na kuvunja Mkataba kinyume na utaratibu

Ukaguzi maalumu ulibaini kuwa Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 55,500,000 kwa mkandarasi M/s Robby Traders Co. Ltd katika kipindi cha miaka ya fedha 2017/18 hadi 2019/20 ikiwa ni malipo yaliyotokana na kuvunjwa kwa mkataba Na. HWK/KOG/RWSSP/C1/2004 LOT NO.KOGG2 wa utekelezaji wa mradi maji Kijiji cha Kiteto. Malipo hayo yalilipwa baada ya mkandarasi kufungua na kushinda kesi Na. 7 ya 2010 iliyosababisha hasara ya Sh. 55,500,000 kwa Halmashauri, ambayo ingeweza kuzuilika kama utaratibu uliokubalika kisheria ungezingatiwa

Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuchukua hatua stahiki kwa kuhakikisha matumizi ya miradi yote iliyokamilika ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na thamani ya fedha. Pia, Halmashauri ihakikishe kuwa Mkandarasi anarejeshea kiasi cha Sh. 32,883,000 zilizolipwa kugharamia shughuli ambazo hazikutekelezwa.

Vile vile, maofisa walioshiriki katika kuvunja mkataba kinyume na utaratibu wachukuliwe hatua stahiki kutokana na uzembe uliopelekea hasara ya Sh. 55,500,000.

HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA

13.3.3.26 Fedha za matazamio zilizotunzwa akaunti ya amana na Maendeleo ambazo hazijulikani matumizi yake Sh. 139,535,281.

Ilibainika wakati wa ukaguzi maalum kuwa fedha za matazamio kupitia makatabata Na. LGA/136/2014-2015/2016/W/07/02 kati ya Halmashauri na Mkandarasi Boya building Contractor Company Sh.139,535,281 zilizokatwa kwa mkandarasi, Sh. 121,822,773 zilipelekwa akaunti ya amana na 17,712,508 zilibaki akaunti ya maendeleo. Mradi ulikamilika na kupokelewa Halmashauri tarehe 29 Septemba, 2017 na muda wa matazamio ulikwisha tarehe 28 Septemba, 2018 na fedha za matazamio zilikuwa bado kulipwa kwa mkandarasi. Hadi ukaguzi unakamilika Agosti 2020, akaunti ya amana ilikuwa na salio la Sh 21,444,070 ambazo hazikuthibitishwa mchanganuo wake na hivyo kuashiria kuwa fedha za matazamio Sh. 139,535,281 zilitumika nje ya malengo tarajiwa.

13.3.3.27 Hasara ya Sh. 227,125,080 na mapungufu yaliyojitokeza katika Ujenzi jengo la Utawala la Ofisi ya Halmashauri (Awamu ya kwanza).

Halmashauri ya Chemba iliingia Mkataba namba LGA/136/2014-2015/2016/W/07/02 tarehe 31/8/2015 na Kampuni ya Boya building contractor Company kwa ajili ya Ujenzi jengo la Utawala la Ofisi ya Halmashauri (awamu ya kwanza) kwa gharama ya Sh. 1,369,915,609.64 ikijumuisha mabadiliko yaliyoridhiwa na Bodi ya Zabuni. Mkataba ulisainiwa tarehe 31 Agosti, 2015 na ulitarajiwa kukamilika tarehe tarehe 17/7/ 2017.

Ukaguzi ulibaini kuwa Halmashauri ilipata hasara ya Sh. 227,125,080 kwa kulipa fedha ya dharura (contingency) Sh 20,000,000 na Sh 30,000,000 za makisio (Provisional sums) pasipokuwa na uthibitisho wa kutokea kwa dhararua na bila kuwa na michoro ya umeme na makadirio halisi (BOQ) ya kazi hiyo pamoja na ongezeko la kazi (variations) lenye jumla ya Sh 177,125,080 pasipo kuwepo kwa uthibitisho wa nyaraka za vipimo halisi (measurement sheets).

Aidha, ukaguzi ulibaini kutumika kwa michoro ambayo haikuainisha mahitaji muhimu na ubora wa kazi unaohitajika na kupelekea kujengwa nguzo nne ambazo hazikutakiwa kujengwa na kushauriwa zibomolewe wakati wa ukaguzi wa mwisho. Ilibainika pia kutokuwepo kwa miundo mbinu ya kuondoa maji katika eneo la uwazi katikati ya jengo (Courtyard) ambayo ilitakiwa kuwekwa katika hatua ya msingi.

Ninatoa rai kwa uongozi wa Halmashauri kuimarisha udhibiti wa akaunti ya amana ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha za amana ambazo zinafikia Sh. 139,535,281 zilizotumiwa bila idhini stahiki. Aidha, hatua zinazostahili kuchukuliwa dhidi ya wafanyikazi wa Halmashauri waliotajwa katika ripoti husika ya ukaguzi huu maalum kwa kushindwa kuimarisha udhibiti wa usimamizi wa matumizi ya fedha za akaunti ya Amana.

HALMASHAURI YA WILAYA CHAMWINO

13.3.3.28 Hasara zilizopatikana katika hatua (Phase) mbalimbali za ujenzi wa Jengo la utawala Sh. 281,219,946.35

Ukaguzi ulipitia nyaraka mbalimbali za mradi wa ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, ambao ulifanyika katika awamu nne kwa kutumia wakandarasi wajenzi na baadae kufanyika kwa utaratibu wa "force account" na ulibaini hasara zifuatazo katika ujenzi wa jengo hilo:

Katika awamu ya kwanza H/W ya Chamwino ilimlipa mkandarasi jumla ya Sh. 889,885,734.20 badala ya kiasi cha mkataba cha Sh. 799,941,818.10, hivyo kusababisha hasara ya Sh. 89,943,916.10

katika awamu ya pili Sh. 1,038,416,045 zililipwa kwa mkandarasi badala ya Sh. 1,025,874,324 na hivyo kulikuwa na malipo yenye thamani ya Sh. 12,541,721 ambayo yalilipwa zaidi.

Katika awamu ya nne H/W ya Chamwino ilipata hasara iliyotokana na malipo ya kazi mbalimbali za ujenzi wa Jengo la utawala Sh. 101,694,310. Kati ya hizi Sh. 11,080,000 zilizolipwa kwa mkandarasi M/S National Service construction Department (SUMA JKT) kwa kazi za ujenzi wa msingi (substructure) na kuweka kiyoyozi ambazo hazikufanyika, Sh. 7,227,000 ambazo zimelipwa

zaidi ya kazi kwenye kipengele cha makisio ya gharama za vifaa (BOQ), Sh. 7,665,000 ni hasara iliyotokana na udanganyifu kwenye vipimo vya viwango vya kazi za kuweka vigae vya sakafu (floor tiles) ambapo eneo la mraba lililotakiwa kulipwa ni mita 1517.01 na sio mita 1670 na Sh. 75,722,310 iliyotokana na udanganyifu kwenye vipimo vya viwango vya kazi za kuchimba eneo na kumwaga kifusi kilichochimbwa.

Mnamo tarehe 23/10/2019 Halmashauri ilipovunja mkataba na mkandarasi M/S NATIONAL SERVICE CONSTRUCTION LTD (SUMA JKT), ambapo jumla ya kiasi cha Sh.148,961,562.75 tu ndicho kilichokuwa kimefidiwa (advance payment recovery) na halmashauri kutoka kwenye vyeti vya malipo ya Sh. 198,615,417 na hivyo kuacha kiasi cha Sh. 49,653,854.25 ambacho hakikufidiwa wala haikuwezekana kukipata kwani mkandarasi hakuwa amewasilisha dhamana ya mkataba wa kazi (performance bond) na dhamana ya malipo ya awali (advance payment bank guarantee)

H/W ya Chamwino ilipata hasara ya Sh. 13,500,000 kwa kumlipa Mkandarasi M/S National Service Construction Department (SUMA JKT), kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa jengo la muda (Temporary building) ambalo lilikuwa limekwisha jengwa na mkandarasi wa awali M/S Ebenezer Destefanos Co.Ltd na ndilo alilokuwa akitumia.

Baada ya mikataba na wakandarasi kuvunjwa na ujenzi kuendelea kufanyika kwa njia ya Force Account, H/W ya Chamwino ilifanya malipo ya manunuzi yenye thamani ya Sh. 17,384,220 kwa ajili vifaa vya kuweka mfumo wa umeme, licha ya kwamba kazi hizo za mfumo wa umeme zilikuwa zimeshafanywa na mkandarasi M/S National Service Construction Department (SUMA JKT) ambae alikuwa ameshalipwa kiasi cha Sh. 50,422,425 na alikuwa akidai kiasi cha Sh. 3,498,075 katika eneo hilo. Hii ina maana kuwa Halmashauri ilipata hasara ya Sh. 13,886,145 .

13.3.3.29 Hasara zilizopatikana katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Sh. 82,167,779

Mwaka wa fedha 2019/2020, halmashauri ilipokea fedha kiasi cha Sh. 3,410,333,660, kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru. Hadi tarehe 30/6/2020, kiasi cha Sh. 3,143,461,051.90 kilikuwa kimetumika na kubaki na salio la Sh. 266,872,598.10. Katika ujenzi wa Hospitali hii Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo ambayo yameisababishia Serikali hasara ya Sh. 82,167,779

- ✓ Tarehe 16/08/2019 Halmashauri ilifanya malipo kiasi cha Sh. 995,182,000 kwa National Service Construction Department (SUMA JKT), bila ya kuwa na mkataba nae. Hata hivyo, tarehe 23/10/2019 Halmashauri ilisaini mkataba wenye thamani ya Sh. 928,685,225.35 na SUMA JKT construction company LTD-central zone kwa ajili ya Ujenzi wa hospitali ya Uhuru, kwa kipindi cha miezi sita (6). Hii ilisababisha kampuni ya SUMA JKT Construction Company LTD, kulipwa zaidi kwa Sh. 66,667,778.75 (Sh. 995,182,000 – Sh. 928,685,225.35).
- ✓ Pamoja na kwamba, Halmashauri ilimlipa mkandarasi jumla ya Sh. 15,500,000 kwa jili ya ujenzi wa Ofisi ya muda yenye samani muhimu na chumba cha stoo pamoja na bango la mradi wakati wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), Ukaguzi ulibaini kuwa Mkandarasi (SUMA JKT) hakujenga ofisi/kibanda cha ofisi kama ilivyoelezwa kwenye mkataba na badala yake alikuwa akitumia nyumba iliyokutwa eneo la ujenzi na wala hakuna bango eneo la mradi.

Kwa kuzingatia mapungufu yaliyotajwa hapo juu, ninapendekeza kuwa hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya pande zote zilizotajwa katika taarifa mahususi ya ukaguzi maalum kwa kuwezesha malipo ya ulaghai na kusababisha hasara kwa serikali. Kwa kuongezea, ninapendekeza hatua stahiki zichukuliwe kwa wakandarasi kwa kuomba na kukubali malipo ya kazi ambayo haijafanywa kwa mujibu wa mkataba na kuisababishia serikali hasara. Aidha ninashauri mamlaka zinazohusika kuchukua hatua stahiki dhidi ya wakandarasi waliolipwa isivyostahili.

HALMASHAURI YA MJI GEITA

13.3.3.30 Hasara iliyosababishwa na halmashauri kutozingatia sheria, Kanuni na taratibu za manunuzi ya umma na usimamizi bora wa miradi ya maendeleo Sh 328,739,667

Katika kipindi cha Miaka mitutu (3) ya fedha kuanzia 2017/18 hadi 2019/20 halmashauri ilibainika kupata hasara ya jumla Sh. 328,739,667 kutokana na kutokuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu za manunuzi ya umma na usimamizi bora wa miradi ya maendeleo. Maeneo ya kiutendaji yaliyochangia hasara hii yameorodheshwa kama ifuatavyo:

(a) Kwenye mkataba Na. LGA/160/NCT/OS/W/2016/2017/01 wa ujenzi wa soko kuu la dhahabu, Halmashauri ilimpa mzabuni M/s Send Star mwenye bei kubwa ya Sh.1,517,187,133 na kumuacha mzabuni M/s Home Africa Investment Corporation Limited mwenye bei ndogo ya Sh. 1,329,233,965 isivyostahili na hivyo kuisababishia Halmashauri hasara ya Sh 187,953,168.

(b) Kutokata kodi ya zuio kwenye utekelezaji wa miradi mbali mbali iliyokuwa inatekelezwa chini ya mpango ya 'Corporate Social Responsibilities (CSR)' Sh. 4,410,757.

(c) Katika mwaka wa fedha 2017/18 kampuni ya GGML ilitoa kiasi cha sh.300,000,000 kama CSR ambayo ilipangwa kutumika kwa ajili manunuzi ya vifaa vya ujenzi katika H/W za Bukombe, Chato na Mbogwe. Nilifuatilia kuhakiki fedha hizo zilivyotumika na kubaini kuwa katika halmashauri ya Chato mabati yalinunuliwa kwa bei kubwa kuliko bei ya soko kwani bati moja lilinuliwa kwa Sh. 49,000 badala ya Sh. 27,000 hivyo kwa mabati ya 1400 yaliyonunuliwa H/W ilipata hasara ya Sh.30,800,000

(d) Wakati wa mapitio ya jinsi miradi ya CSR ilivyotekelezwa kati ya Halmshauri ya Mji wa Geita na GGML, timu ya ukaguzi maalum ilitembelea miradi hiyo na kubaini kuwa kuna idadi kubwa ya vifaa vilikuwa vinabaki baada ya mradi kukamilika kutokana na kutokuwa na uandaaji wenye tija wa BOQ za miradi husika kitu kilichopelekea GGML kununua vifaa vingi kuliko mahitaji kwa jumla ya Sh. 50,059,074. Pia H/W haikuwa na mpango mkakati wa kuvitumia vifaa hivi

,hivyo hakukuwa na thamani ya fedha kwa vifaa hivi vilivyobaki.

(e) Jengo la Machinjio la Mpomvu haliendani na thamani ya fedha kwani jengo hilo limejengwa kwa Sh. 25,000,000 lakini baada kulitemblea jengo hilo pamoja na timu ya wahandisi nilibaini jengo hili lina thamani ndogo kuliko gharama iliyotumika ya Sh.25,000,000

(f) Pia kulikuwa na Hasara ya Sh.30,516,668 ambayo ilitokana na H/M Geita kushindwa kusimamia vizuri mradi wa ujenzi wa machinjio Mpovu na hivyo kusababisha Mkandarasi Home Africa Kushindwa kumaliza kwa wakati na hivyo kupelekea Mkandarasi Mshauri Geometry Ltd kuongezewa muda wa kwa gharama ya Sh. 30,516,668

13.3.3.31 Miradi ya maendeleo iliyokamilika lakini haitumiki yenye thamani ya Sh. 3,467,436,715

Ukaguzi maalumu ulibaini uwepo wa Miradi ya maendeleo iliyokamilika lakini haitumiki kwa malengo yaliyotarajiwa zenye thamani ya jumla ya Sh. 3,467,436,715 kama ilivyo kwenye orodha ifuatayo:

(a) Majengo ya upasuaji na chumba cha kuhifadhia maiti ya kituo cha Afya Kasamwa zenye thamani ya Sh.400,000,000

(b) Soko la wafanyabiashara wadogo wadogo Geita lililogharimu Sh.650,000,000

(c) Majengo ya Chuo cha Ujasiriamali cha Magogo kupitia mradi wa CSR yaligharimu Sh. 2,417,436,715

Ninapendekeza kwamba hatua zinazofaa zichukuliwe dhidi ya maafisa ambao waliunda sehemu ya kamati ya tathmini na wajumbe wa Bodi za Zabuni kwa kumuengua isivyohalali mzabuni aliyekuwa na bei ya chini katika mchakato wa zabuni hivyo kuisababishia Halmashauri hasara na wale wote walioshindwa kusimamia mkataba kwa ufanisi. Aidha, ninashauri uongozi wa Halmashauri kuchukua hatua stahiki za kutumia miradi yote iliyokamilishwa ili kufikia lengo lililokusudiwa na kupata thamani ya fedha katika miradi hiyo.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

13.3.3.32 Kutokukusanywa Kikamilifu kwa Ushuru wa Mazao ya Misitu Sh. 2,141,829,191

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo haina mfumo au utaratibu mahsusi unaoweza kusaidia kujua bei ya mauzo ya nguzo na idadi ya nguzo zinazouzwa na kampuni zinazojihusisha na uchakataji wa mbao na mauzo ya nguzo. Kwa sababu hiyo nilibaini kuwa, kati ya jumla ya ushuru uliotakiwa kulipwa na kampuni wa Sh. 3,141,829,191 kwa muda wa miaka mitatu ya fedha kuanzia 2017/18 hadi 2019/20, Halmashauri ilikusanya kiasi cha Sh. 1,000,000,000 pekee na hivyo kushindwa kukusanya kiasi cha Sh. 2,141,829,196 ikiwa ni 5% ya mauzo baada ya kupunguza gharama za usafiri.

13.3.3.33 Fedha za Miradi Kutumika kwa Matumizi Mengine Sh.210,129,530

Katika mwaka wa fedha 2016/17 na 2017/18 Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo iliingia mkataba na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Kilolo kwa mikataba yenye jumla ya Sh. 4,202,389,627. Katika malipo yaliyofanywa ili kuwalipa wakandarasi kwa kazi walizofanya kwa mujibu wa mikataba, Halmashauri walikata asilimia 5% ya malipo kiasi cha Sh. 210,129,530 kama fedha ya matazamio na kuzihifadhi kwenye akaunti ya Amana na akaunti ya maendeleo. Hata hivyo nilibaini kuwa fedha hazikuwepo kwenye account ya amana na wala hazikulipwa kwa wakandarasi kama dhumuni la kukata fedha hiyo lilivyokuwa na badala yake zilitumika katika matumizi ambayo hayakufahamika.

Ninapendekeza kuwa menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ifanyike upembuzi yakinifu wa namna sahihi ya kukusanya ushuru wa mazao ya misitu ili kuiongezea Halmashauri ya Wilaya mapato ya ndani na kuziboresha Sheria ndogo ndogo za Halmashauri. Aidha ninapendekeza Halmashauri irejeshe fedha za zuio kiasi cha Sh. 210,129,530 ilizozitumia kwa matumizi yasiyostahili. Vilevile Kutokana na mapungufu tajwa hapo juu nazishauri mamlaka husika

kuwachukulia hatua stahiki watu wote waliohusika na mapungufu haya kama inavyoonekana katika taarifa maalum za ukaguzi wa Halmashauri hii.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

13.3.3.34 Fedha za Matazamio za Miradi ya Mpango wa Uboreshaji Miji katika Serikali za Mitaa (ULGSP) Kutumika Kinyume na Matumizi Yake Sh. 1,078,815,035

Nilikagua malipo yaliyokuwa yakifanywa kwa wakandarasi katika utekelezaji wa miradi ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na kubaini kuwa jumla ya Sh. 1,078,815,035 zilikatwa kama fedha za matazamio kwa miradi ya Mpango wa Uboreshaji Miji katika Serikali za Mitaa (ULGSP) kwa kandarasi. Kati ya fedha hizo zilizokatwa, jumla ya Sh. 812,433,893 zilipelekwa kwenye akaunti ya amana ya Halmashauri na Sh. 266,381,142 zilikatwa kwenye malipo na kuachwa kwenye akaunti ya Maendeleo ya Halmashauri. Nilipitia salio lililopo katika akaunti ya Amana na Akaunti ya Maendeleo ya Halmashauri na kubaini kuwa Akaunti ya Maendeleo ilibakiwa na bakaa la Sh. 34,024 wakati akaunti ya Amana ilikuwa na bakaa la Sh. 4,336,888 tu. Ukaguzi wangu ulibaini pia kuwa fedha za matazamio hazikuwa zimelipwa kwa wakandarasi waliokatwa fedha hizo kwani sikuweza kupata ushahidi wa malipo hayo. Kwa mantiki hiyo ni wazi kuwa jumla ya Sh. 1,078,815,035 zilikuwa zimetumika katika matumizi mengineyo.

13.3.3.35 Kughushiwa kwa Nyaraka za Zabuni na Ununuzi bila ya Ushindani katika Kuwapata Wataalamu Washauri Kulikopelekea Kuingiwa kwa Mikataba Miwili Yenye Thamani ya Sh. 85,900,000

(a) Mkataba wa Kufanya Upembuzi Yakinifu (Feasibility Study) kwa Ajili ya Ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi na Ukumbi wa Mikutano

Tarehe 30 Desemba, 2019, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa iliingia mkataba na Mtaalam Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga jengo la kitega uchumi na ukumbi wa mikutano kwa gharama ya Sh. 54,400,000, ambapo mkataba ulikuwa unatakiwa kutekelezwa ndani ya siku 90 kuanzia tarehe

30 Disemba, 2019. Katika kupitia mkataba huu nilibaini kuwapo na mapungufu kadhaa kama ifuatavyo: -.

(i) Zabuni hii ilikuwa na ushindani wa wataalamu washauri watatu waliosadikika kuleta wasifu na makadirio ya gharama. Katika kutaka kujiridhisha juu ya uwepo wa uwazi, haki na ushindani wa ukweli katika mchakato wa uzabuni huu nilifanya mawasiliano kwa njia ya simu na barua pepe na wataalamu washauri waliohusishwa katika mchakato wa zabuni mpaka kumpata mkandarasi aliyekuwa na bei ya chini. Katika kufanya hivyo nilibaini kuwa nyaraka zilizosadikika kuwasilishwa na washindani hao wawili ambazo ni pendekezo la kitaalam (technical proposal) na makadirio ya gharama (financial proposal) zilikuwa zimeghushiwa kwa kuwa wataalamu washauri hao walikana kushiriki katika kuandaa nyaraka husika na wala hawakuwa wamejulishwa wala kufahamu kuwepo kwa zabuni hiyo.

(ii) Vilevile, katika hali isiyo ya kawaida nilibaini kuwa Mtaalamu Mshauri aliwasilisha taarifa ya kazi yake tarehe 09 Januari, 2020 ikiwa ni siku tisa tu baada ya kusaini mkataba huo mnamo tarehe 30 Disemba, 2019; huku mkataba ukiwa ni wa siku tisini (90) kitendo kilichoashiria kazi ilianza kabla ya mkataba kusainiwa. Katika kufanya mahojiano na Mtaalam Mshauri huyo, alieleza kuwa alipata kibali cha kuanza kazi mwezi Agosti, 2019 (japo hakuweza kuwasilisha ushahidi wa hilo).

(b) Mkataba wa Sh. 30,870,000 wa Kuwajengea Uwezo Wahasibu Kuhusu Ukusanyaji wa Mapato na Usimamizi Bora wa Mifumo ya Fedha

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, ilimlipa Mtaalam Mshauri jumla ya Sh. 30,870,000 kupitia hati ya malipo Na.72004V2001821 ya tarehe 29 Januari, 2020 kwa ajili ya kuwajengea uwezo wahasibu kuhusu ukusanyaji wa mapato na usimamizi bora wa mifumo ya fedha wenye thamani ya Sh. 30,870,000.

Katika kupitia mchakato wa upatikanaji wa mtaalam mshauri aliyeshinda zabuni hiyo, nilifanya mawasiliano baina ya wahusika waliosadikika kushindanishwa katika zabuni hii, ambapo walikana kuhusika wala kuifahamu zabuni hii. Vilevile, baada ya jitahada za kumtafuta mzabuni mwingine aliyekua katika zabuni hii kukwama, niliamua kufanya mawasiliano na moja ya vyuo vikuu nchini aliposadikika kufanya kazi kwa mujibu wa wasifu ulioambatishwa kwenye kabrasha la zabuni. Hata hivyo, baada ya mawasiliano na Chuo husika, nilijulishwa kuwa mtaalamu huyo hawamtambui na kwamba hajawahi kuwa mkufunzi wa chuo hicho hata kwa kazi ya muda (part time), jambo lililoashiria udanganyifu katika mchakato mzima wa kumpata mzabuni.

Kutokana na madhaifu yaliyo ainishwa hapo juu hasa kuzingatia kughushiwa kwa nyaraka za zabuni ninashauri kuwa mamlaka husika zifanye uchunguzi na kuwachukulia hatua stahiki watu wote waliohusika katika mapungufu tajwa hapo juu. Vile vile Menejimenti ya H/M ya Iringa inashauriwa ichukue hatua stahiki za kutengeneza mifumo imara ya utangazaji, upokeaji, na kufanyika kwa tathmini mpaka kuwapata wazabuni.

HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA

13.3.3.36 Kutopokelewa kwa vifaa tiba kutoka bohari ya dawa (MSD) vyenye thamani ya Sh. 1,084,825,580

Kwa mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 Halmashauri kupitia vituo vya afya Kishanje, Katoro na Maruku ilipokea vifaa tiba vyenye jumla ya Sh. 347,103,250. Vifaa tiba hivi ni sehemu ya jumla ya vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. 1,431,928,830 vilivyopaswa kupokelewa kutoka bohari ya madawa (MSD) kwa ajili ya huduma ya dharura ya uzazi na watoto wachanga (CEmONC) ambapo kila kituo kilipaswa kupokea vifaa vyenye thamani ya Sh. 477,309,610. Kwa mantiki hiyo nilibaini kuwa vifaa ambavyo havijapokelewa hadi ukaguzi wangu unakamilika vina thamaani ya Sh. 1,084,825,580. Kutokupelekwa kwa vifaa tiba hivyo kunasababisha majengo mengi yaliyojengwa kushindwa kuanza kutoa huduma kwa wananchi kwa wakati.

Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba inapaswa kuchukua hatua stahiki za ufuatiliaji wa vifaa tiba hivyo, na kuhakikisha kuwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) inapeleka vifaa tiba kama vilivyoagizwa vikiwa na maelekezo na idadi sahihi bila kuchelewa. Vilevile,ninashauri kuwa OR-TAMISEMI wakishirikiana na mamlaka zingine ikiwa ni pamoja na Wizara ya Afya kutengeneza mifumo sahihi ili kuweza kulimaliza tatizo hili ambalo limekuwa likijirudia mara kwa mara.

HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE

13.3.3.37 Wafanyabiashara Kutokuwa na Mikataba ya Upangaji Katika Vibanda 110 vya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe

Katika kupitia taarifa za makusanyo ya mapato yatokanayo na pango la vibanda vya biashara katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kwa mwaka wa fedha 2017/18, hadi 2019/20, nilibaini kuwa Halmashauri ina jumla ya vibanda 260 vya biashara katika maeneo ya Kayanga na Omurshaka. Vibanda hivyo vinatumiwa na wafanyabiashara mbalimbali ambapo kati ya hivyo vibanda 150 vina mikataba ya upangaji na Halmashauri na vibanda 110 havina mikataba ya wapangaji na Halmashauri. Kutokuwepo kwa mikataba ya upangaji wa vibanda vya Halmashauri kunaweza kusababisha wafanyabiashara kukwepa kulipa kodi ya pango au kusababisha watumishi wa Halmashauri kujiingizia kipato binafsi kupitia mali za Halmashauri kinyume na taratibu na hivyo kuisababishia Halmashauri kukosa mapato.

Ninapendekeza kuwa uongozi wa Halmashauri uchukue hatua zote stahiki ili kuwezesha kuletwa kwa vifaa tiba kutoka MSD na kuhakikisha kuwa MSD wanatekeleza majuku yao kama walivyopewa mahitaji na Halmashauri.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA

13.3.3.38 Manunuzi ya Gari la Kubebea Taka Ngumu Bila Ushindanishi wa Bei na Lenye Mapungufu Mbalimbali Sh. 175,000,000

Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ilinunua gari la kubebea taka ngumu lenye uzito wa tani 22 kutoka kwa kampuni ya uuzaji wa magari kwa gharama ya Sh. 175,000,000 bila ya kuwepo kwa

ushindani. Halmashauri kupitia tangazo la zabuni Na. LGA.101./2019/2020/CQ/G/01 la tarehe 23 Machi, 2020 ilitoa mwaliko wa nukuu ya bei kwa kampuni moja pekee.

Aidha, nilibaini kuwa maamuzi ya kutunuku zabuni yalifanyika kabla ya zabuni hiyo kutangazwa. Kati ya Sh. 175,000,000 zilizotakiwa kulipwa kwa mzabuni kwa ajili ya manunuzi ya lori hilo, nilibaini kuwa Halmashauri ilitoa malipo ya awamu ya kwanza ya Sh. 100,000,000 kupitia Hati ya Malipo Na. 362027V2001509 ya tarehe 20 Aprili, 2020, hivyo kubaki na deni la Sh. 75,000,000 ingawa gari lilipokelewa tarehe 09 Aprili, 2020.

13.3.3.39 Malipo Hewa Kwa Ajili ya Utengenezaji wa Sanamu za Wanyama (Twiga Mweupe na Kiboko) Sh. 4,000,000.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ilimchagua na kufanya makubaliano na mzabuni, kwa ajili ya kutengeneza sanamu za wanyama (Twiga Mweupe na Kiboko) kwenye eneo la mzunguko wa Hotel ya Mpanda, kwa gharama ya Sh 4,000,000. Hata hivyo, nilibaini kuwa mnamo tarehe 15 Mei, 2020, Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 4,000,000 kupitia hati ya madai namba 362027V2001659 kwa mzabuni mwingine tofauti na yule aliyekuwa na mkataba na Halmashauri.

Aidha, tarehe 23 Julai, 2020, timu ya ukaguzi ilitembelea eneo la mzunguko wa Mpanda Hotel, mahali palipokusudiwa kujengwa sanamu hizo na kubaini kuwa, kazi hizo hazijafanyika kwa kuwa hapakuwa na sanamu zilizowekwa.

Ninaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kuhakikisha kuwa wazabuni wanashindanishwa ili kupata bei shindani na bidhaa na huduma zenye ubora na thamani ya fedha. Endapo mzabuni mmoja atatumiwa katika manunuzi, lazima kuwepo na ushahidi kuthibitisha uhalali wa maamuzi hayo. Vilevile ninaishauri Halmashauri kuhakikisha kuwa inachunguza tukio la kumlipa mzabuni mwingine badala ya mzabuni aliyekuwa na Mkataba na Halmashauri. Pia Halmashauri iangalie uwezekano wa kuweza kurudishiwa fedha alizolipwa mzabuni husika kwa kuwa hakuweza kutekeleza kazi iliyokusudiwa.

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE

13.3.3.40 Malipo Yaliyofanywa kwa Mkandarasi Bila Uthibitisho wa Thamani ya Kazi Zilizofanyika Sh. 88,440,305.90

Nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe ilifanya malipo ya Sh. 88,440,305.90 kwa Mkandarasi kwa ajili ya mkataba wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Buhigwe. Hata hivyo, nyaraka za malipo zilizotumika kumlipa mkandarasi huyo, hazikuambatana na mchanganuo wa kazi zilizofanywa na vipimo (measurement sheets), ili kuthibitisha kiasi cha malipo yaliyostahili kulipwa.

13.3.3.41 Malipo yaliyofanyika kwa mzabuni asiyekuwa na mkataba na Halmashauri Sh. 23,792,000.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe iliingia mkataba na mzabuni kwa ajili ya kutengeneza na kuweka milango katika jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kwa gharama ya Sh. 23,792,000. Hata hivyo, malipo yalifanyika kwa mzabuni mwingine ambaye hakuwa na mkataba na Halmashauri hiyo.

Ninaishauri menejimenti ya Halmashauri kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na kuhakikisha kuwa malipo yote ya kazi zilizofanyika yanaambatishwa na uthibitisho wa kufanyika tathmini ya vipimo kujiridhisha kwamba malipo yamefanyika kwa kazi ambazo zimekamilika tu. Vilevile Ninashauri mamlaka husika kuchukua hatua stahiki dhidi ya maafisa wa Halamashauri waliotajwa katika taarifa rasmi ya ukaguzi wa Halmashauri hii kwa ushiriki wao wa kuomba, kuidhinisha na kufanya malipo bila ya kuwepo kwa tathmini ya vipimo vya kazi zilizofanyika na kumlipa mkandarasi fedha nyingi kuliko kiasi cha mkataba.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU

13.3.3.42 Hasara Iliyosabishwa na Kuwalipa Wakusanya Mapato isivyostahili Sh. 16,997,890

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ililipa kiasi cha Sh. 20,680,000 kwa mawakala wa kukusanya mapato kama ujira

(commission) ya ukusanyaji mapato. Hata hivyo, nilibaini kuwa kwa mujibu wa mkataba, Halmashauri ilipaswa kuwalipa mawakala hao kiasi cha Sh. 3,682,110 tu, kwa kuwa hawakuwa wamefikia vigezo vinanyostahili kulipwa zaidi ya hapo. Kwa hatua hiyo, Halmashauri iliingia hasara ya Sh. 16,997,890 kwa kufanya malipo kinyume na mkataba.

13.3.3.43 Kuidhinisha na Kupitisha Malipo kwa Mafundi wa Ujenzi Bila Kupima Ukubwa wa Kazi Zilizofanyika Sh. 221,411,951.32

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu nilibaini uwepo wa malipo ya jumla ya Sh. 221,411,951.32 kwa mafundi wa ujenzi, waliolipwa bila kupima ukubwa wa kazi zilizofanyika. Malipo hayo yalihusisha mafundi wa ujenzi katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu Sh. 146,327,571.32 na Kituo cha Afya Nyamidaho Sh. 75,084,380. Kufanya malipo bila kuzingatia ukubwa wa kazi kunaweza kupelekea Halmashauri kupata hasara kwa kuwalipa wakandarasi na mafundi ujenzi fedha nyingi kuliko kazi iliyofanyika.

13.3.3.44 Malipo Yaliyofanyika Zaidi ya Kiasi cha Mkataba kwa Mafundi Sh. 76,675,687

Nilibaini kuwa Jumla ya Sh. 316,647,212, zililipwa kwa mafundi ujenzi saba, ikiwa ni zaidi ya kiasi cha makubaliano yaliyohusu ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Kwa mujibu wa mkataba, mafundi ujenzi hao walipaswa kulipwa Sh. 239,971,524 tu; hata hivyo, Halmashauri iliwalipa kiasi cha ziada cha Sh. 76,675,687 bila uthibitisho wa sababu za kufanya hivyo. Kwa kufanya hivyo Halmashauri ilipata hasara kwa malipo hayo yasiyo akisi ukweli wa kazi iliyofanyika.

Ninapendekeza kwamba, katika siku zijazo, Wahasibu, Mwanasheria wa Halmashauri, Timu ya ukusanyaji wa Mapato pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wazingatie mikataba ya kukusanya mapato iliyoingiwa kabla ya kufanya malipo. Pamoja na kuimarisha udhibiti wa ndani kama hatua ya kushughulikia udhaifu uliojitokeza katika Ukaguzi huu, ninapendekeza kuwa hatua stahiki zichukuliwe kwa wale maafisa ambao hawakutimiza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kusababisha hasara kwa Halmashauri.

HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA

13.3.3.45 Vitabu 163 vya Mapato ya Ndani Havikuwasilishwa kwa Ajili ya Ukaguzi

Katika tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani wa Halmashauri juu ya utolewaji na urudishwaji wa vitabu vya kukusanyia mapato, nilibaini kuwa kuanzia mwaka 2013 hadi mwaka 2016, Mtunza Fedha Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza alikabidhiwa vitabu 163 *(open receipt books)* kwa ajili ya kukusanya mapato. Hata hivyo, uongozi wa Halmashauri ulieleza kuwa haujui vitabu hivyo vilipo na wala havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Kwa hatua hiyo, nilishindwa kubaini iwapo vitabu hivyo vilitumika kukusanya mapato au la, na kama vilitumika, kiasi gani kilikusanywa.

13.3.3.46 Malipo Yaliyofanyika kwa Mafundi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Bila Kuonesha Vipimo vya Kazi na Mchanganuo wa Kazi Zilizofanyika Zenye Thamani ya Sh. 130,986,445

Nilipitia hati za malipo zilizotumika katika kufanya malipo ya mafundi ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na kubaini kuwa malipo ya Sh. 130,986,445 yalifanyika kwa kazi mbalimbali. Katika kupitia hati hizo na nyaraka zilizoambatanishwa kwenye hati za malipo hayo nilibaini kuwa malipo yaliidhinishwa na kulipwa bila kuwepo kwa vyeti vinavyoonesha kazi zilizofanyika (interim payment certificate), na baadhi ya malipo yaliyofanyika kwa kutumia vyeti vya kazi bila kuonesha orodha ya kazi zilizofanyika (valuation sheets) na vipimo vya kazi hizo (measurement sheets). Vilevile, nilibaini pia kuwa kuna hati ambazo hazikukamilika kwa kusainiwa na watu wote waliopaswa kuzisaini.

13.3.3.47 Kodi ya Zuio Kutowasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania Sh. 17,009,255

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza haikuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania fedha kiasi cha Sh. 17,009,255, ikiwa ni kodi ya zuio iliyokatwa kutoka kwa watoa huduma na wazabuni mbalimbali katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2018/19 na mwaka 2019/20.

13.3.3.48 Hasara Iliyotokana na Kutokukatwa kwa Mrabaha wa Madini na Ada ya Ukaguzi Madini Ujenzi Sh. 10,788,480

Kinyume na kifungu Na.87 cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 yakisomwa pamoja na Kipengele Na.7 cha mikataba ya ugavi wa madini ujenzi, nilibaini kuwa kulikuwa na uzembe katika kukata kiasi cha mrabaha kutoka kwenye malipo ya wazabuni wa madini ujenzi yaliyotumika kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na hivyo kuiingiza Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza hasara ya kiasi cha Sh. 10,788,480 kwa kulipa mrabaha ambao ulitakiwa kulipwa na wazabuni wenyewe.

13.3.3.49 Mabadiliko ya Aina ya Msingi wa Hospitali ya Wilaya Bila Idhini Yaliyoongeza Gharama za Ujenzi kwa Sh. 83,588,400

Kinyume na angalizo lililopo katika michoro yote ya usanifu (structural drawings) kinachotaka mabadiliko au mapungufu yoyote ya ramani kupata kibali kutoka kwa Mhandisi wa Usanifu wa OR-TAMISEMI, nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza ilibadili urefu wa kina cha kwenda chini cha msingi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya kutoka mita 1 (230mm ikiwa ni zege na 770mm ikiwa ni tofali) na badala yake kujenga kina kisichozidi 750mm; na pia ilijenga msingi wa mawe badala ya ule wa zege na tofali uliopendekezwa na OR-TAMISEMI na hivyo kusababisha gharama za kujenga msingi kuongezeka kwa Sh. 83,588,400 kutoka Sh. 94,104,680 hadi Sh. 177,693,080 sawa na ongezeko la asilimia 88, bila ya kupata kibali

Ninapendekeza kuwa Mamlaka zinazohusika ziwachukulie hatua stahiki watumishi wote waliotajwa katika taarifa mahsusi ya ukaguzi huu maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza kwa kuhusika kwao katika matumizi mabaya ya fedha za Umma.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO

13.3.3.50 Upotevu wa Fedha za Mfuko wa Jimbo Kutokana na Kulipa Malipo Yasiyostahili Sh. 76,106,000

Nilibaini kuwa Jumla ya Sh. 76,106,000 za kuchochea maendeleo ya jimbo zililipwa kwa vikundi vya wajasiriamali na kukopeshana kinyume na Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2009, inayoelekeza fedha hizo kutumika kwenye miradi ya maendeleo inayohusisha jamii kwa upana wake; na iwe imependekezwa na jamii kutoka kwenye maeneo husika na kuidhinishwa na Kikao cha Maendeleo ya Kata (WDC). Aidha, vielelezo vya matumizi ya fedha hizo havikuwasilishwa kwangu kwa ajili ya uhakiki.

Ninatoa wito kwa mamlaka husika kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wa Halmashauri waliohusika katika kufanyika matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo yasiyostahili kama walivyotajwa kwenye ripoti ya ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

13.3.3.51 Mapokezi ya Fedha za Mradi Kutoka UNCDF Yasiyothibitishwa USD 238,000

Nilibaini kuwa UNCDF iliingia makubaliano ya kuisaidia Halmashauri ya Manispaa ya Moshi jumla ya Dola za Kimarekani 238,000 sawa na Sh. 547,400,000 ili kuiwezesha Manispaa ya Moshi kuweka mtaji (Equity) katika kampuni yake tanzu iliyojulikana kwa jina la 'Moshi City Development Company (MOCIDECO). Kupitia barua yenye Kumb.Na.MMC/CL.40/4/83 ya tarehe 20 Disemba, 2017, nilibaini kuwa Halmashauri ilimjulisha Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro juu ya kupokelewa kwa Dola za Kimarekani 238,000 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa kituo cha Ngangamfumuni.

Hata hivyo, nilibaini kuwa taarifa iliyotumwa kwa Katibu Tawala ilitaja akaunti tofauti na akaunti zilizokuwa zimewekwa kwenye mkataba wa makubaliano baina ya UNCDF na Manispaa ya Moshi. Kwa mkutadha wa mkanganyiko huo, ilinibidi kufanya uhakiki

kupitia taarifa za kibenki (Bank statements) nilizoziomba kwa Uongozi wa Benki husika juu ya uwepo wa akaunti husika na endapo miamala hiyo iliwekwa na UNCDF. Baada ya kupokea taarifa husika na mawasiliano niliyofanya na uongozi wa Benki nilibaini kuwa akaunti zote mbili zenye majina MOSHI CITY DEVELOPMENT SPECIAL COMPANY na MOSHI CITY DEVELOPMENT hazikuwahi kupokea miamala hiyo na kwamba akaunti yenye jina la MOSHI CITY DEVELOPMENT SPECIAL COMPANY ilifunguliwa na kufungwa bila kufanya miamala.

Kutokana na mkanganyiko huo, nimeshindwa kufahamu iwapo fedha tajwa zilitolewa na mfadhili au bado hazijatolewa, na iwapo zimetolewa zimekwenda kwenye Akaunti gani na nani anawajibika kwa kitendo hicho. Vile vile nimeshindwa kujua sababu za kufunguliwa kwa akaunti nyingine yenye majina karibu sawa na akaunti aliyopewa mfadhili kuweka fedha. Lakini pia, endapo fedha hizo hazikutolewa, nimeshindwa kujua sababu za kumpa taarifa za uongo Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro.

13.3.3.52 Hasara Itokanayo na Mafundi Kulipwa Zaidi ya Kiwango cha Mkataba Sh. 73,022,583

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi iliwalipa mafundi jamii jumla ya Sh. 202,067,848, kinyume na kiasi cha mkataba cha Sh. 129,045,265 na kusababisha hasara ya jumla ya Sh. 73,022,583. Kazi husika zilijumuisha ujenzi wa kituo cha afya eneo la Pasua Sh. 68,653,483, na ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Moshi Sh. 4,369,100, bila ya uthibitisho wa ongezeko la kazi

Kulingana na makosa yaliyotajwa hapo juu, ninapendekeza wahusika wote waliotajwa katika ripoti ya ukaguzi wachukuliwe hatua stahiki kwa udanganyifu wa malipo walioufanya na kuisababishia Serikali hasara ya Sh. 73,022,583. Vilevile, Uongozi wa Halmashauri unashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuweza kurejeshwa kiasi cha fedha kilicholipwa kimakosa kwa mkandarasi.

13.3.3.53 Ubadhirifu wa Fedha za Ada ya Leseni Ambazo Hazijarejeshwa na Maafisa Biashara Sh. 80,476,833

Nilipitia taarifa za ukusanyaji wa mapato ya kasma ya ada za leseni za biashara pamoja na jalada lenye mkataba wa tarehe 12/09/2019 wenye makubaliano baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha na watumishi waliokuwa maafisa biashara wa Halmashauri na kubaini kuwa Maafisa biashara wawili walithibitika kufanya ubadhirifu wa fedha za leseni za biashara, kiasi cha Sh. 80,476,833 na, hivyo, kuamriwa kuzirejesha; lakini hadi ukaguzi unakamilika mnamo mwezi Agosti, 2020, fedha hizo zilikuwa bado hazijarejeshwa.

13.3.3.54 Udanganyifu Katika Maombi ya Nyongeza ya Fedha za Ujenzi wa Hospitali kwa Kazi Ambazo Zilikwishafanyika Sh. 44,103,200

Nilipitia taarifa ya ujenzi wa majengo saba ya hospitali ya wilaya kwenye barua yenye kumb. Na.SDC/B.10/7/67 ya tarehe 18 Novemba, 2019 iliyoandikwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kwenda kwa Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kuhusu nyongeza ya fedha Sh. 370,040,765 kwa ajili ya umaliziaji wa majengo saba ya Hospitali ya Wilaya ya Siha.

Hata hivyo, mapitio ya taarifa husika yalibaini kuwa Halmashauri, iliweka gharama ya Sh. 44,103,200 kwa shughuli ambazo zilikuwa zimeshafanyika katika awamu ya kwanza na hivyo kufanya udanganyifu wa jumla ya Sh. 44,103,200.

13.3.3.55 Hasara Iliyotokana na Wizi wa Vifaa vya Ujenzi Katika Eneo la Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Sh. 14,169,320

Ukaguzi wa malipo ya vifaa vya ujenzi, nyaraka za mapokezi ya vifaa vya ujenzi pamoja na Mihtasari ya kamati ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Siha pamoja na mapitio ya Mihustasari ya kamati za ujenzi ulibaini hasara ya jumla ya kiasi cha Sh. 14,491,804. Hasara hiyo ilitokana na wizi uliotokea stoo ya kuhifadhia vifaa ambapo jumla ya vifaa vyenye thamani ya Sh. 12,840,640 viliibiwa; huku vifaa vyenye thamani ya Sh. 1,328,680

vikiwa havionekani na havikujulikana vilipo wakati wa zoezi la uhakiki.

13.3.3.56 Ubadhirifu wa Fedha Taslim za Uboreshaji wa Daftari la Mpiga Kura Jumla ya Sh. 18,673,000

Mnamo tarehe 29 Juni, 2019, Halmashauri ya Wilaya ya Siha kupitia Akaunti ya Amana Na. 40110000772 ilipokea kiasi cha Sh. 177,300,000 na kukiri mapokezi ya fedha husika kwa stakabadhi Na. 753103C19000113. Fedha hizi zilitokea Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa ajili ya uboreshaji wa daftari la wapiga kura. Aidha, hadi kufikia tarehe 12 Julai, 2020 nilibaini kuwa jumla ya Sh. 164,244,000 zilikuwa zimetolewa benki kwa ajili ya matumizi ya shughuli za uboreshaji wa daftari la wapiga kura; kiasi kilichobaki cha jumla ya Sh. 13,056,000 kilirejeshwa kwenye Akaunti ya Tume ya Uchaguzi Akaunti ya Maendeleo Na. 9921190701.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kati ya mwezi Julai na Agosti, 2019 Halmashauri ilitoa jumla ya Sh. 83,918,000 ambazo zilitumika kugharamia shughuli za uboreshaji wa daftari la kudumu la mpiga kura; kati yake Sh. 65,245,000 zilithibitika kutumika kwenye zoezi hilo na aliyekuwa mtunza fedha mkuu wa Halmashauri. Kiasi cha Sh. 18,673,000 ikiwa ni fedha zilizobaki kilipaswa kurejeshwa benki, lakini matumizi yake hayakuthibitishwa kutumika wala hakikurejeshwa kwenye akaunti ya Tume ya kupigia kura.

Kwa kuzingatia mapungufu yaliyobainishwa hapo juu, ninapendekeza kuwa:

- **Katibu Mkuu -TAMISEMI na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro washirikiane na kuwachukulia hatua stahili wahusika wote waliotajwa kwenye ripoti ya ukaguzi maalumu na warejeshe kiasi cha fedha kilichokuliwa kutokana na uzembe kama ilivyokubalika kwenye makubaliano yaliyosainiwa tarehe 12 Septemba 2019.**

- **Pia, menejimenti za Halmashauri zinahimizwa kusimamia na kufuatilia miradi yote inayotekelezwa kwa utaratibu wa "Force Account" na kuhakikisha kuwa miradi hiyo wanapewa mafundi wenye uzoefu.**

- **Katibu Mkuu -TAMISEMI na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro wanashauriwa kuweka utaratibu ambao utawezesha fedha zilizochukuliwa Sh. 18,673,000 zirejeshwe na wahusika wote waliotajwa kwenye ripoti za kaguzi maalumu.**

HALMASHAURI YA WILAYA SAME

13.3.3.57 Malipo Yaliyofanywa kwa Makandarasi wa Miradi ya Maji Isivyostahili Sh. 51,000,000

Nilibaini kuwa Sh. 39,000,000 za miradi ya maji zililipwa kwa wakandarasi mbalimbali kama malipo ya gharama ya kuweka dhamana ya kazi (performance guarantee), wakati gharama hizo ni wajibu wa mkandarasi. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Same ililipa kiasi cha Sh. 12,000,000 kwa wakandarasi kwa ajili ya kuweka bima. Hata hivyo, hakuna ushahidi wa miradi hiyo kukatiwa bima na hivyo kusababisha malipo hayo kulipwa kwa wakandarasi isivyostahili. Malipo hayo yote yaliingizwa katika makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ) wa miradi ya maji na kulipwa.

13.3.3.58 Hasara Iliyotokana na Kutotumika kwa Betri na Kupotea kwa Betri na Paneli za Umeme wa Jua katika Mradi wa Maji Hedaru Sh. 51,980,000

Halmashauri ya Wilaya ya Same iliingia mkataba wa kufunga mitambo ya kutumia umeme wa jua katika visima viwili pamoja na tenki la kupokelea maji kabla ya kupandishwa kwenda tenki kuu 'Booster,' kupitia mkataba Na.LGA/049/W/WSDP/2013/14/11 Lot VII, wenye thamani ya Sh. 255,979,835.

Hata hivyo, baada ya kutembelea na kukagua mradi wa maji Hedaru, nilibaini kuwa betri 77 na panel nne (4) za umeme wa jua katika visima vya Maboma na Hedaru 'A', zenye thamani ya Sh. 31,400,000 zilikuwa zimeibiwa. Aidha, nilibaini kuwepo kwa betri 45 katika tenki la kusukuma maji 'Booster' zenye thamani ya Sh. 20,700,000, ambazo hazikuwa zikitumika baada ya kukosa ufanisi, hivyo kulazimu paneli za umeme wa jua kuunganishwa moja kwa

moja kwenye pampu hali iliyopelekea hasara ya jumla ya Sh. 51,980,000 kwa Halmashauri hiyo.

Ninapendekeza kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kushirikiana na menejimenti ya Wilaya ya Same wahakikishe kuwa wakandarasi wanarejesha jumla ya fedha zote za bima za miradi na dhamana ya bima ya utendaji. Pia, wakandarasi wana wajibu wa kuthibitisha matumizi ya fedha za bima za mradi zilizotolewa kwao kwa kuwasilisha mikataba ya bima na dhamana ya bima ya utendaji.

Kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na vyombo vingine ya uchunguzi, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro anashuariwa kuwafuatilia wahusika wote walioharibu miundo mbinu ya maji kwa kuiba betri za sola kwenye visima vya maji.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

13.3.3.59 Kutokurejesha Fedha za Malipo ya Awali Baada ya Mkandarasi Kushindwa Kufanya Kazi Kadri ya Matakwa ya Mkataba Sh. 92,088,610

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi iliingia mkataba Na. LGA-53/2015/2016/HQ/W/24 mnamo tarehe 30 Aprili, 2016, kwa ajili ya ujenzi wa machinjio ya kisasa katika eneo la Ngongo. Mkandarasi alipokea malipo ya awali ya Sh. 92,088,610 mnamo tarehe 23 Juni, 2016 na kutakiwa kukamilisha kazi ndani ya miezi mitatu.

Ukaguzi wangu wa utekelezaji wa mradi huu ulibaini kuwa mkandarasi alishindwa kutekeleza majukumu yake ya kimkataba mpaka kufikia mwisho wa muda wa utekelezaji wa mkataba ikiwa ni pamoja na muda wa miezi sita ya nyongeza aliyopewa. Kufuatia hali hiyo, Halmashauri ilivunja mkataba na mkandarasi huyo mnamo tarehe 27 Aprili, 2017. Nilibaini pia kuwa, mpaka mkataba huu unavunjwa, mkandarasi alikuwa amechimba msingi tu. Kufuatia kuvunjwa kwa mkataba, Halmashauri ilimtaka mkandarasi kurudisha fedha alizokuwa amelipwa kama malipo ya awali, lakini mpaka ukaguzi huu unakamilika mkandarasi alikuwa hajarejesha fedha yeyote.

13.3.3.60 Halmashauri Kutowatoza Wakandarasi Gharama ya Kuchelewesha Kukamilisha Miradi Sh. 507,988,618

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi iliingia mikataba ya kazi mbalimbali na wakandarasi huku mikataba hiyo ikiwa na kifungu kinachotaka kuwakata wakandarasi fedha kama tozo ya kuchelewa kukamilisha miradi husika iwapo miradi hiyo ingechelewa kukamilika. Hata hivyo, nilibaini kuwa wakandarasi hao walichelewa kukamilisha miradi yao; lakini, Halmashauri haikuwatoza tozo ya kucheleweshe kazi kiasi cha Sh. 507,988,618.

13.3.3.61 Malipo Yaliyolipwa Zaidi ya Gharama ya Makubaliano Sh. 24,207,740

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi iliingia Mkataba Na. LGA-053/2017/2018/HQ/W/ kwa kazi ya ujenzi wa machinjio ya kisasa kwa gharama ya Sh. 1,493,144,604. Hata hivyo, nilibaini kuwa Halmashauri ilimlipa mkandarasi Sh. 1,517,352,344 na kusababisha malipo ya ziada juu ya makubaliano ya mkataba kwa Sh. 24,207,740.

Ninapendekeza kwa Mamlaka zinazohusika kuweka utaratibu ambao utahakikisha kiasi cha Sh. 92,088,610 kilicholipwa awali na ambacho hakijarejeshwa kinarejeshwa. Pia, hatua zichukuliwe dhidi ya wafanyakazi wa Halmashauri waliotajwa kwenye ripoti ya ukaguzi maalumu kwa ushiriki wao wa kutokusimamia ipasavyo fedha za serikali.

Ninapendekeza menejimenti za Halmashauri kuwatoza wakandarasi gharama za uchelewashaji Sh. 507,988,618 kwa kushindwa kukamilisha miradi kwa wakati.

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi inatakiwa kuhakikisha kuwa udhibiti wa malipo unafanyika ambapo malipo yatalipwa tu kwa huduma halisi iliyofanyika kwa mujibu wa mikataba. Pia, sababu zitolewe kwa maandishi na kuwasilishwa kwa mamlaka husika kuhusu kiasi cha Sh. 24,207,740 kilicholipwa zaidi ya kazi zilizotekelezwa.

HALMASHAURI YA WILAYA KILWA

13.3.3.62 Fedha za Miradi Kuhamishiwa Kwenye Akaunti Binafsi Sh. 35,994,000

Ukaguzi ulibaini kuwa mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nainokwe, alijihamishia fedha kiasi cha Sh. 15,180,000 zilizokuwa zimekusudiwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya walimu kwenye akaunti yake binafsi katika mwaka wa fedha 2019/20. Vilevile, mnamo tarehe 09 Oktoba, 2018, Mkuu wa Shule ya Msingi Muungano naye alijihamishia jumla ya Sh. 20,814,000 kutoka kwenye akaunti Na.7013700189 iliyoko katika benki ya Shule na kwenda kwenye akaunti yake binafsi.

Kutokana na kukiukwa kwa taratibu za kutumia fedha za Serikali kwenye akaunti binafsi, nilibaini kuwa malipo ya jumla ya Sh. 12,500,500 yalifanyika bila ya kuwepo na ushindanishi wa bei (Single Source). Fedha taslimu kiasi cha Sh. 2,613,000 zililipwa kwa wahusika bila kuwepo uthibitisho wa saini zao. Kiasi cha Sh. 4,354,000 kililipwa kwa watoa huduma mbalimbali bila kuwepo kwa uthibitisho wa viambatisho vyovyote kuonyesha aina ya huduma iliyotolewa na wala hapakuwepo na daftari linaloonesha upokeaji na utoaji wa vifaa vya ujenzi

Napendekeza kwa menejimenti ya Halmashauri kutoa elimu ya fedha na ununuzi kwa wasimamizi wa miradi inayojengwa kwa kutumia ''Force Account''. Pia, menejimenti ya Halmshauri ichukuwe hatua stahili kuhakikisha mkuu wa shule anarejesha kiasi cha Sh. 6,967,000 ambacho walishindwa kuwasilisha nyaraka za matumizi yake.

HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI

13.3.3.63 Kutokutumika kwa Zahanati ya Nkaiti kwa Muda Mrefu Sh. 610,188,846

Mnamo tarehe 16 Desemba, 2017, Halmashauri ya Wilaya ya Babati ilipokea Sh. 400,000,000 kutoka kwa Benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Nkaiti (Jengo la Maabara, Upasuaji, Mama na Mtoto, Kuhifadhi Maiti na Nyumba ya Mtumishi) kilichoanza mwezi Februari 2018 na kukamilika mwezi

Septemba, 2018. Pia kwa mwaka huo, Halmashauri ilipokea vifaa tiba vya Sh. 210,188,846 kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD). Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 15 Julai, 2020, ilibainika kuwa jumla ya Majengo matatu yakijumuisha Jengo la mama na mtoto, Jengo la upasuaji na jengo la kuhifadhi maiti yalikuwa hayajaanza kutoa huduma zilizokusudiwa kutokana na kukosa kwa huduma za umeme na maji. Hali hii itasababisha miundombinu ya kituo cha afya kuharibika, vifaa kupotea au kuchakaa na thamani ya fedha iliyowekezwa kwenye miundombinu hiyo kutopatikana.

Napendekeza Katibu Tawala wa Mkoa kwa kushirikiana na Katibu Mkuu-TAMISEMI kuisaidia halmashauri na kuhakikisha kuwa vituo ya afya vilivyojengwa zinakuwa na umeme, maji na magari ya kubebea wagonjwa ili viweze kutoa huduma za afya zilizokusudiwa kwa walengwa.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

13.3.3.64 Ukosefu wa Vitabu 347 vya Kukusanyia Mapato (Open Receipt Books)

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, vitabu 347 kati ya 533 vya kukusanyia mapato (HW5) ngazi za kata na vijiji vilivyotumika kati ya mwaka 2017/18 hadi 2018/19 havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ili kuthibitisha iwapo kiasi cha fedha kilichokusanywa kupitia vitabu hivyo kiliwasilishwa katika akaunti ya benki ya Halmashauri. Hali hii inaashiria kuwa Halmashauri haina mfumo madhubuti wa usimamizi wa mapato ya ndani ya halmashauri yanayokusanywa kwa kutumia vitabu vya mapato.

Menejimenti ya Halmashauri ya Kiteto inashauriwa kutafuta vitabu vya mapato ambavyo havikuonekana na kuviwasilisha Ofisi kwangu kwa ajili ya uhakiki. Pia, ninasisitiza menejimenti kuboresha mifumo ya udhibiti mapato ili kuweza kupunguza mianya ya upotevu wa mapato yaliyokusanywa.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

13.3.3.65 Malipo ya Uwakala wa Mapato Katika Akaunti Binafsi Sh. 188,499,328

Nilibaini kuwa kati ya miaka ya fedha 2018/19 na 2019/20, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ilimlipa Mkurugenzi wa Kampuni ya Uwakala wa kukusanya mapato jumla ya Sh. 188,499,328 kupitia akaunti yake binafsi kinyume na matakwa ya mkataba yaliyotoa akaunti ya kampuni ambayo ndiyo iliyopaswa kutumika kufanya malipo. Kufanya malipo kwenye akaunti binafsi badala ya Kampuni kumeifanya kampuni kutokulipa kodi stahiki zitokanazo na mapato na faida ya kampuni ambapo imebainika kuwa kampuni imekuwa ikiwasilisha ritani tupu (Nil Return of Income) kwa mwaka 2017, 2018 na 2019.

13.3.3.66 Hasara ya Fedha za Mradi Baada ya Mkataba Kuvunjwa Sh. 126,072,257

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu iliingia mkataba na mkandarasi kutekeleza mradi wa maji wa Tumati na Mongahay. Hata hivyo mkataba huo ulivunjwa na Halmashauri kutokana na mkandarasi kutotimiza matakwa ya mkataba. Kabla ya kuvunjika kwa mkataba huo, mkandarasi alikwishalipwa kiasi cha Sh. 298,775,043 ikiwa ni Sh. 114,775,043 zaidi ya thamani ya kazi alizofanya zilizokuwa na thamani ya Sh. 184,000,000. Aidha Sh. 11,297,214 zilikuwa ni kwa ajili ya gharama ya ucheleweshwaji wa mradi, hivyo kusababisha hasara ya jumla ya Sh. 126,072,257 ambayo hadi kufikia mwezi Agosti, 2020 hazikuwa zimerejeshwa.

Ninapendekeza menejimenti ya Wilaya ya Mbulu kuboresha mifumo ya udhibiti kwenye eneo la usimamizi wa mikataba na kuhakikisha Halmashauri inafanya malipo kulingana na matakwa ya vipengele vya mkataba. Kuhusiana na malipo yaliyolipwa kwa mkandarasi aliyeshindwa kukamilisha matakwa ya mkataba, ninapendekeza hatua stahili za ufuatiliaji zifanywe na menejimenti ili kiasi cha Sh. 126,072,257 kirejeshwe.

13.3.3.67 Mkataba wa Gharama za Usafiri Ulioghushiwa Sh. 272,000,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilifanya malipo ya Sh. 272,000,000 kwa mshauri wa mradi, kama gharama za usafiri wa usimamizi wa mradi wa ujenzi wa barabara za lami za Manispaa, kupitia mkataba LGA/064/2016/2017/CS/01. Hata hivyo ilibainika kuwa kampuni ya ushauri wa mradi ilighushi mkataba wa kukodisha gari T 621 DCT na T 163 DJW kutoka kwa mtu mwingine kwa Sh. 8,000,000 kwa mwezi kwa muda wa miezi 34. Kutokana na uthibitisho wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa barua yenye Kumb. Na. TRA/MAR/RM/0016/VOL.II/181 ya tarehe 15 Julai 2020, mmiliki halali wa magari hayo ni Mkandarasi mshauri wa mradi. Hivyo malipo ya Sh. 272,000,000 yalikosa uthibitisho na uhalali wa ulipwaji wake.

13.3.3.68 Hasara Kutokana na Malipo Juu ya Kiwango cha Mkataba Bila Uthibitisho Sh. 91,631,300

Katika kipindi cha kati ya mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilifanya malipo ya Sh. 101,920,000 kwa mkandarasi mshauri ikiwa ni gharama za marejesho 'Reimbusrable Cost' na mishahara ya wafanyakazi wa ujenzi wa barabara katika Manispaa ya Musoma, wakati gharama halisi zilikuwa ni Sh. 10,288,700 tu. Malipo hayo yalifanyika kinyume na vifungu vya mkataba na hivyo kuisababishia Halmashauri hasara ya Sh. 91,631,300.

13.3.3.69 Malipo Yaliyofanyika Bila Kudai Risiti za Kieletroniki Sh. 11,694,518,760.80

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilifanya malipo ya Sh. 11,694,518,760.80 kwa ajili ya gharama za ujenzi na usimamizi wa mradi wa barabara kwa kiwango cha lami. Kati ya malipo hayo, Sh. 9,983,464,711.30 zilikuwa kwa ajili ya mkandarasi M/s Nyanza Road Works, Sh. 1,415,691,711.50 za msimamizi M/s Norplan (T) Ltd na Sh. 295,362,338.00 za msimamizi M/s Data Consult Ltd. Nilibaini kuwa malipo hayo hayakuambatana na risiti za

kielectronic (EFD). Kutokudai risiti kumesabisha upotevu wa Sh. 2,105,013,377 za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Kwa mapungufu yalibainishwa hapo juu, ninapendekeza mamlaka husika kuchukua hatua stahili dhihi ya wafanyakazi wote waliotajwa kwenye ripoti ya ukaguzi maalumu kwa ushiriki wao kwenye ubadhirifu wa fedha za umma kwa kumlipa mkandarasi jumla ya Sh. 91,631,300 zaidi ya kiasi cha fedha kilichokubalika kurejeshwa kwenye mkataba na kuchukua hatua zaidi ili kuhakikisha mshauri anarejesha kiasi alichopokea ambacho hastahili. Pia, halmashauri ya manispaa ya Musoma iache kuwapa zabuni wazabuni na wakandarasi ambao hawatoi risiti za kielekroniki au kutoa taarifa husika kwa TRA kwa ajili ya hatua stahili za ufuatiliaje.

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO

13.3.3.70 Jumla ya Hasara Kiasi cha Sh. 656,533,708 Katika Miradi ya Halmashauri

Katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha 2017/18 hadi 2019/20, Halmashauri ya Wilaya ya Busekelo ilipata hasara ya Sh. 656,533,708 kutokana na kutozingatiwa kwa kanuni za manunuzi ya umma na usimamizi wa miradi. Kwa muhtasari, mchanganuo wa hasara hiyo ni kama ifuatavyo:

- Hasara ya Sh. 439,225,288 kwa Halmashauri kushindwa kudai fidia kutoka kwa Kampuni binafsi ya Bima ambayo iliweka dhamana kumfadhili Mkandarasi ambaye ilishindwa kutekeleza mkataba namba LGA/157/W/2017/2018/01 wa ujenzi wa jengo la utawala;

- Hasara ya Sh. 58,165,386 kwa kumpa zabuni ya ujenzi wa Jengo la Utawala mkandarasi aliyeweka bei ya Sh. 1,464,084,292 ambayo ilikuwa kubwa na kumwacha mzabuni aliyekuwa na bei ya Sh. 1,417,440,898 katika zabuni LGA/157/W/2017/2018/01 ya kujenga jengo la utawala;

- Hasara ya Sh. 4,821,421 kwa kumpa Mkandarasi zabuni Na. LGA/157/W/2017/2018/15/LOT 01 ya mradi wa Maji katika

eneo la Mpata kwa bei ya 283,411,161 na kumwacha mzabuni aliyekuwa na bei ya Sh. 278,589,740;

- Hasara ya Sh. 26,347,732 kwa kumlipa mara mbili mkandarasi kwa kazi zinazofanana kwenye cheti cha malipo namba 10 na namba 4 kwenye kandarasi namba LGA/157/W/2017/2018/01 ya ujenzi wa jengo la utawala awamu ya kwanza.

- Hasara ya Sh. 76,421,500 iliyosababishwa na kuanza kwa ujenzi wa shule ya wasichana Busokelo bila kuwalipa fidia wananchi wa Kata ya Kandete, hali iliyopelekea wananchi kufungua kesi mahakamani; na mahakama ikasimamisha ujenzi kwa siku 235 hali iliyopelekea gharama za ujenzi kupanda kwa Sh. 76,421,500.

- Hasara ya Sh. 22,574,125 kwa kutokukatwa kwa kodi ya zuio kwa mafundi uashi, watoa huduma za usafirishaji na kwa wauzaji wa bidhaa na malighafi za ujenzi katika miradi mbalimbali ya Halmashauri ya Busekelo;

- Hasara ya Sh. 28,978,260 iliyosababishwa na ununuzi wa mifuko 20,422 ya saruji kwa Sh. 328,569,000 kwa wazabuni wadogo wadogo badala ya kununua kwa wazalishaji wa viwandani kwa gharama ya Sh. 299,590,740 na hivyo Halmashauri ingeweza kuokoa kiasi cha Sh. 28,978,260.

Ninapendekeza kuwa halmashauri iimarishe udhibiti kwenye usimamizi wa mikataba na mamlaka za uchunguzi zifanye uchunguzi kwenye viashiria vya ubadhirifu kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ya ukaguzi maalumu na kuchukua hatua stahili dhidi ya wahusika wote.

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

13.3.3.71 Ubadhirifu wa Viwanja 29 Vilivyopimwa Vyenye Thamani ya Sh. 204,828,000

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilipima viwanja 101 katika eneo la block T lililopo Tukuyu mjini. Viwanja hivyo vilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama biashara, makazi, maeneo ya

wazi pamoja na ofisi za Taasisi. Nilibaini kuwa viwanja 72 tu ndivyo vilivyokuwa vimetolewa taarifa kwenye vikao vya Halmashauri na vilikuwa kwenye kumbukumbu mbalimbali za Halmashauri, huku viwanja 29 vyenye thamani ya Sh. 204,828,000 vikiwa vimefichwa na mauzo yake hayakuwepo kwenye kumbukumbu za Halmashauri.

13.3.3.72 Kuondolewa kwa Mzabuni Bila Sababu za Msingi Kulikopelekea Ongezeko la Gharama kwa Sh. 71,614,244

Kinyume na Kifungu cha 72 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2011 na Kanuni namba 203 (2) na Kanuni ya 17 (2-4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013, nilibaini kuwa mkandarasi mwenye bei ya chini aliondolewa wakati wa kufanyika tathmini bila sababu za msingi, kwa kuwa vigezo ambavyo havikuwa sawa, hali iliyopelekea Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuingia mkataba kwa gharama ya ziada ya Sh. 71,614,244. Mzabuni aliyeondolewa alikuwa na bei ya Sh. 6,148,394,776.77 na aliyepewa kazi alikuwa na bei ya Sh. 6,220,009,021.

Ninapendekeza kwa menejimenti ya Halmshauri na Bodi ya Zabuni kuhakikisha kuwa , kamati ya tathmini inatumia vigezo vilivyopo kwenye kabrasha la zabuni ama gazeti na kutafuta ufafanuzi wa utofauti wa bei. Pia, Afisa Masuuli afuatilie zabuni iliyosababisha hasara ya Sh. 71,614,244. Pia, napendekeza mamlaka husika kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahusika wote waliotajwa kwenye taarifa ya ukaguzi maalumu.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO

13.3.3.73 Malipo Yaliyofanyika kwa Wazabuni Pasipo Kukatwa Kodi ya Zuio Kiasi cha Sh. 10,315,688

Katika kipindi cha miaka 3 kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2019/20, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ililipa kiasi cha Sh. 515,784,400 kwa wazabuni mbalimbali; hata hivyo, kodi ya zuio kiasi cha Sh. 10,315,688 hakikukatwa kwa wazabuni hao na hivyo kuikosesha Serikali mapato.

Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro inapaswa kuhakikisha kuwa kodi ya zuio katika siku zijazo inakatwa ipasavyo na

kuwasilishwa kwa Kamishna kama inavyotakiwa na Vifungu vya 83 (1) na 84 (1) vya Sheria ya Kodi ya Mapato (ITA), 2004 (na marekebisho ya 2008)

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA

13.3.3.74 Kushindwa Kuthibitisha Gharama za Matengenezo ya Jengo la Biashara Yaliyofanywa na Mpangaji Sh. 51,888,000

Nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2017/18, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilikarabati jengo la biashara la kitega uchumi kwa gharama ya Sh. 51,888,000 kinyume na mkataba uliotaka gharama za marekebisho zifanywe na mwekezaji. Vilevile, Halmashauri ilishindwa kuonyesha mchanganuo wa namna fedha hiyo Sh. 51,888,000 ilivyotumika katika kufanya matengenezo hayo.

Halmashauri, kupitia idara ya ujenzi inapaswa kutathmini ukarabati uliofanywa kwa kulinganisha gharama ambayo mpangaji anadai kutumia kwenye matengenezo na bei halisi ambayo inaakisi kazi iliyofanyika.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

13.3.3.75 Hasara iliyosababishwa na kuingia mkataba na mzabuni wa kukusanya mapato tofauti na aliyependekezwa na timu ya tathmini Sh. 27,000,000

Tarehe 30 Juni 2019 Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro iliingia mkataba namba LGA/079/2018-2019/HQ/NCS/16 LOT 17 na M/S Nashazi Company Ltd kwa ajili ya ukusanyaji wa ushuru katika stendi ya mabasi mjini kama wakala kwa makubaliano ya kukusanya Sh. 108,000,000 ambayo ni sawa Sh. 9,000,000 kwa mwezi. Kwa kufanya hivyo Halmashauri ilimuengua kwenye mchakato wa zabuni mzabuni M/s Larries and Company Ltd aliyependekezwa na Kamati ya Tathmini ambaye aliomba kukusanya Sh. 144,000,000 kwa mwaka. Aidha, Halmashauri inapaswa kubaki na asilimia 75% ya makusanyo. Kwa kufanya hivyo Halmashauri imepata hasara ya Sh. 27,000,000 [75% x (144,000,000-108,000,000)] ambayo ingepatikana endapo ingesaini mkataba na mzabuni M/s Larries and Company Ltd.

13.3.3.76 Hasara iliyosababishwa na kamati ya tathmini ya zabuni kutoa zabuni kwa kampuni ambayo haikukidhi vigezo vya uzoefu wa kazi Sh. 44,114,375

Kinyume na matakwa ya nyaraka za zabuni ukaguzi ulibaini kuwa mnamo tarehe 15 Oktoba 2019, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro iliingia mkataba namba LGA/079/2018-19/HQ/W/08 na kampuni ya M/s Fast Construction Company Ltd ya S.L.P 71622, Dar es Salaam, ambaye hakuwa amekidhi vigezo vya zabuni ya ujenzi wa stendi ya daladala Kaloleni kwa Sh. 724,762,500 kwa kipindi cha miezi mitatu na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kimkataba hivyo kupelekea kuvunjwa kwa mkataba husika na kuisababishia hasara hamshauri ya Sh. 44,114,375 ambayo ilitokana na malipo ya awali ambayo haikuweza kufidiwa na mkandarasi baada ya mkataba kuvunjika.

13.3.3.77 Kutowasilishwa kwa mkataba wenye thamani ya Sh.12,630,868,635 na nyaraka za kuthibitisha mchakato wa zabuni ya ujenzi wa barabara ya Tubuyu, Nanenane na Maelewano

Nilishindwa kukagua mikataba miwili yenye thamani ya Sh. 12,630,868,635, iliyosainiwa baina ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na mkandarasi M/s Group Six International Ltd, akishirikiana na Lukolo Company Ltd na nyaraka za mchakato wa zabuni ya mradi wa kuinua hadhi ya barabara za Tubuyu (km 2.4), Nanenane (km 1.6), na Maelewano (km 0.6) yenye namba LGA/079/2016-2017/HQ/W/04 ambayo haikuwasilishwa kwenye ukaguzi japokuwa nilifanya jitihada mbali mbali za kupata nyaraka hizo.

Ninapendekeza menejimenti kufanya uchunguzi na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahusika wote waliotajwa kwenye ripoti ya ukaguzi maalumu. Pia, hapo baadae menejimenti ihakikishe kuwa inazingatia mapendekezo iliyopewa na timu ya tathmini na pale ambapo menejimenti itatofautiana na mapendekezo iliyopewa na timu ya tathmini ni lazima ifuate taratibu zilizoelezwa kwenye Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma. Menejimenti ya halmashauri ichukue hatua za kurejesha fedha za malipo ya awali iliyolipa.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

13.3.3.78 Manunuzi ya Mashine ya Umeme ya Kufyatua Tofali Isiyotumika Katika Ujenzi wa Kituo cha Afya Nagaga Sh. 24,770,000

Nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2018/19, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ilitumia jumla ya Sh. 24,770,000 zilizojumuisha Sh. 17,700,000 kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya umeme ya kufyatulia tofali na Sh. 7,070,000 kwa ajili ya ununuzi wa vibao vya tofali pamoja na usafirishaji wake. Hata hivyo, baada ya kutembelea mradi huo, nilibaini kuwa mashine husika haikuweza kutumika kutokana na changamoto ya umeme.

13.3.3.79 Malipo Yaliyofanyika kwa ajili ya Ununuzi wa Madawati ya Shule tatu za Msingi Ambayo Hayakupokelewa Sh. 10,230,000

Nilibaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2017/18, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ilimlipa mzabuni kiasi cha Sh. 18,840,000 kwa ajili ya matengenezo ya madawati 168 katika shule za msingi Chidya, Chiwale na Nairombo. Hata hivyo, mzabuni alileta madawati 71 tu. Hadi nakamilisha ukaguzi wangu mwezi Agosti, 2020, madawati 93 yenye thamani ya Sh. 10,230,000 hayakuwa yamewasilishwa kwenye shule husika; na wala fedha kurejeshwa kwenye shule hizo, ingawa mahakama ilishaamuru kuuzwa kwa mali za mzabuni ili kufidia fedha alizokuwa amelipwa.

Kulingana na makosa yaliyotajwa hapo juu, ninapendekeza kuwa wahusika wote walioshiriki katika ununuzi wa madawati yaliyotajwa hapo juu na mashine ya kufyatua matofali wachukuliwe hatua stahiki kwa kushindwa kufanya utafiti / upembuzi yakinifu kabla ya ununuzi wa mashine na kwa kulipia madawati kabla ya kupokelewa. Aidha, Halmashauri inashauriwa kuihamisha mashine hiyo kwenda katika eneo lingine la Halmashauri kama itakavyoonekana inastahili ili iweze kutumika na kuleta tija kama ambavyo ilikusudiwa.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU

13.3.3.80 Malipo ya Kazi Hewa Kutokana na Udanganyifu Katika Vyeti vya Malipo (Payment Certificates) Sh. 656,555,186

Nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2019/20, Halmashauri ya Wilaya ya Magu ilifanya malipo ya Sh. 1,157,904,440 kwa mkandarasi zaidi ya kiasi alichostahili kulipwa cha Sh. 501,349,253, kutokana na udanganyifu wa kazi zilizofanyika katika Cheti namba 3 (Sh. 11,603,511), Cheti namba 4 (Sh. 51,186,031), Cheti namba 5 (Sh. 101,777,013), Cheti namba 6 (Sh. 225,434,500) na Cheti cha kukamilisha kazi namba 7 (Sh. 266,554,131). Kukosekana kwa usimamizi bora katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kumechangia uwepo wa malipo ya jumla ya Sh. 656,555,186 kwa kazi hewa.

13.3.3.81 Hasara Iliyotokana na Malipo Yasiyostahili kwa Mkandarasi Sh. 96,738,000

Halmashauri ya Wilaya ya Magu ilimlipa mkandarasi kiasi cha Sh. 96,738,000 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri, awamu ya pili (Phase II), ikiwa Sh. 80,615,000 ni kwa ajili ya kazi za maandalizi ya awali ambazo alikwishalipwa katika ujenzi wa awamu ya kwanza na Sh. 16,123,000 kama gharama ya kuondoa vifaa sehemu ya mradi baada ya mkataba kuvunjwa tarehe mnamo tarehe 23 April, 2020

Halmashauri inashauriwa kuimarisha mfumo wa udhibi wa ndani na kuhakikisha inaukagua na kupima kiasi cha kazi zilizotekelezwa kabla ya kuthibitisha malipo ili kuzuia kufanya malipo kwa kazi ambazo hazikutekelezwa. Aidha, nashauri Halmashauri kuchukua hatua stahiki ili kuweza kurejesha kiasi cha fedha kilicholipwa kimakosa zaidi ya kazi husika. Zaidi ya hayo, hatua stahiki zichukuliwe kwa watumishi wa Halmashauri kama walivyotajwa katika ripoti husika kwa kuisababishia Serikali hasara.

HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

13.3.3.82 Hasara Itakayopatikana kwa Kutolipa Fidia ya Ardhi kwa Maeneo Ambayo Yameshafanyiwa Uthamini Sh. 1,945,281,258

Nilibaini kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020, Jiji la Mwanza lilikuwa na malimbikizo ya fidia za ardhi kiasi cha Sh. 4,831,761,220. Kwa mujibu wa sheria za ardhi, deni hili linapelekea riba ya Sh. 1,945,281,258. Kuchelewa kulipwa kwa fidia kunaiongezea Halmashauri ya Jiji gharama za kulipa riba, na riba hii itaendelea kupanda kadri fidia itakavyokuwa inachelewa kulipwa.

13.3.3.83 Kutofanya Kazi kwa Kituo cha Redio "City FM Mwanza" Licha ya Kuwekeza Sh. 102,574,467

Mnamo mwaka 2010, Halmshauri ya Jiji la Mwanza liliwekeza kiasi cha Sh. 102,574,467 katika kuanzisha redio ya "City FM Mwanza". Hata hivyo, redio hii ilizimwa mwaka 2017 na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kupitia barua yenye Kumb.Na.DB.96/188/02/86, kwa sababu mawimbi yake yalikuwa yanaingiliana na mawasiliano ya ndege. Hadi ukaguzi unakamilika mwezi wa nane 2020, bado redio ilikuwa imefungwa, hivyo kutokwepo kwa thamani ya fedha kwa kiasi cha Sh. 102,574,467 iliyowekezwa.

13.3.3.84 Kutozingatia Masharti ya Mkataba wa Mkopo wa Benki ya CRDB Kulikopelekea Hasara ya Tozo na Riba kwa Halmashauri Kiasi cha Sh. 89,814,942

Nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2014/15, Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilikopa kiasi cha Sh. bilioni 1.279 kutoka Benki ya CRDB kwa marejesho ya miezi 60. Kwa mujibu wa mkataba, deni hili lilipaswa kumalizika mnamo tarehe 30 Mei, 2020. Hata hivyo, Halmashauri ilichukua mkopo huu pasipo kupata idhini ya OR-TAMISEMI. Aidha, hadi ukaguzi huu unakamilika, Halmashauri ilikuwa haijamaliza kurejesha mkopo huo huku tayari ikiwa imeshalipa riba ya adhabu kiasi cha Sh. 89,814,942. Riba hii itaendelea kupanda kadri Jiji litakavyochelewa kulipa deni hilo.

13.3.3.85 Matumizi ya Sh. 872,601,115 Kutoka Katika Akaunti ya Amana ya Muda Maalum Kwa Shughuli Zingine

Mnamo tarehe 21 Septemba, 2011, Halmashauri ya Jiji la Mwanza iliuza eneo la Kliniki ya Makongoro kwa Benki Kuu ya Tanzania kwa kiasi cha Sh. 3,100,000,000 na kuziweka fedha hizo kwenye akaunti ya amana yenye namba 01D6553384598 iliyopo katika Benki ya CRDB kwa madhumuni ya kuzitumia kwenye ujenzi wa Kliniki ya Mama na Mtoto, pamoja na Ofisi ya Idara ya Afya.

Hata hivyo nilibaini kuwa kiasi cha Sh. 872,601,115 kilichukuliwa kutoka kwenye akaunti hiyo na kutumika kwa matumizi mengine na hivyo kupelekea miradi tarajiwa kutotekelezwa.

13.3.3.86 Uwekezaji Usio na Wanufaa wa Ubia na iliyokuwa LAPF katika "Mwanza City Commercial Complex" Sh. 4,800,000,000

Mapitio ya Hesabu za Halmashauri ya Jiji la Mwanza zinazoishia tarehe 30 Juni, 2019 yanaonyesha kuwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza imewekeza kiasi cha Shilingi bilioni 4.8 kwenye kitega uchumi cha "Mwanza City Commercial Complex". Uwekezaji huu ni sawa na umiliki wa asilimia (6%) ya mtaji wote wa "Mwanza City Commercial Complex". Hata hivyo, Halmashauri ya Jiji haijamalizia kulipia hisa kwa kiasi cha Sh. 1.099 bilioni na hivyo haina haki ya kuziuza wala kupata gawio mpaka imalizie kulipia deni hilo. Hivyo Halmashauri ya Jiji hainufaiki na uwekezaji huu wa shilingi bilioni 4.8 katika kitega uchumi cha "Mwanza City Commercial Complex."

Ninapendekeza kwa Serikali kupitia OR-TAMISEMI kuja na mikakati / sera ambazo zitahakikisha deni lililosalia linalipwa mapema iwezekanavyo ili kuepusha gharama zisizo Zaidi zitakazojitokeza kama riba inayotokana na ucheleweshwaji wa marejesho;

Uongozi wa Halmashauri uhakikishe kuwa mitambo ya redio (transmitter) inahamishiwa sehemu zilizopendekezwa na TCRA ili redio "City FM Mwanza" irudi hewani na kuanza kusikika tena ili kuwe na tija katika uwekezaji huu wa redio. Pia, uongozi ufanyie kazi changamoto zote za redio ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya studio

Ninapendekeza kuwa hatua stahiki zichukkuliwe dhidi ya wahusika wote waliotajwa kuhusika na mapungufu yaliyoonekana kama ilivyo katika taarifa ya ukaguzi maalum kwa kutotimiza majukumu yao kikamilifu na hivyo kutofaulu kufikia lengo la kuweka fedha kwa uuzaji wa zahanati ya Makongoro katika Akaunti iliyowekwa.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKAMBAKO

13.3.3.87 Usimamizi Usioridhisha wa Mikataba ya Mawakala wa Kukusanya Mapato Uliopelekea Halmashauri Kutokusanya Mapato yenye Jumla ya Sh. 221,029,800

Sharti la nane (8) na tano (5) la mikataba ya mawakala wa kukusanya mapato linataka wakala kuwasilisha makusanyo yote ya mwezi kwa mwajiri (Halmashauri); na iwapo makusanyo hayo yatakuwa chini ya kiwango kilichokubalika katika Mkataba basi mwajiri atatumia dhamana iliyowekwa na wakala kufidia hasara hiyo, na hapo Mkataba baina ya Halmashauri na Wakala utavunjwa na kupewa zabuni hiyo mzabuni aliyeshika nafasi ya pili wakati wa zoezi la tathmini ya zabuni husika. nilibaini kuwa viwango vya makusanyo vilivyowekwa kutoka katika vyanzo vya ushuru wa ada za uzoaji taka ngumu, ushuru wa masoko na vibanda, ushuru wa maegesho na ushuru wa huduma ya choo havikufikiwa na mawakala katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa kiasi cha Sh. 221,029,800. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Makambako haikuchukua hatua yoyote kufidia hasara hiyo.

13.3.3.88 Kuondolewa kwenye Mchakato wa Manunuzi kwa Mkandarasi Isivyo Halali Kulikopelekea Halmashauri kuingia Mkataba Wenye Gharama Zaidi kwa Kiasi cha Sh.201,200,978

Katika kupitia taarifa za mchakato wa zabuni Na.LGA/166/ W/2015-2016/01 ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Makambako, nilibaini kuwa Mkandarasi aliyeomba kazi kwa Sh. 846,386,974, aliondolewa katika mchakato wa zabuni katika hatua za awali kwa kukosa vigezo ikiwemo fomu ya zabuni kutojazwa na kusainiwa na mtu aliyeteuliwa, dhamana ya zabuni (Bid security) iliyo katika muundo tofauti na ule uliotolewa katika kabrasha la zabuni na

haikusainiwa na nyaraka za zabuni kutosainiwa katika baadhi ya kurasa hivyo kupelekea kazi hii kutunukiwa kwa mwingine, kwa bei ya Sh. 1,047,587,952. Hata hivyo, nilivyopitia kabrasha la zabuni lililowasilishwa na Mkandarasi huyo, nilibaini kuwa alikuwa amekidhi vipengele vyote vilivyotumika kumuondoa katika hatua za awali. Kwa kumuacha mzabuni mwenye gharama ndogo, kulipelekea Halmashauri kuingia mkataba wenye Gharama zaidi ya Sh. 201,200,978 ambayo ingeweza kuepukika.

13.3.3.89 Kutokuzuia/ Kukata Tozo kwa Mkandarasi Ambaye Hakuhuisha Mpango Kazi na Kukamilisha Kazi kwa Wakati Kulikopelekea Halmashauri Kupoteza Sh. 20,000,000

Kipengele cha 30.3 cha Masharti ya jumla ya Mkataba Na.LGA/166/2016-2017/W/HQ/01 kilimtaka mkandarasi kuwasilisha Mpango kazi uliohuishwa kwa Meneja wa mradi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makambako ili uthibitishwe katika vipindi tofauti, kama ilivyoelezwa katika vipengele vya masharti Maalumu. Endapo hilo halijafanyika, Halmashauri inapaswa kumkata mkandarasi kiasi cha Sh. 1,000,000 kwa kila malipo ya Mkandarasi huyo, mpaka atakapowasilisha mpango huo. Nilibaini kuwa, ingawa Mkandarasi hakuwasilisha mpango kazi uliohuishwa, Halmashauri haikumkata kiasi cha Sh. 20,000,000 kwa hati za malipo zilizolipwa.

Ninapendekeza kuwa uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako ufanye jitihada mahsusi za kuhakikisha kuwa Mawakala wa kukusanya mapato wanarejesha kiasi cha Sh. 221,029,800 walizolipwa kimakosa na Halmashauri huku wakiwa hawajafikia lengo walilokuwa wamekubaliana kimkataba. Vilevile kitengo cha mapato na Mwanasheria wa Halmashauri wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kuwa kila kitengo kinafanya kazi yake ipasavyo hivyo mawakala walipwe kutookana makusanyo yao na mikataba iliyoingiwa.

Ninapendekeza kwa uongozi wa halmashauri husika kuzingatia Kifungu cha 72 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 pamoja na Kanuni ya 203(2) ya Kanuni za Manunuzi wa Umma ya Mwaka 2013 wakati wa kutathmini na kutunuku

zabuni. Pia, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wajumbe wote wa kamati za tathmini ya zabuni pamoja na wajumbe wa bodi za zabuni waliosababisha hasara hii.

Ninapendekeza Halmashauri kuhakikisha kuwa inafanya jitihada za kuweza kurejesha kiasi cha Sh. 20,000,000 kilichobainika kulipwa kimakosa wakati wa ukaguzi. Vilevile, napendekeza kuwa hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa wote walioshindwa kutumia nafasi zao kumshinikiza mkandarasi kuleta mpango kazi hai au kukata fedha katika malipo yaliyokuwa yakifanyika ili kumtaka mkandarsi awasilishe mpango kazi huo.

HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

13.3.3.90 Malipo Yaliyofanywa kwa Mkandarasi na Mafundi Mchundo wa Ujenzi Bila Uthibitisho wa Thamani ya Kazi Zilizofanyika Sh. 1,561,749,561

Nilibaini kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2019/20, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ilifanya malipo ya Sh. 1,561,749,561 kwa mkandarasi na mafundi mchundo wa ujenzi wa miradi ya maji Kidegembye, miradi ya ujenzi wa jengo la mionzi, Utawala, Maabara na OPD na ujenzi wa majengo saba ya Hospitali. Hata hivyo hati za malipo zilizotumika kuwalipa wakandarasi na mafundi mchundo wa miradi hiyo, hazionyeshi orodha na vipimo vya kazi (measurement sheets), vilivyothibitisha kiasi cha malipo yaliyostahili kulipwa.

Ninapendekeza Halmashauri kuhakikisha katika siku zijazo, kuwa malipo yote ya kazi zilizofanyika yanaambatishwa na uthibitisho wa kufanyika tathmini ya vipimo ili kuweza kudhibiti malipo yasifanyike kwa kazi ambazo hazijatekelezwa au kulipa zaidi ya kiwango stahiki.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE

13.3.3.91 Kutowasilishwa Vitabu 189 vya Kukusanyia Mapato ya Ndani kwa Ajili Ukaguzi

Vitabu 189 vya kukusanyia mapato ya ndani, vilivyotolewa kwa watumishi wa vituo vya afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20, havikuwasilishwa kwangu kwa ajili ya ukaguzi hivyo nilishindwa kufahamu ni kiasi gani kilikusanywa na Halmashauri katika kipindi hicho.

Ninaishauri Serikali kupitia OR-TAMISEMI kuwachukulia hatua stahiki wahusika wote wanaopaswa kuvitunza vitabu vya kukusanyia mapato ambavyo haijulikani vilipo na wala havikuwasilishwa kwangu wakati wa ukaguzi. Aidha Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Makete inatakiwa kufuatilia na kutafuta vitabu vya kukusanyia mapato ambavyo havikuonekana ili viwasilishwe katika Ofisi yangu kwa ajili ya uhakiki. Zaidi ya hayo, ninaendelea kusisitiza uimarishaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuondoa mianya ya ubadhirifu wa fedha za makusanyo.

HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

13.3.3.92 Wapangaji wa Vibanda/Fremu vya HalmashauriWalipangisha Wapangaji Wengine kwa Kodi Kubwa na Kujipatia Sh. 71,050,000

Nilibaini kuwa kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2019/20, wapangaji wa vibanda 199 vya Halmashauri ya Mji wa Kibaha katika soko la Mnarani, waliwapangisha watu wengine kwa bei kubwa zaidi ya wanayotozwa na Halmshauri na hivyo kujipatia kiasi cha Sh. 71,050,000 kinyume na utaratibu.

Kwa kuzingatia hayo niliyoyabaini hapo juu ninapendekeza kuwa Halmashauri ya mji wa Kibaha ifanye tafiti ya bei halisi ya soko ili iweze kubadili bei ili kufanya mapato ya Halmashauri kuongezeka na kuondoa tatizo la wapangaji kuwapangisha watu wengine.

HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

13.3.3.93 Vitabu 103 vya Mapato ya Ndani Havikuwasilishwa kwa Ajili ya Ukaguzi

Jumla ya vitabu 103 vya wazi vilivyotumika kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo nilishindwa kuthibitisha kiwango cha fedha kilichokusanywa. Vitabu hivyo vilitolewa kwa Msaidizi wa hesabu wa Halmashauri ya Bagamoyo.

13.3.3.94 Mashine za X Ray na Kukausha Nguo Zilizonunuliwa kwa Sh. 207,334,000 Lakini Hazitumiki

Nilibaini kuwa mnamo tarehe 24 Januari, 2019, Bohari ya Dawa (MSD)iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo mashine ya X Ray yenye thamani ya Sh. 120,334,000 na mashine ya kukaushia nguo yenye thamani ya Sh. 87,000,000; lakini, tangu kupokelewa kwa mashine hizo, zimekuwa hazitumiki kwa kuwa mashine ya X Ray haina jengo maalum la X RAY, na mashine ya kukaushia nguo haifanyi kazi kwa sababu hakuna mashine ya kufulia nguo. Kutokufanya kazi kwa mashine hizi kunasababisha kutokuwepo kwa thamani ya fedha iliyotumika kuzinunua.

Endapo mashine hiyo ya mionzi na ya kufua zikiendelea kukaa bila kutumika, thamani ya fedha haitofikiwa. Hivyo basi naishauri Halmashauri kuchukua hatua ili kufanya mashine hizi zitumike. Vilevile, nishauri mamalaka husika kuchukua hatua za kichunguzi dhidi ya vitabu 103 ambavyo havijulikani vilipo ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua stahiki wahusika wote wa utunzaji wa vitabu hivyo.

HALMASHAURI YA MANISPAAA SUMBAWANGA

13.3.3.95 Upotevu wa Mapato kwa Kuchagua Wakala Ambaye zabuni yake ya ukusanyaji Mapato Ilikuwa Chini Bila ya Kutoa Sababu za Msingi Sh. 85,200,000 na kushindwa kukata jumla ya Sh. 117,001,187

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga iliingia mkataba na wakala wa kukusanya mapato

katika chanzo cha mazao mchanganyiko kwa kiasi cha Sh. 19,000,000 na kulipa mzabuni asilimia 15 ya makusanyo ya mwezi. Kwa kufanya hivyo, Halmashauri ilimuacha mzabuni wa uwakala wa mapato ambaye alikuwa na bei ya zabuni ya Sh. 25,000,000 na kuomba kulipwa asilimia saba (7) ya makusanyo ya mwezi kwa kutumia kigezo ambacho hakikuwepo kwenye vigezo vya uchambuzi wa zabuni kama ilivyooneshwa kwenye kabrasha la zabuni. Maamuzi ya kumchukua mzabuni mwenye bei ya chini yalisababisha Halmashauri kupoteza kiasi cha Sh. 85,200,000

Vile vile katika kupitia mkataba huo nilibaini kuwa kulikuwa na kifungu kilichomtaka wakala kukusanya Sh. 22,500,000 kwa mwezi, na ikiwa hatafikisha kiasi hicho wakala atakatwa tofauti ya kiasi hicho kutoka kwenye amana aliyoweka (bond) kwa ajili ya kufidia mapungufu hayo. Kinyume na matakwa ya mkataba huo, nilibaini kuwa Halmashauri haikumkata wakala tofauti ya kiasi alichokusanya na kiasi ambacho angepaswa kukusanya, hivyo kupelekea hasara ya Sh. 117,001,187.

13.3.3.96 Udanganyifu Uliofanywa Kwenye Mashine za Kukusanyia Mapato (POS) Uliopelekea Kutowasilishwa kwa Sh. 9,974,650

Mfumo wa ukusanyaji mapato ya ndani (LGRCIS) ulianzishwa nchini katika mwaka wa fedha 2015/16. Hata hivyo, katika Halmshauri ya Manispaa ya Sumbawanga nilibaini kuwa mapato kiasi cha Sh. 9,974,650 yalionekana kukusanywa na POS 18 kuanzia tarehe 01 Julai, 2009 hadi 30, Juni 2015 wakati ambapo mfumo huo ulikuwa haujaanza kutumika. Hii inaashiria kuwa mawakala walirudisha tarehe nyuma (*back date*) katika POS zao wakati wa ukataji wa risiti kwa nia ya kufanya udanganyifu.

13.3.3.97 Malipo kwa Mkandarasi Mjenzi Zaidi ya Mchanganuo wa Matumizi (BOQ) Sh. 1,584,725,260

Nilipitia Hati za Malipo, Hati za Kazi na Taarifa ya utekelezaji ya mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Kisasa ya Mabasi Katumba Azimio wenye mkataba Na.LGA/098/HQ/2018/19/W/10 wa thamani ya Sh. 5,473,976,005 na kubaini kuwa mkandarasi alilipwa kiasi cha Sh. 1,584,725,260 zaidi ya kiwango kilichokuwa kimeoneshwa kwenye mchanganuo wa matumizi (BOQ).

13.3.3.98 Malipo Yaliyofanywa kwa Mafundi Mchundo wa Ujenzi Bila Uthibitisho wa Thamani ya Kazi Zilizofanyika Sh. 100,859,226.62

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilifanya malipo ya Sh. 100,859,226.62 kwa mafundi mchundo wa mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Mazwi. Hata hivyo, Hati za Malipo zilizotumika kuwalipa mafundi mchundo hao, hazikuambatanishwa na orodha na vipimo vya kazi *(measurement sheets)*, ili kuthibitisha kiasi cha malipo yaliyostahili kutolewa.

13.3.3.99 Kukosekana kwa Mchanganuo Mpya wa Gharama (BOQ) Baada ya Majadiliano ya Punguzo Sh. 5,473,976,005.13

Kwa mujibu wa mkataba Na.LGA/098/HQ/2018/2019/W/10 wa ujenzi wa Stendi ya Kisasa ya Mabasi eneo la Katumba Azimio, ulioingiwa tarehe baina ya Halmashauri na Mkandarasi nilibaini kuwa mkandarasi aliomba kufanya kazi hiyo kwa kiasi cha Sh. 9,932,908,686.99. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti, majadiliano yalifanyika mnamo tarehe 04 Aprili, 2019 ili kushusha gharama na kufikia kiasi cha Sh. 5,473,976,005.13.

Nilibaini kuwa licha ya makubaliano hayo kuafikiwa na pande zote mbili, mkataba uliosainiwa baina ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na mkandarasi una mchanganuo wa gharama (BOQ) ya Sh. 9,932,908,686.99, ingawa gharama ya mkataba ilikwishabadilika na kuwa Sh. 5,473,976,005.13 na hivyo kufanya mkataba kukinzana na mchanganuo wa gharama.

Katika muktadha huu, ninapendekeza mfumo wa udhibiti wa ndani katika H/M Sumbawanga kuboreshwa. Pamoja na hayo, napendekeza pia hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa ambao hawakutimiza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kusababisha makosa yaliyotajwa hapo juu na kama ilivyoelezewa katika ripoti mahususi ya Ukaguzi huu.

HALMASHAURI YA WILAYA SUMBAWANGA

13.3.3.100 Malipo ya Madeni ya Fedha za Mapato ya Ndani Ambayo Hayakuthibitishwa Sh. 235,563,283

Katika mwaka wa Fedha 2019/20, Halmashauri ya Wilaya Sumbawanga ililipa madeni ya wakusanya mapato ya miaka ya nyuma kiasi cha Sh. 235,563,283, lakini malipo haya hayakuthibitishwa kwa nyaraka halisi na pia madeni haya hayakuwa kwenye taarifa za fedha za Halmashauri za mwaka 2018/19.

13.3.3.101 Tofauti ya Mapato Kati ya Daftari la Fedha na Taarifa ya Benki Sh. 670,894,820

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, nilibaini kuwa kiasi cha Sh. 6,496,006,380 kilikusanywa na Halmashauri na kuingizwa katika daftari la fedha (cash book) katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2017 hadi Juni 2020. Lakini mpaka kufikia mwezi Juni, 2020, kiasi ambacho kilionekana katika taarifa za benki kilikuwa ni Sh. 5,825,111,560 tu, hivyo kupelekea tofauti ya Sh. 670,894,820.

13.3.3.102 Watu Binafsi Waliokusanya Mapato Bila ya Kuwa na Mikataba Sh. 1,400,867,380

Nilibaini kuwa watu binafsi 23 wasio watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga walikabidhiwa mashine za (POS) katika nyakati tofauti kwa ajili ya kukusanyia mapato kwa niaba ya Halmashauri bila kuwa na mikataba ya ajira kama wakusanya mapato wa Halmashauri hiyo. Watu hao walikusanya kiasi cha Sh. 1,400,867,380 kwa mwaka wa fedha 2019/2020

13.3.3.103 Wakusanya Mapato waliokusanya mapato ya Sh. 1,400,867,380 bila ya kuwa na Mikataba ya kukusanyia Mapato

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kuna wakusanya mapato 23 wasio wafanya kazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ambao walipewa machine 23 (POS) za kukusanyia mapato. Nilibaini kuwa watu hawa hawakuwa na mikataba ya kukusanyia mapato japokuwa walikuwa wamekusanya jumla ya Sh. 1,400,867,380.

13.3.3.104 Fedha za Zuio za Miradi ya Maji Kutojulikana Zilivyotumika Sh. 164,091,492

Katika makabidhiano ya miradi ya maji kati ya RUWASA na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, nilibaini kuwa fedha za zuio za miradi ya maji kiasi cha Sh. 164,091,492 zilizokuwa zinapaswa kukabidhiwa kwa RUWASA Sumbawanga, hakikukabidhiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga haikuweza kuelezea namna zilivyotumika.

Ninapendekeza kwa mamlaka husika kuhakikisha kuwa, inafanyia kazi mapungufu yote yaliyobainika wakati wa ukaguzi. Pia, uchunguzi unapaswa kufanywa kuhusiana na malipo ya madeni ya watoza ushuru yanayolipwa bila uthibitisho kiasi cha Sh. 235,563,283. Kwa kuongezea, Halmashauri kupitia Kitengo cha Mapato na Kitengo cha Sheria inalazimika kupanga namna bora ya kuandaa mikataba, ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba pamoja na malipo yafanywayo kwa mawakala wa kukusanyia mapato wakizingatia aina ya mapato na vyanzo vyake. Aidha, mamlaka husika zinapaswa kuchukua hatua stahiki dhidi ya wafanyikazi waliohusika katika kasoro zilizoorodheshwa hapo juu na kama ilivyoelezwa katika ripoti ya ukaguzi husika.

HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA

13.3.3.105 Malipo kwa Kazi Ambazo Hazikufanyika na Vifaa Ambavyo Havikuwasilishwa Kwenye Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mpitimbi Sh. 24,678,000

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, nilibaini malipo ya Sh. 9,450,000 yaliyofanywa kwa kazi ambazo hazikufanyika kwenye ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mpitimbi na Sh. 15,228,000 zilizolipwa kwa ajili ya manunuzi ya vifaa ambavyo havikuwasilishwa kwa Halmashauri kutokana na usimamizi usioridhisha wa mradi. Jumla ya upotevu uliobainika ni Sh. 24,678,000.

Kwa kuwa taraibu za Serikali zinahitaji malipo kufanyika kwa wazabuni mara baada ya kuwasilisha bidhaa alizoagizwa na mara baada ya Ukaguzi wa bidhaa hizo kufanyika na kukubalika

ninapendekeza kuwa, Halmashauri iheshimu na kuzitii sheria, kanuni na taratibu za manunuzi ya umma ili kuweza kuiondolea Halmashauri athari za kufanyika malipo bila kuletewa bidhaa zilizoagizwa kwa usahihi. Aidha, ninaishauri Halmashauri ya wilaya ya Songea kuhakikisha kuwa vifaa vilivyoagizwa vinapelekwa Hospitali ya Wilaya na kutumika kama ilivyokusudiwa au fedha za Serikali zirudishwe haraka iwezekanavyo na mzabuni huyo ili kuwezesha kufanyika manunuzi hayo kwa mzabuni mwingine mwenye sifa stahiki. Vilevile napendekeza kuchukuliwa hatua stahiki dhidi ya wahusika wote waliohusika katika kuidhinisha na kufanya malipo hayo bila vifaa kufikishwa katika Hospital ya Mpitimbi.

HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA

13.3.3.106 Fedha za Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala la Ofisi ya Halmashauri Zilizotumika Kufanya Shughuli Nyingine Sh. 554,362,635

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2018/2019, nilibaini kuwa kiasi cha Sh. 1,450,000,000 kilipokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa. Jumla ya Sh. 895,637,365 zilitumika kwa ajili ya ujenzi huo na kubakia na kiasi cha Sh. 554,362,635, ambacho kilitumika kufanya shughuli nyingine zisizohusiana na ujenzi wa Jengo la hilo, ambazo hata hivyo sikuweza kuzithibitisha.

Ninaishauri Halmashauri pamoja na mamlaka zingine husika kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi wote waliohusika katika kuandaa hati za malipo, kuidhinisha na kufanya malipo mbalimbali kwa kutumia fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri kama ilivyoelezwa kwa undani katika ripoti ya ukaguzi maalum wa Halmashauri. Aidha ninapendekeza kuwa Halmashauri irejeshe fedha hizo kupitia mapato yake ya ndani ili kazi iliyotarajiwa iweze kukamilika.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

13.3.3.107 Malipo Yaliyofanywa kwa Wakandarasi Zaidi ya Gharama ya Mkataba Sh. 2,449,991,166.5

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaaa ya Shinyanga ilifanya malipo mbalimbali ya jumla ya Sh. 2,449,991,166.5 zaidi ya kiwango kilichoainishwa kwenye mikataba, yaliyolipwa kwa wakandarasi na wasimamizi wa miradi mbalimbali. Kiasi cha Sh. 2,263,685,478 kililipwa zaidi kwa kampuni ya Jassie & Company Ltd (JASCO) kutokana na kubadilisha vipengele vya mkataba wakati wa kuomba malipo ya ujenzi wa barabara ya lami. Pia, kiasi cha Sh. 49,331,800 kililipwa zaidi ya stahili kwa Mhandisi Howard Humphreys Tanzania kwa ajili ya kusimamia ujenzi wa barabara za lami, huku kiasi cha Sh. 136,973,888.5 kikiwa ni malipo zaidi ya kiasi stahili kwa Jassie & Company Ltd (JASCO) kwa ajili ya mkataba wa ujenzi wa barabara za lami.

Hadi kufikia Agosti, 2020, fedha hizo hazikuwa zimerejeshwa katika Akaunti ya Benki ya Halmashauri na hivyo kusababisha hasara kwa Halmashauri.

13.3.3.108 Hasara Kutokana na Ongezeko la Muda wa Kazi kwa Barua Iliyoghushiwa Sh. 120,181,274.57

Mnamo tarehe 01 Juni,2015, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga iliingia mkataba namba LGA/112/2014-2015/ULGSP/W/13 na Kampuni ya Jassie & Company Ltd (JASCO) kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami. Mkataba ulipaswa kukamilika tarehe 24 Februari, 2017; hata hivyo ulichelewa kukamilika, hivyo kupitia hati ya malipo Na. PV2017-002678 ya tarehe 06 Mei, 2017, Halmashauri ilimkata mkandarasi Sh. 120,181,274.57 ikiwa ni gharama ya kuchelewesha mradi. Gharama hizo zilidaiwa na kurudishwa tena kwa mkandarasi kupitia Hati ya Malipo Na.832013V1900011 ya tarehe 03 Agosti, 2018, kutokana na mkandarasi kudai alikuwa ndani ya muda baada ya kuongezewa miezi 18, kupitia barua yenye Kumb. Na.SHY/MC/C.50/8 VOL XVIII/335 ya tarehe 19 Oktoba, 2016. Hata hivyo, nilibaini kuwa barua hiyo ilikuwa imeghushiwa na

mtumishi, hivyo kuisababishia Halmashauri hasara ya Sh. 120,181,274.57.

13.3.3.109 Hasara Kutokana na Kucheleweshe Malipo ya Mkandarasi Sh. 114,476,330.75

Mnamo tarehe 01 Juni, 2015, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga iliingia mkataba Na.LGA/112/2014-2015/ULGSP/W/13 na Kampuni ya Jassie & Company Ltd (JASCO) kwa ajili ya ujenzi wa barabara kiwango cha lami, kilomita 13.1, kwa kipindi cha siku 390. Hata hivyo, Halmashauri ilichelewa kumlipa Mkarandasi kwa siku 454 kinyume na mkataba na hivyo kulazimika kumlipa mkandarasi huyo kiasi cha Sh. 114,476,330.75 kupitia hati ya malipo PV2017-002675 ya tarehe 04 Mei, 2017, ikiwa ni riba kutokana na kucheleweshewa malipo.

13.3.3.110 Fedha za Wakandarasi Kutumika kwa Matumizi Yasiyopangwa Sh. 2,660,379,506.67

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ilitumia kwa matumizi yasiyopangwa kiasi cha Sh. 2,660,379,506.67 kilichokuwa kwenye akaunti ya Amana kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh. 483,348,665.20 kilikuwa kwa ajili ya matazamio ya miradi *(retention money)* na Sh. 2,177,030,841.47 zilikuwa za mradi wa ujenzi wa machinjio ya kisasa zilizotumika kwenye mradi wa ujenzi wa barabara bila kibali, ambapo hadi kufikia Agosti, 2020 fedha hizo zilikuwa hazijarejeshwa.

13.3.3.111 Malipo kwa Wakandarasi Bila Uthibitisho wa Kazi Zilizofanyika Sh. 875,156,177

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ilifanya malipo ya jumla ya Sh. 875,156,177 kwa wakandarasi, bila ya kuwepo kwa nyaraka za uthibitisho wa kazi zilizofanyika. Kiasi cha Sh. 110,855,840 kililipwa kwa PSM Architect Co. Ltd na BJ Amuli Architect Partnership kwa ajili ya matumizi mengineyo *(reimbursable expenses)* ya ujenzi wa machinjio ya kisasa, na Shillingi 764,300,337 zililipwa kwa Home Africa ikiwa ni malipo ya awali (*advance payment*). Hadi ukaguzi unakamilika mwezi

Agosti, 2020, uongozi wa Halmashauri haukuweza kuwasilisha nyaraka husika kwa ajili ya ukaguzi.

13.3.3.112 Hasara Iliyotokana na Kutumia Vipimo Visivyo Sahihi Kufanya Malipo Sh. 217,922,196.12

Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ililipia jumla ya kilo 32,711 za rangi zenye thamani ya Sh. 228,977,000 kwa mkandarasi M/s Home Africa Investment Corporation Ltd, kwa ajili ya kupaka vyuma vya paa katika machinjio, pamoja na jengo la kupumzikia mifugo. Hata hivyo, nilibaini kuwa kipimo halisi kilichopaswa kutumika kitaalamu ni eneo la mraba (square area) 1579. 26 m2 (1,267.83 – jengo la machinjio na 311.43 – jengo la kupumzikia mifugo). Hivyo, kwa bei ya Sh. 7,000 kwa mita ya mraba gharama zingepaswa kuwa Sh. 11,054,820. Kutumia kipimo kisicho sahihi kumeisababishia Halmashauri hasara ya Sh. 217,922,196.12.

HALMASHAURI YA MJI KAHAMA

13.3.3.113 Vitabu 150 vya Kukusanyia Mapato Ambavyo Havikuwasilishwa kwa Ajili ya Ukaguzi Vyenye Thamani ya Sh. 150,000,000

Katika Halmashauri ya Mji wa Kahama nilibaini kuwa vitabu 150 vyenye thamani ya Sh. 150,000,000 havikuorodheshwa katika daftari la vitabu vya mapato na wala havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Vitabu hivyo ni sehemu ya vitabu 250 vilivyopokelewa mnamo tarehe 30 April, 2015 huku kila kimoja kikiwa na stakabadhi 100 zenye thamani ya Sh. 10,000.

13.3.3.114 Hasara Iliyopatikana kwa Kuwalipa Wazabuni Fedha Nyingi Kuliko Walizokusanya Katika Chanzo cha Mapato Yatokanayo na Ukusanyaji Taka Sh. 290,804,106

Katika kupitia mikataba baina ya Halmashauri ya Mji wa Kahama na na wazabuni, vikundi na watu mbalimbali kwa ajili ya kukusanya taka ngumu pamoja na tozo zake, pamoja na kupitia taarifa kwenyemfumo wa LGRCIS, nilibaini kuwa chanzo hiki cha mapato kilikusanya jumla ya Sh. 678,184,550 na kuwalipa wazabuni na vikundi vilivyohusika na ukusanyaji taka ngumu kiasi cha Sh. 968,988,656, hivyo kusababisha hasara ya Sh. 290,804,106.

13.3.3.115 Kutolipwa kwa Deni la Ushuru wa Huduma kwa Muda Mrefu Sh. 15,745,237,911

Nilibaini kuwepo kwa deni la ushuru wa huduma kiasi cha Dola za Kimarekani 6,780,894.88, sawa na Sh. 15,745,237,911 (kwa bei ya kubadilishia fedha ya Sh. 2,322) kutoka kwa kampuni ya ACACIA katika mgodi wa Bulyanhulu na mgodi wa Buzwagi, kuanzia mwaka 2001 hadi 2015. Licha ya mazungumzo ya muda mrefu yaliyofanyika kati ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Shinyanga, OR-TAMISEMI, Tume ya Madini, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Halmashauri ya Mji wa Kahama na kuthibitisha uhalali wa deni hilo na kuwasilishwa kwa hati ya madai kwa ACACIA, hakuna kiasi chochote kilicholipwa mpaka wakati namaliza ukaguzi mwezi Agosti, 2020.

13.3.3.116 Upotevu wa Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri Yaliyotumiwa na Mtunza Fedha wa Halmashauri Baada ya Kuwasilishwa Kwake na Wakusanya Mapato Sh. 141,606,500

Nilibaini kuwa jumla ya kiasi cha Sh. 141,606,500 kilichokuwa kimekusanywa na wakusanya mapato, kilitumiwa na mtunza fedha wa Halmashauri ya Mji wa Kahama kwa matumizi yake binafsi. Kati ya fedha hizo, kulikuwa na kiasi cha Sh. 98,779,700 kilichokusanywa kwa mkusanya mapato mwenye namba ya utambulisho (Payer's ID) 203300028237 na mkusanya mapato mwenye namba ya utambulisho 203300028235 aliyekusanya Sh. 42,826,800.

13.3.3.117 Zabuni Kutolewa Bila Kutangazwa Sh. 139,991,660

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, nilibaini kuwa Halmashauri ya Mji wa Kahama ilitoa zabuni ya ukarabati wa barabara na stendi ya Zongomera katika eneo la viwanda Dodoma kwa mzabuni mmoja kupitia mkataba wenye kumbukumbu namba LGA/155/2018/2019/W/01 wenye thamani ya Sh. 139,991,660 bila kuitangaza kinyume na Kanuni Na. 181 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013. Nilibaini pia kuwa Halmashauri haikupaswa kutumia hati msako ya bei (direct quotation) kwa mkandarasi huyu kwani njia hii ina vigezo ambavyo vinavyotakiwa kufikiwa ili kutumika.

13.3.3.118 Gharama Zilizozidi Uhalisia wa Kazi Sh. 76,950,000

Nilibaini kuwa jumla ya Sh. 76,950,000 zililipwa kimakosa kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi katika Halmashauri ya Mji wa Kahama. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh. 61,280,000 zililipwa kwa Mkandarasi alietekeleza mradi wenye mkataba namba GA/155/2019/2020/CSR-BARRICK/W/51 ulioingiwa mnamo tarehe 17 Mei, 2020 kwa ajili ya kukarabati stendi ya CDT na barabara zake, ambapo ilibainika kuwa eneo lililopaswa kujazwa mawe kwa mujibu wa mkataba lilikuwa kubwa kuliko eneo halisi lililofanyiwa kazi. Aidha, Mkandarasi Audacity Intercom (T) Ltd mwenye mkataba LGA/155/2018/2019/W/01 alilipwa jumla ya Sh. 15,670,000 zaidi baada ya kuzidisha baadhi ya vipengele vilivyokuwa katika mkataba.

13.3.3.119 Mkataba na Ubia wa Wakandarasi Ambao Hawajasajiliwa na CRB

Kinyume na matakwa yaliyopo katika kabrasha la zabuni, nilibaini kuwa Halmashauri ya Mji wa Kahama ilikubali kuingiza kwenye tathmini ya zabuni na hatimae kuupa kazi ushirika wa wakandarasi wawili (Joint Venture) bila ya ushirika huo kusajiliwa kwa ajili ya kazi hiyo na Bodi ya Usajili ya Wakandarasi (CRB). Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa wakandarasi walioomba kazi hii walikua wa daraja la saba wakati kazi hii ilihitaji kufanywa na mkandarasi wa daraja la tano na kuendelea.

13.3.3.120 Malipo kwa mzabuni Bila Ushahidi wa Matumizi Sh. 25,432,500

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Mji wa Kahama iliingia mkataba wenye namba ya zabuni LGA/155/2018/2019/C/01 na mzabuni mmoja kwa ajili ya kuandaa mpango wa biashara na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa stendi ya mabasi ya Kahama, ambao ulitaka mzabuni kurudishiwa baadhi ya gharama (reimbursable cost) endapo tu atazitumia na kuwasilisha nyaraka za matumizi yake. Hata hivyo, Halmashauri ilimlipa mzabuni huyo kiasi cha Sh. 25,432,500 bila ushahidi wa matumizi husika.

13.3.3.121 Ushindanishi wa Zabuni kwa Kutumia Nyaraka Zilizoghushiwa Sh. 641,628,500

Baada ya uhakiki wa nyaraka za zabuni na mawasiliano yaliyofanywa baina ya Ofisi yangu na Wazabuni waliodaiwa kushindanishwa kwenye zabuni za Halmashauri ya Mji wa Kahama, nilibaini kuwa Halmashauri hiyo kwa nyakati tofauti ilighushi nyaraka za zabuni kutoka kwa wazabuni waliokuwa wamedaiwa kushindanishwa katika zabuni yenye Na. LGA/155/2018/2016/C/01, kwa ajili ya kumtafuta mzabuni wa kuandaa mpango wa biashara (*business plan*) na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa stendi ya mabasi Kahama, yenye thamani ya Sh. 131,632,500 na zabuni yenye Na. LGA/155/2018/2019/C/02, kwa Wazabuni waliodaiwa kushiriki zabuni ya kuandaa michoro na makadirio ya kina ya gharama za ujenzi wa stendi kuu ya mabasi Kahama, yenye thamani ya Sh. 509,996,000.

HALMASHAURI YA WILAYA BARIADI

13.3.3.122 Ubadhirifu Kwenye Uwekaji Umeme Katika Kiwanda cha Mafuta ya Alizeti Dutwa Sh. 27,965,614

Katika kupitia nyaraka za malipo za Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, nilibaini kuwa jumla ya Sh. 27,965,614 zililipwa kwa njia ya fedha taslimu, ikiwa ni gharama za uwekaji umeme kwenye kiwanda cha kuchakata mafuta ya alizeti kilichopo eneo la Dutwa. Katika kuthibitisha uhalali wa malipo hayo, niliomba kupatiwa taarifa ya utafiti uliofanyika, (survey report), ankara za madai ya malipo, stakabadhi za mapokezi ya fedha hizo pamoja na taarifa ya utekelezaji kwa ajili ya uwekaji umeme katika kiwanda hicho, ambazo mpaka ukaguzi wangu unakamilika, TANESCO na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ulishindwa kunipatia nyaraka. Kukosekana kwa nyaraka hizo kunatia mashaka uhalali wa malipo yaliyofanyika.

13.3.3.123 Hasara Iliyopatikana Kwenye Ukodishaji Mitambo Pamoja na Ununuzi wa Bati Katika Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Sh. 28,958,909

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo Hati za Malipo katika mradi wa umwagiliaji Mwasubuya pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bariadi, nilibaini kuwa Kamati ya mradi wa umwagiliaji Mwasubuya iliridhia kuwalipa wakandarasi wawili jumla ya kiasi cha Sh. 51,920,000 badala ya Sh. 42,000,000 na hivyo kuipa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi hasara ya Sh. 9,830,000 ikiwa ni kosa lililosababishwa na ukodishaji mitambo kwa gharama ya Sh. 1,180,000 badala ya Sh. 1,000,000 kwa siku.

Pia, katika hatua nyingine, Halmashauri ya Bariadi ilimlipa mzabuni mmoja kiasi cha Sh. 114,959,126.92, ikiwa ni gharama ya manunuzi ya bati 2,392 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya badala ya Sh. 95,830,938 ambazo angelipwa mzabuni mwingine kwa manunuzi ya idadi sawa ya mabati 2,392, hivyo kusababisaha hasara ya Sh. 19,128, 990.

13.3.3.124 Manunuzi Yaliyofanyika Bila Vifaa na Huduma Iliyokusudiwa Kupatikana Sh. 7,336,000

Katika kupitia nyaraka za utekelezaji wa mradi wa Shule ya msingi Mwauchumu katika mwaka wa fedha 2017/18 kupitia mradi wa P4R, nilibaini kuwa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. 23,695,500 viliagizwa na kulipiwa kwa mzabuni ndugu Mabula Madoshi Mwandiki. Katika kujiridhisha juu ya mapokezi yake, ilibainika kuwa vifaa vyenye thamani ya Sh. 6,336,000 havikuletwa na mzabuni huyo kama vilivyoagizwa, pamoja na kulipwa Sh. 1,000,000 ya gharama za usafirishaji wa vifaa hivyo vya ujenzi.

HALMASHAURI YA WILAYA ITILIMA

13.3.3.125 Hasara ya Sh.241,948,610 iliyopatikana kwa kuwapa zabuni Wazabuni Wenye bei kubwa na kuwaacha Wazabuni Wenye bei ndogo pasipo sababu za msingi

Kwa kipindi cha miaka mitatu 2017/18 hadi 2019/20, H/W Itilima ilibainika kupata hasara ya jumla ya Sh. 241,948,610, baada ya

kutoa kandarasi kwa wazabuni waliokuwa na bei kubwa zaidi ya washindani wao kama ifuatavyo;

Katika mradi wa usambazaji wa mabomba ya maji katika kijiji cha mwamapalala Namba IDC/151/2016-2017/HQ/W/O5/LOT 1 mzabuni Best one Co.ltd aliyekuwa na bei ya Sh 616,128,097 alipewa dhidi ya mzabuni mwenye bei ya chini aliyekuwa na bei ya Sh 408,710,874, hivyo kusababisha hasara ya Sh. 207,417,223

Katika mradi Namba LGA/151/2016-2017/HQ/W/O5/LOT III wa usambazaji mabomba ya maji katika kijiji cha kabale, mzabuni M/s Juin Company Ltd, S.L.P. 62079, DSM aliyekuwa na bei ya Sh. 480,745,837 alipewa dhidi ya mzabuni mwenye bei ya chini aliyekuwa na bei ya Sh. 446,214,450, hivyo kusababisha hasara ya Sh. 34,531,387. Hivyo jumla katika zabuni zote mbili H/W Itilima ilipata hasara ya Sh. 241,948,610

13.3.3.126 Mkandarasi Kulipwa Sh.24,574,000 zaidi ya alichostahili kulipwa

Mkandarasi na M/s Sepro Engineering and General Traders wa S.L.P 20862, Dar es salaam aliyekuwa na Mkataba namba.IDC/151/2016-2017/HQ/W/O5/LOT IV wa kusamabaza maji katika kijiji cha Isengwa, alilipwa jumla sh. 92,204,000 badala ya Sh. 67,630,000 kwenye kipengele 3.9.1 , 2.5.1 na kipengele 2.2.1 na hivyo kuisababishia hasara halmashauri kiasi cha Sh. 24,574,000.

Ninapendekeza kuwa hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watumishi waliotajwa katika ripoti husika ya Ukaguzi kuhusiana na Ukaguzi wa Halmashauri hii kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo na hivyo kusababisha matumizi yasiyo na tija na matumizi mabaya ya fedha za umma na kuisababishia Serikali hasara kwa kuwalipa wakandarasi fedha nyingi kuliko walizostahili kulipwa. Pia, ninaishauri menejimenti ya Halmashauri kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani wakati wa kufanya malipo.

HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

13.3.3.127 Fedha za Miradi Kutumika Katika Shughuli Zisizopangwa Sh. 1,078,868,254

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2019/2020, fedha za miradi kiasi cha Sh. 1,078,868,254 zilitumika kwa shughuli zisizo za miradi bila kuwa na kibali cha kubadilisha matumizi kutoka kwa mamlaka husika. Fedha hizi zilitengwa kwa ajili mradi wa maendeleo wa EQUIP wenye gharama ya Sh. 101,657,462 na Sh. 977,210,792 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri.

13.3.3.128 Miradi Iliyotelekezwa Muda Mrefu Bila Kukamilishwa Sh. 760,650,799

Nilibaini kuwa hadi kufikia mwezi Agosti, 2020, miradi hamsini na tisa (59) iliyoibuliwa kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 yenye jumla ya Sh. 760,650,799, ilitelekezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Itigi bila kukamilishwa. Kati ya miradi hiyo, miradi 13 ni ya 2013/14, miradi 22 ya 2017/18, miradi 17 ya 2018/19, mradi 1 wa mwaka 2008/2009 na miradi 6 ya mwaka 2019/20. Miradi hii iliibuliwa katika Sekta za Elimu na Afya na ilikuwa inatekelezwa kwa ufadhili wa nguvu ya wananchi pamoja na Serikali.

HALMASHAURI YA WILAYA MKALAMA

13.3.3.129 Malipo Yaliyofanyika Zaidi ya Gharama za Mkataba kwa Mkandarasi Sh. 112,839,784.50

Nilibaini kuwa jumla ya Sh. 112,839,784.50 zililipwa kwa Mkandarasi M/S Mzinga Holdings Co.Ltd katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya, wenye namba Na.LGA/147/2014/15/W/01 zaidi ya kiasi kilichokubalika kimkataba. Kwa mujibu wa mkataba, Mkandarasi alipaswa kulipwa Sh. 758,180,798, ingawa Halmashauri ilimlipa Sh. 871,020,667.56. Kiasi cha Sh. 112,839,784.50 kilichoongezeka kilifanywa kwenye malipo ya mwisho kwa Mkandarasi M/s Mzinga Holdings Co Ltd kupitia Cheti Na. 6.

13.3.3.130 Malipo yaliyofanyika kwa uthibitisho wa stakabadhi/risiti zisizo na thamani ya fedha iliyolipwa ya Sh. 61,016,760

Ukaguzi wangu katika halmashauri ya wilaya ya Mkalama ulibaini kuwa jumla ya Sh. 61,016,760 kwa mzabuni mmmoja wa Halmashauri kupitia hati za Malipo yenye kumbukumbu namba 2017-001717 na 2017-000635 zilizokuwa zimelipa Sh. 23,900,000 Na Sh. 38,362,000 mtawalia kwa kutumia risiti za udanganyifu na zisizoonesha thamani ya mali zilizonunuliwa. Hili lilifanyika kwa kuwa stakabadhi ya kielektroniki iliotolewa na mzabuni ilithibitisha kupokelewa kwa Sh. 61,016,760 lakini pia risiti hiyo ilionesha kuwa mzabuni alirudisha chenji ya kiasi hicho hicho cha fedha na hivyo kuifanya risiti kutokuwa na thamani.

Ninazishauri Mamlaka husika kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi waliotajwa katika ripoti ya Ukaguzi maalum kwa halmashauri hii kwa kushiriki kuandaa hati za malipo, kuidhinisha na hatimaye kulipa fedha kwa mkandarasi fedha nyingi kuliko alizostahili. Vilevile Halmashauri wanashauriwa kuitaarifu Ofisi ya Mamlaka ya Mapato juu ya mzabuni huyo. Vile vile Mamlaka ya Mapato Tanzania Inashauriwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Halmashauri ili kuweza kubaini risiti zenye mapungufu au zilizoghushiwa.

HALMASHAURI YA WILAYA MOMBA

13.3.3.131 Mshauri Mwelekezi kulipwa Sh. 88,505,340 Mara Mbili kwa Kazi Ambazo Hastahili Kulipwa

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Momba ilimlipa asilimia 30 Mshauri Mwelekezi M/s MUST Consultancy Bureau, kiasi cha Sh. 88,505,340 kwa hati ya malipo namba 903114V1900659 ya terehe 10 Januari, 2019 kwa ajili ya kuandaa na kuwasilisha taarifa ya awali (*inception report)*. Pia Halmashauri ilimlipa tena Mshauri Mwelekezi asilimia 30 ya makubaliano ya Sh. 88,505,340 kwa hati ya malipo Na. 903114V1901505 ya terehe 08 Mei, 2019, kwa ajili ya uandaaji wa taarifa ya usanifu wa awali pamoja na gharama za mradi, kazi zinazoonekana kufanana.

13.3.3.132 Gharama Zisizostahili Katika Ujenzi wa Nyumba za Watumishi Sh. 719,189,008.39

Katika kupitia mchanganuo wa makadirio ya ujenzi (Bill of Quantities) wa Nyumba za Watumishi wa Halmashauri, nilibaini uwepo wa malipo ya jumla ya Sh. 719,189,008.39, ikiwa ni gharama za kazi ambazo hazikupaswa kujumuishwa kwenye mradi na ambazo zingeweza kuepukika kwa sababu hazihusiani moja kwa moja na utekelezaji wa mradi. Hata hivyo, hadi mwezi Juni, 2020, Halmashauri ya Wilaya ya Momba ilikuwa inadaiwa jumla ya Sh. 384,878,929.01 na mkandarasi ili kukamilisha malipo kama mkataba unavyotaka.

Uongozi wa Hlamashauri unashauriwa kuchukua hatua zinazofaa kuhakikisha kuwa malipo hayo yanarudishwa kwa Halmashauri kwa kuwa hayakuwa na tija kwa utekelezaji wa mradi. Pia, hatua zinazofaa zinapaswa kuchukuliwa na mamlaka zinazohusika dhidi ya mkandarasi mshauri kwa kuomba malipo kulipwa kwa shughuli moja mara mbili. Hatua inapaswa pia kuchukuliwa dhidi ya wafanyakazi wa Halmashauri waliotajwa katika ripoti maalumu kwa kuhusika kwao katika matumizi mabaya ya fedha za serikali.

HALMASHAURI YA MANISPAA TABORA

13.3.3.133 Vitabu 84 vya Kukusanyia Mapato (HW5) Kutowasilishwa kwa Ajili ya Ukaguzi

Jumla ya vitabu 84 vya kukusanyia mapato vilivyogawiwa kwa wakusanya mapato katika Halmshauri ya Manispaa ya Tabora kwa kipindi cha mwaka 2017/18 hadi 2019/2020, havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Hivyo, ukaguzi wangu haukuweza kujua kiasi cha fedha kilichokusanywa na kuwasilishwa benki kupitia vitabu hivyo.

13.3.3.134 Hasara Itokanayo na Malipo ya Ziada Yaliyosababishwa na Ucheleweshaji wa Ukamilishaji wa Mradi Sh. 107,770,000

Katika kipindi cha mwaka 2017/2018 na 2018/2019, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilimlipa mshauri mwelekezi M/s Advanced Engineering Solution Ltd Sh. 107,770,000 ikiwa ni nyongeza ya

gharama ya kusimamia mkataba namba LGA/124/2016/2017/W/02 LOT-10. Ukaguzi ulibaini kuwa wakandarasi Salum Motors Transport Co. Ltd na JV Anam Road Works, waliomba ongezeko la muda wa kumaliza kazi kupitia kwa mshauri mwelekezi M/s Advanced Engineering Solution Ltd, ambaye alikataa maombi hayo na kuishauri Halmashauri kutoongeza muda; badala yake, iwatoze wakandarasi makato kwa kushindwa kukamilisha kazi kwa muda na kwa mujibu wa mkataba.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Halmashauri hakuzingatia ushauri huo na kuamua kuwaongezea muda bila sababu za msingi, jambo ambalo lilipelekea Mshauri mwelekezi kulipwa ongezeko la Sh. 107,770,000 kwa ajili ya kuwasimamia wakandarasi hao, katika kipindi hicho cha nyongeza.

13.3.3.135 Hasara Kutokana na Malipo ya Fidia ya Ardhi Yenye Nyaraka za Kughushi Sh. 52,400,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora iliwalipa fedha kiasi cha Sh. 60,000,000 wakandarasi Salum Motors Transport Co. Ltd na JV Anams Road Works, kupitia mkataba Na. LGA/124/2016-2017/W/02-LOT11, ikiwa ni gharama ya ununuzi wa sehemu ya kuchimbia vifusi kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Hata hivyo, mapitio ya mikataba ya ununuzi na maelezo kutoka kwa wauzaji watatu wa maeneo manne ya ardhi yaliyotumika kuchimba vifusi, walikiri kupokea Sh. 7,600,000 tu kutoka kwa wakandarasi na hivyo kupelekea wakandarasi kulipwa zaidi kwa Sh. 52,400,000, ambazo hazikuthibitishwa kuwa na nyaraka halali.

13.3.3.136 Malipo ya Fedha za Matazamio Zaidi ya Kiasi Kilichokatwa Sh. 212,262,734

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/2020, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilimlipa mkandarasi kiasi cha Sh. 630,003,259.39 kama marejesho ya fedha za matazamio (retention money) badala ya Sh. 417,740,525 iliyokatwa awali na hivyo kupelekea malipo zaidi ya Sh. 212,262,734, kinyume na Sharti la 50.2 la Masharti ya Jumla ya Mkataba Na.

LGA/124/2016/2017/W/02/LOT10 wenye gharama ya Sh. 8,222,664,626.25, kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji uliotekelezwa katika kijiji cha Hedaru.

Ninapenda kuishauri Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kuchukua hatua stahiki dhidi ya wafanyakazi wa halmashauri waliohusika katika usimamizi wa miradi husika kwa kutosimamia kikamilifu na walioandaa hati za malipo, kuidhinisha na hatimaye kulipa fedha hizo kwa wakandarasi na hivyo kupekea matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha, Halmashauri inashauriwa kufanya jitihada za kurejesha fedha hizo kutoka kwa wakandarasi tajwa hapo juu. Vilevile, Menejimenti ya Halmashauri wanapaswa kuvitafuta vitabu vyote vya kukusanyia mapato kama vinavyooneka na katika ripoti husika na kuviwasilisha ofisini kwangu kwa ajili ya Ukaguzi.

HALMASHAURI YA MJI NZEGA

13.3.3.137 Fedha za Ujenzi na Ukarabati wa Kituo cha Afya Zogolo Kutumika Katika Shughuli Zisizopangwa Sh. 97,811,500

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Mji wa Nzega ilitumia fedha Sh. 97,811,500 za ujenzi wa jengo la upasuaji, wodi ya kina mama na watoto, nyumba moja ya mtumishi inayojitegemea, maabara, jengo la kuhifadhia maiti na kichomea taka, ukarabati wa wodi ya wanaume na wanawake, nyumba sita za watumishi, jengo la kufulia, ukarabati na ujenzi wa njia za kupitia wagonjwa, vyoo vya wagonjwa wa nje na upakaji rangi bati la jengo la wagonjwa wa nje (OPD) kinyume na muongozo Na.AD.296/303/01/1/70 kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI wa tarehe 16 Agosti, 2017.

13.3.3.138 Hasara Kutokana na Wazabuni Kuondolewa Kimakosa Wakati wa Tathmini Sh. 54,444,020

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora iliingia mkataba wenye namba LGA/170/2017-18/06 wa Sh. 438,226,040 na mkandarasi kwa ajili ya utafiti wa kijiografia, kuchimba na kujenga visima 15 na mkataba Na.LGA/170/2017-18/02 wenye thamani ya Sh. 398,530,840 kwa ajili ya kuchimba

na kujenga visima 13 vya kusambaza maji. Katika mkataba wa visima 15, mzabuni aliyeomba kufanya kazi hiyo kwa Sh. 400,683,160 alienguliwa na kusababisha hasara ya Sh. 37,542,880 baada ya kumpa mzabuni aliyetekeleza mradi huo kwa Sh. 438,226,040 bila sababu yoyote ya msingi kwani uhakiki wangu ulibainisababu za kumuondoa mzabuni huyo hazikuwa sahihi.

Aidha, kama ilivyokuwa kwa mkataba hapo juu ukaguzi wangu ulibaini pia kuwa katika mkataba wa visima 13, mzabuni aliyeomba zabuni hiyo kwa Sh. 381,629,700 alienguliwa katika mchakato wa zabuni na hivyo kusababisha hasara ya Sh. 16,901,140 baada ya kumpa mzabuni aliyetekeleza mradi huo kwa Sh. 398,530,840. Hivyo Halmashauri ilipata hasara ya jumla ya Sh. 54,444,020.

Ninapendekeza hatua zstahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa ambao waliunda sehemu ya kamati ya tathmini na wajumbe wa Bodi za Zabuni kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kusababisha Halmashauri kupata hasara kwa kuwapa wazabuni wenye bei kubwa na kuwaacha wazabuni wenye bei ndogo bila sababu za msingi. Kadhalika, hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa kwa watumishi wa Halmashauri waliotajwa katika ripoti maalum ya ukaguzi huu ambao kwa namna moja ama nyingine walishiriki katika kuridhia na kufanya malipo kwa kutumia fedha za ujenzi na ukarabati wa kituo cha afya Zogolo kwa matumizi mengine yaliyokuwa hayajakusudiwa. Menejimenti ya Halmashauri, katika utekelezaji wa majukumu yao, inapaswa kuhakikisha inafikia viwango vya juu zaidi vya usawa, kwa kuzingatia- (a) usawa wa fursa kwa wazabuni wote; (b) usawa kwa pande zote; na (c) hitaji la kupata thamani halisi ya fedha ikizingatia ubora na bei.

HALMASHAURI YA WILAYA SIKONGE

13.3.3.139 Malipo Ambayo Hayakustahili Kiasi cha Sh. 56,500,000 Katika Ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya Sikonge

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge nilibaini kuwa malipo yenye jumla ya Sh. 56,500,000 yalilipwa kwa mkandarasi kinyume na taratibu, ikiwa ni Sh. 20,500,000 kwa huduma ambazo

hazikutolewa na Sh. 36,000,000 kwa gharama ambazo zilikwisha jumuishwa kwenye vipengele vingine vya mradi husika.

13.3.3.140 Mapungufu Katika Michoro ya Majengo Yaliyopelekea Hasara ya Sh. 28,187,800

Ukaguzi ulibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ilipata hasara ya Sh. 28,187,800 kwa kutumia michoro yenye mapungufu katika ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri, na jengo la maabara, wodi ya wazazi na nyumba ya mtumishi. Kati ya hasara hiyo, Sh. 10,443,000 ilitokana na kazi za nyongeza za kuvunja kuta zilizojengwa kimakosa na kujenga upya kuta katika ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri. Aidha, kiasi cha Sh. 17,744,800 kilitokana na ujenzi wa Kituo cha Afya Kitunda uliosababishwa na kuanza kazi za ujenzi bila ya kutumia ramani rasmi baada ya kutembelewa na timu ya Mganga Mkuu wa mkoa akiongozana na maafisa toka Ofisi ya Rais-TAMISEMI na kuagiza kuvunjwa kwa kuta za jengo hilo.

Mamlaka husika zinapaswa kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi wa Halmashauri waliohusika katika ujenzi wa jengo bila kufuata ramani rasmi .Vilevile Hatua stahiki zichukuliwe ili kurejesha fedha zilizolipwa kwa kazi ambazo hazijatekelezwa.

HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

13.3.3.141 Malipo ya kamisheni kwa wakala yasiyostahili Sh. 164,946,176

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 na 2019/20, Halmashauri ililipa Sh. 164,946,176 kwa wakala wa kukusanya ushuru wa madini ya mawe, chokaa, mchanga na kokoto. Katika barua ya uteuzi aliyopewa mzabuni huyo iliainishwa kwamba, wakala angelipwa 25% ya makusanyo aliyowasilisha Halmashauri. Hata hivyo mkataba haukuainisha kiwango cha asilimia ya makusanyo atakacholipwa wakala kama kamisheni ya ukusanyaji wa mapato kwenye chanzo hicho. Fedha hiyo iliyolipwa ni 25% ya Sh. 659,784,702.25 ambayo ni mapato yaliyolipwa moja kwa moja katika akaunti ya Halmashauri na kampuni za madini. Hivyo basi, Halmashauri haikuwa makini vya kutosha katika kuingia mkataba huu kwa kuwa Kampuni zinalipa moja kwa moja kwenye akaunti za Halmashauri na kwamba inapohitajika, Halmashauri ingeweza

kutumia vikosi kazi vya mapato ya ndani na kwa hivyo wakala hakuwa lazima kutumika katika chanzo hiki cha mapato, na malipo yaliyofanywa hayastahili na hayana manufaa kwa Serikali. Mpaka kufikia Agosti, 2020, fedha hizo hazikuwa zimerejeshwa katika akaunti ya benki ya Halmashauri kutoka kwa wakala huyo.

13.3.3.142 Malipo yaliyolipwa zaidi kinyume na matakwa ya Mkataba Sh. 24,521,890

Kwa mujibu wa mkataba, fundi anapaswa kulipwa asilimia 25 ya gharama za vifaa vinavyotumika katika ujenzi. Katika kupitia malipo yaliyofanywa kwa fundi katika mwaka wa fedha 2017/18 na 2018/19 katika mkataba wa ukarabati wa majengo ya shule, nilibaini kuwa Halmashauri ya Jiji la Tanga ilimzidishia fundi malipo kwa kiasi cha Sh. 24,521,890 kilichosababishwa na kulipwa Zaidi ya asilimia 25 ya gharama za ununuzi wa vifaa iliyoko kwenye mkataba. Badala ya kumlipa Fundi Sh 64,059,138 (25% ya gharama ya vifaa ya Sh.256,236,546), nilibaini kuwa fundi alilipwa Sh.88,581,028. Hata hivyo, Halmashuri haikufanya juhudi za kurejesha fedha hizo hadi kufikia mwisho wa ukaguzi maalumu (Agosti, 2020).

13.3.3.143 Hasara iliyotokana na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kulipwa kwa wazabuni wasiosajiliwa Sh. 48,131,185

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2018/19, nilibaini malipo ya Sh. 267,395,471 yaliyofanywa na Halmashauri kwa zabuni mbalimbali wa vifaa vya ujenzi. Malipo hayo yalijumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya Sh. 48,131,185, kwa wazabuni ambao hawakustahili kulipwa kutokana na wazabuni hao kutosajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kulipa kodi ya ongezeko la thamani.

13.3.3.144 Matofali yaliyotolewa kwa wateja zaidi ya kiwango walicholipia Sh. 56,371,200

Mnamo agosti, 2018, Halmashauri ilianza mradi wa kuuza tofali. Ukaguzi maalumu ulibaini kuwa kuanzia tarehe 3 Septemba, 2018 hadi tarehe 5 Julai, 2020, wateja 11 walilipia jumla ya matofali 129,467 na kuchukua matofali 164,699, hivyo kusababisha tofauti ya matofali 35,232 yenye thamani ya Sh. 56,371,200 kuchukuliwa

Zaidi ya kiwango kilicholipiwa, na ikiwa matofali hayo hayatalipiwa, hiyo itakuwa ni hasara kwa Halmashauri.

13.3.3.145 Manunuzi yaliyofanywa kwa Mtumishi wa Halmashauri Sh 120,970,000

Katika kupitia malipo yaliyofanywa kwa wazabuni mbali mbali wa Halmashauri katika mwaka wa fedha 2019/20 ilibainika kuwa jumla ya Sh. 120,970,000 zililipwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi, mchanga na kokoto katika kutekeleza miradi ya ujenzi katika Halmashauri. Uhakiki wa Kampuni iliyotoa huduma hiyo kwa Halmashauri kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na upembuzi wa taarifa mbalimbali za Halmashauri ulibaini kuwa, mzabuni aliyetoa huduma hiyo kwa Halmashauri ni mtumishi wa Halmashauri aliyeko idara ya manunuzi. Ununuzi wa vifaa mbalimbali kutoka kwa mtumishi wa kitengo cha manunuzi cha Halmashauri unaweza kusababisha Halmashauri kukosa haki ya kupata bei shindanishi.

13.3.3.146 Kutotumika kwa muda mrefu Mashine ya kufyatua Matofali iliyonunuliwa kwa gharama ya Sh.130,000,000

Mnamo mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri kupitia TISS Na. 50000392 ya tarehe 8 Machi, 2019, ilinunua mashine ya kufyatua matofali yenye thamani ya Sh. 130,000,000. Mashine ilipokelewa kwa hati ya mapokezi Na. 0041 ya tarehe 15 Machi, 2019. Kufanya kazi kwa mashine hii kulihitaji uwepo wa mashine ya kubebea mizigo (fork lift) ili kubeba tofali kutoka kwenye mashine na kupelekwa eneo la kupangia kwa ajili ya kukaushwa. Ukaguzi ulibaini kuwa hadi wakati wa Ukaguzi huu tarehe 11 Agosti, 2020 ikiwa ni takribani miezi kumi na sita tangu kununuliwa kwa mashine hiyo ya kufyatulia tofali, ilikuwa haijaanza kutumika kwa sababu Halmashauri haikuwa imenunua mashine hiyo ya kubebea Mizigo. Kwa maoni yangu, hali hii ilisababishwa na kutofanyika kwa upembuzi yakinifu wa mahitaji stahiki kabla ya kuibuliwa miradi na kuanza utekelezaji. Kitendo hicho kinaweza kupelekea uharibifu wa mashine hiyo, kuchakaa na kusababisha hasara kwa Halmashauri.

13.3.3.147 Hasara kutokana na udanganyifu kwenye vipimo vya mageti Sh. 10,987,019

Ukaguzi uliofanyika tarehe 14 Agosti, 2020 ulibaini kuwa, Halmashauri ilimlipa Mkandarasi Sh. 30,000,000 kwa ajili ya kutengeneza na kuweka mageti katika shule za msingi Kombezi na Makorora. Kutokana na vipimo halisi, mkandarasi alistahili kulipwa Sh.19,012,981, hivyo kuisababishia Halmashauri hasara ya Sh.10,987,019 zilizolipwa kinyume na matakwa ya mkataba.

13.3.3.148 Vifaa tiba vilivyolipiwa lakini havijafikishwa Kituo cha Afya Duga Sh. 175,679,500

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Halmashauri kupitia hati ya malipo Na.862018V1901710 ya tarehe 1 Machi, 2019 ililipa Sh. 200,000,000 Bohari ya dawa (MSD) kwa ajili ya vifaa tiba vya kituo cha afya Duga. Hata hivyo, kati ya kiasi kilicholipiwa, vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. 24,320,500 tu ndivyo vilivyopokelewa hadi tarehe 3 Agosti, 2020. Vifaa Tiba vyenye thamani ya Sh. 175,679,500 vilibainika kutofikishwa Kituo cha Afya Duga, ikiwa ni zaidi ya siku 480 tangu tarehe ya malipo.

Ninapendekeza kwamba menejimenti ya Halmashauri ya Jiji la Tanga inapaswa kufuatilia MSD ili kuhakikisha vifaa tiba hivyo vinaletwa. Kwa kuongezea, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wafanyikazi wa Hlamashauri waliotajwa katika ripoti maalum ya ukaguzi kwa madhaifu yaliyobainishwa. Vilevile, ninapendekeza menejimenti ya Halmashauri kuimarisha udhibiti wa ndani juu ya mambo yote yaliyojitokeza katika ukaguzi.

HALMASHAURI YA WILAYA MKINGA

13.3.3.149 Malipo yaliyolipwa zaidi ya gharama ya makubaliano kimkataba Sh. 11,613,667

Halmashauri ya Wilaya Mkinga iliingia makubaliano ya nyongeza ya Mkataba Na. MKG/DC/BLD/DHQ/F07/08/6 na mkandarasi, kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kwa gharama ya Sh. 121,179,250.

Hata hivyo, ukaguzi maalumu ulibaini kuwa, Halmashauri ilimlipa mkandarasi Sh. 132,792,917 na kusababisha malipo ya ziada ya Sh. 11,613,667.18 juu ya makubaliano ya nyongeza ya mkataba yaliyoridhiwa na kupitishwa.

Ninapendekeza kwamba mkandarasi arejeshe kiasi cha Sh. 11,613,667 zilizolipwa kwa kazi ambazo hazijatekelezwa. Pia, mamlaka husika ziichukulie hatua stahiki kampuni iliyolipwa malipo Zaidi ya makubaliano pamoja na wafanyikazi ambao wametajwa katika kufanya malipo hayo.

HALMASHAURI YA MJI WA KOROGWE

13.3.3.150 Kushindwa kukusanya mapato ya ndani kutoka kwenye vibanda na vizimba Sh.1,855,512,000

Kwa muda wa miaka mitatu kuanzia 2017/18 hadi 2019/20, ukaguzi ulibaini upotevu wa mapato ya jumla ya Sh. 1,855,512,000 katika maeneo mawili tofauti ya vibanda na vizimba kama ifuatavyo:

(i) Halmashauri haikukusanya mapato ya ndani kutoka kwenye vibanda vilivyoko maeneo ya maduka yaliyozunguka soko la Manundu, Kituo cha zamani cha mabasi na maduka yaliyopo eneo la Hekuse yenye thamani ya Sh.1,836,720,000

(ii) Halmashauri ilishindwa kukusanya mapato ya jumla ya Sh.18,792,000 yatokanayo na kodi ya upangishaji vizimba katika soko la Manundu vinavyomilikiwa na Halmashauri na kupangishwa kwa wafanyabiashara

13.3.3.151 Mapato yanayopotea kwa kutokusanywa ushuru wa taka ngumu Sh.186,768,000

Nimepitia mfumo wa ukusanyaji wa takataka wa Halmashauri na kubaini kuwa, Halmashauri ilitoa trekta, dereva na mafuta ya trekta kwa vikundi vidogo vya wananchi vinavyokusanya taka ngumu. Kwa taarifa iliyotolewa, makadirio ya ukusanyaji wa mapato yalifanywa kwa kuzingatia idadi ya kaya na ukusanyaji wa ada zilizolipwa ili kuhakikisha kiasi cha fedha ambazo zingekusanywa endapo Halmashauri ingekusanya taka ngumu

yenyewe, na fedha hizo kuwekwa kwenye akaunti. Kwa kufanya hivyo, nilibaini kuwa Halmashauri ilipoteza fursa ya kukusanya jumla ya Sh. 186,768,000 kutoka mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 ikiwa Halmashauri yenyewe ingekusanya fedha katika chanzo hiki.

13.3.3.152 Udanganyifu uliosababishwa na kubadili tarehe zinazosomeka katika mfumo wa mapato kwa mashine za kukusanyia mapato (POS)

Ingawa mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani (LGRCIS) ulianzishwa nchini katika mwaka wa fedha 2015/16, ilibainika kuwa kifaa cha POS kilichokuwa na usajili "Device-13 Prezzdar 6", IMEI namba 352388079881382 na utambulisho wa Mlipaji Namba 202500005757 kilikusanya mapato kwa tarehe za mbele na tarehe za kabla ya mfumo kuanzishwa. Matokeo yake baadhi ya makusanyo kwa kutumia kifaa hiki hayakuweza kuonekana katika mfumo wa ukusanyaji mapato wa Halmashauri.

13.3.3.153 Fidia ya ucheleweshaji kazi haikutozwa katika Mradi wa barabara Sh. 84,344,509

Halmashauri ya mji wa Korogwe ilifanya makubaliiano ya kimkataba na mkandarasi kupitia mkataba Na. LGA/126/2018/2019/W/09-LOT, ulioanza tarehe 7 Agosti, 2019 na kupaswa kuisha tarehe 8 Juni, 2020 (ikiwa ni tarehe ya ongezeko la muda wa kutekeleza kazi alilopewa mkandarasi), kwa thamani ya mradi ya Sh. 1,102,542,600. Ukaguzi wa mkataba pamoja na tathmini iliyofanyika baada ya kutembelea mradi husika ulibaini kuwa, hadi wakati ukaguzi huu unakamilika tarehe 10 mwezi Agosti, 2020, mkandarasi alikuwa hajakamilisha kazi. Kinyume na matakwa ya kifungu namba 5.1.1 cha Masharti ya jumla ya mkataba (GCC) na kifungu namba 22 ya masharti maalum ya mkataba (SCC) vikisomwa pamoja na kanuni ya 112 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 zinazotaka mkandarasi kukatwa ama kulipa fedha ya fidia inayotokana na ucheleweshwaji wa kazi, nilibaini mkandarasi hakukatwa fidia hiyo katika malipo yake kwa siku 51 alizochelewesha kazi mpaka Ukaguzi huu unakamilika. Kimkataba mkandarasi alipaswa kukatwa jumla ya Sh. 1,653,813.90 (ikiwa ni sawa na 0.15% ya

thamani ya mkataba) kwa kila siku anayochelewa kumaliza kazi, ila makato yote kwa ujumla yasizidi 10% ya jumla ya mkataba ambayo ni sawa na kuchelewa kukamilisha kazi kwa siku 100. Hivyo, hadi tarehe hiyo ya ukaguzi, mkandarasi alipaswa kukatwa Jumla ya Sh. 84,344,508.90 (siku 51 X Sh.1,653,813.90)

Halmashauri ya Mji wa Korogwe inapaswa kuhakikisha kuwa upembuzi yakinifu unafanywa kabla ya kufanya maamuzi. Vilevile, ninapendekeza Serikali kuhakikisha kuwa udhibiti wa ndani unatengenezwa na kuimarishwa ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye tarehe zilizowekwa kwenye mashine za kukusanyia mapato ya POS. Pia, Halmashauri zinapaswa kutoza tozo ya ucheleweshwaji wa kazi ya Sh. 84,344,509 kwa miradi iliyocheleweshwa na kuendelea kufuatilia utendaji wa mkataba kwa kuzingatia masharti ya mikataba.

13.4 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

13.4.2 HITIMISHO

Ukaguzi Maalumu uliofanyika katika Halmashauri zilizokaguliwa ulibaini ukiukwaji mkubwa wa taratibu katika mfumo wa uibuaji wa vyanzo vya mapato na ukusanyaji wa mapato ya ndani, mchakato wa matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo, usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, utunzaji wa amana za Halmashauri, usimamizi wa fidia za ardhi na mfumo wa udhibiti wa ndani. Mapungufu yaliyobainika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni pamoja na kwenye ujenzi wa majengo ya halmashauri, Ujenzi wa Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya, ujenzi wa mashule na miradi ya maji, kwa njia ya wakandarasi na “Force Account”.

Ukaguzi pia umebaini ubadhilifu mkubwa wa fedha za umma ndani ya Halmashauri zilizokaguliwa; hali inayoonekana ndani ya sampuli ya Halmashauri hizi inaweza kuwa inaakisi hali ilivyo kwenye Halmashauri nyingine nchini ambazo hazikufanyiwa ukaguzi maalumu. Pia, Ukaguzi Maalumu umebaini viongozi wamekuwa wakitoa maelekezo/maagizo kwa njia ya mdomo kwa

watendaji nao kuyatekeleza hivyo kuathiri utendaji kazi wao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

13.4.3 MAPENDEKEZO YA JUMLA

Kwa Mujibu wa Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 pamoja na Kanuni ya 34 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka, 2009; Mdhibiti na Mkaguzi MKuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kutoa mapendekezo pale atakapoona kufanya hivyo kutazuia ama kupunguza matumizi yasiyo na tija, kuongeza makusanyo ya Serikali na kuepusha hasara kwa Serikali kutokana na uzembe, kutojali, wizi, ubadhilifu ama rushwa.

Kufuatia mambo yaliyoonekana wakati wa ukaguzi huu maalum ikiwa ni pamoja na hatua za kiutawala na kisheria zitakazochukuliwa na mamlaka husika kwa wahusika wa kila suala, kwa ujumla ninashauri mambo yafuatayo kwa ajili ya kuboresha hali ya utendaji kazi katika Halmashauri ili kuleta ufanisi katika kukusanya mapato na kufikia malengo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo:

Mapendekezo kwa Wizara ya Maji

a) Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watendaji wa Halmashauri kama walivyotajwa kwenye taarifa za ukaguzi maalumu kwa kushindwa kusimamia mikataba na matumizi ya fedha za Serikali na kupelekea matumizi yasiyo husiana na miradi ya maji.

b) Wizara inapaswa kuandaa mpango mkakati wa kuhakikisha kuwa jamii iliyolengwa kwenye miradi isiyofanya kazi wala kutoa huduma kwa jamii, inapata huduma ya maji kama ilivyokusudiwa.

c) Wizara ya Maji ichukue hatua za haraka za kulipa madeni ya kiasi cha Sh 4,055,776,641.24 kwa muda muafaka, ili kuinusuru miradi yote ya maji na kuepusha fidia itokanayo na ucheleweshaji wa kulipa madeni hayo.

d) Hatua stahiki zichukuliwe kwa Maafisa Masuuli kwa kushindwa kutekeleza mwongozo wa kuomba msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika miradi ya maji. Aidha, katika siku zijazo,

Halmashauri zisisitizwe kufuata miongozo kwa kuomba msamaha wa kodi kwa mamlaka husika.

e) Hatua stahiki zichukuliwe kwa watendaji wa Halmashauri waliohusika katika matumizi ya fedha zaidi ya mkataba bila kibali kutoka Wizara ya Maji

f) Wizara ifanye usimamizi na ufuatiliaji wa mara kwa mara katika mamlaka za serikali za mitaa, ili kuhakikisha kuwa zinazingatia sheria na kanuni za manunuzi pamoja na miongozo mingine katika kutekeleza miradi ya maji. Pia, Serikali itoe mafunzo ya mara kwa mara kwa wajumbe wa bodi za zabuni na vitengo vya manunuzi, ili kuwaongezea watumishi hao maarifa katika michakato ya manunuzi. Zaidi ya hayo, kwa ushirikiano na OR – TAMISEMI hatua stahiki zichukuliwe kwa mamlaka za serikali za mitaa na watumishi ambao wanakiuka sheria, kanuni na taratibu za manunuzi

Mapendekezo kwa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA)

a) Mameneja wa RUWASA husika wanapaswa kuandaa mpango mkakati wa kuhakikisha jamii iliyolengwa kwenye miradi isiyofanya kazi wala kutoa huduma kwa jamii, inapata huduma ya maji kama ilivyokusudiwa hasa katika ile miradi ambayo maamuzi yake yanaweza kufanyika katika ngazi ya Mkoa au Wilaya.

b) RUWASA inapaswa kuyafanyia kazi mapungufu yote yaliyobainishwa ili kufanya miradi ya maji idumu kwa muda mrefu. Pia ukaguzi wa mara kwa mara ufanyike, ili kuweza kubaini mapungufu mapema kabla hayajaleta madhara makubwa na kusababisha gharama kubwa za matengenezo.

c) Kuunda na kuimarisha kamati za watumia maji ili kuongeza uwajibikaji kwa jamii katika kulinda vyanzo vya maji na miundombinu ya maji.

d) Kutoa Elimu kwa watumia maji, ili kuboresha matumizi ya maji, kuboresha na kulinda mazingira ya vyanzo vya maji na kulinda na kutunza miundombinu ya maji iliyokwishajengwa

Mapendekezo kwa OR-TAMISEMI

a) OR-TAMISEMI ihakikishe kuwa wakuu wa Idara na vitengo wanaoteuliwa, hasa kitengo cha TEHAMA pamoja na Idara ya Ujenzi wanakuwa na sifa stahiki ili waweze kusimamia vitengo na Idara zao.

b) Katika kuzingatia masuala ya maadili kazini, watumishi ambao wanathibitika kufanya makosa ya kiutumishi na jinai ni vyema wakachukuliwa hatua stahiki na siyo kuwahamisha kutoka kituo kimoja cha kazi kwenda kituo kingine.

c) Hatua stahiki zichukuliwe ili kuwezesha kurejeshwa kwa fedha zote zilizolipwa kama malipo ya awali kwa mashirika ya umma au idara katika ujenzi wa majengo ya umma ambazo Halmashauri zilishindwa kuzifidia kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuvunjwa mikataba au kulipwa fedha zaidi ya mikataba. Pia, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watumishi wa Halmashauri waliotajwa katika ripoti husika kutokana na kuhusika kwao katika matumizi mabaya ya fedha za serikali.

d) Wahandisi na wataalam ufundi (Technicians) wawepo wa kutosha katika Halmashauri ili kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo ya chini (lower levels) hasa ikizingatiwa kuwa, kwa sasa Serikali imekuwa ikituma fedha nyingi za kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo katika ngazi za vijiji, kata, zahanati, vituo vya afya na mashuleni.

Kwa Menejimenti za Halmashauri

a) **Kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani**
Kitengo cha ukaguzi wa ndani kiimarishwe kwa kuongezewa watumishi na kiwe na vitendea kazi toshelevu. Pia kitengo cha ukaguzi wa ndani kiwezeshwe kupata mafunzo mbalimbali kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya manunuzi ya umma. Vilevile kitengo hiki kiongezewe uwezo wa kukagua mifumo ya manunuzi, uhasibu yaani LGRCIS pamoja na ule wa EPICOR/MUCE, bajeti na LAWSON. Hii itasaidia Halmashauri kuimarisha udhibiti wa ndani kwa kubaini kasoro zinazojitokeza kwa wakati na kuzirekebisha. Aidha, kitengo hiki kiwezeshwe kukagua miradi ya maendeleo

ikiwemo ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika Halmashauri. Na hili litakamilika kama kitengo hiki kitapata bajeti toshelevu pamoja na kuwa na vitendea kazi maalum kwa ajili ya kazi za kitengo hiki.

b) Kuimarisha idara ya ujenzi

Idara ya ujenzi ni idara muhimu sana kwa utendaji wa Halmashauri. Awepo mkuu wa idara ya ujenzi ambaye ni Mhandisi mwenye sifa na vigezo vinavyotakiwa pamoja na mafundi sanifu wenye uwezo ili kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi za chini.

c) Kuimarisha idara ya fedha

Idara ya Fedha ni idara muhimu katika Halmashauri hususani katika kubainisha vyanzo vya mapato na kukusanya mapato hayo ili kuifanya Halmashauri iwe na uwezo wa kutoa huduma kwa wananchi wake. Ili kufanikisha azma hii, ni jambo la muhimu kuwa na watumishi wenye uwezo wa kuweka kumbukumbu sahihi, waaminifu na wenye nidhamu katika matumizi ya fedha. Ili kuhakikisha jambo hili linafanikiwa, Ninapendekeza vitengo vya fedha vifanyiwe mabadiliko ikiwemo kuwahamisha wote walio na muda mrefu katika Halmashauri husika ili kuweza kuleta chachu ya utendaji kazi na kuondoa kasumba ya kufanya kazi kwa mazoea.

d) Kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa awali

Halmashauri zinatakiwa kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa awali kwa kuteua mhasibu mwenye uwezo ili kuzuia malipo yasiyostahili kulipwa au yale yanayotaka kufanyika bila ya kuwa na viambata timilifu. Ukaguzi wa awali uhusike pia katika kupitia malipo yanayofanywa katika miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri. Aidha kitengo cha ukaguzi wa awali kiwezeshwe kupata mafunzo mbalimbali kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya manunuzi ya umma. Hii itasaidia Halmashauri kuimarisha udhibiti wa ndani kwa kubaini kasoro zinazojitokeza kwa wakati na kuzirekebisha.

e) Kuimarisha uzingatiaji wa sheria ya manunuzi ya umma

(i) Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuzingatia sheria ya

manunuzi ya umma na kanuni zake wakati wa uingiaji wa mikataba mbalimbali kwa ajili utekelezaji wa miradi.

(ii) Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuhakikisha kuwa masharti ya mikataba, taratibu, miongozo, kanuni na sheria vinafuatwa wakati wa utekelezaji wa mikataba au wakati wa manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali.

(iii) Manunuzi yote kabla ya kufanyika lazima yapitie kwenye vyombo vinavyohusika ili kuhakikiwa na kuidhinishwa. Vyombo hivyo ni kama kitengo cha usimamizi wa manunuzi (PMU)-na Bodi ya Zabuni.

(iv) Uteuzi wa kamati za tathmini za zabuni zenye uwezo na uadilifu wa kufanya kazi hiyo kwa umakini na kutenda haki kwa walioomba zabuni. Vilevile Bodi za Zabuni zitimize wajibu wake ipasavyo kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani katika manunuzi ya umma.

f) Kuchukuliwa hatua stahiki dhidi ya watumishi, wakandarasi, wataalam washauri na mawakala wa kukusanya mapato waliohusika na udanganyifu ulioisababishia Serikali hasara

Halmashauri zikishirikiana na mamlaka husika ziwachukulie hatua stahiki wakandarasi wajenzi au washauri na kiutawala kwa watumishi wa umma ambao wako chini ya mamlaka hizo pamoja na wale wote watakaobainika wameitia hasara Serikali au walitumia madaraka yao vibaya katika kujinufaisha wao binafsi kama ilivyoonekana katika vipengele mbalimbali vya taarifa husika.

g) Kuwa na utunzaji sahihi wa hati za malipo na viambatanisho vyake na nyaraka za mikataba

(i) Halmashauri ziboreshe mfumo wa utunzaji nyaraka, hii ikiwa ni pamoja na kutenga chumba maalum kwa ajili ya kutunzia nyaraka husika. Wakuu wa Idara waelimishwe kuhakikisha kuwa viambatisho vyote muhimu vinakuwepo kabla ya kuidhinisha malipo; na

(ii) Ateuliwe mtumishi mmoja makini atakayehusika na utunzaji wa nyaraka mbalimbali za fedha zikiwemo hati za malipo. Ahakikishe hati zote za malipo zinakuwa na viambatisho vyake na hati hizo zinatunzwa katika hali ya usalama na kuhakikisha kwamba anaratibu mienendo ya hati zote kuwa zinapochukuliwa zinakuwa zimekamilika. Pia Halmashauri itayarishe chumba maalum kwa ajili ya kuhifadhi hati za malipo na mtumishi huyo awajibishwe kwa upotevu wowote utakaojitokeza.

h) Kuimarisha usimamizi wa Amana zinazotunzwa na Halmashauri
Halmashauri iboreshe mfumo wake wa namna ya utunzaji na mwenendo mzima wa amana zote zinazotunzwa na katika akaunti ya benki ya amana za Halmashauri. Yasiruhusiwe matumizi yoyote ya fedha hizi za amana isipokuwa ni kwa ajili ya matumizi yaliyokusudiwa pekee. Vilevile akaunti hii ya amana haipaswi kuwa akaunti ya matumizi ya kawaida; yaani, fedha nyingine yoyote hairuhusiwi na wala haipaswi kuhamishiwa katika akaunti hii kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

SURA YA 14

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

14.0 Utangulizi

Ripoti hii inaelezea kwa ufupi masuala niliyoyaona wakati wa ukaguzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambayo nimeyawasilisha kwa maofisa masuuli husika. Pia, inaonesha majukumu ya Ofisi yangu katika kuhakikisha kunakuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha, uwazi, uwajibikaji na utawala bora.

Licha ya kujirudia kwa hoja na mapendekezo katika ripoti zangu, ni muhimu kutambua kuwa ingawa Ofisi yangu inatetea uwepo wa utamaduni wa uwajibikaji, kisheria haina mamlaka ya kuwawajibisha wakaguliwa kwa utendaji duni au matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma.

Ingawa hoja za ukaguzi pamoja na mapendekezo yameelezwa kwa kina katika sura zingine za ripoti hii, ni muhimu kwangu kuikumbusha Serikali juu ya hoja muhimu, mapendekezo, na hatua stahiki za kuchukua.

14.1 Hitimisho na Mapendekezo ya Jumla

(i) Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka ya nyuma na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa

Ninapongeza juhudi zinazofanywa na Serikali kupitia kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kufanyia kazi mapendekezo ya ripoti zangu, na hatua zinazochukuliwa ili kukabiliana na mapungufu yaliyojitokeza katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, bado nina shaka kutokana na kujirudia kwa mapendekezo yangu; hali inavyoonesha mapendekezo yangu hayajapewa umuhimu stahiki ili kuleta maboresho. Kuwepo kwa mapendekezo yasiyotekelezwa kwa muda mrefu hadi kufikia miaka kumi, kunaziweka halmashauri katika hatari za uendeshaji na kifedha.

Serikali inatakiwa kuweka mkazo kuhakikisha kuwa halmashauri zinatekeleza na kukamilisha mapendekezo yangu ya miaka iliyopita; na kuweka utaratibu utakaohakikisha mapungufu hayo hayajirudii.

(ii) Utayarishaji na Utekelezaji wa Bajeti

Shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sehemu kubwa zinatekelezwa kwa kutumia fedha zinazotokana na mapato ya ndani, na ruzuku za matumizi ya kawaida na maendeleo. Tathmini ya bajeti kwa miaka mitano mfululizo inaonesha kuwa kuna makusanyo pungufu ya ndani, na kutolewa kwa fedha pungufu za matumizi ya kawaida na maendeleo. Hali hii inapelekea kuchelewesha na wakati mwingine kutotekelezwa kabisa kwa miradi iliyokasimiwa. Pia, nimeona kuwa, halmashauri nyingi zinategemea ruzuku kutoka Serikali kuu kujiendesha.

Ninaishauri Serikali kuhakikisha kwamba bajeti iliyoidhinishwa inatolewa kulingana na mtiririko wa uhitaji wa fedha katika halmashauri. Hatua hii itaziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukamilisha utekelezaji wa miradi kwa wakati na ufanisi wa hali ya juu na katika kutoa huduma kwa jamii katika sekta mbalimbali ikiwemo elimu, afya, miundombinu, kilimo na maji. Hivyo, ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kubaini vyanzo vipya vya mapato na kuweka mikakati ya ukusanyaji mapato kutoka vyanzo hivyo.

(iii) Ukaguzi wa Taarifa za Fedha

Nimeendelea kuona mapungufu katika uandaaji wa taarifa za fedha. Wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha zilizoishia tarehe 30 Juni 2020, niliona mapungufu yafuatayo kwenye taarifa za fedha zilizowasilishwa na halmashauri 185:

- ✓ Toleo la kwanza la taarifa za fedha zilizowasilishwa na halmashauri zote 185 lilikuwa na makosa ya msingi na miamala iliyokosa ulinganifu na isiyoakisi uhalisia wa shughuli zote zilizofanywa na halmashauri hizo. Mapungufu mengi yaliyobainika yaliweza kurekebishwa na mamlaka husika, ingawa baadhi yake hazikufanya marekebisho yaliyopendekezwa. Kwa uzito wa makosa yaliyobainika, imenilazimu kutoa hati zenye shaka/zisizoridhisha kwa halmashauri husika.

- ✓ Uwepo wa madai ya muda mrefu kutokana na huduma zilizotolewa kwa wateja kabla ya kupokea malipo na malipo yaliyofanywa na halmashauri kabla ya kupokea bidhaa au huduma. Madai haya yanapunguza uwezo wa halmashauri kutoa huduma kwa jamii kama zilivyopangwa na baadhi

ya madai haya yanaweza yasilipwe kama hayatafuatiliwa kwa umakini stahiki.

- ✓ Uwepo wa madeni yasiyolipwa na halmashauri kwa watumishi, wazabuni, na wadau wengine kwa zaidi ya mwaka mmoja wa fedha. Madeni yasipolipwa yanaongeza mzigo kwa halmashauri, na hupunguza imani ya wakopeshaji au wadai kuhusiana na utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

- ✓ Uwepo wa madai na mashauri mahakamani na kwenye mabaraza dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na madai ya Mamlaka za Serikali za Mitaa dhidi ya wadau wake. Mashauri ya kimahakama yanatakiwa yafuatiliwe kwa weledi na umakini mkubwa ili kupunguza uwezekano wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupoteza rasilimali nyingi kwa kulipa fidia baada ya hukumu, pia kuongeza uwezekano wa kulipwa fidia pale inapotokea madai ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yamekubaliwa na mahakama.

Ninaishauri OR-TAMISEMI ihakikishe inaboresha mfumo wa mafunzo kazini hasa kwa wahasibu na wakaguzi wa ndani, na kutoa vitendeakazi vinavyokidhi mabadiliko yanayotokea kwenye nyanja mbalimbali ili kuwawezesha kuandaa kwa wakati taarifa za fedha zenye ubora na zinazokidhi viwango vya kimataifa vya uhasibu.

Pia, ninashauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuata sheria, kanuni, na miongozo stahiki katika kufanya maamuzi yanayogusa maslahi ya jamii ili kupunguza migongano inayopelekea uwepo wa mashauri ya kisheria na kesi mahakamani.

(iv) Tathmini Juu ya Udhibiti wa Ndani, Usimamizi wa Vihatarishi na Mifumo ya Utawala Katika Halmashauri

Nilibaini mapungufu ya kiutendaji katika vitengo vya ukaguzi wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yaliyochangiwa na uhaba wa wafanyakazi, ukosefu wa vitendeakazi muhimu, ukaguzi bila kuzingatia maeneo hatarishi, bajeti duni, baadhi ya kaguzi kutotekelezwa, na ukosefu wa mafunzo ya mifumo na viwango vya uhasibu.

Nilibaini pia udhaifu katika udhibiti wa jumla kwenye mazingira ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kwani hakukuwa na sera ya teknolojia

ya habari na mawasiliano, kompyuta hazikuwa na programu za kukinga virusi vya kompyuta, uhaba wa wafanyakazi, uhaba wa vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano, kutokuwepo kwa mpango wa mafunzo, kutowepo kwa kamati za usimamizi, bajeti isiyokidhi, na kutokuwepo kwa mpango wa kudhibiti majanga na matukio ya dharura. Pia, nilibaini udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani, kwani tathmini za udhibiti wa ndani hazifanyiki kikamilifu na hivyo kupelekea uwepo wa miamala ya kughushi katika halmashauri.

Hakukuwa na sera ya usimamizi wa vihatarishi; hakukuwa na mpango wa usimamizi wa vihatarishi; kutokuwepo kwa rejesta ya vihatarishi; tathmini rasmi ya viatarishi haikufanyika katika baadhi ya halmashauri; na kutokuwepo kwa mchakato wa kutambua na kushughulikia vihatarishi vya kughushi na udanganyifu. Nilibaini pia udhaifu katika utendaji wa kamati za ukaguzi kama vile kutotayarisha ripoti za mwaka; kamati kutokagua taarifa za fedha za halmashauri na mipango ya ukaguzi ya mwaka; kushindwa kufanya tathmini ya vihatarishi na mifumo ya udhibiti wa ndani wa halmashauri; kushindwa kukutana mara kwa mara; na wajumbe wa kamati za ukaguzi kutohudhuria mafunzo ya wajibu wa kamati na kujengewa uwezo katika utendaji.

Pia, kuna mapungufu makubwa katika uendeshaji wa mifumo ya uhasibu kwani mifumo mingi inayotumiwa kama EPICOR, FFARS, LGRCIS, GOT-HOMIS si jumuishi. LGRCIS hairuhusu kuweka muda wa kikomo kwa miamala; na watumiaji wengi wanaohamishiwa kwenye halmashauri zingine wanaweza kuingia kwenye mifumo; mifumo ya kihasibu inafanya kazi kwa taslimu na kutotambua miamala ambayo si taslimu; na mapungufu yaliyobainika katika matumizi ya mifumo ya FFARS na GOT-HOMIS katika ngazi za chini kwa sababu ya uhaba wa vifaa, ukosefu wa ujuzi wa kutumia mifumo, na kutopata msaada wa kitaalamu kutoka halmashauri.

Ninapendekeza mapungufu yaliyotajwa hapo juu yafanyiwe kazi ipasavyo na kwa wakati ili kuhakikisha kuwa taarifa za fedha zilizotolewa na halmashauri mwishoni mwa mwaka zinakuwa sahihi na bila kuwa na makosa yanayosababishwa na udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani kama ilivyobainishwa hapo juu.

(v) Tathmini ya Mishahara na Usimamizi wa Rasilimali-Watu

Rasilimali-watu ni jambo linaloamua ufanisi na utoaji bora wa huduma katika halmashauri. Licha ya jukumu lake muhimu, nimeona kuwa kuna madai makubwa ya watumishi; kutokurudishwa kwa mishahara isiyolipwa; baadhi ya wafanyakazi wanaopokea chini ya theluthi moja ya mishahara

yao; ucheleweshaji wa kupanda madaraja wafanyakazi wanaostahili; idadi ya wafanyakazi katika halmashauri nyingi imeendelea kuwa pungufu; uwepo wa watumishi wanaokaimu ukuu wa idara/vitengo kwa zaidi ya miezi sita; kutosahihisha taarifa za wafanyakazi katika Mfumo wa LAWSON; na kutotumwa kwa makato ya wafanyakazi katika taasisi husika. Mapungufu niliyoyaona yanapunguza utendaji wa watumishi, hali inayoweza kusababisha halmashauri husika kushindwa kutoa huduma bora.

Ili kutatua masuala haya, OR-TAMISEMI, sekretariati za mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kufanya kazi kwa pamoja ili kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma katika halmashauri. Pia, Serikali iangalie namna bora ya kushughulikia maslahi ya watumishi, ajira, mafunzo, upimaji wa utendaji kazi, na upandishaji wa madaraja ili kufikia lengo la kutoa huduma bora kwa jamii.

(vi) Tathmini ya Miradi ya Maendeleo na Miradi Mingine

Ukaguzi wangu kuhusiana na miradi ya maendeleo ulionesha fedha zisizotumika ambazo zilipangwa kutekeleza miradi mbalimbali; miradi ambayo haijakamilika ikiwa ni pamoja na miradi iliyotelekezwa bila kukamilika kwa kipindi kirefu kuanzia mwaka 2000 hadi 2018 kutokana na kutotolewa kwa fedha za kutosha pamoja na usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa halmashauri ambazo pia husababisha kasoro juu ya utekelezaji wa miradi. Kuna miradi ambayo imekamilika lakini bado haina manufaa kwa Jamii, ambapo inaweza kuharibika kama haitatumika.

Mapitio ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu yalionesha baadhi ya halmashauri hazikuchangia kama inavyotakiwa na sheria. Vilevile, Mfuko una madeni makubwa ya marejesho ya mikopo ambayo hayajakusanywa kutoka kwa vikundi vya wanufaika. Hivyo, halmashauri zinapaswa kufuatilia kwa karibu makusanyo ya madeni hayo.

Tathmini ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulionesha madai mengi yaliyokataliwa na Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa kutokana na kutozingatia taratibu.

Vilevile, nilibaini kuwa fidia ya ada, ruzuku ya uendeshaji wa shule na ya chakula shuleni zilitolewa kwa upungufu hivyo kuathiri utekelezaji wa Sera ya Elimu bila Malipo.

Ninatoa wito kwa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha miradi ambayo haijakamilika, hususani miradi iliyotelekezwa kwa kipindi kirefu inakamilika ndani ya muda mfupi kwa kutenga bajeti na kutoa fedha za kutosha; na kufuatilia na kusimamia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi ili kuepuka kasoro katika miradi. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuzingatia taratibu za kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi ambazo ni pamoja na kufungua kesi ya madai dhidi ya vikundi vilivyoshindwa kurejesha mikopo na kuhakikisha michango ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu inatolewa kikamilifu.

(vii) Usimamizi wa Manunuzi

Katika ukaguzi wa mwaka huu, niliendelea kubaini kuwa halmashauri nyingi hazikutumia mifumo iliyotengenezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma na hivyo kuikwamisha Mamlaka hiyo kufanya ufuatiliaji wa shughuli za manunuzi. Pia, halmashauri nyingi hazikuzingatia matakwa ya sheria juu ya uwasilishaji wa taarifa za manunuzi hivyo kukwamisha utendaji wa Mamlaka hiyo katika kutoa huduma zilizokusudiwa.

Vilevile, nilibaini utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu za manunuzi na hivyo kuathiri mawanda yangu ya ukaguzi, upungufu wa wafanyakazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya usimamizi hadi utekelezaji ambao umechangia utendaji duni pamoja na ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi na kusababisha ongezeko la gharama na muda wa utekelezaji wa miradi.

Aidha, nimebainisha katika ripoti yangu, changamoto za muda mrefu kama vile ukosefu wa uadilifu, vitendo vya rushwa na ulaghai miongoni mwa maofisa wa umma na wazabuni mambo ambayo yameathiri kupatikana kwa thamani ya pesa katika manunuzi.

Kwa ujumla, dosari zilezile katika manunuzi na mapendekezo yaleyale yamekuwa yakitolewa bila hatua za kurekebisha dosari hizo kuchukuliwa na halmashauri husika. Ninatoa wito kwa serikali, kwamba endapo itathibitishwa kuwa maofisa masuuli wamehusika katika manunuzi yasiyo na tija, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao kwa mujibu wa Kanuni ya 67 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 kwa madhumuni ya kuzuia au kupunguza matumizi yasiyokuwa na tija ya fedha za umma

pamoja na kuepusha hasara au uzembe wakati wa mchakato wa manunuzi.

(viii) Usimamizi wa Mikataba

Ukaguzi wa kina juu ya usimamizi wa mikataba ulifanywa katika halmashauri 25 katika mikoa 15. Lengo kuu lilikuwa kutathmini iwapo kulikuwa na mifumo madhubuti katika kusimamia miradi ya maji ndani ya halmashauri husika ili kubaini kama kulikuwepo na matumizi bora ya rasilimali zilizotengwa na kama malengo yaliyokusudiwa yalifikiwa.

Miongoni mwa mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi huu ni kutoshirikishwa kwa jamii katika uchaguzi wa miradi iliyotekelezwa; kuanzisha miradi bila ya kufanya upembuzi yakinifu au mikataba kutohakikiwa na mwanasheria; kutekeleza miradi kabla ya kufanya tathmini ya athari za mazingira; na kuanzisha miradi kabla ya kupata vibali na michoro ya ujenzi.

Pia, nilibaini mikataba ilitekelezwa bila kuwa na wakandarasi washauri na bila kubainisha vigezo vinavyohitajika; mapungufu katika usanifu wa miradi kulikosababisha gharama za ziada; utoaji wa kandarasi kwa wazabuni wasio na sifa; na ucheleweshaji bila sababu za msingi katika kuanza kwa utekelezaji wa miradi.

Ninatoa wito kwa serikali kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za manunuzi wa umma na kuchukua hatua stahiki dhidi ya halmashauri zilizobainika kuwa na dosari zilizosabishwa na kukiuka taratibu za usimamizi wa mikataba.

(ix) Usimamizi wa Matumizi

Ukaguzi wangu mwaka huu umebaini mapungufu mbalimbali ikiwa pamoja na kutowasilishwa kwa hati za malipo; hati za malipo kutokuwa na nyaraka stahiki kama risiti za EFD, matumizi yasiyo ya lazima na yasiyo na tija; usimamizi hafifu wa masurufu; pamoja na uandaaji na uidhinishaji wa hati za malipo usiofuata taraibu.

Pia, kumekuwa na kutokukata na kuwasilisha kodi ya zuio kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania; mapungufu kwenye akaunti za amana; matumizi yaliyofanyika katika vifungu visivyo sahihi bila kupata idhini; matumizi ya

mafuta ambayo hayajathibitishwa; na fedha za matazamio kutopelekwa RUWASA na TARURA.

Ili kuzuia mapungufu yaliyobainika yasijirudie wakati mwingine, ninatoa ushauri kwa menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinazingatia vifungu vya bajeti; zinaongeza udhibiti wa bajeti; zinaimarisha udhibiti wa uandaaji, upitishaji wa malipo, na ukaguzi wa awali; kuhakikisha zinatekeleza majukumu kwa wakati hasa uwasilishaji wa michango ya watumishi pamoja na madai mengine; kuweka utaratibu utakaohakikisha hati za malipo zinaambatishwa na nyaraka zinazojitosheleza; usimamizi na ufuatiliaji kwa ukaribu wa masurufu; na namna nzuri ya kutunza akaunti ya amana.

(x) Usimamizi wa Mapato

Tathmini niliyoifanya juu ya sera za ukusanyaji mapato, mikakati na mifumo ya udhibiti wa ndani katika halmashauri mbalimbali iligundua mapungufu kadhaa kama usimamizi dhaifu wa vifaa vya POS; mapato yasiyokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali; ukosefu wa sheria ndogondogo zilizoidhinishwa au kuhuishwa; kutowekwa kwa mifumo ya usimamizi wa afya katika zahanati, vituo vya afya, na hospitali; pesa zilizokusanywa lakini hazikupelekwa benki; makusanyo ambayo hayajafanyiwa usuluhishi; mapato yaliyokusanywa nje ya LGRCIS; kutofautiana baina ya taarifa moja na nyingine za mapato yaliyokusanywa; na kuwapo kwa vitabu vya risiti ambavyo havikutumiwa.

Mapungufu yaliyotajwa yanaweza kuondolewa kwa kutungwa au kuhuishwa sheria ndogondogo za halmashauri; kuongeza juhudi za kukusanya mapato yote yasiyokusanywa; kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kufunga mifumo ya ukusanyaji mapato katika vituo vya afya; kuweka adhabu ya kutowasilisha fedha inayokusanywa kwa wakati; mapato yote kukusanywa kwa kutumia LGRCIS; vitabu vya risiti vya karatasi vinapaswa kuondolewa; usuluhishi wa mapato yasiyowasilishwa ufanyike kwa wakati; na mfumo wa udhibiti wa ndani unapaswa kuboreshwa ili kuongeza ufanisi katika michakato ya ukusanyaji wa mapato.

(xi) Usimamizi wa Mali za Halmashauri

Nilibaini mapungufu kadhaa katika usimamizi wa mali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama kutokuwepo kwa hati za miliki za ardhi na kadi za

usajili kwa mali zinazomilikiwa na halmashauri; kuwepo kwa muda mrefu mali zisizoweza kufanyiwa matengenezo au kutelekezwa; magari na pikipiki ambazo hazijakatiwa bima; uwepo wa dawa zilizokwisha muda wake bila kuharibiwa; mapungufu kwenye rejesta za mali zisizohamishika; na kutokuwepo kwa kumbukumbu za matengenezo, ukarabati na ubadilishaji wa mali. Niligundua pia kulikuwa na mali zilizonunuliwa lakini hazikusajiliwa au kuingizwa kwenye rejesta na mali zilizonunuliwa lakini hazitumiki.

Ninazishauri menejimenti za halmashauri kupanga bajeti kwa ajili ya upimaji wa ardhi inayomilikiwa na halmashauri; ukarabati au uuzaji wa mali zilizokaa kwa muda mrefu bila kutumika; kuwasiliana na taasisi zingine za serikali kuharakisha mchakato wa kuuzwa kwa mali ambazo haziwezi kukarabatiwa na kuharibu dawa zilizokwisha muda wake; kutunza rejesta ya matengenezo, ukarabati na ubadilishaji wa mali; kuhakikisha kuwa mali zilizonunuliwa zinasajiliwa papo hapo; na mali zote zinunuliwe kwa mujibu wa bajeti na mipango ya manunuzi na zinatumika mara tu baada ya kununuliwa.

14.2 Mapendekezo kwa Serikali chini ya Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008

Kwa kuzingatia Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya 2008 kinachosema "Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kwa madhumuni ya kuzuia au kupunguza matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma; kuongeza ukusanyaji wa mapato ya umma; kuzuia hasara kwa uzembe, wizi, udanganyifu, na ufisadi unaohusiana na pesa na rasilimali za umma; na kutoa mapendekezo na kuwasilisha mapendekezo hayo kwa waziri mwenye dhamana na endapo waziri ataona yana umuhimu katika usimamizi bora wa fedha za umma atayajumuisha katika marekebisho ya kanuni, maagizo au miongozo inayotolewa kwa mujibu wa sheria husika", ninapenda kushauri yafuatayo:

14.2.1 Miradi Iliyotelekezwa kwa Muda Mrefu Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miradi mingine hugharamiwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani pamoja na michango ya jamii. Nilikagua ripoti za utekelezaji wa miradi pamoja na kutembelea miradi mbalimbali na kubaini kuwa miradi mingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ilikuwa imetelekezwa kwa muda mrefu huku kiasi kikubwa cha fedha kikiwa kimeshatumika, na hakukuwa na jitihadi za makusudi za kutenga fedha ili

kuikamilisha. Hali hii ilipelekea thamani ya fedha iliyotumika kutoonekana na gharama za kukamilisha miradi hiyo zingeweza kuongezeka kwa kuwa bei za vifaa zingeweza kupanda kutokana na mfumuko wa bei.

Ninaishauri serikali kufikiria upya uamuzi wa kuanzisha miradi mipya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zina miradi viporo, na kujikita zaidi katika kutafuta fedha za kukamilisha miradi iliyotelekezwa kwa muda mrefu. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuanzisha miradi ambayo ipo ndani ya uwezo wao wa kifedha, na pale inapowezekana kutekeleza miradi kwa awamu kwa kuhakikisha kila awamu inakamilika na kuanza kutumika kama sehemu ya utekelezaji wa miradi kwa ujumla.

14.2.2 Miradi Iliyoanzishwa Bila Kuainisha Mahitaji ya Watumiaji Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Tathmini yangu juu ya utekelezaji wa miradi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ilibaini kuwa baadhi ya miradi ilianzishwa kutokana na ushawishi wa kisiasa na hii ilipelekea miradi mingi kutokamilika au kutotumika mara baada ya kukamilika. Miradi hiyo ilianzishwa bila kufanya upembuzi yakinifu na bila kuwashirikisha wadau au wanufaika wake. Kutowahusisha wadau wote muhimu katika utekelezaji wa miradi hiyo hupelekea miradi husika kuhujumiwa na baadhi ya wananchi wasio waaminifu au watumiaji kukataa kutumia miradi hiyo kutokana na kukosa ubora au miradi kujengwa kwenye maeneo yasiyowavutia watumiaji.

Ninazishauri menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya upembuzi yakinifu wa kina kabla ya kuanza kutekeleza miradi hiyo na kuwashirikisha wadau wote muhimu katika hatua ya upembuzi na wakati wa kutekeleza miradi hiyo. Halikadhalika, miradi iliyoanzishwa inapaswa kuzingatia mahitaji halisi ya jamii husika na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi husika; hii itaepusha kuwa na miradi mingi isiyokamilika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

14.2.3 Utendaji Duni wa Masoko ya Kisasa Katika Halmashauri

Ninaona juhudi kubwa za Serikali katika kujenga masoko ya kisasa kwenye halmashauri mbalimbali. Hata hivyo, baadhi ya masoko hayafanyi vizuri kwa kuwa hakuna wafanyabiashara wa kukodi vizimba. Suala hili limesababishwa na utoaji wa vitambulisho vya wamachinga, pia masoko mengi ya kisasa yapo mbali na vituo vya mabasi hivyo kupelekea kukosa wateja.

Ninaishauri Serikali pamoja na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kujenga masoko ya kisasa jirani na sehemu ambazo watu hupita ili kuongeza ufanisi wa miradi hiyo.

14.2.4 Miradi ya Maji Isiyo na Tija na Iliyosimama

Kifungu cha 43 cha Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 inatoa mamlaka kwa RUWASA juu ya usimamizi na uendelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Licha ya uwezo wa RUWASA kutekeleza majukumu yake ya kusambaza maji safi katika jamii, kuna baadhi ya miradi haitoi maji, miradi kuchukua muda mrefu bila kukamilika, na miradi mingine kukamilika lakini haina manufaa kwa jamii husika. Miradi isiyo na tija inawanyima wananchi fursa ya kupata maji safi.

Ninaishauri Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuitambua na kuchukua hatua stahiki dhidi ya miradi ya maji isiyo na tija ili kuhakikisha miradi husika inakuwa na manufaa kwa jamii kama ilivyokusudiwa.

14.2.5 Matumizi ya Taasisi au Mashirika ya Umma au Idara za Serikali Katika Ujenzi Wa Miradi ya Umma kwa Kutumia Njia ya "Force Account"

Kanuni ya 167(2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa mwaka 2016) inaeleza kuwa 'force account' ni mchakato ambao kazi zinafanywa na taasisi, idara au mashirika ya umma kwa kutumia watumishi na vifaa vyake au kwa kushirikiana na taasisi yoyote ya umma au ya kibinafsi".

Aya ya 9 ya Waraka Na. CAB.39/156/01/111 wa tarehe 10 Mei 2019 uliotolewa na OR-TAMISEMI unazitaja taasisi za umma au idara za Serikali ambazo taasisi nunuzi inaweza kushirikiana nazo katika utekelezaji wa miradi kwa kutumia utaratibu wa force account. Taasisi hizo ni pamoja na SUMA JKT, vikosi vya ujenzi chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Shirika la Nyumba la Taifa, Wakala wa Majengo Tanzania, Jeshi la Magereza, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Shirikala la Mzinga chini ya Jeshi la Wananchi Tanzania, Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA - kwa kazi za ufundi wa umeme na elekitroniki), na Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Majengo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Nyaraka za zabuni zinazotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma zinatoa nafasi kwa wakandarasi wa taasisi za umma kupata malipo

ya awali kwa masharti ya kuweka dhamana ya malipo ya awali na kutakiwa kuthibitisha uhitaji wa matumizi hayo na kwamba ni lazima matumizi husika yawe na lengo la kugharamia manunuzi ya mitambo, mashine, vifaa, gharama za kuleta vifaa vinavyohitajika katika utekelezaji wa mikataba, na malipo kwa wafanyikazi wakati wa mwezi wa kwanza.

Wakati wa kufanya ukaguzi maalumu kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu manunuzi kupitia utaratibu wa "force account" tathmini ilifanyika ili kubaini iwapo halmashauri zinafuata matakwa ya sheria ya manunuzi ya umma pamoja na kanuni zake, miongozo inayotolewa, pamoja na matakwa ya mikataba.

Katika kufanya tathmini hiyo, nilibaini kuwa baadhi ya taasisi za umma na idara mbalimbali za Serikali zilishirikishwa na kupata kazi za ujenzi katika halmashauri mbalimbali nchini hivyo kuwa na mikataba halali ya ufanyaji kazi. Wakati wa tathmini niligundua kuwa malipo ya awali yaliyofanyika yalikuwa na mapungufu mbalimbali.

Niligundua kuwa kulikuwa na matukio ya halmashauri kupata hasara mara zote yalipotokea matatizo yaliyopelekea kuvunjwa kwa mikataba kwa sababu taasisi za umma hazikurejesha fedha zilizolipwa kama malipo ya awali wala hakukuwa na namna halmashauri husika zingeweza kufidiwa malipo hayo kutoka kwa wazabuni hao.

Vilevile, nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ilipata hasara iliyotokana na kumlipa mzabuni fedha za malipo ya awali nyingi kuliko gharama nzima ya mkataba. Fedha hizo za ziada zilizolipwa hazikuweza kurejeshwa kwa halmashauri. Hili lilitokea kwa sababu malipo ya awali yalilipwa kabla gharama za makisio za utekelezaji wa mradi hazijaandaliwa; kabla ya mkataba kuadaliwa na kusainiwa na pande zote mbili; na bila ya dhamana ya malipo ya awali na ya utendaji kazi.

Zaidi ya hayo, nilibaini uwepo wa taasisi iliyopewa ujenzi wa miradi mitatu mikubwa ndani ya mwaka mmoja wa fedha. Nilibaini kuwa taasisi hiyo haijishughulishi na masuala ya ujenzi, hivyo haikuwa na utaalamu na masuala ya ujenzi. Vilevile, ilibainika kwamba halmashauri ilikuwa ikikodisha mitambo, ikinunua kokoto, mchanga, matofali na vifaa vingine kwa taasisi hiyohiyo bila ya kuwa na ushindani wowote. Kwa mantiki hiyo, nina mtazamo kuwa miradi hiyo ilikuwa ikitekelezwa kwa kutumia mkandarasi huru kwa kivuli cha "force account".

Ninashauri Ofisi ya Rais-TAMISEMI ikishirikiana na ofisi za makatibu tawala wa mikoa nchini ihakikishe kuwa kunakuwepo utaratibu mzuri wa kutumia fedha zilizotengwa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hasa ujenzi inayohitaji halmashauri kutumia vyombo au mashirika ya umma au idara za serikali ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na thamani ya fedha zinazotolewa kwa wajenzi hao.

14.2.6 Makadirio Yasiyo na Uhalisia ya Muda wa Matumizi ya Mali za Kudumu

Aya ya 72 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma Toleo la 2019 imeaininsha mambo ya kuzingatiwa kwenye kukadiria muda tarajiwa wa matumizi ya mali za kudumu ambayo yanajumuisha (a) matumizi yanayotarajiwa ya mali ya kudumu, (b) uchakavu unaotarajiwa kutokea kwenye mali ya kudumu, (c) masuala ya kiufundi au kupitwa na muda, na (d) zuio la kisheria au zuio linalofanana na hilo kwenye matumizi ya mali ya kudumu kama vile tarehe ya kwisha kwa mali iliyokodishwa.

Aidha, Aya ya 21 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa Mwaka 2019 uliotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali umetoa maelekezo kuwa, ili kupata muda tarajiwa wa matumizi wa mali ya kudumu, mambo yanayopaswa kuzingatiwa ni nyenzo zilizotumika kutengeneza mali ya kudumu, matumizi, matunzo, na matengenezo ya mali za kudumu.

Hata hivyo, mapitio ya Kiambatisho cha 3 kilichopo kwenye Mwongozo huo yalibainisha kuwa, miaka tarajiwa ya matumizi iliyoainishwa na inayotumika kwa mali za kudumu za Serikali haina uhalisia kutokana na yafuatayo:

- ✓ Idadi ya miaka iliyokadiriwa kwa majengo ya shule ni 75 wakati ile ya majengo ya ofisi na makazi ni miaka 50. Hii inapingana na uhalisia kwa sababu matumizi tarajiwa ya majengo ya shule ni zaidi ya majengo ya ofisi kutokana na idadi ya watumiaji na matarajio ya uchakavu; hivyo inatarajiwa kuwa, majengo ya shule huwahi kuchoka kuliko majengo mengine.

- ✓ Miaka tarajiwa ya matumizi ya majengo iliyowekwa haikuzingatia namna majengo hayo yalivyojengwa kwa kuzingatia nyenzo zilizotumika. Kwa mfano, baadhi ya majengo ya shule yamejengwa kwa kutumia matofali ya udongo huku mengine yakijengwa kwa kutumia matofali ya saruji. Majengo yaliyojengwa kwa kutumia matofali ya udongo hayawezi kuwa na ubora sawa na yale yaliyojengwa kwa matofali ya saruji. Pia, kuna majengo ambayo yamejengwa kwa

kutumia wakandarasi wakati mengine kupitia nguvu ya jamii, hivyo hayawezi kuwa na ubora ulio sawa na muda tarajiwa wa matumizi ulipaswa kutofautiana.

- ✓ Miaka tarajiwa ya matumizi ya magari na pikipiki haujazingatia ubora wa barabara zinazotumika. Ubora wa barabara katika halmashauri za majiji, manispaa, na miji haupo sawa na wa halmashauri nyingi za wilaya. Hivyo, uchakavu wa magari na pikipiki katika majiji, manispaa, au miji hauwezi kuwa sawa na ule wa magari na pikipiki zilizopo kwenye halmashauri za wilaya na hivyo muda tarajiwa wa matumizi na kiwango cha uchakavu cha magari na pikipiki kwa yaliyopo mijini na vijijini/wilayani unatarajiwa kuwa tofuati.

Ninapendekeza Mlipaji Mkuu waa Serikali kufanya utafiti na kuja na makadirio sahihi ya muda tarajiwa wa matumizi ya mali za kudumu kwa kufuata matakwa ya Aya ya 72 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma na kuhuisha Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa Mwaka 2019.

14.2.7 Kutofanyika kwa Mapitio ya Muda Tarajiwa wa Matumizi ya Mali za Kudumu Kutokana na Kutokuwepo kwa Mwongozo Sahihi

Aya ya 67 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma inataka thamani ya mabaki na makadirio ya muda wa matumizi ya mali za kudumu kufanyiwa mapitio angalau kila tarehe ya kufunga mwaka wa fedha na, ikiwa makadirio mapya yanatofautiana na makadirio ya awali, mabadiliko ya makadirio ya muda wa matumizi ya mali za kudumu yataripotiwa kama mabadiliko ya makadirio ya kihasibu ya muda wa matumizi ya mali za kudumu kama inavyoelezewa kwenye Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma.

Kinyume na sharti hili, nilibaini kuwa, Serikali kupitia kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali imetoa viwango vya uchakavu kwenye sera yake ya uhasibu na kupitia Kiambatisho cha 3 cha Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Serikali wa Mwaka 2019 lakini hakuna maelekezo yaliyo wazi juu ya namna ambavyo viwango vinavyokadiriwa vya uchakavu vitafanyiwa mapitio katika kila mwisho wa mwaka wa fedha ili kuhakikisha halmashauri zinazingatia matakwa ya Aya ya 17 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma.

Hakuna mwongozo unaoonesha nani anapaswa kufanya mapitio (muundo wa timu) na mamlaka ya kuidhinisha mabadiliko ya kiwango cha uchakavu baada ya mapitio. Halmashauri nyingi hazijazingatia matakwa ya Aya ya 17 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma; matokeo yake, halmashauri zina mali nyingi za kudumu ambazo hazina thamani kwenye vitabu vya kihasibu kutokana na kupunguzwa thamani yote lakini bado zinatumika.

Vilevile, nimebaini kuwa, kupitia waraka Na. EG.3/102/02/03 wa tarehe 28 Mei 2019 kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, maofisa masuuli waliagizwa kubadili muda tarajiwa wa matumizi ya mali zote za kudumu ambazo zilikuwa hazina thamani kwenye vitabu vya kihasibu kutokana na kupunguzwa kwa thamani, lakini hawakuongozwa ipasavyo jinsi ya kufanya mabadiliko hayo. Matokeo yake, halmashauri nyingi hazikuzingatia matakwa ya Mwongozo huo na zimeendelea kuonesha kwenye hesabu za mwisho orodha ya mali ambazo hazina thamani kwenye vitabu vya kihasibu lakini bado zinatumika.

Ninapendekeza Mhasibu Mkuu wa Serikali kutoa mwongozo wa jinsi ya kufanya mapitio ya kila mwaka ya makadirio ya muda wa matumizi wa mali za kudumu.

14.2.8 Kutokuwepo kwa Mawasiliano ya Moja kwa Moja Baina ya Mifumo Inayotumika Kwenye Halmashauri na Hesabu za Mwisho Kutengenezwa Nje ya Mfumo wa Uhasibu

Kuwepo kwa mifumo zaidi ya mmoja ya uhasibu katika halmashauri kunaleta changamoto juu ya usahihi wa data zinazotolewa taarifa kwenye hesabu za mwisho. Halmashauri zinatumia Mfumo wa EPICOR kwa malipo, Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS) kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato ya halmashauri, Mfumo wa Upokeaji na Ulipaji kwa Taasisi za Ngazi ya Chini (FFARS), na Mfumo wa Usimamizi na Ukusanyaji Mapato katika Zahanati, Vituo vya Afya, na Hospitali za Serikali.

Hata hivyo, mifumo yote hii haiwasiliani moja kwa moja yenyewe kwa yenyewe na hivyo halmashauri haziwezi kuandaa hesabu zake za jumla za mwisho zinazojumuisha taarifa na data kutoka mifumo yote hiyo. Hivyo, taarifa za kifedha zinachukuliwa kutoka kwenye kila mfumo ama kwa kutumia kibebeo (flash) au kwa njia ya kuingilia kati mfumo kupitia dirisha maalumu (import window) kwa ajili ya kuandaa taarifa ya jumla nje ya

mfumo. Hii inahatarisha taarifa jumuishi zilizoandaliwa kuwa na makosa, na kupoteza usiri wa taarifa hizo na hivyo taarifa za jumla zilizoandaliwa kutoweza kuaminiwa moja kwa moja kuwa ni sahihi. Ukaguzi zaidi ulibaini kuwa serikali za vijiji na ofisi za kata hazichakati malipo yao kupitia mfumo wa uhasibu ikiwepo uandaaji wa hati za malipo jambo ambalo linafanya iwe vigumu zaidi kuingiza malipo yake kwenye hesabu jumuishi za mwisho za halmashauri

Ninapendekeza OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuunganisha mifumo yote ya uhasibu inayotumika katika halmashauri na kuhakikisha kuwa mifumo yote inawasiliana moja kwa moja na mfumo mkuu yaani EPICOR ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa zinazoaminika kwenye mfumo mmoja mkuu wa uhasibu kwa ajili ya uandaaji wa taarifa jumuishi za fedha. Aidha, hesabu za mwisho za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuzalishwa kutoka kwenye mfumo na kusiwepo na marekebisho ya hesabu hizo nje ya mfumo wa EPICOR. Pia, marekebisho yote yasiyo ya fedha taslimu yanapaswa kufanywa ndani ya mfumo wa uhasibu.

14.2.9 Kutokuwepo kwa Nyaraka za Mikataba Iliyosanifiwa kwa Ajili ya Mafundi Katika Utaratibu wa "Force Account"

Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 inaelezea kuwa, moja ya majukumu la Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ni kuandaa, kuhuisha na kutoa nyaraka maalumu za hati za zabuni, fomu za kiutaratibu, na nyaraka zingine kwa taasisi zinazonunua huduma na vifaa mbalimbali.

Katika kipindi cha ukaguzi, nilibaini Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na nyaraka zisizofanana kwa ajili ya mikataba ya mafundi wa mitaani. Kanuni ya 243 (2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) inaeleza kuwa taasisi inayofanya manunuzi inatakiwa kufanya malipo baada ya kujiridhisha kwa vipimo na ubora wa kazi, katika hatua mbalimbali kama ilivyokubalika katika mkataba. Aidha, katika kila asilimia ya malipo, fedha ya matazamio ikatwe kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba. Hata hivyo, baadhi ya mikataba katika Mamlaka za Serikali za Mitaa haikujumuisha kipengele cha kuzuia fedha ya matazamio.

Pia, Kanuni ya 29 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) inaelekeza kuwa, taasisi inayofanya manunuzi inatakiwa kupewa dhamana ya kazi kutoka kwa mzabuni aliyeshinda zabuni ili kuhakikisha ubora wa kazi. Nilibaini kuwa matakwa haya ya kanuni hayakujumuishwa katika mikataba ya mafundi wa mtaani na dhamana ya kazi pia haikudaiwa kutoka kwa wazabuni walioshinda.

Ikumbukwe kwamba, ikiwa fedha za matazamio hazizuiliwi na dhamana za utendaji hazidaiwi, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakuwa katika hatari ya kutumia gharama zaidi kwa miradi inayoendelea ikiwa fundi atashindwa kutekeleza kazi zake vizuri.

Pia, fundi anaweza akakosa uwajibikaji unaotakiwa katika mradi husika na halmashauri ikakosa haki ya kufidiwa kwa kurekebisha makosa ya mradi baada ya mradi kukamilika na kuwa ndani ya muda wa matazamio.

Kutokana na changamoto hizi za tofauti ya mikataba ya mafundi kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa moja na nyingine pamoja na athari zake, ninatoa wito kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma kuzingatia na kuandaa nyaraka za mikataba zilizosanifiwa pamoja na nyaraka zingine katika taasisi zote Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakazotumia mafunzi wa mtaani katika utekelezaji wa miradi.

14.2.10 Matumizi ya Risiti za Kielekitroniki (EFD)

Kanuni ya 55(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi za Mwaka 2016 zinataka mtu ambaye amepokea bidhaa au huduma kudai na kuhifadhi risiti na kuiwasilisha endapo ataombwa kufanya hivyo na kamishna mkuu au ofisa yeyote aliyeidhinishwa na kamishna mkuu wa Mamlaka ya Kodi Tanzania.

Katika ukaguzi wangu wa manunuzi ya bidhaa na huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, nilibaini idadi kubwa ya stakabadhi za EFD zilizoambatishwa katika manunuzi ya halmashauri mbalimbali hazikuwa madhubuti na hazidumu kwani kadiri muda unavyozidi kupita zilikuwa zikififia kufikia hadi hatua ya maelezo ya risiti hizo kutosomeka kwa urahisi.

Agizo la 104 (2) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka utunzaji sahihi wa nyaraka kwa muda usiopungua miaka mitano. Hivyo, baadhi ya halmashauri zimekuwa zikitoa nakala mara baada ya kupokea risiti hizo ili kuepuka kupoteza taarifa muhimu katika risiti baada ya muda mfupi. Hata hivyo, utaratibu huo unaleta changamoto hasa wakati wa kazi ya ukaguzi nakala za nyaraka kila mwaka.

Ninapendekeza Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kutazama upya risiti za sasa kwa kubadilisha karatasi zinazotumika kuchapisha risiti za EFD na badala yake kuwe na risiti zingine ambazo zitadumu kwa muda mrefu ili kuendana na mahitaji ya sheria ya muda wa utunzaji wa nyaraka na kurahisisha kazi ya ukaguzi.

14.2.11 Ubadhirifu wa Makusanyo ya POS Ambayo Kawaida Huchukuliwa Kama Mapato Ambayo Hayajawasilishwa na Hatua Zinazopendekezwa Kurekebisha Hali Hiyo

Moduli za mashine za kukusanyia mapato (POS) katika mfumo wa LGRCIS hupokea miamala ya kutoka mashine za POS zinazofanya kazi katika vituo mbalimbali kwa wakati halisi. Mfumo hujumlisha viwango vya miamala binafsi kulingana na tarehe ya kukusanya, mkusanyaji, na chanzo cha mapato na kuongeza jumla ya kiasi cha makusanyo katika akaunti ya mkusanyaji. Mkusanyaji anapopeleka kiasi cha pesa aliyokusanya katika akaunti ya benki ya halmashauri, deni katika akaunti yake hufutika. Ukaguzi wa makusanyo ya mapato ya halmashauri kupitia POS kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 ulibaini udhaifu uliosababisha wadaiwa kama inavyooneshwa hapa chini:

- ✓ **Marekebisho ya Miamala ya Mapato Katika Mfumo wa Kukusanyia Mapato (LGRCIS) Bila Ushahidi na Idhini Kutoka kwa Maofisa Masuuli**

Nilibaini marekebisho ya miamala ya mapato yaliyofanywa ndani ya mfumo wa LGRCIS bila ushahidi na idhini inayofaa kutoka kwa ofisa masuuli. Kwa mfano, kupitia ukaguzi maalumu uliofanywa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2019/20, nilibaini kuwa halmashauri 28 zilifanya marekebisho ya miamala ya mapato ndani ya mfumo wa LGRCIS ya jumla ya Sh. 327,815,714,881,270 bila ushahidi na idhini kutoka kwa maofisa masuuli. Hii inatengeneza mianya ya ubadhirifu wa mapato yanayokusanywa kupitia POS, kwani watumiaji wa mfumo wanaweza, kwa makusudi, kuamua kurekebisha/kufuta miamala ya mapato kwa faida binafsi.

Ninapendekeza kuanzisha utaratibu ambao utadhibiti marekebisho ya miamala ya mapato ndani ya mfumo wa LGRCIS; na kuhakikisha kuwa marekebisho yote yanakuwa na ushahidi unaofaa na kupitishwa na maofisa masuuli.

- ✓ **Makosa ya mara kwa mara katika mfumo wa LGRCIS kama vile, kulazimisha watumiaji kuingia na kupata taarifa za mapato za halmashauri za wilaya nyingine.**

LGRCIS inalazimisha watumiaji kuingia katika halmashauri nyingine hivyo kutengeneza miamala ya mapato ambayo si ya halmashauri husika na kusababisha wadaiwa wasiojulikana. LGRCIS pia wakati mwingine hutengeneza kiasi hasi cha wadaiwa na kusababisha ugumu katika kuthibitisha kiasi ambacho hakijawasilishwa katika akaunti za benki za halmashauri.

Hii inaweza kusababishwa na ukosefu wa udhibiti wa ndani wa mfumo wa LGRCIS. Hali hii inaweza kusababisha uaminifu na usiri wa taarifa ndani ya LGRCIS kuingiliwa na kusababisha ubadhirifu na matumizi mabaya ya mapato unaoweza kufanywa na watumishi wa halmashauri wasio waaminifu.

Ninapendekeza OR-TAMISEMI kufanya juhudi na kuboresha mfumo wa LGRCIS ili kukidhi mahitaji ya mtumiaji na kuhifadhi uaminifu na usiri wa taarifa za halmashauri.

- ✓ **Ucheleweshaji wa Makusudi wa Uwasilishaji wa Mapato Katika Akaunti za Benki za Halmashauri Unaofanywa na Wakusanya Mapato Pamoja na Watumiaji wa POS**

Wadaiwa wa mapato wakati mwingine hutengenezwa kutokana na ucheleweshaji wa kuwasilisha fedha kwenye akaunti za benki za halmashauri. Wakusanya mapato huwa wanabaki na fedha za mapato zilizokusanywa au wakati mwingine hutumia mapato yaliyokusanywa kwa faida zao binafsi, hivyo kusababisha uwepo wa wadaiwa.

Ninashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa zitumie utaratibu ambao utawalazimisha wakusanyaji wa mapato kuingia katika makubaliano ya kurudisha kiwango wanachodaiwa, ikiwa mapato yaliyokusanywa hayakuwasilishwa katika akaunti za benki.

- ✓ **Mfumo wa LGRCIS Hautoi Nafasi kwa Halmashauri Kupata Taarifa za Wadaiwa Muda Wowote Wanapozihitaji**

LGRCIS hutoa kiasi cha mapato kisichokusanywa kwa ujumla, na hairuhusu watumiaji kupata kiwango kinachodaiwa wakati wowote. LGRCIS inatoa tu jumla ya kiasi kinachodaiwa bila kuzingatia kipindi chake. Hii inazuia

ufuatiliaji wa mapema juu ya kiasi kinachodaiwa kutoka kwa wakusanyaji wa mapato.

Ninapendekeza kwa OR-TAMISEMI kuboresha mfumo wa LGRCIS ili kukidhi mahitaji ya mtumiaji na kumruhusu mtumiaji kupata taarifa za wadaiwa wakati wowote ili kuwezesha ufuatiliaji mapema wa miamala inayodaiwa kwa muda unaohitajika.

- ✓ **Kukosekana kwa Utaratibu Ambao Miamala ya Mapato Yaliyokusanywa Kupitia Mashine za POS na Yale Yaliyo Kwenye Mfumo wa LGRCIS Kusuluhishwa**

Mapato yaliyokusanywa kupitia POS yanaingia moja kwa moja katika mfumo wa LGRCIS na kutambuliwa kama mapato. Hata hivyo, hakuna utaratibu ambao miamala ya mapato yaliyokusanywa kupitia mashine za POS na yale yaliyo kwenye mfumo wa LGRCIS kusuluhishwa ili kuweka kiwango sahihi kinachodaiwa na kuchukua hatua za kurekebisha mapema.

Ninapendekeza kwa mamlaka inayohusika kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani na kuhakikisha kuwa miamala ya mapato katika POS na LGRCIS inasuluhishwa mara kwa mara kwa hatua za haraka endapo kosa lolote linajitokeza

- ✓ **Kutoaminika kwa Huduma za Mtandao**

Kutoaminika kwa huduma za mtandao kunaleta changamoto hasa katika maeneo ya pembezoni na hivyo kusababisha huduma kutopatikana kwa muda mwingi. Hii inasababisha ugumu wa kupata kwa wakati ripoti za mapato kutoka katika mfumo wa LGRCIS.

Ninapendekeza OR-TAMISEMI kuwezesha upatikanaji wa mtandao wa kuaminika katika halmashauri zote hasa kwa maeneo ya pembezoni ili kuruhusu miamala ya mapato kupatikana kwa wakati katika LGRCIS; na kutoa nafasi ya ufuatiliaji wa kiwango kiinachodaiwa na kuchukua hatua stahiki mapema.

- ✓ **Ukosefu wa Udhibiti wa Kutosha Juu ya Utoaji wa Mashine za POS na Utunzaji wa Rejesta Zake**

Ukaguzi wa rejesta za utunzaji wa mashine za mapato (POS) ulibaini kuwa nyingi katika halmashauri haziendani na wakati na hazijumuishi taarifa za

POS kama vile mtengenezaji, namba ya mfano, namba ya IMEI; namba ya mfuatano ya POS na eneo POS ilipo. Niligundua pia kuwa halmashauri hazikuhuisha rejesta pale POS zinapoongezeka, zinapohamishwa eneo, zinapopotea na zinapoacha kutumika .

Ninapendekeza kwa menejimenti za halmashauri kuhakikisha kuwa rejesta za mashine za POS zinatunzwa na kuhuishwa wakati wote kwa kuonesha taarifa zinazohitajika, na kuhuisha rejesta mara tu mashine za POS zitakapotolewa au kuhamishiwa kwa mkusanyaji mwingine wa mapato au wakati zinapoacha kutumika kwa lengo la kuzidhibiti. Hii itasaidia kufuatilia kiasi kinachodaiwa kutoka kwa wakusanya mapato, ikitokea mashine za POS zinahamishwa mara kwa mara kwa wakusanya mapato mbalimbali.

14.2.12 Uhalalishaji wa Taratibu za Ukusanyaji Mapato kwa Vitambulisho vya Wajasiliamali

Tangu mwaka wa fedha 2017/18 Serikali imekuwa ikikusanya mapato kupitia vitambulisho vya wajasiriamali kwa kiwango cha Sh. 20,000 kwa kila mjasiriamali kwa mwaka. Katika ukaguzi wangu kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2019/20 nilibaini kuwa mapato haya yamekusanywa na halmashauri kwa niaba ya tawala za mkoa bila kuwepo sheria inayoruhusu halmashauri kufanya hivyo.

Ninashauri Serikali kujumuisha taratibu za ukusanyaji wa mapato kwa vitambulisho vya wajasiriamali katika sheria za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. 2-1: Orodha ya Halmashauri Zilizopata Hati Inayoridhisha

Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri
1	Halmashauri ya Wilaya ya Handeni	43	Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela	85	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro
2	Halmashauri ya Wilaya ya Karatu	44	Halmashauri ya Wilaya ya Itilima	86	Halmashauri ya Wilaya ya Moshi
3	Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama	45	Halmashauri ya Mji wa Kahama	87	Halmashauri ya Manispaa ya Moshi
4	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	46	Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo	88	Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda
5	Halmashauri ya Manispaa ya Songea	47	Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua	89	Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda
6	Halmashauri ya Wilaya ya Nyanghw'ale	48	Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha	90	Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe
7	Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba	49	Halmashauri ya Mji wa Kibaha	91	Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara
8	Halmashauri ya Wilaya ya Makete	50	Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	92	Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara
9	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe	51	Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo	93	Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi
10	Halmashauri ya Wilaya ya Uyui	52	Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni	94	Halmashauri ya Wilaya ya Muheza
11	Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga	53	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	95	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba
12	Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma	54	Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	96	Halmashauri ya Wilaya ya Musoma

Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri
13	Halmashauri ya Wilaya ya Pangani	55	Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe	97	Halmashauri ya Manispaa ya Musoma
14	Halmashauri ya Mji wa Babati	56	Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto	98	Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero
15	Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba	57	Halmashauri ya Wilaya ya Kyela	99	Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga
16	Halmashauri ya Wilaya ya Longido	58	Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa	100	Halmashauri ya Jiji la Mwanza
17	Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto	59	Halmashauri ya Wilaya ya Lindi	101	Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea
18	Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga	60	Halmashauri ya Manispaa ya Lindi	102	Halmashauri ya Mji wa Nanyamba
19	Halmashauri ya Wilaya ya Meru	61	Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa	103	Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu
20	Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi	62	Halmashauri ya Wilaya ya Madaba	104	Halmashauri ya Wilaya ya Newala
21	Halmashauri ya Wilaya ya Rombo	63	Halmashauri ya Wilaya ya Mafia	105	Halmashauri ya Mji wa Newala
22	Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro	64	Halmashauri ya Mji wa Mafinga	106	Halmashauri ya Wilaya ya Ngara
23	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	65	Halmashauri ya Wilaya ya Magu	107	Halmashauri ya Wilaya ya Njombe
24	Halmashauri ya Wilaya ya Babati	66	Halmashauri ya Mji wa Makambako	108	Halmashauri ya Mji wa Njombe
25	Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo	67	Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi	109	Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo
26	Halmashauri ya Mji wa Bariadi	68	Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	110	Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa
27	Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	69	Halmashauri ya Wilaya ya Masasi	111	Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri	Na.	Jina la Halmashauri
28	Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli	70	Halmashauri ya Mji wa Masasi	112	Halmashauri ya Wilaya ya Same
29	Halmashauri ya Mji wa Bunda	71	Halmashauri ya Wilaya ya Maswa	113	Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti
30	Halmashauri ya Wilaya ya Busega	72	Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali	114	Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga
31	Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo	73	Halmashauri ya Jiji la Mbeya	115	Halmashauri ya Wilaya ya Songwe
32	Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze	74	Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya	116	Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga
33	Halmashauri ya Wilaya ya Chato	75	Halmashauri ya Mji wa Mbinga	117	Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga
34	Halmashauri ya Jiji la Dodoma	76	Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi	118	Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba
35	Halmashauri ya Wilaya ya Gairo	77	Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu	119	Halmashauri ya Jiji la Tanga
36	Halmashauri ya Mji wa Geita	78	Halmashauri ya Mji wa Mbulu	120	Halmashauri ya Wilaya ya Tarime
37	Halmashauri ya Wilaya ya Hai	79	Halmashauri ya Wilaya ya Meatu	121	Halmashauri ya Mji wa Tarime
38	Halmashauri ya Mji wa Handeni	80	Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi	122	Halmashauri ya Mji waTunduma
39	Halmashauri ya Mji wa Ifakara	81	Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga	123	Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo
40	Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi	82	Halmashauri ya Wilaya ya Mlele	124	Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe
41	Halmashauri ya Manispaa ya Ilala	83	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli		
42	Halmashauri ya Wilaya ya Ileje	84	Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro		

Kiambatisho Na. 2-2: Orodha ya Halmashauri Zilizopata Hati yenye Shaka na Sababu Zake

Jina la Halmashauri na sababu zilizopelekea
1. Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi
a) **Hati za madai ya fedha zilizofanyiwa marekebisho bila ya kuwa na nyaraka toshelezi Sh. 320,033,902** Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilifanya marekebisho ya hati za madai kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) ya jumla ya Sh. 320,033,902, lakini marekebisho hayo hayakuwa na nyaraka muhimu kama vile hati zilizoidhinishwa za kufanya marekebisho (journal vouchers) pamoja na nyaraka nyingine za kuhalalisha marekebisho hayo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha juu ya usahihi na uhalali wa marekebisho hayo. b) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi, Sh. 9,991,616** Halmashauri ilifanya malipo yenye jumla ya Sh. 9,991,616 kwa walipwaji mbalimbali, lakini malipo hayo hayakuwa na nyaraka zifuatazo; hati za madai, hati za kupokelea bidhaa, stakabadhi za kielektroniki, na nyaraka za matumizi/ugawaji wa bidhaa. Kwa kutokuwepo nyaraka hizo, nimeshindwa kujiridhisha juu ya usahihi wa kiasi kilicholipwa na kama bidhaa zilizonunuliwa zilipokelewa na kutumika kwa usahihi. c) **Matumizi yaliyoripotiwa pungufu kwa Sh. 160,795,205** Maelezo Na. 25 ya taarifa za kifedha yameainisha madeni ya jumla ya Sh.160, 795,205 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020; hata hivyo, kiasi hicho cha madeni hakikuoneshwa kama matumizi kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha kwa mwaka (statement of financial performance).
2. Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe
a) **Uhamisho wa fedha kutoka kwenye akaunti ya mapato ya ndani kwenda kwenye akaunti ya masurufu (Korogwe DC Imprest Account) bila ya vielelezo vya kutosha Sh. 23,586,000** Halmashauri ilihamisha Sh. 30,800,000 kutoka akaunti ya makusanyo ya mapato ya ndani kwenda kwenye akaunti ya masurufu bila kutumia hati za malipo. Kati ya kiasi kilichohamishwa, sikupata nyaraka zinazoonesha jinsi kiasi cha Sh. 23,586,000 kilivyotumika. Kufanya

malipo pasipo kutumia hati za malipo, sio tu kinyume na matakwa ya Aya ya 6.7.3(b) ya Mwongozo wa Uhasibu wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019, bali pia, inapelekea kushindwa kupata undani wa matumizi yaliyofanywa.

b) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi, Sh. 32,679,130**
Nimeshindwa kuthibitisha matumizi ya Sh. 19,602,736 kati ya kiasi cha Sh. 56,720,600 kilichohamishwa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Korogwe kwa sababu hakukuwa na nyaraka za kuhalalisha matumizi hayo. Pia, Halmashauri ilifanya jumla ya malipo ya Sh. 13,076,394 kwa walipwaji mbalimbali, lakini hakukuwa na nyaraka za kuthibisha uhalali wa matumizi ya kiasi hicho kilicholipwa.

c) **Tofauti ambayo haikusuluhishwa kati ya kiasi cha mapato kiliochoripotiwa kwenye LGRCIS na EPICOR, Sh. 87,888,537**
Ukaguzi wa mapato yaliyokusanywa kupitia LGRCIS kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, ulibaini kuwa, mfumo wa LGRCIS ulionesha makusanyo ya jumla ya Sh. 663,921,720 wakati kiasi cha makusanyo kwenye mfumo wa Epicor kilikuwa Sh. 751,810,257, hivyo kupelekea tofauti ya Sh. 87,888,537ambayo haikufanyiwa usuluhisho. Tofauti hii inatilia mashaka kuaminika kwa taarifa zilizozalishwa na mifumo hiyo miwili kwa kuwa taarifa zinazozalishwa na mfumo wa LGRCIS hutumika kwenye mfumo wa Epicor, na ndizo ambazo zinapelekea uandaaji wa taarifa za fedha.

d) **Kutokuonesha kwenye taarifa za fedha mapato yaliyokusanya lakini hayakupelekwa benki Sh. 144,774,106**
Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, nimebaini kuwa Halmashauri ilikusanya mapato ya Sh. 144,774,106 kupitia POS ambapo; Sh. 52,835,177 zilikusanywa na watumishi wa Halmashauri na Sh. 91,938,929 zilikusanywa na mawakala, lakini makusanyo hayo hayakupelekwa benki na wala hayakuoneshwa kwenye taarifa za fedha.

e) **Malipo yaliyofanywa kutoka akaunti ya amana hayakuoneshwa kwenye taarifa za fedha Sh. 104,343,605**
Nimebaini kuwa, malipo ya Sh. 104,343,605 yalifanywa kutoka katika akaunti ya amana bila kuonesha kumbukumbu za mwekaji wa fedha hizo, na pia hakukuwa na marekebisho yaliyofanyika kwenye taarifa

za fedha (taarifa ya utendaji wa kifedha) ili kuhakikisha kuwa kiasi hicho kimeripotiwa kikamilifu.

3. Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro

a) **Mapato mengine yalioneshwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 3,500,000**

Taarifa ya utendaji wa kifedha pamoja na maelezo Na. 10 kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi cha mapato cha Sh. 1,074,670,443 ambacho kilijumuisha kiasi ambacho hakikuwa kimepokelewa kufikia tarehe 30 Juni 2020 cha Sh. 3,500,000; hata hivyo hakukuwa na madai yaliyohusiana na mapato hayo, hivyo kupelekea mapato kuoneshwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 3,500,000.

b) **Malipo yalifofanyika kabla ya bidhaa kupokelewa kutotambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, Sh. 15,739,235**

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilifanya malipo ya mbele ya Sh. 15,739,235 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta, hata hivyo, kiasi hicho hakikutambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, hivyo kiasi cha malipo kilichooneshwa kuhusiana na gharama za matengenezo kilikuwa pungufu kwa Sh.15,739,235.

c) **Matumizi yaliyofanywa kwa fedha zilizoazimwa kutoka akaunti ya amana kutotambuliwa kwenye taarifa za fedha, Sh. 213,052,970**

Maelezo Na.30 kwenye taarifa za fedha yalionesha madeni yaliyohusiana na fedha zilizowekwa na wakandarasi mbalimbali kwenye akaunti ya amana ya jumla ya Sh. 678,236,141. Hata hivyo, kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh. 213,052,970 kiliazimwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kawaida, lakini matumizi ya fedha hizo hayakutambuliwa kwenye taarifa za fedha, hivyo jumla ya matumizi yaliyooneshwa yalikuwa pungufu kwa Sh. 213,052,970.

4. Halmashauri ya Wilaya ya Chunya

a) **Tofauti ambayo haikusuluhishwa kati ya mapato yaliyoripotiwa kwenye mfumo wa LGRCIS na mfumo wa Epicor ya Sh. 515,671,878**

Nimebaini tofauti ambayo haikusuluishwa ya Sh. 515,671,878 kutokana na mapato yaliyokusanywa ambapo mfumo wa LGRCIS ulionesha jumla ya makusanyo ya Sh. 3,123,702,179 wakati mfumo wa Epicor ulionesha jumla ya makusanyo ya Sh. 3,639,374,057 na

kupelekea tofauti ya Sh. 515,671,878, hivyo sikuweza kujiridhisha na usahihi wa kiasi kilichotumika katika kuandaa taarifa za fedha.

b) Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 118,295,759

Maelezo Na. 17 na 25 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 118,295,759 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

5. Halmashauri ya Wilaya ya Iringa

a) Ongezeko la thamani ya misitu ambalo halikutambuliwa kwenye taarifa za fedha, Sh. 284,263,064

Maelezo Na. 25 ya taarifa za fedha yamebainisha ongezeko la thamani ya misitu kutoka Sh. 756,623,300 mwaka 2018/19 hadi Sh. 1,040,886,364 kwa mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la Sh. 284,263,064, hata hivyo ongezeko hilo halikutambuliwa kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha kinyume na matakwa ya aya ya 30 ya IPSAS 27. Hii imepelekea faida iliyoripotiwa kwa mwaka 2019/20 kuwa pungufu kwa Sh. 284,263,064.

b) Madeni ambayo hayakuthibitika yaliyotokana na kiasi ambacho hakikupelekwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa Sh. 19,503,165

Maelezo Na. 25 ya taarifa za fedha yameonesha pamoja na mambo mengine, madeni ya Sh. 19,503,165 kwa mwaka 2018/19 yaliyotokana na kiasi ambacho hakikupelekwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, kiasi hicho hakikuwa na sifa ya kuwa sehemu ya madeni ya Halmashauri. Pia ilibainika kuwa, kiasi hicho cha Sh. 19,503,165 kilitumika katika kukokotoa kiasi cha malipo ya wazabuni kwenye Maelezo Na. 43 yaliyoripotiwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, wakati kiuhalisia hakukuwa na malipo yaliyokuwa yamemelipwa, hivyo kumepelekea madeni na malipo yaliyoripotiwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kutokuwa sahihi.

c) Mchango uliolipwa ALAT ulioneshwa kimakosa kwenye taarifa za fedha Sh. 13,663,000

Nimebaini kuwa, kiasi cha mchango wa fedha cha Sh. 13,663,000 kilicholipwa ALAT kilitambuliwa kimakosa kwenye taarifa za fedha kama vifaa na bidhaa zinazotumiwa (Maelezo Na. 43) badala kutambulika kama ruzuku na malipo mengine (Maelezo Na. 19), hivyo kupelekea kiasi kilichooneshwa kwa ruzuku na malipo mengine kuwa pungufu, na kiasi kilichooneshwa kama vifaa na bidhaa zinazotumiwa kuwa zaidi kwa Sh. 13,663,000.

6. Halmashauri ya Wilaya ya Bunda

a) Marekebisho ambayo hayakuthibitishwa, yaliyoripotiwa kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji Sh. 867,080,000

Halmashauri iliripoti marekebisho ya madai ya Sh. 867,080,000 kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020; hata hivyo hakukuwa na maelezo ya ziada au nyaraka zinazohusiana na marekebisho hayo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha uhalali wake.

b) Limbikizo la faida lililoripotiwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 370,015,000

Maelezo Na. 24 ya taarifa za kifedha yalionesha kurejeshwa kwa kiasi kilichokuwa kimetengwa kwa ajili ya malipo ya mbeleni (reversal of provisions) kulingana na mwenendo wa kesi za madai zilizokuwa mahakamani kwa kiasi cha Sh. 370,015,000 kutoka Sh. 452,895,000 kilichoripotiwa mwaka 2018/19 hadi Sh. 82,880,000 kilichoripotiwa kwa mwaka 2019/20; hata hivyo, kiasi hicho cha marejesho hakikujumlishwa kwenye limbikizo la faida kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji, hivyo kupelekea limbikizo hilo kuripotiwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 370,015,000 kufikia tarehe 30 Juni 2020.

c) Kutokuainisha sababu za mabadiliko yaliyofanyika kwenye taarifa za fedha kwa mwaka 2018/19 Sh. 3,130,700,000

Nimebaini kuwa, Halmashauri ilifanya mabadiliko kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka 2018/19 kiasi cha Sh. 3,130,700,000 lakini hakukuwa na maelezo kwenye taarifa za fedha au nyaraka zozote za kuthibitisha uhalali na usahihi wa mabadiliko hayo yaliyofanywa.

7. Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

a) Limbikizo la faida liliripotiwa zaidi kwa Sh. 1,787,116,485

Halmashauri ilihamishia kiasi cha mtaji (Taxpayers fund) cha Sh. 17,044,445,000 kwenda kwenye limbikizo la hasara la Sh. 1,787,116,485 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019, ambapo ilitakiwa kupelekea kuwa na ongezeko la limbikizo la faida la Sh. 15,257,328,515, badala yake, Halmashauri iliripoti ongezeko la Sh. 17,044,445,000 hivyo kupelekea ongezeko la faida kuripotiwa zaidi kwa Sh. 1,787,116,485.

b) **Ongezeko la kiasi cha fedha kilichokuwepo kwenye akaunti ya amana ambalo halikuoneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, Sh. 377,294,008**

Maelezo Na. 24 ya taarifa za fedha yamebainisha ongezeko la Sh. 377,294,008 kwenye akaunti ya amana kutoka kwenye bakaa iliyokuwepo mwaka jana ya Sh. 57,633,613 hadi kufikia bakaa ya Sh. 434,927,621 kwa mwaka huu wa 2019/20; ila, mapokezi na matumizi ya fedha kutoka akaunti ya amana hayakuoneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha hivyo kupelekea bakaa ya fedha kuripotiwa pungufu kwenye taarifa hiyo kwa Sh. 377,294,008.

c) **Kuripotiwa zaidi kwa bidhaa za stoo zilizotumika kulikopelekea kuripotiwa pungufu kwa bidhaa zilizokuwepo stoo kwa Sh. 166,332,740**

Maelezo Na. 18 ya taarifa za fedha yalionesha kuwa, Halmashauri iliripoti matumizi bidhaa zinazohusiana na madawa na vifaa tiba ambayo hayakuwa yametumika yenye jumla ya Sh. 166,332,740 ambapo ni kinyume na matakwa ya aya ya 44 ya IPSAS 12 inayotaka bidhaa kutambulika kama matumizi pale ambapo zimetumika. Hii imepelekea kuripotiwa kwenye taarifa za fedha kwa zaidi matumizi kuhusiana na bidhaa zilizotumika na kuripotiwa pungufu bidhaa zilizobakia stoo mwisho wa mwaka kwa Sh. 166,332,740.

d) **Kutosuluhishwa kwa tofauti ya stahiki za watumishi ambazo hazikuwa zimelipwa kwenye taarifa za fedha Sh. 102,347,461**

Nimebaini kuwa bakaa ya kuanzia ya madeni ya stahiki za watumishi (mishahara) kwenye Maelezo Na. 17 ilitofautiana na bakaa la kuanzia kuhusiana na madeni ya mishahara hiyo hiyo kwenye maelezo Na. 34 kwa Sh. 86,478,543. Pia bakaa ya mwisho kwenye maelezo Na. 17 inatofautiana na maelezo ya ziada kuhusiana na madeni ya mishahara

(Maelezo Na. 34) kwa kiasi cha 15,868,918. Hii imepelekea jumla ya tofauti ambayo haikusuluhishwa ya Sh. 102,347,461.

e) Mchango wa Halmashauri kwenye akaunti ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuripotiwa kimakosa kama matumizi, Sh. 102,580,000 kwa mwaka 2018/19 na Sh. 104,000,000 kwa mwaka 2019/20

Maelezo Na. 20 ya taarifa za kifedha yameonesha matumizi yaliyohusiana na mchango wa asilimia 10 ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya jumla ya Sh. 104,000,000 kwa mwaka 2020 na Sh. 102,580,000 kwa mwaka 2019. Michango hiyo inahusisha uhamisho wa fedha ndani ya Halmashauri kutoka akaunti moja kwenda nyingine na hivyo haikuwa na sifa ya kuwa matumizi ya Halmashauri. Hii imepelekea faida iliyoripotia kwa miaka husika kuwa pungufu kwa kiasi cha michango kilichoripotiwa kama matumizi.

f) Hasara iliyotokana na mauzo ya pikipiki, kutokutambuliwa kwenye taarifa za fedha Sh. 60,324,281

Maelezo Na. 29 ya taarifa za kifedha yalionesha mauzo ya pikipiki kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 zilizokuwa na gharama ya Sh. 188,616,621 na malimbikizo ya uchakavu ya Sh. 128, 292,340 bila ya kupata fedha yeyote kutokana na mauzo hayo, hivyo kupelekea hasara ya Sh. 60,324,281, lakini hasara hiyo haikutambuliwa kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha na hivyo kufanya faida iliyoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh. 60,324,281.

8. Halmashauri ya Manispaa ya Singida

a) Madeni yaliyoripotiwa zaidi kwa Sh. 247,296,200

Maelezo Na. 25 ya taarifa za kifedha yalibainisha madeni ya Sh. 1,589,968,739 badala ya Sh. 1,342,672,538.68 tofauti iliyotokana na makosa ya kujumlisha, hivyo kupelekea madeni yaliyoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh. 247,296,200.

b) Gharama ya kazi za ujenzi uliokuwa unaendelea kuripotiwa pungufu kwa Sh. 273,897,985

Maelezo Na. 30 ya taarifa za kifedha yamebainisha gharama ya kazi za ujenzi uliokuwa unaendelea ya Sh. 2,205,228,197 badala ya Sh. 2,479,126,182 kutokana na makosa ya ukokotoaji, hivyo kupelekea gharama hiyo kuripotiwa pungufu kwa Sh. 273,897,985.

c) Uchakavu wa mali, mitambo na vifaa ulioripotiwa zaidi kwa Sh. 227,709,760 kwa mwaka 2018/19

Maelezo Na. 30 ya taarifa za kifedha yameonesha kiasi za uchakavu wa mali, mitambo na vifaa ya Sh. 1,106,769,716 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2019; hata hivyo, kiasi cha uchakavu kilichoripotiwa kwenye taarifa ya utendaji ya kifedha kilikuwa Sh. 1,334,479,476, hivyo kupelekea ziada ambayo haikuwa na maelezo ya Sh. 227,709,760 iliyopelekea kupungua kwa faida iliyoripotiwa kwa mwaka huo.

d) Mishahara na stahiki za watumishi zilizokuwa hazijaliwa kutotambuliwa kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha Sh. 140,280,033

Maelezo Na. 26 kwenye taarifa za kifedha yameonesha ongezeko la madeni yanayotokana na mishahara na stahiki za watumishi ya Sh. 140,280,033 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020; hata hivyo, ongezeko hilo halikujumuishwa kwenye Maelezo Na. 15 (mishahara na stahiki za watumishi); hivyo kiasi cha mishahara kilichoripotiwa kama matumizi kilikuwa pungufu kwa Sh. 140,280,033.

9. Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo

a) Hati za madai zilizoidhinishwa kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) bila ya kuwa na nyaraka toshelezi Sh. 191,935,660

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri iliidhinisha marekebisho ya hati za madai (bill) za mapato kwa kufuta jumla ya madai ya Sh. 191,935,660 kwenye mfumo wa LGRCIS; hata hivyo, marekebisho hayo hayakuwa na nyaraka zilizohalalisha. Hali hii ilinizuia katika kujiridhisha na sababu zilizopelekea kufutwa kwa hati hizo za madai ya mapato.

10. Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa

b) Fedha za ruzuku ya maendeleo ziliripotiwa zaidi ya kiasi kilichopokelewa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa Sh. 199,233,000

Maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha za ulinganisho yalionesha ongezeko la fedha za maendeleo zilizopokelewa Sh. 3,271,717,759 kwa mwaka wa fedha 2018/19 wakati taarifa ya mtiririko wa fedha iliripoti kiasi cha fedha za maendeleo kilichopokelewa cha Sh.

3,470,950,759 hivyo kupelekea kiasi cha fedha za maendeleo kilichopokelewa kuripotiwa zaidi kwa Sh. 199,233,000.

c) Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 203,774,328

Maelezo Na. 21 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 203,774,328 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

11. Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko

a) **Kiasi cha matumizi ya fedha za ruzuku ya kawaida ambacho hakikuthibitishwa Sh. 725,663,000**

Maelezo Na. 11 kwenye taarifa za kifedha yameonesha matumizi ya fedha za ruzuku za kawaida ya Sh. 11,695,780,000; hata hivyo, mchanganuo wa matumizi hayo kwenye maelezo Na. 44 umeonesha jumla ya matumizi hayo ni Sh. 10,970,117,000, hivyo kupelekea tofauti ambayo haikuthibitishwa uhalali wake ya Sh. 725,663,000.

b) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 194,415,821**

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, nimebaini kuwa, halmashauri ilifanya malipo ya jumla ya Sh. 132,311,821 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, wakati hati za malipo zenye jumla ya Sh. 62,104,000 hazikupatikana kabisa wakati wa ukaguzi. Kukosekana kwa nyaraka na hati hizo kulipelekea kushindwa kukidhi mawanda ya ukaguzi wangu, kwa kuwa nimeshindwa kujiridhisha na uhalali wa malipo hayo yaliyofanyika.

c) **Kushindwa kujiridhisha na marekebisho ya hati za madai yaliyofanyika kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato Sh. 64,651,714**

Nimebaini marekebisho ya hati za madai ya mapato (ankara za mapato zilizofutwa) kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) ya jumla ya Sh. 64,651,714 lakini hakukuwa na ushahidi kuwa, marekebisho hayo yaliidhinishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri na hakukuwa na nyaraka za maandishi zilizohalalisha marekebisho

hayo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha juu ya usahihi na uhalali wa marekebisho hayo.

d) **Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 242,820,000**

Maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 242,820,000 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

12. Halmashauri ya Wilaya ya Butiama

a) **Malipo ya mishahara na stahiki za watumishi yaliripotiwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 804,585,770**

Maelezo Na. 17 kwenye taarifa za fedha pamoja na taarifa ya mtiririkio wa fedha imeonesha malipo ya Sh. 17,750,093,142 yaliyohusiana na mishahara na stahiki za watumishi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020; hata hivyo, kiasi hicho kilikuwa pungufu kwa Sh. 804,585,770 kwa kuwa Maelezo Na. 17 hayakujumuisha mabadiliko ya mikopo kwa watumishi kama yalivyoripotiwa kwenye maelezo Na. 25 na mabadiliko ya madeni ya stahiki za watumishi kama yalivyoripotiwa kwenye Maelezo Na. 38.

b) **Malipo ya bidhaa linazotumika yalioneshwa pungufu kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa Sh. 26,272,555**

Halmashauri iliripoti malipo ya fedha kiasi cha Sh. 3,116,539,186 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na bidhaa zinazotumiwa kwenye taarifa ya mtiriko wa fedha (sehemu ya mtiririko wa fedha kutoka kwenye shughuli za kawaida za uendeshaji wa taasisi) kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020; hata hivyo, ukaguzi wa Maelezo Na.18, 25 na 35 kwenye taarifa za fedha ulibaini kuwa jumla ya malipo hayo yalitakiwa kuwa Sh. 3,142,811,741, hivyo, kiasi kilichoripotiwa kilikuwa pungufu kwa Sh. 26,272,555.

c) **Matumizi ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa yalioneshwa pungufu kwa Sh.18,211,856**

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilionesha matumizi ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa ya Sh. 3,232,913,648, hata hivyo, kiasi hicho hakikuwa kimefanyiwa marekebisho ya mabadiliko

ya salio anzia na salio ishia la bidhaa zilizokuwepo stoo la Sh. 18,211,857 kama ilivyooneshwa kwenye maelezo Na. 26 ya taarifa za fedha. Hivyo matumizi yaliyooneshwa kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha yalikuwa pungufu kwa Sh. 18,211,856.

d) **Madai ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu yalioneshwa pungufu kwa Sh. 32,523,380**

Maelezo Na.21 kwenye taarifa za fedha na taarifa ya mtiririko wa fedha yalionesha jumla ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya kina mama, vijana na watu wenye ulemavu ya Sh. 32,523,380 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020; hata hivyo, hakukuwa na marejesho yeyote yaliyofanyika, na madai hayo hayakutambuliwa kwenye mizania ya hesabu, hivyo kupelekea kuripoti wadaiwa pungufu kwa kiasi hicho.

Pia nimebani kuwa, kwa mwaka ulioishia tarehe 30 June 2019, Halmashauri ilitoa jumla ya mikopo ya Sh.20,000,000 kulingana na maelezo Na. 21 kwenye taarifa za fedha, lakini kiasi hicho hakikuoneshwa kwenye taarifa ya ulinganisho ya mtiririko wa fedha kwa mwaka 2018/19.

e) **Kiasi cha ruzuku ya shughuli za kawaida kilichotumika kilioneshwa zaidi kwa Sh. 49,710,685**

Halmashauri ilionesha kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha malipo ya Sh. 49,710,685 ikiwa ni kiasi kilichorejeshwa Wizara ya Fedha na Mipango kama kiasi cha ruzuku kilichopokelewa lakini hakikuwa kimetumika. Kiasi hicho pia kilitumika kwenye kukukotoa mapato yaliyotokana na ruzuku wakati kiasi hicho hakikustahili kujumuishwa kama mapato na wala hakikustahili kuwa sehemu ya matumizi, hivyo kiasi cha mapato na matumizi kilichoripotiwa kilikuwa zaidi kwa Sh. 49,710,685.

f) **Fedha zilipokelewa kwenye akaunti ya amana kutotambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, Sh. 66,617,710**

Maelezo Na. 24 (Bakaa ya fedha) yalionesha ongezeko la Sh. 66,617,710 kutoka bakaa lililooneshwa mwaka 2018/19 ya Sh. 286,864,497 hadi bakaa ya Sh.353,482,207 iliyooneshwa kwa mwaka 2019/20; hata hivyo, mapato na matumizi kuhusiana na akaunti ya amana hayakutambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, hivyo

kupelekea bakaa ya fedha iliyooneshwa kwa mwaka 2019/20 kuwa pungufu kwa Sh. 66,617,710.

g) **Mchango wa Halmashauri ambao haukuwa umepelekwa kwenye akaunti ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ulitambuliwa kimakosa kama madeni, Sh. 4,568,800**
Halmashauri ilionesha madeni ya Sh. 4,568,800 yanayohusiana na wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye maelezo Na. 35 ya taarifa za fedha kufikia tarehe 30 Juni 2020. Hata hivyo, kiasi hicho hakikutakiwa kuonekana kwenye taarifa za fedha kwani kilitakiwa kiwe kimeondolewa na madai yaliyokuwa kwenye taarifa za fedha za mfuko wa wanawake vijana na watu wenye ulemavu wakati wa ujumuishaji wa taarifa za fedha za Halmashauri, hivyo, kiasi cha madeni kilichooneshwa kilikuwa zaidi kwa Sh. 4,568,800.

13. Halmashauri ya Wilaya ya Rorya

a) **Malipo ya mishahara na stahiki za watumishi yalioneshwa pungufu kwa mwaka 2018/19 kwenye taarifa za fedha za mwaka 2019/20, Sh. 31,910,065**
Nimebaini kuwa, kiasi cha Sh. 20,759,262,225 kilioneshwa kama malipo ya mishahara na stahiki za watumishi kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, badala ya kiasi sahihi cha Sh. 20,791,172,290 hivyo kupelekea pungufu ya malipo hayo kwa Sh. 31,910,065. Hii ilisababishwa na kutokuhusishwa mabadiliko ya salio anzia na salio ishia la madai ya watumishi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019.

b) **Ongezeko la bakaa ya fedha kwenye akaunti ya amana halikuoneshwa kwenye taarifa za fedha za ulinganifu kwa mwaka 2018/19, Sh. 272,859,009**
Nimebaini kuwa, katika taarifa ya ulinganishi kwa mwaka wa fedha 2018/19, ongezeko la fedha kwenye akaunti ya amana la Sh. 272,859,009 (kutoka Sh. 90,329,535 lililooneshwa kwa mwaka 2017/18 hadi Sh. 363,188,544 kwa 2018/19) halikutambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka huo.

c) **Mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu haikuwa na maelezo, Sh. 69,850,000**
Halmashauri ilionesha mikopo ya Sh. 69,850,000 iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye

taarifa ya mtiririko wa fedha; lakini kiasi hicho, hakikuwa na maelezo kinyume na matakwa ya Aya ya 128 ya IPSAS 1.

d) **Usuluhisho wa faida/(hasara) halisi na mtiririko halisi wa fedha kutoka kwenye shughuli za kawaida haukuandaliwa**

Halmashauri haikuandaa usuluhisho wa faida/(hasara) halisi na mtiririko halisi wa fedha kutoka kwenye shughuli za kawaida, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya Aya ya 28 na 29 ya IPSAS 2 pamoja na waraka Na. EG.3/102/05/03/000 wa tarehe 8 Mei 2020 kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali.

14. Halmashauri ya wilaya ya Chamwino

a) **Kushindwa kujiridhisha na marekebisho yaliyofanywa kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji Sh. 104,989,135**

Halmashauri ilifanya marekebisho ya Sh. 104,989,135 kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji, lakini hakukuwa na maelezo ya ziada ikiwepo maeneo ambayo yaliathirika kutokana na marekebisho hayo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wa marekebisho hayo.

b) **Kiasi chenye utata cha malipo ya vifaa na bidhaa zilizoripotiwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha Sh. 2,740,856,056**

Maelezo Na. 30 kwenye taarifa za fedha na taarifa ya mtiririko wa fedha yalionesha malipo kwa ajili ya vifaa na bidhaa ya Sh. 2,740,856,056; hata hivyo, ukokotozi wangu wa kiasi kilichooneshwa kwenye Maelezo Na. 30 ulibaini kuwa kiasi sahihi kilitakiwa kuwa Sh. 3,189,309,026 badala ya Sh. 2,740,856,056 hivyo kupelekea tofauti ya Sh. 448,452,970. Vilevile, kiasi hicho kilifanyiwa marekebisho kwa kutoa bakaa ya mwisho ya bidhaa/vifaa vya stoo ya Sh. 224,226,485 badala ya bakaa sahihi ya Sh.134, 091,985 na kupelekea tofauti ya Sh. 90,134,500, pia, masurufu ya Sh. 107,428,826 yaliondolewa katika mwaka 2019/20 badala ya kwenye mwaka 2018/19.

c) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 8,885,649**

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 8,885,649 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, hivyo sikuweza kujiridhisha juu ya madhumuni na uhalali wa malipo hayo.

d) **Kutokutenga hasara ya mbeleni kutokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki, Sh. 126,060,358**

Maelezo Na. 22 kwenye taarifa za fedha yalionesha madai ya jumla ya Sh. 126,060,358 yaliyotokana na mapato yaliyokusanywa na watumishi wa Halmashauri pamoja na mawakala wa ukusanyaji mapato kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato papo kwa papo (POS), lakini hayakupelekwa benki/kuwasilishwa Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri haikutenga hasara inayoweza kujitokeza mbeleni kutokana na kiasi hicho kutowasilishwa, hivyo kupelekea madai na faida iliyoripotiwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kuwa zaidi kwa Sh. 126,060,358.

15.Halmashauri ya Wilaya ya Chemba

a) **Malipo yaliyooneshwa mara mbili kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, Sh. 255,060,710**

Maelezo Na. 70H kwenye taarifa za fedha yalionesha malipo ya ruzuku na malipo mengine ya Sh. 501,002,410 ambayo yalijumuisha kiasi cha Sh. 255,060,710 kilichorudishwa Hazina. Hata hivyo, kiasi hicho pia kilijumuishwa tena kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha sehemu ya mtiriko wa fedha kutoka kwenye shughuli za kifedha, hivyo kupelekea kiasi cha malipo kuoneshwa mara mbili.

b) **Marekebisho ya gharama za mishahara na stahiki za watumishi ambayo hayakuwa na nyaraka, Sh. 1,191,622,347**

Maelezo Na. 70E kwenye taarifa za fedha na taarifa ya mtiririko wa fedha yalionesha malipo ya gharama za mishahara na stahiki za watumishi ya Sh. 12,969,205,361, lakini kiasi hicho kilijumuisha marekebisho ya jumla ya Sh. 1,191,622,347 ambayo hayakuwa na nyaraka za kuyahalalisha, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi wake.

c) **Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 455,953,000**

Maelezo Na. 11.19 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 455,953,000 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

16. Halmashauri ya Mji wa Korogwe

a) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi, Sh. 5,089,200**

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 5,089,200 kwa walipwaji mbalimbali, lakini malipo hayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wa malipo hayo.

b) **Madai ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yalioneshwa pungufu kwa Sh. 28,373,670**

Maelezo Na. 21 kwenye taarifa za fedha yalionesha jumla ya madai ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu ya Sh. 82,422,730, lakini, ukaguzi wa nyaraka zilizohusiana na utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo ulibaini kuwa, kiasi kilichokuwa hakijarejeshwa kufikia tarehe 30 Juni 2020 kilikuwa Sh. 110,796,400; hivyo, madai yaliyooneshwa yalikuwa pungufu kwa Sh. 28,373,670.

c) **Mapato toka vyanzo vya ndani yalioneshwa pungufu kwa Sh. 137,824,709**

Halmashauri ilionesha jumla ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani (ushuru, ada, adhabu na kwenye shughuli za biashara) ya Sh. 1,633,721,631 kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha; hata hivyo, mapato ambayo hayakuwa yamekusanywa ya Sh. 1,581,525,668 kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha yalikuwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 137,824,709.

d) **Matumizi ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa yalioneshwa pungufu kwa Sh. 218,222,589**

Taarifa ya mtiririko wa fedha ilionesha malipo kutokana na vifaa na bidhaa ya Sh. 2,176,967,990; hata hivyo, ukaguzi wa mwenendo wa madeni ili kujiridhisha na usahihi wa matumizi yaliyooneshwa ulibaini kuwa, ongezeko halisi la bidhaa za stoo, madai na madeni lilikuwa ni jumla ya Sh. 392,016,324 badala ya kiasi kilichoongezwa cha Sh. 173,793,735 hivyo kupelekea matumizi yaliyooneshwa kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha kuwa pungufu kwa Sh. 218,222,589.

e) **Makosa kwenye kiasi kilichoazimwa kutoka akaunti ya amana Sh. 21,271,843**

Halmashauri ilitambua kiasi cha fedha kilichoazimwa kutoka akaunti ya amana cha Sh. 21,271,843 kama madeni kwenye maelezo Na. 26; hata hivyo, kiasi hicho hakikutakiwa kutambuliwa hivyo badala yake,

ilitakiwa tu kutolewa maelezo kwenye taarifa za fedha. Vilevile, nimebaini kuwa, kiasi kilichoazimwa kilitumika kutekeleza majukumu ya kawaida ya Halmashauri, lakini matumizi ya hela hiyo hayakutambuliwa kwenye taarifa za fedha.

f) **Malipo yaliyofanyika kabla bidhaa kupokelewa hayakutambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha Sh.15,048,382**

Halmashauri ilifanya malipo ya mbele kiasi cha Sh. 15,048,382 kwa Bohari ya Madawa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba; hata hivyo, kiasi hicho hakikuoneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha.

g) **Madeni yaliyooneshwa zaidi kwa Sh. 11,202,772**

Maelezo Na. 26 kwenye taarifa za fedha yalionesha madeni ya Sh. 11,202,772 yaliyohusiana na michango ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, lakini hakukuwa na matumizi yaliyooneshwa yaliyotokana na madeni hayo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na uwepo wa madeni hayo.

17. Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe

a) **Marejesho ya mkopo wa Sh. 20,999,000 kwa mwaka 2019/20 na Sh.17, 856,000 kwa mwaka 2018/19 yaliripotiwa kimakosa kama malipo kutokana na shughuli za kawaida.**

Nimebaini kuwa, Halmashauri ilifanya marejesho ya mkopo kwa jumla ya Sh. 20,999,000 kwa mwaka 2019/20 na Sh. 17,856,000 kwa mwaka 2018/19, lakini marejesho hayo yalioneshwa kwenye sehemu ya mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kawaida badala ya mtiririko wa fedha kutoka kwenye shughuli za kifedha.

b) **Mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 bila maelezo, Sh. 4,350,362,000**

Halmashauri ilifanya mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 kwenye taarifa za fedha za mwaka 2019/20 kutoka kwenye kiasi halisi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka 2018/19 ya jumla ya Sh. 4,350,362,000, lakini mabadiliko hayo hayakubainisha chimbuko na sababu zilizopelekea mabadiliko hayo.

c) **Kutokuonesha mali tarajiwa (contingent assets) kutokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki Sh. 48,160,000**

Maelezo Na. 20 kwenye taarifa za fedha yameonesha fedha tarajiwa iliyotokana na mapato yaliyokusanywa na watumishi wa Halmashauri na mawakala wa ukusanyaji mapato lakini hayakupelekwa benki/hayakuwasilishwa Halmashauri ya Sh. 48,160,000, lakini kiasi hicho hakikuoneshwa kwenye maelezo kama mali tarajiwa (contingent assets) na hakukuwa na maelezo ya ziada kuhusiana na hatua zilizochukuliwa na Halmashauri kuhakikisha kiasi hicho kinawasilishwa.

d) **Matumizi yaliyooneshwa pungufu kwa mwaka 2018/19, Sh. 62,467,000**

Maelezo Na. 20 kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi cha mapato kilichokusanya lakini hakikupelekwa benki kama hasara tegemewa cha Sh. 62,467,000 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019, lakini kiasi hicho hakikuoneshwa kama matumizi kwenye taarifa ya utendaji wa fedha; hivyo, matumizi yaliyooneshwa kwenye taarifa ya ulinganifu kwa mwaka 2018/19 yalikuwa pungufu kwa Sh. 62,467,000.

e) **Limbikizo la faida /(hasara) lilioneshwa pungufu kwa Sh. 89,989,000**

Maelezo Na.22 kwenye taarifa za fedha (mali, mitambo na vifaa) yalionesha thamani ya Sh.2, 145,476,000 ya mali, mitambo na vifaa ukiondoa malimbikizo ya uchakavu ya mali na mitambo iliyohamishiwa RUWASA, hata hivyo marekebisho ya kiasi cha mali na mitambo hiyo yaliyofanyika kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji kilikuwa Sh. 2,235,465,000, hivyo kupelekea tofauti ambayo haikutolewa maelezo ya Sh. 89,989,000.

f) **Usuluhisho wa faida/(hasara) halisi na mtiririko halisi wa fedha kutoka kwenye shughuli za kawaida haukufanyika kwa ukamilifu**

Halmashauri iliandaa usuluhisho wa faida/(hasara) halisi na mtiririko halisi wa fedha kutoka kwenye shughuli za kawaida kwa mujibu wa matakwa ya Aya ya 28 na 29 ya IPSAS 2 pamoja na waraka Na. EG.3/102/05/03/000 wa tarehe 8 Mei 2020 kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali; lakini, ongezeko la fedha la Sh. 67,505,000 kwenye akaunti ya amana halikujumuishwa.

18. Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa

a) **Kiwango cha uchakavu wa mali, mitambo na vifaa kilioneshwa zaidi kwa Sh. 699,769,049**

Maelezo Na. 26 kwenye taarifa za fedha yameonesha kiasi cha uchakavu wa mali, mitambo na vifaa cha Sh. 1,045,699,858, wakati kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kilikuwa Sh. 1,745,468,907 hivyo kupelekea kiasi hicho kuripotiwa zaidi kwa Sh. 699,769,049.

b) **Kutofautiana kwa kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichotumika kwenye taarifa za fedha**

Maelezo Na.30 (CAPEX) na taarifa ya utendaji wa fedha ilionesha kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichotumika cha Sh. 762,755,151.75, hata hivyo, kiasi hicho kilitofautiana na Maelezo Na. 23 (kiasi cha ruzuku ya maendeleo ambacho hakikutumika) ambayo yalionesha kiasi kilichotumika kuwa ni Sh.975,045,007, na kupelekea tofauti ambayo haikuwa na maelezo ya Sh. 212,289,855.25, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi wa kiasi cha mapato kilichotokana na ruzuku ya maendeleo kilichooneshwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha na kiasi cha ruzuku ambayo haikutumika kilichooneshwa kwenye mizania ya hesabu.

c) **Limbikizo la faida lilioneshwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 484,830,928**

Taarifa ya mabadiliko ya mtaji ilionesha salio anzia la limbikizo la faida Sh. 19,918,927,759 kwa tarehe 1 Julai 2019; lakini salio hilo lilitofautiana na salio halisi lililooneshwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019 la kiasi cha Sh. 19,434,096,831; hivyo kupelekea tofauti ambayo haikutolewa maelezo ya Sh. 484,830,928; hivyo limbikizo la faida kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 lilikuwa zaidi kwa Sh. 484,830,928.

d) **Kushindwa kuthibitisha malipo yaliyooneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha Sh. 212,289,855**

Halmashauri ilionesha kiasi cha Sh. 994,169,674 kama malipo kwa ajili ya ununuzi wa mali, mitambo na vifaa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha; hata hivyo, ukaguzi wa maelezo Na. 30 ulibaini kuwa malipo yalikuwa ya Sh. 781,789,818.19 hivyo kupelekea tofauti ya Sh. 212,289,855, ambayo haikuwa na maelezo.

19. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni

a) **Kishindwa kujiridhisha na malipo ya vibarua wa kufanya usafi na kuzoa taka ngumu, Sh. 454,550,000**

Halmashauri ilifanya jumla ya malipo ya Sh. 454,550,000 kwa vibarua wa usafi na uzoaji taka bila ya kuwepo kwa uthibitisho wa kazi walizofanya kwa kuwa hakukuwa na mkataba ulioainisha majukumu na wajibu wa vibarua hao na wigo/ukubwa wa kazi waliyotakiwa kufanya, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na vigezo vilivyotumika kufanya malipo hayo.

b) **Malipo yaliyofanywa zaidi ya makubaliano ya mkataba Sh. 216,000,000**

Halmashauri ilifanya malipo kwa klabu ya mpira ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni (KMC-FC) ya jumla ya Sh. 432,000,000 kwa ajili ya ukusanyaji taka ngumu; hata hivyo, kiasi hicho kilikuwa kikubwa zaidi ya mkataba ulioingiwa wa Sh. 216,000,000; hivyo kupelekea malipo ya zaidi kwa Sh. 216,000,000.

c) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 314,005,000**

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 314,005,000 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, hivyo sikuweza kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo hayo.

d) **Kushindwa kujiridhisha na matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa Sh. 51,369,427**

Halmashauri ilinunua na kugawa mafuta yenye thamani ya Sh. 51,369,427 kwa magari ya Halmashauri na watu binafsi, lakini hakukuwa nyaraka muhimu kama vile daftari la kutunzia kumbukumbu za magari (logbooks), hati za kutolea/kugawia mafuta, leja za stoo, n.k. na hakukuwa na sababu zilizotolewa za kutumia mafuta ya Serikali kwenye magari ya watu binafsi.

e) **Bidhaa zilizolipiwa hazikuwa zimepokelewa na wala hazikutambuliwa kwenye taarifa za fedha, Sh. 48,620,725**

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh.59, 054,575 kwa ajili ya ununuzi wa bati kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa mpira, ambapo bati zenye thamani ya Sh. 48,620,725 hazikuwa zimepokelewa kufikia tarehe 30 Juni 2020 na pia malipo hayo hayakutambuliwa kwenye taarifa za fedha malipo mbele.

20. Halmashauri ya Wilaya ya Msalala

a) **Malipo ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa yaliyoripotiwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 139,099,458**

Taarifa ya mtiririko wa fedha ilionesha malipo ya Sh. 3,635,838,380 kwa mwaka 2019/20 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na bidhaa zinazotumiwa (supplies and consumables); uchambuzi wa maelezo Na. 15, 21 na 25 kwenye taarifa za fedha ulibaini kuwa kiasi kilichooneshwa kilikuwa zaidi kwa Sh. 139,099,458.

b) **Mapato yaliyokusanywa lakini hayakuwasilishwa Halmashauri hayakutambuliwa kwa usahihi kwenye taarifa za fedha, Sh. 73,947,146**

Maelezo Na. 19 kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi kilichotengwa kama hasara ya mbeleni kutokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki ya Sh. 73,947,146, lakini kiasi hicho hakikutolewa kwenye madai yaliyoripotiwa kwenye maelezo Na. 21; hivyo madai yaliripotiwa zaidi kwa Sh. 73,947,146.

c) **Ongezeko la mkopo halikutambuliwa kwenye taarifa za fedha, Sh. 484,612,153**

Maelezo Na. 28 kwenye taarifa za fedha yalibainisha ongezeko la mkopo la Sh. 484,612,153 kutoka Sh. 600,055,811 ulioripotiwa mwaka 2018/19 hadi Sh. 1,084,667,964 ulioripotiwa kwa mwaka 2019/20 kutokana na riba na adhabu kwa kushindwa kulipa mkopo kwa wakati bila ya kuonesha matumizi yaliyotokana na ongezeko hilo kwenye taarifa ya utendaji wa fedha.

d) **Mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 bila maelezo, Sh. 1,878,387,215**

Halmashauri ilifanya mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 kwenye taarifa za fedha za mwaka 2019/20 kutoka kwenye kiasi halisi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka 2018/19 ya jumla ya Sh. 1,878,387,215, lakini mabadiliko hayo hayakubainisha chimbuko na sababu zilizopelekea tofauti hiyo

e) **Kushindwa kujiridhisha na mapokezi ya fedha zinazohusiana na wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yaliyoripotiwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, Sh. 247,000,000**

Taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2020 ilionesha fedha iliyopokelewa kiasi cha Sh. 247,000,000 kwa ajili ya wanawake, vijana na watu ulemavu. Nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wa kiasi hicho kilichooneshwa kwa kuwa fedha za mfuko huo zinatokana na mchango wa Halmashauri kutoka kwenye

makusanyo yake ya ndani na pia hakukuwa na nyaraka muhimu za kuhalalisha kiasi hicho.

f) **Makosa kwenye usuluhisho wa faida/(hasara) halisi na mtiririko halisi wa fedha kutoka kwenye shughuli za kawaida**

Ukaguzi wa usuluhisho wa faida/(hasara) halisi na mtiririko halisi wa fedha kutoka kwenye shughuli za kawaida kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 ulibaini kuwa, kiasi kilichotumika kufanya marekebisho kwenye faida/(hasara) ili kufikia kwenye kiasi halisi cha fedha kutokana na shughuli za kawaida kwa mwaka 2019/20 na mwaka 2018/19 kilikuwa tofauti kwa kiasi kikubwa na kiasi nilichokikokotoa kutokana na maelezo yaliyopo kwenye taarifa za fedha (mabadiliko ya kiasi cha mali na madeni ya muda mfupi) ya mwaka na mwaka husika. Hivyo, nimeshindwa kujiridhisha usahihi wa usuluhisho huo.

g) **Mapato yaliyooneshwa pungufu ya ilivyostahili kwa Sh. 22,500,000**

Maelezo Na.38 (CAPEX) kwenye taarifa za fedha yalionesha mapokezi ya mashine hamsini za kukusanyia mapato kutoka Serikali kuu zenye thamani ya Sh. 22,500,000, lakini kiasi hicho hakikutambuliwa kama mapato kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kwa mujibu wa Aya ya 96 ya IPSAS 23, hivyo kupelekea jumla ya mapato yaliyooneshwa kuwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 22,500,000.

h) **Matumizi kutokana na mishahara na stahiki za watumishi yameoneshwa zaidi kwa Sh. 252,871,818**

Maelezo Na. 15 kwenye taarifa za fedha yamebainisha matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi yenye jumla ya Sh. 15,261,403,538 katika taarifa ya ulinganifu ya mwaka 2018/19. Hata hivyo, kiasi hiki kinakinzana na kiasi cha Sh. 15,514,275,356 kilichoripotiwa katika ukurasa wa 24 wa taarifa ya utendaji wa fedha, hivyo kupelekea matumizi hayo kuoneshwa zaidi kwa Sh. 252,871,818.

i) **Mgawanyo usio sahihi wa mkopo kati ya kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa muda mfupi na muda mrefu**

Ukaguzi wa Maelezo Na. 27 na 28 kwenye taarifa za fedha pamoja na jedwali la ukokotoaji wa marejesho ya mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania ulibaini kuwa, Halmashauri ilikopa kiasi cha Sh. 995,836,800 kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania tarehe 31 Desemba 2015 ukiwa na muda wa mwisho wa kulipa (kuiva) tarehe 31 Desemba

2020. Kufikia tarehe 30 Juni 2020, kiasi ambacho kilikuwa hakijalipwa (kikijumuisha riba na adhabu kwa kushindwa kulipa kwa wakati) kilikuwa Sh. 1,286,952,010 ambapo kiasi chote kilitakiwa kuoneshwa kama mkopo unaotakiwa kulipwa ndani ya miezi 12 baada ya mwaka wa fedha kuisha. Hata hivyo, Maelezo Na. 28 yalionesha kiasi cha Sh.1,084,667,964 kama kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa zaidi ya miezi kumi na mbili. Hii inapotosha watumiaji wa taarifa za fedha kuhusiana na kiasi cha mkopo kilichopitiliza muda wake wa kulipa.

j) **Gharama za mkopo zilizooneshwa kwa mwaka 2019/20 na mwaka 2018/19 hazikuwa sahihi**

Maelezo na. 19 kweye taarifa za fedha yameonesha gharama za mkopo ambazo zilikuwa hazijalipwa kwa mwaka 2019/20 za Sh. 202,284,046 na kwa mwaka 2018/19 za Sh.140, 800,893. Hata hivyo, ukaguzi wa jedwali la ukokotoaji marejesho ya mkopo huo ulibaini kuwa riba ya mkopo iliyotakiwa kulipwa kwa mwaka 2019/20 ni Sh. 80,084,582.15 wakati kwa mwaka 2018/19 kilipaswa kuwa Sh. 130,752,654.63 hivyo kupelekea kiasi cha riba kuripotiwa zaidi kwa Sh. 122,199,463.85 kwa mwaka 2019/20 na Sh. 10,048,238.37 kwa mwaka 2018/19.

k) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 66,973,550**

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 66,973,550 ambayo hayakuwa na nyaraka kama vile orodha iliyosainiwa ya walipwaji, hati za kupokelea bidhaa, hati za madai, ripoti ya ukaguzi na kukubali bidhaa, n.k. hivyo sikuweza kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo hayo.

21.Halmashauri ya Wilaya Hanang

a) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 18,053,550**

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 18,053,550 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, hivyo sikuweza kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo hayo.

b) **Kukosekana kwa hati za malipo za jumla ya Sh. 8,703,000**

Nimebaini kuwa, hati za malipo pamoja na nyaraka zake muhimu zenye jumla ya Sh. 8,703,000 ambazo malipo yake yalihusiana na ujenzi wa kituo cha afya cha Hirbadaw hazikuwepo kwenye mafaili husika na hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na uhalali wa malipo yaliyofanywa kupitia hati hizo.

c) **Bakaa ya fedha ya kufungia mwaka ilioneshwa zaidi kwa Sh. 13,539,063**

Maelezo Na.16 (Cash and Cash Equivalent) kwenye taarifa za fedha kwa mwaka 2018/19 yalijumuisha bakaa ya fedha ya Sh,13, 539,063, kwenye akaunti Halmashauri ya Sekta ya maji, hata hivyo, kiasi hicho kilikuwa kimeshahamishiwa kwenda akauti ya RUWASA kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanyika kwenye maelezo Na. 25; lakini marekebisho hayo hayakufanyika pia kwenye maelezo Na. 16, hivyo, bakaa ya fedha iliyooneshwa ilikuwa zaidi kwa Sh. 13,539,063.

d) **Mapato (non-exchange transactions) ambayo hayakuoneshwa kwenye taarifa za fedha, Sh. 112,760,000**

Maelezo Na. 32 kwenye taarifa za fedha (mali, mitambo na vifaa) yalijumuisha mapokezi ya msaada wa kompyuta na pikipiki zenye thamani Sh.112, 760,000, lakini kiasi hicho hakikutambuliwa kama mapato kwenye taarifa za fedha kwa mujibu wa IPSAS 23, hivyo, mapato yaliyooneshwa yalikuwa pungufu kwa kwa kiasi hicho cha Sh.112, 760,000.

e) **Matumizi yaliyotokana na mishahara na stahiki za watumishi yalioneshwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 23,904,866**

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilionesha malipo kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi ya Sh. 25,733,520,277; hata hivyo, malipo hayo yalikuwa yamefanyiwa marekebisho kwa kuongeza bakaa ya kufungia mwaka ya madai ya stahiki za watumishi ya Sh. 1,359,255,420 na kutoa bakaa anzia ya Sh. 1,161,132,291, ambapo ilitakiwa kupata kiasi cha matumizi cha Sh.25,709,615,411 badala ya Sh. 25,733,520,277 iliyoripotiwa hivyo kupelekea matumizi kuripotiwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 23,904,866

f) **Mapato yatokanayo na ada, adhabu na ushuru yalioneshwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 114,126,868**

Maelezo Na. 18 kwenye taarifa za fedha yalijumuisha mapato ambayo hayakuwa yamekusanywa yaliyotokana na ada, faini na adhabu ya Sh. 33,947,300, na maelezo Na.17 mapato yaliyotokana na ushuru ya kiasi cha Sh. 80,179,568; lakini hakukuwa na madai yaliyotambuliwa kwenye taarifa za fedha kutokana na kiasi hicho kilichooneshwa kama mapato.

g) **Matumizi yaliyooneshwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 106,268,388**

Maelezo Na. 28 kwenye taarifa za fedha yalionesha matumizi ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa ambayo hayakuwa yamelipwa ya Sh. 182,296,343 na maelezo Na. 29 yalionesha matumizi yasiyolipwa ya Sh.30,352,832 yaliyohusiana na ukarabati na matengenezo, ambayo yanafanya jumla ya matumizi kuwa Sh.212, 649,175. Hata hivyo, uchambuzi wa mwenendo wa madeni kati ya bakaa ya kuanza mwaka na ya kufunga mwaka kwa malipo ya mbele (prepayment) na vifaa vya stoo; nimebaini kuwa, kiasi sahihi cha matumizi ambayo hayakuwa yamelipwa kilikuwa Sh.318, 917,563 badala ya kiasi kilichooneshwa Sh. 212,649,175 hivyo kupelekea matumizi kuoneshwa pungufu kwa kiasi cha Sh.106, 268,388.

h) **Mapato yaliyokusanywa kwenye ngazi ya vijiji yalioneshwa zaidi kwa Sh.146,573,486**

Ukaguzi wa nyaraka za makusanyo ya mapato kwenye ngazi za vijiji pamoja na taarifa za fedha ulibaini kuwa, jumla ya mapato yaliyokusanywa kwenye ngazi hizo yalikuwa Sh.868,146,785, lakini maelezo Na.20 na taarifa ya utendaji wa fedha ilionesha jumla ya mapato ya vijiji ya Sh. 1,014,720,271 hivyo kupelekea mapato kuripotiwa zaidi kwa Sh. 146,573,486

i) **Kutotambua madeni yaliyotokana na fedha zilizowekwa kwenye akaunti ya amana kama dhamana ya utendaji, Sh. 102,000,000**

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 200, Halmashauri iliazima kiasi cha Sh.102, 000,000 kutoka kwenye akaunti ya amana (kilichokuwa kimewekwa na wakandarasi mbalimbali kama dhamana), kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kawaida za Halmashauri; hata hivyo kiasi hicho kilichoazimwa hakikuwa kimerejeshwa kufikia mwisho wa mwaka na wala kiasi hicho hakikutambuliwa kama madeni kwenye taarifa za fedha.

j) **Mapato yatokanayo na biashara (revenue from exchange) yalioneshwa pungufu kwa Sh. 90,486,330**

Maelezo Na. 19 kwenye taarifa za fedha yalionesha mapato yatokanayo na biashara ambayo hayakuwa yamekusanywa kiasi cha Sh. 308,237,638. Hata hivyo, upitiaji wa maelezo Na. 12 ulibaini kuwa, madai yanayotokana na mapato hayo yaliongezeka kutoka Sh. 36,940,100 yaliyooneshwa kwa mwaka 2018/19 hadi Sh. 435,664,068 yaliyooneshwa kwa mwaka 2019/20 hivyo kupelekea ongezeko la madai kwa mwaka 2019/20 kuwa Sh. 398,723,968 badala ya kiasi

kilichooneshwa cha Sh. 308,237,638; hivyo, mapato yalioneshwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 90,486,330.

k) **Mapungufu kwenye kiasi kilichooneshwa kama fedha zilizohamishiwa kwenda ngazi za chini Sh. 20,714,284**

Maelezo na. 14 kwenye taarifa za fedha (malipo ya mbele) yalijumuisha kiasi cha Sh.20, 714,284 kama malipo ya mbele kilchopelekwa kwenye ngazi za chini za Halmashauri, lakini menejimenti haikutoa maelezo ya chimbuko la malipo hayo ya mbele. Hata hivyo, nimebaini kuwa, kiasi hicho cha malipo ya mbele kwenye ngazi za chini hakikutambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020.

22.Halmashauri ya Wilaya ya Siha

a) **Marekebisho ya hati za madai yaliyofanyika bila ya kibali cha afisa masuuli, Sh. 624,153,964**

Nimebaini marekebisho ya hati za madai ya mapato (bili za mapato zilizofutwa) kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) ya jumla ya Sh. 624,153,964 lakini hakukuwa na ushahidi kuwa, marekebisho hayo yaliidhinishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri na hakukuwa na nyaraka za maandishi zilizohalaliisha marekebisho hayo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wa marekebisho hayo.

b) **Mafuta yaliyogawiwa lakini hayakuwa na nyaraka za matumizi ya mafuta hayo, Sh. 20,408,853**

Halmashauri ilinunua na kugawa mafuta yenye thamani ya Sh. 20,408,853 kwa ajili ya wakuu wa idara lakini hakukuwa na nyaraka zinazoonesha jinsi mafuta hayo yalivyotumika, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na matumizi ya mafuta hayo.

c) **Malipo yaliyofanywa bila ya kuwa na nyaraka muhimu, Sh. 111,584,100**

Nimebaini kuwa, hati za malipo zenye jumla ya Sh. 111,584,100 hazikuwa na nyaraka muhimu, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na uhalali wa malipo hayo.

d) **Kukosekana kwa hati za malipo za Sh. 59,273,255**

Hati za malipo pamoja na viambatisho vyake za jumla ya Sh. 59,273,255 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo nimeshindwa

kujiridhisha na uhalali na madhumuni ya malipo yaliyofanyika kupitia hati hizo.

e) **Kutokuonesha mali tarajiwa (contingent assets) kutokana na mapato yaliyokusanya lakini hayakupelekwa benki Sh. 112,539,000**

Maelezo Na. 18 kwenye taarifa za fedha yameonesha hasara iliyotokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki/hayakuwasilishwa Halmashauri ya Sh. 112,539,000, lakini kiasi hicho hakikuoneshwa kwenye maelezo kama mali tarajiwa (contingent assets) na hakukuwa na maelezo ya ziada kuhusiana na hatua zilizochukuliwa na Halmashauri kuhakikisha kiasi hicho kinawasilishwa.

23. Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi

a) **Madai ambayo hayakutambuliwa kwenye taarifa za fedha, Sh. 126,297,316**

Nimebaini mapato ya Sh. 126,297,316 ambayo yalikusanywa lakini hayakupelekwa benk/hayakuwasilishwa Halmashauri na wala hayakutambuliwa kwenye taarifa za fedha kama madai. Vilevile, Maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha yalionesha kupungua kwa thamani (kutambuliwa kama hasara tarajiwa) ya madai yaliyotokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki ya kiasi cha Sh. 70,363,784, lakini hakukuwa na maelezo yanayojitosheleza nkuhusiana nan a hatua zilizochukuliwa na Halmashauri ili kuhakikisha kiasi hicho kinapelekwa benki.

24. Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa

a) **Bakaa ya madai ambayo haikuwa na maelezo ya kuihalalisha, Sh. 181,326,000**

Maelezo Na. 18 kwenye taarifa za fedha yalionesha madai ya Sh. 181,326,000 yaliyotokana na kuazima fedha kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine kwa mwaka 2019/20 na Sh. 181,979,000 kwa mwaka 2018/19, lakini hakukuwa na maelezo juu ya chimbuko la madai hayo. Pia, Maelezo Na.18 yalionesha kiasi ambacho hakikutumika kwenye akaunti ya amana Sh. 8,010,000 kama madai kwa mwaka wa 2019/20 na Sh. 31,677,000 kwa mwaka 2018/19 lakini hakukuwa na ufafanuzi au taarifa juu ya chimbuko lake, hivyo sikuweza kuthibitisha uhalali na usahihi wa kiasi kilichooneshwa.

b) **Kutokuonesha mali tarajiwa (contingent assets) kutokana na mapato yaliyokusanya lakini hayakupelekwa benki Sh. 96,031,000**

Maelezo Na. 18 kwenye taarifa za fedha yameonesha hasara iliyotokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki/hayakuwasilishwa Halmashauri ya Sh. 96,031,000 lakini kiasi hicho hakikuoneshwa kwenye maelezo kama mali tarajiwa (contingent assets) na hakukuwa na maelezo ya ziada kuhusiana na hatua zilizochukuliwa na Halmashauri kuhakikisha kiasi hicho kinawasilishwa

c) **Mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 bila maelezo, Sh. 2,686,035,000**

Halmashauri ilifanya mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 kwenye taarifa za fedha za mwaka 2019/20 kutoka kwenye kiasi halisi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka 2018/19 ya jumla ya Sh. 2,686,035,000, lakini mabadiliko hayo hayakubainisha chimbuko na sababu zilizopelekea ambapo, si tu kinyume na matakwa ya aya ya 54 ya IPSAS 3 bali pia nimeshidwa kujiridhisha na uhalali wa mabadiliko hayo

d) **kukosekana kwa maelezo ya ziada kwa fedha zilizokopeshwa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu Sh 411,723,000 na marejesho ya mkopo ya Sh 72,070,000 kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha**

Taarifa ya mtiririko wa fedha iliripoti mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ya Sh 411,723,000 na mkopo iliyorejeshwa ya Sh 72,070,000, lakini fedha hizo hazikuwa na maelezo yoyote ya ziada ili kuthibitisha usahihi wake.

e) **Thamani ya mali, mitambo na vifaa vilioneshwa zaidi kwa Sh. 308,500,000**

Maelezo Na. 27 kwenye taarifa za fedha (CAPEX) yalionesha jumla ya matumizi ya fedha za maendeleo ya Sh 2,191,970,000 ambayo yalijumuisha malipo ya mbele kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi vya Sh 930,685,000; hivyo kiasi kilichopaswa kuripotiwa kama thamani ya mali ni Sh 1,261,284,000, lakini Maelezo Na. 23 (mali, mitambo na vifaa) yalionesha thamani ya mali iliyoongezwa ya Sh 1,569,784,000 na kupelekea ongezeko la thamani ya mali kwa Sh. 308,500,000.

f) **Thamani ya mali zilizohamishiwa RUWASA zilioneshwa pungufu kwa Sh 308,500,000**

Maelezo Na. 23 kwenye taarifa za fedha yalionesha uhamisho wa mali, mitambo na vifaa vyenye jumla ya thamani ya Sh 4,611,500,000, hata hivyo kiasi kilichopunguzwa kwenye malimbikizo ya faida/ (hasara) kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji ilikuwa Sh 4,303,000,000, hivyo kupelekea thamani ya mali iliyohamishwa kuwa pungufu hivyo kupelekea malimbikizo ya yaida yaliyoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh.308, 500,000.

g) **Usuluhisho wa taarifa ya mtiririko wa fedha haukutayarishwa kwa usahihi**

Halmashauri ilijumuisha taarifa ya usuluhisho kati ya faida / (hasara) halisi na kiasi halisi cha fedha kutokana na shughuli za kawaida, lakini taarifa hiyo ya usuluhisho ilikuwa na mapungufu yafuatayo;

i. Ilijumuisha ongezeko la malipo ya awali kwa mkandarasi kiasi cha Sh.570,907,000, wakati malipo hayo hayakuathiri mtiririko wa fedha kutokana na shughuli kawaida, hivyo hakikupaswa kujumuishwa wakati wa uandaaji wa taarifa ya usuluhisho;

ii. Ilijumuisha mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kiasi cha wa Sh 291,171,000 pamoja na dhamana ya Sh 279,879,000 ambazo hazikutakiwa kuwa sehemu ya shughuli za kawaida.

h) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh 83,833,127**

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh 83,833,127 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, hivyo sikuweza kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo hayo.

25. Halmashauri ya Wilaya ya Geita

a) **Bakaa ya fedha kwenye akaunti ya amana ilioneshwa pungufu kwa Sh. 214,918,283**

Maelezo Na. 43 kwenye taarifa za fedha na taarifa ya mtiririko wa fedha iliripoti jumla ya mapokezi kwenye akaunti ya amana ya Sh. 1,163,526,000 na jumla ya malipo kutoka kwenye akaunt hiyo ya Sh. 719,361,118. Kulikuwa pia na bakaa iliyoanza mwaka ya Sh. 449,046,863 kufikia tarehe 1 Julai 2019 ambayo ilipaswa kupelekea

jumla ya bakaa ya kufunga mwaka kuwa Sh. 893,211,745 kufikia tarehe 30 Juni 2020; Lakini, Halmashauri iliripoti bakaa la kufungia mwaka ya Sh. 754,718,862 hivyo kupelekea bakaa kuwa pungufu kwa Sh. 138,492,883. Pia, nimebaini kuwa, maelezo Na. 9 kwenye taarifa za fedha (pesa taslimu) yaliripoti salio la kufunga mwaka kwenye akaunti ya fedha ya amana la Sh. 525,472,000 kufikia tarehe 30 Juni 2019 ambalo lilipaswa kuwa bakaa ya kuanza mwaka tarehe 1 Julai 2019 badala ya Sh. 449,046,863 iliripotiwa kwenye maelezo Na. 43 na kupelekea kuripotiwa pungufu kwa Sh. 76,425,137. Hii ilisababisha bakaa hiyo kuoneshwa pungufu kwa jumla ya Sh. 214,918,020.

b) **Kutokupunguza thamani ya magari yaliyouzwa kwenye jedwali la mali za kudumu na kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji, Sh. 14,788,000**

Nimebaini kuwa, Halmashauri iliuza magari mawili yenye thamani ya Sh. 14,788,000 lakini thamani ya magari hayo haikutolewa kwenye maelezo Na. 13 (mali, mitambo na vifaa) na wala haikutolewa kwenye malimbikizo ya faida kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji, Hivyo kupelekea mali za kudumu na malimbikizo ya faida kuoneshwa kwa thamani zaidi kwa Sh. 14,788,000.

c) **Malimbikizo ya faida yaliripotiwa pungufu kwa Sh. 1,196,460,096 kwa mwaka 2018/19**

Maelezo Na. 42 kwenye taarifa za fedha yalionesha mabadiliko ya kiasi cha malimbikizo ya faida kutoka Sh. 9,455,293,785 kilichooneshwa kwa mwaka 2018/19 hadi Sh. 50,507,997,096 kilichooneshwa kama ulinganisho kwa mwaka 2019/20, hata hivyo, Halmashauri ilionesha kiasi cha Sh. 49,311,537,000 kwenye taarifa za fedha badala ya Sh. 50,507,997,095.70 kama ilivyooneshwa kwenye maelezo Na.42 na hivyo kupelekea malimbikizo ya faida kuoneshwa pungufu kwa Sh. 1,196,460,096.

d) **Mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 bila maelezo, Sh. 13,858,644,000**

Halmashauri ilifanya mabadiliko ya kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 kwenye taarifa za fedha za mwaka 2019/20 kutoka kwenye kiasi halisi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka 2018/19 ya jumla ya Sh. 13,858,644,000, lakini mabadiliko hayo hayakubainisha chimbuko na sababu zilizopelekea

ambapo, si tu kinyume na matakwa ya aya ya 54 ya IPSAS 3 bali pia nimeshidwa kujiridhisha na uhalali wa mabadiliko hayo.

e) **Kutokuonesha mali tarajiwa (contingent assets) kutokana na mapato yaliyokusanya lakini hayakupelekwa benki Sh. 32,097,000**

Maelezo Na. 18 kwenye taarifa za fedha yameonesha hasara iliyotokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki/hayakuwasilishwa Halmashauri ya Sh. 32,097,000 lakini kiasi hicho hakikuoneshwa kwenye maelezo kama mali tarajiwa (contingent assets) na hakukuwa na maelezo ya ziada kuhusiana na hatua zilizochukuliwa na Halmashauri kuhakikisha kiasi hicho kinawasilishwa.

26. Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe

a) **Kiasi cha vifaa na bidhaa zinazotumiwa kwa mwaka 2018/19 kilioneshwa pungufu kwa Sh.165,704,000**

Nimebaini kuwa, kwa mwaka 2018/19, Halmashauri haikujumuisha kwenye kiasi cha vifaa na vifaa na bidhaa zinazotumiwa bakaa ya kuanza mwaka ya vifaa vya stoo vya Sh. 165,704,000 hivyo kupelekea matumizi yaliyooneshwa kama vifaa na vifaa na bidhaa zinazotumiwa kuwa pungufu kwa kiasi hicho.

b) **Kiasi cha ulinganisho cha mishahara na stahiki za watumishi kilioneshwa pungufu kwa Sh.2,225,480,000**

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, halmashauri iliripoti kiasi cha ulinganisho kwa mishahara na stahiki za watumishi kwa Sh. 15,017,026,000 wakati kiasi kilichohitakiwa kuripotiwa kama ulinganisho kilikuwa Sh. 17,242,506,000; kwa sababu ya kutorekebishwa na gharama za madeni ya stahiki za watumishi ya sh. 2,225,480,000, na hivyo kupelekea kiasi cha matumizi hayo kilichoripotiwa kuwa pungufu kwa Sh. 2,225,480,000.

c) **Malipo ya mbele yaliyofanywa kwenda Bohari ya Madawa yalioneshwa zaidi kwa Sh. 28,818,982 na madeni ya Bohari hiyo yalioneshwa pungufu kwa Sh. 17,546,524**

Maelezo Na. 17 kwenye taarifa za fedha yaliripoti madai kutoka Bohari ya madawa ya Sh. 23,072,969.12. Pia, Halmashauri ililipa malipo ya mbele ya Sh. 14,455,748.79 Bohari ya madawa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na kufanya jumla ya madai na malipo ya

mbele kuwa Sh. 37,528,717.91 kufikia tarehe 30 Juni 2020. Lakini, ukaguzi wa taarifa ya bakaa ya madai kutoka kwenye vituo vya afya vya Halmashauri ulionesha kuwa, jumla ya salio la madai na malipo ya mbele kwa MSD ilikuwa Sh. 8,709,736.08 kufikia tarehe 30 Juni 2020; hivyo madai na malipo ya mbele yalizidishwa kwa Sh. 28,818,981.83.

Pia, maelezo Na. 21 kwenye taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 yaliripoti bakaa sifuri kuhusiana na matumizi ambayo hayakuwa yamelipwa bohari ya madawa. Lakini, taarifa ya baka ya madeni ya vituo vya afya vya Halmashauri ilionesha bakaa la jumla ya Sh. 17,546,524.39 kufikia 30 Juni 2020; hivyo salio lililoripotiwa la madeni lilikuwa pungufu kwa kiasi hicho.

d) Malipo kuhusiana na vifaa na bidhaa zinazotumiwa yalioneshwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 8,836,788.31

Maelezo Na. 14 kwenye taarifa za fedha na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020 yaliripoti malipo ya pesa ya Sh. 2,652,051,717.99 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na bidhaa zinazotumiwa. Hata hivyo, ukokotoaji wangu uliozingatia ujumuishaji wa bakaa ya malipo ya mbele na bakaa ya madeni ya Bohari ya Madawa kufikia tarehe 30 Juni 2020 ilipelekea kupata jumla ya malipo ya Sh. 2,643,214,929.68, hivyo kiasi kilichoripotiwa kilizidishwa kwa Sh. 8,836,788.31.

e) Marejesho ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu hayakutambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, Sh. 13,752,000

Ukaguzi wa maelezo Na. 17 na 25 kwenye taarifa za fedha pamoja na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 ulibaini kuwa, kwa mwaka 2019/20, Halmashauri ilitoa mikopo ya Sh. 84,248,400 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Hakukuwa na bakaa ya mikopo ya kuanza mwaka na halmashauri iliripoti bakaa ya kufunga mwaka ya madai ya mikopo hiyo ya Sh. 70,496,400 kufikia tarehe 30 Juni 2020, ikimaanisha kuwa kulikuwa na urejeshwaji wa Sh. 13,752,000.

Hata hivyo, kiasi kilichorejeshwa cha Sh. 13,752,000 hakijaoneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kinyume na aya ya 25 (f) ya IPSAS 2, ambayo inataka mapokezi ya fedha kutokana na marejesho

ya mikopo itambuliwe kwenye sehemu ya mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji.

f) Ongezeko la masurufu halikutambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha Sh. 7,550,000

Ukaguzi wa maelezo Na. 17 kwenye taarifa za fedha ulibaini kuwa, masurufu yaliyotolewa kwa watumishi yaliongezeka kwa kiasi cha Sh. 7,550,000 kutoka Sh. 855,000 kilichoripotiwa kufikia tarehe 30 Juni 2019 hadi Sh. 8,405,000 kufikia tarehe 30 Juni, 2020. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilicholipwa kutokana na ongezeko hilo hakikutambuliwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha.

g) Kukosekana kwa hati za malipo za jumla ya Sh. 38,607,100

Nimebaini kuwa, hati za malipo pamoja na nyaraka zake muhimu zenye jumla ya Sh. 38,607,100 hazikuwepo kwenye mafaili husika na hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo yaliyofanywa kupitia hati hizo.

h) Madeni yaliyooneshwa bila ya kuwa na nyaraka muhimu za kuyahalalisha Sh. 28,762,780

Maelezo Na.20 kwenye taarifa za fedha yalionesha wazabuni wanaodai kiasi cha Sh. 28,762,780 lakini hawakuwa na nyaraka muhimu kama vile hati za kuagizia vifaa na hati za madai ili kuhalalisha madeni hayo.

27. Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe

a) Malipo ya mishahara na stahiki za watumishi yalioneshwa pungufu kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa Sh. 225,078,826

Halmashauri ilionesha malipo ya Sh.25, 271,817,474 ikiwa ni mishahara na stahiki za watumishi kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020; hata hivyo kiasi hicho hakikujumuisha mabadiliko ya madeni yenye jumla ya Sh. 225,078,826 kama yalivyoahinishwa kwenye maelezo Na. 38.

b) Malipo ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa yaliripotiwa zaidi kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa Sh. 36,206,417

Halmashauri ililiripoti malipo ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa (supplies and consumables) ya Sh. 5,048,444,674 kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020, lakini kiasi hicho, kilijumuisha kiasi cha Sh. 36,206,417 kutokana na makosa

kwenye ukokotoaji wa mwenendo wa madai na malipo ya mbele (maelezo Na. 25) na madeni (maelezo Na.35) kati ya bakaa ya kuanza mwaka na bakaa ya kufunga mwaka.

c) **Kutojiridhisha na kiasi cha madai ya Sh. 256,562,603 kwa mwaka 2019/20 na Sh. 517,282,107 kwa mwaka 2018/19**

Maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha (madai na malipo ya mbele) yalijumuisha salio la Sh. 256,562,603 kama madai kutokana na fedha zilizoazimwa kutoka akaunti ya amana kufikia tarehe 30 Juni 2020 na Sh. 517,282,107 kwa mwaka 2018/19. Hata hivyo, hakukuwa na ufafanuzi uliotolewa juu ya kiasi hicho cha fedha, hivyo sikuweza kupata uhalali wa kiasi kilichoripotiwa kwa miaka hiyo.

d) **Uhamishaji usio sahihi wa kiasi cha Sh. 14,414,510 kutoka mikopo ya muda mrefu kwenda kwa madai ya stahiki za mfanyakazi**

Nimebaini kuwa, katika mwaka fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilihamisha kiasi cha Sh. 14,414,510 cha mikopo ya muda mrefu na kukionesha kwenye madeni ya stahiki za mfanyakazi bila kutoa maelezo au sababu, hivyo sikuweza kujiridhisha na usahihi wa muhamala huo.

e) **Kiasi cha masurufu ambacho hakikutolewa wakati wa ukokotoaji wa malipo yaliyooneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha Sh. 15,178,590**

Maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha (Madai na malipo ya mbele) yalionesha kupungua kwa masurufu ya Sh. 15,178,590 kutoka Sh.26,886,840 iliyoripotiwa kufikia tarehe 30 Juni, 2019 hadi Sh. 11,708,250 iliripotiwa kufikia tarehe 30 Juni, 2020. Hata hivyo, kiasi hicho kilichopungua kilichokuwa kimeoneshwa kama matumizi hakikutolewa ili kupata malipo halisi ya kuonesha kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha.

f) **Usuluhisho wa taarifa ya mtiririko wa fedha haukuandaliwa kwa usahihi**

- Halmashauri ilijumuisha taarifa ya usuluhisho kati ya faida / (nakisi) na mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kawaida, lakini taarifa ya usuluhisho ilikuwa na mapungufu yafuatayo;
- Kupungua kwa madeni ya stahiki za mfanyakazi kiasi cha Sh.260,639,630 hayakujumuishwa katika usuluhishi;

- Madeni yaliyotokana na shughuli za kawaida yalipungua kwa Sh.691,324,825, lakini Halmmashauri ililiripoti kupungua kwa Sh. 185,387,019;
- Madai yaliyotokana na shughuli za kawaida yalipungua kwa Sh. 302,432,471 lakini Halmashauri ililiripoti kupungua kwa Sh. 646,695,522;
- Ongezeko la bakaa kwenye akaunti ya amana la Sh. 721, 096,421 halikujumuishwa kwenye taarifa ya usuluhushi.
- Hasara iliyotengwa (provision for loss) ya Sh. 216,050,248 kutokana na kiasi cha mapato kilichokusanywa lakini hakikuwasilishwa Halmashauri haikujumuishwa kwenye taarifa ya usuluhisho.

28. Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu

a) Thamani ya Ardhi isiyojumuishwa katika taarifa za kifedha

Nimebaini kuwa, Halmashauri ina takribani viwanja 200 ambavyo vina majengo lakini viwanja hivyo havijafanyiwa tathmini ilii vitambuliwe kwenye taarifa za fedha kwa mujibu wa matakwa ya Aya ya 27 na 28 ya IPSAS 17.

b) Michango ya jamii isiyo ya fedha ambayo haikujumuishwa kwenye taarifa za fedha

Ukaguzi wa hati za malipo na ziara iliyofanywa kwenye maeneo mbalimbali ambapo miradi mbalimbali ilikutekelezwa, nimebaini kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020, Halmashauri ilitoa kiasi cha Sh. 253,822,412 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa majengo ambayo yalianzishwa na wananchi ikiwepo ardhi iliyotolewa na wananchi. Hata hivyo, Halmashauri haikutathmini na kutambua thamani ya michango hiyo kwenye taarifa za fedha kinyume na matakwa ya Aya 96 na 97 ya IPSAS 23.

c) Fedha za ushuru wa mapato ya ndani zilizopokelewa zilioneshwa pungufu kwa Sh. 46,718,500

Maelezo Na. 9 kwenye taarifa za fedha yalionesha jumla ya makusanyo katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kuwa ni Sh. 1,221,294,879.86; hata hivyo, kiasi hicho kilikokotolewa kimakosa kwani jumla ya mapato yaliyoripotiwa ya Sh. 1,279,992,379.86 yalitakiwa yaongezwe kwa bakaa ya kuanza mwaka ya madai yatokanayo na ushuru la Sh.58,697,500 na kupunguza na bakaa la mwisho wa mwaka la Sh.70,676,500 hivyo kupelekea makusanyo ya

jumla ya Sh. 1,268,013,379.86 badala ya kiasi kilichoripotiwa cha Sh.1,221,294,879.86; hivyo kupelekea mapato hayo kuoneshwa pungufu kwa Sh. 46,718,500

d) **Kiasi cha ruzuku ya kawaida kilichokuwa hakijatumika kilioneshwa zaidi kwa Sh. 21,948,859.03**
Maelezo Na. 11 kwenye taarifa za fedha yalionesha bakaa ya ruzuku ya kawaida kufikia tarehe 30 Juni 200 la Sh. 1,186,245,220.37; hata hivyo, kiasi cha bakaa kilichooneshwa kwenye taarifa ya mizania kilikuwa Sh.1,208,194,079.40; hivyo kupelekea bakaa hilo kuoneshwa zaidi kwa kiasi cha Sh.21,948,859.03

e) **Kiasi cha ruzuku ya shughuli za kawaida kilichopokelewa kiloneshwa zaidi kwa Sh. 12,418,491.69 kwa mwaka 2019/20 na Sh.318,966,026 kwa mwaka 2018/19**
Maelezo Na. 11 kwenye taarifa za fedha na taarifa ya mtiririko wa fedha ilionesha jumla ya kiasi cha ruzuku ya kawaida kilichopokelew kuwa ni Sh. 17,254,774,303.63 kwa mwaka 2019/20 na Sh. 19,206,294,427.05 kwa mwaka 2018/19. Hata hivyo kiasi hicho kilijumuisha mapokezi ya fedha vifaa vya matibabu kutoka Bohari ya Madawa vya Sh. 12,418,491.69 kwa mwaka 2019/20 na Sh. 318,966,026 kwa mwaka 2018/19; hivyo, kiasi kilichopokelewa kiliripotiwa zaidi kutoka na vifaa vya matibabu vilivyojumuishwa kwa miaka husika.

f) **Kiasi cha madeni kiliripotiwa kimakosa kwa mwaka 2018/19 kwa Sh. 85,344,504**
Maelezo Na. 27 kwenye taarifa za fedha yalijumuisha madeni yanayohusiana mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ya Sh. 85,344,504 kwa mwaka 2018/19. Madeni hayo hayakustahili kuonekana kwenye taarifa za fedha kwa sababu, madeni hayo yalipaswa kufutwa na madai yaliyotambuliwa kwenye taarifa za fedha za mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wakati wa kuandaa taarifa jumuifu za fedha za Halmashauri.

g) **Kiasi cha malipo ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa kiliripotiwa na makosa**
Maelezo Na. 18 kwenye taarifa za fedha haikuandaliwa kwa usahihi ili kupata kiasi sahihi cha malipo kilichooneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha. Matumizi ya jumla ya Sh. 2,232,089,577.27

yalirekebishwa kwa kuongeza bakaa ya kuanza mwaka ya madeni ya Sh. 677,665,466 wakati kiasi cha kilichotakiwa kujumuishwa ni Sh. 412,076,114.95 (kama ilivyooneshwa kwenye Maleleo Na. 27) na kwa kupunguza bakaa ya mwisho wa mwaka ya madeni ya Sh. 513,635,153.25 wakati kiasi kilichopaswa kurepotiwa ni Sh. 329,238,270 (kama ilivyooneshwa kwenye Maelezo Na. 27). Aidha Maelezo yalijumuisha mapokezi ya vifaa tiba kutoka MSD vya Sh. 258,078,929 ambayo havikuripotiwa sehemu nyingine yeyote kwenye taarifa za fedha; hivyo kiasi cha fedha kilichoripotiwa kwa mwaka wa 2020 kilikuwa pungufu kwa Sh. 156,573,415.88

Vilevile, kwa mwaka 2018/19, matumizi ya Sh. 3,534,028,080.02 yalifanyiwa marekebisho kwa kuongeza bakaa ya madeni iliyoanza mwaka ya Sh. 838,268,260.86 wakati kiasi kilichopaswa kutumika (kama ilivyooneshwa kwenye Maelezo Na. 27) ni Sh. 568,858,916.10 na kupunguza bakaa ya madeni iliyofungia mwaka ya Sh. 677,665,466.79 badala ya Sh. 412,076,114.95 wakati (kama ilivyooneshwa kwenye Maelezo Na. 27) hivyo kupelekea kiasi kilichooneshwa kuwa pungufu kwa Sh. 437,094,475.39

Licha ya mapungufu yaliyobainika, Maelezo Na. 18 iliripoti jumla ya malipo ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa kiasi cha Sh. 3,253,716,405.78 wakati kiasi kilichoripotiwa katika taarifa za fedha ni Sh. 3,414,319,199.85 hivyo kupelekea tofauti ambayo haikutolewa maelezo ya Sh. 160,602,794.07

h) Kiasi cha matumizi yaliyotokana na vifaa na bidhaa zinazotumiwa kilichooneshwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kilikuwa na makosa

Maelezo Na. 18 kwenye taarifa za fedha yalionesha matumizi ya Sh. 3,414,319,199 ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa kwa mwaka 2018/19; lakini, kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kilikuwa Sh.3, 255,916,405 hivyo kupelekea matumizi yaliyooneshwa kuwa pungufu kwa Sh. 158,402,793.05.

i) Kutofanyika kwa marekebisho kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji kutokana na mauzo/ uhamishaji wa mali, mitambo na vifaa

Kwa mwaka 2018/19 Halmashauri ilihamisha/kuuza mali zilizokuwa na thamani ya Sh. 1,526,379,626, lakini Halmashauri haikufanya marekebisho (kiasi hicho hakikutolewa kwenye malimbikizo ya

faida); hivyo kupelekea kiasi cha limbikizo la faida lililooneshwa kuwa zaidi kwa Sh.1, 526,379,626.12.

j) Bakaa ya fedha iliripotiwa pungufu kwa mwaka 2018/19 kwa Sh. 74,225,607

Nimebaini makosa ya ujumlishaji kwenye maelezo Na. 22, kwani bakaa ya fedha kwa mwaka 2018/19 iliripoti kwa kiasi cha Sh. 1,605,236,651.24 wakati kiasi sahihi kilichopaswa kuripotiwa ni Sh. 1,679,462,258.24 hivyo kusabbabisha upungufu wa bakaa ya fedha kiasi cha Sh. 74,225,607.

k) Kiasi cha ruzuku na malipo mengine yaliyohamishwa kilioneshwa zaidi kwa Sh. 1,249,399,069 kwa mwaka 2018/19

Maelezo Na. 20 kwenye taarifa za fedha yalionesha jumla ya ruzuku na malipo mengine ya kiasi cha Sh. 1,731,283,994.52 kwa mwaka 2018/19, hata hivyo, kiasi hicho kinatofautiana na kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa mwaka jana kiasi cha Sh. 481,884,925; hivyo kupelekea tofauti isiyoelezeka (kiasi kilichoripotiwa kuwa zaidi) kwa Sh. 1,249,399,069.

l) Kiasi kilichotengwa kama hasara tarajiwa hakikutambuliwa sawasawa Sh. 70,676,500

Maelezo Na. 35 kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi kilichotengwa kama hasara tarajiwa kutokana na kiasi cha makusanyo ya ushuru wa ndani ambacho hakikupelekwa benki/hakikuwasilishwa Halmashauri cha Sh. 70,676,500, hata hivyo, kiasi hicho hakikupunguzwa kwenye madai yaliyoripotiwa kwenye Maelezo Na. 24 na walahakikutolewa kama matumizi kqwenye taarifa ya utendaji wa fedha.

Aidha, maelezo kwenye taarifa za fedha kuhusiana na hasara hiyo iliyotengwa hayakuwa yanajitosheleza ili kujiridhisha na hatua zilkizochukuliwa au zitakazochukuliwa na Halmashauri ili kuhakikisha kiasi hicho kinapokelewa.

m) Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 47,310,856

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 47,310,856 ambayo hayakuwa na nyaraka kama vile orodha iliyosainiwa ya walipwaji, hati za kupokelea bidhaa, hati za madai, ripoti ya ukaguzi na kukubali

bidhaa, n.k. hivyo sikuweza kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo hayo.

29. Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga

a) **Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 32,846,325**
Halmashauri ilifanya jula ya malipo ya Sh. 32,846,325 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, hivyo sikuweza kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo hayo.

b) **Kukosekana kwa hati za malipo za jumla ya Sh. 16,859,150**
Nimebaini kuwa, hati za malipo pamoja na nyaraka zake muhimu zenye jumla ya Sh. 16,859,150 hazikuwepo kwenye mafaili husika na hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo yaliyofanywa kupitia hati hizo.

c) **Madeni yaliyooneshwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 88,866,713**
Maelezo Na. 31 kwenye taarifa za fedha yalionesha madeni kutokana na fedha zilizowekwa kwenye akaunti ya amana ya Sh. 88,866,713; hata hivyo, hakukuwa na maelezo na nyaraka zilizohalalisha madeni hayo.

d) **Hasara iliyotokana na uuzwaji wa mali, mitambo na vifaa iliripotiwa zaidi kwa Sh.126,155,986**
Halmashauri ilihamisha mali, mitambo na vifaa kwenda RUWASA. Kwa mujibu wa Maelezo Na. 34 kwenye taarifa za fedha, thamani ya mali na mitambo hiyo iliyohamishwa ilikuwa Sh. 7,307,814,955 wakati thamani iliyooneshwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 ilikuwa Sh. 7,433,970,941 na hivyo kupelekea hasara iliyoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh. 126,155,986.

30. Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru

a) **Marekebisho ya hati za madai yaliyofanyika bila ya kuwa na nyaraka toshelezi, Sh. 1,232,598,827**
Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilifanya marekebisho ya hati za madai ya mapato (ilifuta bili za mapato) kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) ya jumla ya Sh. 1,232,598,827, lakini marekebisho hayo hayakuwa na nyaraka muhimu kama vile hati zilizoidhinishwa za kufanya marekebisho (journal vouchers) pamoja na nyaraka nyingine za kuhalalisha

marekebisho hayo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wa marekebisho hayo.

b) Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 24,296,173

Maelezo Na. 17 na 20 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 24,296,173 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

31. Halmashauri ya Wilaya ya Bahi

a) Kiasi cha ruzuku ya maendeleo ambacho hakikutumika kilioneshwa zaidi kwa Sh. 27,068,000

Maelezo Na.14 kwenye taarifa za fedha (ruzuku ya kawaida) yalijumuisha mapokezi ya Sh. 27,068,000 kama ruzuku ya kawaida kuhusiana na wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; hata hivyo, kiasi hicho hakikuwa sehemu ya ruzuku kutoka Serikali kuu, bali kilikuwa ni mchango wa Halmashauri kutoka kwenye makusanyo ya mapato ya ndani kwenda kwenye mfuko wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

b) Ruzuku iliyopokelewa kutoka Serikali kuu ilioneshwa pungufu kwa Sh.538,406,479

Nimebaini kuwa, Halmashauri ilipokea kiasi cha Sh. 309,575,933 kwa ajili ya kuwezesha shughuli za uchaguzi wa serikali za mitaa, lakini kiasi hicho hakikuoneshwa kama sehemu ya ruzuku iliyopokelewa kwenye maelezo Na. 14, hivyo ruzuku ya kawaida ilioneshwa pungufu kwa Sh. 309,575,933. Pia, Halmashauri ilipokea Sh. 300,000,000 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, ambapo Halmashauri ilionesha mapokezi ya Sh.71, 169,454 tu badala ya Sh. 300,000,000 na kupelekea pungufu ya Sh. 228,830,546. Hivyo ruzuku iliyopokelewa ilioneshwa pungufu kwenye taarifa ya fedha kwa jumla ya Sh. 538,406,479.

c) Kukosekana kwa hati za malipo na malipo ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi Sh. 54,481,806

Halmashauri ilifanya malipo ya jumla ya Sh. 22,709,606, lakini hayakuwa na nyaraka toshelezi. Pia, hati za malipo pamoja na

nyaraka zake muhimu zenye jumla ya Sh. 31,772,200 hazikuwepo kwenye mafaili husika na hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo ya jumla ya Sh. 54,481,806 yaliyofanywa kupitia hati hizo.

d) Kutokutenga hasara ya mbeleni kutokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki, Sh. 364,107,100

Maelezo Na. 27 kwenye taarifa za fedha yalionesha madai ya jumla ya Sh. 364,107,100 yaliyotokana na mapato yaliyokusanywa na watumishi wa Halmashauri pamoja na mawakala wa ukusanyaji mapato kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato papo kwa papo lakini hayakupelekwa benki/kuwasilishwa Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri haikutenga hasara inayoweza kujitokeza mbeleni kutokana na kiasi hicho kutowasilishwa, hivyo kupelekea madai na faida iliyoripotiwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kuwa zaidi kwa Sh. 364,107,100.

32. Halmashauri ya Mji wa Kondoa

a) Malipo ya mishahara na stahiki za watumishi yalioneshwa zaidi kwa Sh. 1,245,198,397

Maelezo Na. 33 kwenye tarifa za fedha na taarifa ya mtiririko wa fedha ilionesha malipo ya mishahara na stahiki za watumishi ya Sh. 10,438,765,149; hata hivyo, ukokotoaji wangu kwa kutumia maelezo yaliyopo kwenye taarifa za fedha nimebaini kuwa kiasi sahihi kilichotakiwa kuoneshwa ni Sh. 9,193,566,752 badala ya kiasi kilichooneshwa cha Sh. 10,438,765,149; hivyo kupelekea malipo hayo kuoneshwa zaidi kwa Sh. 1,245,198,398.

33. Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa

a) Malipo ya mishahara na stahiki za watumishi yalioneshwa zaidi kwa Sh. 650,786,971

Maelezo Na.15A kwenye taarifa za fedha yalionesha jumla ya malipo ya mishahara na stahiki za watumishi ya Sh. 20,176,881,280 kwa mwaka 2018/19, lakini kiasi cha malipo ya mishahara kilichooneshwa kwenye taarifa ya mtiriko wa fedha kilikuwa Sh. 20,827,668,251 hivyo kupelekea malipo yaliyooneshwa kuwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 650,786,971.

b) **Malipo kwa watoa huduma ambayo hayakuwa na maelezo (Disclosure Note), Sh. 1,122,836,308**
Taarifa ya mtiririko wa fedha ilionesha kiasi cha Sh. 1,122,836,308 kama malipo kwa watoa huduma kwa mwaka 2019/20; hata hivyo, taarifa hiyo ilionesha kuwa maelezo yake zaidi yanapatikana kwenye Maelezo Na.15 na 16; maelezo hayo (noti hizo) hazikuwa kwenye taarifa za fedha, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi wa malipo hayo.

c) **Malipo ya gharama za matengenezo yalioneshwa pungufu kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha**
Malelezo Na.17B kwenye taarifa za fedha yalionesha jumla ya malipo ya gharama za matengenezo ya Sh. 533,234,908 kwa mwaka 2019/20 na Sh. 270,110,956 kwa mwaka 2018/19; lakini malipo hayo hayakuoneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha hivyo kupelelkea malipo ya matengenezo kuoneshwa pungufu kwa Sh. 533,234,908 kwa mwaka 2019/20 na Sh. 270,110,956 kwa mwaka 2018/19.

d) **Kiasi cha ruzuku ya kawaida kilichotumika kilioneshwa pungufu kwa Sh. 391,440,986**
Maelezo Na. 18C kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi cha ruzuku ya kawaida kilichotumika cha Sh. 27,020,686,170; lakini, ukokotoaji wangu kwa kutumia taarifa zilizowasilishwa kwenye maelezo Na. 18C inapelekea kiasi sahihi cha Sh. 27,412,127,156, hivyo kupelekea kiasi cha mapato kilichooneshwa kuwa pungufu na kiasi cha ruzuku ambacho hakikutumika kuwa zaidi kwa Sh. 391,440,986.

e) **Marekebisho yaliyofanywa kwa kiasi kilichoripotiwa mwaka jana yalikuwa pungufu kwa Sh. 50,000,000**
Taarifa ya mabadiliko ya mtaji na maelezo Na. 34 kwenye taarifa za fedha yalionesha marekebisho yaliyohusiana na kiasi kilichoripotiwa mwaka jana ya Sh. 5,140,646,463; lakini, ukokotoaji wangu kwa kutumia taarifa zilizowasilishwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa, inapelekea kiasi sahihi cha marekebisho kuwa Sh. 5,190,646,463, hivyo kupelekea kiasi kilichorekebishwa kuwa pungufu kwa Sh. 50,000,000.

34. Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe

a) **Tofauti isiyo na maelezo kutokana na kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa mwaka jana na kiasi cha ulinganisho kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha kwa mwaka huu ya Sh. 1,981,864,000**

Maelezo Na. 14A kwenye taarifa za fedha yalionesha matumizi yaliyotokana na mishahara na stahiki za watumishi kwa mwaka wa ulinganisho (mwaka jana) ya Sh. 12,491,002,000; lakini kiasi cha mishahara na stahiki za watumishi kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa mwaka jana kilikuwa Sh.14,472,866,000, hivyo kupelekea tofauti ambayo haikutolewa maelezo ya Sh. 1,981,864,000.

b) **Marekebisho yaliyotokana na madeni ya stahiki za watumishi hayakuoneshwa sawasawa kwenye taarifa za fedha, Sh. 542,711,000**

Maelezo Na. 42 na 28 kwenye taarifa za fedha yalionesha masahihisho ya makosa yaliyofanyika mwaka jana ya mishahara na stahiki za watumishi kutoka Sh. 2,049,559,000 kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha kufikia tarehe 30 Juni 2019 hadi Sh. 1,506,848,000 kilichooneshwa kama kiasi cha ulinganisho kwa kupunguza madeni ya Sh. 542,711,000, lakini hakukuwa na muamala uliionesha eneo lililoongezeka (credit entry) kulingana na kupungua kwa madeni hayo. Pia, maelezo juu ya chimbuko la makosa hayo ya mwaka jana halikuelezewa, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wake.

35. Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu

c) **Thamani ya mali, mitambo na vifaa iliripotiwa pungufu kwa Sh. 673,117,065**

Maelezo Na. 29 kwenye taarifa za fedha yalionesha thamani ya mali, mitambo na vifaa ikiwa haina malimbikizo ya uchakavu ya Sh. 42,899,406,370.31; hata hivyo, thamani iliyooneshwa kwenye daftari la mali za kudumu ilikuwa Sh. 43,572,523,435.44, hivyo kupelekea thamani iliyoripotiwa kuwa pungufu kwa Sh. 673,117,065.13.

d) **Mali, mitambo na vifaa vilivyoripotiwa kwa thamani hasi ya Sh. 198,586,000**

Ukaguzi wa daftari la mali za kudumu ulibaini kuwa samani za Shule ya Msingi Kakungwe zilikuwa na thamani hasi ya Sh. 198,586,000

ikimaanisha kuwa samani hizo zilitolewa uchakavu zaidi ya gharama zilizonunuliwa. Hivyo mali, mitambo na vifaa vilivyoripotiwa vilikuwa pungufu kwa Sh. 198,586,000.

e) Madai na malipo ya mbele yalioneshwa pungufu kwa Sh. 20,499,000

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilifanya malipo ya mbele kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa zenye thamani ya Sh.20, 499,000 ambapo bidhaa hizo hazikuwa zimepokelewa kufikia tarehe 30 Juni 2020; lakini kiasi hicho kilicholipwa hakikutambuliwa kwenye taarifa za fedha (kwenye maelezo Na. 26), hivyo madai na malipo ya mbele yalioneshwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 20,499,000.

36. Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji

a) Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 320,106,707

Maelezo Na. 20 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 320,106,707 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

b) Mapato yatokanayo na huduma ya maegesho ya pikipiki ambayo hayakupokelewa Sh. 105,780,900

Nimebaini kuwa, Halmashauri ilitoa stika zenye namba maalumu kwa wamilikiwa wa pikipiki, ambapo kiasi cha Sh. 172,848,000 kilitakiwa kiwe kimekusanywa kama mapato ya ada ya maegesho ya pikipiki; lakini ni kiasi cha Sh. 67,067,100 tu ndicho kilithibishwa kupokelewa benki wakati kiasi cha Sh. 105,780,900 hakikuonekana benki na wala hakikutambuliwa kwenye taarifa za fedha.

c) Kushindwa kujiridhisha na marekebisho ya hati za madai Sh. 31,301,318

Nimebaini kuwa, marekebisho ya hati za madai ya mapato ya Sh. 31,301,318 yaliithinishwa kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) na afisa ambaye hakuwa na mamlaka ya kuithinisha marekebisho hayo. Pia, nimebaini kuwa marekebisho hayo

yalianzishwa na afisa wa Halmashauri bila ya kuwepo kwa maombi ya kufanya marekebisho hayo kutoka kwa wakusanya mapato.

d) Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 20,953,230

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 20,953,230 kwa walipwaji mbalimbali ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, hivyo sikuweza kujiridhisha na usahihi na uhalali wa malipo hayo.

37. Halmashauri ya Wilaya ya Iramba

a) Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslim bila ya kuwa na nyaraka toshelezi Sh. 7,610,200

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 7,610,200 kwa fedha taslim badala ya kufanywa malipo hayo kupitia akaunti zao za benki, na malipo hayo hayakuwa na nyaraka toshelezi; hivyo, nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na madhumuni ya malipo hayo.

b) Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 215,918,233

Maelezo Na. 20 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 215,918,233 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

38. Halmashauri ya Mji wa Nzega

a) Kutotambua bidhaa zilizopokelewa kama mapato, Sh. 151,032,088

Ukaguzi wa maelezo Na. 22 kwenye taarifa za fedha (mali, mitambo na vifaa) na mizania ya hesabu, nimebaini kuwa Halmashauri ilipokea mali (gari pamoja na vifaa vya idara ya ardhi) yenye thamani ya Sh. 151,032,088 kutoka Wizara ya Afya; lakini havikutambuliwa kama mapato kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kinyume na matakwa ya Aya ya 96 ya IPSAS 23; hivyo, jumla ya mapato yaliyooneshwa yalikuwa pungufu kwa Sh. 48,455,137.

b) Kutokutenga hasara ya mbeleni kutokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki, Sh. 28,888,308

Maelezo Na. 19 kwenye taarifa za fedha yalionesha madai ya jumla ya Sh. 28,888,308 yaliyotokana

na mapato yaliyokusanywa na watumishi wa Halmashauri pamoja na mawakala wa ukusanyaji mapato kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato papo kwa papo lakini hayakupelekwa benki/kuwasilishwa Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri haikutenga hasara inayoweza kujitokeza mbeleni kutokana na kiasi hicho kutowasilishwa, hivyo kupelekea madai na faida iliyoripotiwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kuwa zaidi kwa Sh. 28,888,308.

39. Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe

a) Kiasi kilichotolewa kama mkopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kiliripotiwa mara mbili kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha, Sh. 345,570,160

Nilibaini kuwa, kwa mwaka wa fedha 2019/20, kiasi cha Sh. 197,978,000 kiliripotiwa kama mkopo uliotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha sehemu ya shughuli za uwekezaji; pia kiasi hicho hicho kiliripotiwa kwenye maelezo Na. 16 kama ruzuku na malipo mengine ya uhamisho kwenye sehemu ya shughuli za kawaida ambapo inapelekea kiasi hicho kuwa kimeripotiwa mara mbili kwenye taarifa hiyo. Wakati kwa mwaka wa fedha 2018/19, kiasi cha Sh. 147,592,000 kiliripotiwa kama mkopo uliotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye sehemu ya shughuli za uwekezaji na kiasi hicho hicho kwenye sehemu ya shughuli za kawaida.

b) Matumizi yaliripotiwa zaidi kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kwa Sh. 197,978,000

Nilibaini kuwa maelezo Na. 16 (ruzuku na malipo mengine ya uhamisho) na taarifa ya utendaji wa fedha iliripoti matumizi ya Sh. 197,978,000 kama uhamishaji wa fedha kwenda kwenye akaunti ya wanawake na vijana na watu wenye ulemavu. Kiasi hiki hakikutakiwa kuatmbuliwa kama matumizi kwani ni uhamisho wa fedha kutoka akaunti moja ya Halmashauri kwenda akaunt nyingine, hivyo, kiasi kilichoripotiwa cha ruzuku na malipo mengine ya uhamisho kilikuwa zaidi kwa Sh. 197,978,000.

c) Kushindwa kujiridhisha na bakaa ya fedha iliyoripotiwa kwenye maelezo Na.18, Sh. 25,700,000

Nilibaini kuwa Halmashauri iliripoti kiasi cha Sh. 25,700,000 kwenye maelezo Na. 18 kama baka ya fedha kwa mwisho wa mwaka 2019/20, lakini hakukuwa na maelezo au nyaraka zinazohalalisha uwepo wa bakaa hiyo; hivyo nilishindwa kujiridhisha na uhalali na usahihi wa wa bakaa hiyo iliyoripotiwa.

40. Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema

a) Kiasi kilichooneshwa kama marekebisho ya mwaka jana hayakuwa na maelezo ya kuyahalalisha Sh. 821,023,000

Taarifa ya mabadiliko ya mtaji ilionesha kiasi cha 821,023,000 kama marekebisho ya mwaka uliopita bila maelezo yoyote ya ufafanuzi. Kukosekana maelezo au ufafanuzi nimeshindwa kubaini usahihi na uhalali wa kiasi hicho kilichorekebishwa.

b) Kutokutenga hasara ya mbeleni kutokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki, Sh. 414,149,569

Taarifa za fedha zilionesha madai ya jumla ya Sh. 414,149,569 yaliyotokana na mapato yaliyokusanywa na watumishi wa Halmashauri pamoja na mawakala wa ukusanyaji mapato kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato papo kwa papo lakini hayakupelekwa benki/kuwasilishwa Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri haikutenga hasara inayoweza kujitokeza mbeleni kutokana na kiasi hicho kutowasilishwa, hivyo kupelekea madai na faida iliyoripotiwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kuwa zaidi kwa Sh. 414,149,569.

c) Kiasi kilichowekezwa kama (MCR) hakikuoneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha Sh. 1,999,400

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilifanya uwekezaji wa nyongeza ya Sh.1, 999,400 kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB); lakini, kiasi hicho hakikuoneshwa katika taarifa ya mtiririko wa fedha.

41. Halmashauri ya Wilaya Kishapu

a) Kukosekana kwa hati za malipo za jumla ya Sh. 27,223,421

Nimebaini kuwa, hati za malipo pamoja na nyaraka zake muhimu zenye jumla ya Sh. 27,223,421 hazikuwepo kwenye mafaili husika na hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na madhumuni na uhalali wa malipo yaliyofanywa kupitia hati hizo.

b) **Kushindwa kujiridhisha na marekebisho ya thamani ya bidhaa yaliyoripotiwa kwa mwaka 2018/19;**
Taarifa ya mabadiliko ya mtaji ilionesha mabadiliko ya thamani ya bidha kwa mwaka 2018/19 kwa kiasi cha Sh. 87,753,418, lakini mabadiliko hayo hayakuwa na maelezo au nyaraka zinazoonesha uhalali wake.

c) **Madai yaliyotambuliwa kimakosa (Halmashauri kuidai Serikali Kuu), kiasi cha Sh. 566,310,029**
Maelezo Na.18 kwenye taarifa za fedha yalionesha madai ambayo Halmashauri inaidai Serikali Kuu ya Sh.566, 310,029 kwa mwaka 2019/2020 na Sh. 815,802,678 kwa mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi yaliyooneshwa kwenye Maelezo Na.23. Nimeshindwa kujiridhisha na utambuzi wa madai hayo kwa kuwa utambuzi wa madeni ya watumishi inahusisha utambuzi wa matumizi sambamba na madai husika, hivyo sikuweza kujiridhisha utambuzi wa madai hayo yalitambuliwa sambamba na nini. Hivyo ilipelekea madai yaliyooneshwa kuwa zaidi kwa kiasi kilichooneshwa kwa miaka husika.

d) **Kukosekana kwa nyaraka zilizohalalisha marekebisho ya kiasi cha vifaa na bidhaa zinazotumiwa ya Sh. 26,467,932**
Maelezo Na. 13 kwenye taarifa za fedha yalionesha marekebisho ya kiasi cha Sh. 26,467,932 kuhusiana na vifaa na bidhaa zinazotumiwa kwa mwaka 2018/19; lakini marekebisho hayo hayakuwa na maelezo na nyaraka muhimu za kuyahalalisha, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na uhalali wa marekebisho hayo.

e) **Kutowasilishwa kwa jedwali la ukokotoaji wa marejesho ya mkopo**
Maelezo Na. 22 kwenye taarifa za fedha yalionesha marejesho ya mkopo wa muda mrefu wa Sh. 4,500,000 kwa mwaka 2019/20 na Sh. 57,000,000 kwa mwaka 2018/19; hata hivyo, hakukuwa na jedwali la ukokotoaji wa marejesho ya mkopo huo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi wa kiasi cha riba na kiasi cha mkopo kilicholipwa. Pia nimeshindwa kujiridhisha na usahihi wa mgawanyo wa mkopo kwa kiasi kinacholipika ndani ya miezi kumi na mbili tangu mwaka wa fedha kuisha cha Sh. 208,411,086 na kiasi kinacholipika zaidi ya miezi kumi na mbili cha Sh. 799,073,907.

Pia, nimebaini ongezeko la mkopo huo wa muda mrefu kwa kiasi cha Sh. 30,255,000, lakini sikuweza kujiridhisha kama ongezeko hilo lilitambuliwa pia kama gharama za deni hilo (corresponding debit entry).

f) Ushuru wa ndani ulioneshwa pungufu kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa Sh. 8,705,771

Nimebaini kuwa kiasi cha Sh. 120,500,715 kilioneshwa kwenye taarifa za fedha kama mapato mengine yaliyotokana na ukusanyaji wa madeni kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha (sehemu ya mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kawaida), lakini kiasi kilichooneshwa kama madai kwa mwaka 2018/19 kilikuwa Sh. 111,794,944, hivyo mapato yaliyooneshwa mwaka jana yalikuwa pungufun kwa Sh. 8,705,771.

42. Halmashauri ya Mji wa Kasulu

a) Kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichotumika kilioneshwa zaidi kwa Sh.256,751,210

Maelezo Na.37 kwenye taarifa za fedha (CAPEX) yalijumuisha kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichopokelewa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri na ukumbi wa mikutano cha Sh. 1,680,411,099 na matumizi halisi kuhusiana na ujenzi huo yalikuwa Sh. 1,353,444,931; lakini kiasi kilichooneshwa kama matumizi kilikuwa Sh. SH. 1,610,196,141 na hivyo kupelekea matumizi ya ruzuku hiyo kuonesha zaidi kwa kiasi cha Sh. 256,751,210 na kuoneshwa pungufu kiasi ambazo hakikuwa kimetumika kwa kiasi hicho hicho.

b) Kiasi cha ruzuku ya shughuli za kawaida kilichotumika kilioneshwa pungufu kwa Sh. 30,738,564

Maelezo Na.14 kwenye taarifa za fedha na taarifa ya utendaji wa kifedha ilionesha matumizi ya ruzuku ya kawaida ya Sh.18, 180,816,553. Hata hivyo, ukokotoaji wangu ulibaini kuwa kiasi cha matumizi sahihi kilitakiwa Sh. 18,211,555,118, hivyo kupelekea matumizi yaliyooneshwa kuwa pungufu kwa Sh. 30, 738,564.

c) Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 5,786,242

Maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 5,786,242 kulikotokana na mapato

yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

43. Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa

a) Mapungufu kwenye kiasi kilichooneshwa kama zuruku na malipo mengine kwenye taarifa za fedha

Maelezo Na. 20A kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi cha ruzuku na malipo mengine cha Sh.1,358,700,277; wakati kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha ni Sh. 1,297,161,276.54 hivyo kupelekea kiasi hicho kuwa pungufu kwa Sh.61,539,000. Pia, taarifa ya mtiririko wa fedha ilionesha ruzuku ya Sh. 1,358,700,277 wakati Maelezo Na. 20B yalionesha kiasi cha Sh. 1,297,161,277, hivyo kupelekea kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kuwa zaidi kwa Sh. 61,539,000.

b) Kiasi cha ruzuku ya kawaida kilichotumika kilioneshwa zaidi kwa Sh. 331,294,397

Maelezo Na. 11C kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi cha ruzuku ya kawaida kilichotumika cha Sh.21,042,364,585 kilichohusiana na mishahara na stahiki za watumishi; lakini, ukaguzi wa Maelezo Na. 17B (mishahara na stahiki za wafanyikazi) ulibaini kuwa kiasi hicho hakikurekebishwa na kiasi cha mishahara iliyolipwa kwa kutumia mapato ya vyanzo vya ndani ya Sh. 331,294,396.83, hivyo kiasi cha ruzuku ya kawaida kilichotumika kiliripotiwa zaidi kiasi cha Sh. 331,294,396.83

c) Limbikizo la uchakavu liliripotiwa zaidi kwa Sh. 133,882,178

Ukaguzi wa jedwali la mali, mitambo na vifaa lililoambatishwa kwenye taarifa za fedha ulibaini kuwa, mali zilizoripotiwa sehemu ya samani za ofisini na majumbani na sehemu ya vifaa vya ofisi zilitolewa uchakavu zaidi ya gharama zake kwa kiasi cha Sh. 133,882,178.

d) Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 478,264,480

Maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 478,264,480 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na

Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

44. Halmashauri ya Wilaya ya Nzega

a) Limbikizo la faida /(hasara) lilionesha pungufu kwa Sh. 131,578,958

Maelezo Na.27 kwenye taarifa za fedha (mali, mitambo na vifaa) yalionesha thamani ya Sh. 3,488,388,306 ya mali, mitambo na vifaa ukiondoa malimbikizo ya uchakavu ya mali na mitambo iliyohamishiwa RUWASA, hata hivyo marekebisho ya kiasi cha mali na mitambo hiyo yaliyofanyika kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji kilikuwa Sh. 3,619,967,264, hivyo kupelekea limbikizo la faida kuwa pungufu kwa Sh. 131,578,958

b) Mali, mitambo na vifaa viliripotiwa vikiwa na thamani zaidi kwa Sh. 317,965,659

Maelezo Na.27 kwenye taarifa za fedha (mali, mitambo na vifaa) yalionesha thamani ya Sh. 36,766,431,849 ambayo imejumuisha visima vyenye thamani ya Sh. 317, 965,659 ambavyo taarifa zake za fedha zilipaswa kuhamia RUWASA, hivyo, kupelekea mali, mitambo na vifaa kuripotiwa kwa Sh. 317,965,659 zaidi.

c) Mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 bila maelezo, Sh. 3,556,446,441

Ukaguzi wa taarifa za fedha ulibaini kuwa, Halmashauri ilifanya mabadiliko ya kiasi cha gharama ya mishahara, vifaa na bidhaa zinazotumiwa, na gharama za matengenezo yenye jumla ya Sh. 3,556,446,441 kutoka kwenye kiasi kilichoripotiwa kweye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka 2018/19 bila ya kuahinisha chimbuko na sababu za mabadiliko hayo ambapo, si tu kinyume na matakwa ya aya ya 54 ya IPSAS 3 bali pia nimeshidwa kujiridhisha na uhalali wa mabadiliko hayo.

45. Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza

a) Kutokutenga hasara ya mbeleni kutokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki, Sh. 264,104,000

Maelezo Na. 27 kwenye taarifa za fedha yalionesha madai ya jumla ya Sh. 264,104,000 yaliyotokana na mapato yaliyokusanywa na watumishi wa Halmashauri pamoja na mawakala wa ukusanyaji

mapato kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato papo kwa papo lakini hayakupelekwa benki/kuwasilishwa Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri haikutenga hasara inayoweza kujitokeza mbeleni kutokana na kiasi hicho kutowasilishwa, hivyo kupelekea madai na faida iliyoripotiwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kuwa zaidi kwa Sh. 264,104,000.

b) Mali, mitambo na vifaa viliripotiwa vikiwa na thamani hasi ya Sh. 16,494,000

Maelezo Na. 30 kwenye taarifa za fedha yalionesha thamani hasi ya mali, mitambo na vifaa ukiondoa malimbikizo ya uchakavu ya Sh. 16,494,000, ikimaanisha mali na mitambo hiyo ilipunguzwa kwa kiasi cha uchakavu zaidi ya gharama zake za ununuzi.

c) Limbikizo la faida /(hasara) lilioneshwa zaidi kwa Sh. 117,327,000

Maelezo Na.30 kwenye taarifa za fedha (mali, mitambo na vifaa) yalionesha thamani ya Sh. 5,662,313,000 ya mali, mitambo na vifaa ukiondoa malimbikizo ya uchakavu ya mali na mitambo iliyohamishiwa RUWASA, hata hivyo marekebisho ya kiasi cha mali na mitambo hiyo yaliyofanyika kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji kilikuwa Sh. 5,544,986,000, hivyo kupelekea limbikizo la faida kuwa zaidi kwa Sh. 117,327,000.

46. Halmashauri ya Jiji la Arusha

a) Kiasi cha matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi kiliripotiwa zaidi kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kwa Sh. 221,678,000

Kwa mwaka 2019/20, Halmashauri iliripoti kiasi cha matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi ya Sh. 45,566,141,000 kwenye Taarifa ya Utendaji wa Fedha kama ilivyofafanuliwa kwenye maelezo Na. 18 kwenye taarifa za fedha. Kiasi hicho kilijumuisha mwenendo wa madeni ya mishahara na stahiki za watumishi ya Sh. 110,839,000. Kiasi hicho kilirekebishwa kwa kuongezwa kwenye malipo ya mshahara na stahiki za watumishi ya Sh. 43,716,646,000 badala ya kutolewa na hivyo kupelekea gharama za matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi kuripotiwa zaidi kwa Sh.221, 678,000.

b) Mapato ya kodi na ushuru wa ndani yaliripotiwa zaidi kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kwa Sh. 1,988,446,000

Maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha za (madai na Malipo ya mbele) yalionesha kuwa, madai ya ushuru wa ndani yalipungua kwa kiasi cha Sh. 994,233,000 kutoka Sh. 1,710,076,000 kilichoripotiwa mwaka uliopita hadi Sh. 715,843,000 kilichoripotiwa katika mwaka huu ikimaanisha kuwa, Halmashauri ilikusanya kiais cha Sh. 994,233,000 kutokana na madai ya mapato ya miaka iliyopita ingawa kiasi hicho hakikuripotiwa kama mapato ya mwaka huu kama ilivyoripotiwa katika Taarifa ya utendaji wa fedha. Kwa upande mwingine, kiasi kilichoripotiwa cha tozo na ushuru kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kilikuwa Sh. 8,924,263,000 na kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha ilikuwa TZS 7,930,030,000 na kusababisha tofauti ya TZS 994,233,000. Hii inamaanisha kiasi cha mapato kilichoripotiwa katika taarifa ya utendaji wa fedha kilitakiwa kuwa kidogo kuliko kiasi cha fedha kilichokusanywa. Hivyo, kiasi cha tozo na ushuru kilichoripotiwa kwenye Taarifa ya Utendaji wa Fedha kilikuwa kikubwa zaidi kwa Sh. 1,988,446,000

c) Kushindwa kujiridhisha na kiasi cha matumizi kilichoripotiwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha cha Sh. 681,059,000

Ukaguzi wa maelezo Na.36 na taarifa ya utendaji wa fedha, ulibaini kuwa kiasi cha Sh. 1,181,200,000 kilitolewa zaidi kwenye akaunti ya amana na kilioneshwa kama matumizi (vifaa na bidhaa zinazotumiwa) kwenye taarifa ya utendeji wa fedha. Hata hivyo, ukaguzi wa taarifa ya mtiririko wa fedha ilionesha kiasi kilichotolewa zaidi kwenye akaunti ya amana kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kawaida na kuoneshwa kwenye taaarifa hiyo kilikuwa Sh.500, 141,000. Hii imepelekea tofauti ya Sh. 681,059,000 kati ya kiasi cha matumizi kilichooneshwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha cha Sh. 1,181,200,000 kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha cha Sh. 500,141,000.

Imeripotiwa chini ya Kumbuka 36 Amana iliyotolewa zaidi ya TZS 1,181,200,000. Kiasi sawa kililipwa katika Taarifa ya Utendaji wa Fedha chini ya vifaa na matumizi yaliyotumika. Uhakiki wa kiasi kilichotengwa katika Taarifa ya Mtiririko wa Fedha ulibaini kuwa, TZS 500,141,000 zilichukuliwa kupita kiasi ili kufadhili gharama za kawaida. Ikilinganishwa na matumizi yaliyoripotiwa ya Shilingi 1,181,200,000 na kiasi kilichochukuliwa cha TZS 500,141,000

kulingana na Taarifa ya Mzunguko wa Fedha ilisababisha tofauti ya TZS 681,059,000.

d) Madai ya mapato yaliripotiwa zaidi kwa Sh. 669,168,000

Taarifa ya Utendaji wa Fedha iliripoti matumizi ya kiasi cha Sh. 669,168,000 kilichotengwa kama hasara tarajiwa ya mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki (hakikuwasilishwa Halmashauri). Ukaguzi wa maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha ulibaini kiasi hicho cha hasara hakikutolewa kwenye madai yanayohusiana na kiasi hicho kwenye maelezo Na. 25 na hivyo kupelekea kiasi cha madai kilichoripotiwa kwenye mizania ya hesabu kuwa zaidi kwa Sh. 669,168,000.

e) Kiasi kilichotumika kununulia mali, mitambo na vifaa kilioneshwa zaidi kwenye taarifa ya mtirriko wa fedha Sh. 113,269,000

Taarifa jumuifu ya mtiririko wa fedha iliripoti malipo ya kiasi cha Sh. 21,517,412,000 kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji kwa ajili ya ununuzi wa mali, mitambo na vifaa. Kiasi hicho kilijumuisha Sh. 21,404,143,000 kwa mali zilizonunuliwa na Halmashauri yenyewe na Sh.113, 269,000 zilinunuliwa na kampuni tanzu (Arusha Meat Co Ltd). Ukaguzi wa maelezo Na. 42 kwenye taarifa za fedha (CAPEX) ulibaini kuwa, mali zilizonunulia na Halmashauri za Sh. TZS 21,404,143,000 tayari zilikuwa zimejumuisha mali za kampuni tanzu za Sh. 113,269,000, hivyo malipo yaliyoripotiwa yalikuwa zaidi kwa Sh. 113,269,000.

f) Malipo ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, Sh. 32,514,972

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, nilibaini kuwa kiasi cha Sh. 32,514,972 kililipwa, lakini hakukuwa na nyaraka toshelezi; hivyo nilishindwa kujiridhisha na uhalali wa malipo hayo.

g) Hati za malipo hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi, Sh.41,010,000

Ukaguzi wa taarifa ya benki ya mwezi Desemba, 2019 ulibaini kuwa, Shule ya Msingi Arusha ililipa kiasi cha Sh. 41,010,000 kutoka kwenye akaunti ya makusanyo ya ada ya shule; hata hivyo hati za malipo hayo hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi. Hivyo nilishindwa kujiridhisha na uhalali wa malipo yaliyofanywa kupitia hati hizo.

47. Halmashauri Wilaya ya Kilolo

a) **Marekebisho ya hati za madai yaliyofanyika bila ya kuwa na nyaraka toshelezi, Sh. 34,754,281**

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilifanya marekebisho ya hati za madai ya mapato (ilifuta bili za mapato) kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) ya jumla ya Sh. 34,754,281, lakini marekebisho hayo hayakuithinishwa na afisa masuuli na hayakuwa na nyaraka muhimu kama vile hati zilizoidhinishwa za kufanya marekebisho (journal vouchers) pamoja na nyaraka nyingine za kuhalalisha marekebisho hayo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wa marekebisho hayo.

b) **Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 117,102,025**

Maelezo Na. 21 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 117,102,025kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

48. Halmashauri ya Manispaa Iringa

a) **Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 227,414,984**

Maelezo Na. 24 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 227,414,984 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

49. Halmashauri ya Wilaya ya Songea

a) **Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 1,111,287,071**

Maelezo Na. 24 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 1,111,287,071 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko

la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

50. Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

a) Taarifa za fedha za kampuni tanzu kutokujumuishwa kwenye taarifa

Maelezo Na. 27 kwenye taarifa za fedha za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam yalionesha kuwa Halmashauri ina kampuni tanzu tatu (Shirika la Maendeleo Dar es Salaam, linalomilikiwa kwa asilimia 100; Machinga Complex inayomilikiwa kwa asilimia 100 na Soko la Kariakoo linalomilikiwa kwa asilimia 51). Halmashauri ilitambua uwekezaji kwenye kampuni mbili ambazo ni Shirika la Maendeleo Dar es Salaam na soko la Kariakoo, wakati uwekezeji kwa Machinga Complex haukutambuliwa, hivyo sikuweza kujiridhisha na usahihi na ukamilifu wa uwekezaji uliooneshwa kwenye taarifa za fedha. Pia, Halmashauri haikuandaa taarifa jumuifu kwa mujibu wa matakwa ya IPSAS 35 amabayo yanataka kampuni mama kuandaaa taarifa jumuifu. Hivyo, sikuweza kujiridhisha kama uwekezaji uliofanywa na Halmashauri ulitambuliwa kwa usahihi kwenye taarifa za fedha.

b) Madai

Maelezo Na. 25 yalionesha jumla ya madeni ya Sh. 4,910,239,000, hata hivyo mapungufu yafuatayo yalibainika;

- Uongozi wa Halmashauri haukuandaa mchanganuo wa umri wa madai hayo, hivyo haikuweza kuweka kiwango kilichotakiwa kutolewa kutokana na kupungua thamani ya madai hayo kwa mujibu wa IPSAS 29 matokeo yake kuna uwezekano kuwa, madai na faida iliripotiwa zaidi;
- Madai yalioneshwa pungufu kwa Sh. 322,256,000 kutokana na kutojumuishwa kwa madai ya kodi ya pango kwenye rejesta ya madai; na
- Kiasi cha Sh. 116,250,000 kilijumuishwa kwenye madai kilichohusiana na mikopo iloiyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu weneye ulemavu, ambapo sikuweza kudhibithisha vikundi hivyo; hivyo nilishindwa kujiridhisha na uhalali wa kiasi kilichotolewa kama mkopo kilichooneshwa kama madai.

c) **Kushindwa kujiridhisha na malipo ya fidia kwa wakazi wa Mbezi Luis Sh. 22,044,500**

Nilibani fidia ya ziada ya Sh 22,044,500 iliyolipwa kwa wakazi wanne ambao majina yao hayakuwa kwenye orodha ya wakazi waliofanyiwa tathmini wala kwenye orodha iliyopelekwa mahakamani.

d) **Makusanyo ya mapato kwenye Stendi Kuu ya Mabasi Ubungo hayakupelekwa benki, Sh. 26,693,900**

Nilifanya ulinganisho kati ya kitabu (dispachi) kilichotumika kuwasilisha fedha kwa mtunza fedha mkuu, taarifa ya makusanyo kutoka kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) na taarifa za benki, na kubaini kuwa, kiasi cha Sh. 26,693,900 kilikusanywa lakini hakikupelekwa benki, kinyume na matakwa ya Agizo Na. 37(2) & (3) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za mitaa ya mwaka 2009.

e) **Mapungufu yaliyobainika wakati wa marekebisho ya miamala kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS)**

Marekebisho yaliyohusiana na ufutaji wa miamala 48,993 ya mapato kwenye mfumo wa ukusanyaji mapoto wa serikali za mitaa yalifanyika bila ya kuwa na kibali cha kufanya hivyo. Pia baadhi ya marekebisho yaliombwa na kurekebishwa na mtu huyo huyo mmoja, na muamala mmoja uliombwa na mtu ambaye hakuwa mtumishi wa Hamshauri. Kutokana na mapungufu hayo sikuweza kujiridhisha na usahihi na uhalali wa marekebisho yaliyofanywa na kama mapato yaliyoripotiwa yalikuwa kamili na sahihi.

51. Halmashauri ya Wilaya ya Liwale

a) **Mapato yaliyokusanywa kwa kutumia POS hayakuwasilishwa benki na wala hayakutambuliwa kwenye taarifa za fedha Sh. 102,043,448**

Nilibaini kuwa, jumla ya mapato ya Sh. 102,043,448 yaliyokusanywa kwa kutumia vifaa vya kukusanyia mapato (POS) hayakupelekwa benki /hayakuwasilishwa Halmashauri na wala hayakutambuliwa kwenye taarifa za fedha kama madai.

b) **Marekebisho ya hati za madai yaliyofanyika bila ya kuwa na nyaraka toshelezi, Sh. 258,737,465**

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilifanya marekebisho ya hati za madai ya mapato (ilifuta bili za mapato) kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) ya jumla ya Sh.

258,737,465, lakini marekebisho hayo hayakuwa na nyaraka muhimu kama vile hati zilizoidhinishwa za kufanya marekebisho (journal vouchers) pamoja na nyaraka nyingine za kuhalalisha marekebisho hayo, hivyo nimeshindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wa marekebisho hayo.

c) Utata kwenye ununuzi wa vipuri vya magari na mitambo Sh. 42,143,314

Halmashauri ilinunua spea za magari zenye thamani ya Sh. 92,170,629 kwa ajili ya kuwezesha matengenezo na ukarabati wa magari, mali na mitambio ya Serikali, ambapo kati ya kiasi hicho, malipo ya Sh. 42,143,314 hayakuwa na hati za madai na hati za kupokelea bidhaa kutoka kwa watoa huduma.

52. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

a) Kiasi cha thamani ya hisa kilichopungua zilizowekezwa kwenye Benki ya DCB haikutambuliwa kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji, Sh. 171,112,600

Maelezo Na. 30 kwenye taarifa za fedha yalionesha kuwa bei ya hisa 3,422,252 zilizowekezwa katika Benki ya DCB ilipungua kutoka Sh. 340 kwa hisa moja mwaka 2018/2019 hadi Sh. 290 kwa mwaka 2019/2020 hivyo kusababisha kupungua kwa thamani ya hisa hizo kwa Sh. 171,112,600 ambapo kiasi hicho kilitabuliwa kimakosa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kama gharama ya uwekezaji (finance cost) badala ya kutambuliwa kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji kwa mujibu wa aya ya 7 na 20 ya IPSAS 7.

b) Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 117,241,834

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 117,241,834 kwa walipwaji mbalimbali ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, hivyo sikuweza kujiridhisha na usahihi na uhalali wa malipo hayo.

c) Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 344,113,493

Maelezo Na. 24 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 344,113,493 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

53. Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba

a) Ongezeko la madai ya kisheria lilitambuliwa kimakosa kwa Sh. 8,500,000

Maelezo Na. 22 kwenye taarifa za fedha (madeni) yalionesha ongezeka la madeni ya kisheria kwa Sh. 8,500,000 kutoka Sh. 85,612,546 kwa mwaka 2018/19 hadi TZS 94,112,546 kwa mwaka 2019/20. Hata hivyo, ongezeko la madeni hayo lilitambuliwa kimakosa kwa sababu hakukuwa na ongezeko la matumizi lililotambuliwa kwenye taarifa za fedha sambamba na ongezeko hilo la madai.

b) Matumizi ambayo hayakuwa yamelipiwa hayakufanyiwa marekebisho kwa usahihi, Sh. 245,312,225

Ukaguzi wa taarifa ya fedha kwenye maenelzo Na. 14 (vifaa na bidhaa zinazotumika), maelezo Na. 15 (gharama za matengenezo) na maelezo Na. 16 (ruzuku na malipo mengine ya uhamisho) zimeonesha kuwa, marekebisho ya jumla ya kiasi cha Sh. 245,312,225 ambacho ni matumizi ambayo hayakuwa yamelipiwa hayakujumuishwa kwenye vifungu husika vya matumizi ambapo imepelekea mapungufu kwenye malipo halisi yaliyoripotiwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwenye maeneo yaliyotajwa hapo juu.

c) Matumizi ya vifaa na bidhaa zinazotumika yaliripotiwa zaidi kwa Sh. 48,870,089

Halmashauri ilifanya marekebisho ya kiasi cha vifaa na bidhaa zinazotumika kwa kutumia bakaa isiyo sahihi ya vifaa vya stoo kama ilivyooneshwa kwenye maelezo Na 19 ya Sh. 4,785,191,455 badala ya Sh. 4,939,246,768. Hii ilipelekea gharama ya matumizi ya fifaa na bidhaa zinazotumika kuripotiwa zaidi kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kwa Sh. 48,870,089.

d) Matumizi ya gharama za ukarabati yaliripotiwa zaidi kwa Sh. 21,383,600

Halmashauri ilifanya marekebisho ya kiasi cha gharama za matengenezo kwa kutumia bakaa isiyo sahihi ya malipo ya mbele (fuel prepaid) kama ilivyooneshwa kwenye maelezo Na 19 ya Sh. 836,840,312 badala ya Sh. 815,456,712. Hii ilipelekea gharama ya matumizi ya fifaa na bidhaa zinazotumika kuripotiwa zaidi kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kwa Sh. 21,383,600.

e) Kiasi halisi cha mtiririko wa fedha kutokana na shughuli kawaida hakikusuluhishwa Sh. 1,297,802,850

Kwa mujibu wa taarifa zilizopo kwenye taarifa za fedha, ukokotoaji wangu wa usuluhisho wa kiasi halisi cha fedha kutoka kwenye mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kawaida nilipata kiasi cha Sh. 2,848,027,156 badala ya Sh. 1,550,224,306 kilichoripotiwa kwenye taarifa ya upatanisho wa mtiririko wa fedha, ambapo ni zaidi kwa Sh. 1,297,802,850.

Kiambatisho Na. 2-3: Orodha na Halmashauri Zilizopata Hati Mbaya na Sababu Zake

Vigezo vya kutoa Hati Mbaya
1. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga
a) **Mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 bila maelezo** Maelezo Na. 9 kwenye taarifa za fedha, yalionesha mapato yatokanayo na kodi (local taxes) ya Sh. 1,492,074,216 kwa ulinganisho wa mwaka 2018/19; hata hivyo kiasi hicho kilitofautiana na kiasi halisi kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa mwaka 2018/19 cha Sh. 1,677,192,906, hivyo kupelekea tofauti ambayo haikutolewa ufafanuzi ya kiasi cha Sh. 185,118,690. Vilevile, Maelezo Na. 10 kwenye taarifa za fedha yameripoti mapato ya ada, faini na leseni ya Sh. 567,495,933 kwa ulinganifu wa mwaka wa fedha 2018/19, ambapo yanayotofautiana na kiasi halisi kulichoripotiwa cha Sh. 382,377,242 kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa ya mwaka uliopita huku tofauti hiyo ikiwa haina nyaraka za kujitosheleza. Licha ya mapungufu, kiasi halisi kilichokaguliwa kwenye mwaka uliopita kama kodi za ndani, ada, tozo, faini na leseni kilioneshwa kwenye uso wa taarifa ya utendji wa fedha, hii inamaanisha kuwa, kulikuwa na tofauti ya Sh. 185,118,690 kati ya kiasi kilichopo kwenye maelezo husika na kiasi kilichoripotiwa kwenye uso wa taarifa ya utendaji wa fedha. Aidha, Maelezo Na. 11 ya taarifa za fedha yalionesha mapokezi ya fedha taslimu yaliyotokana na ruzuku ya fedha za kawaida kutoka Serikali Kuu ya Sh. 26,238,107,896 kwa ulinganifu wa mwaka wa fedha 2018/19, hata hivyo, kiasi hiki kinatofautiana na kiasi halisi kilichokaguliwa mwaka wa fedha uliopita cha Sh. 26,506,716,348 bila ya maelezo. Licha ya udhaifu huu, kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha klikuwa Sh. 26,652,648,195 hivyo kupelekea kiasi cha fedha zilizopokelewa kuoneshwa zaidi kwa Sh. 145,931,847. b) **Kiasi cha fedha za kodi za ndani kilichopokelewa kilioneshwa pungufu kwa Sh. 249,922,879**

Malelezo Na. 9 ya Taarifa za Fedha yameonesha kuwa madai ya mapato ya Sh. 884,173,302 yalipunguzwa kwenye kiasi cha mapato ya kodi za ndani ili kufikia kwenye kiasi halisi cha mapokezi ya fedha kwa mwaka huu. Mapitio ya Maelezo Na. 21 (madai) yalionesha kuwa, madai ya mwisho wa mwaka yalikuwa Sh 634,250,423 badala ya kiasi kilichotolewa kwenye madai chenye thamani ya Sh. 884,173,302; hivyo, kiasi cha mapokezi ya fedha zinazohusiana na kodi za ndani kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kiliripotiwa zaidi kwa Sh. 249,922,879.

c) **Kuripotiwa zaidi mapokezi ya fedha za ada, faini, adhabu na leseni kwa Sh. 33,843,800**

Maelezo Na. 10 kwenye Taarifa za Fedha yameonesha ongezeko la Sh. 33,000,000 kama bakaa ya kuanzia mwaka linalotokana na ada, faini, tozo na leseni ili kupata kiasi halisi cha fedha kilichopokelewa kwenye Taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka wa Ukaguzi. Hata hivyo, kwenye Maelezo Na. 21 (Madai) nilibaini kuwa, kufikia tarehe 30 Juni 2019, hakukuwa na bakaa ya madai ya ada, faini, tozo na leseni, hivyo kiasi cha fedha kilichopokelewa kilioneshwa pungufu kwa mwaka 2018/19 wa ulinganifu. Pia, kiasi cha Sh. 106,097,000 kilitolewa kama bakaa ya mwisho wa mwaka badala ya Sh. 106,940,800 kilichoripotiwa kwenye Maelezo Na. 21, na kusababisha kuripotiwa zaidi kwa Sh. 843,800. Kwa maana hiyo, kiasi kilichoripotiwa cha mapokezi ya fedha kwa mwaka 2019/20 kiliongezwa kwa ujumla kwa Sh. 33,843,800, huku mwaka 2018/19 kilkipunguzwa kwa Sh. 33,000,000.

d) **Kuripotiwa zaidi kwa matumizi ya bidhaa zinazotumika kwa Sh. 302,137,002**

Kwenye uso wa Taarifa ya utendaji wa fedha imeonesha matumizi ya bidhaa ya Sh. 2,088,459,666; hata hivyo, Maelezo Na. 14 yameonesha Jumla ya matumizi ya bidhaa ya Sh. 1,786,322,664 kwa mwaka wa fedha wa ulinganifu unaoishia 30 Juni 2019, hivyo kusababisha kuripotiwa zaidi kwa matumizi ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa kwa Sh. 302,137,002.

Aidha, Maelezo Na. 14 yameonesha malipo ya fedha ya bidhaa ya Sh. 1,783,115,424, hata hivyo, kiasi kilichoripotiwa kwenye taaarifa ya

mtiririko wa fedha ni Sh. 2,085,252,426 na kusababisha malipo yaliyoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh. 302,137,002.

Pia, kiasi kilichoripotiwa cha vifaa na bidhaa zinazotumiwa cha Sh. 3,102,014,299 kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2020 kilioneshwa pungufu kwa Sh. 273,014,872 kwa sababu kilikuwa hakijarekebishwa kwa kuongezwa bakaa ya mwaka uliopita ya vifaa vya stoo ya Sh. 459,542,772 na kupunguzwa na bakaa ya mwaka huu ya stoo ya Sh. 186,527,900.

e) **Kuripotiwa pungufu kwa malipo ya matengenezo ya Sh. 782,270,572**

Maelezo Na. 16 ya Taarifa za Fedha yameripoti Jumla ya fedha iliyolipwa kwenye matengenezo ya Sh. 3,869,619,537 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2019; hata hivyo, kiasi kilichoripotiwa kwenye uso wa Taarifa ya mtiririko wa fedha ni Sh. 3,087,348,965, na kusababisha kiasi cha malipo kilichoripotiwa kuwa pungufu kwa kwa Sh. 782,270,572.

f) **Matumizi ya matengenezo yaliripotiwa pungufu kwa Sh. 777,667,970**

Maelezo Na. 16 ya Taarifa za Fedha yaliripoti matumizi ya matengenezo ya Sh. 3,865,016,935 kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2019; hata hivyo, kiasi kilichoripotiwa kwenye uso wa Taarifa ya utendaji wa fedha ni Sh. 3,087,348,965 na kusababisha kiasi kilichoripotiwa kuwa pungufu kwa Sh. 777,667,970.

g) **Mali zilizohamishwa ambazo hazijaripotiwa kwenye Taarifa ya mabadiliko ya mtaji, Sh. 1,321,297,728 kwa mwaka 2018/19 na Sh. 555,627,260 kwa mwaka 2019/20**

Maelezo Na. 24 ya Taarifa za fedha (mali, mitambo na vifaa) ilionesha uhamishaji wa jengo lenye thamani ya Sh. 1,321,292,728 ambalo lilikuwa na malimbikizo ya uchakavu ya Sh. 158,555,127 kwa mwaka wa fedha 2019. Hata hivyo, ni kiasi cha malimbikizo ya uchakavu tu ndicho kilichoripotiwa kwenye malimbikizo ya faida huku gharama ya jengo ya Sh. 1,321,292,728 haikuondolewa kwenye malimbikzo ya

faida, na hivyo, kupelekea malimbikizo ya faida kuoneshwa zaidi kwa Sh. 1,321,292,728.

Pia, Halmashauri ilihamisha jengo lenye gharama ya Sh. 555,627,260 kwa mwaka huu wa fedha bila ya kuondoa kiasi cha malimbikizo ya uchakavu kama ilivyoonekana kwenye Maelezo Na. 24. Hata hivyo, nimebaini kuwa kiasi hicho hakijaripotiwa kwenye Taarifa ya mabadiliko ya mtaji na kusababisha ongezeko la bakaa lililooneshwa kwenye malimbikizo ya faida.

h) **Thamani ya kazi za ujenzi zilizokuwa zinaendelea ilihamishiwa kuwa mali iliyokamilika kwa zaidi ya gharama ya ujenzi kwa Sh. 225,012,564**

Ukaguzi wa Maelezo Na. 24 ulibaini kuwa Ujenzi uliokuwa unaendelea wa uchimbaji visima na majosho ya kuoshea ng'ombe wenye thamani ya Sh. 4,330,579,223 ilihamishwa kuwa mali iliyokamilika; hata hivyo, gharama ya ujenzi ya kazi iliyohamishwa kwenye mali ilikuwa Sh. 4,105,566,659, hivyo kusababisha gharama iliyohamishwa zaidi kwa Sh. 225,012,564.

i) **Makosa kwenye thamani ya mali, mitambo na vifaa yaliyoripotiwa kwenye Taarifa ya Mizania ya hesabu na kwenye Maelezo Na. 24**
Ukaguzi wa Maelezo Na. 24 kwenye taarifa ya fedha ilibaini makossa yafuatayo:

i. Halmashauri ilihamisha gharama ya kazi za ujenzi zilizokuwa zinaendelea (WIP) ya Sh. 1,394,231,788 kwenda kwenye mali iliyokamilika; hata hivyo, kiasi hicho hakikujumuishwa kwenye kundi husika la majengo;
ii. Maelezo Na. 39 yalionesha kuwa gharama ya ununuzi wa mali, mitambo na vifaa kwa mwaka 2019/20 ilikuwa Sh.1,139,135,620; hata hivyo, ongezeko la mali, mitambo na vifaa lililooneshwa kwenye Maelezo Na. 24 lilikuwa Sh. 6,627,194,067 na hivyo, kusababisha kiasi kilichoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh. 5,488,058,447;
iii. Nilipojumlisha gharama ya sehemu ya majosho ya kuoshea ng'ombe nilibaini jumla ya Sh. 4,330,579,223; hata hivyo, Jumla iliyowekwa ilikuwa sifuri, na hivyo, kusababisha

upungufu wa gharama ya mali, mitambo na vifaa kwa kiasi hicho.

j) **Mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 bila maelezo, Sh. 303,017,904**

Ukaguzi wa taarifa za fedha ulibaini kuwa, Halmashauri ilifanya mabadiliko ya kiasi chenye jumla ya Sh. 303,017,904 kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha kwa mwaka 2018/19 kwenye taarifa za fedha za mwaka 2019/20, kutoka kwenye kiasi kilichoripotiwa kweye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka 2018/19 bila ya kuainisha chimbuko na sababu za mabadiliko hayo ambapo, si tu kinyume na matakwa ya aya ya 54 ya IPSAS 3 bali pia nilishidwa kujiridhisha na uhalali wa mabadiliko hayo.

k) **Utambuzi usio sahihi wa madeni ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ya Sh. 122,523,297 kwa mwaka 2020 na Sh. 115,663,185 kwa mwaka 2019**

Halmashauri iliripoti madeni ya Sh. 122,523,297 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020 na Sh. 115,663,185 kwa mwaka 2019 kuhusiana na mchango wa mfuko wa wanawake, vijana na watu weney ulemavu kwenye Maelezo Na. 26 kwenye taarifa za fedha. Hata hivyo, kiasi hiki kinawakilisha miamala ya ndani ambayo ilitakiwa iondolowe wakati wa kuandaa taarifa jumuifu za fedha za Halmashauri.

l) **Utambuzi usio sahihi wa madeni ya asilimia 20 ya uchangiaji wa vijiji na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

Halmashauri iliripoti madeni ya Sh. 45,219,514 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020 na Sh. 209,038,788 kwa mwaka 2018/19 yanayohusiana na kiasi cha asilimia 20 ambacho Halmashauri haikuchangia kwenye vijiji kama ilivyooneshwa kwenye Maelezo Na. 26 ya taarifa za fedha. Hata hivyo, kiasi hiki kinawakilisha miamala ya ndani ambayo ingetakiwa kuondolewa wakati wa uandaaji wa taarifa jumuifu za fedha. Pia, halmashauri iliripoti kwenye Maelezo hayohayo, madeni ambayo hayakupelekwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaaa ya Sh. 24,529,350 kwa mwaka wa fedha 2018/19 ambayo hayakupaswa kuripotiwa kama madeni.

m) **Makosa kwenye ukokotoaji wa kiasi halisi cha mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kawaida kwa mwaka 2018/19**

Nilibaini kuwa, Halmashauri iliripoti kiasi kilichofanyiwa mabadiliko cha jumla ya mapokezi ya fedha kutokana na shughuli za kawaida kwa mwaka 2018/19 cha Sh. 32,868,726,061 na jumla ya malipo ya Sh. 29,307,933,531 ambapo yalitakiwa kupelekea kiasi halisi cha fedha kutokana na shughuli za kawaida kuwa Sh. 3,560,792,530 badala ya kiasi kilichoripotiwa cha hasara ya Sh. 87,589,428. Hii ingetakiwa kupelekea ongezeko la bakaa halisi la fedha la Sh. 57,837,988 badala ya kiasi kilichoripotiwa cha Sh. (235,212,549) kwa mwaka 2019/20, na bakaa ya Sh. 2,020,788,145 badala ya iliyoripotiwa ya Sh. 1,727,737,608 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019.

2. Halmashauri ya Wilaya ya Singida

a) **Madeni ya mwaka jana yalioneshwa pungufu kwenye mizania ya hesabu Sh. 190,307,000**

Halmashauri iliripoti jumla ya deni la Sh. 1,409,381,000 kwenye mizania ya hesabu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019. Hata hivyo, baada ya kujumlisha tena vitu vilivyoripotiwa nilibaini kuwa jumla sahihi ilitakiwa kuwa Sh. 1,599,688,000 badala ya TZS 1,409,381,000, hivyo, madeni yaliyoripotiwa yalikuwa pungufu kwa Sh. 190,307,000

b) **Thamani ya mali, mitambo na vifaa iliripotiwa zaidi kwa Sh. 1,202,120,000**

Maelezo Na. 28 kwenye taarifa za fedha (Mali, mitambo, na vifaa) yalionesha thamani ya mali, mitambo na vifaa ya Sh. 91,584,313,000; lakini ukokotoaji wangu ulibaini kuwa, thamani sahihi ilitakiwa kuwa Sh. 90,382,193,000, hivyo kupelekea thamani iliyoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh. 1,202,120,000

c) **Mapato yatokanayo na ruzuku ya maendeleo iliripotiwa zaidi kwa Sh. 713,771,000**

Maelezo Na. 24 kwenye taarifa za fedha yaliripoti kiasi kilichotumika cha ruzuku ya maendeleo cha Sh. 837,911,000 kwa mwaka 2019/20, lakini kiasi ambacho kiliripotiwa katika taarifa ya utendaji wa fedha

kama mapato ya ruzuku maendeleo kilikuwa Sh. 1,551,682,000; hivyo kupelekea kiasi cha mapato kilichoripotiwa kama ruzuku ya maendeleo kuwa zaidi kwa Sh. 713,771,000.

d) **Jumla ya matumizi yaliyoripotiwa kwa mwaka jana kwenye taarifa ya utendaji wa fedha yalikuwa pungufu kwa Sh. 42,934,000**

Halmashauri iliripoti jumla ya matumizi ya TZS 24,571,168,000 kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019; lakini, ukokotoaji wangu ulibaini kuwa jumla ya matumizi yalipaswa kuwa Sh. 24,614,102,000; hivyo, jumla ya matumizi yaliyoripotiwa yalikuwa pungufu kwa Sh. 42,934,000.

3. Halmashauri ya Wilaya ya Itigi

a) Thamani ya mali iliyoripotiwa kwenye taarifa za fedha ilioneshwa pungufu kwa Sh. 328,030,250

Mizania ya hesabu iliripoti thamani ya mali za muda mfupi (current assets) kwa mwaka 2018/19 ya Sh. 1,856,546,000 badala ya Sh. 2,184,576,250 kwa sababu ya makosa ya ujumlishaji, hivyo kupelekea kiasi kilichoripotiwa kuwa pungufu kwa Sh. 328,030,250 kufikia tarehe 30 Juni 2019.

b) Marekebisho ya matumizi ambayo hayakuwa yamelipwa yaliyohusiana na mishahara na stahiki za watumishi; vifaa na bidhaa zinazotumika na matengenezo, hayakuwa na nyaraka, Sh. 129,023,400

Halmashauri ilifanya marekebisho ya jumla ya Sh. 129,023,400 kwenye matumizi yaliyooneshwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha (Maelezo Na. 13 – mshaharana stahiki za watumishi, Maelezo Na. 14 - vifaa na bidhaa zinazotumiwa na maelezo Na. 15 - gharama za matengenezo) ili kupata kiasi halisi cha malipo ya fedha kilichoripotiwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha; Lakini, marekebisho hayo hayakuwa jedwali la madeni ; hivyo nilishindwa kujiridhisha na usahihi, uhalisi na ukamilifu wa marekebisho yaliyofanywa.

c) Madai yaliyofutwa hayakuondolewa kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji, Sh. 969,629,000

Halmashauri ilifuta madai na malipo ya mbele (Maelezo Na. 18 & 19) ya Sh. 1,260,858,000 kwa mwaka 2019/20 kwa kuonesha kuwa, matokeo ya ufutaji huo yalioneshwa kwenye malimbikizo ya faida (hasara); lakini, ni kiasi cha Sh. 291,229,000 tu kati ya kiasi kilichofutwa kilitolewa kwenye malimbikizo ya faida / (hasara)) huku kiasi cha Sh. 969,629,000 hakikutolewa.

d) Matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi ambayo hayakuwa yamelipiwa yalioneshwa pungufu kwenye taarifa ya utendaji wa kwa Sh. 346,823,000

Maelezo Na. 13 kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi cha mishahara na stahiki za watumishi cha Sh. 8,082,686,000 ambacho kilijumuisha mishahara ambayo haikuwa imelipwa ya Sh. 60,506,000. Lakini, maelezo Na. 21 (madeni) yalionesha ongezeko la madai ya wafanyikazi kutoka Sh. 571,702,000 yaliyoripotiwa kwa mwaka 2018/19 hadi Sh. 979,031,000 yaliyoripotiwa kwa mwaka 2019/20, na kupelekea ongezeko la Sh. 407,329,000; hivyo kiasi cha mishahara kilichoripotiwa kilikuwa pungufu kwa Sh. 346,823,000.

e) Kutokutenga hasara ya mbeleni kutokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki, Sh. 43,099,712

Maelezo Na. 20 kwenye taarifa za fedha yalionesha madai ya jumla ya Sh. 43,099,712 yaliyotokana na mapato yaliyokusanywa na watumishi wa Halmashauri pamoja na mawakala wa ukusanyaji mapato kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato papo kwa papo lakini hayakupelekwa benki/kuwasilishwa Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri haikutenga hasara inayoweza kujitokeza mbeleni kutokana na kiasi hicho kutowasilishwa, hivyo kupelekea madai na faida iliyoripotiwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kuwa zaidi kwa Sh. 43,099,712.

4. Halmashauri ya Wilaya ya Igunga

a) Jumla ya madeni yaliyooneshwa kwenye mizania ya hesabu kwa mwaka 2018/19 yalikuwa zaidi kwa Sh. 268,940,299

Mizania ya Hesabu ilionesha jumla ya madeni ya Sh. 7,654,422,258 kwa mwaka 2018/19 badala la Sh. 7,385,481,959, kutokana na makosa ya ujumlishaji; hivyo, madeni yalioneshwa zaidi kwa Sh. 268,940,299.

b) Kusindwa kuniridhisha na utambuzi wa madai yaliyopungua Sh. 615,623,268

Maelezo Na. 19 kwenye taarifa za fedha yalionesha kupungua kwa madai kutoka Sh. 615,623,268 yaliyoripotiwa kwa mwaka 2018/19 wakati kwa mwaka 2019/20 yalionesha bakaa sifuri, lakini hakukuwa na muamala wowote uliotambuliwa kwenye taarifa za fedha kuhusiana na kupungua huko, hivyo taarifa za fedha zilikuwa na mapungufu ya kiasi hicho.

c) Mabadiliko ya kiasi kilichoripotiwa kwa mwaka 2018/19 bila maelezo, Sh. 7,486,233,350

Ukaguzi wa mizania ya fedha ulibaini kuwa, Halmashauri ilifanya mabadiliko ya gharama za mali, mitambo na vifaa na kazi za ujenzi zilizokuwa zinaendelea ya jumla ya Sh. 7,486,233,350 kwa mwaka 2018/19 kwenye taarifa za fedha za mwaka 2019/20 kutoka kwenye kiasi kilichoripotiwa kweye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka 2018/19 bila ya kuainisha chimbuko na sababu za mabadiliko hayo ambapo, si tu kinyume na matakwa ya aya ya 54 ya IPSAS 3 bali pia nilishindwa kujiridhisha na uhalali wa mabadiliko hayo.

d) Mali, mitambo, na vifaa viliripotiwa tha thamani hasi ya Sh.363,045,123

Maelezo Na. 27 kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi cha malimbikizo ya uchakavu kikiwa ni zaidi ya gharama zilizotumika kununua mali hizo (kompyuta na magari) ambapo ilipeleke thamani ya mali hizo kuripotiwa kwa jumla ya hasi Sh.363, 045,123; hivyo thamani ya mali hizo ilikuwa pungufu kwa kiasi hicho.

e) Kutotambuliwa kwa mapato yasiyotokana na fedha taslim, Sh. 48,455,135

Ukaguzi wa maelezo Na. 26 kwenye taarifa za fedha na mizania ya hesabu ilionesha kuwa, Halmashauri ilipokea mali isiyo ya kifedha

kutokana na michango ya jamii yenye thamani ya Sh. 48,455,135; lakini mali hizo hazikutambuliwa kama mapato kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kinyume na matakwa ya Aya ya 96 ya IPSAS 23; hivyo, kiasi cha mapato kilichoripotiwa kilikuwa pungufua kwa Sh. 48,455,137.

f) Ruzuku ya shughuli za kawaida iliripotiwa zaidi kwenye taarifa ya mtitiko wa fedha Sh. TZS 684,964,115

Taarifa ya mtiririko wa fedha ya 2019/20 iliripoti mapokezi ya fedha za ruzuku ya kawaida ya Sh. 26,889,718,541, kiasi kilichojumuisha mapokezi yasiyo ya fedha (Madawa na vifaa tiba) vya Sh. 684,964,115 kutoka Bohari ya Madawa kama ilivyoonesha kwenye maelezo Na. 11 kwenye taarifa za fedha, hivyo, kiasi cha mapokezi ya ruzuku kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kilioneshwa zaidi kwa Sh. 684,964,115.

g) Kusindwa kujiridhisha na kiasi cha madai ya mishahara na stahiki watumishi Sh. 982,346,690

Maelezo Na. 14 kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi cha matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi cha Sh. 25,007,905,667 ambacho kilijumuisha matumizi ambayo hayakuwa yamelipiwa ya Sh. 982,346,690, ambapo nilishindwa kujiridhisha na uhalali wake kutokana na kutokuwepo kwa uchambuzi wa kina wa kiasi hicho.

h) Vifaa na bidhaa zinazotumiwa zilizooneshwa kwenye taarifa ya mtitiko wa fedha zilijumuisha kiasi ambacho kilikuwa hakijalipwa Sh. 181,371,201

Maelezo Na. 15 na taarifa ya mtiririko wa fedha iliripoti malipo ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa za Sh. 4,657,633,758, lakini ukaguzi wa maelezo Na.15 ulibaini kuwa, kiasi hicho kilijumuisha matumizi ambayo yalikuwa hayajalipwa ya Sh. 181,371,201, hivyo, malipo hayo yaliripotiwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 181,371,201.

5. Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

a) Limbikizo la faida liliripotiwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 4,905,984,873

Maelezo Na. 29 kwenye taarifa za fedha yalionesha thamani ya mali, mitambo na vifaa vilivyohamishiwa RUWASA ya Sh. 4,905,984,873;

lakini, kiasi hicho hakikutolewa kwenye limbikizo la faida hivyo kupelekea limbikizo la faida lililoripotiwa kuwa ziada kwa kiasi cha Sh. 4,905,984,873.

b) Kiasi kilichooneshwa kama marekebisho ya mwaka jana hayakuwa na maelezo ya kuyahalalisha. Sh. 4,975,140,401

Halmashauri ilionesha marekebisho kwenye kiasi kilichoripotiwa mwaka jana kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji yaliyohusiana na mabadiliko ya sera za uhasibu (uchakavu). Hata hivyo, sikuweza kujiridhisha na usahihi na uhalali wake kwa kuwa hakukuwa na uchambuzi wa kina kuhusiana na kiasi hicho kwenye taarifa za fedha.

c) Kiasi cha ruzuku ya maendeleo ambacho hakikutumika kilioneshwa zaidi kwa Sh.3,811,363,758

Maelezo Na. 41 kwenye taarifa za fedha na mizania ya fedha, iliripoti ruzuku ya maendeleo iliyoahirishwa ya Sh. 5,337,807,042 kufikia tarehe 30 Juni 2020; lakini, ukaguzi wa Maelezo Na.55 (CAPEX) ulibaini kuwa, kiasi cha ruzuku ya maendeleo isiyotumika ilikuwa TZS 1,526,443,284, hivyo kupelekea kiasi kilichoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh. 3,811,363,758.

d) Thamani ya Mali, mitambo na vifaa vilivyoongezwa kwa mwaka iliripotiwa pungufu kwa Sh. 683,001,667

Maelezo Na. 29 kwenye taarifa za fedha yalionesha ongezeko la mali, mitambo na vifaa vyenye thamani ya Sh. 1,363,978,430 kufikia tarehe 30 Juni 2020; lakini ukaguzi wa Maelezo Na.55 (CAPEX) ulibaini kuwa manunuzi halisi ya mali na mitambo yalikuwa Sh. 2,046,980,097, hivyo kupelekea kiasi kilichoripotiwa kuwa pungufu kwa Sh. 683,001,667.

e) Kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichotumika kilioneshwa pungufu kwa Sh. 520,454,989

Maelezo Na. 41 kwenye taarifa za fedha na taarifa ya utendaji wa fedha iliripoti kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichotumika cha Sh.1, 211,607,267; lakini maelezo Na. 55 kwenye taarifa za fedha yalionesha ruzuku ya maendeleo iliyotumika ya Sh. 1,732,062,256,

hivyo kupekea kiasi kilichotumika kuoneshwa pungufu kwa Sh. 520,454,989.

f) Kiasi cha ruzuku ya kawaida kisichotumika kilioneshwa pungufu kwa Sh. 469,213,741

Maelezo Na. 11 kwenye taarifa za fedha yalionesha kiasi cha ruzuku ya kawaida iliyoahirishwa cha Sh. 590,819,455; hata hivyo, ukokotoaji wangu kwa kutumia taarifa zilizopo kwenye maelezo Na. 11, ulipelekea kupata kiasi sahihi kisichotumika cha Sh. 1,060,033,196 badala ya kiasi kilichoripotiwa, na hivyo kupelekea kiasi kilichoripotiwa kuwa pungufu Sh. 469,213,741.

g) Malipo ya fedha kutokana na shughuli za uwekezeji yaliripotiwa zaidi kwa Sh. 365,280,141

Maelezo Na. 55 kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha (chini ya mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji) yaliripoti ununuzi wa mali, mitambo na vifaa vya Sh. 2,046,980,097; lakini, ukaguzi wa maelezo Na. 55 ulibaini kuwa, kiasi kilichoripotiwa kilijumuisha mchango ambao sio wa kifedha wa TZS 365,280,141, hivyo kupelekea thamani ya mali na mitambo iliyonunuliwa kuripotiwa zaidi kwa Sh. 365,280,141.

h) Kushindwa kujiridhisha na ongezeko lililofanywa kutokana na kufutwa kwa madai ya Sh. 358,050,610

Maelezo Na. 25 kwenye taarifa za fedha yalionesha madai yaliyofutwa ya Sh. 358,050,610; lakini, nilishindwa kujiridhisha na eneo liliongezeka (debit entry) kwenye taarifa za fedha kutokana na kufutwa kwa madai hayo.

i) Kushindwa kujiridhisha na punguzo lililofanywa kutokana na kufutwa kwa madeni ya Sh. 836,248,442

Maelezo Na. 35 kwenye taarifa za fedha yalionesha madeni yaliyofutwa ya Sh. 836,248,442 yanayohusiana na kiasi ambacho hakikuchangiwa kwenye akaunti ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambacho kilitambuliwa kimakosa kama madeni kwa mwaka ya nyuma; lakini, sikuweza kujiridhisha kama kiasi hicho kilichofutwa

kilipunguzwa pia eneo lipi (credit entry) kwenye taarifa za fedha, hivyo taarifa za fedha zilikuwa na mapungufu ya kiasi hicho.

j) Kiasi cha malipo ya mishahara na stahiki za watumishi kiliripotiwa pungufu kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kwa Sh. 746,475,041

Taarifa ya mtiririko wa fedha iliripoti jumla ya malipo ya TZS 14,750,696,011 kama gharama za mishahara ya wafanyakazi; hata hivyo, ukokotoaji wangu kwa kutumia taarifa zilizotolewa, nilibaini kuwa, kiasi sahihi ambacho kilipaswa kuripotiwa kilikuwa Sh. 15,497,171,052, hivyo kupelekea malipo yaliyoripotiwa kuwa pungufu kwa Sh. 746,475,041.

k) Gharama ya kazi za ujenzi zilizokuwa zinaendelea ziliripotiwa zaidi kwa Sh. 894,041,608

Ukaguzi wa jedwali la ukokotozi wa gharama ya kazi za ujenzi zilizokuwa zinaendelea ulibaini kuwa, bakaa ya kufungia mwaka kwa 2018/19 ilikuwa Sh. 6,203,833,109; lakini Halmashauri iliripoti kwa mwaka 2018/19 Sh. 7,097,874,717 kwenye mizania ya hesabu, hivyo kupelekea gharama iliyoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh. 894,041,608.

6. Halmashauri ya Wilaya ya Urambo

a) Limbikizo la faida liliripotiwa pungufu kwa Sh. 995,378,016

Kupitia maelezo No. 29 kwenye taarifa za fedha, nilibaini kuwa, kwa mwaka 2019/20, Halmashauri ilihamisha mali, mitambo na vifaa kwenda RUWASA yenye thamani ya Sh. 2,855,925,466 badala ya thamani halisi ya Sh. 1,860,547,450, hivyo kupelekea kiasi cha limbikizo la faida kilichoripotiwa kuwa pungufu kwa Sh. 995,378,016.

b) Kushindwa kujirithisha na thamani ya mali zilizohamishwa kwenye taarifa ya usuluhisho wa taarifa ya mtiriko wa fedha, Sh. 1,869,316,991

Halmashauri iliripoti uhamishaji wa mali zenye thamani ya Sh. 1,869,316,991 kwenye taarifa ya usuluhisho wa mtiririko wa fedha; lakini, kiasi hicho hakikuweza kudhibitishwa kwa sababu ya ukosefu wa uchambuzi wa jinsi thamani hiyo ilivyopatikana. Mbali na hayo,

ununuzi / uhamishaji wa mali hauendani na shughuli za kawaida (operating activites), hivyo haikupaswa kutumiwa katika usuluhishi.

c) Gharama ya mali, mitambo na vifaa iliripotiwa zaidi kwa Sh. 234,668,178

Maelezo Na. 29 kwenye taarifa za fedha yalionesha gharama ya Mali, Mitambo na Vifaa (PPE) ya Sh. 35,952,407,019; lakini, jumla ya gharama iliyoripotiwa kwenye daftari la mali isiyohamishika kufikia tarehe 30 Juni 2020 ilikuwa Sh. 35,717,738,84; hivyo kupelekea gharama iliyoripotiwa kuwa zaidi kwa Sh. 234,668,178.

d) Kiasi cha mapokezi ya fedha kutokana na shughuli za kawaida kiliripotiwa zaidi kwa mwaka 2018/19 kwa Sh. 1,083,613,348

Nilibaini kutoka kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kuwa, gharama za kusafiri za Sh. 541,806,674 ziliongezwa kwenye mapokezi ya fedha sehemu ya mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kawaida kwa mwaka wa fedha 2018/19 badala ya kutolewa kama malipo, hivyo kupelekea kiasi kilichopokelewa kuripotiwa zaidi kwa Sh. 1,083,613,348.

e) Kiasi cha ruzuku ya maendeleo kisichotumika kiliripotiwa zaidi kwa Sh. 120,000,000

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ilipokea msaada wa gari lenye thamani ya Sh. 120,000,000; ingawa thamani ya gari ilitambuliwa kwenye maelezo Na. 29, thamani ya gari hilo haikutambuliwa kama mapato kulingana na matakwa ya IPSAS 23, badala yake kilitambuliwa kama ruzuku ambayo haikuwa imetumika mwisho wa mwaka kama ilivyooneshwa kwenye maelezo Na. 27; hivyo kulipelekea jumla ya deni kuoneshwa zaidi na mapato kuripotiwa pungufu kwa Sh. 120,000,000.

f) Kutofanya tathmini kama madai yaliyoripotiwa yaliyopoteza thamani yake, Sh. 171,499,880

Maelezo Na. 21 kwenye taarifa za fedha yameainisha madai ya Sh. 171,499,880 yanayohusiana na mkopo 'power tillers' zilizotolewa kwa wakulima tangu mwaka wa fedha 2014/15, lakini Halimashauri haikufanya tathmini ili kujiridhisha na ukusanyaji wa madai hayo ili

kuhakikisha madai hayo yanaoneshwa kwa usahihi kwenye taarifa za fedha.

g) Malipo na marekebisho ya hati za madai yaliyofanyika bila ya kuwa na nyaraka toshelezi, Sh. 220,512,062

Nilibaini marekebisho ya hati za madai ya mapato ya Sh. 220,512,062 kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS), lakini marekebisho hayo hayakuwa na nyaraka muhimu za kuyahalalisha. Pia, malipo ya Sh. 183,898,464 yalifanywa kwa walipwaji mbalimbali lakini hakukuwa na nyaraka muhimu; hivyo, nilishindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wa marekebisho na malipo hayo.

7. Halmashauri ya Wilaya ya Momba

a) Marekebisho yaliyofanyika kwenye taarifa ya mabadiliko ya mtaji kwa mwaka 2019 kutokuwa na nyaraka za kuyahalalisha Sh 891,341,312

Nilibaini kuwa, taarifa ya mabadiliko ya mtaji kwa mwaka 2019 ilifanyiwa marekebisho kwa kuongeza kiasi cha Sh 1,271,697,601 kwenye malimbikizo ya faida; lakini, kati ya kiasi hicho, ni kiasi cha Sh 380,356,289 tu kilikuwa na nyaraka muhimu za kuhalalisha marekebisho hayo, wakati kiasi kilichobakia cha Sh 891,341,312 hakikuwa na nyaraka; hivyo kiasi cha malimbikizo ya faida kiliripotiwa zaidi kwa Sh 891,341,312.

b) Malipo ya madeni ambayo hayakuwahi kutambuliwa kwenye taarifa za fedha kwa miaka iliyopita Sh 18,150,000

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2020, Halmashauri ililipa kiasi cha Sh 18,150,000 kwa ajili ya kulipa madeni ya miaka ya nyuma, lakini madeni hayo yaliyolipwa hayakuwahi kuripotiwa kwenye taarifa za fedha kwa miaka ya nyuma, na wala hakukuwa na marekebisho yoyote yaliyofanyika kwenye taarifa za fedha ili kutambua madeni hayo pamoja na matumizi yaliyotokana na madeni hayo.

c) Makosa kwenye gharama zilizoongezwa za mali, mitambo na vifaa kwa mwaka 2020

Nilibaini kuwa, Maelezo Na. 33 kwenye taarifa za fedha yalionesha ongezeko la mali, mitambo na vifaa vyenye thamani ya Sh 2,430,597,312 wakati maelezo Na. 32 (CAPEX) yalionesha jumla ya kiasi cha mali, mitambo na vifaa vilivyonunulia cha Sh 2,427,097,312 hivyo kupelekea tofauti ya Sh 3,500,000. Vilevile, nilibaini vifaa vya ujenzi vilivyokuwa stoo mwaka jana ambavyo vilitumika kwa mwaka huu wa 2020 vya Sh 126,960,476, gharama yake haikujumuishwa kwenye ukokotoaji wa ongezeko la gharama ya kazi za ujenzi zilizokuwa zinaendelea hivyo kupelekea kuripotiwa pungufu kwa Sh 126,960,476.

d) Kiasi cha ruzuku ya maendeleo ambacho hakikutumika kiliripotiwa zaidi kwa Sh. 1,981,430,536

Nilibaini kuwa, kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019, Halmashauri ililipa malipo ya mbele ya Sh. 781,430,536 kwa watoa huduma na makandarasi mbalimbali na kuhamisha kiasi cha Sh. 1,200,000,000 kwenda SIBICO (SPV iliyoanzishwa katika ngazi ya mkoa kusimamia ujenzi wa soko la kimataifa); hata hivyo kiasi hicho bado kilitambuliwa kama sehemu ya ruzuku ya maendeleo ambayo haikutumika kama ilivyooneshwa kwenye maelezo Na. 32 (CAPEX). Hii ilisababisha bakaa ya kuanzia mwaka kuripotiwa zaidi kwa kiasi cha Sh.1, 981,430,536.

e) Bakaa ya fedha ambayo haikuthibitishwa inayohusiana na akaunti ya maendeleo ya Halmashauri Sh. 2,184,214,087

Maelezo Na. 19 kwenye taarifa za fedha yalijumuisha bakaa ya Sh. 2,184,214,087 kufikia tarehe 30 Juni 2020 kwenye Akaunti ya Maendeleo Na. 9921210301 ya Halmashauri. Hii pia ilithibitishwa kwenye vitabu vya fedha vya Halmashauri (TSA na Epicor) na taarifa ya usuluhisho. Lakini, kiasi hicho tayari kilikuwa kimeshahamishwa na kutumika kwa mwaka 2019/20 kupitia Akaunti Na. 9921211001, lakini kiasi hicho bado kilionekana kama bakaa ambayo haikutumika kufikia tarehe 30 Juni 2020; hivyo nilishindwa kuthibitisha usahihi na uhalali wa bakaa la fedha lililoripotiwa la Sh. 2,184,214,087.

f) Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 583,092,186

Maelezo Na. 20 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 583,092,186 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa yakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

8. Tabora MC

a) Kiasi kilichoripotiwa zaidi kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha Sh. 703,600,000

Maelezo Na. 15 kwenye taarifa za fedha yalionesha malipo halisi kwa mwaka 2019/20 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na bidhaa zinazotumiwa ya Sh. 4,835,679,311, lakini kiasi kilchoripotiwa kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha kilikuwa Sh. 4,332,079,311, na kupelekea malipo hayo kuripotiwa zaidi kwa Sh. 503,600,000. Vivyo hivyo, maelezo Na. 16 yalionesha malipo ya gharama za matengenezo ya Sh. 715,903,786 wakati taarifa ya mtiririko wa fedha iliripoti Sh. 515,903,786, na kusababisha kuripotiwa zaidi kwa Sh. 200,000,000.

b) Gharama za matumizi ya vifaa na bidhaa zinazotumika zilioneshwa pungufu kwa Sh. 39,927,840

Maelezo Na. 15 kwenye taarifa ya utendaji wa fedha yalionesha gharama ya matumizi ya vifaa na bidhaa zinazotumiwa ya Sh. 4,835,679,311. Lakini, ukokotoaji wangu kulingana na taarifa zilizopo kwenye maelezo Na. 15, kiasi sahihi kilipaswa kuwa Sh. 4,875,607,151, hivyo kupelekea matumizi hayo kuwa pungufu kwa Sh. 39,927,840.

c) Kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichopokelewa kilioneshwa pungufu kwa Sh. 672,066,781

Taarifa ya Matumizi ya Maendeleo na Ufadhili wake ilionesha jumla ya ruzuku ya maendeleo iliyopokea kwa mwaka 2019/20 ya Sh. 3,690,263,041, lakini kiasi ambacho kiliripotiwa kwenye uso wa taarifa ya mtiririko wa fedha kilikuwa Sh. 3,018,196,260 na kupelekea kiasi kilichopokelewa kuoneshwa pungufu kwa Sh. 672,066,781.

d) Kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichopokelewa kiliripotiwa zaidi kwa Sh.900,000,000 na matumizi yake kwa Sh. 607,409,138

Nilibaini kuwa, Taarifa ya Matumizi ya Maendeleo na Ufadhili wake ilionesha mara mbili kiasi kilichopokelewa cha Sh 500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Tabora na matumizi yanayohusiana na ujenzi huo ya Sh. 207,409,138. Pia, imeripoti kiasi cha Sh. 400,000,000 kama mapokezi na malipo kwa mwaka 2019/20 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Maili Tano, lakini kiasi hicho kilipokelewa mwaka 2017/18 na kilitumika katika mwaka 2018/19.

e) Kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichotumika kiliripotiwa zaidi kwa Sh. 299,946,362

Halmashauri iliripoti mapato (ruzuku ya maendeleo iliyotumika) ya Sh. 10,836,925,347 kwenye taarifa ya utendaji wa fedha. Lakini, ukaguzi wa taarifa ya matumizi ya maendeleo na ufadhili wake pamoja na jedwali la mali za kudumu ulibaini kuwa kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichotumika kilikuwa Sh. 10,536,978,985, hivyo kupelekea mapato yaliyotokana na ruzuku hiyo kuripotiwa zaidi kwa Sh. 299,946,362.

a) Kutokutenga hasara ya mbeleni kutokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki, Sh. 334,730,634

Maelezo Na. 20 kwenye taarifa za fedha yalionesha madai ya jumla ya Sh. 334,730,634 yaliyotokana na mapato yaliyokusanywa na watumishi wa Halmashauri pamoja na mawakala wa ukusanyaji mapato kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato papo kwa papo lakini hayakupelekwa benki/kuwasilishwa Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri haikutenga hasara inayoweza kujitokeza mbeleni kutokana na kiasi hicho kutowasilishwa, hivyo kupelekea madai na faida iliyoripotiwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kuwa zaidi kwa Sh. 334,730,634.

b) Marekebisho ya kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa ya ulinganisho kwenye taarifa ya utendaji wa fedha hayakuwa na nyaraka , Sh.4,067,368,089

Nilibaini kuwa, kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa ya ulinganisho kwa mwaka 2019/20 zilitofautiana sana kwa jumla ya Sh. 4,067,368,089

kutoka kweye kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka 2018/19 kama ifuatavyo; mishahara na stahiki za watumishi ilioneshwa zaidi kwa Sh. 3,764,240,808, vifaa na bidhaa zinazotumiwa zilioneshwa zaidi kwa Sh. 274,334,789, na gharama za matengenezo zaidi kwa Sh. 28,792,492. Lakini, Halmashauri haikutoa sababu za mabadiliko hayo.

Kiambatisho Na. 2-4: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Miaka Minne

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
1	Halmashauri ya Manispaa ya Tabora	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati mbaya
2	Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati mbaya
3	Halmashauri ya Wilaya ya Igunga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati mbaya
4	Halmashauri ya Wilaya ya Itigi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati mbaya
5	Halmashauri ya Wilaya ya Momba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati mbaya
6	Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati mbaya
7	Halmashauri ya Wilaya ya Singida	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati mbaya
8	Halmashauri ya Wilaya ya Urambo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati mbaya
9	Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
10	Halmashauri ya Wilaya ya Butiama	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
11	Halmashauri ya Wilaya ya Songea	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
12	Halmashauri ya Manispa ya Kigoma/Ujiji	Hati mbaya	Hati mbaya	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
13	Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
14	Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
15	Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
16	Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
17	Halmashauri ya Wilaya ya Siha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
18	Halmashauri ya Jiji la Arusha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
19	Halmashauri ya Wilaya ya Bahi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
20	Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
21	Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
22	Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
23	Halmashauri ya Wilaya ya Bunda	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
24	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
25	Halmashauri ya Wilaya ya Chemba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
26	Halmashauri ya Wilaya ya Chunya	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
27	Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
28	Halmashauri ya Wilaya ya Geita	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
29	Halmashauri ya Wilaya ya Hanang	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
30	Halmashauri ya Wilaya ya Iramba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
31	Halmashauri ya Wilaya ya Iringa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
32	Halmashauri ya Manispaa ya Iringa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
33	Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
34	Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
35	Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
36	Halmashauri ya Mji wa Kasulu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
37	Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
38	Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
39	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
40	Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
41	Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
42	Halmashauri ya Mji wa Kondoa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
43	Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
44	Halmashauri ya Mji wa Korogwe	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
45	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
46	Halmashauri ya Wilaya ya Liwale	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
47	Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
48	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
49	Halmashauri ya Wilaya ya Msalala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
50	Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
51	Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
52	Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
53	Halmashauri ya Wilaya ya Nzega	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
54	Halmashauri ya Mji wa Nzega	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
55	Halmashauri ya Wilaya ya Rorya	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
56	Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
57	Halmashauri ya Manispaa ya Singida	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
58	Halmashauri ya Manispaa ya Temeke	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
59	Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
60	Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
61	Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
62	Halmashauri ya Wilaya ya Handeni	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
63	Halmashauri ya Wilaya ya Karatu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
64	Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
65	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
66	Halmashauri ya Manispaa ya Songea	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
67	Halmashauri ya Wilaya ya Nyanghw'ale	Hati inayoridhisha	Kushindwa kutoa maoni	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
68	Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
69	Halmashauri ya Wilaya ya Makete	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
70	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
71	Halmashauri ya Wilaya ya Uyui	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
72	Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
73	Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma	Hati mbaya	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
74	Halmashauri ya Wilaya ya Pangani	Hati mbaya	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
75	Halmashauri ya Mji wa Babati	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
76	Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
77	Halmashauri ya Wilaya ya Longido	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
78	Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
79	Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
80	Halmashauri ya Wilaya ya Meru	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
81	Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
82	Halmashauri ya Wilaya ya Rombo	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
83	Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
84	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
85	Halmashauri ya Wilaya ya Babati	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
86	Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
87	Halmashauri ya Mji wa Bariadi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
88	Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
89	Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
90	Halmashauri ya Mji wa Bunda	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
91	Halmashauri ya Wilaya ya Busega	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
92	Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
93	Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
94	Halmashauri ya Wilaya ya Chato	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
95	Halmashauri ya Jiji la Dodoma	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
96	Halmashauri ya Wilaya ya Gairo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
97	Halmashauri ya Mji wa Geita	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
98	Halmashauri ya Wilaya ya Hai	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
99	Halmashauri ya Mji wa Handeni	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
100	Halmashauri ya Mji wa Ifakara	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
101	Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
102	Halmashauri ya Manispaa ya Ilala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
103	Halmashauri ya Wilaya ya Ileje	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
104	Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
105	Halmashauri ya Wilaya ya Itilima	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
106	Halmashauri ya Mji wa Kahama	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
107	Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
108	Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
109	Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
110	Halmashauri ya Mji wa Kibaha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
111	Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
112	Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
113	Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
114	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
115	Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
116	Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
117	Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
118	Halmashauri ya Wilaya ya Kyela	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
119	Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
120	Halmashauri ya Wilaya ya Lindi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
121	Halmashauri ya Manispaa ya Lindi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
122	Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
123	Halmashauri ya Wilaya ya Madaba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
124	Halmashauri ya Wilaya ya Mafia	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
125	Halmashauri ya Mji wa Mafinga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
126	Halmashauri ya Wilaya ya Magu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
127	Halmashauri ya Mji wa Makambako	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
128	Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
129	Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
130	Halmashauri ya Wilaya ya Masasi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
131	Halmashauri ya Mji wa Masasi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
132	Halmashauri ya Wilaya ya Maswa	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
133	Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
134	Halmashauri ya Jiji la Mbeya	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
135	Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
136	Halmashauri ya Mji wa Mbinga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
137	Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
138	Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
139	Halmashauri ya Mji wa Mbulu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
140	Halmashauri ya Wilaya ya Meatu	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
141	Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
142	Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
143	Halmashauri ya Wilaya ya Mlele	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
144	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
145	Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
146	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
147	Halmashauri ya Wilaya ya Moshi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
148	Halmashauri ya Manispaa ya Moshi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
149	Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina la Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
150	Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
151	Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
152	Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
153	Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
154	Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
155	Halmashauri ya Wilaya ya Muheza	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
156	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
157	Halmashauri ya Wilaya ya Musoma	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
158	Halmashauri ya Manispaa ya Musoma	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
159	Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
160	Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
161	Halmashauri ya Jiji la Mwanza	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
162	Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
